INSHA

- Utungo unaoundwa kwa mfululizo wa sentensi zinazozungumzia jambo, tukio au kitu fulani

Aina

1. INSHA ZA KAWAIDA

a) Insha ya Picha

- Ambapo mwanafunzi amepewa picha kadha na kutakiwa kutunga kisa na kueleza yote yanayotokea kwenye picha hizo. Chunguza vizuri ujue kinachotokea katika hizo picha.
  - ✓ Kichwa kiafikiane na picha ulizopewa. Kila picha ipangwe na kuwa na aya moja.

b) Insha ya Methali

- Insha inayosimulia kisa kinachoonyesha ukweli au uongo wa methali Fulani.
  - ✓ Wazia methali nyingine za kutilia mkazo methali uliyopewa.

Muundo

1. Kichwa
1. methali yenyewe
2. Utangulizi

i. Maana ya juu/wazi

i. Maana ya ndani/batini

3. Mwili
    1. kisa kinachofungamana na methali cha kweli au cha kubuni
4. Hitimisho
1. funzo/maadili

c) Insha ya Maelezo

1. Inayohusu kutoa ufafanuzi kuhusu mahali, kitu au jambo fulani kama vile ugonjwa wa ukimwi, umuhimu wa maji, n.k.

d) Insha ya Masimulizi

2. Ambapo unatakiwa kusimulia hadithi, kisa au tukio kuhusu jinsi mambo fulani yalivyotokea. Huweza kuanzia kwa ‘Ilikuwa…'

e) Insha ya Mdokezo

3. Ambapo umepewa mdokezo wa kuanzia (xxx…) au kumalizia (…xxx) k.m. ‘…tangu siku hiyo alikula yamini kutopuuza ushauri wa wazazi wake tena'

f) Insha ya Mjadala

4. Ambapo unatakiwa kujadili suala fulani k.m. ‘Shule za mabweni zina manufaa' au ‘Kujiajiri ni bora kuliko kuajiriwa' Jadili.

Unapaswa:

1. Kuunga
2. Kupinga
3. Kutoa uamuzi kutegemea upande ulio na hoja nyingi au nzito.

g) Insha ya Mawazo

1. Inayohusu mambo ya kuwaza kuhusu jambo fulani k.m. ‘MIMI NYUKI'

- ✓ Ni nani asiyenifahamu mimi nyuki.

a) Insha ya Mazungumzo

- ✓ Maongeo ya kawaida ambayo huandikwa kama tamthilia
- ✓ MAZUNGUMZO BAINA YA…

Muundo

- ✓ Kichwa
- ✓ Jina la msemaji kwa herufi kubwa likifuatwa na koloni
- ✓ Maneno ya msemaji
- ✓ maelezo ya mandhari na vitendo vya msemaji kwenye mabano
- ✓ Wazungumzaji wasikike kama watu wa kawaida
- ✓ Pawepo na sentensi ndefu na fupi
- ✓ Matumizi ya vihisishi
- ✓ Ukatizaji wa maneno…

2. TUNGO ZA KIUAMILIFU

- Ambazo hutekeleza kazi maalum na huwa na muundo maalum.

Dayalojia

- Mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi kuhusu jambo au mada fulani
  1. DAYALOJIA BAINA YA…
  2. Huwa na utangulizi, mwili na hitimisho

Mahojiano

- Mazungumzo yanayoendeshwa kwa muundo wa maswali na majibu
    1. (MAHOJIANO BAINA YA…)

Barua ya Kirafiki

- Inayoandikwa kwa ndugu, jamaa na marafiki.

Muundo

1. Anwani ya mwandishi (wima au mshazari. Jina lisiwekwe!)
2. Tarehe ya kuandikwa barua (22 Februari, 2011)
3. Mwanzo wa barua (kwa … mpendwa/kwenu…
4. utangulizi (salamu, kumjuliana hali)
5. mwili/yaliyomo (ujumbe)
6. Hitimisho (Kwa leo sina mengi. Wasalimie jamaa wote. Ni mimi wako/wenu, Jina (wima au mshazari)

Barua Rasmi/Kwa Mhariri

1. Barua ambazo huandikwa na kutumwa ofisini kwa kutaka kuomba kazi, kuomba msaada, malalamiko, kutoa maoni gazetini, n.k.

Muundo

- ✓ Anwani ya mwandishi (wima au mshazari)
- ✓ Tarehe ya kuandikwa (usiweke jina).
- ✓ Marejeleo k.m. REJ: SUD/MSS/054/009 (nambari ya kumbukumbu, faili au nambari ya barua)
- ✓ Cheo na anwani ya mwandikiwa k.m. Mkurugenzi, Kiwanda cha majani chai cha Kangaita, S.L.P, 12000, Kerugoya au Mhariri wa Gazeti la ‘Nation', S.L.P 89000, Nairobi au KWA ANAYEHUSIKA
- ✓ Kupitia kwa: MWALIMU MKUU, anwani
- ✓ Mtajo k.m. Kwa Bwana/Bibi/Profesa/Daktari/Mhubiri
- ✓ Kichwa cha barua k.m. MINT: OMBI LA KAZI YA UALIMU/MAPENDEKEZO KUHUSU JUMA MRISHO/ MWALIKO WA KUHUDHURIA KONGAMANO LA KISWAHILI
- ✓ Utangulizi **(**Mintaarafu ya tangazo mlilochapisha… naandika kuomba…jinsia…ahadi kufanya kazi kwa bidii)

- ✓ Mwili (matatizo, madhara, mapendekezo (naomba, paswa, stahili, naonelea ni bora)
- ✓ Hitimisho (Natumai, Nitashukuru…Wako mwaminifu/mtiifu, sahihi, jina /cheo, Chama cha Kiswahili. Nakala kwa: (i), (ii) (wima au mshazari)

Barua ya Gazetini Iliyohaririwa

- ✓ Kichwa (kwa herufi ndogo na usemi halisi)
- ✓ mtajo (Mhariri,)
- ✓ Utangulizi (Naandika kueleza…)
- ✓ Mwili (malalamiko, maoni, maombi, mapendekezo)
- ✓ Hitimisho (Natumai…) jina na anwani ya mwandishi)

Tahariri

1. Maelezo mafupi ya mhariri wa gazeti kutoa mawazo, maoni au msimamo wa chombo cha habari anachowakilisha kuhusu suala maalum na muhimu.

Muundo

GAZETI LA MZALENDO
Februari 24, 2011
HATIMA YA WATAHINIWA
Yaliyomo
Imeandikwa na…

Hotuba

- Maelezo yanayotolewa mbele ya watu.
- ✓ Hutolewa kwa usemi halisi na huanzia na kuishia kwa alama za usemi.

Muundo

- ✓ Anwani (HOTUBA KUHUSU…)
- ✓ Utangulizi (kutaja hadhira kuanzia walio mashuhuri, kuwasalimu, kujitambulisha na kuwakaribisha na kutambulisha kiini cha hotuba)
- ✓ Yaliyomo (kutaja na kufafanua hoja)
- ✓ Hitimisho (shukrani na kuwatakia mema katika shughuli zao za kila siku)

Ratiba

- Mpangilio wa jinsi shughuli fulani inavyofanyika kulingana na wakati fulani uliotengwa k.m. sherehe ya arusi, mazishi, siku ya michezo, kutoa zawadi n.k.

Muundo

- ✓ Kichwa (Ratiba ya shughuli gani, ya nani, mahali na tarehe, mgeni wa heshima: …Wageni mashuhuri: 1….2….3….)

SAA	**TUKIO**	**MHUSIKA**
Asubuhi/ adhuhuri	**Ku…/ watu …**	

- ✓ Makaribisho
- ✓ Maombi
- ✓ Kutoa tuzo
- ✓ Kutoa shukrani
- ✓ Kufungwa kwa maombi
- ✓ Kuondoka/kufumkana

Shajara

1. Daftari ambayo huhifadhiwa matukio yanayofanyika kila siku. Yaweza kuwa ya siku moja, wiki au mwezi mmoja.

Aina

a) **Ya kibinafsi**

JUMANNE 30/8/10

Leo tulizuru…

b) **Rasmi (hutumiwa katika ofisi)**

SHAJARA

JUMANNE MEI 7, 2008

1. asubuhi	**Ku…**
2.	

Onyo

1. Makatazo.

Tahadhari

2. Julisho kuhusu jambo la hatari.

ONYO! USISIMAMISHE WALA KUEGESHA GARI KWENYE ENEO HILI!

TAHADHARI!
DARAJA HILI LINA KASORO
TAFADHALI USILITUMIE

Ilani

3. Julisho, tangazo au notisi.

ILANI
TAFADHALI
USITUMIE SIMU
YA MKONO NDANI YA
BENKI

ILANI YA SERIKALI KUHUSU KUZUKA KWA UGONJWA WA KIPINDUPINDU

Serikali imetoa ilani kwa wananchi kuhusu kuzuka kwa ugonjwa wa kipindupindu. Kila mwananchi anatakikana kuzingatia mambo yafuatayo ili kudhibiti maambukizi.

a) Mtu asinywe maji kabla kuyachemsha
b) Kupika chakula hadi kiive vizuri
c) Kutoenda haja nje bali kutumia vyoo vya mashimo
d) Mtu anawe mikono yake kwa sabuni baada ya kutoka msalani
e) Mtu asile matunda au mboga za majani bila kuziosha kwanza
f) Anayeonyesha dalili ya ugonjwa wa kipindupindu apelekwe katika kituo cha afya mara moja.
g) Uchuuzi wa vyakula umepigwa marufuku
h) Ufuliaji nguo motoni pia umepigwa marufuku

Watakaokaidi maagizo katika (g) na (h) watachukuliwa hatua kali za kisheria ya kutozwa faini ya shilingi elfu tano au kifungo cha miezi miwili gerezani.

Matangazo

4. Majulisho kuhusu jambo fulani.

a) Arifa

SHULE YA UPILI YA GATWE
Anwani, tarehe
USAJILI WA …
Sahihi
Jina

Cheo

b) Kibiashara

Sifa

- ✓ Lugha kwa kifupi
- ✓ Chuku
- ✓ Takriri
- ✓ Alama ya (!) na (?)
- ✓ Michoro
- ✓ Maonyo
- ✓ Maelezo kukihusu
- ✓ Kinavyotumika
- ✓ Ubora wake
- ✓ Watengenezaji

JINUNULIE UNGA WA MAHINDI WA JAMBO SIKU YA LEO. UNGA WA JAMBO UMEONGEZEWA VITAMINI NA MADINI MUHIMU. BEI IMEPUNGUZWA KUTOKA SHILINGI 120 HADI SHILINGI 90. JIPAPIE PAKITI YAKO LEO KABLA BEI HII KUACHA KUTUMIKA

C) Kifo

TANGAZO LA KIFO

Tunasikitika kutangaza kifo cha …Alikuwa…

Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi

c) kazi

SHULE YA UPILI YA GATWE

Anwani, tarehe

NAFASI YA KAZI YA UHASIBU

SIFA ZA MWOMBA KAZI

JINSIA

Awe wa jinsia ya kike.

UMRI

Awe na umri wa miaka isiyopungua25 na isiyozidi 40.

ELIMU

i. Awe na shahada ya uhasibu kutoka chuo kikuu au awe na shahada ya diploma ya juu ya uhasibu
ii. Awe amepata alama ya c katika kingereza

KAZI

i. Kuidhinisha hati za malipo za shirika
ii. Kusimamia shughuli za uhasibu katika idara inayohusika

UZOEVU/TAJRIBA

Awe na uzoevu wa kazi usiopungua miaka 5 kwenye shirika au taasisi kubwa.

DINI

Awe muumini wa dini ya kikristu na awe ameokoka.

MUDA WA KAZI

Kuanzia saa mbili hadi saa kumi na moja jioni na masaa mengine ikibidi.

MSHAHARA

Mshahara utategemea elimu ya anayehusika lakini utakuwa baina ya ksh 24,000 na ksh 45000.

MAELEZO YA ZIADA

i. Maombi yote yawe yamewasilishwa kabla ya tarehe 30 mei 2010.
ii. Maombi yatumwe kwa:
Katibu,
Halmashauri ya shule ya upili ya Gatwe,
Anwani
iii. Maombi yatakayopelekwa baada ya muda wa mwisho hayatajibiwa.
iv. Maombi yaandamane na hundi ya shilingi elfu moja ambazo hazitarejeshwa.

Maagizo/Maelekezo

✓ Maelezo kuhusu namna ya kufika mahali kutoka kituo fulani au maelezo kuhusu njia ya kutumia kitu au huduma fulani.

Sifa

a) Maelezo wazi
b) Michoro au ramani
c) Dira
d) Huhusika maonyo
e) Tarakimu k.m. 1×3
f) Matumizi ya herufi nzito.

Mifano

a) Maagizo ya daktari kwa mgonjwa wa kisukari.
b) Maelekezo ya kutoka nyumbani hadi shuleni mwenu.
c) Jinsi ya kutumia dawa za wadudu

Kujaza Fomu

- Karatasi ambayo ina nafasi ya kuandika maelezo ambayo yanatakiwa.

a) Soma fomu kwa makini kabla ya kujaza chochote.
b) Andika maelezo kwa muhtasari.
c) Usijaze kama huna hakika kwenye sehemu Fulani.
d) Usifutafute.
e) Itumie alama inayostahili wakati wa kujaza fomu.

MAELEZO YA KIBINAFSI
TAREHE……
JINA……
JINSIA……
UMRI……
TAREHE YA KUZALIWA……
URAIA……
NAMBARI YA KITAMBULISHO……
KAZI……
MKOA……
WILAYA……
SIMU……
SAHIHI……
TAREHE……

Hojaji

- Maswali ambayo hutumiwa kama msingi wa kufanyia utafiti na huelekezwa kwa mhojiwa.

Aina

a) Hojaji Wazi

- Hojaji yenye maswali ambayo mhojiwa anaruhusiwa kuyajibu kwa maneno yake mwenyewe.

UCHAGUZI NA VIONGOZI

1. Una maoni gani kuhusu uchaguzi wa kila baada ya miaka mitatu?
   .....
   .....
   .....
2. Kwa nini una maoni hayo?
   .....
   .....
   .....
3. Wewe ungependelea utaratibu gani wa uchaguzi?
   .....
   .....
   .....
4. Je ni kweli viongozi hung'ang'ania mamlaka? .....
   .....
   .....
   .....
5. Je viongozi hung'ang'ania uongozi kwa sababu zipi?

a) .....
   .....
b) .....
   .....
c) .....
   .....

b) Hojaji Funge

1. Hojaji ambapo mhojiwa anapewa majibu kadha ambayo anatakiwa kuchagua mojawapo bila kuwa na uhuru wa kuandika atakayo.

MATATIZO YA KIJAMII

Tia alama kwenye jibu unaloafiki

a) Jamii yetu inawakandamiza wanawake?
   Ndiyo ( ) La ( )
b) Tatizo kubwa la jamii yetu kwa sasa ni umaskini na ugonjwa.

Kweli ( ) Si kweli ( )

Mialiko

- Barua ambayo hupeleka taarifa kwa mtu kumuomba ahudhurie sherehe fulani.

a) **Rasmi (kadi au barua rasmi)**

Muundo

- ✓ Jina la mwalikaji/waalikaji (Bwana/mabwana/bibi/kasisi/daktari
- ✓ Jina la mwalikwa
- ✓ Sherehe (ndoa, mchango wa pesa, Kuna aina mbili za mialiko.
- ✓ Kusherehekea/kuadhimisha…)
- ✓ Kuhusu nani
- ✓ Mahali pa kukutanika
- ✓ Tarehe
- ✓ Wakati
- ✓ Anwani na nambari ya simu ya mwalikaji ambapo jibu litapelekwa kushoto chini (Majibu kwa…wima)

b) **Kirafiki (barua ya kirafiki)**

1. Sehemu ya mwili itoe habari zote muhimu katika mwaliko.

Risala

1. Taarifa inayotoka kwa mtu au watu inayoeleza haja fulani k.m. risaala ya rambirambi, risala ya heri njema, ya waajiriwa kwa mwajiri au kinyume.

RISALA YA RAMBIRAMBI/HERI NJEMA KWA…

KUFUATIA

Mimi wako…

Resipe

2. Jumla ya hatua na kanuni ambazo hufuatiwa na mtu anayenuia kupika au kuandaa kitu fulani.

UPISHI WA PILAU

Walengwa/walaji

Mipakuo mine (kwa watu wanne)

Viambata

a) Vikombe viwili vya mchele

b) Gramu 25 za mafuta ya majimaji

c) Vijiko viwili vidogo vya pilau masala
d) Nusu kilo ya nyama
e) Vitunguu vinne vya ukubwa wa wastani
f) Vikombe vinne vwa maji

Hatua za Upishi

a) Kaanga vitunguu katika mafuta hadi rangi yake ikaribie rangi ya udhurungi
b) Chemsha nyama pekee hadi ilainike
c) Ongeza nyama kwenye sufuria yenye vitunguu na upike kwa dakika tano
d) Ongeza mchele na uchanganye kwa mwiko
e) Ongeza maji na uache mchanganyiko utokote kwa dakika kumi na tano
f) Pakua pilau ikiwa tayari

Orodha Ya Mambo

1. Mlolongo wa vitu vilivyoandikwa.

MAHITAJI MUHIMU YA KURUDI SHULENI TAREHE 5/1/2010

a) Sukari kilo mbili
b) Dawa ya meno ya gramu hamsini
c) Koko gramu 500
d) Sabuni sita za kipande
e) Kalamu nne za rangi
f) Penseli moja
g) Rangi ya viatu ya gramu 40

Tahakiki

1. Maandishi ya kuchambua maandishi ya fasihi.

USASA WAKUTANA NA UKALE

Anwani: Kitumbua Kimeingia Mchanga
Mwandishi: Said A. Mohamed
Mchapishaji: Oxford University Press
Mhakiki: Amina Fuzo
Maudhui

Meme

2. Barua ambazo huhusisha matumizi ya ya vifaa vya umeme kama talakilishi, kiepesi/nukulishi/faksi au simu ya mkonono/tamba/rukono.

Barua za Mdahilisi/Pepe

2. Ambazo hutumwa kwa tarakilishi kwa njia ya mtandao.

Ijumaa Machi 30, 2007 saa 08:09:19
Kutoka: aisha@yahoo.com
Kwa: ahmed@african online.ke
Nakala kwa: amina @ mwananchi.com
MINT/KUH:
Barua ya kawaida
Hitimisho: Aisha Kizito Makwere
Memo

3. Taarifa fupi ambayo huandikwa ofisini kuhusu mambo ya ndani kutoa maelekezo, maelezo au kukumbusha kuhusu jambo fulani. Ujumbe huwa mfupi na huhusu suala moja tu.

SHULE YA UPILI YA GATWE
Anwani
MEMO
REJ: km/01/06
KUTOKA: Mwalimu Mkuu
KWA: wafanyakazi wote
MADA: likizo fupi
TAREHE: 28/2/2011
Ujumbe
Sahihi
Jina
Cheo (mwalimu mkuu)

Taarifa

4. Kuarifu kuhusu habari mpya

UCHOCHEZI
Hitimisho
Mariga Mununga
Mwanahabari

Wasifu

5. Maelezo ya mtu kuhusu mtu mwingine tangu kuzaliwa mpaka alipo au kufa kwake.

WASUFU WA NDUGU YANGU JUMA

Tawasifu

6. Maelezo ya mtu kujihusu

TAWASIFU YANGU

Vidokezo

- ✓ Jina lake/lako
- ✓ Jinsia
- ✓ Anakotoka
- ✓ Umri
- ✓ Kuzaliwa
- ✓ Maumbile
- ✓ Elimu
- ✓ Kazi
- ✓ Hadhi ya ndoa
- ✓ Lugha
- ✓ Lakabu na sababu
- ✓ Umaarufu
- ✓ Uraibu

Wasifutaala/Wasifu Kazi

- Maelezo rasmi kuhusu mtu binafsi ambayo huambatanishwa na barua ya kuomba kazi.

WASIFUTAALA WANGU

MAELEZO BINAFSI

Jina : Farida Almasi Juma
Tarehe ya Kuzaliwa : 7-6-1980
Umri : miaka 22
Mahali pa kuzaliwa : Voi
Jinsia : mwanamke
Hadhi ya ndoa : **Nimeolewa/kapera**
Nambari ya kitambulisho : **12345678**
Uraia : **Mkenya**
Lugha : **Kiswahili, Kingereza, Kikuyu**
Anwani ya kudumu : **S.L.P. 1600, Voi**
Barua pepe : **Farial@yahoo.com**
Simu tamba : **9876543210**

ELIMU

Chuo Kikuu cha Maseno (Shahada ya Uhasibu)
Shule ya upili ya Shimoni (Shahada ya KCSE)
1978-1987 Shule ya Msingi ya Umazi (shahada ya KCPE)

TAJRIBA
Mpaka sasa Mhasibu katika shule chekechea ya Mtakatifu Yohana
HABARI ZA ZIADA
URAIBU

a) **Kusoma vitabu vya sarufi na fasihi**
b) **Kutembelea wajane, mayatima na wagonjwa**
c) **Kuandika mashairi**

AZIMIO LANGU

a) **Kupaa kitaaluma kwa kuendeleza masomo yangu hadi kiwango cha uzamifu**
b) **Kuwa mhasibu bora zaidi nchini kwa matendo na kuwapa wananchi huduma za kufaa**

WAREJELEWA

1. **Profesa Hassan Muoso,**
   Chuo Kikuu Kenyatta,
   S.L.P.43844,
   Nairobi.
2. **Maimuna Njavu Mukota,**
   Shule ya Upili ya Alliance,
   S.L.P. 1 234,
   Nairobi.

Kumbukumbu

- Maelezo kuhusu yaliyojadiliwa na kuafikiwa katika mkutano.

Muundo

- Kichwa (kumbukumbu za mkutano wa kamati/jopo gani, uliofanyika wapi, tarehe gani, saa ngapi hadi gani na majira)
- Waliohudhuria (mwenyekiti, katibu, mweka hazina, wanakamati)
- Waliotuma udhuru kwa kutohudhuria
- Waliokosa kutuma udhuru wa kutohudhuria
- waalikwa
- Ajenda

a) Kufunguliwa kwa mkutano (KUMB 3/2OO9)

- ✓ Kufunguliwa kwa mkutano, mwenyekiti kuwakaribisha na kuwashukuru waliohudhuruia na kumwomba … aongoze kwa maombi.

b) Kusoma na kudhibitisha kumbukumbu za mkutano uliotangulia

- ✓ Kusomwa na katibu, aliyependekeza na aliyedhibitisha.

c) Masuala yaliyotokana na kumbukumbu hizo

- ✓ (a) KUMB 8/2008 ununuzi wa miti

d) Shughuli nyinginezo

e) Kufunga mkutano (KUMB 7/2009)

- ✓ Mkutano uliisha saa ngapi, maombi yaliongozwa na nani, na mwingine ukapangwa kuwa wa siku gani.
- ▪ Maneo kama walikubaliana, waliafikiana, alipendekezwa, ilisemekana, waliambiwa, ilionelewa ni bora, walishauriwa, ilidaiwa, aliomba, n.k.

THIBITISHO

KATIBU TAREHE……. SAHIHI …….

MWENYEKITI TAREHE ……. SAHIHI …….

Ripoti

- ☟ Maelezo kuhusu mtu, kitu au tukio

a) Ripoti ya Kawaida

1. Swali huanzia kwa ‘Wewe kama katibu wa chama…'

Muundo

- ▪ Kichwa (ripoti ya kamati/jopo gani)
- ▪ Utangulizi (maelezo mafupi ya jumla kuhusu chama)
- ▪ Shughuli za chama (i, ii, iii)
- ▪ Hitimisho (matumaini, mwito kwa wengine wajiunge, wajitahidi)
- ▪ Ripoti imeandikwa na (jina, cheo/katibu, sahihi, tarehe)

b) Ripoti Maalum

- ▪ Kichwa (ripoti ya jopo la kutathmini usalama barabarani)

- Utangulizi/Hadidu za rejea (ripoti ilihitajika na kamati gani, uchunguzi ulifanywa kubainisha nini, matokeo kuelezewa chini pamoja na mapendekezo kutolewa)
- Jopo (majina na vyeo vya wanajopo waliohusika)
- Utaratibu/ hatua za utafiti (wanakamati walifanya nini (kamati iliwahoji…ilifanya ukaguzi wa magari, iliwapa baadhi ya wasafiri hojaji wakajaza, ilipiga picha za video, mashauriano)
- Matokeo (kamati iligundua kuwa: (a)
- Mapendekezo (suluhisho la shida)
- Hitimisho (ripoti imeandikwa na, sahihi, jina, cheo/katibu, tarehe 21 Machi 2011.

3. UTUNGAJI WA/INSHA ZA KISANII

a) michezo ya kuigiza
b) hadithi fupi
c) mashairi
d) mafumbo
e) vitanza ndimi

USHAIRI

Istilahi za Kishairi

1. arudhi
   - sheria za jadi zzinazofuatwa na watunzi wa mashairi:
     a) kugawa shairi katika beti
     b) beti kugawika katika mishororo inayolingana kiidadi
     c) mishororo kugawika katika vipande
     d) mishororo kuwa na mizani zinazolingana kiidadi (urari wa mizani)
     e) kuwa na vina vya kati na vya mwisho vinavyotamkika kwa namna sawa (urari wa vina)
     f) mtoshelezo wa beti au beti kutoa wazo kamili
2. bahari
   - aina tofauti tofauti za mashairi k.m. ukara
3. ubeti/beti
   1. kifungu katika shairi kinachojitosheleza kimaaa

4. mshororo
   - mstari katika ubeti
5. mwanzo
   - mshororo katika ubeti
6. mloto
   - mshororo wa pili katika ubeti
7. mleo
   - mshororo wa tatu katika ubeti
8. kimalizio
   - mshororo wa mwisho ambao haurudiwi katika kila ubeti
9. kibwagizo/mkarara/kipokeo/kiitikio
   - mshororo wa mwisho ambao hurudiwarudiwa katika kila ubeti na hubeba maudhui au kiini cha shairi.
10. kipande/mgao
    - sehemu katika mshororo ambayo huonyeshwa na koma na huwa na kina
11. ukwapi
    - kipande cha kwanza katika mshororo
12. utao
    - kipande cha pili katika mshororo
13. mwandamizi
    - kipande cha tatu katika mshororo
14. mizani
    - silabi zinazotamkika katika mishororo
15. urari wa mizani
    - kuwepo kwa idadi sawa ya mizani katika mishororo
16. kina/vina
    - silabi zinazotamkika kwa namna sawa zinazopatikana katikati na mwishoni mwa sentensi.
17. urari wa vina/vue
    - kuwepo kwa silabi zinazotamkika kwa namna sawa

Aina za Mashairi

a) mashairi la arudhi/ushairi wa kijadi
   1. Ambayo huzingatia sheria za jadi za utunzi wa mashairi.

b) mashairi huru

- Ambayo hayazingatii sheria za jadi za utunzi wa mashairi.

Mashairi ya Arudhi

a) Aina

i. tathmina (mshororo mmoja katika kila ubeti)
ii. tathnia (miwili)
iii. tathlitha (mitatu)
iv. tarbia (minne)
v. takhmisa (mitano)
vi. tasdisa (sita)
vii. ushuri (kumi)

b) Bahari

viii. mtiririko (mfanano wa vina vya kati na vya mwisho katika shairi zima)
ix. ukara (vina vya mwisho kufanana na vya kati kutofautiana)
x. ukaraguni (vina vya kati na vya mwisho kutofautiana katika shairi zima)
xi. kikwamba (mishororo kuanza kwa neno fulani katika shairi zima)
xii. pindu (neno au maneno mawili ya mwisho ya kila mshororo kutumiwa kuanzia mshororo unaofuata) k.m. kicha changu wachezea. Wachezea kichwa changu.
xiii. Tenzi/tendi (mgao mmoja, kina kimoja)
xiv. Mathnawi (migao miwili, vina viwili)
xv. Ukawafi (migao mitatu, tumbuizo 8,8,8)
xvi. Ngonjera (majibizano)
xvii. Malumbano (kujinaki/kuonyesha ugwiji akimdunisha mshairi mpinzani ili kutaniana)
xviii. Msuko (mshororo wa mwisho mfupi kuliko inayotangulia)
xix. Sakarani (mchanganyiko wa bahari)
xx. Dura mandhuma (kauli/swali katika ukwapi na mjalizo/jibu katika utao k.m. shida zikishinda, hazishindiki. Unalolipenda, halipendeki. Unapopaenda, hapaendeki)
xxi. Gungu (mizani 12, kina kimoja cha mwisho)

xxii. Upeo (mishororo inayozidiana ki mizani)
xxiii. Kikai (mizani 12, 4:8 au 8:4, hakuna ulinganifu wa mizani katika ukwapi na utao)
xxiv. Zivindo (hutoa maana tofauti za neno k.m.
xxv. Sumbila (kila ubeti una kimalizio tofauti na beti nyingine)

c) Muundo/Umbo/Sura ya Nje

xxvi. Kutaja idadi ya beti
xxvii. Mishororo mingapi katika kila ubeti
xxviii. Vipande vingapi katika kila mshororo-aina
xxix. Mpangilio wa mizani na jumla k.m. ukwapi 8, utao 8, jumla 16.

8 8
8 8
8 8
8 8

xxx. Mpangilio wa vina au kufanana, kutofanana katika shairi zima au vina vya mwisho kufanana na vya kati kutofautiana-bahari

na ma
na ma
na ma
ka ba

Vina na Mizani

8a 8b
8a 8b
8a 8b
8c 8b

xxxi. Kibwagizo(linacho au halina. Kinakili kama kipo)
xxxii. Majibizano (ngonjera)
xxxiii. Malumbano (majinaki)

d) Uhuru/Idhini za Kishairi

1. kibali mshairi alichonacho kukiuka sheria fulani.

i) Inkisari (kufupisha ili kuwe na urari wa mizani na vina. Aghalabu huonyeshwa kwa matumizi ya ritifaa k.m. ‘sikate-usikate)

xxxiv. Mazda/mazida (kurefusha neno ili kuwa na urari wa mizani na vina)

xxxv. Tabdila (kubadilisha tahajia ya neno bila kuzidisha au kupunguza mizani k.m. siachi-siati)
xxxvi. Utohozi
xxxvii. Kuboronga/kufinyanga sarufi (kubadili mpangilio wa maneno katika sentensi k.m. upesi jielimishe)
xxxviii. Kiswahili cha kikale/ujadi (mtima, ngeu, insi, mja)
xxxix. Lahaja k.m. ficha-fita
xl. Matumizi ya ritifaa

e) Lugha ya Nathari

- lugha ya kawaida na kimtiririko
  - ✓ Kutotumia koma au vipande
  - ✓ Kutumia maumbo ya kawaida ya maneno
  - ✓ Ubeti kutengewa aya moja
  - ✓ Kuondoa uhuru na kusanifisha lahaja na kikale

f) matumizi ya lugha/fani
g) matumizi ya maneno (kama yalivyotumiwa)
h) ujumbe
i) maudhui
j) dhamira

- kusimanga, kusuta, kudharau, kusifu, kufunza, n.k.

Mashairi Huru

Sifa/Mbinu

a) urudiaji
   i) wa neno (takriri neno)
   ii) wa kifungu (usambamba)

   Umuhimu

   1. kusisitiza ujumbe
   2. kutia ridhimu/mapigo fulani katika usomaji

b) mishata
   1. mishtari ambayo haikamiliki. Mistari toshelezi ni mistari iliyokamilika.

c) sehemu za beti kuingizwa ndani

   Umuhimu

   - ✓ ili kusisitiza
   - ✓ kuzifanya zionekane wazi

Ulinganishaji wa Shairi la Arudhi na Shairi Huru

Kufananisha

a) yote mawili ni sanaa ya ushairi
b) mishororo kupangwa katika beti
c) yametumia mbinu za lugha za namna moja
d) alama za kuakifisha zinazofanana
e) kufanana kimuundo
f) uhuru wa kishairi

Kutofautisha

a) moja ni la arudhi jingine ni huru
b) mishata
c) sehemu za beti kuingizwa ndani
d) kuwa au kutokuwa na urari wa mizani
e) kuwa au kutokuwa na urari wa vina
f) tofauti kimaudhui
g) idadi ya beti
h) idadi ya mishororo katika beti
i) vipande
j) kutumia alama za uakifishi tofauti
k) uhuru wa kishairi

MASUALA IBUKA

Magonjwa

Aina

d) malaria
e) mafua
f) macho
g) ngozi
h) meno
i) kifua kikuu
j) homa ya mapafu
k) kifaduro
l) zinaa (kaswede/syphilis)
m) kipindupindu
n) homa ya matumbo
o) homa ya mapafu
p) shinikizo la damu
q) ugonjwa wa moyo
r) matumbwitumbwi/machapwi
s) saratani

t) utapia mlo
u) ukambi/surua
v) tetewanga
w) homa
x) malale

Jinsi ya Kujikinga na Magonjwa

- ✓ Kula chakula chenye virutubisho vyote na madini
- ✓ Kutotumia chumvi, sukari au mafuta mengi
- ✓ Kufanya mazoezi
- ✓ Kupimwa mara kwa mara
- ✓ Kupika vyakula vizuri
- ✓ Kunawa mikono na macho
- ✓ Kuchemsha maji au kuyatia dawa kabla ya kuyanywa
- ✓ Kutozini au kutumia kinga
- ✓ Chanjo kwa watoto
- ✓ Kutochangia vifaa kama vitana na nyembe na mavazi ili kujikinga na magonjwa ya ngozi.
- ✓ Kulala ndani ya neti iliyotiwa dawa
- ✓ Kufyeka nyasi karibu na nyumba na kutupa mikebe iliyo na maji
- ✓ Kuweka dawa kwenye vidimbwi ili kuua mbu
- ✓ Kutotumia vileo kama vile pombe na sigara
- ✓ Kuzuia kunyeshewa na mvua na kuvaa mavazi mazito wakati wa baridi au usiku
- ✓ Kukohoa au kupiga chafya mtu akiwa ameziba pua na midomo na kutotema kikohozi ovyo
- ✓ Kutubu dhambi, kujua Mungu na kuomba kwa afya ya kiroho

Ukimwi

- Ugonjwa unaosababishwa na virusi vya HIV unaofanya mwili kupungukiwa na kinga dhidi magonjwa.

Njia za Maambukizi

a) Uzinzi, ubakaji au ulawiti
b) Tohara ambapo ngariga anatumia kisu kimoja kwa watahiriwa wote
c) Kuchangia vifaa vyenye ncha kali k.v. nyembe, vinyoleo n.k.

d) Utumiaji wa sindano moja na vifaa vya upasuati ambavyo havijatiwa dawa au kutokoswa ili kuua viini
e) Wanawake kuambukiza watoto wakijifungua
f) Kuongezewa damu ambayo haijapimwa au haijapimwa vizuri.
g) Utumiaji wa dawa za kulevya kwa kujidunga kwa sindano moja
h) Ulevi kumfanya mtu kupotewa na utambuzi kisha kufanya ngono na mtu aliyeambukizwa.
i) Kubusu mtu aliye na virusi ukiwa na vidonda kinywani
j) Wakati wa ajali watu walio na viini wanapojeruhiwa na kutokwa na damu na inafikia majeraha katika miili ya wasio na hivyo viini

Dalili

- ✓ Kukohoa kwa muda mrefu
- ✓ Kuendesha kwa muda mrefu
- ✓ Kupoteza hamu ya kula
- ✓ Kukonda au kupoteza uzani wa zaidi ya kilo 10 kwa muda mfupi
- ✓ Mwili kudhoofika/unyonge
- ✓ Kunyonyoka nywele
- ✓ Jipu lmwilini
- ✓ Mwasho mkali katika ngozi
- ✓ Vidonda kinywani na kooni
- ✓ Homa na kutokwa na jasho jingi usiku
- ✓ Magonjwa ya kifua kikuu na homa ya mapafu
- ✓ Saratani ya ngozi
- ✓ Kuvimba shingoni
- ✓ Utaahira wa akili k.v. kusahau na kutokumbuka mambo

Madhara

- ✓ Jamaa kuathirika kisaikolojia wakiona mtu wao akiteseka na ugonjwa
- ✓ Vifo kwa kuzidiwa na ugonjwa
- ✓ Huzuni baada ya mgonjwa kuaga dunia
- ✓ Watoto kuachwa wakiwa mayatima baada ya wazazi kufa
- ✓ Gharama kubwa ya kugharamia matibabu

- ✓ Unyanyapaa/kutengwa/kubaguliwa
- ✓ Ndoa kuvunjika kutokana na lawama
- ✓ Ubakaji wa watoto wa kike ili kujitakasa
- ✓ Kuathiri uchumi wa nchi pesa nyingi zinapotumiwa kununulia dawa za kupunguza makali hata za kifua kikuu
- ✓ Serikali kupoteza wataalamu iliyogharamia elimu yao kulazimika kuajiri wataalamu kutoka nje kwa gharama ya juu sana

Jinsi ya Kujikinga

- ✓ Kutofanya zinaa kabla na nje ya ndoa
- ✓ Walioambukizwa kutumia dawa za kupunguza makali (A.R.Vs)
- ✓ Aliyebakwa kupewa dawa za A.R.V kabla ya saa 72
- ✓ Kuwapa mama waja mzito wenye virusi dawa kabla ya kujifungua kukinga mtoto
- ✓ Ngariba kutotumia kisu kimoja kwa watahiriwa wote
- ✓ Kutumia sindano mpya hospitalini na matumizi ya dawa za kulevya
- ✓ Kupima damu vizuri kabla ya kuwaongezea wagonjwa
- ✓ Kupimwa kabla ya ndoa na mara kwa mara ili kujua hali ili kujikinga dhidi ya maambukizi au kujitunza kama mtu ameambukizwa
- ✓ Kutumia mipira
- ✓ Walioambukizwa kutofanya mapenzi bila kinga ili wasipate virusi aina tofauti na sugu au magonjwa mengine ya zinaa
- ✓ Kula chakula vinavyofaa na kufanya mazoezi
- ✓ Kupata matibabu wakati ufaao mtu anapougua magonjwa mengine
- ✓ Kumjua Mungu ili kumwamini na kumtumainia ili kuondoa uoga na mahangaiko na hivyo kumwezeha mtu kuishi siku zaidi

Unyanyasaji/Udunishaji wa Wanawake na Utamaduni/Taasubi ya Kiume

- ✓ Kutorithi mali
- ✓ Wanawake wajane kunyang'anywa mali na kufukuzwa
- ✓ Ndoa za wake wengi (uke wenza)

- ✓ Kupata watoto wengi
- ✓ Kurithi wanawake
- ✓ Kupashwa tohara
- ✓ Kutawishwa au kunyimwa uhuru wa kutoka
- ✓ Kutoelimishwa eti kwa akiolewa hatafaidi familia, atapanda wanaume vichwa au atakuwa malaya
- ✓ Ndoa za mapema/lazima zinazosababisha kukatiza elimu yake (mahari haiwezi kurudishwa)
- ✓ Kulazimishwa kuolewa na mtu asiyempenda
- ✓ Kunyimwa haki ya kusema
- ✓ Kupigwa na kutusiwa
- ✓ kubakwa
- ✓ Kutalikiwa
- ✓ Wanaume kutokuwa waminifu kwao hata kuwanyima mahitaji na kuwapa mahawara zao
- ✓ Wanaume kupuuza majukumu ya kukimu familia
- ✓ Ubadhirifu wa wanaume na hali wake zao ndio walifanya kazi za kupatia hizo pesa
- ✓ Kubughudhiwa
- ✓ Kulaumiwa mtoto akikosekana hata mke mwingine kuolewa
- ✓ Mahali pa mwanamke kuwa nyumbani au haruhusiwi kufanya kazi ofisini au kuongoza
- ✓ Kulazimishwa kuvaa mavazi aina fulani na kukatazwa kuvaa aina mengine
- ✓ Kufanyishwa kazi za nyumbani kama mtumwa

1. Kudhibitiwa na wanaume zao kwa sababu ya vivu.
2. Kunyimwa ajira kwa vile akipata mimba atajikokota kazini na atahitaji likizo baada ya kujifungua.
3. Ajira ya mtoto wa kike ambapo anafanyishwa kazi ya sulubu na kupewa mshahara duni

Suluhisho

1. Hatua kali za kisheria kwa wanaowapiga, wanaowabaka na wanaotekeleza mila ya tohara na ndoa za mapema
2. Kufanya kampeni dhidi ya mila zinazochangia udunishaji wa wanawake

3. Kuwashauri watoto wa kike badala ya kuwapasha tohara
4. Kuanzisha makao ya watoto wa kike wanaotishiwa na mila mbaya
5. Kumwelimisha mwanamke kuhusu haki zake
6. Kuhimiza wanawake kupigania haki zao
7. Serikali kutenga pesa za kuelimisha watoto wa kike ili kuwapa uwezo wa kiuchumi kwani wengi hunyanyaswa kutokana na umaskini na ujinga.
8. Mashirika ya kutetea haki za wanawake kama FIDA na Maendeleo ya Wanawake.
9. Hazina ya kutoa mikopo kwa makundi ya wanawake k.v. K.W.F.T
10. Kuwapa wanawake nafasi sawa za ajira na katika uongozi.
11. Kupunguza alama ambazo wasichana wanazopaswa kufikisha ili kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.
12. Kubuni sheria za kuwawezesha kumiliki mali

Jinsi Wanaume Wanavyodhulumiwa

1. Kupigwa
2. Kuchomwa kwa maji moto
3. Kukatwa sehemu nyeti
4. Wanawake kutokuwa waminifu kwao
5. Kutusiwa
6. Kutofuliwa nguo
7. Kunyimwa chakula
8. Kunyimwa unyumba kama njia ya kulipiza kisasi au kumwadhibu
9. Kufanyishwa kazi fulani k.v. kufulishwa nguo na kupikishwa mke akiwepo hata mbele ya wageni
10. Kuzomewa/ kugombezwa
11. Kunyimwa pesa kama hana ajira

Ufisadi

- Uovu, ubaya au uharibivu.

Aina

1. Wanafunzi kudanganya katika mtihani
2. Kufanyiwa mtihani na watu wa nje

3. Kutoza mwanafunzi wa kidato cha kwanza pesa au chakula kama nyama ili kuwalinda.
4. Kujipakulia chakula kingi.
5. Waalimu wakuu kuitisha hongo ili kuruhusu wanafunzi wajiunge na shule zao
6. Kupita wengine katika foleni wanapokwenda kupata chakula au chai hata benki
7. Kurudishiwa bakaa/chenji nyingi dukani na kutoirejesha kwa muuza duka.
8. Kuokota pesa njiani na kutoulizia ni za nani
9. Kughushi stakabadhi za mtihani, hati za umiliki shamba
10. Kunakili kanda za muziki za wengine na kuziuza
11. Waajiri kuajiri watu wa familia zao au makabila yao
12. Daktari kuitisha hongo ili amhudumie mgonjwa
13. Polisi kuitisha hongo ili aruhusu magari ya huduma kwa umma yasiyofaa kupita
14. Kutohoa maziwa au kuyaongezea maji ili yawe mengi
15. Wenye maduka kuuza bidhaa kwa bei ghali
16. Kuuza bidhaa kama sukari, nyama, nafaka, gesi na mafuta ya petroli ambazo hazijatimiza uzani unaotakikana
17. Madereva wanaoendea mafuta ya petroli kuuza kiwango fulani cha hayo mafuta na kuongezea ya taa au diseli
18. Kuuzia watu dawa bandia zisizotibu magonjwa
19. Ulanguzi wa dawa za kulevya
20. Kuiba pesa kwa kutumia risiti bandia au kufuruisha bei za bidhaa ili pesa zilizo juu wahusika wagawane
21. Kutoa ushahidi wa uongo
22. Kunyang'anya wajane na yatima mali zao
23. Uporaji wa mali ya umma k.v. nyanja za kuchezea watoto na misitu
24. Hakimu kuchukua hongo aididimize kesi

25. Madaktari kutoza wawele ada ya juu hata kuwafanyia upassuaji wasiouhitaji ili wapate pesa.

26. Wafanyakazi wa halmashauri za miji kujificha wanapomwona mtu akiegesha gari ili wadai anakwepa kulipa ada ya uegeshaji ili wahongwe au walikokote gari wapate pesa zaidi.

Sababu Ya Watu Kuushiriki Ufisadi

- ✓ Tamaa ya kutajirika
- ✓ Kutofahamu madhara/matokeo yake
- ✓ Kukosa njia za kukimu mahitaji
- ✓ Mishahara au mapato duni yasiyomwezesha mtu kukimu mahitaji yake au ya familia
- ✓ Kutotosheka kwa kile mtu alichonacho
- ✓ Hofu ya kupata hasara au kukosa ajira
- ✓ Kutomjua mungu hivyo hawana imani
- ✓ Kuzugwa au kutekwa nyara kimawazo na kuwa mtumwa na shetani
- ✓ Wengine hulichukulia kama jambo la kawaida tu au hali ya maisha
- ✓ Imani kuwa siku hizi mtu hawezi kupata chochote bila kutoa hongo

Madhara

- ✓ Vifo kutokana na aajali barabarani au kutotibiwa bila hongo
- ✓ Majeruhi wa ajali za ajalini wengine hulemaa wasiweze kujifanyia kazi zao
- ✓ Kufutiliwa kwa matokeo ya mtihani
- ✓ Kufukuzwa shuleni au chuoni
- ✓ Umaskini kutokana na utoaji hongo ya pesa nyingi kisha kutopata kazi na ununuzi wa bidhaa kwa bei ghali
- ✓ Kushuka kwa viwango vya elimu wasiohitimu ipasavyo wanaporuhusiwa kujiunga na shule ama vyuo fulani
- ✓ Kushuka kwa viwango vya huduma kwa umma kutokana na kuajiriwa kwa watu ambao hawajahitimu vizuri.
- ✓ Afisi za serikali kuchomwa wafisadi wakijaribu kusitiri ushahidi wa ufisadi

- ✓ Nchi kurudishwa nyuma kiuchumi na kimaendeleo kutokana na pesa za miradi au ambazo zingewekezwa katika vitega uchumi kuporwa
- ✓ Kupoteza ajira baada ya kufutwa kazi kutokana na ufisadi
- ✓ Familia kuteseka baada ya kupoteza ajira
- ✓ Kufungwa jela kwa wanaopatikana na kosa la ufisadi
- ✓ Uharibifu wa mazingira na madhara yanayoendana nao kutokana na ufyekaji wa misitu
- ✓ Kudidimiza haki pale kesi inakatwa vibaya kutokana na hongo hata asiye na makosa aweza kufungwa
- ✓ Viongozi wafisadi katika mashirika na asasi kupoteza nyadhfa

Suluhisho/Njia za Kuukabili Ufisadi

- ✓ Hatua kali kisheria kwa wafisadi
- ✓ Kulipa wafanyakazi mishahara mizuri
- ✓ Kuelimisha kuhusu madhara ya usisadi
- ✓ Kufuta kazi wafisadi
- ✓ Kunyang'anywa pesa au mali walizopata kifisadi
- ✓ Watu kutangaza mali zao k.v. kwa kujaza fomu kudhihirisha hayo
- ✓ Shirika la kukagua vipimo na ubora wa bidhaa
- ✓ Majina ya wafisadi kutangazwa hadharani
- ✓ Ukaguzi wa hesabu za matumizi ya pesa katika asasi za serikali
- ✓ Shirika la kupambana na ufisadi
- ✓ Kufumania wafisadi
- ✓ Kupiga picha kwa kamera ya video wafisadi k.v. polisi wakichukua hongo
- ✓ Kujifunza kutosheka kwa kile mtu alichonacho na kuishi maisha ya kiwango chake.
- ✓ Kuarifu polisi au shirika la mkupambana na ufisadi kuhusu visa vya ufisadi
- ✓ Kumjua na kumcha Mungu

Dawa za Kulevya/Mihandarati

- ☟ Dawa ambazo huathiri utendakazi wa mwili.

Sababu za Kutumiwa

- ✓ Masurufu au kuwapa vijana pesa nyingi za matumizi

- ✓ Kujipa burudani
- ✓ Shinikizo la rika kwa vijana
- ✓ Ukosefu wa ushauri/kutojua madhara
- ✓ Matangazo ya biashara
- ✓ Shida k.v. ukosefu wa ajira na mahitaji ya kimsingi
- ✓ Marafiki wabaya
- ✓ Kukaa katika mazingira zinamotumiwa
- ✓ Malezi
- ✓ Kuvunjika kwa ndoa
- ✓ upweke
- ✓ Kujitoa haya k.m. makahaba
- ✓ Shida kazini
- ✓ Kudanganywa zina manufaa k.m. kumpa mtu nguvu ya kufanya kazi au kuerevusha
- ✓ Kujipa hisia za kuwa huru na ujitambuaji

Madhara

- ✓ Magonjwa k.v. saratani na ya zinaa
- ✓ Vifo kutokana na ajali, magonjwa au dawa zenyewe
- ✓ Kuiba ili kupata pesa za kununulia dawa za
- ✓ Ubakaji
- ✓ Hufilisi watu kwa kutumia pesa nyingi hata kuuza au kuzikodisha mali zao ili kuzigharamia
- ✓ Jamaa kuathirika kisaikolojia wanapoona mwenzao akiKushindwa kuendelea na masomo.
- ✓ Visa vya ubakaji.
- ✓ Kupotoka kimaadili k.m. kuwa mwenye matusi, kupiga wengine, kuwa mgomvi hata mzinifu.
- ✓ Kuwa mchafu kama fungo k.m. kutooga, kutofua nguo, kutochanua nywele n.k.
- ✓ Kuhisi mambo yasiyokuwepo (hallucination).
- ✓ Wengine kushindwa kuolewa na kutoweza kupata watoto k.m. watumiaji wa miraa.
- ✓ Kuvunjika kwa ndoa kutokana na kupiga mke, kutumia pesa vibaya.
- ✓ Kufutwa kazi k.m. kutokana na ulevi.
- ✓ Wazimu
- ✓ Uhalifu

- ✓ Jamaa ya mtumizi kuteseka ikimwona mwenzao akiangamia kutokana na kuzitegemea dawa za kulevya
- ✓ Mhusika huathirika kimwili na kisaikolojia
- ✓ Huathiri ukuaji wa mwili na akili
- ✓ Wazimu
- ✓ Huathiri uwezo wa kufikiri kwa kuua seli za ubongo
- ✓ Hufanya mtu kupotoka kimaadili k.m. upyaro, vita, uchoyo, uzinifu
- ✓ Kuvunjika kwa ndoa
- ✓ Kufukuzwa shuleni
- ✓ Kufungwa jela
- ✓ Kuzaa watoto ambao hawajatimiza uzani wa wastani
- ✓ Kufa kwa neva na viungo kukatwa

Suluhisho

- ✓ Kuelimisha watu kuhusu madhara ya dawa za kulevya
- ✓ Watu kumjua Mungu
- ✓ Matibabu ya kurekebisha watumwa wazo
- ✓ Kujitenga na marafiki wabaya
- ✓ Kutoingia katika mandhari zinamotumiwa
- ✓ Maelekezo kuhusu dawa za matibabu kufuatwa ipasavyo
- ✓ Kutotumia dawa za matibabu kwa matumizi mengine yasiyo ya kutibu
- ✓ Ukaguzi wa wageni na mizigo katika viwanja vya ndege
- ✓ Hatua za kisheria kwa walanguzi, wauzaji na watumiaji
- ✓ Kuongeza nafasi za ajira
- ✓ Kukomesha matangazo ya biashara ya dawa hizo
- ✓ Kuandika matahadharisho katika chupa na pakiti za vileo

Uhalifu/Utovu wa Usalama

Chanzo

- ✓ Umaskini kusababisha wizi na uisadi
- ✓ Dawa za kulevya kusababisha wizi au kubaka
- ✓ Marafiki wabaya
- ✓ Malezi mabaya

- ✓ Malezi mabaya k.m. mtoto akiiba na kupelekea wazazi, wazazi hawamuulizi alikotoa vitu hivyo.
- ✓ Tamaa ya mali kufanya watu kuiba, kushiriki ufisadi, n.k.
- ✓ Hasira au kushindwa kujidhibiti kusababisha kumpiga na kumuumiza mtu hata kumuua
- ✓ Tamaa kubwa au uchu kusababisha ubakaji.
- ✓ Chuki na wivu huweza kusababisha mauaji

Suluhisho

- ✓ Hatua kali za kisheria
- ✓ Kuongeza askari kwani idadi yao ni dogo ikilinganishwa na raia
- ✓ Kuunda vikundi vya kujilinda
- ✓ Vituo vya polisi kuongezwa
- ✓ Vitu vya thamani kuwekwa mahali salama k.m. benki
- ✓ Kutotembea nyakati za usiku
- ✓ Kutoendea mahali kusikofaa k.v. vichochoroni
- ✓ Kuweka ua na lango
- ✓ Mavazi yanayofaa kuzuia ubakaji
- ✓ Kutoa mafunzo ya kujikinga
- ✓ Nambari za simu za dharura za kuripotia uhalifu
- ✓ Kumjua Mungu
- ✓ Kuongeza nafasi za ajira

Haki za Binadamu

- ✓ Kuishi
- ✓ Kuingiliana/kutangamana
- ✓ Uhuru na usawa
- ✓ Elimu
- ✓ Makazi
- ✓ Afya
- ✓ Kiwango cha kurithisha cha maisha
- ✓ Chakula
- ✓ Kuabudu
- ✓ Ajira ya watoto
- ✓ Kufanya kazi
- ✓ Kumiliki mali
- ✓ Kutunzwa uzeeni/ hifadhi ya jamii/wasio na uwezo
- ✓ Kupiga kura

- ✓ Kutobaguliwa
- ✓ Kutoteswa kuminya habari
- ✓ Uhuru wa kuongea/usemi
- ✓ Kutembea na kuishi popote
- ✓ Kesi kuendeshwa kwa haki
- ✓ Kujitetea
- ✓ Kuoa au kuolewa na unayemtaka
- ✓ Utulivu k.m. mtoto au mke asipigwe ama kuteswa
- ✓ Huduma za matibabu
- ✓ Jina na utaifa wakati wa kuzaliwa
- ✓ Mtoto mlemavu apewe huduma maalum
- ✓ Alindwe kutokana na mateso, kazi ya sulubu na kuhusishwa vitani
- ✓ Alindwe dhidi ya mila na tamaduni zisizofaa
- ✓ Haki ya kupata burudani
- ✓ Haki ya faragha/ kuhifadhi siri zake
- ✓ Asiajiriwe
- ✓ asiteswe

Jinsi ya kuwalinda na kuwatunza watoto

- ✓ Sheria kubuniwa za kuwalinda
- ✓ Hatua kali kisheria kwa wanaodhulumu watoto
- ✓ Shirika la kupigania haki za watoto
- ✓ Makao ya watoto wanaokimbia wa dhuluma
- ✓ Hazina ya wizara na maeneo bunge ya kufadhili watoto maskini (bursary)
- ✓ Watoto kuelimishwa kuhusu haki zao
- ✓ Kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda mtoto
- ✓ Elimu ya bure ili watoto maskini wafaidi
- ✓ Shule maalum kwa watoto walemavu
- ✓ Wananchi kuchanga kusaidia watoto maskini
- ✓ Makanisa kusaidia watoto yatima
- ✓ Shule kuwapa watoto maskini ufadhili

Mazingira

- ☟ Hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anakoishi.

Jinsi Yanavyoharibiwa

- ✓ Kufyeka misitu ili kupata mahali pa makazi ama kulima

- ✓ Kufuga mifugo kupita kiasi
- ✓ Kutupa taka ovyoovyo
- ✓ Moshi kutoka katika magari na viwanda huchafua hewa
- ✓ Dawa na mbolea za kemikali za kilimo huchafua udongo na maji.
- ✓ Migodi kuacha mashimo ardhini ambayo hujaa maji na kuwa hatari kwa binadamu na kizalio cha mbu.
- ✓ Kelele za vyombo vya mziki, viwanda, honi za magari na ndege
- ✓ mafuriko kuchanganya choo pamoja na maji safi
- ✓ Taka kutoka nyumbani na viwandani kuelekezwa mitoni.

Madhara

- ✓ Ongezeko la joto duniani
- ✓ Mvua za gharika
- ✓ Uhaba wa mvua
- ✓ Ukame na njaa
- ✓ Uhaba wa maji
- ✓ Kufa kwa wanyama wa majini kama samaki
- ✓ Magonjwa na vifo kutokana na kuathiriwa na maji machafu
- ✓ Magonjwa ya mapafu kutokana na hewa chafu

Suluhisho

- ✓ Kupanda miti kusiko na miti na kule misitu imefyekwa
- ✓ Elimu kuhusu madhara ya kuharibu mazingira na jinsi ya kuyatunza Uhaba wa maji.
- ✓ Kukagua viwabda na hatua za kisheria kama vinavyoachilia taka katika mazingira
- ✓ Kutumia samadi badala ya mbolea za kemikali na dawa za kiasili kuua wadudu katika mimea na mifugo
- ✓ Kutaifisha misitu
- ✓ Askari wa kulinda misitu
- ✓ Kutumia kawi mbadala na ambazo hazichafui mazingira k.v. kutokana na maji na jua
- ✓ Mashimo na mapipa ya kutupa taka
- ✓ Kuweka mifugo kulingana na eneo la malisho

- ✓ Kutolima kando ya mito
- ✓ Kutia choo cha binadamu dawa kabla ya kukiachilia mitoni
- ✓ Kutumia magari ya umma
- ✓ Kutumia taka kama malighafi na kutumia vile vitu vyaweza kutumika tena

Usalama Barabarani

Vyanzo vya ajali

- ✓ Madereva kutohitimu vizuri
- ✓ Magari mabovu
- ✓ Kutotii sheria za barabarani
- ✓ Njia mbovu
- ✓ Kubeba abiria na mizigo kupita kiasi
- ✓ Kuendesha magari kwa kasi
- ✓ Waabudu shetani kusababisha magari kupoteza mwelekeo
- ✓ Kupita magari mengine bila uangalifu
- ✓ Ulevi
- ✓ Wenda miguu kutokuwa waangalifu wanapovuka barabara
- ✓ Kutodhibiti usukani vizuri
- ✓ Uchovu kusababisha usingizi
- ✓ Dawa za matibabu
- ✓ Abiria kutolalamika au hata kumwambia dereva aendeshe kwa kasi wafike haraka
- ✓ Kuchanganyikiwa

Suluhisho

- ✓ Hatua za kisheria kwa wakiukaji kanuni za barabarani
- ✓ Kuondoa polisi wafisadi barabarani
- ✓ Kukarabati barabara
- ✓ Ukaguzi wa magari ili kuhakikisha yafaa kuwa barabarani
- ✓ Kufunza madereva upya
- ✓ Mikanda au mishipi ya kujifunga kuzuia kujeruhiwa vibaya na vifo ajali ikitokea
- ✓ Kuweka vidhibiti mwendo
- ✓ Vifaa vya kutambulia madereva walevi na kasi ya magari

- ✓ Uangalifu wakati wa kupita magari mengine
- ✓ Kuwa mwangalifu wakati wa kuvuka barabara

Sayansi na Teknolojia

- ✓ Uvumbuzi wa umeme unaotumiwa kuangazia na kuendesha vyombo vingi
- ✓ Matibabu kuwezesha watu kuishi kwa muda mrefu k.m. dawa,chanjo, upasuaji, upachikwaji viungo, miale ya kutibu saratani, n.k.
- ✓ Kurahisisha na kuharakisha usafiri k.m. magari, pikipiki, ndege, k.m.
- ✓ Kurahisisha na kuharakisha mawasiliano kunakosaidia wakati wa dharura k.m. rununu, mtandao, nukulishi, n.k.
- ✓ Upashaji wa habari kuwezesha kupata habari kutoka kote duniani k.m. satalaiti, mtandao, redio, runinga, n.k.
- ✓ Utengenezaji bidhaa viwandani kuharakishwa kutokana na mitambo inazoendesha na tarakilishi
- ✓ Mimea na mifugo wanaokomaa haraka na walio na mazao mengi
- ✓ Roketi inayowezesha kwenda katika mwezi na sayari nyingine
- ✓ Silaha kama bunduki za kupambana na maadui na wahalifu
- ✓ Burudani bora k.m. sidi, video, mtandao, n.k.

Madhara

- ✓ Uavyaji mimba
- ✓ Mauaji ya huruma
- ✓ Tishio la dunia kuangamia kutokana na silaha za nuklia na viini vinavyotengezezewa maabarani
- ✓ Uhalifu kuongezeka kutokana na wingi wa bunduki, simu na mtandao
- ✓ Vyakula kutokana na mimea ina mifugo iliyokuzwa kisayanzi kudhuru afya
- ✓ Wizi wa viungo vya mwili hata kuhasiwa bila hiari
- ✓ Ajali za barabarani na za ndege zinazoua watu wengi
- ✓ Upotoshaji kimaadili kama vile filamu chafu katika mitandao na sidi

- ✓ Kutumia vijusi kutengenezea viungo
- ✓ Ongezeko la joto duniani kutokana na uchafuzi wa hewa
- ✓ Ugaidi kutokana unaotekelezwa kwa mabomu

Simu za Rununu

Faida

- ✓ Kurahisha na kuharakisha mawasilano
- ✓ Kupunguza gharama za usafiri
- ✓ Mtandao huelimisha na hufahamisha habari
- ✓ Kutuma pesa
- ✓ Kuweka pesa/akiba
- ✓ Burudani k.m. nyimbo, michezo
- ✓ Kupiga nduru uhalifu unapotokeo
- ✓ Ajira kwa wauzaji na watengenezaji
- ✓ Ushuru kwa serikali
- ✓ Shajara, kalenda, kamera, kikokotozi

Madhara

- ✓ Burudani kusababisha ajizi
- ✓ Uhalifu
- ✓ Gharama kubwa hasa kuweka chaji na malipo kabla ya kutumia kuongea au mtandao
- ✓ Mtandao kupotosha kimaadili
- ✓ Hutoa miale ambayo yaweza kusababisha saratani
- ✓ Kudanganya katika mitihani
- ✓ Kufungwa jela kutokana na arafa za vitisho na matusi

Runinga/magazeti

- ✓ Burudani
- ✓ Habari
- ✓ Ajira kwa wanahabari na watangazaji
- ✓ Matangazo ya biashara
- ✓ Kufunza maadili k.m. michezo ya kuigiza na vichekesho.
- ✓ Kutuwezesha kufahamu sehemu nyingine za nchi na dunia
- ✓ Kuelimisha k.v. vipindi vya fasihi
- ✓ Utalii
- ✓ Kuangazia sehemu na watu wenye shida
- ✓ Kukuza lugha

- ✓ Kukuza uzaleno

Madhara

- ✓ Ajizi
- ✓ Kupotosha kimaadili
- ✓ Filamu ziazohimiza watu kuwa wazinifu.
- ✓ Matangazo ya vileo
- ✓ Kuenezea chuki na propaganda
- ✓ Kuiga utamaduni wa kigeni usiofaa k.v. mavazi, talaka
- ✓ Gharama ya kununulia
- ✓ Kutopata muda wa kushauri watoto na kuomba
- ✓ Wanafunzi kutosoma jioni
- ✓ Mke na mume kutoongea kujadili mwelekeo wa familia
- ✓ Wanaume kuchelewa kurudi nyumbani usiku wakitazama mpira
- ✓ Migogoro kwa kutaka kutazama vipindi tofauti
- ✓ Kelele na usumbufu kwa waliolala

Utalii

1. hali ya kusafiri mbali ili kuvinjari au kufurahia mandhari

Faida

- ✓ Fedha za kigeni
- ✓ Ajira katika hoteli, udereva, n.k.
- ✓ Uhifadhi wa mazingira
- ✓ Kuboreshwa kwa miundo msingi
- ✓ Mapato kwa serikali kutokana na ada ya kuingilia mbugani na kodi za mikahawa
- ✓ Amani na maelewano nchini na duniani
- ✓ Kuhifadhi mila na tamaduni zetu
- ✓ Kupa nchi umaarufu duniani
- ✓ Maeneneo kame kuweza kutumiwa ipasavyo kama kivutio chao
- ✓ Soko kwa mazao ya kilimo
- ✓ Kuwapa wauzaji vinyago mapato

Ubaya

- ✓ Magonjwa k.v. ya zinaa
- ✓ Matumizi ya mihandarati
- ✓ Tabia zisizofaa k.v. Usenge zinazovunja ndoa na kueneza magonjwa kama ukimwi

- ✓ Upuuzaji wa miradi ya maendeleo serikali ikijengea watalii hoteli za kifahari na viwanja vya ndege ambavyo hutumika kwa nadra sana
- ✓ Kusababisha watoto kuacha shule ili wawe wanawaelekeza wapate pesa
- ✓ Kuhimiza mauaji wa wanyama kwa kununua pembe na ngozi
- ✓ Kelele za magari yao husumbua wanyama na kukanyaga na kuharibu lishe yao

Jinsi ya kuvutia watalii zaidi

- ✓ Kudumisha usalama
- ✓ Kuimarisha miundo msingi
- ✓ Kutangaza nchi na vivutio nje
- ✓ Kupunguza malipo katika hoteli za watalii
- ✓ Kufahamisha wananchi kuhusu vivutio kupitia vyombo vya habari
- ✓ Kuongezea wafanyakazi mishahara ili kuweka akiba waweze kuzuru maeneo yenye vivutio
- ✓ Kuwapa wafanyakazi likizo ya kutosha

Umaskini

Suluhisho

- ✓ Kuongeza nafasi za ajira
- ✓ Kutoa mikopo rahisi kulipa
- ✓ Kupunguza bei ya pembejeo
- ✓ Elimu ya bure
- ✓ Kupigana na ufisadi
- ✓ Upangaji uzazi ili kupunguza idadi ya watu
- ✓ Bei bora ya mazao ya kilimo
- ✓ Kazi kwa vijana

Ukeketaji

Sababu

- ✓ Kupunguza tamaa
- ✓ Njia ya kukomaa
- ✓ Mila na tamaduni

Madhara

- ✓ Kifo kwa kutokwa na damu sana
- ✓ Uenezaji wa magonjwa
- ✓ Shida wakati wa hedhi na kujifungua

- ✓ Ndoa kuvunjika
- ✓ Kibali cha kujiingiza katika myenendo isiyofaa
- ✓ Utengano kati ya waliotahiriwa na ambao hawajatahiriwa -migogoro
- ✓ Kuzua utabaka baina ya waliopashwa na wasiopashwa tohara

Suluhisho

- ✓ Hatua za kisheria
- ✓ Elimu kuhusu madhara
- ✓ Mawaidha kwa wasichana
- ✓ Makao ya watoto

Njaa

- ✓ Kilimo cha unyunyizaji maji
- ✓ Kupunguza bei za pembejeo
- ✓ Njia bora za kuhifadhi mazao
- ✓ Mimea na mifugo inayokomaa haraka
- ✓ Utumizi wa samadi na mbolea
- ✓ Kuelimisha wakulima kuhusu kilimo bora
- ✓ Kutayarisha mashamba mapema
- ✓ Serikali kununua mazao ya wakulima na kuyahifadhi

Dini

Uzuri

- ✓ Kufunza maadili
- ✓ Kusaidia maskini
- ✓ Kuanzisha shule na hospitali
- ✓ Ajira kwa padri, kasisi n.k.
- ✓ Kuandaa watu kwa maisha baada ya kifo
- ✓ Kufariji/kuliwaza wenye dhiki

Ubaya

- ✓ Tamaa ya pesa
- ✓ Biashara
- ✓ Ubakaji wa watoto
- ✓ Kuuza uponyaji
- ✓ Nyingine kutosaidia wenye shida
- ✓ Vita/jihadi
- ✓ Kuruhusu waovu bora watoe pesa
- ✓ Kutoenda hospitalini

- ✓ Kuendeleza maovu k.v. uzinifu, ushirikina, uabudu shetani, n.k.

Maasi ya vijana

- ✓ dawa za kulevya
- ✓ shiniko la kikundi
- ✓ filamu mbaya
- ✓ kudhibitiwa kupita kiasi
- ✓ kukosa nidhamu
- ✓ malezi mabaya/udekezaji
- ✓ kubomoka kwa msingi wa jamii
- ✓ Ufukara kusababisha kujiunga na makundi haramu
- ✓ Kukata tamaa
- ✓ Kutumiwa vibaya na wanasiasa

Suluhisho

- ✓ Kujiondoa kundini
- ✓ Kuimarisha uchumi
- ✓ Kuwashauri vijana
- ✓ Kujenga udhabiti wa jamii
- ✓ Kuwaadhibu kulingana na makosa yao
- ✓ Vijana kujisaka na kujikosoa
- ✓ Vijana kumjua mungu
- ✓ Uhuru wa kadiri
- ✓ Uongozi bora
- ✓ Malezi bora
- ✓ Kuongeza nafasi za ajira

Umoja na Utangamano katika Familia

- ✓ Kuheshimiana
- ✓ Utiifu na unyenyekevu
- ✓ Kuwa na usemi
- ✓ Kuvumiliana na kusameheana
- ✓ Uaminifu na kuaminiana
- ✓ Kutochagulia watoto taaluma na wachumba
- ✓ Wazazi kutolazimisha watoto taaluma au kozi wasizotaka
- ✓ Kutumia pesa vyema bila ubadhirifu
- ✓ Kutopendelea na kulinganisha watoto kiuwezo
- ✓ kutotumia dawa za kulevya
- ✓ Kuomba pamoja

- ✓ wazazi kutopendelea watoto fulani
- ✓ Baba kutimiza majukumu yake ya kukimu jamii
- ✓ Kutodhibiti mke na watoto kupita kiasi
- ✓ Uadilifu
- ✓ Kushiriki kazi

Mambo yanayoathiri utaifa/umoja na utangamano/amani

- ✓ Ufisadi k.v. kuajiri watu kimapendeleo
- ✓ Ukabila
- ✓ Viongozi kueneza chuki
- ✓ serikali kutoakisi uwakilishaji wa taifa zima
- ✓ Usalama kukosekana
- ✓ Ukosefu wa ajira
- ✓ Matamshi mabaya ya viongozi
- ✓ Kupanda kwa gharama ya maisha
- ✓ Majanga ya kiasili
- ✓ Kutojenga miundo msingi kwa usawa
- ✓ Kupendelea maeneo fulani katika ugawaji wa raslimali
- ✓ Ukimbizi wa ndani kwa ndani
- ✓ Ubomoaji wa nyumba

Suluhisho

- ✓ Lugha ya taifa
- ✓ Kukabiliana na ufisadi
- ✓ Usawa katika ugawaji wa raslimali
- ✓ Kuelimisha kuhusu umoja wa kitaifa
- ✓ Tamasha za kitamaduni
- ✓ Kutalii sehemu nyingine za nchi
- ✓ Ndoa za makabila tofauti
- ✓ Serikali ya muungano
- ✓ Viongozi wachochezi kuchukuliwa hatua kisheria

Matatu

Faida

- ✓ Kurahisisha na kuharakisha usafiri
- ✓ Ajira
- ✓ Ushuru
- ✓ Biashara
- ✓ Huduma za dharura

Madhara

- ✓ Ajali
- ✓ Wizi
- ✓ Ufisadi wa polisi kuongezeka
- ✓ Kuongeza nauli ghafla
- ✓ Ujeuri wa madereva na mataniboi
- ✓ Kuchelewesha watu njiani

Magazeti

- ✓ Habari za taifa na kimataifa
- ✓ Kuelimisha k.m. kuhusu afya
- ✓ Kuburudisha k.m. vibonzo
- ✓ Matangazo ya biashara
- ✓ Ajira k.m. wahariri, wauzaji
- ✓ Mapato kwa serikali
- ✓ Kutangaza nafasi za ajira
- ✓ Elimu k.m. uchambuzi wa vitabu vya fasihi na mashairi
- ✓ Hutumiwa kufungia bidhaa

Ubakaji

- ✓ Sura mbaya
- ✓ ulevi
- ✓ Ulemavu
- ✓ Unyonge wa kiakili
- ✓ Kushindwa kudhibiti jicho na tamaa za mwili
- ✓ Njaa ya kimapenzi
- ✓ Kisasi
- ✓ Kujihisi duni
- ✓ Kisomo duni
- ✓ Mavazi

Athari

- ✓ Waliobakwa huathirika kisaikolojia
- ✓ Kujikosea heshima na kujihisi mchafu
- ✓ Magonjwa ya zinaa
- ✓ Mimba zisizotakikana
- ✓ Vifo
- ✓ kujeruhiwa
- ✓ Kupoteza imani na wanaume/wanawake
- ✓ Kutengwa
- ✓ Kufungwa jela

3. UTUNGAJI WA KISANII

a) Mashairi mepesi (huru/arudhi)
b) Hadithi fupi
c) Vitendawili
d) Mafumbo/chemshabongo
e) Vitanza ndimi
f) Michezo ya kuigiza

Mambo ya Kuzingatia katika Uadishi wa Insha

1. maagizo
2. Usijibu swali usilolielewa
3. Uandishi mzuri wa nambari ya swali unalofanya
4. Kuandika vidokezi
5. Kuandika kila hoja katika aya yake
6. Kuanzia aya kwa njia tofauti
7. Lugha sahili
8. Miundo tofauti ya sentensi
9. maudhui
10. muundo
11. Kichwa kwa herufi kubwa, kipigwe mstari na kisizidishe maneni sita
12. Upatanisho/uwiano za kisarufi
13. Tahajia/hijai
14. Kuakifisha
15. Mtiririko
16. Uhalisi
17. tafsiri ya moja kwa moja k.m. kurudisha mlango, mguu wa gari, kutoa/kuweka nguo
18. Maadili (lugha na mawazo safi na mtazamo wa kusaidia taifa)
19. Urefu
20. Uasilia (utungo wako si kurejelea vitabu vya fasihi)
21. Usafi (mwandiko unaosomeka na ambao haujapigwapigwa mistari na kufutwa)
22. Tamathali za usemi
23. Msamiati na tamathali zinazokubalika wala si za kupachika. Usitumie msamiati wa kishairi k.v. mtima, ja, n.k.
24. Kutofupisha k.v. k.m., n.k., Bi.

25. Kutumia kistari ikiwa neno linaendelea katika mstari wa pili na kutokata silabi
26. Herufi f, u, i, j, m, l
27. Kutaja na kueleza kikamilifu
28. Kukamilisha maneno
29. Kutotenganisha sehemu za neno k.m. walilo zungumzia, walioenda
30. Kutounganisha maneno k.m. kwasababu, ni mimi
31. Mdokezo kuoana na maneno yako.
32. Usiongeze maneno kwenye dondoo la kumalizia.
33. Kutoweka dondoo ni kupotoka
34. Kusoma insha baada ya kuandika

4. UANDISHI WAKAWAIDA

Ufahamu

1. Kuelewa
2. Kuandika idadi ya hoja kulingana na alama
3. Hoja kwa muhtasari
4. Andika hoja ulizo na uhakika nazo kwanza
5. Kuorodhesha hoja kwa nambari wala si kistari
6. Jibu lililokamilika
7. Kutoa majibu kutoka katika ufahamu si fikra zako
8. Maana za maneno kama yalivyotumiwa kwa muundo ule ule

Muhtasari/Ufupisho

1. Kutoa mawazo makuu huku kiini cha taarifa kikidumishwa.

Hatua

- ✓ Andika nambari za aya
- ✓ Soma makala
- ✓ Elewa swali
- ✓ Andika mambo muhimu ukizingatia swali ukiondoa maneno yasiyo muhimu
- ✓ Usibadilishe chochote hata kama unatakiwa kutumia maneno yako
- ✓ Andika hoja kikamilifu
- ✓ Andika nakala safi ukizingatia mtiririko

- ✓ Epuka viunganishi vingi
- ✓ Zingatia idadi ya maneno uliyopewa
- ✓ Zingatia kanuni za uandishi
- ✓ Piga mshazari nakala chafu

Matumizi ya lugha

- ✓ Kuzingatia sehemu za swali
- ✓ Sehemu zinazobadilika
- ✓ Kuzingatia neno moja moja
- ✓ Kuzingatia hatua au mbinu
- ✓ Kutojibu maswali kwa pupa
- ✓ Kusoma jibu ili kusahihisha makosa
- ✓ Kuelewa swali k.m. tunga sentensi moja, eleza maana
- ✓ Tunga sentensi fupi
- ✓ Kuonyesha neno, fungu la maneno au kiambishi unachotumia kutunga sentensi
- ✓ Kubainisha (eleza kikamilifu kwa kuandika neno au maneno na jina lake)
- ✓ Tahajia k.m. yabwa, kitendo

Isimu jamii

- ✓ Kutaja, kueleza na kutoa mifano

Fasihi

- ✓ Kufikiri ili kuelewa swali
- ✓ Usijibu maswali zaidi ya manne. Kama jibu halikuridhishi, lipige mshazari
- ✓ Maagizo (swali la kwanza ni la lazima, usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- ✓ Chagua maswali utakayoweza kujibu na kupata hoja nyingi
- ✓ Andika nambari vizuri
- ✓ Usiandike hoja nyingi kuliko alama
- ✓ Andika hoja ulizo na uhakika nazo kwanza
- ✓ Hoja kwa aya moja
- ✓ Kutaja, kueleza kikamilifu na kuthibitisha kwa mifano kutoka kitabuni (kutaja alama moja, kueleza mbili)
- ✓ Usirudie hoja kwa njia tofauti
- ✓ Kutochanganya wahusika
- ✓ Kusoma vitabu mara nyingi ili kujua dondoo limetolewa wapi

- ✓ Maswali ya dondoo (msemaji, anayeambiwa, wapi, lini)
- ✓ Maswali ya kujadili
- ✓ Swali la methali
- ✓ kulinganisha

FASIHI SIMULIZI

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu.
Sanaa ni ufundi wa kuwasilisha fikra na hisia za binadamu kama vile maneno, maandishi, uchoraji, uchongaji, ufinyanzi n.k.
Fasihi simulizi ni sanaa kwa vile:
a) Huwasilisha ujumbe kuhusu binadamu kuhusu utamaduni na uchumi.
b) Huwa na umbo mahsusi k.m. hadithi huwa na mwanzo, kati na mwisho na mashairi huwa na beti, mishororo, n.k.
c) Hutumia lugha kwa ufundi k.v. ya kitamathali.
d) Husawiri mandhari/mazingira mahsusi kwa ufundi mkubwa.
e) Hujenga wahusika kwa ustadi mkuu ili kusawiri tabia za watu katika jamii.

Tofauti Kati ya Fasihi na Sanaa Nyingine

fasihi	sanaa nyingine
✓ Kutumia lugha	✓ Kutotumia lugha
✓ Sanaa tendi	✓ Si tendi
✓ Kutumia wahusika kuwasilisha maudhui	✓ Hutumia maumbo kumithilisha watu
✓ Kutumia maudhui na fani kuwasilisha ujumbe	✓ Kutumia maumbo na sura za vitu
✓ Kujikita katika mazingira na wakati maalum	✓ Hazijikiti katika muktadha na wakati maalum.

Aina/makundi ya fasihi
a) **Fasihi simulizi**
⇒ Fasihi inayowasiolishwa kwa njia ya mdomo.
b) **Fasihi andishi**
⇒ Fasihi inayowasilishwa kwa njia ya maandishi.

Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi/sifa za fasihi simulizi/zinazofanya utanzu uwe wa fasihi simulizi

a) Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo ilhali fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.
b) Fasihi simulizi huhifadhiwa akilini ilhali fasihi aandishi huhifadhiwa kwa maandishi.
c) Fasihi simulizi ni mali ya jamii ilhali fasihi andishi ni mali ya mtu binafsi/mwandishi.
d) Fasihi simulizi ina wahusika wa kila aina k.v binadamu, wanyama na ndege, mazimwi na majitu, miungu, mizimu, mashetani na vitu visivyo na uhai k.v. mawe na miti ilhali fasihi andishi ina wahusika binadamu kwa kiasi kikubwa.
e) Fasihi simulizi ina tanzu nyingi kuliko fasihi andishi.
f) Uwasilishaji wa fasihi simulizi huweza kuandamana na utendaji k.v matumizi ya ishara, nyimbo, makofi, kuimba, kubeba zana katika majigambo n.k ilhali ule wa fasihi andishi hauandamani na utendaji isipokuwa inapowasilishwa mbele ya hadhira.
g) Fasihi simulizi huwasilishwa mbele ya hadhira ilhali fasihi andishi si lazima iwasilishwe mbele ya hadhira.
h) Fasihi simulizi huwasilishwa mahali maalum k.v jandoni, matangani, arusini, n.k ilhali fasihi andishi haina mahali maalum.
i) Fasihi simulizi huandamana na shughuli fulani ya kitamaduni ilhali fasihi andishi haiandamani na shughuli ya kitamaduni.
j) Fasihi andishi huhitaji muda kutunga ilhali baadhi ya fasihi simulizi huzuka papo hapo k.m. semi, maigambo.
k) Fasihi simulizi ina uwezo mkubwa wa kubadilishwa na fanani anapowasilisha ufaraguzi) bali fasihi andishi haibadiliki isipokuwa mwandishi aiandike upya.
l) Fasihi simulizi ina historia ndefu kuliko fasihi andishi kwa kuwepo tangu mwanzo wa maisha ya binadamu
m) Fasihi simulizi huwasilishwa wakati maalum k.v. usiku, kipindi fulani cha mwaka ilhali andishi haina wakati maalum.

- **Tofauti kati ya hadhira**

n) Hadhira ya fasihi simulizi huweza kuwasiliana moja kwa moja na mwasilishaji ilhali ile ya fasihi simulizi sio lazima iwasiliane na mwandishi.
o) Hadhira huchangia katika uwasilishaji wa fasihi simulizi k.v kwa kuimba, kupiga makofi n.k (hadhira tendi/hai) ilhali hadhira ya fasihi andishi haichangii katika uandishi.
p) Hadhira ya fasihi simulizi huonana na mwasilishaji ilhali ile ya fasihi andishi si lazima ionane na mwandishi.
q) Hadhira ya fasihi simulizi ni kubwa kuliko ile ya fasihi andishi kwani huhusisha hata wasiojua kusoma na kuandika.
r) Hadhira ya fasihi simulizi ni hai yaani inajulikana na fanani ilhali ile ya fasihi simulizi si hai yaani haijulikani na mwandishi.
s) Hadhira ya fasihi simulizi hainunui kazi ilhali ile ya fasihi andishi hununua kazi.
t) Hadhira ya fasihi simulizi yaweza kumiliki kazi ya fanani lakini ile ya fasihi andishi haiwezi kumiliki kazi ya mwandishi.
u) Hadhira ya fasihi simulizi huchagua kwa kulenga watu wa rika fulani lakini ile ya fasihi andishi hailengi watu wa rika yoyote.

Jinsi Fasihi Simulizi na Andishi Zinavyofanana

a) Zote mbili hushughulikia masuala yanayohusu maisha maisha ya binadamu.
b) Zote mbili Huhumia lugha kwa ubunifu kuwasilisha maudhui.
c) Zote mbili huwa na vipengele viwili vikuu, maudhui na fani (jumla ya mbinu msanii alizotumia kuwasilisha maudhui).
d) Zote mbili majukumu sawa k.v. kuburudisha, kuadilisha, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, n.k.
e) Zote mbili zina utendaji-pale tamthilia na riwaya zinapoigizwa.
f) Zote mbili huzaliwa, hukua na hufa kutegemea mabadiliko ya wakati.

g) Zote mbili huwa na wawasilishaji-fanani k.m. mtambaji/mganaji au manju/yeli katika fasihi simulizi na mwandishi upande wa fasihi andishi
h) Fasihi simulizi imekopa tanzu za fasihi simulizi k.v. methali, mashairi, n.k.

Majukumu ya Fasihi Simulizi/Umuhimu wa Kufunza Fasihi Simulizi Katika Shule za Upili

a) Kuburudisha-kustarehesha, kufurahisha, kuchangamsha, kutuliza, kusisimua na kupumbaza akili na kiwiliwili - nyimbo, hadithi, vitendawili
b) Kufunza maadili kwa wanajamii kwa kuwahimiza kuiga sifa chanya na kukataa sifa hasi za wahusika.
c) Kukuza uwezo wa kufikiri/kudadisi k.m vitendawili na chemshabongo.
d) Kufariji k.m mbolezi na methali k.m. ‘Baada ya dhiki faraja’.
e) Vipengele vya fasihi simulizi k.v mashairi, nyimbo, nahau, hutumiwa katika uandishi wa fasihi andishi.
f) Kuhifadhi historia ya jamii k.m. mighani, visaviini, mapisi, tarihi n.k.
g) Kukejeli tabia zinazokiuka matarajio ya jamii k.v soga, methali, n.k.
h) Kuendeleza tamaduni za jamii kwani husawiri imani na desturi za jamii. k.v kitendawili ‘Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini siwezi kulichuma.’ - Mtu hawezi kumwoa dadake.
i) Kuunganisha watu pamoja kwa kuwajumuisha pamoja wakati wa ngoma, kuimba, utambaji, n.k.
j) Kukuza lugha k.v. misimu inapokita kimatumizi na kujumuishwa katika lugha sanifu.
k) Kukuza uwezo wa kutumia lugha kadiri mtu anapoendelea kuwasilisha k.v. hotuba, vitanza ndimi husaidia kuboresha matamshi na kutofautisha maana za maneno.
l) Kuza uwezo wa kubuni k.v. malumano ya utani, vitanza, ndimi ngonjera, n.k.

m) Kukuza uzalendo kwa kufanya wanajamii kuonea fahari jamii zao na kuiga mashujaa au watu waliotendea jamii makuu.
n) Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, n.k.

Sababu za Ufaraguzi/Kubadilika kwa Fasihi Simulizi

a) Kuwasilishwa vibaya.
b) Fanani kusahau na kubadilisha yaliyomo na mtiririko.
c) Kubadilisha ili kukidhi mahitaji ya hadhira k.m. umri na uelewa wao- kutumia lugha nyepesi kwa watoto na pevu kwa watu wazima.
d) Mabadiliko ya mandhari/mazingira-vitu vilivyo katika mazingira halisi kukosekana katika mazingira ya usimulizi na msimulizi kutumia vitu katika mazingira yake vinavyokaribiana navyo.
e) Kutoeleweka na hivyo kuhifadhiwa vibaya.
f) Mabadiliko ya wakati k.m kitendawili cha wakati wa mkoloni kutumia mzungu na cha wakati wa mwarabu kutumia mwarabu na maana ni ile ile-Mzungu/mwarabu amesimama kwa mguu mmoja-mwavuli.
g) Mabadiliko ya falsafa ya vizazi na maingiliano katika jamii kusababisha kurithisha tu yale ambayo ni muhimu na kuacha mengine.
h) Kila fanani huwa na mtindo wake wa kuwasilisha/kisanii.
i) Ubunifu wa fanani ili uwasilishaji uweze kuvutia saidi na uwezo wake wa lugha.
j) Teknolojia kusababisha kuhifadhiwa na hivyo kuiua.

Wahusika katika Fasihi Simulizi

⇒ Wahusika ni viumbe wa sanaa ambao hutumiwa katika kazi ya fasihi kuwasilisha maswala mbalimbali.
a) Fanani-anayetunga na kuwasilisha fasihi simulizi.
b) Hadhira-kusikiliza, kutazama, kushiriki wa kuimba, kuuliza maswali, kutegua vitendawili, kupiga makofi, n.k. kuna aina mbili za hadhira: (i) hadhira tendi/hai na (ii) hadhira tuli.
c) Wanyama-wanaofanya kama binadamu na kuwakilisha sifa kama vile ujanja, ulaghai, tamaa na ujinga na wanaobakia wanyama tu.

d) Binadamu
e) Mazimwi na majitu-viumbe vyenye matendo na maumbile ya kutisha kama vile jicho moja, vichwa viwili au zaidi, nusu mtu na nusu myama, wenye tamaa iliyokithiri ya kuweza kumeza kila kitu, kuhifadhi na kutunza binadamu ananyoyapendeza.
f) Wahusika vitu (visivyo na uhai) mawe, miti, vijaluba, vibuyu-hutumiwa kuibua imani za kidini.
g) Mizimu-roho za waliokufa-hutembea, hula na huathiri binadamu.
h) Miungu-viumbe vyenye uwezo mkubwa dhidi ya binadamu k.m. katika mighani na visasili.

Njia za Kukusanya Fasihi Simulizi

a) Kuchunza/utazamaji

⇒ Kutazama kwa makini yanayotokea na kuandika.

Umuhimu/ubora/uzuri

a) Kupata habari za kutegemewa na kuaminika.
b) Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
c) Ni njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika
d) Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
e) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji

Udhaifu

a) Shida ya mawasiliano.
b) Ugeni wa mtafiti kusababisha washiriki kumshuku na kusitisha uwasilishaji
c) Ghali kwa kumbidi mtafiti kusafiri
d) huhitaji muda mrefu

b) Kusikiliza wasanii wakiwasilisha tungo zao.

Umuhimu

a) Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
b) Kupata habari za kutegemewa na kuaminika.
c) Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
d) Kikwazo cha mawasiliano-Si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.

e) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji.

Udhaifu

a) Shida ya mawasiliano-Si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
b) Huhitaji muda mrefu-kusafiri na kusikiliza.
c) Ugeni wa mtafiti kusababisha washiriki kutowasilisha ipasavyo.
d) Ghali kwa gharama ya usafiri.

c) Mahojiano

⇒ Kuhoji wanaofahamu mengi kuhusu fasihi simulizi.

Umuhimu

a) Kuweza kung'amua wakati mhojiwa anatoa habari zisizo za kweli.
b) Kuweza kufafanulia mhojiwa maswali ili kuweza kupata habari sahihi zaidi.
c) Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
d) Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
e) Kupata habari za kutegewa na kuaminika

Udhaifu

a) Huhitaji muda mrefu.
b) Mhojiwa kutotoa habari kwa kutomwamini mtafiti kwa ugeni wake.
c) Kikwazo cha mawasiliano-si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
d) Ghali kwa gharama ya usafiri.

d) Kurekodi katika kanda za sauti/tepurekoda

Umuhimu

a) Kuweza kudumu na kufikia vizazi vingi.
b) Sifa za uwasilishaji/uhai kama vile toni na kiimbo kuhifadhiwa.
c) Mkusunyanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa.
d) Kupata habari za kutegewa na kuaminika
e) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji

Udhaifu

a) Chaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti kuathirika.
b) Hakiwezi kunasa uigizaji.

c) Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
d) Ghali kwa kuhitaji kununua kifaa na kumbidi mtafiti kusafiri.

e) Kurekodi kwa filamu na video

⇒ Hunasa picha zenye miondoko na sauti.

Umuhimu

a) Video huhifadhi uigizaji, ishara na kiimbo/toni.
b) Kuonyesha uhalisi wa mandhari
c) Mkusunyanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa
d) Kazi iliyokusanywa hivi hudumu kwa muda mrefu.
e) Njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika
f) Kupata habari za kutegewa na kuaminika

Udhaifu

a) Chombo chaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti kuathirika.
b) Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
c) Njia ghali.
d) Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
e) Ghali kwa gharama ya ya usafiri na kununua filamu na kamera ya video.
f) Data yaweza kufisidiwa na hivyo kutowafikia walengwa.

f) Kupiga picha kwa kamera

⇒ Hunasa picha zisizo na miondoko na sauti

Umuhimu

a) Huonyesha uhalisi wa mandhari.
b) Huweza kuhifadhi ishara.
c) Mkusunyanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa.
d) Kupata habari za kuaminiwa na kutegemeka.

Udhaifu

a) Ghali kwa gharama ya ya usafiri na kununua kamera.
b) Sifa za uhai kama vile kiimbo haziwezi kuhifadhiwa.
c) Yaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti kuathirika.
d) Data yaweza kufisidiwa na hivyo kutowafikia walengwa

f) Kushiriki katika kazi ya fasihi simulizi k.v. ngoma, soga, n.k.

Umuhimu

a) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji.
b) Kupata habari za kutegewa na kuaminika.
c) Njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
d) Kukuza utangamano wa mtafiti na wanajamii.
e) Kuweza kunasa na kuhifadhi sifa za kiimbo, toni na ishara.

Udhaifu

a) Kuchukua muda mrefu.
b) Ugeni wa msanii kusababisha washiriki kuwa na wasiwasi na kutotenda kama kawaida.
c) Njia ghali kwa kuhitaji mtafiti kusafiri mbali.
d) Mtafiti aweza kusahau kwa kuhifadhi akilini.

g) Kutumia hojaji

⇒ Fomu yenye maswali funge au wazi.

Umuhimu

a) Gharama ya chini.
b) Yaweza kutumika katika mahojiano.
c) Huokoa muda kwani mtafiti aweza kuituma na kuachia mhojiwa kujaza.
d) Hupatia habari za kuaminika na kutegemeka.

Udhaifu

a) Utata wa maswali kusababisha majibu yasiyo sahihi.
b) Si nzuri kwa wasiojua kusoma na kuandika.
c) Kutopata sifa za uwasilishaji kama vile kiimbo, toni na ishara.
d) Wahojiwa kukataa kuijaza kutokana na mwelekeo hasi dhidhi ya hojaji na hivyo kukwamiza utafiti.

Vifaa vya Kukusanya Fasihi Simulizi na Udhaifu Wake

a) Vinasa sauti/tepu rekoda
b) Kamera
c) Filamu na video
d) Diski za kompyuta
e) Kalamu na karatasi

Umuhimu

a) Kuweza kudumu na kufikia vizazi vingi.
b) Si rahisi kusahaulika-hubakia vile vile.
c) Si njia ghali kama vile video

Udhaifu

a) Sifa za uwasilishaji kama vile toni, kiimbo/toni na ishara haziwezi kuhifadhika hivyo kupotea.
b) Hupunguza hadhira kwa kulenga tu wanaojua kusoma na kuandika na hivyo kuathiri usambazaji wake.

Mbinu za Kuhifadhi Fasihi Simulizi

a) Huhifadhiwa na binadamu akilini k.m. ngano hupokewa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
b) Katika maumbile au mazingira k.m. fisi daima huchechemea , kinyonga naye hutembea pole pole.
c) Katika vifaa meme k.m. nyimbo, hadithi, maigizo n.k. huweza kuhifadhiwa katika kanda za sauti, video, sidi na diski za kompyuta.
d) Katika michoro k.m. picha huhifadhi matukio maalum k.v. za kabila fulani likiwinda au likisherehekea.

Umuhimu wa Kukusanya/Kuhifadhi Fasihi Simulizi

a) Ili isipotee k.m. kwa kusahaulika.
b) Kuirekodi ili kuiendeleza kwa kuirithisha kwa vizazi vijavyo.
c) Ili kulinganisha fasihi simulizi za jamii mbalimbali na kuonyesha tofauti zake.
d) Ili kuhakikisha mtiririko katika uwasilishaji.
e) Kutunza historia ya jamii ili vizazi vijavyo viijue.
f) Ili kuziba mapengo ya utafiti yaliyomo kwa vile kuna tungo ambazo hazijatafitiwa kwa kina.
g) Kuendeleza elimu ya jadi ya jamii.
h) Kuingiliana na jamii iliyo chanzo cha fasihi humwezesha kuelewa na utamaduni na fasihi yake kwa ujumla
i) Humwezesha mwanafunzi kuona vipengele hai vya fasihi k.v. uigizaji, toni na kiimbo ambavyo husaidia kuielewa kwa kina.
j) Husaidia kuhifadhi tamaduni za jamii kwa nia ya kuzipitisha kwa vizazi vijavyo.
k) Husaidia kuelewa utamaduni wa jamii nyingine.
l) Humwezesha mwanafunzi kupata maarifa ya kufanya utafiti katika taaluma nyingine k.v. sosholojia.
m) Kujua fasihi simulizi za jamii nyingine humfanya mtafiti kuzielewa na kuzikubali jamii hizo na hivyo kuendeleza amani katika nchi.

n) Ili kusahihisha mawazo mapotovu kuhusu baadhi ya tanzu na vipera vya fasihi simulizi.

Matatizo Yanayomkabili Mkusanyaji wa Fasihi Simulizi

a) Gharama ya utafiti kuwa kubwa kiasi cha mtafiti kutoimudu k.v. kusafiria, kununulia vifaa.
b) Kutojaziwa hojaji kutokana na mtazamo hasi wa jamii dhidi ya ujazaji wake.
c) Wanajamii kukataa kutoa habari wakishuku mtafiti anawapeleleza au kwa kuona haya.
d) Wanajamii wengine kudai walipwe kabla ya kutoa habari na hivyo kukwamiza utafiti.
e) Mbinu nyingine k.v. hojaji huhitaji watu wanaojua kusoma na kuandika na ikiwa mhojiwa hajui utafiti utakwamizwa.
f) Uchache wa wazee na wataalamu wa fasihi simulizi kusababisha kukosekana au kupatikana kwa data isiyo ya kutegemewa.
g) Utawala kukataa kutoa idhini ya kufanya utafiti.
h) Kukosa ufadhili na utafiti kutofanywa kwa kutomudu gharama.
i) Muda wa utafiti kutotosha na hivyo kutopata habari za kutosha kuhusiana na mada yake.
j) Kikwazo cha mawasiliano ikiwa mtafiti na mhojiwa hawatumii lugha moja na mhojiwa hajui lugha nyingine na kumbidi mtafiti kukodi mkalimani na gharama kuongezeka.
k) Ukosefu wa vyombo vya usafiri kunakochelewesha utafiti na kutomalizika katika muda uliopangwa.
l) Ukosefu wa usalama k.v. kuvamiwa kwa kushukiwa anapeleleza na kuibiwa vifaa.

Changamoto Zinazokabili Ukusanyaji wa Fasihi Simulizi

a) Ukosefu wa utafiti wa kutosha kwani kuna vipera ambavyo bado havijaandikwa.
b) Uchache wa wataalamu wa kutafitia na kuendeleza utafiti.

c) Watu kuhamia mijini na kuingiliana na wa jamii nyingine na kufanya uhifadhi na urithishaji wa fasihi kutowezekana.
d) Mtaala wa elimu kupuuza lugha ya kiasili inayotumiwa kuhifadhia na kurithisha fasihi simulizi na hivyo kukatiza ukuaji wake.
e) Fasihi simulizi kuhusishwa na ukale na hivyo kutoona haja ya kuirithisha na kuihifadhi.
f) Kuhifadhiwa kwa fasihi simulizi akilini kusababisha kusahaulika, kubadilika hata kufa kwake.

Jinsi Jamii ya Sasa Inavyojaribu Kuhifadhi Fasihi Simulizi

a) Tamasha za muziziki kunakokaririwa na kuimbwa mashairi.
b) Sherehe za arusi, jando, mazishi mawaida.
c) Utegaji na uteguaji wa vitendawili kupitia redio na runinga.
d) Sarakasi za wasanii huhifadhi kipera cha vichekesho.
e) Ngoma za kienyeji kama isukuti katika hafla za kisiasa na harusi.
f) Utambaji wa hadithi hasa katika sehemu za mashambani.

Tanzu za Fasihi Simulizi

⇒ Tanzu ni aina za tungo zenye muundo uliokaribia kufanana.
e) hadithi
f) semi
g) ushairi
h) mazungumzo
i) maigizo
⇒ Kipera ni utungo wa fasihi simulizi unaowasilishwa mbele ya watu.

HADITHI

⇒ Masimulizi yanayotumia lugha ya mtiririko au nathari.

Sifa

a) Hutumia ya lugha ya mtiririko au nathari-kueleza matukio moja kwa moja.
b) Hurithishwa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
c) Huwasilishwa mbele ya hadhira

d) Hutambwa mahali maalum k.v. ndani ya nyumba, chini ya mti, uwanjani, n.k.
e) Huweza kutokana na matukio halisi (kihistoria) au ya kubuni.
f) Huwa na mafunzo fulani kwa jamii/hadhira.
g) Hutumia wahusika wa aina tofauti k.v. nyumbani, wanyama, ndege, mazimwi, n.k.
h) Hutumia aina nyingine za sanaa k.v nyimbo, methali, ushairi, n.k.
i) Huwa na utendaji k.v. mtambaji kuiga fisi anavyokula.
j) Aghalabu hutambwa jioni.

Sababu za Ngano Kutambwa Jioni/Usiku

a) Ndio wakati watu walikuwa wamejumuika nyumbani baada ya kazi.
b) Utambaji ulikuwa njia ya kupitisha wakati chakula kikingojewa.
c) Wakati huu ulihakikisha mwanajamii hapotezi wakati wa kazi.

Majukumu ya Hadithi

a) Kufunza maadili yaliyo nguzo kuu kwa wanajamii.
b) Kukuza ujasiri wa kuzungumza hadharani.
c) Kuburudisha baada ya kazi ya kutwa.
d) Kukuza uwezo wa watoto wa kukumbuka ili kutamba baadaye.
e) Kueleza asili ya mambo k.m visaviini, visasili na ngano za usuli.
f) Kutahadharisha wanajamii dhidi ya kufanya mambo yasitofaa.
g) Kuunganisha watu katika jamii wanapojumuika pamoja kusikiliza utambaji.
h) Ngano za mtanziko hukuza uwezo wa kutathmini na kutoa uamuzi ufaao.
i) Kukuza lugha hasa kwa hadhira ya watoto.
j) Kuhifadhi na kuendeleza historia ya jamii k.v. mighani, tarihi, n.k.
k) Kuelimisha hadhira kuhusu utamaduni wao.
l) Njia ya kupokeza kizazi historia na utamaduni wa jamii.

Sifa za Mtambaji/Mganaji Bora

1. Asiwe mwoga ili kuweza kuzungumza hadharani.
2. Asiwe na haya ili kuweza kuzungumzia mambo ya aibu inapobidi.
3. Awe na uelewa wa mazingira na masuala ibuka katika jamii ili kuweza kuwasilisha dhana zisizopatikana katika mazingira yake k.m. kutumia rais kuelezea dhana ya mfalme.
4. Awe na ufahamu mpana wa lugha ili aweze kuitumia kwa uhodari na kuwasilisha kwa wepesi.
5. Awe mchanganfu na mcheshi ili kunasa makini ya hadhira na kuzuia isikinai.
6. Awe na ufahamu mpana wa utamaduni husika ili kuzuia kutumia maneno na ishara zinazoweza kuwaudhi au kupingana na imani za hadhira.
7. Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira k.v. kuimba, maswali ya balagha ili isikinai, n.k.
8. Aweze kujua, matarajio, kiwango cha elimu na tajriba ya hadhira ili kuweza kubadilisha kwa kiwango kinachofaa.
9. Awe na uwezo wa kuingiliana vizuri na hadhira ili aivutie.
10. Awe na kumbukumbu nzuri ili usimulizi wake utiririke vizuri.
11. Awe na uwezo wa kudramatisha ili kuonyesha picha fulani k.v. kuiga toni, sauti, na kiimbo kulingana na swala analowasilisha.
12. Kubadilisha toni au kiimbo ili hadhira isikinai.
13. Awe na ujuzi wa kutumia ishara za uso, mwili na miondoko kulingana na hali anayoigiza.
14. Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
15. Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazoigiza k.v. huzuni
16. Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira kwa nyimbo na maswali ya balagha ili kuondoa uchovu wa kutazama na kusikiliza.
17. Awe na uwezo wa ufaraguzi/ kubadilisha utambaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake na kutoa

mifano inayofahamika kutoka katika mazingira ya hadhira.

18. Awe na uwezo wa kutumia mtuo wa kidrama ili kuongeza taharuki, kusisitiza ujumbe na kuteka makini ya hadhira.

Aina za Hadithi

a) **Hadithi za Kubuni**

⇒ Hazisimulii matukio ya kweli bali ya kutungwa

b) **Hadithi za Kisalua/Kihistoria**

⇒ Zinazosimulia matukio yaliyowahi kutendwa na wahusika waliowahi kuishi.

⇒ Huongezewa ubunifu ili kuvutia zaidi.

1. **Hadithi za Kubuni**

Ngano

⇒ Hadithi zinazosimulia kisa chenye funzo na zenye wahusika aina ya binadamu, viumbe na vitu visivyo na uhai.

Sifa za Ngano

j) Zina fomyula ya kuanzia/mwanzo maalum.

k) Zina fomyula ya kumalizia/mwisho maalum.

l) Zina wahusika aina mbalimbali.

m) Zina matumizi ya nyimbo.

n) Hutumia takriri (usambamba) ili kusisitiza k.m. zimwi likakimbia, likakimbia.

o) Huwa na na maadili/mafunzo

p) Hutumia maswali ya balagha kuongeza taharuki.

q) Hutumia tanakali za sauti.

r) Zina matumizi ya fantasia au matukio yanayokiuka uhalisi/mambo ya ajabu k.v. binadamu kuruka kama ndege, zimwi kumeza watu na baadaye kutapika wote, n.k.

⇒ Kutambua mbinu zilizotumiwa katika hadithi/ngano

⇒ Kutambua wahusika

Aina za Fomyula za Kuanzia/Mianzo Maalum

i) Paukwa, Pakawa. Sahani. Ya mchele. Giza. La mwizi. Na kiboko je? Cha mtoto mrorofi…
ii) Hapo zamani za kale/za kongamawe…
iii) Ilitokea…
iv) Hadithi! Hadithi! Hadithi njoo…
v) Kaondokea chenjangaa, kajenga nyumba kakaa, mwanangu mwanasiti, kijino kama chikichi, cha kujengea kikuta, na vilango vya kupita…
vi) Hapo jadi na jadudi…

Umuhimu wa Fomyula ya Kuanzia/Mwanzo maalum

i) Kuvuta makini ya hadhira.
ii) Kumtambulisha mtambaji kwa hadhira.
iii) Kuashiria mwanzo wa hadithi.
iv) Kutoa hadhira kutoka ulimwengu halisi hadi ule wa hadithi.

Aina za Fomyula za Kumalizia/Miishio Maalum

ii) Hadithi inaishia hapo.
iii) Tangu siku hiyo…
iv) Wakaishi raha mustarehe.
v) Maadili

Umuhimu wa Fomyula ya Kumalizia/Mwisho Maalum

i) Kuashiria mwisho wa hadithi.
ii) Kutoa hadhira katika ulimwengu wa hadithi hadi ule halisi.
iii) Kumpisha/kumpa fursa mtambaji anayefuata.
iv) Kupisha shughuli inayofuata.
v) Kutoa funzo la hadithi kwa muhtasari.
vi) Kupa hadhira nafasi ya kupumzika baada ya kuwa makini kwa muda.

Umuhimu wa Nyimbo katika Ngano

i) Kushirikisha hadhira.
ii) Kusisimua hadhira na kuondoa ukinaifu
iii) Kuteka makini yao.
iv) Kuwasilisha mafunzo/maadili.
v) Kutenganisha matukio katika hadithi.
vi) Kuburudisha hadhira.
vii) Kupunguzia hadhira mwemeo.

Umuhimu wa Tanakali za Sauti/Onomatopeya katika Ngano

i) Kuongeza utamu.
ii) Kusaidia msomaji kupata picha kamili.
iii) Kusaidia kupata hisia halisi

Aina za Ngano

i) **Hurafa**

⇒ Hadithi zenye wahusika wanyama na ndege.
⇒ Hurafa za kijanja ni hadithi ambapo wanyama wadogo hutumia ujanja wa hali ya juu ili kujinasua na hali ngumu au mitego wanayotegewa.

Sifa

a) Wahusika ni wanyama au na au ndege.
b) Wanyama na ndege hupewa sifa za binadamu
c) Ni kazi ya ubunifu.
d) Hutoa mafunzo kwa njia ya kuchekesha na isiyoumiza.
e) Huwa na ucheshi mwingi.
f) Hutumia mbinu ya uhuishi.
g) Huwa na sifa zinazohimizwa na zinazoshutumiwa.
h) Ujanja au uongo hujitokeza katika hurafa za kijanja.
i) Ushindi hujitokeza katika hurafa za kijanja.

Umuhimu

a) Kutahadharisha watu dhidi ya kuwa wa danganyifu/kudanganyika kwa urahisi.
b) Kuonyesha jinsi tabia ya udanganyifu inavyoweza kujitokeza na kuathiri watu.
c) Hurafa za kijanja hufunza jinsi ya kupampana na hali ngumu.

ii) **Hekaya/Ngano za Kiayari**

⇒ Hadithi zinazomsawiri mhusika anayetumia ulaghai kupata matilaba yake kutoka kwa wengine (Abunuwasi).

Sifa

a) Wahusika wakuu ni binadamu.
b) Huwa na ubunifu mkubwa.
c) Hustaajabisha na kuchekesha.
d) Ujanja na uongo hujitokeza.
e) Ushindi hujitokeza.
f) Ni za kubuni.

Umuhimu

a) Hutahadharisha watu dhidi ya kuhadaika kwa wepesi.
b) Huonya dhidi ya matokeo yanayoweza kuwapata wanaojinyakulia mali kwa udanganyifu.
c) Kuonya dhidi ya usaliti.
d) Kukashifu viongozi dhalimu na matendo maovu.
e) Kukejeli wanaotumia nguvu badala ya akili/hekima.

iii) **Visasili**

⇒ Hadithi zinazoeleza asili ya matukio fulani katika jamii k.m. kifo, jua, lugha, zilizala n.k.

Sifa

a) Husimulia mambo ya kiimani na kidini.
b) Huwa na misingi ya kihistoria.
c) Hueleza asili ya matukio katika jamii.
d) Wahusika ni wanyama na binadamu.
e) Huwa na maadili.
f) Hurithishwa kizazi hadi kingine.

Umuhimu

a) Kueleza asili ya mambo kama vile kifo, utamaduni n.k.
b) Kueleza utaratibu wa kutekeleza desturi k.v. mahari.
c) Kuhalalisha baadhi ya mila na desturi za jamii k.v. ulipaji mahari, uabudu miti, n.k.
d) Kukitisha mizizi imani fulani ya watu.
e) Kupunguza athari za majanga kama vile kuhalalisha kifo.
f) Kutambulisha jamii kwani kila jamii ina aina yake ya visasili.
g) Kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii

iv) **Ngano za usuli**

⇒ Hadithi zinazoeleza asili ya hali, tabia, mahusiano au wasifu. k.v. asili ya kuku kuchakura, asili ya kinyonga kwenda kwa tahadhari, n.k.

Sifa

a) Wahusika ni wanyama na binadamu
b) Ni kazi ya kubuni.
c) Hueleza kuhusu asili ya sifa, tabia au hali.
d) Hutumia mbinu ya uhuishi.

e) Huwa na maadili.

Umuhimu

a) Kueleza sababu ya tabia, hali au sifa Fulani.
b) Kuonya dhidi ya tabia hasi kama vile ulafi.

v) **Ngano za mazimwi**

⇒ Hadithi ambazo wahusika ni mazimwi.

Sifa

a) Wahusika ni mazimwi
b) Mazimwi huwakilisha sifa hasi za binadamu k.m ulafi, ukatili, uovu n.k.
c) Hujaa uharibifu.
d) Huwa na matumizi mengi ya fantasia.
e) Kipengele cha safari hujitokeza k.v. kwenda nchi za mbali kutafuta suluhisho.
f) Ushindi hujitokeza (mazimwi hushindwa).
g) Ni kazi ya kubuni.
h) Huwa na maadili.
i) Mazimwi huwa na sifa zinazokiuka mipaka ya binadamu k.m. kinywa kisogoni, jicho moja kubwa, n.k.

Umuhimu

a) Kukashifu tabia ya uovu, ulafi, na ukatili.
b) Kutahadharisha dhidi ya kuwa na ulafi, ukatili n.k.
c) Kutia moyo waliodhulumiwa kuwa waliowanyanyasa wataadhibiwa siku moja.

vi) **Ngano za Mashujaa**

⇒ Ambazo zinazohusu watu waliotenda matendo ya kishujaa katika jamii zao kama vile kuokoa jamii.

Sifa

a) Kipengele cha motifu au kusafiri nchi za mbali, kupigana na mazimwi kuokoa jamii.
b) Husawiri mapigano kati ya wema (lila) na ubaya (fira).
c) Uovu huwakilishwa na mazimwi au viongozi dhalimu
d) Hatimaye wema hushinda uovu kwa juhudi za mashujaa

⇒ Ngano za mashujaa ni za kubuni ilhali katika mighani, mashujaa wanaaminiwa waliishi.

Umuhimu

a) Kuhimiza uzalendo na ujasiri miongoni mwa vijana.
b) Kuhimiza ujasiri miongoni mwa vijana.

c) Kusifu mashujaa katika jamii
d) Kuelimisha jamii kwa kuwapa maarifa ya kukabiliana na changamoto, inda na ila.
e) Kuhimiza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga mashujaa na kupigania jamii.
f) Kuonya dhidi ya matendo hasi k.v. ukatili.
g) Kuhimiza watu kutokata tamaa

vii) **Ngano za mtanziko**

⇒ Hadithi ambapo mhusika hukabiliwa hali ngumu ya kuamua baina ya mambo wawili au zaidi yanayomkabili.

Sifa

a) Wahusika ni wanyama au binadamu.
b) Ni kazi ya kubuni.
c) Mhusika hulazimika kufanya uteuzi mgumu.
d) Hali mbili au zaidi zinazotatanisha huwepo.

Umuhimu

a) Hutuerevusha jinsi ya kupambana na hali ngumu.
b) Kuonya/kutahadharisha dhidi ya kujiponza.
c) Kukuza uwezo wa kupima mambo na kuteua lililo muhimu.
d) Kuonya dhidi ya kutenda bila kuwaza kwa kina.

viii) Ngano za Kimafumbo

⇒ Ambazo huwa na maana ya ndani/iliyofichika.

a) **Istiara**

⇒ Hadithi ambayo maana yake huwakilisha maana nyingine iliyofichika k.v. hurafa ambapo wanyama huwakilisha binadamu.

b) **Mbazi**

⇒ Hadithi fupi inayotolewa inayotolewa kama mfano kumkanya au kumwelekeza mtu k.v. katika biblia.

2. **Hadithi za Kisalua/Kihistoria**

i) Mighani

⇒ Hadithi za mashujaa/majagina wa jamii fulani k.m. Rwanda Magere wa Waluo, Fumo Liyongo wa Wapate, Koome Njue wa Wameru, Wangu wa Makeri wa Wakikuyu na Syokimau wa Wsakamba.

Sifa

a) Huhusu mashujaa wa jamii fulani.

b) Wahusika hupambana na hali ngumu inayosababishwa na maadui.
c) Wahusika hupewa sifa na uwezo usiokuwa wa kawaida k.v. ukubwa wa ajabu, nguvu katika kivuli, nguvu katika nywele, kutoulika n.k.
d) Wahusika hupigania haki za wanyonge.
e) Mhusika hukomboa jamii yake dhidi ya maadui.
f) Mhusika hufa kifo cha huzuni (tanzia) kwa kusalitiwa na mtu wa karibu k.v. mwanamke au jamaa zao.
g) Mashujaa huuliwa kwa njia ya ajabu kama vile kunyolewa nywele, kivuli kuchomwa mkuki, kuchomwa shindano ya shaba kitovuni
h) Mighani huzungumzia matukio ya kihistoria.
i) Kuna tabia ya kupiga chuku matukio yaliyo hadithini.
j) Mighani hurithishwa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
k) Huchukuliwa na jamii kama hadithi zenye ukweli na jamii hujinasibisha na mighani hiyo.
g) Husimulia mambo ya kiimani na kidini.

Umuhimu

a) Kutambulisha jamii kwani kila jamii ina aina yake ya mighani.
b) Kuhifadhi na kumbusha historia yajamii.
c) Kusifu mashujaa katika jamii.
d) Kuhimiza ujasiri miongoni mwa vijana.
e) Kuelimisha jamii kwa kuwapa maarifa ya kukabiliana na adui au changamoto.
f) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga mashujaa na kupigania jamii.
g) Kuonya dhidi ya matendo hasi kama vile usaliti.
h) Kuhimiza watu kutokata tama.

Tofauti Kati ya Mighani na Visasili

mighani	visasili
⇒ Husimulia kuhusu mashujaa.	⇒ Husimulia asili ya vitu.
⇒ Husimulia historia ya jamii.	⇒ Husimulia mianzo ya vitu au mambo.
⇒ Wahusika wakuu	⇒ Wahusika ni k.v.

ni majagina.
⇒ Hueleza sifa za majagina.

binadamu, miungu, wanyama, n.k.
⇒ Hueleza mianzo ya desturi.

ii) Visakale

⇒ Masimulizi ya matukio yaliyotendeka zamani k.v. vita, majanga kama njaa na magonjwa na hamahama za jamii k.v. waisraeli kutoka misri.

iii) Visaviini

⇒ Hadithi zinazoeleza chimbuko la jamii Fulani

iv) Mapisi

⇒ Maelezo ya kihistoria yasiyo na ubunifu wowote k.v. chimbuko la kundi la wabantu kutoka Afrika ya Kati na kuenea sehemu mbalimbali za Afrika.

v) Tarihi

⇒ Maelezo kuhusu matukio ya kihistoria kulingana na yalivyofuatana ki wakati

vi) Kumbukumbu

⇒ Maelezo ya kitawasifu kuhusu mtu au jamii inayotambulika kwa kutoa mchango fulani mkubwa.

3. **Vipera Vingine vya Hadithi**

i) Soga

⇒ Hadithi fupi za kuchekesha zinazolenga kutania au kudhihaki.

Sifa

a) Wahusika ni wa kubuni.
b) Hutaja ukweli unaoumiza.
c) Hutumia vichekesho kupunguza ukali wa dhihaka.
d) Hutumia chuku kupita kiasi.
e) Huhusu tukio moja.
f) Ni fupi.

Umuhimu

a) Kukashifu matendo hasi kwa njia ya ucheshi
b) Kuonya na kutahadharisha dhidi ya matendo hasi k.v. ulaghai.
c) Kufunza maadili.
d) Kuburudisha kwa kuchekesha.

ii) Vigano

⇒ Hadithi fupi zinazosimulia kuhusu matendo mabaya katika jamii na wakati uo huo kuonya na kuelekeza dhidi yayo.
⇒ Aghalabu huandamana na methali kwa lengo la kufafanua linalokusudiwa au kudhibitisha funzo la methali fulani.

Sifa

a) Huwa vifupi.
b) Husimulia kisa kimoja tu.
c) Wahusika ni binadamu na wanyama.
d) Hufunza maadili kutokana na methali.

iii) Kisa

⇒ Masimulizi mafupi yenye tukio moja lenye funzo kwa njia ya kufurahisha.

Mambo ya Kuzingatia katika Uchambuzi wa Hadithi/Ngano

a) Kueleza aina ya ngano kwa kuzingatia wahusika na maudhui
✓ Ngano yaweza kuwa ya mazimwi na ya mashujaa kwa wakati mmoja.
✓ Ngano yaweza kuwa hurafa, ya usuli na ya kiayari.
b) Kutaja wahusika
c) Kufafanua sifa za wahusika wakuu
d) Maadili/mafunzo yanayojitokeza katika hadithi
e) Kubainisha sifa za ngano/hurafa/hekaya, n.k. zinazojitokeza katika hadithi.
f) Kueleza umuhimu wa fomyula ya kuanzia/wimbo uliotumiwa katika hadithi.
g) Kubainisha tamathali za usemi zilizotumiwa katika hadithi fulani
h) Kuonyesha jinsi ngano inavyoshughulikia maudhui fulani.
i) Kufafanua ufaafu wa methali fulani zilizotumiwa katika hadithi.
j) Katika ngano ya mtanziko, ungekuwa mhusika mkuu ungefanya nini?
k) Kubainisha matumizi ya mbinu ya fantasia
l) Kufafanua maswala ibuka/maudhui yaliyoshughulikiwa k.m. usaliti, ujinga, ulaghai, n.k.

m) Kuchanganua utungo kifani-ploti, wahusika, mbinu za lugha, fantasia, nyimbo, n.k.
n) Kueleza majukumu ya hadithi.

SEMI

⇒ Tungo fupi zinazowasilisha ujumbe kwa kufumba au kuchora picha.

Sifa

a) Huwa fupi kwa kuwasilisha ujumbe mrefu kwa maneno machache.
b) Ni tanzu tegemezi kwa hutegemea tanzu nyingine kama vile hadithi, mazungumzo, n.k.
c) Hazibadiliki vivi hivi.
d) Baadhi ni kielelezo cha maadili k.v. methali.
e) Hutumia lugha ya kimafumbo.
f) Huibua taswira.
g) Huwa na mchezo wa maneno.
h) Baadhi huwa na muundo maalum k.v. methali na vitendawili.
i) Nyingine ikikosa kutumika hutoweka k.v. misimu.

Umuhimu

a) Kuonya k.m methali, ‘Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.’
b) Kukuza uwezo wa kufikiri k.m. vitendawili na chemsha bongo.
c) Kutafsidi lugha au kupunguza ukali wa maneno k.m. nahau ‘jifungua’ badala ya ‘zaa’.
d) Kuburudisha k.m. vitendawili, chemsha bongo na vitanza ndimi.
e) Kuhifadhi siri k.m. nahau, misemo, misimu.
f) Kuelimisha k.m. kutofanya mambo kwa pupa-mla kwa pupa hadiriki kula tamu.
g) Kuongeza utamu katika lugha.
h) Kuboresha matamshi k.m. vitanza ndimi.
i) Kukuza lugha k.m misimu.
j) Kukuza utangamano katika jamii kwa kuleta watu pamoja wakati zinawasilishwa.

Vipera vya Semi

i) **Methali**

⇒ Semi fupi ambazo hueleza kwa muhtasari au mafumbo ukweli fulani wa kimaisha.

Sifa

a) Huwa fupi k.m. ‘Msafiri kafiri.’
b) Hutumia tamathali za usemi.
c) Hutumkia lugha ya kimafumbo.
d) Huwa na maana ya ndani na nje.
e) Kunazo hufanana kimaana k.m. ‘Haraka haraka haina baraka’ na ‘Polepole ndio mwendo.’
f) Hupingana zenyewe k.m ‘Polepole ndio mwendo’ na ‘Chelewa chelewa utamkuta mwana si wako.’
g) Huwa na sifa za kishairi k.v. ukwapi, utao na vina -Ha**b**a na ha**ba,** hujaza kiba**ba.**
h) Sifa za utegemezi kwa kuingiliana na tanzu nyingine za fasihi.
i) Huwa na muundo maalum wa sehemu mbili:
i) Wazok.m ‘Haba na haba…’
ii) Kukamilisha wazo ‘…hujaza kibaba.’

Umuhimu

a) Kukuza uwezo wa kufikiri kwani mpokezi hufikiri ili kupata maana ya ndani.
b) Kuonya dhidi ya matendo yasiyofaa k.m. ‘Mchimba kisima huingia mwenyewe’na ‘Ukiambiwa jiambie usijeishia kumbe.’
c) Kufariji walio katika hali ngumu, Baada ya dhiki faraja, Hakuna marefu yasiyo na ncha, Liandikwalo ndilo liwalo, Ajaliwalo ndilo apatalo.
d) Kuhimiza watu kujitahidi maishani/kuonyesha jambo jema huja kwa kufanyiwa kazi k.m. ‘Mtaka cha mvunguni sharti ainame,’ ‘Chumia juani ulie kivulini.’
e) Kupamba lugha iwe na mvuto kwani huwa na usanii mkubwa.
f) Kuhimiza ushirikiano, ‘Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, ‘Jifya moja haliijiki chungu.’
g) Kuelimisha mtu ajue jambo muhimu k.m. ‘Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi’, ‘Pema usijapo pema ukipema si pema tena.’

h) Kushauri k.m. ‘Enga kabla ya kujenga’ na ‘Mchama ago hanyeli.’
i) Kufupisha maadili katika ngano.
j) Kubuni lakabu k.m. ‘kikulacho.’
k) Kufunza maadili k.m. kuwa na subira-‘Subira huvuta heri.’
l) Kuhimiza kutokata tama k.m. ‘Bandu bandu huisha gogo’ ‘Papo kwa papo kamba hukata njiwe.’
m) Kuonyesha umuhimu wa kuthamini jamaa zako kuliko marafiki k.m. ‘Damu ni nzito kuliko maji’ ‘Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.’
n) Kuonyesha umuhimu wa kuthamini vitu vyako-‘Usiache mbachao kwa msala upitao’ ‘Afadhali dooteni kama ambari kutanda,’
o) Kukashifu ubinafsi k.m. ‘Mwamba ngoma huvutia kwake’ ‘Kila mchukuzi husifu mzigo wake.’
p) Kukashifu kiburi k.m. ‘Maskini akipata matako hulia mbwata’ ‘Zingwi zingwi lipe nguo utaona mashauo.’

Mbinu za Lugha/Fani /Tamathali za Usemi katika Fasihi

⇒ Maneno au vifungu vya maneno vinavyotumiwa kutia fasihi urembo ili kufanya ujumbe ueleweke vyema zaidi.

Aina

1. Tashbihi

⇒ Ulinganishi kwa kutumia viunganishi kama, mithili, mfano na sawa.

2. Sitiari/ Istiara

⇒ Ulinganishi usio wa moja kwa moja.

3. Tashhisi/Uhaishaji

⇒ Kukipa kitu sifa ya uhai.

4. Taashira/ Ishara

⇒ Kitu kuwakilisha kingine.

5. Chuku/udamisi

⇒ Kutia chumvi au kufanya kitu kionekane kikubwa sana au kidogo sana.

6. Takriri

⇒ Urudiaji wa neno au mafungu ya maneno.

7. Tanakuzi

⇒ Maneno yaliyo kinyume
8. Tabaini
⇒ Msisitizo kwa njia ya kinyume kwa kutumia kikanushio si.
9. Ritifaa
⇒ Kusemesha asiyekuwapo kama yupo.
10. Taharuki
⇒ Kuacha msomaji akiwa na hamu ya kutaka kujua kipi kitakachojiri halafu.
11. Majazi
⇒ Majina yanayooana na sifa za wahusika, vitu au mahali.
12. Mbinu rejeshi
⇒ Kukumbusha mambo yaliyopita.
13. Methali
⇒ Semi fupi ambazo hueleza kwa muhtasari au mafumbo ukweli fulani wa kimaisha.
14. Nahau
⇒ Fungu la maneno lenye maana tofauti na maana ya kawaida ya maneno hayo.
15. Misemo
⇒ Semi zinazobeba ukweli wa kujumla Mifano:
16. Mdokezo
⇒ Mambo kuachwa bila kumalizwa.
17. Balagha
⇒ Maswali yasiyohitaji majibu.
18. Taswira
⇒ Ujenzi wa picha akilini.
19. Kinaya
⇒ Mhusika kutumia maneno au matendo yaliyo kinyume cha inavyotarajiwa.
20. Koja
⇒ Kuorodhesha maneno na vitenzi kwa kutumia koma.
21. Kejeli
⇒ Kudharau au kubeza.
22. Jazanda
⇒ Kufananisha vitu kwa mafumbo k.m. katika biblia.
23. Nidaha/ Siyahi
⇒ Maneno ya kuonyesha hisia za moyoni.

24. Tanakali/onomatopeya
⇒ Miigo ya sauti zinazotokea baada ya kitendo.
25. Uzungumzi nafsia
⇒ Kujisemesha mwenyewe.
26. Dayalojia
27. Utohozi/ Uswahilishaji
28. Kuchanganya ndimi
⇒ Kutumia lugha ngeni.
29. Tafsida/usafidi
⇒ Kutumia lugha ya adabu au kupunguza ukali wa maneno.
30. Mkengeuko
⇒ Kwenda kinyume na matakwa ya jamii k.v. usenge, ndoa ya watu wasio wa rika rika moja, mapenzi nje ya ndoa.
31. ulinganuzi
⇒ Kuweka pamoja mambo yanayopingana ili kulinganisha
32. Kweli kinzani
⇒ Hoja mbili zinazopingana/kutowezekana.

Matumizi ya Lugha Katika Methali

Sitiari

a) Mgeni ni kuku mweupe.
b) Ahadi ni deni.
c) Upweke ni uvundo.
d) Mgeni ni kuku mweupe.
e) Ujana ni moshi.
f) Mapenzi ni kikohozi.
g) Kukopa arusi kulipa matanga.

Tashbihi

a) Kawaida ni kama sheria.
b) Riziki kama ajali ijapo huitambui.
c) Usilolijua ni kama usiku wa giza.
d) Ufalme kama mvua hupiga na kupita.

Tashhisi

a) Siri ya mtungi muulize kata.
b) Paka akiondoka panya hutawala.
c) Jembe halimtupi mkulima.
d) Ukupigao ndio ukufunzao.
e) Adhabu ya kaburi aijuaye maiti.

Takriri

a) Haba na haba hujaza kibaba.
b) Chovya chovya humaliza buyu la asali.
c) Hauchi hauchi unakucha.
d) Hayawi hayawi huwa.
e) Mtoto wa nyoka ni nyoka.
f) Bandu bandu huisha gogo.

Balagha

a) Pilipili usiyoila yakuwashiani?
b) Angurumapo samba mcheza ni nani?
c) Wameshindwa wenye pembe seuze wewe kipara?
d) Simba mla watu akiliwa huwani?
e) Mzigo uko kichwani, kwapa lakutokeani jasho?
f) Mavi usiyoyala wayawingiani kuku?
g) Mla ni mla leo mla jana kalani?

Taswira

a) Mpanda farasi wawili hupasuka msamba.
b) Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.
c) Mtupa jongoo hutupa na ung`ong`o wake.
d) Angeenda juu kipungu hafikii mbingu.

Chuku

a) Mzigo wa mwenzio ni kanda la sufi.
b) Maji ya kifuu bahari ya chungu.
c) Usipoziba ufa utajenga ukuta.

Tanakali za sauti

a) Chururu si ndondondo!
b) Ndo! Ndo! Hujaza ndoo.
c) Kiliacho pa kijutie.

Kinaya

a) Bara Hindi ndiko kwenye nguo na waendao uchi wapo.
b) Kwenye miti hakuna wajenzi.
c) Asante ya punda ni mateke.
d) Kigumba kwa nguruwe kwa binadamu ki uchungu.
e) Kikiharibika cha fundi kikiongoka cha bwana Sudi.

Kejeli/dhihaka/stihizai

a) Umekuwa mung`unye waharibikia ukubwani.
b) Hawi Musa kwa kubeba fimbo.
c) Ucha Mungu si kilemba cheupe.
d) Kichwa cha kuku hakistahili kilemba.

e) Kichwa cha nyoka hakibandikwi mtungi.

Jazanda

a) Joka la mdimu hulinda watundao

⇒ Mtu mwovu huwanyima wengine vitu asivyovihitaji.

b) Kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma

⇒ Ni rahisi kujitia katika matata kuliko kujitoa.

Taashira

a) Kimya kingi kina mshindo mkubwa.

b) Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.

Kweli kinzani

a) Wagombanao ndio wapatanao.

b) Ukupigao ndio ukufunzao.

c) Kuinamako ndiko kuinukako.

d) Mwenye kelele hana neno.

e) Kimya kingi kina mshindo mkubwa.

Tanakuzi

e) Tamaa mbele mauti nyuma.

f) Mpanda ngazi hushuka.

g) Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.

⇒ Kuainisha methali kutokana na matumizi ya lugha ni kusema mbinu ambazo imetumia.

Vigezo vya Kuainishia Methali/Kuziweka Pamoja na kuzichambua

a) Mandhari/mazingira k.m. kilimo.

⇒ Ukipanda pantosha utavuna pankwisha.

⇒ Jembe halimtupi mkulima.

b) Maudhui k.m. ulezi

⇒ Samaki mkunje angali mbichi.

⇒ Mcha mwana kulia hulia yeye

c) fani/tamathali k.m. takriri

⇒ Haba na haba hujaza kibaba

⇒ Mtoto wa nyoka ni nyoka.

d) Jukumu k.m. kuonye

⇒ Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

⇒ Ukiambiwa jiambie usijeishia kumbe.

f) Maana k.m. sawa

⇒ Haraka haraka haina baraka.

⇒ Polepole ndio mwendo.

Vigezo zaidi vya kuchambua methali

g) Inarejelea vitu gani? K.m. Hindi ndiko kwenye nguo na waendao uchi wapo.

⇒ Nchi-Hindi

⇒ Vitu-nguo

⇒ Watu-waendao uchi

h) Inakupa wazo gani kuhusu jamii husika?

⇒ Utamaduni na njia za kiuchumi.

ii) **Vitendawili**

⇒ Semi ambazo hutolewa kwa mtu kwa mfano wa swali ili azifumbue.

Sifa

a) Huwa vifupi kimaelezo.

b) Hutumia lugha ya kimafumbo.

c) Hutolewa mbele ya hadhira.

d) Hutumia ufananisho wa kijazanda.

e) Kunazo huhusiana na methali k.m. mzee amekufa vyombo vimevunjikavunjika.

f) Huwa na wakati maalum wa kutolewa yaani jioni.

g) Huwa na mchezo wa maneno k.m. Ukiona njigi utadhani njege.

⇒ Maziwa na tui

h) Hujisimamia vyenyewe.

i) Kunavyo huwa na jibu zaidi ya moja k.v. Gari la kila mtu

⇒ miguu, kifo au jeneza

j) Hutumia tamathali za lugha kwa ufanifu mkubwa

k) Huweza kuwa na fomyula/muundo maalum

i. Mteguaji: Kitendawili
ii. Mteguaji: Tega
iii. Mteguaji: Kitendawili chenyewe- Popoo mbili zavuka mto
iv. Mteguaji : Mlango
v. Mtegaji: Umenoa. Nipe mji.
vi. Mteguaji: Ninakupa Nairobi.
vii. Mteguaji: Nilienda Nairobi watu wa Nairobi wakaniambia nije niwasalimu. Jibu ni macho.

Umuhimu

a) Kuburudisha jioni baada ya kazi.
b) Kukuza ubunifu wa kuvitunga kwa kulinganisha vitu katika mazingira ili kuviunda.
c) Kuimarisha uwezo wa kukumbuka.
d) Kukuza uwezo wa kufikiri kwani mfumbiwa huhitaji kufikiri sana ili kupata jibu.
e) Kuleta umoja na ushirikiano katika jamii kwa kuleta watu pamoja wakati vinategwa.
f) Kuimarisha ujuzi wa kujieleza kwa lugha.
g) Kupanua ujuzi wa mazingira wa mtoto.
h) Kuendeleza utamaduni wa jamii k.m. Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini. siwezi kulichuma
⇒ Ndugu wa kiume asimuoe nduguye wa kike.
i) Kukejeli au kudharau tabia mbaya k.m. Wazungu wawili wanachungulia dirishani
⇒ makamasi

Aina za vitendawili

a) Sahili
⇒ Vina muundo rahisi/maneno machache k.m Akiona mwangaza wa jua hufa-samaki.
b) Tata
⇒ Vyenye majibu tofauti
c) Kisimulizi
⇒ Masimulizi k.m. Kulikuwa na baba ng’ambo moja ya mto na binti zake wawili ng’ambo ya pili. Alikuwa na maembe mawili aliyopaswa kuyavukisha pamoja apelekee binti zake. Angefanya nini?
d) Vya tanakali k.m. Parrrr! Mpaka Makka-utelezi.
e) Mkufu
⇒ Vyenye sehemu zinazochangizana kimaana k.m. Nikitembea yuko lakini nikiingia nyumbani hupotea-kivuli.

Matumizi ya Lugha Katika Vitendawili

Tashhisi

a) Amefunika kote kwa blanketi lake jeusi-giza.
b) Akivaa nguo hapendezi, akiwa uchi hupendeza mno-ndizi.
c) Anakula lakini hashibi-kifo/mauti.

d) Amchukuapo hamrudishi-kaburi.
e) Akizungumza kila mtu hubabaika-radi.
f) Daima nasababisha mafarakano-uke wenza.

- **Tashbihi**

a) Boi wangu kazama kaibuka kama mzungu-mwiko wa ugali.

Sitiari

b) Bibi hatui mzigo-konokono.
c) Mamangu hachoki kunibeba-kitanda.
d) Fatuma mchafu-ufagio.
e) Saa yetu kadiri inavyotembea ndivyo inavyopunguza nguvu-moyo.
f) Mzungu kujishika kiuno- kikombe.
g) Nina mapapai yangu mawili ambayo siwezi kuyala- matiti ya mwanamke.
h) Ng`ombe wangu nisipomshika mkia hali nyasi-jembe.
i) Kitu changu kitumiwacho na wengine kuliko mimi-jina.
j) Popoo mbili zavuka mto-macho.
k) Gari la kila mtu-miguu.
l) Dada ni mrembo lakini akiguzwa analia-papai.

Takriri

a) Huku ng`o na kule ng`o-giza.
b) Amezaliwa Ali, amekufa Ali, amerudi Ali-nywele.
c) Huku fungu katikati bahari-naz.i

Tanakali

a) Parrr! Mpaka Makka-utelezi.
b) Huku pi kule pi-mkia wa kondoo atembeapo.
c) Ba funika ba funua (Bak bandika, bak bandua)-nyayo.
d) Tang! Yaanguka-sarafu.

Kweli kinzani

a) Ana meno lakini hayaumi-kitana.
b) Ajenga ingawa hana mikono-ndege.
c) Hukopa lakini halipi-kifo.
d) Nina shamba langu kubwa lakini nikivuna halijai hata kofi-nywele.
e) Hufa akifufuka-bahari kupwa.
f) Nameza lakini sishibi-mate.

Taswira

a) Adui tumemzingira lakini hatumwezi-moto.
b) Nyama nje, ngozi ndani, mchanga ndani-firgisi ya kuku.
c) Wanatazamana tu lakini hawaamkiani-ardhi na bingu.
d) Askari wangu wote wamevaa kofia upande-mahindi shambani.
e) Samaki wangu aelea kimgongomgongo-merikebu.
f) Babu amebeba machicha meupe kichwani- mvi.

Stihizai/dhihaka/kejeli

a) Akivaa miwani hafanyi kazi vizuri-mlevi.
b) Mzungu anachungulia dirishani-makamasi.
c) Uzi mwembamba umefunga dume-usingizi.
d) Mtani wangu hata akiishi majini hatakati-chura.
e) Kisiki chetu hakikui-mbilikimo.
f) Nimemuona bi kizee amejitwika machicha-mvi.

Jazanda

a) Mungu alinipa shilingi mbili, moja nitumie nyingine niweke-ardhi na mbingu.

⇒ Kuchambua kitendawili kwa kueleza mbinu za lugha zilizokiunda.

Kulinganisha vitendawili na methali

Kufanana

✓ Zote mbili ni tungo fupi.
✓ Zote mbili huwa na maana fiche.
✓ Zote mbili hutumia lugha inayojenga taswira.
✓ Zote mbili hupata maana kulingana na jamii.
✓ Zote mbili Huwa na muundo maalum.
✓ Zote mbili hufumbata ukweli fulani wa kijamii.

Tofauti

Vitendawili	**Methali**
✓ Vina fomyula maalum ya uwasilishaji.	✓ Hazina fomyula.
✓ Fumbo lazima lifumbuliwe papo hapo.	✓ Fumbo halifumbuliwi papo hapo.
✓ Maarufu zaidi miongoni mwa watoto/vijana.	✓ Kuonyesha hekima hasa miongoni mwa watu wazima na wazee.
✓ Hutolewa katika vikao maalum.	✓ Si lazima zitengewe vikao.
✓ Hadhira tendi inayotoa	✓ Hadhira si tendi.
	✓ Kauli moja ya msemaji

maana
- ✓ Hutumia lugha ya majibizano.

iii) **Chemsha Bongo**

⇒ Maswali ambayo huhitaji mtu kutumia akili na ujuzi kuyajibu.

⇒ Mafumbo ni kauli zenye maana iliyofichika na hujumuisha vitendawili na chemshabongo.

Mifano

a) Kilo moja ya chuma na kilo moja ya nyama ipi nzito?
b) Amada ana wafanyikazi saba, wanne hufanya kazi vizuri, wawili ni kama wamekufa, mmoja ni kama mwenda wazimu- miguu, pembe na mkia wa ng'ombe.
c) Kipungu alipita juu, mama na ndege wawili wakamwangalia. Je macho mangapi yalimuona kipungu?- manne.
d) Nina watu wangu watatu, wawili ni watoto na wawili ni baba- mtoto, baba na babu.
e) Chura alitumbukia katika shimo la futi 30 na anaruka futi 10. Aruke mara ngapi ili atoke?- Hawezi.
f) Watu watatu wanavuka mto. Mmoja aliyaona maji na kuyakanyaga. Wapili aliyaona lakini hakuyakanyaga. Watatu hakuyaona wala kuyakanyaga. Watu hao ni kina nani?

Sifa

a) Ni kauli fupi au ndefu.
b) Hutuia lugha ya kimafumbo.
c) Hutumia ufananisho wa kijazanda.
d) Huhitaji mtu kuwaza ili kupata jibu.
e) Hujengwa na vitu vinavyotokana na mazingira.
f) Hazina muundo maalum kama methali, nahau na vitendawili
g) Hupima uwezo wa msikilizaji wa kutambua jambo lililofichwa.

Umuhimu

a) Kuimarisha stadi ya kusikiliza.
b) Kunoa uwezo wa kufahamu.
c) Kutoa mawaidha.

d) Kufunza kuhusu maumbile.
e) Kuimarisha uwezo wa kukumbuka.
f) Kufunza mambo kuhusu mazingira na maumbile.
g) Kukuza uwezo wa kutumia lugha.
h) Kukuza uwezo wa kufikiri.
i) Kuburudisha na kuchekesha.
j) Kukuza uwezo wa kubuni.

iv) **Vitanza Ndimi**

⇒ Sentensi zenye mfuatano wa sauti zinazotatanisha kimatamshi zinapotamkwa kwa haraka.

Mifano

c) Wataita wataita Wataita wa Taita.
d) Waite wale wana wa liwali wale wali wa liwalii
e) Kupa mpe akupao kumpa asokupa si kupa ni kutupa.
f) Shirika la Reli la Rwanda limefungwa.
g) Hilo lililoliwa ndilo nililolitaka.
h) Mchuuzi wa mchuzi hana ujuzi wa mjusi wa juzi.
i) Cha mkufuu mwanafuu ha akila hu cha mwanafuu mkufuu hu akila ha
j) Pema usijapo pema ukipema si pema tena
k) Nguo zisizotakikana zitachomwa zote.

Sifa

a) Ni kauli fupi.
b) Huwa na mchezo wa maneno.
c) Huundwa kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi.
d) Hutumia maneno yenye maana zaidi ya moja au yenye sauti sawa.
e) Hutanza/hutatiza ndimi za wengi wakalemewa kutamka.
f) Hukanganya kimatamshi.

Umuhimu

a) Kukuza matamshi bora mtu anapoendelea kutamka.
b) Kukuza uwezo wa kufikiri haraka ili kujua maana za maneno ili kutamka ipasavyo.
c) Kupanua ujuzi wa msamiati.
d) Kuburudisha kwa kufurahisha na kuchangamsha.
e) Husaidia kutofautisha maana za maneno.
f) Kujenga stadi ya kusikiliza.

g) Kukuza ubunifu kwa kuteua maneno yanayotatanisha kisauti na kimaana.
h) Kujenga uhusiano bora kwa ucheshi.
v) **Lakabu**
⇒ Jina la msimbo/kupanga/ambalo mtu hupewa au hujipa kutokana na sifa zake.

Asili ya Lakabu
a) Tabia
b) Sifa za kimaumbile
c) Matendo
d) Nasaba atokayo mtu.
e) Tabaka
f) Jinsi mtu anavyotamka maneno k.m. ung'eng'e.

Mifano
a) Nyayo
⇒ Moi
b) Simba wa Yuda
⇒ Haille Selassie
c) Mkuki uwakao
⇒ Kenyatta
d) Nyundo/Tingatinga
⇒ Raila
e) Baba wa taifa
⇒ Rais
f) Mama wa Taifa
⇒ Mke wa Rais

Sifa
a) Huwa neno au fungu la maneno kadha.
b) Huwa na maana iliyofumbwa.
c) Huoana na sifa hasi au chanya za aliyepewa.
d) Huwa za kusifu au kudhihaki.
e) Huweza kudumu hata kusahaulisha jina halisi la mtu.
f) Hutumia sitiari k.m. chui kumaanisha mkali.
g) Hutumia taswira.
h) Hushika sana kimatumizi miongoni mwa watu.

Umuhimu
a) Kufahamisha sifa za mtu kwa kifupi.

b) Huwa njia ya washairi ya kujitangaza bila kujisifu moja kwa moja.
c) Hutumiwa kama ishara ya heshima kwa anayestahili heshima k.m. kiongozi.
d) Kuficha utambulisho au jina halisi la mtu.
e) Hutumiwa katika majigambo na mhusika kuonyesha ubingwa wake.
f) Kuficha siri ili anayemrejelewa asijulikane k.m. kikulacho.
g) Kukuza uhusiano bora miongoni mwa watani wanaporejeleana kwa lakabu.
h) Kusifu tabia njema kwa kumpa mtu lakabu nzuri.
i) Kudhihaki au kukashifu tabia mbaya kwa kumpa mtu lakabu mbaya
j) Kutambulisha asili ya mtu.

vi) **Misemo**

⇒ Semi zinazobeba ukweli wa kijumla.

Mifano

a) Binadamu ni udongo.
b) Mwili haujengwi kwa mbao.
c) Umaskini si kilema.
d) Lila na fira havitangamani.
e) Ndio kwanza mkoko ualike maua.

⇒ Mambo kuzidi kushika kasi.

f) Mgomba haupandwi changaraweni ukamea

⇒ Jambo halifanywi mahali pasipofaa likapendeza.

Sifa

a) Hutumia lugha ya muhtasari.
b) Hutoa ukweli kwa jumla.
c) Hazina muundo maalum.

Umuhimu

a) Kusisitiza ujumbe.
b) Kuongeza utamu katika lugha.
c) Kusisitiza jambo fulani.
d) Kufunza maadili au kuhimiza.
e) Kuchochea hisi fulani.

vii) **Nahau**

Fungu la maneno lenye maana tofauti na maana ya

kawaida ya maneno hayo.

Mifano

a) Kuasi ukapera
   ✓ kuoa
b) Kupiga vijembe
   ✓ sema kwa mafumbo
c) Ndege mbaya
   ✓ bahati mbaya
d) Kidudu mtu
   ✓ mfitini
e) Paka mafuta kwa mgongo wa chupa
   ✓ Danganya au hadaa mtu
f) Visha kilemba cha ukoka
   ✓ Mpa mtu sifa za uongo ili umpumbaze
g) Kubali shingo upande
h) Kuyavulia maji ngu
   ✓ kumaliza jambo fulani ulilolianzia
i) Arusi ya ndovu kumla mwanawe
   ✓ kubwa

Sifa

a) Hutumia lugha ya kimkato.
b) Maneno huwa na maana tofauti na ya kawaida.
c) Kunazo huwa na maana zaidi ya moja k.v. kuja jamvi-kumaliza shughuli au kuondoka.
d) Huundwa kwa neno moja, mawili au zaidi.
e) Huibua taswira.
f) Zina muundo maalum/huundwa kwa aina mbalimbali za maneno.

i. T+T
   ✓ kufa kupona
   ✓ kufumba na kufumbua
ii. T+N
   ✓ kupiga domo
   ✓ kata kamba
iii. T+E
   ✓ Kujikaza kisabuni
   ✓ kufa kiofisa
iv. N+N

✓ donda dugu
✓ domo kaya

v. N+V
✓ nyota njema
✓ dege mbaya

vi. N+T
✓ damu kumkauka
✓ akili kumruka

Umuhimu

a) Kukuza na kuendeleza msamiati wa maneno.
b) Kupunguza ukali wa maneno (tafsida).
c) Kuongeza utamu/ladha katika lugha.
d) Kuhifadhi siri kwani sio wote wanajua maana.
e) Kujaribu uwezo wa msikilizaji kufichua maana iliyofichika.

viii) **Misimu/simo**

⇒ Semi ambazo huzuka katika mazingira na kipindi fulani.

Aina za Mizimu

1. Inayotumika na kutoweka
2. Inayokita kimatumizi kuingizwa katika Kiswahili sanifu k.m. toa chai, chokora, n.k.

Asili

a) Ufupishaji maneno
✓ komp
b) Utohozi
✓ Fathee
✓ hepi
c) Sitiari/jazanda
✓ nyani-mlinda lango
✓ fisi- mlafi
d) Tanakali
✓ mtutu- bunduki
✓ ndala- malapulapu
e) Uundaji maneno mapya
✓ hanya
f) Kupa maneno maana mpya
✓ chuma-gari
✓ toboa- faulu

g) Kugeuza maneno
✓ risto-stori
h) Kuboronga lugha
✓ ashu-ashara/kumi

Mifano

a) Jisikia sukari
⇒ kuringa
b) Kaa ngumu
⇒ kutotishika/kuvumilia
c) Chongoa mtu
⇒ mfanyia mzaha
d) Kula njaro
⇒ kupuuza kazi
e) Piga nduthe
⇒ kimbia/toroka
f) Piga ngeta
⇒ kukaba koo
g) Leta diambo
⇒ zozana/lalamika
h) Ingia baridi
⇒ kuogopa
i) Pewa msomo
⇒ gombezwa
j) Kusota
⇒ kuishiwa na pesa
k) Ingia mitini
⇒ toweka/toroka
l) Kung`ara
⇒ kuvaa vizuri
m) Marehemu George
⇒ nguo za mitumba
n) Vaa chupa
⇒ vaa suruari nyembamba
o) Kujisikia poa
⇒ kuwa na furaha
p) Kula hepi
⇒ kuburudika
q) Lala kibahasha

⇒ tulia tuli baada ya kushindwa katika jambo

Sifa

a) Ni kauli fupi.
b) Hutumiwa na kundi dogo la watu.
c) Huzuka katika mazingira na kipindi maalum.
d) Ni lugha ya kimafumbo.
e) Hutumiwa na kundi dogo la watu katika jamii.
f) Huzuka na kutoweka baada ya muda.
g) Kunazo hudumu na kukubaliwa kama lugha sanifu k.v. matatu, bodaboda, chai, chokora, daladala, n.k.
h) Huwa na maana nyingi k.m. ‘mahewa’ humaanisha mziki, uongo au ulevi wa dawa za kulevya.
i) Maneno yana maana tofauti na ya kawaida.
j) Si lugha sanifu na hivyo haipaswi kutumiwa katika mazungumzo rasmi.
k) Hupendeza miongoni mwa watumizi.
l) Hutoweka baada ya matumizi kwa muda.
m) Hubadilika k.m. mbuyu na buda humaanisha baba.

Umuhimu

a) Kuficha siri ya wanaoitumia.
b) Kupanua lugha kimsamiati ikikubalika.
c) Kurahisisha mawasiliano kwa kuondoa uchovu wa urasmi.
d) Kuonyesha ubingwa wa lugha kwa kuhisi huonyesha umaarufu wa lugha
e) Kutenga wasio wana kikundi.
f) Kutafsidi/kupunguza ukali wa maneno k.m. Amepata bol-mimba.
g) Kupamba lugha na kuifanya ivutie
h) Kufanya wanakikundi wajihisi kuwa pamoja.
i) Kujitambulisha na watu wa kikundi fulani.

ix) **Shirikina**

⇒ Semi ambazo huonyesha imani fulani ya kundi ya watu

Mifano

a) Ukijikuna kiganja cha mikono utapata pesa.
b) Ukila chakula gizani utakula na shetani.
c) Kuzaliwa ukiwa na vidole sita ni kuwa na bahati.

d) Bundi akilia karibu na nyumba mtu mmoja wa nyumba ile atafariki.

Umuhimu

a) Kukataza maovu.
b) Kuhifadhi utamaduni.
c) Kuchangia umoja wa kitaifa kwa aina moja ya itikadi kupatikana katika jamii nyingi.
d) Kutujulisha kuhusu itikadi za watu.

x) **Tanakali za Sauti (Onomatopeya)**

⇒ Maneno ambayo huiga sauti ya jambo, tendo au tukio fulani

Mifano

a) Boboka bobobo!
✓ payuka ovyo ovyo
b) Bwakia bwaku
✓ akia upesi upesi
c) Bwatika bwata
✓ enda chini kwa mshindo
d) Bweka bwebwebwe!
✓ lia kama mbwa
e) Chaga ngungundu
✓ shikilia jambo
f) Ng'o!
✓ kutoambulia chochote
g) Legalega lege
✓ kosa kuwa imara
h) Chakua nyakunyaku
✓ tafuna kwa kutoa sauti ya kuudhi
i) Bingirika bingiribingiri!
✓ pinduka
j) Birua biru!
✓ angusha na kupindua
k) Shindilia ndi!

Mianguko

a) Pu/kacha
✓ tawi
b) Pu, pu, pu
✓ mfululizo

c) Pukupuku!
✓ mvua
d) Pwa!
✓ kwa matope
e) Pwata!
✓ kitu kinene
f) Tang’!
✓ sarafu pagumu
g) Tapwi
✓ matopeni
h) Tifu
✓ mchangani
i) Tubwi/ chubwi
✓ majini

Sifa

a) Ni kauli fupi.
b) Ni miigo ya sauti zinazotokea baada ya tendo fulani.
c) Hazina muundo maalum.
d) Hujumuishwa katika fani nyingine.
e) Hutumia takriri.

Umuhimu

a) Kuwezesha kuunda taswira ya jinsi mambo yanavyotokea.
b) Kuonyesha hisia fulani.
c) Kuongeza uzito kwa maneno.
d) Kuongeza utamu katika mazungumzo.
e) Kusisitiza jambo.
f) Kuipa lugha ladha na mvuto.
g) Kujenga tabia ya kusikiliza kwa makini ili kutambua mlio.
h) Kukuza ustadi wa kuiga na kuigiza.
i) Ni mbinu mojawapo ya mawasiliano.

xi) **Takriri za maana**

⇒ Mafungu ya maneno yanayosisitiza na kueleza maana zaidi ya kitendo.

Mifano

a) Haambiliki hasemezeki
b) Siku nenda siku rudi
c) Tilia huku ukitolea kule

d) Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini

Umuhimu

a) Kutia ladha katika lugha na kuifanya iwe na mnato.
b) Kusisitiza jambo.
c) Kuonyesha ukwasi wa lugha ya mnenaji.

xii) **Tashbihi**

⇒ Misemo ya ulinganisho

Sifa

a) Ni fupi.
b) Hutumia viungio kama, mithili ya, n.k.
c) Hulinganisha.
d) Huwa na ujumbe wa kina.
e) Hutoa taswira ambayo husaidia keleza hulka kikamilifu.

Umuhimu

a) Kueleza sifa za kinazozungumziwa
b) Kuongeza lugha utamu
c) Kuonyesha umilisi wa lugha wa mtumizi

USHAIRI

⇒ Utanzu wa fasihi unaotumia lugha ya mkato inayoeleza maudhui yake kwa ufupi.

Sifa

a) Hutumia lugha ya kimkato.
b) Huwasilishwa mbele ya hadhira.
c) Huwasilishwa na mtu mmoja au kundi la watu.
d) Huwa na muundo maalum k.v. beti, vipande na vina.
e) Hutegemea sauti iliyo kipengele muhimu.
f) Huandamana na ishara za mikono, uso n.k.
g) Una mpangilio maalum wa maneno.
h) Una uteuzi maalum wa maneno.
i) Uwasilishaji wake huandamana na vitendo/uigizaji.
j) Hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa mdomo.
k) Huandamana na shughuli maalum k.v. matanga, kazi, n.k.
l) Huwa na mapigo ya kimziki au huweza kuimbika.
m) Huweza kuambatana na ala za mziki.
n) Hadhira hushiriki katika uwasilishaji wa ushairi simulizi.

Majukumu

a) Kuburudisha watu katika sherehe au shughuli fulani ya kijamii.
b) Kutakasa hisia au kutoa hisia zinazomsumbua mtu.
c) Kufunza maadili au tabia zinazokubalika na jamii.
d) Kufariji watu kutokana na maafa, kifo au kushindwa.
e) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga waliotendea jamii mambo makuu k.v. mashujaa.
f) Kuhifadhi historia ya jamii k.m. maghani simulizi na tenzi.
g) Kuhifadhi na kudumisha utamaduni wa jamii.
h) Kuelimisha kuhusu suala fulani.
i) Kukashifu/kukejeli sifa mbaya za wabaya.
j) Kukuza umoja na ushirikiano katika jamii kwa kujumuisha watu pamoja.
k) Kusifu na kutukuza mashujaa katika jamii (tenzi).
l) Kukanya/kutahadharisha dhidi ya matendo maovu.
m) Kukuza urembo au usanii wa lugha kwa kuwa una ufundi mkubwa wa matumizi ya lugha.
n) Kuhamasisha jamii k.v. kisiasa.
o) Kukuza ubunifu kwa mtunzi na mwasilishaji
p) Kukuza ubunifu kwa kutunga kwa kuzingatia beti, mizani, vina na uteuzi maalum wa maneno.

Vipera vya Ushairi

a) wimbo
b) maghani
c) mashairi mepesi (utungo unaokaririwa)
d) ngojera (kwa majibizano)
e) tendi au rara (husimuliwa kwa mapigo ya kishairi)

1. **Wimbo**

⇒ Uungo wenye mahadhi ya kupanda na kushuka

Sifa

a) Huwasilishwa kwa njia ya mdomo.
b) Hutolewa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti.
c) Hutumia lugha ya mkato.
d) Hadhira yaweza kuwepo au isiwepo.
e) Huwa na mwimbaji au waimbaji wanaoimba.
f) Waimbaji wanaweza kujivika maleba.

g) Huweza kuambatana na ala k.v. ngoma, zeze, kayamba n.k.
h) Huwa na urudiaji wa mstari au kifungu.
i) Aghalabu huimbwa na kupokezanwa baina ya kiongozi na waimbaji
j) Huimbwa tu au huambatana na kucheza.
k) Huweza kuandamana na shughuli fulani k.v. arusi, kazi, matanga, n.k.
l) Huwa na muundo maalum wa beti, mistari, vina, n.k.

Majukumu

a) Kuburudisha k.m. tumbuizo.
b) Nyenzo ya kiuchumi kwa baadhi ya watu.
c) Kuliwaza k.m. mbolezi.
d) Kuhimiza watu wakiwa kazini k.m. hodiya.
e) Kuelimisha kuhusu suala fulani k.m. ukimwi, ufisadi, n.k.
f) Kuhimiza uzalendo k.m. za siasa na taifa.
g) Kumbembeleza mtoto aache kulia au alale k.m. bembelezi.
h) Kukashifu/kukejeli mwenendo mbaya k.v. uchoyo, vivu, n.k.
i) Kufunza maadili au tabia inayokubaliwa na jamii k.v. ukarimu, uaminifu, n.k.

Ubaya wa nyimbo

a) Kutumiwa kueneza hisia za kikabila.
b) Kutia watu kasumba.
c) Hutumiwa kueneza propaganda ili kushawishi watu.
d) Kupotosha kimaadili k.v. kuhimiza zinaa.
e) Mtu akizizoea humlevya.

Aina za nyimbo

i) Bembelezi/bembea

⇒ Nyimbo zilizoimbwa kumbembeleza/kumwongoa mtoto aache kulia au alale.

Sifa

a) Huimbwa na mama au walezi.
b) Aghalabu huwa fupi.
c) Huimbwa kwa sauti ya chini.
d) Huimbwa kwa sauti nyororo.
e) Zina mapigo ya polepolena taratibu.

f) Huwa na mahadhi mazuri.
g) Huimbwa aghalabu mtoto akiwa amebebwa kwa mbeleko na mwimbaji akimpapasapapasa.
h) Zina urudiaji wa maneno ya kibwagizo.
i) Huwa na lugha ya kushawishi k.v. kutoa ahadi ya kununulia mtoto zawadi.

Majukumu

a) Kumnyamazisha mtoto anapolia.
b) Kuwaongoa watoto walale.
c) Kutumbuiza watoto.
d) Kusuta wasiowapa watoto malezi mema.
e) Kuonya mtoto dhidi ya tabia hasi k.v. kulia ovyo.
f) Kusifu mtoto.
g) Kuonyesha msimamo wa jamii kuhusu mtoto.
h) Kumfariji mtoto k.m. kutokana na kuumia akicheza.

ii) Nyimbo za watoto/chekechea

⇒ Zilizoimbwa na watoto wakati wa kucheza/shughuli zao

Majukumu

a) Kuburudisha watoto.
b) Kuwaelimisha watoto kuhusu jamii.
c) Kukuza umoja na ushirikiano baina ya watoto kwa kuwajumuisha pamoja na kucheza bila kujali kabila, tabaka, n.k.
d) Kukashifu tabia hasi miongoni mwa watoto k.v. uchoyo.
e) Kukuza ubunifu miongoni mwa watoto wanapobuni nyimbo zinazooana na michezo yao.
f) Kuifanya michezo ya watoto ipendeze.

iii) Nyimbo za sifa/sifo

⇒ Za kujisifu au kusifu mtu kwa mchango wake katika jamii.

Sifa

a) Zaweza kuwa nyiso, za arusi za kutawazwa n.k.
b) Huimbwa katika muktadha maalum k.v. arusini, jandoni, n.k.
c) Hutumia sitiari au kufananisha na mnyama, mkuki, n.k.
d) Hupiga chuku sifa za anayesifiwa.

Majukumu

a) Kusifu mtu kutokana na matendo yake mazuri.

b) Kutangaza mchango na mafanikio ya anayesifiwa.
c) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga matendo mazuri ya anayesifiwa.
d) Kuburudisha watu katika sherehe fulani.
e) Kuangazia matendo ya wahusika.

iv) Hodiya/yimbo za Kazi

⇒ Zilizoimbwa wakati wa kazi.

Sifa

a) Huimwa watu wakifanya kazi k.v. uwindaji, ukulima, uvuvi, ubaharia, n.k.
b) Huimbwa na mfanyakazi mmoja au kundi lao.
c) Zina maneno ya kuhimiza.
d) Urefu wake hutegemea kazi.
e) Mdundo hutegemea kasi ya kazi ikama inafanywa kwa kasi mdundo ni wa kasi, kama polepole mdundo ni wa polepole.

Majukumu

a) Kuburudisha watu wakifanya kazi.
b) Kurahisisha kazi kwa kupunguza fikra za uchovu.
c) Kuhimiza bidii kazini.
d) Kuhimiza watu wapende kazi zao.
e) Kuondoa uchovu na ukinaifu wakati wa kazi.
f) Kuwatia moyo wafanyakazi wasikate tamaa.
g) Kutambulisha jamii kwa kuonyesha shughuli zake za kazi.
h) Kusifu kazi.
i) Kukashifu uvivu.
j) Kuonyesha matatizo na changamoto za wafanyikazi.
k) Kujenga umoja na ushirikiano baina ya wafanyakazi wanapoziimba pamoja. **Aina za hodiya**

a) **Wawe/vave**

⇒ Zinazoimbwa wakati wa kulima.

b) **Nyimbo za uwindaji**

⇒ Zilizoimbwa watu wakienda au kutoka katika uwindaji.

Majukumu

a) Kumburudisha mwindaji.
b) Kumtoa mwindaji upweke.
c) Kusifu mnyama.

d) Kujasirisha wawindaji.

c) **Kimai**

⇒ Zinazoimbwa katika shughuli za majini k.v. uvuvi na ubaharia.

Majukumu

a) Kuburudisha wavuvi na mabaharia.
b) Kuwajasirisha ili kukabili adha za baharini.
c) Kuwatoa upweke.

v) Nyimbo za mapenzi

⇒ Zilizoimbwa kutoa hisia za mapenzi.

Sifa

a) Huwa na ujumbe wa kimapenzi.
b) Maneno matamu yenye hisia nzito.
c) Matumizi ya chuku k.m. sili wala silali.
d) Huwa zina sifa au kashfa.

Mjukumu

e) Kuburudisha anayezisikiliza.
f) Kuomba uchumba au mapenzi.
g) Kusifu tabia au urembo/umbo la mpenzi.
h) Kusifu wapenzi.
i) Kukashifu mpenzi asiye na sifa nzuri.
j) Kusuta waliodhani penzi lisingefaulu.
k) Kupunguza uzito wa hisia k.v. huzuni au udhia baada ya kusalitiwa na mpenzi.

vi) Nyimbo za arusi

⇒ Zinazoimbwa wakati wa kufunga ndoa.

Sifa

a) Huimbwa kuonyesha hisia za wazazi, jamaa na marafiki
b) Hushauri maharusi na waliohudhuria kuhusu majukumu ya ndoa
c) Wakati mwingine husifia maharusi.

Majukumu

a) Kutumbuiza maharusu na waliohudhuria.
b) Kusifu maharusi.
c) Kutoa pongezi kwa Bw. na Bi. arusi kwa kujihifadhi vyema.
d) Kufunza majukumu ya ndoa.
e) Kutoa mwongozo wa kupambana na vikwazo ndoani

f) Kusuta mahasidi waliodhani ndoa isingefaulu.
g) Kukanya na kutahadharisha watu wanaoingilia ndoa za watu kuziharibu.

vii) Nyimbo za Dini

⇒ Zilizoandamana na shughuli za kidini.

Majukumu

a) Kuabudu Mungu ama miungu.
b) Kusifu mungu/miungu.
c) Kutoa shukrani kwa mungu.
d) Kuomba mema kutoka kwa Mungu au miungu.
e) Kutoa mafunzo ya kidini.

viii) Tumbuizo

⇒ Nyimbo za kujipa burudani
⇒ Huimbwa wakati wa mapumziko

Majukumu

a) Kutumbuiza watu k.v. ngomani, arusini, n.k.
b) Kuwapa vijana mwongozo/kuadilisha.

ix) Nyiso/Nyimbo za Tohara

⇒ Zinazohusiana na tohara.

Mfano

Ewe kilizi
Ulozowea kujificha
Nyuma ya mama kujikinga, dhidi ya milio
ya radi ilo juu mbinguni
Jua kesho ni siku ya siku
Siku ya kujua mbichi na mbivu
Kutofautisha jogoo na vipora,
Ngariba taposhika, chake kijembe
Ndipo utakapojua bayani
Ukoo wetu si wa kunguru
Ikiwa hu tayari
Kisu kukidhihaki
Sithubutu kamwe, wanjani kuingia
sije kuniaibisha miye, amiyo na akraba nzima!

Sifa

a) Huambatana na shughuli za jando (wavulana) na unyago (wasichana).
b) Huimbwa faraghani katika mazingira ya tohara pekee.

c) Huimbwa usiku wa kuamkia siku ya tohara.
d) Zilitoa sifa kwa waliotahiriwa, wazazi na wasimamizi wao.
e) Ziliimbwa kuwapa wavulana ujasiri wa kukabili kisu cha ngariba.
f) Zilitoa mafunzo kuhusu majukumu mapya baada ya kutahiriwa.
g) Hujumuisha watu maalum walioteuliwa kushiriki katika sherehe.
h) Huhusisha watu wa jinsia na umri fulani.
i) Maudhui yake hutegemea jinsia.

- **Majukumu**

a) Kuonyesha vijana wamevuka kutoka utotoni hadi utu uzima.
b) Kuwaandaa vijana kwa uchungu watakaouhisi kupitia kijembe.
c) Kuhimiza ujasiri na ukejeli uoga.
d) Kusifu wahusika kwa ujasiri wa kukabili kisu na kuingia katika utu uzima.
e) Kuburudisha waliohudhuria shughuli ya jando au unyago.
f) Kuelekeza vijana kwenye matarajio mapya ya jamii.
g) Kufunza majukumu katika utu uzima.
h) Kukuza umoja na ushirikiano katika jamii kwa kuwaleta wanajamii pamoja.

x) Mbolezo/Mbolezi

⇒ Nyimbo za kuomboleza.

Mfano

Nalitazama jua likichwa,
Matumaini yangu yakizama pamoja
na miale miekundu
Nalidhani lilikuwa jinamizi tu
Kwamba ulikuwa kesha n'acha
Walikuwa wameisha n'ambia
Walimwengu
Ela nilikataa katakata walosema
Nikajitia kuamini waloamba yalikuwa
Uzushi

Hadi siku hii nilopokea waraka,
Waraka ambao ulikuwajeneza ka kuzikia
Pendo letu la miongo miwili.

Sifa

a) Huimbwa wakati wa maafa, kifo, makumbusho ya mtu au kushindwa katika jambo k.v. vita.
b) Huimbwa kwa sauti ya chini.
c) Hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.
d) Huwa na mapigo ya polepole au taratibu.
e) Huimbwa kwa toni ya huzuni/uchungu kuibua hisia za ndani za mwombolezaji.
f) Aghalabu haziandamani na ala.

Majukumu

a) Kuwafariji au kuwasaidia waliofiwa kukabiliana na uchungu wa kupoteza mpendwa wao.
b) Kusifu aliyekufa kwa kutoa sifa zake chanya au michango yao.
c) Kubembeleza roho za wafu(mizimu) ili kusitokee maafa mengine.
d) Kuonyesha msimamo wa jamii kuhusu matokeo ya kifo k.v. husababishwa na pepo, maovu, njia ya kuingia mbinguni.
e) Kutakaswa hisia za huzuni za aliyefiwa kumpunguzia uzito wa kumpotezea mpendwa wake.
f) Kueleza kutoepukika kwa kifo.
g) Kukejeli kifo.

xi) Nyimbo za Taifa

⇒ Nyimbo zinazoimbwa na watu wa taifa fulani.

Majukumu

a) Kutambulisha taifa fulani.
b) Kuonyesha utaifa.
c) Kuonyesha uzalendo (mapenzi kwa nchi).
d) Kuhimiza uzalendo.
e) Kukashifu wasio wazalendo.
f) Kusifu taifa fulani.

xii) Nyimbo za Siasa

⇒ Zinazoimbwa katika shughuli za kisiasa.

Mfano

Ewe mainga wa Ndumi
Siwe uloambia akina mama
Siku tulopiga foleni
Chakula cha msaada kupata
Turudishe vifaranga kwenye miji
Wageuke vijusi tena
Njaa isiwaangamize?
Siwe ulopita
Matusi ukitema
Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?
Ukatununua vihela uloturushia
Ukatununua kura ukapata?
Sasa miaka mitano imetimia
Waja tulaghai tena
Huna lolote safari hii
Ubunge umekudondoka ukitazama
Wanyonge tumea/mua
Kwingine kujaribu

Majukumu

a) Kuburudisha watu katika shughuli za kisiasa.
b) Kupinga dhuluma za viongozi.
c) Kusifu viongozi na sera zao.
d) Kukashifu/kukejeli wanasiasa wabaya.
e) Kuonyesha matarajio ya watawaliwa kwa viongozi.
f) Kusambaza elimu ya kisiasa.
g) Kuwatia wananchi kasumba.
h) Kueneza propaganda za kisiasa.
i) Kuzindua au kuhamasisha jamii kisiasa.
j) Kuliwaza wahasiriwa wa migogoro ya kisiasa.
k) Kutia watu ari ya kufanya jambo fulani k.v. kupigania haki zao.

xiii) Nyimbo za Vita

⇒ Zinazoimbwa na askari vitani au baada ya vita.

Majukumu

b) Kuburudisha washiriki.
c) Kufunza namna ya kukabiliana na adui.
d) Kujasirisha washiriki.

e) Kusifu askari vitani.
f) Kukejeli uoga.
g) Kusifu mashujaa wa zamani.
h) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga masujaa.

xiv) Kongozi

⇒ Za kuaga mwaka katika jamii za waswahili.

xv) Jadiiya

⇒ Nyimbo za jadi ambazo hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
⇒ Huhusu matukio ya kihistoria k.v. shujaa, mateso, njaa, n.k.

xvi) Nyimbo za Kuzaliwa kwa Mtoto

⇒ Za kuonyesha au kuadhimisha kuzaliwa kwa mtoto.

2. **Maghani**

⇒ Ushairi ambao hutolewa kwa kalima.

Sifa

a) Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanapotambwa.
b) Hutolewa kwa kalima.
c) Hutungwa papo hapo.
d) Hutongolewa mbele ya hadhira
e) Hutungwa kwa ufundi mkubwa.
f) Hutolewa na mtu mmoja au kundi la watu.

Aina za Maghani

a) **Maghani ya kawaida**

⇒ Ambayo hugusia maswala ya kawaida kama mapenzi, siasa, harusi, kazi, maombolezo n.k.
⇒ Husemwa/huganwa tu bila kusimuliwa.

b) **Maghani Simulizi**

⇒ Maghani ambayo husimulia hadithi kuhusu tukio la kihistoria.
⇒ Huhusu, mtu, tukio, kitu, mnyama, n.k.

Sifa

a) Hutokea kama hadithi.
b) Husimulia tukio la kihistoria.
c) Ni ndefu.
d) Waimbaji wake huitwa manju/yeli.
e) Huandamana na ala kama zeze, marimba, n.k.

Tofauti kati ya maghani ya kawaida na maghani

simulizi

Maghani ya kawaida	Maghani simulizi
✓ Ni fupi.	✓ Ni ndefu .
✓ Haitumii ala.	✓ Hutumia ala.
✓ Huhusu maswala ya kawaida.	✓ Kihistoria.
✓ Husemwa.	✓ Huimbwa.

Maghani ya Kawaida

i) Vivugo/majigambo

⇒ Utungo wa kujisifu au kujigamba.

Sifa

a) Hutungwa baada ya ushindi wa harakati ngumu k.v. kesi, kumuua simba, kuoa msichana aliyependwa na wengi n.k.
b) Fanani ni mwanamme.
c) Hutungwa papo hapo.
d) Hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe.
e) Hutumia chuku k.m. kujisifu kupita kiasi.
f) Anayejigamba hujipa jina la kiistiari k.m. mnyama.
g) Mhusika huvaa maleba yanayooana na tukio analojisifia.
h) Kuna kutaja jina na ukoo wa baba na mama.
i) Anayejisifu huahidi kutenda maajabu zaidi.

ii) Pembezi/pembejezi

⇒ Aina ya tondozi inayokusudiwa kusifu watu aina fulani katika jamii kutokana na matendo au mchango wao.
⇒ k.v. watawala, walezi wazuri, mashujaa wa vita, waganga mashuhuri hata wapenzi waliopigania pendo lao.

Mfano

Nani kama wewe mama?
Nani anokufana ‘mwaitu’
Subira uliumbiwa
Bidii nd’o jina lako la pili
Moyo wenye heba
Msimamo usoyumba
Anoelekeza kwa imani

Anoadhibu kwa mapenzi makuu
Mzazi, mlezi na rafiki wa dhati
Tangu siku za kusimama dede.

iii) Tondozi

⇒ Utungo wa kutukuza watu, wanyama na vitu.
⇒ k.v. watu mashuhuri, wapenzi, mifugo, miti mikubwa.

Mfano

Kipungu kipungu
Nani kama yeye?
Hashindiki kwa nia
Hashindiki kwa shabaha
Hulenga binguni
Hutia ghera kufikiwa peo
Peo zisofikika kwa wanokata tama
Kipungu, kipungu, hachi tufani za anga.

Maghani Simulizi

i) Sifo

⇒ Tungo za kusifu watu kutokana na matendo yao ya kishujaa.
⇒ Sifa zake hukaribiana na za tenzi hasa ikiwa ni shujaa anasifiwa.

ii) Tendi/tenzi

⇒ Ushairi mrefu unaoelezea maisha ya mashujaa tangu kuzaliwa hadi kufa kwao.
⇒ k.v. Utenzi wa Fumo Liyongo, Sundiata, Shaka Zulu, Wang`ombe waihura n.k.

Mfano

Asiyemjua mjua aliongwe atamjua
Namjuza kwa sifa zake alizokuwa nazo
Alisimika ufalme uliosifiwa
Akawa shujaa asiyetishwa
⇒ Utungo huu waweza kuwa wimbo wa sifa au utendi!

Sifa

a) Huwa masimulizi yanayotolewa kishairi.
b) Hutoa wasifu wa shujaa.
c) Huwa na matumizi ya chuku.
d) Wahusika hupewa sifa zisizo kawaida (kiungu).
e) Ni masimulizi mrefu.

f) Matumizi ya sitiari k.v. kulinganisha wasifiwa na wanyama wakali.
g) Huangazia matendo ya mashujaa.
h) Husimulia matukio ya kihistoria.
i) Huimbwa pamoja na ala ya kimziki.
j) Hutungwa papo kwa papo na kuhifadhiwa katika ubongo.
k) Hujumuisha mbolezi zinazoonyesha anguko la shujaa.

Lengo

a) Kuburudisha wanajamii.
b) Kusifu mashujaa wa jamii.
c) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza wengine kuwaiga mashujaa.
d) Kukuza ubunifu kwa kutunga papo hapo.
e) Kuimarisha uwezo wa kukumbuka kwa kutungwa na kuhifadhiwa akilini.
f) Kuburudisha waliohudhuria sherehe ampapo yanatolewa.
g) Kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za jamii
h) Kukuza ufasaha wa lugha kwa fanani.
i) Kufunza maadili.

iii) Rara

⇒ Hadithi fupi na nyepesi za kishairi zenye visa vya kusisimua.

Mfano

Alichukua mkoba wake
Akanipa kisogo
Kana kwamba hakunijua
Kana kwamba hakusema, “Hadi mauko”.
Hakujali penzi letu
Hakujali wana
Ambao ndiye alowapa uhai
Alijua nilimpenda
Ila hata hilo alijipa kujipurukusha
Akayoyomea
Akamezwa na ulimwengu.

Sifa

a) Huhusu mambo ya kubuni au ya kweli k.v. sherehe ya uhuru, kesi ya mauaji, n.k.
b) Huhusu maswala ibuka na ya kawaida.

c) Hadithi huwasilishwa katika beti.
d) Huimbwa.
e) Huandamana na ala za mziki.
f) Hutolewa kwa toni ya kitanzia.
g) Huwa na visa vya kusisimua.
h) Huwa na ucheshi wenye kinaya.
i) Maswala hayatoleai kwa uwazi bali hufumbwa na kudokezwa.
j) Huwa na uigizaji/utendaji.
k) Mambo yanayosimuliwa hupigwa chuku.

iv) Rara nafsi

⇒ Ushairi ambao hutungwa na mtu kuelezea hisia, matatizo na fikra zake mwenyewe.

Mfano

Muda umefika wa pingu kutiwa
Kutiwa silisili, kwani si utashi wangu
Ukoo waniuza, mithili ya kondoo sokoni
Mwambieni shangazi kwaheri nampigia
Hata angataka kuniopoa hawezi
Kwani mahari imetolewa
Mifugo kikwi nduguye amepokea
Kwaheri mama, kwaheri dada.

Sifa

a) Hugusia maswala yanayoathiri hisia za mtu binafsi kama vile mapenzi, usaliti, talaka, kifo.
b) Huwasilishwa kwa njia ya uimbaji unaoandamana na ala ya mziki.
c) Mzungumzaji huzungumza moja kwa moja na hadhira au aliyeandikiwa rara hii-mkewe, mpenziwe, mwanawe, Mungu, miungu.
d) Hutolewa katika miktadha k.v. mazishi kusifu aliyekufa, harusi na Bi. Arusi kama ameshinikizwa kuolewa.

3. **Ngonjera**

⇒ Mashairi ya kujibizana/kulumbana-yenye muundo wa kimazungumzo.

Sifa

a) Huwa na wahusika wawili au zaidi.
b) Mhusika mmoja huuliza jambo na mwingine hujibu.

c) Huendelezwa kwa njia ya wimbo.
d) Wahusika kupingana mwanzoni.
e) Wahusika huafikiana kufikiwa mwisho.

Umuhimu

a) Majibizano hukuza ubunifu kwa kila mmoja kuonyesha umaarufu.
b) Kukuza ujasiri wa kuzungumza hadharani.
c) Kuimarisha stadi ya kuongea.
d) Kuburudisha hadhira.

4. **Mashairi Mepesi.**

a) Mashairi ya kawaida ambayo hupatikana katika ushairi simulizi.
b) Hujumuisha mashairi mafupi ya kihisia, kimapenzi, kusifu na kukosoa watu.

Vigezo vya Uchanganuzi wa Tungo za Ushairi Simulizi

a) Kuainisha utungo kimaudhui/aina
b) Kuthibitisha ni aina fulani ya utungo wa kishairi/sifa.
c) Kutaja sifa zinazojitokeza za ushairi simulizi/utungo fulani wa ushairi simulizi.
d) Muktadha ambamo unaweza kutolewa.
e) Kuandika mbinu za kifasihi zilizotumiwa katika utungo huo.
f) Kufafanua sifa za jamii zinazojitokeza katika utungo.
g) Kuandika majukumu ya aina hiyo ya utungo wa ushairi katika jamii.
h) Anayeimba/nafsi imbi ni nani?
i) Kuandika maadili yanayojitokeza katika utungo.
j) Kueleza toni ya utungo huo.

MAZUNGUMZO

⇒ Maongezi ya mdomo yenye usanii.

Sifa

a) Huwa maongezi yenye usanii mkubwa.
b) Hutolewa mbele ya hadhira.
c) Hutolewa mbele ya hadhira.
d) Hutolewa kwa njia isiyokera.
e) Huambatana na sherehe fulani k.m. taabili katika matanga.
f) Hutegemea sauti na vitendo.

g) Huhusisha matumizi ya ishara k.v. za uso, mikono na miondoko.
h) Huhitaji ustadi wa kuzungumza ili kuteka hadhira.
i) Hutolewa na watu wenye umilisi mkubwa wa lugha.

Vipera vya Mazungumzo

i) Hotuba

⇒ Maelezo yanayotolewa mbele ya watu kuhusu mada fulani.
⇒ Huhusisha mada maalum sio suala lolote tu.

Umuhimu

a) Kuelimisha kwa kupa maarifa ya kukabiliana na maisha k.v. jandoni na arusini.
b) Kuadilisha au kutoa nasaha hadharani.
c) Huimarisha ukakamavu wa kuzungumza kadiri watu wanavyotoa hotuba hadharani.
d) Kukuza ufasaha na umilisi wa lugha.
e) Kupalilia kipawa cha uongozi.
f) Kuelimisha kwa kupatia watu maarifa ya kukabiliana na changamoto za maisha.

Aina za Hotuba

a) Risala
⇒ Hotuba inayowasilishwa mbele ya watu kueleza jambo fulani k.m. ya wafanyakazi kwa waajiri wao.
b) Mhadhara
⇒ Hotuba inayotolewa kwa hadhira fulani kufafanua somo au mada fulani.
c) Kumbukizi
⇒ Hotuba zinazohusu tukio fulani la kihistoria kuhusu mtu au kitu.
d) Mahubiri
⇒ Hotuba zinazohusu masuala ya kidini.
e) Taabili
⇒ Hotuba kuhusu aliyeaga dunia zinazohusu sifa zake nzuri.

ii) Malumbano Ya Utani

⇒ Mazungumzo ya kutaniana.

Aina

i) Utani wa mawifi na mashemeji

ii) Utani wa marafiki
iii) Utani wa vijana
iv) Utani wa watoto
v) Utani wa marika/ watu wa hirimu moja
⇒ *Wewe ni mweusi kiasi kwamba ukiingia chumbani taa zinazimika.*
vi) Utani wa mababu/mabibi na wajukuu
⇒ *Ee mume wangu, mbona walala mapema hivi? Utawezaje kulilinda boma letu ikiwa wewe ndiwe wa kwanza kujizika kitandani.*
vii) Utani wa maumbu (ndugu na dada)
⇒ *Wewe unajifanya jasiri na juzi baba alikukemea kidogo tu ukaanza kutetemeka kama kondoo aliyenyeshewa.*
viii) Utani wa mazishi
⇒ *Afadhali umekufa tukakuzika, sasa maghala yetu yatasalimika.*
ix) Utani wa makabila/ki ukoo
⇒ *Wakikuyu wanapenda pesa kiasi kwamba maiti ikisikia mlio wa sarafu inaweza kufufuka.*
⇒ *Wakamba wa ukoo wa Akanga wanapenda nyama kiasi cha kula kijusi cha mbuzi.*

Sifa

a) Huwa kati ya watu wawili au makundi mawili ya watu.
b) Hufanywa kwa kujibizana papo hapo.
c) Hufanywa kwa njia isiyo ya kuudhi.
d) Hutumia maneno ya mizaha.
e) Hutumia lugha ya ucheshi.
f) Hufanywa na watu wenye uhusiano mzuri.
g) Huchukua njia ya ushindani kila mmoja akitaka kumpiku mwenzake.
h) Watanianao huwa wamekubaliana kufanya hivyo.
i) Hufanyika katika wakati unaofaa sio baada ya kukutana tu.
j) Huhusisha masimango au kumkumbusha mtu wema uliomtendea.
k) Hutumia chuku sana kusisitiza au kukejeli sifa fulani hasi.

l) Huhusisha wakati mwingine utaniaji wa wasiokuwepo ukiambatanishwa na uigizaji wa kuchekesha.
m) Hutegemea uhusiano ulio kati ya wanajamii au makabila.
n) Huandamana na sherehe kama matanga.

Umuhimu

a) Kuburudisha kutokana na ucheshi.
b) Kuimarisha urafiki wa watu walio na uhusiano mwema wanaotaniana.
c) Hustawisha ufundi wa lugha.
d) Kukashifu tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, wivu, n.k.
e) Kukosoa wanajamii kwa njia ya kejeli/dhihaka
f) Kuimarisha umoja na ushirikiano kati ya wahusika.
g) Kuliwaza k.m. unaofanywa wakati wa maombolezo.
h) Kukuza na kudumisha mila na desturi za jamii.
i) Kukuza utangamano baina ya watu na wanajamii wanapokuja pamoja na kutaniana.
j) Kuhimiza watu kujieleza kwa uwazi kwa kupunguza urasmi miongoni mwa wanajaii.
k) Hudhihirisha uhusiano mwema baina ya watu wa jamii fulani.

Changamoto Sasa

a) Mabadiliko katika jamii yaliyosababisha baadhi ya wanajamii kupoteza nyenzo hii.
b) Kuingiliana kwa watu wa jamii mbalimbali.

iii) Soga

⇒ Mazungumzo ya kupitisha wakati yasiyozingatia mada maalum.

Sifa

a) Hutokea baina ya watu wa rika moja.
b) Humithilisha uhalisia badala ya kuunakili.
c) Hutumia chuku na kufanywa ljambo lionekane kama halina uhalisia.
d) Hukejeli watu au hali fulani.
e) Wahusika ni wa kubuni.
f) Hutumia vichekesho kupunguza ukali wa ukweli uliomo.
g) Wahusika hupewa majina ya wanajamii husika.
h) Huwa na mafunzo au maadili.

Umuhimu

a) Kuburudisha kwa kuchekesha.
b) Kufunza maadili.
c) Kukejeli matendo yasiyofaa katika jamii
d) Kukuza ubunifu baina ya washiriki.
e) Kufunza kuhusu matendo na tabia za kibinadamu.
f) Huwa msingi wa utani unaokuwapo katika jamii.
g) Kuonya na kutahadharisha dhidi ya tabia siyokubalika.

iv) Mawaidha

⇒ Mazungumzo ya kutoa ushauri kuhusu jambo fulani.

Sifa

a) Huwasilishwa mbele ya watu.
b) Hugusia takriban vipengele vyote vya maisha ya binadamu.
c) Aghalabu hutolewa na watu wenye umri mkubwa.
d) Hulenga maudhui maalum na ya aina nyingi kutegemea jinsia, umri, shughuli, n.k.
e) Hutumia lugha ya kubembeleza na isiyoonyesha ukali.
f) Hutumia lugha ya kuathiri hisia.
g) Huwa na ufasaha mkubwa wa lugha.
h) Ni mawazo mazito kuhusu maisha.
i) Hutolewa katika miktadha rasmi na isiyo rasmi.
j) Ujumbe hulenga hadhira maalum k.m. ya kike au kiume.
k) Hutumia fani nyingine za fasihi kama methali, misemo, ngano, nyimbo n.k. kupitisha mawaidha.
l) Huibua maadili yanayohitaji kuzingatiwa.

Muundo wa Mawaidha

a) Utangulizi

⇒ Kutoa kauli ya kuvutia makini ya hadhira k.v. ‘Utu uzima huenda na uwajibikaji’, au kueleza kiini cha mawaidha.

b) Mwili

⇒ Kutoa wosia, maonyo, maelekezo kutegemea suala analotolea mawaidha akitumia jazanda, kupanda na kushuka kwa sauti, kimya, miondoko, kubadilisha kasi ya kuzungumza, kudondoa semi za watu maarufu, n.k.

c) Hitimisho

⇒ Kuonyesha msimamo kuhusiana na suala analozungumzia.

⇒ Kushirikisha hadhira ili kujua msimamo wao kuhusu suala alilowausia.
⇒ Hadhira kutoa changamoto kuhusiana na mawaidha yanayotolewa.

Umuhimu wa mawaidha

a) Kuelekeza jamii kimaadili.
b) Kuelekeza kuhusu jinsi ya kukabiliana na changa moto maishani.
c) Kushauri jinsi ya kutenda jambo fulani.
d) Kujasirisha waoga na kuwapa ukakamavu.
e) Kuwaondolea wanajamii ujinga.
f) Kuhifadhi na kuendeleza mila na desturi za jamii.
g) Njia ya kipato kwa baadhi ya watu.
h) Kuelimisha kuhusu maarifa ya kuendeshea maisha, majukumu na matarajio ya jamii.

v) Ulumbi

⇒ Uwezo na ustadi wa kuzungumza kwa uhodari mkubwa.

Miktadha Ambamo Ulumbi Hutumika Katika Jamii

a) katika mijadala mbungeni
b) katika hotuba za kisiasa
c) katika mahubiri maabadini
d) katika mijadala shuleni
e) kortini
f) katika shughuli za kijamii k.v. posa
g) katika sala/dua
h) katika maapizo
i) katika malumbano ya utani
j) katika majigambo/vivugo

Sifa

a) Hufanywa mbele ya hadhira.
b) Huwa na lengo maalum k.v. kushawishi, kuelimisha, kushauri n.k.
c) Hutumia tamathali za usemi kwa ufanifu mkubwa k.v. chuku, misemo, methali, n.k.
d) Lugha huwa yenye mvuto na ufasaha.
e) Hutumia lugha yenye taharuki na ushawishi.
f) Unenaji huambatana na utumizi wa ishara/ viziada lugha.
g) Uwasilishaji huwa sahili na wenye ujumbe mzito.

h) Huwa na urudiaji mwingi ili kusisitiza na kuvutia usikivu.
i) Huwa na matumizi ya taharuki k.v. mtuo.
j) Huwa na mtiririko mzuri wa mawazo.

Sifa za Mlumbi

a) Asiwe mwoga ili kuweza kuzungumza hadharani.
b) Asiwe na haya ili kuweza kuzungumzia mambo ya aibu inapobidi.
c) Awe mchanganfu na mcheshi ili kunasa makini ya hadhira na kuzuia isikinai.
d) Awe na ufahamu mpana wa utamaduni wa hadhira asitumie maneno na ishara zinazoweza kuwaudhi au kupingana na imani za hadhira.
e) Awe na uwezo wa kuingiliana vizuri na hadhira ili aivutie.
f) Awe na kumbukumbu nzuri ili ulumbi wake utiririke vizuri.
g) Awe na uwezo wa kudramatisha ili kuonyesha picha fulani k.v. ishara za uso, mwili, miondoko kuonyesha picha ya analozungumzia.
h) Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
i) Aweze kubadilisha toni na kiimbo hadhira isikinai.
j) Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira k.v. kwa maswali ya balagha ili kuondoa uchovu wa kusikiliza.
k) Awe na uwezo wa kutumia mtuo wa kidrama ili kuongeza taharuki, kusisitiza ujumbe na kuteka makini ya hadhira.

Umuhimu

a) Hukuza uwezo wa kujieleza na kusema hadharani kwa kujiboresha kadiri anavyoendelea.
b) Kigezo cha kuteulia viongozi wa baadaye kwani ushawishi humtambulisha mlumbi kama mwenye uwezo wa kuongoza.
c) Kuelimisha jamii kwa njia isiyochosha.
d) Kudumisha umoja na ushirikiano jamii inapokusanyika pamoja kusikilizaulumbi.
e) Kuhamasisha na kuzindua jamii juu ya suala fulani.
f) Kushawishi walengwa wakubali jambo fulani.

g) Kukuza uwezo wa mwanajamii kushawishi na kupatanisha.
h) Kushawishi watu wapende jambo fulani.
i) Kuburudisha wasililizaji.

vi) Maapizo

⇒ Maombi maalum ya kumtaka Mungu, miungu au mizimu kumwadhibu mhusika hasidi, mkinzani au muovu.

Mfano

Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,
Nami ndiye nilompa uhai mwana unoringia,
Anokufanya upite ukinitemea mate,
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Miungu nawaone chozi langu, wasikie kilio changu,
Mizimu nawaone uchungu wangu,
Radhi zao wasiwahi kukupa,
Laana wakumiminie,
Uje kulizwa mara mia na wanao,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,
Wakazawanao wasikuuguze katika utu uzima wako!

Sifa

a) Yalitolewa kwa waliokwenda kinyume na matarajio ya jamii.
b) Yalifanywa mahali maalum k.v. makaburini, porini, chini ya miti mikubwa, n.k.
c) Hutolewa kwa ulaji kiapo.
d) Yalitolewa na mwathiriwa au watu maalum walioteuliwa.
e) Maapizo huaminiwa yataleta maafa kwa jamii.
f) Watoaji maapizo walikuwa walumbi.
g) Maapizo hutumia lugha kali inayonuiwa kutia woga ili kutahadharisha dhidi ya maovu.

Umuhimu

a) Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya maovu.
b) Kutambulisha jamii kwani kila mojawapo ina aina yake ya kuapiza.
c) Kukuza umoja katika jamii kwani kaida na miiko hufanya wanajamii kujihisi kuwa kitu kimoja.

d) Kuadilisha wanajamii kwa kujifunza kutenda mema ili kuepuka laana.

MAIGIZO

⇒ Utanzu wa fasihi simulizi unaoambatana na vitendo.

⇒ Sanaa ya mazungumzo yanayoambatana na vitendo.

Sifa

a) Huwa na watendaji au waigizaji.
b) Huwasilishwa mbele ya hadhira.
c) Huwasilishwa mahali maalum k.v. ukumbini.
d) Huwasilishwa kwa mazungumzo na matendo
e) Waigizaji hujivika maleba yanayooana kutia uhai maigizo.
f) Matayarisho kabambe hufanywa kabla ya maigizo.
g) Huweza kuambatana na ngoma pamoja na uimbaji.
h) Lugha ni yenye ufundi wa juu k.v. picha, mafumbo na tamathali.
i) Huweza kuambatana na sherehe fulani ya kitamaduni k.v. jando, matanga, n.k.
j) Huwasilishwa kwa lugha sahili.
k) Hujaa taswira zinazoweza kutambulika na hadhira.

Umuhimu

a) Kuburudisha wahusika na hadhira.
b) Kukuza umoja na ushirikiano kwa kujumuisha watu pamoja.
c) Kuimarisha uwezo wa kuzungumza hadharani-kupata ukakamavu jinsi mtu anapoendelea kuigiza.
d) Kukuza umoja na ushirikiano watu wanapojumuika pamoja kutazama maigizo.
e) Kukuza uwezo wa kukumbuka kwani mwigizaji huhitaji kukumbuka maneno halisi.
f) Kukejeli kitendo kisichofaa/cha kijinga alichofanya mtu.
g) Njia ya kipato/kuwatafutia riziki baadhi ya watu.
h) Kutoa nafasi kwa watu kudhihirisha vipawa vyao.
i) Kuonya na kutahadharisha watu dhidi ya kufaya mambo yasiyofaa.
j) Kuelimisha watu wafahamu jambo fulani k.v. ukimwi, ufisadi, n.k.
k) Kukosoa watu wanaofanya kinyume na matarajio ya jamii k.v. wivu, uchoyo, n.k.

l) Kupitisha maarifa na amali za kijamii.

Ploti

a) Utangulizi-kutambulisha mgogoro
b) Ukuzaji wa mgogoro
c) Kilele cha mgogoro
d) Usuluhishaji wa mgogoro

Aina za maigizo

a) **Maigizo Ya Kawaida**

⇒ Maonyesho ya jadi yakiwa yameondolewa kwenye mazingira yake halisi.

b) **Sanaa ya Maonyesho**

⇒ Matendo ya kweli yanayojitokeza katika jamii kulingana na mazingira yake halisi k.m. uganga, mazishi, unyago, ngoma, n.k.

Tofauti

Maigizo ya kawaida	Sanaa ya maonyesho
✓ Mazingira ya kuzua/maalum	✓ Hutumia mazingira halisi
✓ Matukio ya kuiga	✓ Matukio halisi/ ya kila siku.
✓ Huwa na wahusika na hadhira maalum	✓ Washiriki na waigizaji walio pia hadhira
✓ Matumizi ya ukumbi na jukwaa maalum	✓ akuna haja ya ukumbi wala jukwaa
✓ Hutumia maleba na vifaa vya kuzua mazingira maalum	✓ Hakuna vifaa maalum bali huwa mazingira yenyewe.
✓ Hugawika katika maonyesho Kutumia lugha kwa njia maalum	✓ Muundo wake hufululuza au hayajagawika katika maonyesho.
✓ Wahusika hufanya mazoezi kabla ya igizo halisi	✓ Hawahitaji kufanya mazoezi kwani ni matukio ya kila siku.

Maigizo ya kawaida

i) Michezo ya Kuigiza

⇒ Maigizo ambayo huwasilishwa na watendaji jukwaani mbele ya watu.

Sifa za Mwigizaji bora

a) Awe jasiri ili aweze kuigiza mbele ya watu/hadharani.
b) Awe na ubunifu ili aweze kufanya uigizaji kuvutia na kuondoa ukinaifu.
c) Awe na ujuzi wa kutumia ishara za uso, mwili na miondoko kuonyesha picha ya hali anayoigiza.
d) Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
e) Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazoigiza k.v. huzuni.
f) Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira kwa maswali ya balagha ili kuondoa uchovu.
g) Awe na uwezo wa ufaraguzi/ kubadilisha uigizaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake na kutoa mifano inayofahamika kutoka katika mazingira ya hadhira.
h) Awe anaelewa utamaduni wa hadhira yake ili asitumie maneno na ishara ambazo zinaudhi ama kukinzana na na imani zao.

ii) Vichekesho

⇒ Michezo ya kuigiza inayokusudiwa kuzua kicheko ili kupitisha ujumbe k.m. vioja, vitimbi n.k.

Sifa

a) Vichekesho huigizwa.
b) Huwasilishwa kwa lugha sahili.
c) Hujaa taswira zinazoweza kutambulika na hadhira.
d) Hutumia mbinu ya kejeli, kunaya na tashtiti.
e) Vichekesho huwa vifupi.
f) Havihitaji uchambuzi wa ndani ili kuvielewa au kupata maana.

Jukumu

a) Kuburudisha hadhira kwa kuchekesha.
b) Kuelimisha kwa kuonyesha jambo la kijinga alilofanya mtu.
c) Njia ya kuwapatia watu riziki.
d) Hutumika katika hadithi kuifanya ivutie.
e) Kukejeli kitendo fulani kisichofaa alichofanya mtu fulani.

f) Kukashifu matendo hasi ya kijinga.
g) Kuadilisha ama kutoa funzo fulani la tabia njema.

iii) Ngonjera

⇒ Ngonjera inayoambatana na uigizaji/utendaji.

Sifa

a) Kuweko kwa uigizaji/utendaji k.v. ishara za uso na mikono.
b) Huwa na wahusika wawili au zaidi.
c) Huendelezwa kwa njia ya wimbo.
d) Mhusika mmoja huuliza jambo na mwingine hujibu.
e) Wahusika kupingana mwanzoni.
f) Wahusika hufikia uafikiano kufikia mwisho.

iv) Michezo ya Watoto/Chekechea

⇒ Michezo inayoigizwa na watoto katika shughuli zao.

Aina

a) Mchezo wa baba na mama
b) Kuruka kamba
c) Kujificha na kutafutana
d) Kukimbiza kibaramwezi dhidi ya upepo ili kizunguke
e) Mchezo wa baba na mama

Sifa

a) Waigizaji ni watoto.
b) Huhusu shughuli za kiuchumi na kitamaduni k.v. arusi, siasa, ukulima.
c) Huandamana na nyimbo za watoto.
d) Huwa na miondoko mingi k.v. kujificha, kuruka.
e) Huwa na matumizi mengi ya takriri.
f) Huchezwa popote.
g) Huwa na kanuni fulani.
h) Hukoma watoto wakichoka au wakikiuka kanuni

Umuhimu

a) Kufunza watoto majukumu yao ya utu uzima.
b) Kuwatanguliza watoto katika sanaa ya uigizaji.
c) Kukuza ubunifu wa watoto kadiri wanapoendelea kuigiza.
d) Kudumisha utamaduni wa jamii.
e) Kuburudisha watoto.
f) Kukuza stadi ya uigizaji miongoni mwa watoto.

g) Kukuza utangamano miongoni mwa watoto kwa kuwajumuisha pamoja.
h) Kukashifu matendo hasi ya watu wazima kwa watoto.
i) Kuwapa watoto ukakamavu na kujiamini wakiwa wachanga.

v) Majigambo/vivugo

⇒ Uigizaji ambapo wahusika hujigamba kwa matendo ya kishujaa.

Mfano

Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu
Ulojipamba kwa mabingwa
Wachezaji hodari wa ngoma
Ndimi dume liloingia nyanjani
Makoo yakatetemeka
Yakang'ang'ania, ngozi kusakata nani

Kijiji kizima kilinijua
Wazee walilienzi
Wakamiminika kiamboni
Mabinti kunikabithi.

Sifa

a) Aghalabu huambatana na ngoma.
b) Hujitokeza, kujigamba na kisha kuendelea kucheza ngoma.
c) Anayejigamba hubeba zana zake za vita kama vile mkuki na ngao kuonyesha aliyotenda.
d) Anayejigamba huvaa maleba kuambatana na jambo analojisifia.

vi) Utambaji

⇒ Usimulizi wa hadithi unaoambatana na uigizaji.
⇒ Huwa na matumizi ya vizuizui.

vii) Mazingira

⇒ Uigizaji wa maumbile asilia yaliyozunguka jamii ya watu k.v. sauti za wanyama.
⇒ Kuna matumizi ya viziuzui, matawi n.k.

Sanaa ya Maonyesho

i) Ngoma

⇒ Uchezeshaji wa viungo vya mwili kuambatana na mdundo au miondoko maalum.

Aina

e) Ngoma za wanawake
f) Ngoma za tohara
g) Ngoma za wanaume
h) Ngoma za sherehe
i) Ngoma za vijana
j) Ngoma za unyago na jando
a) Ngoma za wazee
b) Ngoma za arusi
c) Ngoma za kufukuza mapepo
d) Ngoma za kuaga mwaka

Sifa

a) Huandamana na muziki na ala ya muziki k.v. ngoma.
b) Ngoma huchezewa mahali wazi na penye hadhira.
c) Wachezaji huvaa maleba maalum kulingana na funzo linalonuiwa.
d) Huwa na wahusika aina mbili; watendaji na watazamaji kwa wakati mmoja.
e) Huweza kuandamana au kutoandamana na sherehe.
f) Hutofautiana kulingana na jamii husika.

Umuhimu

(a) Kuburudisha kwa ufundi wa kucheza kwa kuzingatia miondoko.
(b) Kitambulisho cha jamii kwani kila moja ina aina yake ya ngoma.
(c) Kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za jamii husika.
(d) Kukuza uzalendo kwa kuwafanya wanajamii kuionea fahari jamii yao.
(e) Kukuza umoja na ushirikiano kwa kujumuisha watu pamoja.
(f) Kuelimisha kwa kupitisha mafunzo na maarifa.

ii) Matambiko

⇒ Utoaji wa kafara kwa Mungu, miungu, pepo au mizimu ili wasaidiwe kutatua shida, kutoa shukrani au kuomba radhi.

Sifa

g) Hutolewa na wazee maarufu walioteuliwa.
h) Hufanywa nahali maalum k.v. pangoni, mwituni, n.k.
i) Huandamana na sala.
j) Huandamana na utoaji kafara k.v. kuchinja mbuzi, n.k.
k) Huandamana na maombi.

iii) Maigizo Ya Uganga wa Ramli

Sifa

a) Mganga hujitia kujua kwa hivyo vitendo vyake ni maigizo ya uganga wa madaktari.
b) Mengi katika matendo ya mganga hayana mashiko.
c) Aghalabu kafara hutolewa.
d) Waganga wanapopiga bao huvaa maleba kama ngozi, vibuyu, pembe, n.k.
e) Huweza kuwa na fimbo maalum.
f) Lugha maalum anayodai kuitumia kuwasiliana na misimu.
g) Mizimu humshauri mganga kuhusu ugonjwa na tiba inayofaa.
h) Mganga humchanja mgonjwa na kumpa dawa za miti shamba.

Umuhimu

a) Wakati mwingine mizizi ya mganga huponya.
b) Huwapa watu matumaini hasa walio na magonjwa yasiyo na tiba.
c) Dawa za mganga hupunga mashetani kwa wagonjwa wake.
d) Hukutanisha ulimwengu wa mizimu na ulimwengu halisi.
e) Waganga huburudisha wanapoigiza.

Hasara

a) Mgonjwa huenda asipone kwani matendo mengi ya mganga ni ya kukisia.
b) Dawa za uganga zaweza kumdhuru mtu.
c) Malipo ni ghali na mtu hata aweza kufilisika akitafuta tiba ya ugonjwa usiopona.
d) Mazingira ya uganga husheheni uchafu mwingi.
e) Mgonjwa huridhika kwa muda mfupi halafu uhalisia hudhihirika.

iv) Ngomezi

⇒ Uwasilishaji wa ujumbe kwa kupiga ngoma au zana nyingine ya kimziki.

Sifa

a) Kuwepo kwa ngoma au ala nyingine kama panda.
b) Mapigo ya ngoma hueleweka tu na jamii husika.
c) Mapigo kufuata toni au ridhimu maalum kuwasilisha maneno fulani.
d) Kuwepo kwa hadhira au wasikilizaji.
e) Kueleweka kwa mapigo hayo na wanajamii husika pekee.
f) Makini huhitajika ili kupata midundo.

Aina za ngomezi

a) Taarifa

⇒ Huarifu kuhusu jambo k.m. msimu wa kuanza kutayarisha mashamba, kuitwa katika mkutano, kazi ya ujima n.k.

b) Tahadhari

⇒ Hutoa tahadhari kuhusu mavamizi kama wizi wa mifugo, vita, majanga kama moto, mafuriko n.k.

c) Uhusiano

⇒ Kuita watu kwa sherehe.

Umuhimu wa Ngomezi

a) Njia ya mawasiliano kwa jamii zisizojua kusoma.
b) Husaidia wanaokabiliwa na ugumu wa mawasiliano.
c) Kuharakisha mawasiliano katika masafa mafupi.
d) Kutoa taarifa kuhusu matukio fulani k.m. ndoa, kifo n.k.
e) Husaidia kupitisha jumbe za dharura.
f) Kutahadharisha wanajamii kuhusu tukio la hatari/dharura k.v. vita, gharika n.k.
g) Kuficha siri kwa kuwasilisha ujumbe kwa njia isiyoeleweka.
h) Kuhifadhi na kudumisha utamaduni wa jamii.
i) Namna ya kudhihirisha ufundi wa kutumia zana kama ngoma.
j) Kitambulisho cha jamii kwani kila jamii hupitisha ujumbe kwa mapigo tofauti.

Udhaifu wa Ngomezi

a) Si kila mtu anaweza kufasiri ujumbe unaokusudiwa.

b) Mapigo hayasikiki mbali na hivyo husikika na idadi dogo ya watu.
c) Mapigo yaweza kuhitilafiana na hivyo kufasiriwa kwa namna tofauti.

Ngomezi za kisasa

a) Milio ya ambulensi, magari ya polisi na zimamoto.
b) Kengele za kubisha hodi nyumbani zinazotumia umeme.
c) Kengele shuleni, makanisani, n.k.
d) Toni za rununu zinazowakilisha aina mbalimbali za jumbe.
e) Ving'ora vya kuashiria moto umetokea katika majumba ya horofa, benki, hospitalini, n.k.

Changamoto za Ngomezi katika Jamii ya Sasa

a) Mwingiliano wa jamii mbalimbali unaosababisha kutofasiri ujumbe kwa njia moja inayotakikana.
b) Viwanda na majumba marefu kusababisha kutosikika kwa sauti au milio ya ngoma.
c) Njia nyingine za kisasa za mawasiliano zinazotumiwa kwa wingi na kwa wepesi.
d) Uhaba wa zana kama baragumu na zumari zilizokuwa zinatumika.
e) Mabadiliko ya maisha kuleta ubinafsi na kusababisha wengi kutoitikia wito wa vyombo.

v) Mivigha

⇒ Sherehe za kitamaduni ambazo hutokea katika kipindi fulani cha mwaka ambazo huonyesha mwanajamii ametoka kiwango kimoja hadi kingine.

Aina za Mivigha

a) Sherehe za tohara
⇒ kutoka utotoni na kuingia utu uzimani.
b) Sherehe za ndoa
⇒ kutoka kapera hadi kuoa
c) Sherehe za kutambika
⇒ kutoa sadaka kwa Mungu, miungu, pepo au mizimu
d) Sherehe kutawazwa kwa kiongozi
⇒ kutoka uraia na kuingia katika uongozi/utawala
e) Shughuli za mazishi/matanga
⇒ kutoka uhai hadi ufu

f) Sherehe za kuwapa watoto majina
g) Sherehe za ulaji kiapo
h) Shughuli za posa
i) ibada

Hatua

a) Kutoa mtu rasmi kutoka kundi moja la wanajamii.
b) Kumfundisha majukumu yanayohusiana na wadhifa mpya.
c) Kumwingiza rasmi katika kundi jingine.

Sifa

a) Huandamana na matendo au kanuni fulani (mivigha).
b) Maleba maalum huvaliwa na wahusika kuwatofautisha na hadhira.
c) Hufanyika kwa kutumia lugha maalum au kimyakimya.
d) Kuna watu aina tatu: watendaji wanaoshiriki kuimba na kucheza, wale sherehe inafanyika kwa sababu yao na wanaoshuhudia tu.
e) Huhusisha vitendo maalum kama kula viapo, kutoa kafara, kucheza ngoma, n.k.
f) Huandamana na utoaji wa mawaidha.
g) Uigizaji hujitokeza pale mwanajamii anaingizwa katika kundi fulani kutoka jingine.
h) Huhusisha maombi.
i) Hufanywa mahali maalum sherehe hiyo inapofanyika k.m. tambiko hufanywa porini au pangoni.
j) Wahusika huweka ahadi za kutenda wema.
k) Huwa na mpangilio wa shughuli kuanzia mwanzo, kati hadi mwisho.

Umuhimu

d) Kuburudisha kwa vile baadhi ya mivigha huhusisha nyimbo, ngoma na uigizaji.
e) Kutoa mafunzo ya utu uzima na elimu ya jadi.
f) Mivigha ya mazishi huliwaza wafiwa.
g) Kukuza utangamano miongoni mwa wanajamii kwa kuwajumuisha pamoja katika mivigha yao.
h) Kuashiria mwanajamii ametoka kiwango kimoja cha maisha hadi kingine.

i) Kujenga uhusiano bora kati ya jamii na miungu au mizimu.
j) Kitambulisho cha jamii kwani kila moja ina aina yake ya mivigha.
k) Kudumisha mila za jamii.
l) Kuelimisha jinsi ya kukabiliana na changamoto maishani.
m) Kuadilisha kwa kufunza tabia zinazokubalika na jamii k.v. uaminifu, utiifu, n.k.
n) Kukashifu vitendo vya uoga.
o) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza wanajamii kuonea fahari tamaduni zao.
p) Msingi wa wanajamii kujitambulisha na kuionea fahari jamii yao.

Hasara

a) Baadhi ya mivigha huhatarisha afya na maisha k.v. kutahiri watoto wa kike.
b) Baadhi ya sherehe hukiuka maadili kama vile kwa kuruhusu matusi hata kushiriki ngono.
c) Baadhi yaweza kusababisha hasara kama vile kueneza ukimwi k.v. tohara kwa kisu kimoja.
d) Huzua tofauti za kijinsia k.v. mwanamme kujiona bora kuliko mwanamke.
e) Kuzua utabaka baina ya waliopashwa na wasiopashwa tohara.
f) Baadhi ya mivigha hukiuka malengo ya kitaifa k.m. ukeketaji ni ukiukaji wa haki za binadamu
g) Kunayo hujaza watu hofu k.v. kufukuza mapepo kunakohitaji kafara ya binadamu.
h) Baadhi huhusisha ushirikina na hivyo kusababisha uhasama baina ya koo.
i) Baadhi hugharimu kiasi kikubwa cha pesa na kuifilisi familia.

FASIHI SIMULIZI (ZIADA)

Fasihi ni Sanaa inayotumia lugha au maneno katika sura mbalimbali kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu. Kuna aina mbili kuu za fasihi; fasihi simulizi na fasihi andishi.

Fasihi simulizi

Huwasilishwa kwa njia ya mdomo toka kizazi kimoja hadi kingine au masimulizi.

Fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.

Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi

Fasihi simulizi

- Huwasilishwa na fanani au masimulizi kwa njia ya masimulizi ya mdomo.
- Huhifadhiwa akilini na kusambazwa kwa njia ya masimulizi.
- Ina uhuru wa kutumia wahusika mbalimbali kama vile binadamu na viumbe vinginevyo.
- Ina tanzu nyingi kuliko fasihi andishi kama vile hadithi, semi, ngonjera, ushairi simulizi, maigizo.
- Ni mali ya jamii nzima inayohusika.
- Ni kongwe kuliko fasihi andishi kwani imekuwepo tangu kuwepo kwa binadamu.
- Hadhira yake ni watu wote katika jamii; watoto, wazee, vipofu, viziwi na kadhalika.
- Hubadilika kulingana na mfumo wa jamii.
- Ina hadhira ya utendaji.
- Ina hadhira hai.
- Inaweza kubadilishwa papo kwa hapo ili kukidhi mahitaji ya hadhira.

Fasihi andishi

- Huwasilishwa na mwandishi kwa njia ya maandishi.
- Huhifadhiwa kwa maandishi na kusambazwa kwa maandishi.
- Ina tanzu chache kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi.
- Mara nyingi wahusika ni binadamu kwani inahusu binadamu na mazingira yake.
- Ni mali ya mwandishi aliyetunga.

Fafanua sifa za mtambaji/fanani wa fasihi simulizi

Mtambaji anapaswa kuothi sifa zifuatazo ili awe mtambaji bora wa ngano au hadithi:

- Kuelewa utamaduni; lazima aelewe utamaduni wa jamii husika vizuri.

- Uwezo wa ufaraguzi, awe na uwezo wa kufaragua au kubadilisha sifa fulani za ngano kutegemea hadhira.
- Awe mcheshi, ucheshi ni mbinu ya kuvuta nadhari ya hadhira.
- Kuifahamu lugha vizuri, aelewe maana ya maneno, misemo na methali.
- Ubingwa wa kuwasilishwa kwa matendo, anaweza kutumia ishara za mkono na kuiga miondoko jukwaani ili kuivutia hadhira yake.
- Kuwa mlumbi mzuri, sauti ni nyenzo kuu ya uwasilishaji wa ngano au utambaji. Mtambaji awe anasikika na anaongea lugha kwa namna inayoeleweka na hadhira yake.

Utangulizi Wa Hadithi

Kuna vitangulizi vya hadithi au fomula:

A) Mtambaji: Paukwa!
Hadhira: Pakawa!

B) Mtambaji: Paukwa!
Hadhira: Pakawa
Mtambaji: Sahani
Hadhira: Ya mchele
Mtambaji: Giza
Hadhira: La mwizi

C) Mtambaji: Hadithi hadithi
Hadhira: Hadithi njoo…

D) Mtambaji: Kaondokea chanjagaa kajenga nyumba kakaa mwanangu mwana siti vijino kama chikichi nitamjengea nyumba na vilango vya kupitia. Hapo zamani za kale…

Majukumu ya ufunguzi.

- ❖ Kuvuta nadhari au makini ya hadhira.
- ❖ Kubainisha mtambaji wa hadithi.
- ❖ Kudhihirisha kuwa msimulizi yuko katika ulimwengu wa hadithi wala si kawaida.
- ❖ Kuitathmini hadhira kama iko tayari kwa hadithi.
- ❖ Kuashiria mwanzo wa hadithi.
- ❖ Kubainisha utanzu wa fasihi simulizi-hadithi.

Kimalizio cha hadithi.

Katika kutamatisha hadithi ni lazima iwe na kimalizio kwa

mfano:
... Na wakaishi kwa amani milele na milele.
... Hadithi yangu imeishia hapo.
...Tangu siku hiyo paka na panya wakawa adui.
...kweli damu ni nzito kuliko maji.
...Alhamdullilahi.

Majukumu ya kimalizio.

- Kuashiria mwisho wa utambaji.
- Njia ya kupumzisha hadhira.
- Kiashiria cha kumwonyesha mtambaji mwengine kuwa anaweza akaanza.

Umuhimu wa hadithi katika fasihi simulizi.

- Hadithi hutumiwa kuipatia jamii mwelekeo, kuna methali isemayo kuwa mwacha mila ni mtumwa hivyo basi jamii inayopuuza kale yake au fasihi yake hukosa mwelekeo.
- Hadithi hutumiwa kuendeleza maadili ambayo huwa kama nguzo kuu ya wanajamii.
- Hadithi: huonya, huelimisha na hushauri jamii. Hadithi huwa na wahusika wenye tabia chanya na sifa hasi. Wenye sifa chanya huweza kuangaliwa kama kielelezo kizuri cha jamii na wenye sifa hasi wanafaa kupuuzwa.
- Hutumiwa kurithisha jamii, elimu na thamani muhimu kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Hutumiwa kama burudani.
- Kuendeleza uhusiano uliopo kati ya wanajamii na hasa uhusiano wa kushirikiana.
- Kukuza uwezo wa kumbukizi.
- Kuendeleza ufahamu.

HADITHI/NGANO

Ni hadithi za kimapokeo ambazo zimerithishwa na hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Sifa za ngano

- Kuwepo kwa mianzo maalum kwa mfano hapo zamani za kale...
- Kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Uwezekano wa kubadilisha kwa sehemu fulani hutegemea hadhira inayohusika.

- Kuwepo kwa maadili au funzo ambalo liko wazi ama linaloweza kuashiriwa kwa kuwepo kwa methali, misemo au kauli fulani.
- Kuwa na matumizi ya urudiaji kama vile wimbo, vifungu au maelezo.

VIPERA VYA HADITHI

(A) Ngano za kibunifu.

1. **Hekaya/Ayari**

Ayari ni mdanganyifu au mtu anayetumia ujanja; kimsingi ngano za ayari zina uhusisha mhusika ambaye anajifanya rafiki huku akiwa na dhamira ya kujinufaisha mwenyewe. Ni ngano ambapo mhusika mmoja anatumia hila au ujanja kulaghai wengine.

Sifa za hekaya

- Ni masimulizi ya moja kwa moja kwa lugha nathari.
- Wahusika wake wakuu huwa sana sana sungura na Abunwasi.
- Matendo yao huwa yamejaa ujanja.
- Kisa huwa kifupi.
- Werevu na ujanja hujitokeza bayana kisani.
- Mara nyingi mafunzo huwa: hekima, maadili na mienendo ya jamii, kwa kuonyesha hila na ujanja.
- Werevu unashinda.

Mfano

Hapo zamani za kale paliondokea sungura na jirani yake Mtajika. Mtajika alikuwa na mali nyingi kama vile sufuria kubwa za kuwapikia wageni naye Sungura alikuwa na visufuria vidogo. Siku baada ya siku Sungura alikuwa akiazima sufuria kwa Mtajika, anaporejesha ile sufuria baada ya kukaa nayo kwa majuma kadhaa anairejesha na nyingine ndogo. Mtajika akamuuliza “Mbona umekawia kunilete sufuria yangu jameni?” Sungura akamjibu kwamba sufuria yako ilikuwa ikizaa ndio maana nimekuletea hii ndogo ambayo ni mtoto wa sufuria yako?” Mtajika alifurahi na kutabasabu kama kibogoyo aliyeota meno wakati wa mlo wa nyama. Siku mosi Sungura alipata wageni wengi na alikuwa na mpango wa kugura eneo hilo. Alimwendea Mtajika na kumwazima sufuria ile kubwa

kabisa ili akawapikie wageni wake. Baada ya majuma mawili Sungura alirejea kwa Mtajika huku akionyesha masikitiko usoni. “Sufuria yangu i wapi? Mtajika aliuliza kwa ukali. Sungura akamjibu “Ilikufa ikiwa inajifungua kwani chochote ambacho kina uwezo wa kuzaa pia hufa.”

Umuhimu Wa Hekaya

- Kutoa maadili kwa wanajamii ili waache kuwatendea wenzao ujanja na kuwalaghai.
- Hufunza watu kuhusu matendo mema.
- Huonya dhidi ya upumbavu.
- Hufunza kuwa katika ulimwengu uliojaa hila na udanganyifu silaha ni maarifa,wema na maadilifu.

2. **Khurafa/Hurafa**

Ni hadithi zinazohusisha wanyama kama wahusika.

Sifa

- Huwa na wahusika wanyama.
- Wanyama hupewa sifa za binadamu.
- Wanyama huwakilisha binadamu wa kawaida.
- Huonyesha maadili katika jamii.

Mifano

Kuchakulo na Nyani

Hapo kale, Kuchakulo alikuwa akiishi mahali palipokuwa na nyani wengi. Nao hao nyani walikuwa wamezoea kumcheka Kuchakulo kila alipopita karibu nao. Tabia hii ilimwudhi sana kuchakulo. Kwa muda, alikaa akifikiria njia ya kuwaadhibu nyani hawa. Siku moja jawabu likamjia. Akaenda mpaka mwituni ambako alipata zabibu tamu sana; akazitia katika mfuko mmoja. Katika mfuko ule ule akatia changarawe. Akaenda moja kwa moja mpaka mahali nyani walipokuwa wamekaa kwa furaha. Akaingiza mkono wake mfukoni na kuzitoa zabibu. Akazitafuna na huku akisema: “Haaa! Meno ya wavulana huzisaga hizi changarawe mpaka unga! Angalieni!”

Akazitoa zabibu na kuzitafuna.

Wale nyani kuona vile wakamwendea wakisema: “ Hebu tupe na sisi tusisage kwa meno.”

Kuchakulo akaingiza mkono mfukoni na badala ya kuzitoa zabibu akatoa changarawe na kuwapa. Nyani

kujaribu kutafuna wakaumwa na meno na kuzitema chini. Kuchakulo akaendelea kuzitoa zabibu kwa akili na kuzitafuna. Hao nyani waliiona hiyo ajabu, wakamwuliza kile kinachomfanya yeye aweze kutafuna kwa urahisi bila kuyaharibu meno na wakati wao hawawezi.

Kuchakulo kwanza alicheka kisha akayatema mate chini na kuwaambia "Msinichezee, mimi nimetahiri na ninyi bado. Meno ya mtu aliyetahiri ni magumu, na anaweza kutafuna hata mawe."

Akatoa zabibu tena, akizitafuna. Baru! Baru! Baru! Huku akiwaangalia nyani kwa dharau. Lo! Wale nyani wakashangaa sana. Wakaanza kuangaliana kisha wakamwuliza kuchakulo: "Sasa twambie tutafanyaje ili tuweze kutafuna zabibu kama wewe?"

Kuchakulo akawaambia: "Hakuna dawa nyingine ila kutahiri tu!"

Nyani wakamwambia awaletee ngariba wa kuwatahiri wawe kama yeye. Wakapanga siku ya kumleta huyo ngariba. Kuchakulo alimwendea chui na kumwambia: "Bwana chui, kila wakati nasikia wanitafuta uniue. Nikikupatia nyani uwafanye kitoweo chako utanifaa namna gani?" Chui akamwambia: "Mimi hupenda sana nyama ya nyani na ukinipatia hata mmoja urafiki wetu utadumu."

Kuchakulo na chui wakapanga mahali watakapokutana akiwa na wale nyani. Kuchakulo akawaendea nyani na kuwaambia: "Nimempata mtu hodari sana wa kutahiri na amekubali kufanya kazi hiyo bure ili awasaidie." Nyani kusikia hawatalipa kitu wakafurahi sana wakawaendea wengine na kuwapasha habari. Siku ile iliyopangwa na kuchakulo na chui ikaonekana inawafaa vile vile. Siku ilipofika kuchakulo alimwendea Chui kumwambia: "Nifuate."

Chui alimfuata mpaka mahali palipokuwa na pango lenye giza akaachwa ndani. Halafu, Kuchakulo aliwaendea nyani na kuwaleta kwenye uwanja uliokuwa karibu na pango lile. Walipokwisha kujipanga, Kuchakulo akawaambia: "Mtakuwa mkija mmoja mmoja mpaka yule

wa mwisho."

Kuchakulo kaenda tena ndani ya pango na kumwambia Chui ajiweke tayari. Ikawa kazi ya Kuchakulo ni kumpelekea mmoja mmoja akiimba wimbo huu:-

"Vumilia, Vumilia
Huwezi kufa,
Vumulia, vumilia
Uondolewe utoto,
Hakuna kulia au kufanya kelele,
Vumulia tu ufanywe mtu mzima."

Kufika pangoni nyani aliingia peke yake na kuchakulo akaachwa mlangoni. Nyani alipofika ndani alimkuta Chui amejiweka tayari kumvunja shingo na kumtupa ndani kabisa mvunguni.

Mtindo huu uliendelea mpaka karibu kumfikia nyani wa mwisho. Kila wakati alipompeleka mmoja alikuwa akiimba wimbo ule wake. Walipokuwa wamebaki wawili tu wakamshuku kuchakulo.

Mmoja akamwambia mwingine: "Wewe ukifika mlangoni uangalie vile wale wenzetu wanavyofanywa ili tujue yanayofanyika."

Kuchakulo akaja tena na kumwambia: "Twende, unasitasita nini? Je, unaogopa?"

Yule nyani hakutaka kumwonyesha anashuku kitu. Kuchakulo akaanza: 'Vumilia, vumilia, Huwezi kufa... Heeeeeeeeeee! Huuuuuuuuuuuu! Haraka twende!"

Yule nyani kufika mlangoni akasimama, akainama na kuangalia ndani. Kwa mwangaza kidogo akamwona Chui Mkubwa mwenye madoadoa ya manjano na meusi anamkodolea macho. Kuangalia uvunguni akawaona wale wenzake wote wamelala wamekufa fo! fo! fo! Akaondoka mbio mpaka alimpomwacha mwenzake na wote wakatimua mbio wakatokomea msituni Kuchakulo alijaribu kuwafukuza asiwapate akarudi kwa Chui. Chui akamshukuru sana akimpigapiga mgongoni na kumhakikishia kuwa urafiki wao utadumu.

Kuchakulo akamwacha Chui na mizoga ya nyani na kurudi nyumbani.

Wale Nyani wawili ndio waliowazaa nyani tunaowaona siku hizi, na tangu siku ile hawajadhubutu kumcheka tena kuchakulo.

Mfano **2**

Nyani na Mamba

Hapo zamani paliondokea nyani na mamba amboa walikuwa marafiki wa kufa kupona wallishi katika kijiji cha mla chake. Maskani ya mamba yalikuwa majini nayeo ya nyani yalikuwa mitini. Siku moja mamake maba aliugua maradhi yasyokuwa na tiba alipoenda kwa mganga alielezwadawa ilikuwa figo ya nyani. Aliprejea nakumsimulia nyani kuhusu masaibu ya mamake nyani alipigwa na mshangao na akajua maisha yake yamo hatarini. Alipanga safari ya kwenda katika kijiji kilochokuwa upande mwingine wa mto, alimjia rafikiye Mamba na kumjuza kwamba kuna figo nyingi upande ngambo ile nyingine na hivyo alimwomba mamba ambebe hadi wavuke mto ili akamchukulie figo.Mamba kusikia hivyo alimbeba hadi wakuvuka mto. Nyani alipovuka mto aliupanda mti uliokuwa karibu na akuonekeana tena

Umuhimu wa khurafa.

- Humwezesha msimulizi na hadhira yake kusema mambo ambayo kwa kawaida ingekuwa muhali kuyatamka hadharani.
- Huwakashifu binadamu bila kuudhi mmoja kati ya hadhira.
- Husaidia katika kupiga chuku mambo yanayotendwa na binadamu na hivyo kuwakosoa.
- Huwakilisha sifa za binadamu kama vile ulafi.

3. **Ngano za mazimwi**

Ni hadithi ambazo huwa na mazimwi kama wahusika wakuu. Zimwi ni kiumbe ambacho ni zao la akili ya binadamu. Zimwi linapofananishwa na bidanadamu, hupewa sifa fulani zinazojitenga na binadamu wa kawaida kama vile kuwa na jicho moja, mikono mingi na miguu kubwa ajabu.

Sifa za mazimwi

- Ni ujumbe wa kuogofya.
- Kila wanapopata nafasi huwatesa wanadamu.
- Huwa na sifa zinazojitenga na wanadamu wa kawaida kama vile macho matatu.
- Ni wenye uwezo kuliko binadamu.
- Ni wajinga, binadamu huweza kuwashinda kwa sababu ya ujanja wao.
- Kiwango cha taharuki ni cha juu.
- Hujumuika na binadamu katika ndoa, densi na vita.
- Ni wadanganyifu na huwa na akili ya binadamu.

Umuhimu wa ngano za mazimwi

- Huonyesha ubunifu wa binadamu, wanabuni mazimwi kwa mawazo yao.
- Kukemea ukatili katika jamii.
- Kuonyesha kuwa wema hushinda uovu kila mara.
- Kuhimiza moyo wa ushujaa.
- Kukaza uwezo wa kufikiri miongoni mwa watoto kupitia fantansia.
- Kuburudisha.
- Kusifu wema.
- Kuendeleza uhusiano katika jamii.
- Kuboresha uwezo wa kukumbuka.

4. Ngano za usuli

Husimulia visa vinavyoeleza asili ya vitu kimaumbile au hali fulani.

Aghalabu sifa fulani za ndege au wanyama huelezwa.

Sifa za ngano za usuli

- Huchukuliwa na wanajamii kuwa ukweli.
- Ni maarufu miongoni mwa jamii nyingi.
- Huonyesha uhusiano wa karibu sana kati ya binadamu na wanyama.
- Huwa na mwelekeo wa kihistoria.

Umuhimu

- Kueleza dhana ambazo ni nzito kueleza kisayansi.
- Kuelezea utamaduni wa jamii.
- Kukuza uwezo wa kufikiria.

Kwa mfano; kwa nini harage lina jicho moja?

Kwa nini fisi ana madoadoa.

KWA NINI KUKU HUCHAKURACHAKURA

Hapo zamani palitokea kuku na mwewe .Ndege hawa walikuwa masaibu wakufa kuzikana . Waliishi pamoja kwa miaka na mikaka.Walishirikiana na kusaidiana kwa lolote lililotokea, la majonzi na la furaha. Walishirikiana katika kazi zote zilizowahusu. Kila mmoja wao alikuwa na bidii ya mchwa walipofanya kazi. Waligawana kazi mbalimbali na kuzifanya bega kwa bega. Kazi ya mwewe ilikuwa kutafuta chakula chao cha kila siku naye kuku alikuwa na wajibu wakuwatunza watoto wao. Alihitajika kuwapa chakula cha kutosha na kuhakikisha walitulia. Kuku pia alihitaji kuwaamsha wengine kulipokucha Ndege hawa waliishi pamoja kwa amani, utulivu na ushirikiano bila ya kukumbwa na tatizo lililowashinda kutatua waliahidiana kuwa wangekuwa marafiki; hadi kifo chao. Urafiki wao wa chanda na pete uliwafanya walale njaa nyakati zingine ili watoto wapate chakula cha kutosha. Sikumoja kuku na mwewe walialikwa katika karamu Fulani na ndege wenzao. Walitarajia kwenda karamuni pamoja na watoto wao. Mwewe aliandaa wanawe na kuhakikisha kuwa walikuwa tayari kwa karamu hiyo kubwa. Kuku aligundua kuwa vifaranga wake walikuwa na kucha ndefu zilizoonekana mbaya. Aliamua kumwomba mwewe wembe, “Tafadhali nipe wembe nikatie wanangu kucha,”

*“Haya chukua.Hakikisha umeuregesha, la sivyo**...**”Alipoupokea wembe alimshukuru rafikiye kasha akaanza kukata kucha za vifaranga wake. Alikata kucha za vifaranga watatu vizuri lakini alipokuwa akimshughulikia wa nne, wembe ulimponyoka ukaanguka. Alijisemea kwa masikitiko, “Ole wangu mie, wembe wa mwewe nitaupata wapi?” Mwewe alipomaliza kujitayarisha alimwita kuku waende karamuni.Kuku aliyekuwa na wasiwasi alikataa kwenda huku akisingizia maumivu mwilini. Mwewe aliwachukua wanawe na kujiendea karamuni.Baada ya mwewe kuondoka, kuku alirudi nje na kuanza kuchakura chakura chini mahali alipokuwa akiwakatia vifaranga kucha. Alitafuta hadi*

machweo bila kufuadafu. Mwenye wembe aliporejea alimwuliza,“Kulikoni ndugu kuku?”
*“Ah, eh, wembe, wajua wembe wako u u u**...**”*
“Wembe umefanya nini? Isijekuwa umeupoteza!”
*“Kwa kweli ndio ume**...**potea”*
“Aka!Hujui wewe huo wembe ni mmoja kama roho. Lazima nitwae fidia.
Nitawala vifaranga wako mmoja hadi uniregeshee wembe wangu.”

5. Ngano za mtanziko

Hadithi ambazo wahusika au mhusika hupambana na hali ambapo analazimika kufanya uteuzi mgumu yaani, kuna hali mbili au zaidi zilizo gumu. Huweza pia kuhusisha kufanya uamuzi fulani aghalabu kimaadili.

Sifa za ngano za mtanziko

- Huishia kwa swali ambalo mtambaji analiachia hadhira ijibu au iliwazie na kulitafutia uvumbuzi.
- Hukusudiwa kuipevusha jamii kwa kuikuza na kuendeleza uwezo wao wa kufanya uamuzi fulani.
- Huweza kuzua mijadala miongoni mwa wanajamii pamoja na kuukuza uwezo wa kushiriki kwenye majadiliano au mazungumzo ya kimjadala.

6. Istiara

Hadithi ambayo huwa na maana mbili; uwazi na ufiche. Ile maana wazi huificha maana ya pili ambayo kueleweka kwake huhitaji ufahamu fulani wa muktadha wa hadithi yenyewe. Wahusika na matukio yaliopo huwa kama mlinganisho wa hali nyinginezo huwa kama sitiari yaani vinasimamia watu halisi.

7. Soga

Ni hadithi ndogo ndogo zinazohusisha utani na ucheshi kwa kiasi Fulani kimsingi soga hutumiwa kwa akili ya kuchekesha, kukejeli au kuumbua au kufanyia dhihaka. Hata hivyo, katika ucheshi huo, mna mafunzo muhimu kwa binadamu.

Sifa za soga

- Wahusika huwa ni wa kubuni.

- Wahusika hupewa majina ya watu wanaopatikana katika jamii.
- Huwa na ukweli fulani unaowaumiza na unaowahusu wanajamii.
- Ucheshi au vichekesho vinavyotumiwa huwa muhimu kama njia ya kupunguza ukali wa ukweli uliomo.
- Hujengwa kwenye tukio moja.

Kwa mfano;

Katika kijiji kimoja paalishi Nafula na bintiye Esikoni. Esikoni alikuwa mrembo wa kupindukia na kila mvulana alitafuta mbinu ya kumtongoza, kwani ilikuwa muhali kumpata. Nafula alikuwa amemwonya mara kadhaa dhidi ya kucheza na wavulana. Siku ya Jumapili Adela ambaye alikuwa jirani wao aliamua kwenda kuazima kisu, kwa bahati nzuri, alikutana na Nafula akienda kanisani, akamweleza " Nafula nimetumwa nije uniazime kisu." Nafula akamweleza "Nenda umwambie Esikoni akupe." Adela akaenda mbio, kufika tu akamweleza Esikoni "Leo umeambiwa na Mamako unipe…" Esikoni akashangaa na kusagaa, akamwuliza Adela " Nikupe nini?" Adela bila kupoteza wakati akamwita Nafula kwa sauti kwani hakuwa ameenda mbali. " Nafula! Nafula-eee! amekataa!" naye Nafula akamjibu " Esikoni! Esikoni! mpeeee…"

Umuhimu wa soga katika jamii

- Kukejeli matendo ya binadamu ambayo huwa na matokeo mabaya au yasiyofaa katika jamii.
- Huwaelekeza wanajamii kwenye mambo au tabia inayofaa au inachukuliwa kama msingi mzuri kwa matendo ya binadamu.
- Huwasilisha mafunzo fulani kuhusu matendo na tabia ya binadamu.
- Ni msingi wa burudani hata kutokana na utani na ucheshi wake.
- Huonyesha utani uliopo katika jamii.

8. Mbazi/vigano

Ni hadithi ambazo huwa za kimafumbo na mafunzo, hutolewa kwa kutumia kielelezo hasa wakati wa maongezi, zina wadhifa wa kama methali.

Sifa za mbazi

- Hutolewa kama kielelezo.
- Kusudi ni kumkanya, kuwelekeza, kuadhibu na hata kumfunza anayesikiliza.
- Hadhira hujifunza kutokana na masaibu yaliyowafika wahusika wa hadithi hiyo.
- Mifano kutoka bibiliani.

Kwa mfano

Kulikuwa na mpanzi aliyetawanya mbegu, nyingine zikaanguka miibani na nyingine kwenye mawe na nyingine kwenye udongo wenye rotuba. Zilizoanguka kwenye mawe zililiwa na ndege, zilizoanguka miibani zikamea lakini zikabanwa na magugu na zilizoanguka kwenye udongo wenye rotuba zikamea zikazaa.

9. Ngano za kichimbakazi/ udhubahi

Ni hadithi ambazo aghalabu hujifunza kwa matendo ya mhusika ambaye hukumbana na matatizo ya kila aina ambayo uhusisha matendo ya kimaumbile lakini mwishoe huishi maisha ya raha mfano katka bibilia Yohana kisa cha Nelson Mandela.

Sifa

Maajabu, uchawi, uganga, itikadi huchukua sehemu kubwa sana kisa maarufu za sinderela.

10. Mchapo au kidahizo

Huwa ni kisa kifupi kinachomhusu mtu au tukio fulani. Aghalabu wahusika wanaopatikana kitaka mchapo huwa na maana ya ziada.

Pasta na mhumini

Siku moja Mritu alimwendea pasta amwombee ili apate bwana, pasta akamjuza awe akienda kanisani jioni kuomba na anapoomba asikize sauti ya “mungu” toka juu. Siku moja pasta alijificha darini akamsikiza Mritu akiomba ndiposa pasta akamjibu akiwa amebadili sauti yake “Toka nje na baada ya dakika kumi urejee utampata bwana wako ameketi humu kanisani” Mritu alitoka nje naye pasta akashuka toka kwa darini na kuketi pembeni. Mritu aliporejea alipigwa na butwaa kuona mungu amempa pasta.

B) NGANO ZA KIHISTORIA

1. **Mighani/Migani**

Huzungumzia watu ambao ni mashujaa katika jamii.Walitenda matendo ya kishujaa, hutokana na watu waliowahi kuishi.

Sifa za mighani.

- Huzungumzia matukio ya kihistoria na wahusika waliowahi kuishi au wanaoaminiwa waliishi.
- Matendo ya wahusika hupewa sifa ambazo zinapita uwezo wa kawaida wa binadamu.
- Chuku hutumiwa katika utambaji wake.
- Huwa na ukweli wa kihistoria.
- Wanajamii wanaamini matendo ya mighani ni ya kweli.
- Kila jamii ina mighani yake.
- Aghalabu majagina huwa na siri ya nguvu na uwezo wao.
- Hatima ya wahusika huwa ni kifo kisicho cha kawaida.
- Majagina mara nyingi huwindwa na maadui zao.

Umuhimu wa mighani

- Ni njia moja ya kupitisha au kuitunza historian ya jamii
- Ni njia ya kutukuza matendo ya kishujaa
- Hutumiwa kukuza ujasiri na ukakamavu wa kijamii
- Huburudisha
- Huelimisha wanajamii kuhusu maisha
- Hufunza utamaduni
- Hukuza lugha
- Hufunza maadili ya jamii

2. Visasili.

Neno visasili huwa ni ufupisho wa visa vya asili. Ni sawa na visa viini. Hii hadithi hueleza chanzo cha mambo, yaani jinsi kitu au watu walivyopata kuwepo.

Sifa.

- Masimulizi ya kuelezea asili ya vitu, watu au matukio mbalimbali.
- Yaweza kuwa hadithi ya sasa au ya kale.
- Wahusika huwa binadamu au wanyama.

- Visa asili vinafungamana na imani ya kidini ya jamii, hasa hadithi zinazohusu asili ya watu; yaani jinsi kundi fulani la watu lilivyoanza.
- Kila jamii ina kisa asili chake na inakiamini.

Umuhimu wa visasili

- Hueleza utaratibu wa kutekeleza desturi kwa mfano, jinsi ya kutoa kafara
- Hueleza chanzo au asili ya tabia au hata watu fulani.
- Huhalalisha baadhi ya mila kwa mfano utoaji wa mahari.
- Husaidia katika kukitisha mizizi tabia fulani ya watu na vitu vinavyowazunguka.
- Huhimiza maadili ya jamii na imani zake.

3. Shajara

Hutumiwa kuelezea maelezo ya matukio au matendo ya mtu au watu fulani kwa mujibu wa kutoka kwake.
Shajara hueleza jinsi matukio hayo yanavyotokea kila siku .
Huwa ni hifadhi ya matukio kwa kutegemea siku hadi siku.

4. Tarihi

Ni hadithi fupi zinazosimulia matukio muhimu ya kihistoria. Matukio yanaweza kuwa ya huzuni au ya furaha. Lengo lake ni kuikumbusha jamii mambo yaliyotukia. Inawezekana matukio yanayosimuliwa yakawa ya kweli yaani yaliwahi kutokea.

5. Kumbukumbu

Ni neno linalotumiwa kuelezea maelezo au hadithi za matukio yanayohusishwa na jamii au mtu fulani. Kwa kiasi kikubwa, huwa pana mwelekeo mkubwa wa kuyaangalia maisha ya mtu huo au jamii hiyo yaani wasifu.

UTANZU WA MAIGIZO

Utangulizi

Maigizo/drama huwa mazungumzo yanayoambatana na matendo. Wahusika huigiza maneno, matendo na tabia ya watu fulani. Nia huwa ni kuburudisha na kupitisha ujumbe fulani. Maigizo hupatikana katika tanzu nyingine za fasihi simulizi ya kiafrika kama vile katika hadithi, mtambaji huambatana na matendo. Uigizaji pia hupatikana katika ushairi simulizi kama vile ngonjera, majigambo, tendi na

mazungumzo kama vile soga, ulumbi na malumbano ya utani.

Vipera Vya Maigizo

- michezo jukwaani
- Michezo ya watoto
- Vichekesho
- Matambiko
- Ngomezi
- Miviga

Sifa za maigizo

- Hutolewa mbele ya hadhira.
- Uigizaji huhitaji mandhari maalum ya utendaji.
- Hufungamana na shughuli za jamii kama vile mtambaji wa hadithi na sherehe za miviga kama jando, harusi na matanga.
- Sharti kuwe na tendo la kuigiza ambalo lina matendo ya watu na viumbe wengine kwa nia ya kuelimisha, kukashifu, kusifu na kuburudisha.
- Waigizaji wanavaa maleba yanayooana na hali wanayoigiza.
- Maigizo huigiza hali ya maisha ya jamii; kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kwa nia ya kuonyesha mafanikio, udhaifu na migogoro katika nyanja za maisha.
- Huwa na muundo mahususi na mtiririko wa matukio tangia mwanzo ukuzaji wa migogoro, kilele na usuluhishaji.
- Maigizo yaweza kuandamana na ngoma, pamoja na uimbaji au ukariri wa tungo za kishairi.

Umuhimu wa maigizo

- Huburudisha watazamaji na waigizaji wenyewe. Burudani hii mara nyingine hupumbaza.
- Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii kama vile upashaji tohara, matambiko, majigambo, ngoma, miviga na michezo ya watoto hudumishwa kupitia maigizo.

- Ni kitambulisho cha jamii; kila jamii ina Sanaa ya maigizo ya jamii husika. Miviga na sherehe za arusi na mazishi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.
- Hukuza umoja na ushirikiano wa watu wanapojumuika kushiriki katika maigizo. Hao hujitambulisha kama jamii moja.
- Ni nyenzo za kupitisha maarifa na amali za jamii kupitia michezo ya jukwaani.
- Husawiri mtazamo wa jamii kuhusu masuala mbalimbali kama vile woga, wizi na usaliti.
- Hukuza ubunifu madhalan watoto wanaposhiriki michezo ya watoto, hujifunza kubuni michezo wakiwa wachanga na pia Sanaa ya uigizaji.
- Hukuza kipawa cha uongozi katika michezo, huweza kujifunza stadi za uongozi
- Ni njia ya kuimarisha urafiki. Kwa vile mizaha na utani katika malumbano hukuza urafiki na uhusiano bora
- Huongoza jamii kupambana na na mazingira wanamojipata. Kutegemea imani ya wanajamii,matambiko yanaweza kuondoa matatizo katika jamii kama vile njaa, ugonjwa na ukame kwa kuomba Mungu
- Maigizo huelimisha kupitia maudhui na hulka za waigizaji na kushauri nafsi zao, kuiga au kukashifu hulka hizo.

1. Malumbano ya utani/mchongoano

Ni kufanyiana dhihaka ili kuchekesha watu. Wanajamii wanaweza kutaniana kwa namna ifuatayo:
Utani wa mababu/mabibi na wajukuu.
Utani wa marafiki.
Utani wa ukoo /makabila.
Utani wa rika moja.

Sifa za malumbano ya utani

Malumbano ya utani hufanywa na watu wawili au makundi mawili ya watu wanapokutana hata hivyo, kila utani una msingi na mpaka wake.
Watu wenye uhusiano mzuri ndio hutaniana, watani hufanya mizaha ambayo inadhibitishwa na masharti

yanayotawala uhusiano wao. Baadhi ya makabila hutaniana mazishini.
Malumbano ya utani inaweza kuwa kati ya makabila, marafiki, wajukuu na mababu, wajukuuu na mabibi, bwana na bi harusi. Katika malumbano ya utani, mbinu ya chuku hutumiwa kwa kiasi kikubwa, mbinu hii hunuiwa kusisitiza sifa fulani au kukejeli sifa fulani wazi. Malumbano ya utani yanaweza kuwa hata na masimango.
Huchukua njia ya ushindani, kila mmoja akijaribu kumpiku mwenzake.Wakati mwingine watu hutania wasiokuweko, utani wa aina hii huandamana na uigizaji wa kuchekesha.

Umuhimu wa malumbano ya utani

a) Hutoa maadili kwa hivyo mila na desturi za jamii huwapa baadhi ya watu katika jamii jukumu la kutaniana na wengine kwa sababu maalum.
b) Malumbano hupunguza urasmi miongoni mwa wanajamii, hivyo huhimiza kujieleza kwa urasmi bila kuficha.
c) Huimarisha urafiki, ni watu walio na uhusiano mwema tu wanaoweza kutaniana.
d) Hukuza utangamano miongoni mwa watu na makabila mbali mbali hasa wanapokuja pamoja kutaniana.
e) Hutambulisha jamii kwa kutaja baadhi ya sifa zake katika utani k.m unaweza kumtania mtu mchoyo, hivyo kumtaka ajirekebishe.
f) Hukosoa na kukashifu tabia hasi baadhi ya malumbano ya utani hudhihaki ulafi, uchoyo, wivu na tabia nyingine mbaya.
g) Huburudisha, ucheshi katika malumbano ya utani huburudisha na kuchangamsha.
h) Huelimisha, kupitia malumbano ya utani, watu hupata maarifa ya kukabiliana na hali mbalimbali maishani.

Mfano wa utani

Mtu A: *Wasee wasee unacheki huyu msee kwao ni wengi hadi wakipika chapo wanatoa photocopy*

Mtu B*: Wasee wasee unacheki huyu msee amezeeka hadi ako na phone number ya Abraham wa bibilia.*

2. Ulumbi

Huu ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee, ni utangulizi wa lugha kwa mvuto na ufasaha. Ulumbi huwezesha mtu kulieleza jambo la kawaida kwa namna ambavyo linaonekana kuwa geni kabisa na kuwashawishi watu kulikubali au kulipenda.

Kuna aina mbili za ulumbi

Ulumbi rasmi

Ulumbi usio rasmi

Ulumbi rasmi unaweza patikana katika miktadha ifuatayo;

a) Kortini, ambapo mawakili hutoa hoja zao kuwatetea wanaowawakilisha.
b) Kanisani au msikitini, kanisani ambapo wahubiri wanatoa sala.
c) Mijadala ya kisiasa ambapo wanasiasa wenye vipawa vya ulumbi huvitumia kuwapiku wanasiasa wenzao na kuwashawishi raia kuwapigia kura.
d) Katika sherehe za arusi au mazishi k.m katika kutoa taabili; maelezo yanayotolewa kuhusu aliyeaga.
e) Katika kuapiza na katika kufukuza pepo.
f) Katika utoaji wa risala.

Ulumbi usio rasmi unaweza kupatikana hali zote zisizo rasmi. K.m vile mazungumzo ya kupitisha wakati; kuapiza, kulaani, kushauri, baina ya wanafunzi n.k

Sifa za ulumbi

1. Mlumbi hutumia lugha kwa njia ya kuvutia na kushawishi hadhira yake
2. Ulumbi hubainika katika miktadha ya kutoa hotuba au katika hali ambapo mtu anahitajika kutetea msimamo wake katika vikao au hata katika mijadala rasmi
3. Hukuza ukakamavu wa kuzungumza hadharani, mlumbi hupenda kuzungumza na hupenda kujisikia akizungumza mbele ya watu.
4. Hutumia vipengele anuwai vya lugha k.v sitiari, maswali ya balagha, methali, nahau, taswira na pia viziada lugha kama vile toni ili kuishawishi hadhira au kutilia mkazo wazo fulani na kutetea misimamo yao, hutumia lugha kutegemea muktadha na hadhira yake.

5. Katika baadhi ya jamii, walumbi walitumika kuzungumza kwa niaba ya viongozi kama maehifu, wanaoomba posa au kwa niaba ya ukoo au mwanajamii aliyedhulumiwa. Walumbi wengi aghalabu huwa na vipawa vya uongozi na huinukia kuwa viongozi wa jamii zao.
6. Ulumbi husisitizwa sana katika matabaka ya juu kama kitambulisho cha tabaka hilo, baadhi ya jamii, watu katika tabaka tawala walifunzwa kutumia msamiati wenye haiba, matumizi ya ishara, toni na sauti zifaazo, hili lilinuiwa na kuimarisha stadi za ulumbi.
7. Walumbi hutumia chuku kwa kiasi kikubwa hata hivyo, lazima wadumishe adabu.

Umuhimu Wa Ulumbi

1. Hukuza uwezo wa kujieleza hadharani, kadri mtu anavyozungumza hadharani, ndivyo anavyojiboresha kama mlumbi
2. Ni nyenzo ya kukuza ujuzi na ufasaha wa lugha, jinsi mtu anavyoitumia lugha kwa ugwiji, ndivyo anavyokuza umairi wake wa kuisarifu lugha.
3. Ni msingi wa kuteua viongozi, uwezo wa mtu kuwashawishi wanajamii kukubaliana na mtazamo wake humfanya kutambuliwa kama mwenye uwezo wa kuongoza jamii. Walumbi wana uwezo mkubwa wa kuishawishi hadhira.
4. Huhifadhi utamaduni wa jamii, ulumbi ni sanaa jaadia, imekuwepo katika jamii kwa muda mrefu, ikipokezwa vizazi na vizazi.
5. Ni nyenzo ya kuburudisha wanajamii na kuwaelimisha bila kuwachosha, walumbi huweza kupitisha maarifa mbali mbali kwa wanajamii kwa njia yenye mvuto.
6. Hukuza uzalendo, vijana wanaposikiza walumbi wakitongoa lugha, huionea fahari lugha yao na kujitambulisha zaidi na jamii zao.
7. Huweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu au ulio na athari kubwa au ambao una makali na usio rahisi kueleza.

8. Ni kitambulisho cha utabaka, katika baadhi ya jamiii ulumbi ulihusishwa zaidi na tabaka tawala au watu wenye vyeo vya juu na heshima katika jamii zao. Katika jamii hizi ulumbi ni kigezo cha kuainisha matabaka.
9. Ulumbi ni msingi wa kuheshimiwa katika jamii, walumbi huheshimiwa kwa sababu ya matumizi ya lugha yenye ubingwa na ustadi katika kuyafafanua maswala ya jamii.

3. Hotuba

Ni maelezo au taarifa itolewayo mbele ya hadhira kuhusu mada fulani, kwa kawaida hotuba ni mazungumzo rasmi kama vile:

1. Hafla za kisiasa (hotuba za wanasiasa)
2. Kanisani au msikitini (mahubiri)
3. Sherehe za kitamaduni k.v vikao vya posa.
4. Kortini kabla jaji hajatoa hukumu, anaweza kutanguliza hotuba.
5. Kwenye mazishi (taabili) taadhiri na risala za rambirambi.
6. Katika harusi mawaidha yanayotolewa kwa maarusi huchukua muundo wa hotuba
7. Katika tamasha za muziki na ukariri wa mashairi au mashindano ya utoaji hotuba.

Sifa za hotuba

1. Kwa kawaida, hotuba hutolewa na watu maalumu au walioteuliwa kuzungumza k.v viongozi au wawakilishi wao na watu wengine wenye hadhi katika jamii. Hata hivyo, baadhi ya hotuba hutolewa katika miktadha isiyo rasmi, katika makazi ya watu hotuba za mawaidha (waadhi) nasaha huweza kutolewa wakati wa chajio au baada ya chajio
2. Watu wanaoteuliwa kutoa hotuba aghalabu huwa na umilisi mkubwa wa lugha, walumbi ni watoaji hotuba na wana stadi za kutoa hotuba zao hadharani.
3. Hotuba hutolewa kwa nafsi ya kwanza.
4. Mtoaji hotuba anaweza kutumia viziada-lugha kama vile ishara za uso na mikono ama miondoko ili kufanya

hotuba ivutie hadhira, maswali ya balagha pia hutumika
5. Hotuba huteuliwa mada mahususi wala haizungumzii jambo lolote lile.

Umuhimu wa hotuba

1. Huadilisha na kuasa, hotuba zinazotolewa jandoni au arusi kwa kawaida hunuiwa kutoa nasaha
2. Huelimisha, hotuba za jandoni kwa mfano huwapa vijana maarifa ya kukabiliana na maisha.
3. Huimarisha ukakamavu wa kuzungumza hadharani, kadri watu wanavyotoa hotuba ndivyo wanavyoimarisha umilisi wao wa lugha na ujasiri wa kuzungumza hadharani.
4. Hukuza ufasaha na umilisi wa lugha
5. Hupalilia kipawa cha uongozi, kwa kawaida mahatibu huteuliwa kadri mtu anavyochukua jukumu la kuhutubu katika hafla mbalimbali, ndivyo anavyojitayarisha kuchukua nyadhifa kubwa zaidi za viongozi.

4. Mawaidha

Haya ni mazungumzo yanayotolewa yanayompa mtu ushauri au nasaha kuhusu jambo fulani, mawaidha hutoa mwongozo na maelekezo ya kukabiliana na changamoto katika maisha na jinsi ya kuhusiana na wanajamii.

Sifa za mawaidha

1. Mawaidha hutolewa katika miktadha mbalimbali; rasmi kama vile jandoni, katika arusi, kwenye maisha darasani na kanisani. Hata hivyo, mawaidha yanaweza kutolewa katika miktadha isiyo rasmi kama vile mzazi anaweza kumpa mwanawe mawaidha nyumbani wakati wa chajio.
2. Katika jamii nyingi, wazee na watu walio na vyeo vikubwa na waliochukuliwa kuwa na hekima ndio waliowapa vijana mawaidha. Hata hivyo, vijana pia wanaweza kutoa mawaidha kwa vijana wenzao wanaohitaji ushauri au pia vijana wanaweza kutoa mawaidha kwa wazee.

3. Hutolewa zaidi kwa wadogo, ambao wanaaminika kuwa wanahitaji kupewa mawaidha maishani. Hata hivyo, yanaweza kutolewa kwa yeyote anayehitaji
4. Mwenye kutoa mawaidha analielewa jambo analowosia kwa undani lazima awe na ujuzi wa kutosha katika mada anayozungumzia.
5. Mwenye kutoa mawaidha hutumia lugha inayoathiri hisia za wanaowosiwa inaweza kuwa na tamathali za usemi kama vile methali.
6. Mawaidha huingiliana na vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile methali hufumbata mawaidha pia utambaji ngano, miviga kama vile jando na arusi huandamana na utoaji wa mawaidha aidha yapo mashairi ya waadhi halikadhalika anayetoa mawaidha anaweza kutumia mbazi/vigano ili kusisitiza ushauri anaotoa.
7. Maudhui katika mawaidha ni mapana yaani huweza kugusia maswala kama dini, uongozi, ujasiriamali, elimu na taaluma, unyumba, mahusiano ya kijamii, malezi na afya.
8. Mawaidha yanayotolewa katika miktadha rasmi mbalimbali huwa na muundo maalum yenye sehemu tatu kuu:
    i) **Utangulizi**, katika sehemu hii anayetoa mawaidha huanza kwa kauli ya kuvuta makini ya hadhira anaweza kuanza kwa kutoa kiini cha mawaidha, kwa mfano utu uzima huenda na uwajibikaji… baadaye anaelezwa anayofaa kufanya
    ii) **Uwili,** mawaidha huwasilishwa na kusisitizwa kwa kutumia kauli sisitizi na tamathali za usemi kama vile methali, tashbihi, istiara hutumika kuwosia, maonyo na maelekezo hutolewa kutegemea lengo
    iii) **Hitimisho**, mwasilishaji huonyesha msimamo wake kuhusiana na swala analowosia kwa kawaida anayetoa mawaidha huishirikisha hadhira kwa kutaka kujua msimamo au maoni yao kuhusu

swala alilowawosia, hadhira inaweza kutaja changamoto zinazohusiana na wosia unaotolewa.

9. Anayetoa mawaidha hutumumia mambo mengi kupitisha mawaidha hayo k.m miondoko ya viungo au ishara, kubadilisha kasi ya kuzungumza na pia kudondoa sehemu za watu maarufu.

Majukumu ya mawaidha

1. Jukumu la mawaidha ni kuelekeza, mawaidha hutoa mwongozo wa jinsi ya kukabiliana na matatizo au jinsi ya kutenda jambo fulani.
2. Huelimisha, mawaidha huwapa wanajamii maarifa ya kuendesha maisha, huwajuza wanajamii kuhusu majukumu ya kijamii na matarajio ya jamiii zao kwao.
3. Huadilisha wanaopewa mawaidha hujifunza maadili kama vile usafi, unyenyekevu, utulivu na kusamehe.
4. Hutambulisha jamii, kila jamii huwa na aina yake ya mawaidha kulingana na thamani zake pia mawaidha hutolewa kwa namna mbalimbali kutegemea jamii.
5. Husaidia kuondoa ujinga katika jamii, huadilisha waliopotoka na kufanya mabaya.
6. Husaidia kuwapa ukakamavu wasio nao na kuwaongezea wengine ujasiri na stadi za kimaisha.
7. Huwaandaa watu kushiriki ipasavyo katika shughuli za kitamaduni, kijamii na kadhalika.

Mfano wa mawaidha

1. *Owa , sandame hadaa, moyo ukahadaiwa*
   Owa, anaye kufaa, mke mwenye kusifiwa
   Owa, upate kuzaa, kama ulivyozaliwa
   Owa, ukijaaliwa, mupendane na mkeyo
2. *Owa, aliye na kheri, muandamane kwa dini*
   Owa, yai la johari, litiye nuru nyumbani
   Owa, mdomo mzuri, ukupandie lisani
   Owa ungiye nyumani, mupendne na mkeyo
3. *Owa, moyo wa imani, wazumbua majuja*
   Owa, susiowe duni, anayeitwa kioja
   Owa, mtenda ya dini, ndiye mke mwenye haja
   Owa, utungiwe koja, mupendanena mkeyo.

4. *Owa, usiowe tambara, linukiyalo vibaya*
Owa, mwanamke jura, umjunze yenye ndiya
Owa, usiowe sura, kutakakuzangaliya
Owa, mzuritabiya, mupendane na mkeyo

5 *Owa, akukubaliye, akuizao siowe*
Owa, upendanenaye, zamani sizo ujuwe
Owa, akuridhiyaye, mujikubali wenyewe
Owa, mukae mutuwe, mupendane na mkeyo

6 *Owa, utukuze cheo, na jina lipate kuwa*
Owa, upate mkeo, aambiwe meolewa
Owa, kama waowao, moyo usiliye ngowa
Owa, ujue kuhuwa, mupendane na mkeyo.

ZOEZI

1.a) Eleza sifa za mawaidha zinazojitokeza

Inaandamana na miviga; arusi au ndoa
Maudhui ya ndoa yanaonekana wazi
Inatolewa kwa wadogo; wale ambao bado hawajaoa

b). Utungo huu unaweza kutolewa katika muktadha upi?

Unaweza kutolewa kwa mtu anayetarajia kuoa

c.)Eleza mawaidha yanayotolewa kuhusiana na ndoa.

Mtu anafaa amwoe mke ambaye wanapendana naye.
Oa mwanamke ambaye anaheshimu dini
Oa mwanamke mwenye tabia njema.

2.a) Taja miktadha mitano ya kutoa hotuba

Katika mikutano ya kisiasa. Katika sherehe za kibinafsi
Katika mikutano shuleni.katika kusoma bajeti.
Viranja wakiongea kwa wanajunzi.

b) Eleza majukumu manne ya mawaidha.

Mawaidha huelimisha wanajamii
Pia husaidia kuondoa ujinga katika jamii
Huwaandaa watu kushiriki katika shughuli za kitamaduni.
Husaidia kuwapa watu ukakamavu katika wasauyayo

5. Soga.

Rejelea soga katika hadithi
Soga ni mazungumzo yanayonuiwa kupitisha wakati

6. **Maapizo**

Maapizo ni maoni maalum ya kumtaka mungu, miungu na

mizimu kumwadhibu mhusika hasidi, mkinzani na mwovu. Hivyo maapizo ni dua yaa laana au maombi mabaya kutoka kwa mtu anayehisi ametendewa wovu au amesalitiwa na mwingine.

Sifa za maapizo

1. Maapizo yalitolewa na watu walioenda kinyume na matarajio ya jamii zao mifano ya watu hawa ni wabakaji, wezi, wauaji na waliowatusi wazazi, wazee au ukoo.Wazazi pia huweza kutoa maapizo kwa wana wao ili kuwaonya dhidi ya hulka mbaya kama vile utumiaji wa vileo.
2. Katika baadhi ya jamii za kiafrika, maapizo yalitolewa kabla ya ulaji viapo.mlaji kiapo anaweza kusema *ambaye amefanya tendo hili chuma hiki kimwingie kwenye mboni ya jicho,asiuone mwangaza wa jua tena*
3. Maapizo yanaweza kutolewa moja kwa moja na yule aliyeathirika, mtu anapopoteza kitu chake anaweza kuapiza ili kumtisha aliyeiba k.m *aliyeiba mbuzi wangu apepenuke na huo mchanga, zizi lake asiweze kulala mbuzi hata mmoja*
4. Kidini, Mungu, miungu au mizimu huweza kutoa maapizo kuhusu mustakabali wa mhusika fulani aidha maapizo ya kidini yanaweza kutolewa kama laana baada ya mhusika kukaidi amri za Mungu au miungu, maapizo ya aina hii huathiri mhusika na jamii yake.
5. Maapizo huaminika kuwa yataleta maangamizi kwa jamii, hivyo wanajamii hushauriwa kuyaepuka kwa kutenda mema.
6. Maapizo hutumia fasaha k.m ulumbi watoaji maapizo katika ulaji wa aghalabu huwa walumbi.
7. Maapizo hutumia lugha kali inayonuiwa kujaza woga ili kuonya dhidi ya uovu.

Umuhimu wa maapizo

1. Kimsingi, maapizo hutumiwa kama nyenzo ya kawaonya wanajamii dhidi ya matendo hasi
2. Hutambulisha jamii, kila jamii ina namna yake ya kuapiza, na mitindo tofauti ya kutoa maapizo.

3. Hukuza umoja katika jamii, kuweka na kaida au miiko sawa huwafanya watu kujihisi kuwa kitu kimoja.
4. Huadilisha, wanajamii hujifunza kutenda mema ili kuepuka laana.

Mfano wa maapizo

Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,
Nami ndiye nilompa uhai mwana unoringia,
Anakufanya upite ukinitemea mate,
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Mzimu na waone uchungu wangu,
Radhi zao wasiwahi kukupa,
Laana wakumiminie,
Uje kulizwa mara mia na wanaa,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,
Wakaza mwanao wakuuguze katika utu uzima wako!

MASWALI

1. **Msemaji ni nani katika utungo huu?**

Mzazi –mkwe

2. Fafanua sifa tatu za anayeelekezewa maapizo haya

Mwenye majivuno, anaringa kupitia mwana wa msemaji
Mchoyo, anamnyima msemaji chakula hata wakati wa kuwa na wajukuu wake.
Mwenye dharau, msemaji anasema kuwa anayerejelewa anapita akimtemea mate.

3. Andika mifano ya maapizo katika miktadha ifuatayo.

a) Dini- *kwa dharau uliomwonyesha mtumishi wa jalali na asikujalie mema uishipo duniani humu*

b) **Familia**-*yule atakayepuuza amri zangu kama kicwa cha familia hii, asiweze kukuza familia yake mwenyewe.*

c**) Kijiji** *–aliyeiba matunda shambani mwangu, na matunda hayo yawe mwisho kuyala, atambae njaa mpaka atakapokabiliana na ziraili wake.*

d) **Darasani**-*aliyeniibia kalamu zangu na asipite mtihani wake wa mwisho wa mwaka*.

4. Eleza majukumu ya maapizo yanayojitokeza katika tungo.

Unaadilisha msemaji anakashifu tabia hasi zilizo kwa mkazamwana wake.

7. Ngomezi

- Ngomezi ni fasihi ya ngoma.
- Midundo na mapigo fulani ya ngoma ubainisha maana na ujumbe maalum kutengemea jamii.

Sifa za ngomezi

- Ujumbe huwa umefichika ile hali ya midundo na mapigo ya ngoma.
- Mapigo na midundo hii hufuata toni na wizani (ridhumu) kwa mujibu wa lugha ya wahusika au jamii husika.
- Ujumbe huweza kueleweka na kutafsiriwa na wanajamii au hadhira iliyonuiwa. Hulenga hadhira teule.
- Kila utaratibu wa ngoma hubainisha suala tofauti na ula mwingine
  Kutegemea mapigo huweza kutofautisha baina ya habari za kutangaza hatari ya vita, harusi, au kifo cha kiongozi.
- Huweza kuwasilisha ujmbe wa dharura kwa njia ya haraka na ambayo si ghali ikilinganishwa na njia zingine.
- Ngomezi huongozwa na watu teule katika jamii ili kuhakikisha kuwa hakuna kutuma ujumbe unapotosha au kuwasilishwa visivyo.
- Ngomezi vilevile hutolewa wakati maalum mfano vita au vifo kitokeapo.

Udhaifu wa ngomezi

- Si kila mtu katika jamii atapata kutafsiri ujumbe vyema.
- Ngoma pia husikika kwa idadi ndogo tu ya watu wanaoishi pengine katika kijiji kimoja.
- Mapigo na midundo yanaweza kuhitilifiana na hivyo kuwasilisha ujumbe amboa haukukusudiwa.
- Utanzu huu haujachunguzwa kwa kina na huenda ukapotea bila kuacha kumbukumbu ridhishi endapo utafiti hautaendelezwa.
- Hubagua wageni wa jamii husika na vilevile wasio na uwezo wa kusikia.

Sio rahisi kutia mpaka baina ya habari moja na nyingine.

USHAIRI SIMULIZI

Utangulizi

Ushairi simulizi ni utanzu unaojumuisha tungo zote zenye mapigo ya kimuziki, mawazo, hisia na hoja katika utanzu huu huwasilishwa kwa njia ya mdomo kutumia lugha ya mkato yenye mpangilio maalumu wa maneno katika mishororo. Ushairi simulizi huimbwa, hughaniwa au hukaririwa ni muhimu kutaja hapa kuwa ushairi simulizi hutofautiana na mashairi ambayo huandikwa kwa lengo la kuwasilisha mbele ya hadhiri katika mashindano ya tamasha za muziki au yanayowasilishwa katika hasia maalumu.

Sifa Za Ushairi Simulizi

1. Ushairi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo mbele ya hadhira kwa kukaririwa, kughanwa au kuimbwa. Nyimbo kwa mfano huimbiwa watu hata hivyo, baadhi ya mashairi huimbwa na watu bila kuhusisha hadhira nyimbo za kazi mara nyingi hazina hadhira.
2. Hubuniwa papo hapo na kuwasilishwa kwa hadhira au tungo za awali huwasilishwa kutoka kwa kumbukumbu za mwasilishaji.
3. Tungo za mashari simulizi hutolewa zikiambatana na ala za muziki, uimbaji wa nyimbo huambatana na ala kama njuga na marimba aidha anayejigamba huweza kutumia ala kama vile mkuki anapojigamba.
4. Ushairi simulizi ni sehemu ya utamaduni wa jamii na hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, nyimbo za jandoni (nyiso) na tendi, kwa mfano hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
5. Ushairi simulizi hutumia lugha yenye mvuto mkubwa, yenye mapigo yaliyopangwa kwa muwala na urari.
6. Utungo wa ushairi simulizi huweza kuwasilishwa na mtu mmoja kama ilivyo katika majigambo au kundi la watu kama vile nyimbo nyingi na ngonjera.
7. Ushairi simulizi hubadilika kulingana na anayeuwasilisha, hadhira na wakati.Wimbo mmoja unaweza kuimbwa kwa mahadhi mbalimbali kulingana

na mwimbaji, mwasilishaji anaweza kubadilisha wimbo au shairi wakati wa kuimba, kukariri au kughani kutegemea hadhira yake.

8. Hadhira huweza kushiriki katika uwasilishaji wa mashairi simulizi, mwimbaji, kwa mfano, anaweza kuishirikisha hadhira yake katika uimbaji kwa kupiga makofi.
9. Uwasilishaji wa mashairi simulizi, kwa kawaida huandamana na uigizaji. Mwimbaji kwa mfano huambatanisha maneno yake na vitendo kama vile ishara za uso, ishara za mkono, miondoko mbalimbali na upigaji makofi.
10. Ushairi simulizi hufungamana na shughuli au muktadha maalumu mathalani nyimbo hufungamana na shughuli tofauti tofauti kama vile:

i) **Hodiya**-nyimbo za kazi.
ii) **Kimai**-nyimbo za uvuvi na shuguli za majini.
iii) **Mbolezi**-nyimbo za kuomboleza/matanga.
iv) **Wawe**-nyimbo za kilimo.

11. Ushairi simulizi una miundo mbalimbali, unaweza kuwa na beti zilizo na kibwagizo kila ubeti unaweza kuwa na idadi tofauti tofauti za mishororo, kama vile 2,3,4,5,6,7 na zaidi.
12. Ushairi simulizi unaweza kuwa na urari wa vina na mizani au ukakosa kuwa nao, kilicho muhimu zaidi ni mapigo ya muziki yanayofanya utungo huo uweze kuimbika.
13. Ushairi simulizi, kama tanzu nyingine za fasihi simulizi hutumia lugha ya kitamathali, kunaweza kuwa na misemo, nahau, methali, ishara, taswira, jazanda na istiara.

Uainishaji wa ushairi simulizi

Mashairi simulizi yanaweza kuainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali kam vile.

1. Maudhui

a) Mapenzi-hupitisha jumbe za mapenzi.
b) Kutuliza-kuna nyimbo za bembea au bembelezi zinazowatuliza watoto.

c) Kuomboleza-mbolezi huimbwa wakati wa msiba.
d) Kusifu-sifa huimbwa kujisifu mashujaa au waliofaidi umma na kustahili kutambuliwa.
e) Siasa-nyimbo za siasa huwasilisha jumbe za kisiasa.

2. Muktadha au mahali pa uwasilishaji

a) Nyiso-nyimbo za jandoni.
b) Mbolezi-zinazoimbwa kwenye mazishi au kwenye maombolezi.
c) Nyimbo za harusi.
d) Nyimbo za matambikoni ambazo hutolewa wakati wa kutoa kafara au sadaka kwa mizimu, labda baada ya janga.
e) Nyimbo za kazi.

3. **Mtindo wa uwasilishaji**

a) Maghani hutolewa kwa kalima bila kuimbwa.
b) Nyimbo huwasilishwa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka.
c) Shairi utungo unaokaririwa.
d) Tendi au Rara husimuliwa kwa mapigo ya kishairi.
e) Ngonjera huwasilishwa kwa kujibizana.

4. **Mwasilishaji**

a) Majigambo huwasilishwa na anayejigamba
b) Kwaya uimbaji wa watu wengi

Umuhimu Wa Ushairi Simulizi

Ushairi simulizi kama kipengele cha fasihi simulizi una umuhimu wa kijumla licha ya kuwa kuna vitanzu mbalimbali vinavyotekeleza majukumu tofauti. Majukumu ya ushairi simulizi hutofautiana kutoka jamii hadi jamii, hata hivyo kuna majukumu ya kijumla kama vile

a) Ushairi simulizi hutumiwa kupitisha maarifa au mafunzo ya jamii fulani nyimbo za jandoni, za harusi na dini hutumiwa kupitisha mafunzo maalumu.
b)Ni nyenzo ya kuhifadhi na kupitisha utamaduni na historia ya jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa mfano, tendi zinazosifu mashujaa huendeleza historia ya jamii hiyo kwa kuonyesha matukio kama vile nyimbo za jandoni (nyiso) husawiri utamaduni wa jamii kuhusu jando na kuuhifadhi.
c) Hukashifu tabia hasi kwa nia ya kuhimiza urekebishaji

wa tabia hizo nyiso kwa mfano, hukashifu woga, hivyo vijana waoga huhimizwa kujirekebisha. Maghani na nyimbo za kisiasa hukashifu tawala dhalimu.
d) Ni nyenzo kuu ya kukuza umoja na uzalendo miongoni mwa wanajamii kupitia kwa nyimbo zinazosifu mashujaa wa vita, huhimiza vijana kuzionea fahari jamii zao na kujitoa mhanga kuzitumikia aidha wanajamii wanapojumuika pamoja kuimba au kughani katika hafla fulani, hujihisi kuwa kitu kimoja, hivyo uzalendo hujengeka.
e)Ni nyenzo ya kutakakasa hisia kupitia kwa mashairi au nyimbo, watu hutoa hisia za moyoni na kutakaza nyoyo zao mfano mwafaka ni nyimbo na mashairi ya mapenzi ambayo kwayo mtu humtolea mpenzi wake hisia. *Rara* pia hutumiwa kutekeleza jukumu hili.
f) Huelimisha, hukosoa na kurekebisha jamii nyimbo hutoa maadili ya kuonya na kuelimisha wanajamii nyimbo au mashairi ya sifa, tendi hata mbolezi huonyesha matendo mazuri ya anayeimbiwa na kukashifu wanaoenda kinyume na matakwa ya jamii.
g) Husawiri mfumo wa jamii fulani kisiasa, kiuchumi na kijamii baadhi ya nyimbo huonyesha shughuli za kiuchumi za jamii kama vile ufugaji. Hodiya (nyimbo za kazi) huonyesha shughuli mbalimbali kama vile uwindaji, kilimona uvuvi. Majigambo pia husawiri mifumo ya jamii kisiasa na kijamii.
h) Huonyesha falsafa na imani za jamii husika kuhusu masuala fulani. Mbolezi huonyesha imani za jamii kuhusiana na kifo. Majigambo husawiri falsafa ya jamii kuhusu ushujaa.
i) Ni nyenzo kuu ya kuhamasisha wanajamii. Nyimbo za kisiasa na kizalendo zimetumiwa na tawala kama nyenzo ya kueneza propaganda za kisiasa.
j) Hukuza ubunifu anayekariri, huimba au kughani mashairi huhitajika kubuni mbinu zifaazo za uwasilishaji. Kwa kufanya hivi, uwezo wake wa kubuni hukuzwa.
k) Hukuza usanii wa lugha wanaotunga na kuimba mashairi huhitajika kubuni mbinu zifaazo za uwasilishaji kwa kufanya hivi, uwezo wake wa kubuni hukuzwa.

l) Husaidia wanajamii kukabiliana na hali ngumu na kuwahimiza wasikate tama kwa mfano mbolezi husawiri na kusawiri kifo kama faradhi kwamba humfika yeyote, hivyo hisia za mwemeo hupungua aidha nyimbo huhimiza waliokwenda vitani au wanaofanya kazi wasikate tamaa.
m) Ushairi simulizi hustarehesha na kufurahisha wanajamii tungo za ushairi simulizi huvutia hisia, huburudisha na kusisimua mwili na akili.

Vipera vya Ushairi Simulizi

Ushairi simulizi una vipera vitatu:

- Nyimbo
- Maghani
- Ngonjera

Nyimbo ni tungo za kishairi zenye mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti, muwala na mapigo ya kimuziki na huwasilishwa kwa kuimbwa, nyimbo hutambuliwa kwa sifa tatu;

i) Huwepo kwa hadhira inayotumbuizwa
ii) Muziki unaoimbwa kwa sauti
iii) Matumizi ya ala

Sifa za nyimbo

a) Sifa bainifu ya nyimbo ni kwamba hutolewa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti.
b) Nyimbo hutumia lugha ya mkato yenye mpangilio maalumu wa silabi, mishororo na beti zenye mapigo ya kimuziki.
c) Nyimbo hutumia lugha nzito yenye kuibua taswira na hisia nzito kama za mapenzi, huzuni na furaha.
d) Nyimbo zinapoimbwa, maana nyingi huandamana na ala za muziki kama vile ngoma, baragumu, msewe na zumari.
e) Katika jamii za kiafrika, nyimbo hufungamana na muktadha fulani kuna nyimbo za kazi harusi jando na unyago kuzaliwa kwa mtoto, kumpa mtoto jina, ibada na matambiko.
f) Baadhi ya vifungu katika nyimbo hurudiwarundiwa vifungu hivi huitwa vibwagizo, viitikio au mikarara ya nyimbo.

g) Nyimbo nyingi huandamana na ucheshaji wa viungo kama vile mabega kupiga makofi na mapigo ya miguu.
h) Kimsingi, nyimbo ziliimbwa na makundi ya watu kwa hadhira hai. Hata hivyo, kuna nyimbo zinazoimbwa na mtu mmoja kwa hadhira yake au hata bila hadhira.

Umuhimu wa nyimbo

a) Nyimbo hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii iliyozibuni mathalan nyimbo katika jamii ya wakulima zitasheheni msamiati unaohusu shughuli za kilimo kama vile kuvuna, kupanda na kupalilia.
b) Nyimbo humwezesha binadamu kutakasa hisia zake kupitia kwa nyimbo, binadamu hutoa hisia za moyoni kama vile kujutia kosa alilofanya, mapenzi ama huzuni. Mbolezi humsaidia aliyehathiriwa kutoa hisia za huzuni. Nyimbo za mapenzi kama vile chombezi, humwezesha mpenzi kumfichulia mwenzake hisia za moyoni.
c) Ni mbinu mojawapo ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii rekodi za matukio muhimu katika jamii huweza kuhifadhiwa kwa nyimbo na kupitishwa kwa vizazi.
d) Nyimbo hutumbuiza hutumiwa kama burudani, kufurahisha, kustarehesha na kusisimua.
e) Hupitisha amali na mambo ambayo jamii inayothamini, amali hizo hurekodiwa katika nyimbo mbalimbali kama vile za kazi na kurithishwa vizazi vya jamii hiyo. Mawaidha na thamani za jamii hukaririwa katika nyimbo kama nyenzo za kuzirithisha.
f) Nyimbo hutumiwa kuhamasisha watu na kuchochea hisia za kuchangamkia jambo fulani. Nyimbo za kisiasa, kwa mfano huweza kuchochea hisia za kuungana pamoja kutetea haki au kuunga mkono jambo fulani.
g) Nyimbo huakisi ukwasi wa tamaduni za jamii umbuji (ufasaha wa kujieleza) na ujamii (mvuto na uzuri wa kazi ya sanaa) wa jamii hujitokeza katika nyimbo

huteuzi wa maneno,ishara na ujumbe katika nyimbo huonyesha ukwasi wa jamii hiyo kifani.

h) Hukuza ubunifu miongoni mwa wanajamii, uimbaji ni kipawa na nyimbo hupalilia kipawa hiki.

Aina mbalimbali za nyimbo

Bembelezi /bembea/bembe/pembezeji

Hizi ni nyimbo zinazowafanya watoto walale au watulie wanapolia, zinapoimbwa.

Sifa

1. Bembea huimbwa kwa utaatibu kwa sauti na mahadhi ya chini.
2. Huimbwa na wazazi au walezi wa watoto kuwaliwaza na kuwabembeleza watoto walale.
3. Huwa fupi.
4. Bembea hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kutokana na thamani za jamii hiyo.
5. Huimbwa kwa kurudiarudia maneno au kibwagizo wakati mwingine hata nyimbo mzima huimbwa kwa kurudiwarudiwa.
6. Hutumia lugha shawishi na wakati mwingine hutolewa ahadi za kumnunulia mtoto zawadi.
7. Aghalabu zinapoimbwa, mtoto huwa amebebwa kwa mbeleko na mwimbaji kutoa mapigo ya kumpapasa.

Umuhimu

1. Hutumbuiza na kuongoa watoto, bembea hupumbaza na kumfanya mtoto anyamaze au alale anapolia
2. Hutumiwa kama sifa kumsifu mtoto mtulivu, husifu pia somo ya mtoto huyo au wazazi wake.
3. Husawiri mfumo wa kiuchumi wa jamii husika, ikiwa baba ni msasi, mtoto atarajiwa kuwa baba ni msasi jasiri au baba yake yuko karibu kutoka usasini.
4. Huonyesha au kusawiri uhusiano katika jamii kupitia bembea, mlezi huweza kuibua migogoro iliyomo kati yake na wazazi wake au wazazi wa mtoto, hivyo kuonyesha uhusiano kati ya waajiri na wajiriwa.
5. Hutakasa hisia ambazo mwimbaji huweza kuwa nazo

6. Humwelimisha mtoto, hata katika umri huu mchanga, kuhusu mambo na shughuli mbalimbali katika jamii na umuhimu wake au thamani yake katika jamii.
7. Husawiri falsafa au mtazamo wa jamii kuhusu jinsia na matarajio ya jamii kwa jinsia Fulani katika bembea, mlezi anaweza kutaja kuwa machozi ni ya kike iwapo anamtuliza mtoto mwanaume, majukumu ya mtoto wa kiume kwa jamii pia huweza kutajwa mlezi huweza kumtajia mtoto wa kike kuwa anatarajiwa kuwa mlezi mwema.
8. Huwaonya watoto dhidi ya tabia hasi. watoto huonywa dhidi ya kulia onyo kwani kulia hukumbusha mtu mambo mabaya.

Mfano

Ewe malaika wangu
Uloshuka toka mbinguni
Mbingu kapasua kwa hei
Siku nipokukopoa
Ulinitia furaha iliyopasua kifua
Tabasamu kipajini pako
Ilinitia tumaini, ikanisahaulisha zingizi
Ikayeyusha madhila, ya utasa wa miaka kumi
Ikapeperusha mbali cheka la ukwenza.
Sasa napolia, wanitonesha jeraha
Waniregesha misri, kwa vitimbi vya firauni
Kwa vitisho vya muhebi
Talaka huahidiwa, hadi mbingu.
Lipofungua milango ya heri,
Silie mwana silie, walimwengu watakusuta.
Tangu hapo tanabahi
Vidume humu mwenu
Kulia hari kuumbiwa
Machozi na kekevu ni za kike fahamu
Jogoo halii, daima huwika
Nikikuona kigugumika hivi wanitia hangaiko
Tumaini kuzima
Udhaifu kiandama, moyo kitia hamaniko
Atanipigania nani

Watesi king’anga’ania chake kujitwalia?
ZOEZI
1(i) Je, mtoto huyu ni wa kike au kiume?
ii) Thibitisha
2. **Mwimbaji ni nani au ana uhusiano gani na anayeimbiwa**?

ii) Thibitisha.
3. Andika sifa tatu za jamii ya mwimbaji
5. Andika mbinu za lugha zilizotumiwa
6. Andika majukumu sita ya wimbo wa aina hii.

Hutumbuiza watoto na kuwaongoa
Hutumika kumsifu mtoto mtulivu
Husawiri mfumo wa kiuchumi wa jamii husika
Husawiri uhusiano katika jamii kupitia migogoro
Hutakasa hisia ambazo mwimbaji huweza kuwa nazo
Huwaonya watoto dhidi ya tabia hasi.

Mbolezi /nyimbo za matanga/tahalili
Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa wakati mtu amefariki au wakati wa maafa ama katika halfa za kuadhibisha makumbusho.
Sifa
1. Mbolezi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kutegemea imani ya jamii kuhusu kifo na pia kulingana na aliyekufa.
2. Huimbwa kwa njia ya kuwafariji waliofiwa
3. Husifu aliyekufa kwa kawaida mbolezi hutoa sifa chanya au nzuri za aliyekufa watu mashuhuri katika jamii huweza kutungiwa mbolezi zao mahususi zinazowasifu na kutuja michango yao kwa jamii.
4. Hufungamana na muktadha maalum, mbolezi huimbwa tu katika matanga au wakati wa kuomboleza jambo fulani.
5. Huimbwa kwa toni ya huzuni na pengine uchungu ili kuibua hisia za ndani za mwombolezaji.
6. Huimbwa kwa mwendo wa utaratibu.
7. Huonyesha imani ya jamii husika kuhusu kifo.

Majukumu

1 Husawiri msimamo wa jamii kuhusu kifo wapo wanaoamini kuwa kifo husababishwa na maovu au pepo fulani na watakao kashifu kifo, watu wengine hutambua kifo kama mlango wa kuingia katika uzima wa milele (kidini)
2. Kuwaliwaza waliofiwa, na kuwasaidia kukabiliana na uchungu au uzito wa kumpoteza mpendwa wao.
3. Hutoa wasifu wa aliyekufa
4. Ni njia ya kutakasa moyo na hisia za aliyefiwa, aliyefiwa huweza kutumia mbolezi kutoa hisia zake za huzuni kwa njia hii, anaweza kupunguza uzito wa kumpoteza mwenzake.

Mfano

“Kama kesho itapambauka
Jua la kinjano kuchomoza
Kuangazia siku mpya
Siku isio tumaini
Siku bila mimi mama mtu.
Kumbuka ewe kipenzi
Usiache chozi kufurika
Kuyeyusha makini yako inuka, mwanangu inuka
Silie daima, yote yatatengenea’’
Mpenzi mama ulolala usingizi usio na mzindushi
Nalikumbuka vyema hili ni beti uloniandikia
Kitandani ukiwa, ukiuguza donda.
Donda walokusababisha walimwengu mahasidi
Ela nataka ujue, kamwe yote si shwari kama uliponambia
Hayawezi kuwa shwari kwa mlezi kikembe
Hayawezi tengea kwa yatima alozungukwa
Na waja wenye tama kila kitu kurithi,
Hayawezi kuwa shwari kumtazama mwezio,
Ulotwambia tumwite baba na kumstahi,
Ati ni amri ya muumba
Akitoka na muhebi, pumbao apata yeye
Wafurahia ulochuma wewe.
Najitahidi mpenzi mama
Ukakamavu kujipa
Machozi kuyafuta

Ela hino kumbuka
Kuondoka kwako huko
Hatukukutarajia japo hukuisha kunikumbusha
Ziraili liingia ja mwewe
Na kukwiba mithili ya kifaranga
Mama yake akitazama.

MASWALI

1a) Andika sifa za mbolezi zinazojitokeza

Huimbwa kwa toni ya huzuni na uchungu kwani anayeimba ana huzuni kwani amempoteza mama.
Inadhihirisha imani ya jamii inatajwa kuwa ziraili alimwiba mama

B) Andika mbinu zilizotumiwa

Tashbihi-ziraili liingia ja mwewe
Inksari-walokusababishia.

Nyiso

Nyiso n nyimbo zinazoimbwa jandoni(wavulana) na unyagoni (kwa wasichana) kila jamii hata hivyo ina desturi zake zinazozingatiwa kama kigezo cha kuvusha vijana kutoka utotoni na kuingia utu uzima.

SIFA

1. Zilitoa sifa kwa waliotiwa jandoni (waliopashwa tohara) wazazi na wasimamizi wao.
2. Ziliimbwa kuwapa wavulana ujasiri wa kukabili kisu cha ngariba
3. Zinatoa mafunzo kwa wavulana kuhusu majukumu yao mapya baada ya kutiwa jandoni.
4. Katika baadhi ya jamii, nyiso huimbwa usiku wa kuamkia siku ya kupasha tohara
5. Maudhui katika nyiso hutofautiana kutoka jamii hadi nyingine.
6. Maudhui yanaweza kuwa ya kuonya dhidi ya kutoa siri, kuwaandaa kwa uchungu watakaohisi au kukejeli woga.

Majukumu

1. Hutumika kuwaondoa kihisia wanaotarajia wanaotahiriwa kuwapa ari ya kuwapa kisu cha ngariba

2. Huwajuza wanaotahiriwa kuhusu majukumu mapya na matarajio ya jamii yao kwao, huwafahamisha kuwa wamevuka na ni muhimu kuwaandaa kiakili kwa majukumu ya utu uzima
3. Huonyesha furaha ya vijana wanaotoka katika utoto na kuingia utu uzima.
4. Huhimiza ujasiri na kukebehi woga.
5. Huhimiza uzalendo na kuonea fahari utamaduni wa jamii, wanaohiriki jandoni hujitambulisha na jamii zao zaidi na hivyo uzalendo huimarika.
6. Nyiso hutoa nasaha kwa vijana, huwafahamisha kuhusu matarajio ya uchungu, matarajio ya utu uzima husa dhidi ya woga na umuhimu wa kuhifadhi siri watakazopewa.
7. Huburudisha waliohudhuria shughuli hii.
8. Huleta umoja miongoni mwa wanajamii, vijana waliotahiriwa wakati mmoja hujitambulisha kama ndugu.

Mfano

Ewe kiii
Ulozowea kujificha
Nyuma ya mama kujikinga, dhidi ya milio
Ya radii ilo juu mbinguni
Jua kesho ni siku ya siku
Siku ya kujua mbichi na mbivu
Kutofautisha jogoo na vipora
Ngaribu taposhika, chake kijembe
Ndipo utakapojua bayani
Ukoo wetu si wa kunguru
Ikiwa u tayari
Kisu kukidhihaki
Si thubutu kamwe, wanjani kuingia
Ije kuniabisha miye, amiyo na akraba nzima.

Nyimbo za kisiasa

Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa katika shuguli au miktadha ya kisiasa.nyimbo za kisiasa huwa na maudhui mapana kama vile mapambano, propaganda, kuzindua, kuhamasisha, kukejeli, kuburudisha, kuhimiza au kutia ari.

Sifa

1. Huwa na maudhui mapana kama vile mapambano, propaganda n.k
2. Huimbwa katika shughuli au miktadha ya kisiasa.
3. Huonyesha hali ya mwenye nguvu kumwonea mnyonge.
4. Huburudisha hutumbuiza na kustarehesha watu katika shughuli za kisiasa au za kitaifa.
5. Hutumiwa kuwatuliza na kuliwaza wahasiriwa wa migogoro ya kisiasa.

Jukumu

1. Hukuza umoja wa kisisa miongoni mwa washiriki .wakati wa kupigania uhuru, nyimbo hizi zilitumiwa kama nyenzo za kuwaunganisha watu.
2. Huzindua na kuhamasisha watu, huwapa watu k.m wafanyi kazi, ari ya kupigania haki zao. Nyimbo za kisiasa huwatanabahisha watu kuhusu haki zao na kuwahimiza kupigana dhidi ya unyanyasaji.
3. Husawiri mfumo wa kisiasa na kijamii wa jamii husika na maoni ya wananchi kuhusu mfumo huo. Je, wanaupenda au wanaupinga?
4. Husawiri migogoro iliyopo katika jamii, je ni ya unyanyasaji, uongozi mbaya, unyonyaji, ubinafsi, usawa na uhuru?
5. Hutumiwa kueneza propaganda za kisiasa, baadhi ya nyimbo za kisiasa huimbwa ili kusawiri uzuri wa utawala fulani.k.m KANU yajenga nchi, ni wimbo wa kisiasa ulionuia kuwavutia watu kukipenda chama hiki cha kisiasa.
6. Huimiza uzalendo na mshikamano wa kitaifa, nyimbo za taifa ni mfano wa nyimbo za kisiasa zinazohimiza raia kuionea fahari nchi yake na kuishi kwa undugu.
7. Huweza kutumiwa kama rekodi ya matukio ya kihistoria katika jamii Fulani, baadhi ya nyimbo za kisiasa huzungumzia mapambano dhidi ya ukoloni na historia ya mapambano hayo.
8. Hutumiwa kukashifu uongozi mbaya.

9. Hutumiwa kama sifo kuwasifia viongozi waadilifu na mashujaa wengine wa kisiasa kama vile Harry thuku,Dedan kimathi, Arap moi, Jaramogi Odinga, Kenyatta wa nchini Kenya
10. Huburudisha, hutumbuiza na kustarehesha watu katika shughuli za kisiasa au za kitaifa.
11. Hutumiwa kuwaliwaza na kupoza waasiriwa wa migogoro ya kisiasa.

Mfano

Mabeberu watu wabaya
Walimfunga kombozi
Nia yao ikiwa moja
Kudidimiza jamii yetu
Katika lindi la istiimari
Ela hawakufua dafu
Mabarobaro waliingia msituni
Bunduki wakashika
Kupigana, kupigania 'wiyathi'

Beberu lipoona
Vita vimechacha
Tama iliwatoka
Wakasalimu amri
Uhuru wakatoa
Hawakutoa kwa hiari
Hilo usisahau
Wazalendo walipigana
Kwa jino au ukucha
Uhuru tukapata
Kombozi akashika sukani

Nyimbo za sifa/sifo

Nyimbo za sifa pia huitwa sifo.ni nyimbo ambazo hutoa sifa za mtu fulani, sifo husifu michango na mafanikio ya watu katika jamii ni muhimu kutaja kuwa nyiso, mbolezi na nyimbo za arusi hutumiwa kama sifo.

Sifa

1. Sifo husifu na kutukuza watu ambao wamefanya jambo fulani k.m husifu maarusi, waliohitimu jandoni,

viongozi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii, mbolezi na walioshinda mashindano ya michezo au wa kumiliki kitu, kipawa au hali fulani.

2. Sifo hutumia sitiari kwa usanifu mkubwa, huwalinganisha wanaosifiwa na wanyama ili kuonyesha sifa fulani k.m kiongozi anaweza kufananishwa na simba ili kuonyesha ujasiri
3. Sifo hutumiwa katika miktadha mbalimbali ya kijamii kama vile miviga.
4. Huimbwa kwenye jando kuwasiu mashujaa na kuwapongeza kwa kuingia katika utu uzima
5. Huimbwa kwenye mazishi kama taabili/taabini kuwasifu na kuwakumbusha waliokufa.
6. Huimbwa kwenye arusi kuwasifu maarusi.
7. Huimbwa katika sherehe za kutawazwa kwa viongozi au wafalme.
8. Kuna sifo za kidini zinazomsifu Mungu au mitume kwa mfano kasida ya mzia zinamsifu mtume mohammed.

9. Sifo pia huweza kuimbwa na mtu au watu binasfi wakijisifu –majigambo au vivugo.
10. Sifo huasi au kuonyesha thamani ya jamii zinazothamini ujasiri wa kivita, nyingine nasaba tukufu, ufugaji wa mifugo wengi, kilimo au arusi.
11. Sifo hupiga chuku sifa za anayesifiwa.

Majukumu

1. Sifo husifu matendo ya viongozi au watu mashujaa katika jamii
2. Hutangaza mafanikio au mchango wa mtu au watu wanaosifiwa kwa jamii, anayeimba sifo hutaja mambo ambayo anayesifiwa alitenda au ametenda.
3. Hukuza uzalendo, sifo huwahimiza vijana kuiga matendo mazuri ya wanaosifiwa, kwa njia hii, watu hujifunza kuionea fahari jamii na kuwa tayari kuitolea mchango wao.
4. Kuweka kumbukumbu au rekodi ya matukio ya kihistoria, wimbo unaomsifu shujaa wa vita, k.m huonyesha vita alivyopigana, alipigana na nani na lini na mbona

5. Huonyesha msimamo na mitazamo ya jamii fulani kuhusu maswala mbalimbali, wimbo unaosifu uzalendo wa mtu fulani, vilevile unaweza kuonyesha chuki kwa usaliti.
6. Hutambua mchango wa watu mbalimbali kwa jamii, sifo hutaja majina ya wanaosifiwa kwa nia ya kutambua na kutambulisha juhudi zao
7. Huburudisha, sifo nyingi hutumbuiza, hutuliza na hupumbaza akili.

Nyimbo za kazi/hodiya

Nyimbo za kazi pia huitwa hodiya, ni nyimbo zinazoimbwa na watu wanapofanya kazi huwa kama kihamasishaji kwa wanaoifanya kazi fulani au zinaonyesha mazingira yao ya kazi, hofu zao shida zao, matumaini na ndoto zao.

Sifa

1. Maneno ya nyimbo hizi huwa ni ya kuhimiza.
2. Urefu wake hutegemea kazi na vifungu fulani vinaweza kurudiwarudiwa.
3. Mdudo hutegemea kazi inayofanywa, iwapo kazi itafanywa kwa utaratibu mdundo utafuata hali hiyo.
4. Huimbwa wakati watu wanapofanya kazi kila aina ya kazi ina hodiya yake, kwa mfano; wawe /vave ni nyimbo za wakulima. Kimai ni nyimbo zinazohusishwa na ubaharia.
5. Huimbwa na kundi la wafanyakazi au mtu mmoja wakati anapofanya kazi yake binafsi
6. Nyimbo hazihusishi ngoma kwa kuwa watu wote walishiriki kazi.

Majukumu

1. Huhimiza watu kutia bidii na kuendeleza kazi bila kufa moyo.
2. Hukashifu uvivu na utegemezi, baadhi ya nyimbo za kazi hukashifu wasiopenda kazi
3. Hurahisisha kazi kwa kupunguza fikra za uchovu, watu wanapofanya kazi wakiimba kazi huonekana kuwa nyepesi na muda kupita kwa kasi.

4. Husawiri imani, mitazamo na thamani za jamii husika kuhusu kazi jamii inathamini kazi gani? Uzembe na bidii kazini huchukuliwaje? Kazi inapewa nafasi gani?
5. Huonyesha changamoto ambayo wafanyakazi hukabiliana nayo katika kazi zao, je, wanahofia nini kazini? Wana matumaini gani katika kazi zao?
6. Hujenga ushirikiano, watu wanapoimba wanapofanya kazi pamoja hujenga ushirikiano; pia huhimizwa katika baadhi ya nyimbo za kazi.

Mfano

Viongozi walisema
Turudi mashambani
Makonde kushughulikia
Mimea kupalilia
Tutie ghera ndugu
Tujifunge masembo
Udongo tutifue
Samadi tutie
Magugu tung'oe
Kilimo tuimarishe
Pasiwe wa kutuvuta
Misri kuturudisha
Kwa pato la kufutia chozi
Ukame tatwandama
Mashamba tukiachilia
Mmomonyoko kuyatoa
Tutabaki mikunguni
Kutegemea wahisani.

Nyimbo za mapenzi

Nyimbo hizi zinaimbwa kueleza hisia za mapenzi, zinasimamia maoni ya jamii kuhusu mapenzi mtu anaweza kumsifu mpenzi au kusikitika kwa kuachwa na mpenzi, nyimbo hizi huwa na maudhui ya mapenzi.

Sifa

1. Huelezwa kwa maneno matamu yenye hisia nzito.
2. Zinaweza kuwa sifa, yaani zikaimbwa kumsifu mpenzif fulani.
3. Huthibitisha mapenzi.

4. Huwa na maudhui mbalimbali kulingana na lengo la mwimbaji k.m
    i) Kuonyesha kusalitiwa au wivu.
    ii) Kuomba uchumba.
    iii) Kumsifu mpenzi-husifu umbo au hulka yake.
    iv) Kutambua uhusiano mzuri na mwenziwe na kumbembeleza mpenzi.

Majukumu

1. Kusifu tabia au umbo la mpenzi, yaani hutaja tabia chanya na umbo zuri la mpenzi.
2. Kutakasa hisia za anayeimba, mwenye mapenzi huweza kutumia nyimbo kutoa hisia zake za huzuni, furaha au kupumbazika kwa kufanya hivi anaweza kupunguza uzito wa hisia alizonazo.
3. Huburudisha, nyimbo za mapenzi huburudisha anayezisikiza.
4. Hukuza ubunifu, nyimbo za mapenzi hubuniwa kwa ubingwa wa hali ya juu ili kuibua hisia za mapenzi, huzuni au huruma.
5. Ni nyenzo ya kupitisha maarifa au elimu, nyimbo za arusi hutumiwa kutoa mawaidha ya unyumba kwa maarusi wapya aidha matarajio ya jamii na majukumu yao mapya kama bibi na bwana hupitishwa kwa nyimbo.

Mfano

Tina analia tina analia
Chozi lausaliti undani wake
Undani ambao ameuficha kwa miaka na mikaka
Undani ambao japo anachelea kutangaza asije
Akaonekana apendaye chongo
Itabidi kuuto kuumwaga mtama

Na kiini chozi hili ni kwamba imewadia
Imewadia siku kanisani kwenda,
Kujitia pingu pingu za aushi

MASWALI

Jibu maswali yafuatayo ukirejelea wimbo huu

1. **Ainisha utungo huu kimaudhui**.

Ukatili-bibi arusi anapoenda kufanya arusi, bwana arusi haonekani
Mapenzi-mwanamke huyu anaonekana kuwa alimpenda sana mchumba wake.
Usaliti-mchumba wa mwanamke huyu, tina anamsaliti kwa kukosa kuja arusini

2. **kwa mujibu wa wimbo huu, jadili kwa mifano nafasi ya mwanaume katika jamii**

Msaliti-mchumba wa tina anamsaliti kwa kukosa kkufika pale katika arusi ili amwone ***tina***
Katili-pia anamwacha tina pale bila yakumwambia kuwa hangependa kumwoa.

9. **Toa mifano ya tamathali za usemi zilizotumika**

Uradidi-tina analia, tina analia
Methali-apendaye chongo…(huita kengeza)
Nahau- kumwaga mtama.

5. **Fafanua umuhimu wa aina ya tungo hii katika jamii yako**.

Huthibitisha mapenzi baina ya watu Fulani
Hutakaja hisia za anayeimba, baadaye anapunguza uzito wa hisia hizo
Huburudisha wale wanaosikiliza
Hukuza ubunifu kwa wanaobuni nyimbo hizo na kuziimba.

Nyimbo za watoto/chekechea

Nyimbo za watoto pia huitwa nyimbo za chekechea
Sifa

1. Huimbwa na watoto wakati wa kucheza ili kuifanya michezo ipendeze,au wanapofanya shughuli zao za kitoto.
2. Huwa na matumizi ya takriri kwa kiasi kikubwa
3. Ni maarufu katika shule za malezi kama vile chekechea
4. Watoto hufunzwa na kuimba nyimbo hizi
5. Maudhui yake hutegemea aina ya mchezo na jamii husika
6. Lugha yake ni sahili au nyepesi
7. Aghalabu huwa fupi
8. Huandamana na miondoko kwa kiasi kikubwa

Umuhimu

1. Hutumiwa kama burudani, ni nyenzo muhimu ya kujipumbaza na kupitisha wakati
2. Hukuza ubinifu miongoni mwa watoto hujifunza nyimbo zinazooana na michezo yao
3. Hukashifu tabia hasi, watoto hutumia nyimbo hizi kuwakashifu walio na tabia hasi k.v uchoyo.
4. Hukuza utangamano, watoto wanapokuja pamoja kucheza na kuimba, hawajali tofauti zao za kinasaba na huwa kama watu wa jamii moja.
5. Hutambulisha jamii, kila jamii ina nyimbo za watoto ambazo hufungamana na utamaduni pamoja na thamani za jamii hiyo.
6. Hukuza kumbukumbu za watoto, kwa sababu ya kukariri vifungu mara nyingi.

MFANO

Kitoto kivivu aia aia
Kikienda skuli aia aia
Saa tatu hazijafika aia aia
Ndicho hicho chalia njaa aia aia
Ticha' naona njaa aia aia
Malimu hadiriki kuandika lolote aia aia
Kitoto machozi yatoka aia aia
Hadi ruhusa kipewe aia aia
Kitazame kilo ndani ya chupa aia aia
Ndipo kitulie aia aia

MASWALI

1. Andika maadili yanayojitokeza katika wimbo

Bidii –inakashifu uvivu
Tabia njemma- inakashifu tabia ya kulia onyo na kusumbua
Masomo-watto wanahimizwa kwenda shuleni

2. Taja mbinu za lugha zilizotumiwa
   Uradidi- aia aia
   Utohozi -ticha
3. Andika miktadha mitatu ambayo nyimbo za watoto hupatikana

Watoto wanapocheza
Watoto wanapopewa elimu.

Jadiya/jadiia
Ni nyimbo za kitamaduni ambazo huimbwa na kupokezwa kwa mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine, kila jamii ina jadia zipokezwazo kwa vizazi vyake kimaudhui, nyimbo hizi husimulia mambo mengi hasa yaliyotukia katika historia ya jamii kama vile matendo ya shujaa fulani, mateso, njaa na ucheshi.
Kongozi
Ni nyimbo za mwaka, huimbwa wakati wa kukaribisha mwaka mpya.
Nyimbo za dini
Huimbwa katika shughuli za kidini
Kimai
Uhusisha shughuli za kibaharini
Nyimbo za vita
Huimbwa na askari wakati wa vita
Nyimbo za usasi
Huimbwa na wasasi wanapokwenda au kutoka usasini
Husifu mtu fulani kwa mchango wake katika jamii
Nyimbo za kuzaliwa kwa mtoto
Huonyesha au kuathimisha kuzaliwa kwa mtoto.
Maghani
Ni ushairi ambao hutolewa kwa kalmia (nusu kuimba nusu kuongea kama afanyavyo padre) badala ya kuimbwa tofauti kati ya maghani na nyimbo ni kuwa maghani hayaimbwi, hata hivyo kimaudhui maghani ni sawa na nyimbo kama za kazi, maombolezi au siasa; kama ilivyo katika nyimbo.
Sifa
a) Ni fungu za kishairi, yaani yana sifa za kishairi za kuwa na mapigo ya kimuziki na maneno mateule yenye muwala (mtiririko) mzuri wa mawazo
b) Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanayotambwa
c) Hutungwa papo hapo na kusemwa au kutongolewa mbele ya hadhira.
d) Hutungwa kwa ufundi mkubwa
e) Hutolewa na mtu mmoja au kundi la watu
Umuhimu
 a) Kuchochea wanotaka kuwa shujaa

b) Kutoa sifa nzuri za kuigwa au kutumiwa kukosewa
c) Kuelezea usuli wa mtu, asili au nasaba ya mtu kitu jambo au familia.
d) Kudhihirisha uhodari wa kutenda

Aina za maghani

Aina mbili kuu
a) Maghani ya kawaida
b) Maghani simulizi

1. Maghani ya kawaida

Tungo za kishairi ambazo hutongolewa kuhusu maswala ya kawaida, njaa, mapenzi, masikitiko, kazi, majonzi, dini hughaniwa tu.

Rara

Ni hadithi fupi nyepesi za kishairi ambazo husisimua

Sifa

- Huweza kuandamana na ala za muziki.
- Nyingi zilihusu koo tukufu/zilizotajika.
- Hutolea kwa ...ya huzuni /kitanzia.
- Masuala hufumbua na kudokezwa tu.
- Lugha hujaa utendaji wa matukio.
- Hushughulikia maswala ya kawaida na ibuka kwa mtindo usio rasmi.
- Huwa na ucheshi wenye kinaya.

4. Maghani simulizi

Maghani ya kihadithi yanayosimulia sifa za mtu, kitu, mnyama, historia au tukio fulani.
Hutolewa na kuambatana na muziki pamoja na ala k.m zeze, marimba, njuga. Mtambaji wa maghani huitwa yeli/manju. Kwa kawaida, yeye huwa bingwa wa kupiga ala aina fulani ya muziki.

1. **maghani ya kawaida**

Ni ya aina tatu.

a) Sifo

Ni mashairi ya sifa yaghaniwayo kumsifu mtu fulani kutokana na matendo yake ya kishujaa.

Sifa

a) Husifu watu, wanyama, mimea na hata vitu visivyo hai.

b) Hutoa sifa chanya na hasi sifa hasi hukashifu vitendo vibaya.
c) Hutegemeana na kuingiliana na tanzu nyingine za fasihi simulizi, hutumiwa katika k.m mazishi kusifu aliyekufa kwa matendo yake ya kipekee pia huweza kutumiwa katika arusi na tohara kusifu wanaohusika katika shughuli hizo.

Aina za sifo

a) Majigambo /vivugo

Tungo za kujisifu, kujitapa au kujigamba anayejigamba huwa mwanasanaa (mshairi) anayeelewa kwa undani analozungumzia.

Sifa

i. Hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe.
ii. Hutungwa kwa usanii mkubwa, anayejigamba hutumia sitiari, ishara, takriri na tashbihi.
iii. Anayejigamba hujitumia kivugo kufuatia tukio mahususi katika maisha yake, anaweza kuongea kuhusu siku za jandoni, ndoa au kuoa, kutoka vitani, michezo, kesi au jambo kali.
iv. Kwa kawaida hutungwa na kughanwa na wanawake.
v. Huwa na matumizi ya chuku kwa kiasi kikubwa, anayejigamba hujisifu kupita kiasi kwa kutaja mafanikio au mchango wake. Anaweza kuahidi kuleta mafanikio makubwa kuliko yale tayari ameletea jamii.
vi. Hutolewa kwa nafsi ya kwanza maadam anayejigamba ni mshairi mwenyewe.
vii. Anyejigamba huweza kubeba baadhi ya vifaa vyake vya kazi au vinavyoonyesha jambo analojisifia. Aidha anaweza kuvaa maleba yanayooana na kazi au jambo ambalo anajisifia
viii. Kwa kawaida, hutungwa papo hapo hata hiyo mengine huandikwa ili kughanwa baadaye katika hafla fulani k.v arusi.
ix. Anayejisifu hutaja usuli wake wa kinasaba, katika baadhi ya jamii anayejigamba huhitajika kutaja na

kusifu nasaba au ukoo wake, upande wa baba na mama kwa majina yake halisi.

x. Wanaojigamba nao huwa walumbi au washauri wanaofahamu wanalolitunga.

xi. Maudhui makuu ni ushujaa.

Umuhimu

a) Hukuza ubunifu –kadri mtu anavyotunga na kughani majigambo ndivyo anavyoimarisha uwezo wa kubuni mitindo mipya ya utunzi na uwasilishaji.

b) Hukuza ufasaha wa lugha watunzi wengine wa majigambo huwa walumbi.

c) Ni nyenzo ya burudani, huangua waliohudhuria sherehe ambapo yanatolewa.

d) Hudumisha utu na utambulisha mwanamume katika familia, kwa sababu ya uchokozi uliokuwa katika jamii, ilikwa muhimu kwa wanaume katika familia kuwa jasiri, wakakamavu na mashujaa ili kutetea jamii zao. Kupitia kwa majigambo wanaume walidhihirisha nafasi zao katika jamii.

e) Nyenzo ya kufanya watu waheshimiwe, hudumisha ari ya kuwafanya wanaume kutaka kuwa mashujaa mtu alipofanya kitendo cha ushujaa, alijigamba na kuheshimiwa na kila mtu alitaka kufanya jambo la kishujaa ili ajigambe na kuheshimiwa

b) Tondozi

Ni tungo ambazo hughanwa kumsifu mtu, mnyama au kitu k.m milima, kijiji, nchi au kitu chochote ambacho huweza kusifiwa.

Tondozi za watu husifu watu mashuhuri, wapenzi, marafki, watani, wake, waume, watoto au adui zao.Wanyama na vitu ambavyo hutungiwa tondozi aghalabu ni mifugo, wanyama wa porini na miti mikubwa, vitu na wanyama hawa hupewa sifa kistiara, zikikusudiwa binadamu.

Mfano

Kipungu kipungu
Nani kama yeye
Hashindiki kwa nia
Hashindiki kwa shabaha

Hulenga mbinguni
Hutulia gera kufikia peo
Peo zisofikika kwa wanaokata tamaa
Kipungu, kipung'u, hachi tufani za sanaa

I. **Kwa kutoa mifano katika utungo huu, thibitisha kuwa utungo huo ni aina ya sifo.**
Utungo huu unasifu kipungu, ambaye ni ndeg. Inatoa sifa chanya kuhusu kipungu; hashindiki hulenga mbinguni na kufikia peo;hakati tamaa

II. **Kipungu anapewa sifa gani?**
Asiyekata tamaa
Asiyeshindika
Mwenye bidii

(c) Pembezi/Pembezeji

Ni aina ya tondozi inayotolewa kusifu watu fulani pekee, kwa kawaida, husifu watu wenye kujipambanua kwa matendo yao ya kishujaa na kujitolea kwao, hutungiwa watu kama:

- Watawala /viongozi.
- Walezi wazuri.
- Mashujaa wa vita.
- Waganga mashahuri.
- Wapenzi waliopigania pendo lao.

UTANZU WA SEMI

Utangulizi

Semi ni kauli fupi za kisanaa zenye maana na mafunzo yaliyofichika. Semi hutoa mafunzo kwa njia ya kufumba, mafunzo katika semi hutokana na imani ya jamii ambayo imezibuni mifano ya semi ni methali, vitendawili, misemo, nahau, misimu, lakabu, mafumbo, chemshabongo na vitanza ndimi. Semi pia huitwa tungo fupi au tungo bainifu.

Sifa za semi

a) Semi hufumba ujumbe wake kwa mfano maana ya ndani ya nahau "piga kalamu' ni'futa kazi' ilhali maana ya juu ni 'kuchapa au kugonga kalamu methali pia huwa na maana iliyofumbwa aidha vitendawili hufumba jibu.

b) Hutumia picha (taswira) na ishara kupitisha ujumbe wake, mtu anaposema ‘kwetu ni jehanamu; ile picha ya jehanamu inajichora akilini mwa msikilizaji, jehanamu hapa inamanisha mahali pabaya penye mateso mengi
c) Maana ya semi hupatikana katika jamii iliyozibuni, methali “mgaaga na upwa hali wali mkavu” kwa mfano itaeleweka na jamii za pwani.Vile vile katika tashbihi weupe au weusi, hulinganishwa na vitu mbalimbali kutegemea jamii na mazingira yake.mathalani, watasema –eupe kama maziwa au theluji-eusi kama mpingo, lami au makaa kutegemea vifaa vinavyopatikana katika jamii husika.
d) Huwasilisha ujumbe mrefu kwa maneno machache mfano ni methali ‘juhudi si pato’ambayo imefupisha ujumbe mrefu kuwa mtu huweza kufanya bidii sana na akakosa kufanikiwa, Semi huwasilisha ujumbe kwa njia ya mkato tofauti na hadithi ambazo ni masimulizi marefu.
e) Semi ni tanzu tegemezi, hii ina maana kwamba semi hutokea kuambatana au kutegemea tanzu nyingine kwa mfano methali hutolewa katika muktadha wa mazungumzo ya kutoa mawaidha au mwishoni mwa hadithi kama funzo la hadhi lakabu, misimu, misemo na nahau pia hupatikana katika utanzu wa mazungumzo.

Umuhimu wa semi

a) Semi huelimisha, vitendawili, methali, mafumbo na nahau zote hutoa mafunzo ya aina Fulani; methali “mwenda pole hajikwai “hutoa maarifa ya kufanya mambo bila pupa.
b) Hukuza uwezo wa kufikiria, vitendawili, methali na mafumbo humhitaji mtu kufikiria ili kupata ujumbe uliofumbwa.
c) Hutambulisha jamii na wanajamii, kila jamii huwa na semi mahususi zinazohusu shughuli zake, misimu kwa mfano hutumiwa na kundi fulani katika jamii.Methali *mkulima ni mmoja walaji ni wengi* inatambulisha jamii inayohusika katika kilimo, kitendawili kimoja kinaweza

kuwa na majibu tofauti kutegemea jamii na mazingira yake.

d) Hukuza utangamano, wakati wa kutegeana vitendawili; kwa mfano watu huja pamoja aidha misimu hujenga uhusiano wa karibu miongoni mwa watu wanaoitumia, lakabu nazo hutumiwa na watu walio na uhusiano wa karibu.
e) Huburudisha, baada ya shughuli za kazi watu hujumuika pamoja katika vikao vya kujiburudisha ambapo hutegeana vitendawili na hushiriki katika vitanza ndimi ili kutuliza bongo na kusisimka.
f) Huhifadhi utamaduni, semi hufumbata desturi za jamii zinapopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, utamaduni huo hufunzwa na kuhifadhiwa.
g) Husawiri mitazamo ya jamii kuhusu masuala Fulani, je, jamii inachukia nini? Inahimiza nini? Kupitia kwa methali *bidii ya mja haiondoi kudura* tunafahamishwa kwamba jamii hii inaamini kuwa binadamu yumo chini ya uwezo wa Mungu nahau, lakabu, vitendawili na mafumbo pia hufumbata tajiriba ya jamii.
h) Hututasfidia lugha, nahau, misemo, misimu na lakabu hutumiwa badala ya msamiati mkali /wenye aibu, badala ya kusema ‘kuzaa’tunasema ‘kujifungua’
i) Hukuza lugha, semi huyapa maneno maana mpya au maana ya ziada. Misimu huweza kukubaliwa na kuwa nahau rasmi za lugha kwa njia hii msamiati wa lugha hupanuliwa.

Vipera vya semi

Methali

Methali ni semi fupifupi za kimapokeo zenye kueleza fikira, maarifa, hekima na mafunzo yanayotokana na uzoefu wa jamii mahususi. Methali hutumia taswira na mafumbo, chukulia kwa mfano, *fimbo ya mbali haiui nyoka,* utungo huu ni mfupi na unatumia neno ‘fimbo kama fumbo la ‘suluhisho’

Methali ni tanzu tegemezi kama ilivyotajwa kutumika kwake hutegemea tanzu nyingine. Methali hutokea katika mazungumzo mazito kama vile kutoa mawaidha au kama

kielelezo na kifupisho cha hadithi si utanzu unaoweza kujisimamia kama tanzu nyingine kama vile hadhithi, ushairi au mazungumzo.

Sifa

- ✓ Methali ni kauli fupi ambazo hutolewa kwa mtindo wa kishairi kinyume na jinsi kauli za kawaida zinavyowasilishwa.
- ✓ Methali zina sifa za kishairi, huwa na vipande vyenye mizani inayolingana na kwamba ni mshororo mmoja.
- ✓ Maudhui katika methali huchotwa katika jamii zinamozaliwa, maudhui hutokana na tajriba na mambo yanayoathiri jamii.
- ✓ Huwa na muundo maalumu wenye sehemu mbili, kwa mfano. *Aliye juu, mngoje chini* sehemu ya kwanza hudokeza wazo na ya pili hulikamilisha kwa kukubali au kukataa.
- ✓ Hujengwa kwa tamathali nyingine za usemi na mbinu za lugha kama vile kinaya, taswira na takriri, methali *kukopa arusi kulipa matanga* imejengwa kwa sitiari.
- ✓ Methali hueleweka na jamii iliyozibuni kwani hubuniwa kutokana na mazingira ya jamii husika.
- ✓ Methali zina sifa ya utegemezi na huingiliana na tanzu nyingine za fasihi.
- ✓ Hutumiwa mwishoni mwa ngano kufupisha maadili ya ngano hiyo.
- ✓ Hutumiwa kubuni lakabu, mtu ambaye huwasaliti marafiki anaweza kuitwa ‘kikulacho’ kutokana na methali ‘kikulacho ki nguoni mwako’
- ✓ Hutumiwa katika tanzu za kimaandishi kama vile riwaya na tamthilia ili kuongeza ladha katika usimulizi.
- ✓ Hutumiwa katika mazungumzo ya kawaida na ulumbi kuleta mvuto.
- ✓ Hutumiwa katika nyimbo na mashairi
- ✓ Hutumika katika hotuba rasmi au hata mahakamani mshtakiwa, mlalamishi na mahakimu wanaweza kutoa maoni yao kutumia methali.
- ✓ Hutumika katika kutoa mawaidha

- ✓ Methali huelezea ukweli ambao unakubalika na jamii ambao imebuniwa
- ✓ Tofauti na vitendawili ,methali hazina muktadha maalumu wa kutolewa .hazitengewi vikao vya kutolewa
- ✓ methali ni mali ya jamii, kama tanzu nyingine za faihi simulizi hakuna anayeweza kudai kumiliki methali
- ✓ methali huambatana na mazingira ya jamii iliyozizaa, hulka, itikadi, tamaduni na tajriba zake busara fulani huwasilishwa kutegemea mazingira ya jamii kwa mfano.

Ulingo wa kwake haulindi manda
Kamba ya mbali haifungi kuni
Fimbo ya mbali haiui nyoka

- ✓ methali zina matumizi mapana.methali moja huweza kuwa na majukumu mbalimbali kama vile kuonya, kuelekeza na kufunza.
- ✓ Methali huwa na maana ya ndani na nje, maana ya nje hutokana na maana halisi ya maneno yaliyoiunda. Vilevile, methali hupewa maana ya ndani yenye fumbo lililofumbwa na maneno yanaoiunda.

Majukumu

a) *Huelimisha,* methali hutumiwa kupitisha maarifa ya kijamii kwa wanajami. *Abebwaye hujikaza* huonyesha kuwa unapopata usaidizi nawe pia jikaze kutia bidii, usingoje tu usaidizi.

b) Huadilisha. methali hufunza maadili kama uvumilivu kwa mfano ‘*mstahimilivu hula mbivu*’

c) *Husawiri mitazamo na falsafa za jamii.* Fulani kuhusu masuala mbaliimbali. Je, jamii inapenda nini? Inachukia nini? Methali *ucha mungu si kilemba cheupe* hudhihirisha kuwa jamii huchukia unafiki.

d) *Hutambulisha jamii,* kila jamii ina methali zake maalum zinazoitambulisha.

e) *Huongeza ladha katika mazungumzo na maandili,* mazungumzo na maandishi yenye matumizi mazuri ya methali huvutia.

f) *Hubudisha,* katika jamii nyingine, methali hutengewa vipindi vya kutolewa na makundi yanayoshindana, hii ni njia mojawapo ya kutuliza bongo.

g) *Hurithisha utamaduni wa jamii,* methali ni zao la utamaduni husika na hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine hivyo utamaduni huweza kurithiwa.

h) *Hufariji,* methali huwatuliza na kuwaliwaza watu wanapokabiliana na matukio au hali zinazohuzunisha, kwa mfano hakuna refu lisilo na ncha.

i) *Hukuza uwezo wa kufikiri,* mtu huhitajika afikiri kwa makini na kuoanisha msamiati uliotumika kwa hali ya maisha ili kupata maana.

j) *Hukuza ushirikiano na mshikamano wa jamii.* Katika jamii ambazo methali hutengewa vikao, watu hujumuika pamoja hivyo kukuza ushirikiano na mshikamano.

Uainishaji wa methali

1. **Muktadha**

Ile kuelewa methali, ni muhimu kujua mazingira, tamaduni na hali zilizozizaa methali hizo methali ambazo zimezaliwa katika muktadha au mazingira sawa huweza kuwekwa katika kundi moja.

2. **Maudhui**

Maudhui na fani ndiyo hutawala methali, maudhui katika methali ni mengi na mapana kama zilivyo jamii na shughuli zao, methali ambazo huwa na maudhui sawa huwekwa katika kundi moja, baadhi ya maudhui yanayojitokeza katika methali za Kiswahili ni ya

a) Malezi

i. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe
ii. Samaki mkunje angali mbichi
iii. Asiyefunzwa na mamake hufunzwa na ulimwengu.

b) Kazi

i) Kazi mbi si mchezo mwema.

ii) Mchagua jembe si mkulima.
iii) Kazi ya bakuli husiri.
v) Kazi isiyo faidi kutenda si ada.

III. Ushirikiano

i) Kidole kimoja hakivunji chawa.
ii) Jifya moja haliinjiki chungu.
(iii) Umoja ni nguvu utengano udhaifu.

3. **Mtindo au fani**

Mbali na maudhui, methali hutawaliwa na fani pia. Fani katika methali hudhihirika katika muundo, tamathali za semi na taswira inayoibuliwa, methali ambazo huundwa kwa kutumia fani sawa huweza kuwekwa katika kundi moja. Methali zifuatazo zimeundwa kwa kutumia kweli kinzani

a) Simba mwenda pole ndiye mla nyama.
b) Kuinamako ndiko kuinukako.

4. **Jukumu**

Methali huweza kuanishwa kulingana na majukumu yake. Je, methali inasifu, inakashifu, inahimiza, inaonya ama inafariji? Methali zifuatazo hutumiwa kuonya:

a) Mwenye pupa hadiriki kula tamu.
b) Asiyeangalia huishia ningalijua.
c) Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.

5. **Maana**

a) Methali zote zenye maana sawa huweza kuwekwa katika kundi moja, kwa mfano.

I. Damu ni nzito kuliko maji
i. Meno ya mbwa hayaumani
ii. Mtoto wa nyoka ni nyoka
iii. Mwana wa mhunzi asiposana, huvukuta.

b) Methali zenye maana zinazokinzana pia zinaweza kuainishwa pamoja, kwa mfano. Mvumilivu hula mbivu. Ngoja ngoja huumiza matumbo. Mtu pweke ni uvundo. Nahodha wengi chombo huenda mrama.

Fani katika methali

1. Sitiari

Sitiari ni mbinu ya kulinganisha kitu na kingine bila kutummia maneno ya kulinganisha, methali zinazoundwa kwa sitiari ni pamoja na:

a. ***Mgeni ni kuku mweupe***, hapo mgeni anafananishwa moja kwa moja na kuku mweupe kuonyesha mgeni hutambulika haraka akiwa kundini.
b. ***Ahadi ni deni,*** ahadi inafananishwa na deni kuonyesha kuwa ni sharti mtu kutimiza ahadi.

2. Takriri

Takriri ni mbinu ya kurudiarudia maneno au sauti kwa nia ya kusisitiza methali zenye takriri ni kama vile;

i) Ngoja ngoja huumiza matumbo.
ii) Haba na haba hujaza kibaba.

3. Tashbihi.

Tashbihi ni tamathali ya usemi na inayo linganisha vitu kwa kutumia maneno ya kulinganisha kwa mfano:

i. Kawaida ni *kama* sheria.
ii. Jambo usilolijua ni *kama* usiku wa kiza.

4. Tanakali za sauti

Hizi ni miigo ya sauti zinazotolewa na kitu au zinazotokea tendo linapotendeka methali zinazotumia tanakali za sauti ni kama vile

i. Chururu si ndo ndo ndo!

5. Taswira

Taswira ni picha zinazojengeka akilini mwa mtu baada ya kusoma, kutazama au kusikia maelezo fulani. Taswira hizi hutokana na tajriba pamoja na mazingira ya mtu ifuatayo ni mifano ya methali zinazotumia taswira.

i. Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.
ii. Mpanda farasi wawili hupasuka msamba.

Kweli kinzani

Katika kweli kinzani, maana ya maneno hukinzana kijuujuu (husikika kuwa haiwezekani) lakini ikichunguzwa kwa undani kuna ukweli fulani uliofichika, ifuatayo ni mifano ya

methali zinazotumia ukinzani.

a. Wagombanao ndio wapatanao.
b. Ukipigao ndio ukufunzao.

6. Chuku

Chuku ni mbinu ya kuongezea sifa kitu zaidi ya kilivyo, mifano ya methali zinazotumia mbinu hii ni:

a. Usipoziba ufa utajenga ukuta.
b. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.

7. Taashira au ishara

Katika taashira, kitu kimoja huashiria kingine. Mifano ya methali zenye taashira.

i. Kimya kingi kina mshindo mkuu.
ii. Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.

8. Dhihaka stihizai au kejeli

Hii ni mbinu ya kufanya mzaha au kudharau tabia au mienendo isiyofaa, kwa mfano.

i. Hawi musa kwa kuchukua fimbo.
ii. Ucha mungu si kilemba cheupe.

9. Tashihisi au uhuishaji

Tashihisi ni mbinu ya kukipa kitu sifa za kibinadamu au kitu kisicho hai kupewa sifa za kitu kilicho hai

mfano

i) Adhabu ya kaburi aijuaye ni maiti.
ii) Siri ya mtungi aijuaye kata.

10. Balagha

Maswali yasiyo hitaji majibu maswali haya humchochea mtu kufikiri.

i. Pilipili usiyoila yakuwashiani?
ii. Mavi usoyala wayaingiani kuku?

Methali hizi zimeundwa kwa mbinu ya swali ambalo linamhitaji mwenye kuambiwa kufikiria.

11. Tanakuzi

Hii ni mbinu inayotumia maneno au kauli zinazopingana, katika tanakuzi sehemu moja ya methali huwa na maana inayopingwa na sehemu ya pili.

i) Tamaa mbele mauti nyuma.
ii) Mpanda ngazi hushuka.
iii) Pole pole ya kobe humfikisha mbali.

12. Kinaya

Kinaya ni kinyume cha matarajio au cha hali ilivyo kwa mfano.

i) Kigumba kwa nguruwe kwa mwanadamu ki uchungu.
ii) Kikiharibika cha fundi kikiongoka cha bwana swedi.

Muundo wa methali

Methali kwa kawaida huwa na muundo na wenye sehemu mbili sehemu ya kwanza hudokeza wazo nayo ya pili hulikamilisha mfano.

i) Baada ya shida, mkasa.
ii) Debe shinda, haliachi kutika.
iii) Dawa ya moto, ni moto.

Uchambuzi wa methali

Maswali yafuatayo husaidia kuchambua au kuhakiki methali

a) Methali imerejelea vifaa gani au inahusu nini? K.m Wanyama, binadamu ama vifaa vya nyumbani?
b) Methali imebuniwa kwa kutumia tamathali gani na mbinu gani za kifasihi? k.m uradidi , kinaya, balagha n.k
c) Methali inaibua taswira gani? Methali ‘simba mwenda pole ndiye mla nyama ‘inaibua taswira ya utulivu makini na subira, kwamba ukitaka kufanikiwa ni sharti uwe na subira.
d) Methali inakupa wazo gani kuhusu jamii? Methali *mtu pweke ni uvundo* inaonyesha kuwa jamii husika inachukia utengano.
e) Je, kuna methali nyingine inayokaribiana kimaana au inayopingana na hii?
f) Je, methali imejikita katika mazingira ama muktadha gani? Kwa mfano.
    i) Jogoo wa shamba hawiki mjini (mashambani /mjini)
    ii) Mgaagaa na upwa hali wali mkavu (pwani)
    iii) Ucha mungu si kilemba cheupe (dini)

g) Je, dhamira ya methali yenyewe ni gani? Inanuia kuonya, kushawishi, kufahamisha au kusifu? Kwa mfano ‘mali bila daftari hupotea bila habari’ inaelimisha; *uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti* ina kejeli ilhali ‘hakuna refu lisilokuwa na ncha” inaliwaza.

Vitendawili

Kitendawili ni kauli yenye fumbo ambalo hutolewa kwa hadhira hai ili ilifumbue jibu la kitendawili ndilo fumbo lenyewe.

Sifa

a) Kwa kawaida, vitendawili ni semi fupifupi zinazotumia lugha ya mkato.kwa mfano ’pa’funika ‘pa’funika (jibu; nyayo wakati wa kutembea)
b) Vitendawili hutolewa kwa hadhira ili vifumbuliwe hivyo, hadhira yake ni hai na tendi.
c) Hutumia lugha ya picha au taswira na vina ukwasi wa tamathali za semi.
d) Vitendawili huhitaji watu au makundi mawili ili kukamilisha uwasilishaji wavyo mtu wa kwanza hutega na mwenzake hutegua.
e) Vitendawili huwa na muundo au fumyula maalumu ya uwasilishaji kwa mfano
Mtegaji: kitendawili
Mteguaji: tega!
Mtegaji: nyumba yangu haina mlango
Mteguaji: yai
f) Vitendawili huwasilisha kwa mtindo wa majibizano kati ya mtegaji na mteguaji mteguaji akishindwa kutegua, huhitajika kutoa mji ndipo kupewa jibu na mtegaji
g) Kitendawili ni fumbo au swali liilofichika ambalo huhitaji jibu.
h) Fumbo au jibu la kitendawili hufahamika tu na jamii ambamo kitendawili hicho kimezaliwa, kitendawili kinaweza kuwa na majibu mawili kutegemea mazingira ya jamii kwa mfano,

vitendawili vifuatavyo huweza kuwa na jibu zaidi ya moja.

i) Wanangu wawili husabihiana majibu tui na maziwa; unga na majivu.

iii) Mwarabu kasimama kwa mguu mmoja majibu uyoga; mwavuli.

j) Vitendaili ni sanaa ambayo kwa kiasi kikubwa hutegemea uwezo wa mtu kutambua na kuhusisha au kulinganisha vitu katika mazingira yake, kwa mfano ili kufumbua fumbo la kitendawili mbili mbili hadi pwani, lazima mtu aweze kuhusiaha vitu viwili ambavyo daima hufanya jambo pamoja (jibu macho) macho hutazama pamoja, hulala pamoja na hulia pamoja.

k) Vitendawili huingiliana na tanzu na vipera vingine vya fasihi simuliza kwa mfano ngano za mtanziko hutumia vitendawili, hasa katika fomyula ya ufunguzi wa ngano. Aidha vitendawili hutangulia vikao vya kusimulia hadithi au hutegwa baada ya vikao hivyo.

l) Vitendawili hubadilika kutegemea wakati au kipindi cha kihistoria na maendeleo ya jamii, kitendawili kimoja kinaweza kuundwa au kutolewa kwa maneno tofauti kulingana na kipindi cha wakati kinapotumiwa kwa mfano.

Mwarabu wangu nimemtupa biwini (machicha ya nazi)

Mzungu katupwa jalalani (machicha ya nazi)

maneno tofauti (mwarabu na mzungu) katika vitendawili hivi viwili ambavyo vina jibu moja yanaonyesha viliathiriwa na nyakati tofauti za kihistoria.

m) Vitendawili ni sanaa inayotendwa kwa hivyo hujisimamia yenyewe tofauti na methali ambazo kwa kawaida ni sanaa tegemezi. Hutegewa vikao maalumu na kutolewa.

n) Kimaudhui, vitendawili hushughulikia masuala katika nyanja zote za maisha ya binadamu na

mzingira yake. Maudhui haya hutofautiana katika jamii mbalimbali ingawa baadhi yao huingiliwa

o) Vitendawili vinaweza kuwa sahili (rahisi) na vingine changamano

Vitendawili ni semi maarufu sana miongoni mwa watoto, katika jamii nyingine watoto na watu wazima hushiriki.Miongoni mwa wakamba, kwa mfano watu wazima walishindana kutegua vitendawili hata kuliko watoto.

Umuhimu

a) Vitendawili huelimisha, vitendawili hujumuisha masuala mengi katika mazingira ya jamii.
b) Hali hii inavifanya kuwa na uwezo mkubwa wa kuelimisha watu kuhusu mazingira yao aidha mtu akikosa jibu haadhibiwi zaidi ya kutoa mji.
c) Huburudisha.vitendawili huwapumbaza na kuwapumzisha wanaoshiriki katika utegaji ua utegauaji wavyo.
d) Hufundisha kaida na maadili ya jamii, vitendawili huwa na utaratibu fulani unaofuatwa na ambao washiriki wanapaswa kuuheshimu na kuuzingatia, hii ni njia moja ya kuadilisha kwa kuwa kila jambo maishani lina kaida zake zinazoheshimiwa.
e) Hukuza ubunifu na stadi ya kufikiri haraka, mteguaji wa kitendawili sharti afikiri na kuoanisha yaliyotajwa na mazingira yake ili kupata jawabu.Vitendawili hukuza ari ya kufikiria na kudadisi mazingira.
f) Vitendawili hudhihaki na kukejeli watu, hali au tabia hasi katika jamii.hukashifu matendo hasi na kusifu yale chanya
g) Husawiri mitazamo na itikadi ya jamii kuhusu hulka fulani, kwa mfano *nyumbani kwetu kuna papai lililoiva sana lakini nashindwa kulichuma* (jibu: kaka au dada) inaonyesha kuwa ndoa kati ya dada na kaka hairuhusiwi.
h) Hukuza uwezo wa kukumbuka vitendawili hutumiwa kama chemshabongo ya kujaribu uwezo wa mtu kukumbuka na kuhusisha mambo

i) Huleta umoja na ushirikiano katika jamii, watu hujumuika wakati wa kutegeana vitendawili kwa njia hiyo utangamano huimarika.
j) Hutambulisha jamii kila jamii huwa na vitendawili vinavyoonyesha mazoea, hali, tajriba na mazingira ya jamii husika.
k) Huchochea tabia ya udadisi, uzoefu wa kutafuta kiini cha kitendawili hujenga tabia ya kutaka kufichua jambo lililofichika kwa kujaribu kupata jibu la jambo ktika kitendawili wanajamii huimarisha ari yao kutafiti mambo ili kubaini kiini chake.
l) Vitendawili hukuza na kusambaza ujuzi wa lugha, vitendawili vina ukwasi mkubwa wa lugha na tamathali za semi kwa hivyo ni nyenzo kuu ya kukuza na kusambaza maswala ya lugha katika jamii.

Fani katika vitendawili

Muundo

Kama tulivyotaja awali, vitendawili huwa na fomyula au muundo maalamu wa uwasilishaji.

1. **Kitangulizi ambacho hutolewa na mtegaji.**

Mtegaji: kitendawili

iii) Hadhira humpa ruhusaya kutega. *Mteguaji: tega!*

iv) Mtegaji hutoa kitendawili mtegaji: *Fatuma mchafu*

iv) Jibu hutolewa na mteguaji*: Mteguaji nguruwe (kosa)*

v) Jibu likikosekana mtegaji huomba *mji :Mtegaji :Umenoa*
Nipe mji.

vi) Mteguaji hutoa mji mteguaji :Ninakupa migingo

vii) Mtegaji akipewa mji hutoa jawabu sahihi*: Mtegaji! Niliienda migingo, watu wa migingo wakaniambia nikija niwasalimu.*

Jibu lake ni ufagio

Mtindo

Vitendawili hutolewa kwa mtindo wa majibizano, majibizano haya huwa kati ya mtegaji na mteguaji na

hadhira ya wasikilizaji utaratibu ulioelezwa katika muundo huzingatiwa na mtegaji na mteguaji /hadhira.

Lugha

1. **Sitiari**

Aghalabu, vitendawili hutumia sitiari k.m

i. Fatuma mchafu (ufagio) hapa fatuma ni sitiari ya ufagio.
ii. Saa yetu kadiri inavyotembea ndivyo inavyopunguza nguvu (moyo) saa ni sitiari ya moyo.
iii. Jani la mgomba laniambia habari zinazotoka ulimwenguni kote (gazeti /jarida) jani la mgomba ni sitiari ya gazeti /jarida.

2. Tashihisi /uhuishaji

Wakati mwingine, vitendawili hutumia mbinu inayoipa kitu kisicho hai sia za kibinadamu k.m

i. Akizungumza kila mtu hubabaika (radi) hapa radi imepewa sifa ya kuzungumza kama binadamu sauti kali ya radi huwaogofya binadamu.
ii. Amenifunika kote kwa blanketi lake jeusi (giza) giza limepewa sifa ya binadamu ya kumfunika mwingine.
iii. Daima nasaabisha mafarakano (ukewenza) ukewenza umerejelewa kwa nafsi ya kwanza.

2. Taashira

a. Faiza akiniona ajificha (mzee kobe) kinachoashiriwa na kujificha kwa Faiza ni kobe.
b. Chonge la nyoka huuma walio mbali (ugonjwa) chonge la nyoka linaashiria ugonjwa.

3. Stihizai /dhihaka/kejeli

Vitendawili vinavyobuniwa kwa dhihika hutumiwa kukashifu mienendo hasi katika jamii pia hueleza sifa ya kitu kwa njia ya dharau k.m

i. Akivaa miwani hafanyi kazi vizuri (mlevi) kitendawili hiki kinakashifu ulevi
ii. Babangu amevaa koti la chuma (mzee kobe)
iii. Upara wa mwarabu unafuka moshi (chai ya maziwa)
iv. Uzi mwembamba umefunga dume kubwa (usingizi)

4. **Kweli kinzani**

Vitendawili vya aina hii huundwa kwa hoja mbili zinazopingana k.m

i) Ajenga ingawa hana mikono (ndege) ndege hana mikono kama binadamu hata hivyo hujenga kiota.
ii) Ana meno lakini hayaumi (kichana) meno ya kichana hutumiwa kuchana wala si kuuma.
iii) Hufa ikifufuka (bahari kupwa) maji ya bahari huwa (kutoka ufukweni)na kurejea.

5. Takriri

Kuna vitendawili vinavyoundwa kwa tanakali za sauti .kwa mfano

i) Aliwa yuala,ala aliwa-(papa)
ii) Amezaliwa ali,amekufa ali,na amerudi ali (nywele)
iii) Mama kazaa mtoto kazao mtoto na mtoto kazaa mtoto (kuku na yai)

6. Tanakali za sauti

i) Chubwi'-(jiwe likianguka ndani ya maji)
ii) Prr' mpaka 'makka'- (utelezi)
iii) 'Pa'funua 'pa'funika – (nyayo wakati wa kutembea)

7. Taswira

Baadhi ya vitendawili vimeundwa kwa jinsi ya kuibua taswira au picha mbalimbali.k.m

i) Nimemwona bi kizee akijitwika machicha –(Mvi)
ii) Ameingia shimoni akiwa uchi, akatoka amevaa nguo-(mbegu)

8. Utata

Baadhi y vitendawili huweza kufasiriwa kwa njia zaidi ya moja tunasema kitendawili cha aina hii kina utata. Utata katika vitendawili husababishwa na hali kwamba jibu la kitendawili hutokana na mazingira.watu tofauti huweza kuwa na majibu tofauti kwa kitendawili hicho hicho kutegemea hali ambayo inawazunguka.

Kwa mfano

i) Inachururа inaganda (asali au gundi)
ii) Gari la kila mtu (miguu au jeneza au kifo)

9. Vitendawili vinavyohusiana na methali
    a. Ukichukua mama chukua mtoto –(sagio /jiwe dogo la kusagia linalopitishwa juu ya jiwe kubwa) methali: ukivuta sagio uchukue kabisa na jiwe dogo la kusagia
    b. Mzee amekufa na vyombo vimevunjikavunjika (kifo cha kiongozi husababisha matatizo) methali :mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba

Mfano

a) Ndege wengi baharini (nyota ngani)
i) Taswira
ii) Istiari
b) Natembea shambani – (wembe wa kunyolea ukiwa kichwani
    i) Taswira
    ii) Tashihisi
c) Pambo juu ya jiwe (upara)
    Taswira
    Sitiari
    Dhihaka /stihizai
d) Hulia huku akiunganisa (cherehani)
i) Tashihisi
ii) Taswira
e) Hukopa lakini halipi-(kifo)
    i) Ukinzani
    ii) Tashihisi
    iii) Kinaya
f) Kisiki chetu hakikui (mbilikimo)
    i. Stihizai /kejeli
    ii. Sitiari
    iii. Taswira

Kufanana na kutofanan kwa methali na vitendawili

Methali na vitendawili hufanana kwa vile.

i) Ni tungo fupi
ii) Huwa na maana fiche
iii) Hutumia lugha inayojenga taswira
iv) Huupata maana kulingana na jamii

v) Hufumbata ukweli Fulani wa kijamii
vi) Huweza kutumiwa katika shughuli rasmi kama vile katika maamuzi ya kesi na utoaji hotuba.
vii) Huweza kutekeleza majukumu sawa k.m kuonya kuburudisha au kunoa bongo.

Methali na vitendawili hutofautiana kama ifuatayo.

vitendawili	**methali**
Kimuundo, huwa na fomula mahususi ya uwasilishaji	Haina fomula
Fumbo lake lazima lifumbuliwe pao hapo	Fumbo halifumbuliwi hapo
Huwa maarufu zaidi miongoni mwa watoto	Huwa maarufu miongoni mwa wazee
Hutolewa katika vikao maalum	Si lazima pawe na vikao maalumu
Huwa na hadhira tendi	Si lazima pawe na hadhira tendi
Huwasilishwa na mtegaji na mteguaji	Huwsilishwa na mtu moja tu

Misimu

Misimu ni semi za muda ambazo hubuniwa na kutumiwa katika mazingira maalumu katika kipindi maalumu cha wakati, msimu huitwa pia *simo*. Misimu inaweza kupata mashiko katika jamii na kukubaliwa kama msamiati au semi rasmi za lugha.

Dhima

1. Kutambulisha makundi mbalimbali ya watu
2. Huhifadhi siri za watumiaji
3. Kuibua hisia mbalimbali
4. Hukuza lugha
5. Huhifadhi historia ya jamii.
6. Hutasfidi lugha
7. Hukuza uwezo wa kufikiri au kudadisi
8. Hukuza ushirikiano na utangamano
9. Huondoa urasmi katika mazungumzo

Sifa

a) Misimu ni semi au msamiati ambao huzuka na kutoweka baada ya muda Fulani.
b) Hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano ya makundi fulani k.m kuna misimu ya vijana ya wafanyakazi katika vyombo vya usafiri na hata ya watoto.
c) Hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano yao katika kipindi fulani cha wakati na mahali fulani
d) Ingawa misimu huzuka na kutoweka baada ya muda, baadhi ya misimu hudumu na kukubalika kama semi au msamiati sanifu wa lugha husika kwa mfano neno *chai* (kwa maana ya hongo) lilianza kama msimu, kisha likashika na kukubalika kama msemo sanifu.
e) Msimu hupata maana yake kutoka kwa watumiaji pamoja na muktadha wa mahali na wakati, kwa mfano neno *sare* ni msimu uliopata maana katika sekta ya usafiri wa matatu likimaanisha kubebwa bila malipo.

Uainishaji wa misimu

Misimu hutofautiana kwa kutegemea

a) *Wahusika* – kuna misimu ya vijana, mabaharia au wanafunzi neno *beste* hutumiwa na vijana kumaanisha rafiki
b) *Matilaba* – kuna misimu ya kuendesha biashara neno ‘*kungara* ‘linamaanisha kuvaa nguo inayopendeza na ‘sare’ lina kubebwa kwenye matatu bila kulipa nauli.
c) *Vifaa*- kuna misimu ya vyakula, pesa na vyombo vingine .maneno ‘*nyaki*’ ni nyama na ‘*ashu*’ ni shilingi kumi.
d) *Mahal*i- kila eneo huibua misimu yake.gari la uchukuzi kwa uma nchini Kenya ni ‘matatu na nchini Tanzania ni ‘daladala ‘
e) *Wakati au kipindi* - misimu hubadilika kulingana na wakati au kipindi kwa mfano, wakati wa uchaguzi wa 2002 nchini Kenya kulizuka neon *unbwogable* lililomaanisha wasioshindwa na lika toweka katika muktadha baadaye.

Lakabu

Lakabu ni jina la msimbo au jina la kupanga ambalo mtu

hujibandika ama hubandikwa kutokana na sifa zake za kimaumbile kitabaka, tabia au kimatendo. Aghalabu lakabu huwa neno moja au fungu la maneno lililo na maana fiche au ya kisitiari sifa zinazodokezwa katika lakabu zinaweza kuwa za kusifu, kudhalilisha au kukosoa.

Sifa

a) Lakabu si jina la mtu ni jina tu la kupangwa.
b) Lakabu aghalau huwa neno au fugu la maneno lililo na maana iliyofumbwa.
c) Lakabu huoana na sifa za mhusika inaweza kusifu kukejeli au kufanyia tashtiti tabia hasi ya mhusika lakabu *baba wa taifa* moja kwa moja inaashiria sifa nzuri za mhusika na kumsifu kwa upande mwingine lakabu kama *kangumu* inaashiria tabia ya uchoyo.
d) Lakabu hupatikana katika tanzu na vipera vingine nya fasihi simulizi kama vile sifo, malumbano ya utani na majigambo (vivugo) ambapo wahusika hujipa majina ya kupanga ya kujitapa.
e) Lakabu huundwa kwa lugha ya picha au taswira na sitiari kwa mfano, lakabu ‘nyayo’ ya Raisi mstaafu inatumia sitiari inamfananisha na nyayo za mtu hivyo kutupa taswira ya kujipata kufuata falsafa ya mtu mwingine.
f) Ingawa lakabu si jina halisi la mtu, huweza kudumu na kufanya jina halisi la mtu kusahaulika kwa mfano Sonko.

Umuhimu/dhima

a) Kusifiwa kwa matendo chanya ya mhusika.
b) Hukashifu au kukejeli matendo mabaya ya mhusika.
c) Ni kitambulisho cha mhusika husawiri tabia au hali ya mtu fulani ka maneno machache.
d) Hutumiwa kama ishara ya hesima katika jamii ambamo kumtaja mkazamwana kwa jina lake ni mwiko, baba mkwe huibua lakabu ya kumrejelea mkazamwanawe.
e) Hutumiwa na baadhi ya wahusika kuficha utambulisho wao baadhi ya waandishi hujibandika majina ya uandishi ili kuficha majina yao halisi.

f) Hutumiwa na wahusika kujigamba na kujinaki katika majigambo, anayejigamba hujipa lakabu ili kujinaki na kuonyesh ubingwa wake.
g) Hutumiwa kuhifadhi siri wakati mwingine watu humpa mtu fulani lakabu ili wanapomrejelea isijulikane ni nani.
h) Hukuza uhusiano bora hasa miongoni mwa watani katika kutaniana watu huweza kubandikana majina.
i) Hutumiwa kuondoa urasmi katika mahusiano ya kijamii.

Vitanza ndimi

Vitanza ndimi ni kauli au sentensi zenye maneno ambayo yana mfuatano wa sauti zinazotatanisha kimatamshi.Vitanza ndimi huundwa kwa maneno yenye sauti zinazokaribiana sana kimatamshi kimsingi, katika jamii nyingi za kiafrika watu hufurahia kucheza na maneno kama njia ya burudani. Watoto kwa mfano, wana mazoea ya kucheza na maneno na sauti katika michezo na nyimbo zao

Sifa

a) Kimsingi, vitanza ndimi ni mchezo wa maneno na sauti.
b) Huundwa kwa maneno ambayo yana sauti zinazokaribiana kimatamshi maneno haya huweza kuwa na maana nyingi au yenye kukabiriana kimaana.
c) Ukinzani wa maneno kisauti na kimaana huyafanya matamshi ya maneno kuutatiza ulimi.

Mifano ya vitanza ndimi

i) Wataita wataita wataita taita.
ii) Waite wale wana wa liwali wale wali wa liwali.
iii) Cha mkufuu mwanafuu ha, akila hu, cha mwanafuu hu, akila ha.

Dhima

a) Vitanza ndimi hukuza matamshi bora mtu anapotamka kwa haraka na kwa usahihi, hutia makali stadi zake za kimatamshi. Kupitia hali hii uzoefu wa kutamka vyema hujengwa.

b) Hukuza uwezo wa kufikiri kwa haraka, baadhi ya vitanza ndimi hutatanisha kuwaza haraka ili kuteua neno sahihi la kutamka.
c) Kuburudisha, kimsingi vitanza ndimi vilinuiwa kuibua ucheshi na kuchangamsha hadhira.
d) Hukuza ubunifu, anayebuni vitanza ndimi anahitaji kuwa na ujuzi mpana wa lugha na ubunifu ili kuteua maneno yanayokaribiana kimatamshi na kimaana.
e) Hukuza lugha, vitanza ndimi vilivyobuniwa katika vipindi mbalimbali huhifadhiwa na kupitishwa kwa vizazi vijavyo kama malighafi katika kipera cha vitanza ndimi.
f) Huhifadhi utamaduni na kuurithisha, maarifa ya kipera cha vitanza ndimi yasingehifadhiwa na kurithishwa kama vipera vingine vya fasihi simulizi, tusingevisoma leo.
g) Ni kitambulisho cha jamii, vitanza ndimi huakisi mazoea ya jamii husika kila jamii ina vitanza ndimi vyake mahususi.
h) Hujenga uhusiano bora wa kirafiki, ucheshi unaoibuliwa na vitanza ndimi hujenga uhusiano bora miongoni mwa washiriki.

Mafumbo na chemshabonga

Mafumbo ni kauli zenye maana iliyojificha, mafumbo hutumia lugha fiche au ya kiistiari pamoja na tamathali nyingine za usemi. Humtaka anayeambiwa kudadisi mazingira yake na kufikiria ili kupata maana, mafumbo huchemsha bongo za wale wanaoshiriki katika kuyafumbua ingawa vitendawili ni aina za fumbo tunadai kwamba mafumbo kwa kawaida ni semi ndefu kuliko vitendawili. Kuna mafumbo yaitwayo chemshabongo, chemshabongo ni maswali ambayo humtaka mtu kutumia akili na ujuzi kuyajibu. Maswali mengi ya aina hii ni ya kimapokeo, mengine hubuniwa na msemaji ili kukidhi mahitaji ya hadhira mahususi. Baadhi ya chemshabongo kwa hakika ni hesabu tu nyingine hutolewa kwa mraba unahitaji kujazwa

Mfano

Nina kilo moja ya mchanga na kilo moja ya pamba kipi

kizito zaidi, mchanga au pamba?
Jibu: vyote vina uzito sawa kwa vile uzito wavyo ni sawa (kilo moja)

Sifa

a) Ni semi zinazofumba jambo.
b) Huhitaji mtu kuwaza ili aweze kubuni fumbo lenyewe.
c) Shughuli, maumbile au vitu vilivyo katika mazingira ya jamii kama vile mifugo, njia za usafiri na nyenzo za biashara vinaweza kufumbiwa.
d) Baadhi ya mafumbo hufananisha kitu kilichotajwa katika fumbo na mazingira halisi.
e) Baadhi ya mafumbo huwa marefu na mengine huwa mafupi.
f) Mafumbo huhitaji mantiki ili kuyatmbua. Mfano nina chui mbuzi na majani ya kuliwa na mbuzi je nitafanya aje ili nivuke ngambo ile …

Dhima /umuhimu

a) Hukuza uwezo na wepesi wa kufikiri ili kufumbua fumbo ni lazima mtu afikiri kwa makini na wakati mwingine kwa upesi.
b) Hustawisha ubunifu fumbo hufumbuliwa kwa kuoanisha yaliyomo katika fumbo, tajiriba na mazingira hivyo mtu hutumia kiwango fulani cha ubunifu ili kupata maana aidha shughuli ya kufumbua huhitaji watu kuwa wabunifu.
c) Hukuza maarifa ya kukabiliana na changamoto na kutumia mantiki kusuluhisha mambo.

Nahau

Nahau ni fungu la maneno ya kawaida lenye maana ambayo haitokani moja kwa moja na maana za maneno yaliyoziunda, nahau **piga kalamu** si kuchapa kalamu bali ni ‘kufuta mtu kazi’
Mifano mingine ni.
Piga maji- Lewa.
Kujitia hamnazo – Kujifanya hujui.
Kukata kamba- Kufa.
Kunja jamvi- Maliza shughuli.
Kwenda nguu- Kukata tama.

Piga vijembe- Kusema kwa mafumbo.
Kumwaga unga- Kuachishwa kazi.
Ndege mbaya- Bahati mbaya.
Kupata jiko- Kuoa.
Shingo upande- Bila kutaka.

Sifa za nahau

a) Nahau huundwa kwa lugha ya mkato iliyo na ujumbe mzito wa mafumbo k.m kidudu mtu-mfitini.
b) Nahau mbili au zaidi zinaweza kuwa na maana moja k.m jamvi la wageni/bao la mkahawani –kahaba.
c) Nahau moja inaweza kuwa na maana zaidi ya moja k.m kushika mguu-kuomba radhi /kutoa shukrani kupiga mbio.
d) Maneno katika nahau hupoteza sifa zake za kawaida na kuchukua maana nyingine iliyo tofauti kabisa .k.m kula chumvi –kuwa mzee.
e) Nahau huundwa kwa maneno mawili au zaidi kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa-danganya.
f) Bega kwa bega pamoja.
g) Nahau huweza kuundwa kwa mitindo mbalimbali au kwa maneno ya kategoria mbambali k.m
    i. Kitenzi na nomino –piga chuku, andika meza
    ii. Kitenzi na kitezi-kufa kupona,pata shika
    iii. Kitenzi na kielezi –jikaza kisabuni, kufa kikondoo
    iv. Noino na nomino-askari kanzu, domo kaya
    v. Nomino na kitenzi-mguu haumshiki, damu kumkauka.
    vi. Nomino na vivumishi –nyoat njema, ndege mbaya

Dhima ya nahahu

a) Nahau hukuza lugha, nahau huyapa maneno maana tofauti na maana ya kawaida kwa njia hii hupanua msamiati wa lugha.
b) Nahau huipa lugha, badala ya kutumia maneno yaliyozoeleka, nahau hutumiwa kukoleza ladha ya lugha.
c) Nahau pia hutumiwa kupunguza ukali wa jambo linalorejelewa k.m jicho la nje-uasherati.

d) Nahau huweza kutumika pia kuhifadhi siri ili wanatengwa wasielewe, si watu wote wanaoelewa maana ya nahau zote.

Misemo

Misemo ni semi ambazo zinabeba ukweli wa kijumla, hutumika kueleza mambo mbalimbali yanayokubali ukweli huo. Misemo hutumiwa kutoa ujumbe kwa muhtasari mfano zaidi.

i. *Binadamu ni udongo* –kumaanisha binadamu aliumbwa kwa udongo na hufa na kurudi udongoni.

ii. *Mwili haujengwi kwa mbao*-mtu lazima ale ili apate kujenga mwili au kunenepa hauwezi kujengwa kwa mbao.

iii. *Umaskini si kilema*-kumaanisha kuwa mambo hubadilika ukizaliwa katika umaskini si lazima uishi na ufe ukiwa maskini.

iv. *Lila na fila havitangamani* –ubaya na wema hayaendi pamoja.

v. *Ndio kwanza mkoka ualike maua* –kumaanisha ndio mambo yamezidi kushika kasi.

vi. *Mgomba haupandwi changaraweni ukamea* –jambo njema halifanywi mahali pabaya likapendeza.

Baadhi ya misemo hutumiwa kama methali kwa mfano, umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

UKUSANYAJI NA UHIFADHI WA FASIHI SIMULIZI

Utangulizi.

Sifa za fasihi simulizi ni kwamba huzaliwa hukua, huishi na huweza kufa. Kadiri jamii inavyobadilika, fasihi simulizi inabadilika na kuathiiriwa na maendeleo ya binadamu kisayansi, kijamii na kiteknolojia.Vipera vipya vya fasihi simulizi huzaliwa kutokana na athari za utandawazi, hukuzwa na kupewa uhai katika mazingira mapya aidha vipera vya zamani k.m matambiko na ngomezi huweza kufa au kupewa sura mpya. Hivyo kuna umuhimu wa kuhifadhi tanzu za fasihi simulizi ili zisipotee lakini kabla ya kuzihifadhi ni lazima kwanza zikusanywe ukusanyaji wa data ya fasihi simulizi hufanywa ili kuendeleza na kutekeleza malengo muhimu yanayokusudiwa na

anayekusanya.
Mkusanyaji apaswa kufuata hatua zifuatazo;

a) Kujiadaa – hapa mtu anatakiwa kuzingatia
   - Mada ya utafiti –anatafiti kuhusu nini?
   - Mawanda ya utafiti – Kama ni kitendawili anatafiti fani? Aina?
   - Walengwa – jamii ipi? Wenye umri gani?
   - Kipindi cha utafiti – utaanza na kutarajia kumaliza lini?
   - Kuomba kibali cha utafiti kutoka kwa taasisi husika k.v wizara ya elimu
   - Mbinu za ukusanyaji na kuhifadhi data, je atatumia: Hojaji au mahojiano je, vifaa hivi vi tayari?
   - Gharama ya utafiti –je, atatumia kiasi gani cha pesa? Nani atafadhili utafiti?

b) Utafiti na ukusanyaji wa data –mtafiti anaweza kukusanya data kupitia hojaji, mahojiano, kushiriki au kutazama.
c) Rekodi ya data –kuna njia mbalimbali za kurekodi data basi vifaa hivi sharti viwen tayari kabla ya utafiti.
d) Kuchunguza upana wa data/maelezo yaliyotolewa na walengwa na kuyanakili ili kuyachunganua baadaye.
e) Uchanganuzi na kufasiri wa data –huchanganuliwa kulingana na vigezo vya uchanganuzi alivyoweka na kulingana na mada yake. Matokeo hutumiwa kutoa hitimisho na mapendekezo kuhusu mada ya utafiti.

Ukusanyaji wa kazi za fasihi simulizi

Kwa vile sifa za fasihi simulizi hutegemea jamii Fulani, sio vyema kulinganisha fasihi ya jamii moja na sanaa ya jamii nyingine.
Ni vyema mkusanyaji kuchunguza ili aelewe umbo, thamani na dhima ya fasihi hiyo. Njia mbalimbali za kukusanya fasihi simulizi ni:

1. **Kusikiliza**

Mkusanyaji anaweza kusikiliza wasanii katika jamii fulani wakitamba, kusimulia au kuimba tungo zao

2. **Kushiriki**

Mkusanyaji aweza kujiunga na jamii kwa kushiriki katika ngoma, soga na masimulizi ya hadithi na tanzu nyingine hapa anayekusanya data ya fasihi simulizi haulizi bali hujirekodia anachokibaini katika ushirika huo.

Umuhimu wa kushiriki

a) Mtafiti huja karibu zaidi na jamii na hupata habari za kuaminika moja kwa moja
b) Ni njia bora ya kukusanya habari kwa watu wasiojua kusoma na kuandika ama wanaona vigumu kujieleza moja kwa moja.
c) Ni rahisi kwa mtafiti kuuliza maswali kuhusu kipera kinachowasilishwa mathalani anaweza kuuliza kuhusu kipidi ambamo wimbo fulani uliimbwa au hadhira mahususi ambayo ilitambiwa aina fulani ya ngano.
d) Mtafiti huweza kunakili anayosikia au kuona, hivyo kuhifadhi sifa za kiimbo, toni na ishara.
e) Mtafiti hupata taathira na hisia halisi ya yanayowasilishwa kwani anakabiliana wazi na watendaji halisi huelewa zaidi.
f) Mtafiti huweza kuthibitisha aliyokusanya kwa hojaji au mahojiano kwa kuyahakiki
g) Kusiriki hukuza utangamano kati ya mtafiti na wanajamii.ni rahisi kwa mtafiti kupata majibu ya masuala anayotafiti kwa kushiriki na kutangamana na wanajamii.

Udhaifu wa kushiriki

a) Huchukua muda mrefu kulingana na njia nyinginezo kama vile hojaji au mahojiano.
b) Mtafiti huweza kutekwa na yaliomo akasahau kurekodi.
c) Ugeni wa mtafiti huweza kuleta wasiwasi miongoni mwa washiriki wakakosa kufanya kama kawaida.
d) Uchanganuzi wa data ikusanywayo kwa njia hii ni ngumu, lakini rahisi kwa mtafiti kuacha maswala muhimu. Ni njia ghali ya utafiti kwani inamhitaji mtafiti kusafiri mbali ili kushiriki katika utendaji pia vifaa vya kuhifadhia data yenyewe kama vile kanda za

video huwa ghali na nguvu za umeme huenda zikakosa.

3. Kurekodi

Mkusanyaji anaweza kusikilizana na wasanii na kuwarekodi katika vinasa sauti, kanda za video filamu au kuwapiga picha .

4. Kutazama

Mkusanyaji anaweza kushuhudia kwa macho fasihi fulani ikiendelezwa hapo atashuhudia mwenyewe bila kushiriki baadaye anaweza kuandika ili kuhifadhi.Mbinu hii hutumika zaidi katika utafiti wa maigizo.

Umuhimu wa utazamaji

a) Ni rahisi kwa mtafiti kurekodi kwani hashiriki utendaji
b) Mafiti hupata habari za kutegemewa zaidi hasa anapotumia kinasasauti kurekodi moja kwa moja.
c) Mtafiti anaweza kukaa mahali asipoonekana na kushuhudia utendaji halisi hivyo utendaji hautaathiriwa k.m kuwa na wasiwasi kwa ugeni wa mtafiti.

Udhaifu wa utazamaji

Wanajamii wanaweza kumshuku mtafiti kuwa anawapeleleza hivyo kusitisha uwasilishaji wao.

5. Kutumia hojaji

Ni fomu yenye maswali yaliyochapishwa ili kukusanya habari fulani huandaliwa na mkusanyaji wa data na kutumwa au kupelekwa kwa mhojiwa au atakayejaza hojaji ni za aina mbili.

a) Hojaji funge

Humfunga mhojiwa kwa majibu fulani tu kila swali huwa na orodha ya majibu na mhojiwa huhitajika kuweka alama tu kwa lile analoona kuwa jibu sahihi

b) Hojaji wazi/huru

Aina hii ya hojaji huwa na maswali ambayo yanahitaji majibu ya maelezo mhojiwa hutoa maoni yake.

Sifa za hojaji

a) Hojaji huwa na maswali yanayojibiwa na kikundi lengwa mtafiti anaweza kulenga watambaji ngano au

walumbi

b) Huweza kutumiwa moja kwa moja na mkusanyaji kwa anyehojiwa hivyo mtafiti humwelekeza mhojiwa namna ya kujibu.
c) Hojji huweza kutumwa kwa mhojiwa bila kuwepo kwa mtafiti. Mhojiwa husoma na kujaza hojaji bila mwongozo wa mtafiti (aina hii ndiyo iliyozoeleka zaidi)

Umuhimu wa hojaji

a) Huwa na gharama ya chini zaidi.
b) Mtafiti huweza kusikia iidadi kubwa ya watoaji habarikwa kipindi kifupi kwani huweza kutumiwa kwa posta.
c) Huweza kutumika katika mahojiano kama mwongozo.
d) Humpa mhojiwa muda wa kuwaza na kuchunguza.
e) Kwa kawaida , hojaji hazina athari za mtafiti kwani aghalabu mtafiti hayupo zinapojazwa .Huweza kubadilishwa kulingana na kiwango cha wajazaji au wahojiwa.

Udhaifu wa hojaji

a) Maswali yenye utata husababisha fasiri mbalimbali zifanyazo mategemeo yasitegemeke.
b) Huenda watu wakakosa kuijaza hojaji kwa kikamilifu kwa sababu mbalimbali kama vile kuhofia lawama au wakakataa kujaza kabisa.
c) Hojaji ndefu huenda baadhi ya watu wakakataa kuijaza.
d) Hojaji wazi huwa ngumu sana kwa mtafiti kuchanganua data, uchanganuzi huchukua muda mrefu.
e) Huenda wahojiwa wasijaze mambo ya kweli, si rahisi kwa mtafiti kuthibitisha kama habari zilizojazwa ni kweli.
f) Wahojiwa wanaweza kuchelewa kutuma hojaji zao, hasa zinazotumwa kwa posta.
g) Baadhi ya wazee, japo wana habari za kutegemewa, hawajui kusoma na kuandika hivyo hawawezi kujaza

hojaji isipokuwa waanaposaidiwa na watafiti.

h) Kwa vile mtafiti hakabiliani na mhojiwa ana kwa ana, hawezi kupata sifa za uwasilishaji wa vipera vya fasihi simulizi kama vile toni na kidatu.

6. Mahojiano

Mkusanyaji hakabiliana ana kwa ana na watu anaonuia kupata maarifa kutoka kwao. Mkusanyaji atakuwa ameandaa maswali atakayouliza katika kikao rasmi mkusanyaji pia anaweza kushiriki mahojiano yasiyo rasmi bila kunakili majibu papo hapo, maelezo huweza kuhifadhiwa katika kanda ya kunasa sauti.

Umuhimu wa mahojiano

a) Kwa vile mtafiti anatazama ana kwa ana na mhojiwa ni rahisi kupata habari za kina na kutegemeka.
b) Mbinu za uwasilishaji k.m toni, ishara za uso na kiimbo hubainika kwa mtafiti hivyo kuimarisha uelewa wake.
c) Mtafiti anaweza kumfafanulia mhojiwa maswali na kumwezesha kupata data ya kuaminika zaidi.
d) Kwa vile mtafiti anamhoji mlengwa moja kwa moja anaweza kurekodi majibu ya mhojiwa moja kwa moja au kuyaandika, si rahisi kupotea.
e) Mtafiti huweza kubadilisha mtindo wa kuhoji kulingana na kiwango cha elimu cha mhojiwa, ili kupata majibu bora zaidi.

Udhaifu wa mahojiano.

a) Mahojiano yanahitaji stadi za mawasiliano za kiwango cha juu ikiwa mtafiti hana hizi stadi huenda akaathiri majibu ya mhojiwa.
b) Urasmi unaotokana na vikao vya mahojiano huenda ukatatiza mawasiliano kati ya mhoji na mhojiwa.
c) Ukosefu wa muda wa kutosha wa mahojiano, mahojiano huchukua muda mrefu na huenda mtafiti akakosa kupata muda kumhoji huenda asimwamini mtafiti ahisi kuwa anapelelezwa na kukataa kutoa habari.

d) Kiwango cha elimu cha mtafiti huenda kikawahajisha na kuwatia wahojiwa hisia za unyonge na kuwafanya kutoa habari za zisizotegemewa.
e) Wahojiwa wengine huenda wakampa mtafiti habari za uongo ili kumfurahisha.
f) Matatizo ya kutafsiri, ikiwa data imeandikwa kwa lugha tofauti huenda yakaathiri mahojiano.
g) Mahojiano ni njia ghali ya kutafiti kutokana na gharama ya usafiri kwenda nyanjani.

Vifaa vya kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi.

Ukusanyaji wa fasihi simulizi huhitaji vifaa vya kuhifadhi ujumbe; vifaa hivi ni pamoja na

i) Kalamu na karatasi (maandishi)

Mkusanyaji wa data ya fasihi simulizi anaweza kutazama au kushiriki na baadaye akaandika aliyoyashuhudia aidha anaweza kuandika wakati maelezo, masimuulizi au sanaa yenyewe inapoendelezwa iwapo anatazama. Hata hivyo vifaa hivi vya kukusanya fasihi simulizi vina udhaifu.

Umuhimu wa maandishi.

a. Data kama vile hadithi, huhifadhiwa kama ilivyotambwa hivyo si rahisi kusahauliwa mashairi na ngano nyingi zimeandikwa vitabuni.
b. Huweza kufikia vizazi vingi kwani maandishi hudumu.
c. Si ghali kama baadhi ya mbinu nyinginezo k.m video
d. Si rahisi kufisidiwa au kupotea, hasa zikiandikwa katika vitabu hadithi, methali na vitendawili vingi vimehifadhiwa hivi.

Udhaifu wa maandishi

a) Kuna mambo k.m kiimbo, toni, ishara, hisia na mapigo ya mziki ambayo hayawezi kuandikwa kama yalivyowasilishwa na fanani, hivyo hupotea.
b) Aidha, kwa vile maandishi si hai, hayawezi kutenda wala kusema ule uhai hasilia wa fasihi simulizi hufifishwa na kupotezwa na maandishi
c) Baadhi ya watafiti huenda wakandika yale ambayo wanahitaji kwa wakati mahususi na kupuuza mengine k.m ikiwa mada yake ni ‘wahusika katika ngano za kimapokeo’ huenda akajihusisha na wahusika na

kupuuza vipengele vingine k.m fanani haya huipunja fasihi simulizi

d) Kuandika fasihi simulizi huifanya kukosa ile taathira asilia kwani kunaipokonya hadhira yake ile fursa ya kushirikiana ana kwa ana na fanani, mtu hawezi kuuliza jambo
e) Kuandika fasihi simulizi huidhibiti na kupunguza hadhira yake na kuathiri vibaya usambazaji wake fasihi inapoandikwa inawafikia wale tu wanajua kusoma

iii) Vinasasauti /tepurekoda

Vinasasauti hupata sauti,toni na mahadhi ya tungo za fashi simulizi.Vinaweza kutumiwa katika mahojiano au mtu anaposhiriki au kutazama fasihi simulizi ikiigizwa ingawa ni bora kuliko kalamu na karatasi, pia haiwezi kurekodi matendo na miondoko ya wasanii.

Umuhimu wa vinasasauti

a. Sauti ya mhojiwa /fanani huweza kuhifadhiwa.
b. Sifa ya uhai wa fasihi simulizi huhifadhiwa kwani kinasasauti hunasa sifa kama vile za kidatu,toni na kiimbo cha mtambaji.
c. Mkusanyaji wa fasihi simulizi anaweza kurudia kusikiliza uwasilishaji au mahojiano iwapo hakuelewa .sifa hii haipatikani katika maandishi.

Udhaifu wa vinasasauti /tepurekodi.

a) Kinasasauti huhitaji nguvu za umeme au betri hivyo hakiwezi kutumiwa katika sehemu zisizo na huduma hizi aidha nguvu za umeme zikikosekana kabla ya utafiti kukamilka utafiti utaathirika. Mtafiti atalazimika kuanza utafiti wake.
b) Kinasasauti hakiwezi kumnasa mtambaji wala uigizaji wake, watu wanaotumia kazi iliyorekodiwa basi hukosa ile taathira ambayo inaibuliwa na kukabiliana ana kwa ana na mtambaji.

iv) Baadhi ya wahojiwa au mfanani wasitambe ikiwa wanajua kuwa wanarekodiwa, mtafiti anaweza kupata data ya kutegemewa kama alivyotarajia kuipata.

v) Kamera

Kamera huweza kunasa picha zinazoonyesha kipengele kimoja tu bila kuonyesha misogeo au miondoko wala sauti hata hivyo, kamera huweza kuonyesha maleba .

vi) Video

Video zinaweza kuchukua picha na pia kunasa sauti na miondoko ni njia nzuri ya kukusanya fasihi simulizi isipokuwa ni ghali.

vii) Sinema au filamu

Filamu pia huonyesha picha za miondoko na sauti kama video kama ilivyo katika video, filamu huwa ghali

Umuhimu

a) Filamu na video hunasa picha na sauti ,hivyo kuhifahi uigizaji, ishara na kiimbo
b) Uhalisi wa mandhari ambamo kazi ya kifasihi inajikita huonekana na watumizi wa kazi iliyohifadhiwa kwa filamu au video
c) Huipa fasihi simulizi uhai na taathira zaidi kuliko kazi zilizohifadhiwa kwa maandisi, kamera na kinasasauti

Udhaifu wa filamu na video

a) Ni njia ghali ya kuhifadhi data
b) Data hii huweza kufisidiwa, hivyo kutofaidi waliolegwa njia nyingine za kisasa ambazo hutumiwa kuhifadhia na kuendeleza fasihi simulizi ni;
   i. Diski za kompyuta: mdaki, diski mweko (hard disk), kadi simaki (memory card) kadiwia/mkamimo(flash disk)
   ii. Magazeti k.m hadithi huandikwa mara nyingine gazetini.
   iii. Michezo ya kuigiza inayopeperushwa moja kwa moja kupitia runinga na redio na mashirika ya uigizaji
   iv. Tamasha za muziki zinazofanywa shuleni kila mwaka.

Umuhimu wa kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi.

a) Fasihi simulizi ni hifadhi ya mitazamo ya kitamaduni ya jamii, ukusanyaji utampa mwanafunzi wa fasihi simulizi fursa ya kuingiliana na jamii iliyozaa fasihi husika ili kuweza kuielewa nyema.

b) Ukusanyaji humpa mwanafunzi wa fasihi simulizi nafasi ya kushuhudia na kuathiriwa moja kwa moja na utendaji wa fasihi simulizi hivyo mwanafunzi huona vipengele hai vya fasihi simulizi k.m uigizaji na hivyo kuielewa kwa kina.
c) Husaidia kurekodi na kuhifadhi tamaduni za jamii na kuzipitisha kwa vizazi vijavyo.
d) Ukusanyaji huiendeleza fasihi simulizi, kwa kurekodi vipera kama ngano, hekiya, historia na mtazamo wa kijumla wa jamii kuhusu maisha huhifadhiwa na kupitishwa
e) Husaidia kuziba pengo la utafiti lililopo, tanzu nyingi za fasihi simulizi hazijafanyiwa utafiti wa kutosha ili kuzihifadhi ukusanyaji utasaidia kuziba pengo hili.
f) Hutumika kama msingi wa uchunguzi wa kiulinganishi wa fasihi simulizi za jamii mbalimbali k.m muundo wa utambaji ngano katika jamii mbalimbali.
g) Ili kuelewa ni kwa nini kwa mfano, utungo mmoja wa fasihi simulizi ukawasilishwa kwa njia tofauti katika muktadha tofauti/jambo hili huwawezesha watafiti na wasomi kuelewa sifa za tungo za fasihi.
h) Utafiti wa fasihi simulizi huwezesha mwanafunzi kupata maarifa au stadi za kufanya utafiti katika taaluma nyingine k.m sosholojia.
i) Husaidia kurekebisha mawazo potovu kuhusu fasihi simulizi k.m kujua ni tanzu gani zilizokuwa za awali kabisa. Umewawezesha wasomi kutambua kuwa tungo nyingi zilizoandikwa zilitokana na simulizi za tungo za fasihi simulizi k.m riwaya, hadithi fupi na novella.

Matatizo yanayomkabili mkusanyaji wa fasihi simulizi

a) Gharama ya utafiti, huenda ikawa kubwa kiasi cha mtafiti kutoimudu huenda akakosa pesa za kusafiri au kununua vifaa.
b) Mtazamo hasi wa wanajamii kuhusu ujazaji wa hojaji huenda ukawafanya wengi wao kutojaza hojaji hizo.
c) Wanajamii wengine huweza kushuku kwamba mtafiti anawapeleleza na wakakatoa kutoa habari.

d) Baadhi ya mafanani au wahojiwa huenda wakadai walipwe kabla ya kutoa habari zozote.
e) Mbinu nyingine k.m hojaji huhitaji watu wanaojua kusoma na kuandika ikiwa watu wanaohojiwa hawajui kusoma na kuandika matokeo ya utafiti huenda yasiwe ya kutegemewa.
f) Vizingiti vya kidini .hutokea pale ambapo wahojiwa wanaamini kuwa matendo ya fasihi simulizi k.m matambika ni kinyume cha dini hivyo kukataa kuhojiwa.
g) Kupotea au kufisidiwa kwa vifaa vya kuhifadhia data, yote yaliyohifadhiwa kwayo pia hupotea.
h) Uchache wa wazee au wataalamu wa fasihi simulizi, fasihi simulizi ilikwa maarufu miongoni mwa wazee na hivyo kukosekana kwao hutatiza ukusanyaji
i) Vikwazo kutoka kwa watawala, huenda watawala wakakataa kutoa idhini ya kufanya utafiti baadhi ya taasisi fadhili pia huenda zikakataa kudhamini utafiti.
j) Wadhamini mara nyingi ndio huamua mambo yanayochunguza, mahali pa kuchunguziwa na mawanda au upeo wa uchunguzi la sivyo, mapendekezo hufutiliwa mbali.
k) Huenda mtafiti asiwe na muda wa kutosha kuwahoji watu wengi, basi hatapata habari za kutosha kuhusu mada husika.
l) Matatizo ya mawasiliano na uchukuzi k.m katika kuenda katika sehemu zilizo kama, bila uchukuzi au vyombo vya usafiri.
m) Matatizo ya kibinafsi, mtafiti anaweza kushindwa kuidhibiti hadhira badala ya kuwauliza maswali, mhojiwa ndio huweza kumuuliza mtafiti maswali pia kutojua lugha husika huwa tatizo
n) Ukosefu wa usalama huenda mtafiti akavamiwa aidha baadhi ya watu si karimu na huenda wakamshuku mtafiti ua kumvamia.
o) Tafsiri za data pia ni tatizo fasihi simulizi huendelezwa kwa lugha za kijamii kupata msamiati unaofaa kufasiri lugha chanzi hadi lugha pokezi ni tatizo.

MASWALI YA UDURUSU

1. Ainisha vipera vya fasihi za simulizi
2. Tofautisha kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi
3. Fafanua umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii ya sasa
4. Linganisha methali na vitendawili
5. Eleza namna ya kuainisha nyimbo
6. Eleza umuhimu wa mawaidha miongoni mwa vijana katika jamii
7. Eleza istilahi zifuatazo
    Ayari
    Simo
    Nyiso
    Mbolezi
    Mbazi
    Lakabu
8. Tofautisha kati ya misemo, nahau misimu huku ukitoa mifano mwafaka
9. Fafanua mambo ya kuzingatia unapoainisha methali
10. Maigizo ni nini?
20. Taja vipera vyovyote viwili vya maigizo
21. Eleza dhima zozote tano za maigizo
22. Jadili njia zinazotumiwa na kizazi cha sasa kuendeleza utanzu huu.
23. Fafanua sifa **nne** za maigizo.
24. Maghani ni nini ?
25. Fafanua aina tano za maghani
26. Eleza majukumu manne ya maghani.
27. Eleza vikwazo mbalimbali vya ukuaji wa fasihi simulizi.
28. Eleza tofauti **mbili** kati ya misimu na misemo katika fasihi simulizi.
29. Eleza maana ya ngomezi.
30. Fafanua sifa zozote tano za ngomezi.

MATUMIZI YA LUGHA

Kiimbo

⇒ Jinsi sauti inavyopanda na kushuka mtu anapoongea.

⇒ Huibua maana halisi ya maneno yanayosemwa kama ifuatavyo:

- Sentensi za taarifa

✓ Mtoto anaandika barua.

- Sentensi za maswali

✓ Mtoto anaandika barua?

- Sentensi za mshangao

✓ Mtoto anaandika barua!

- Sentensi za amri

✓ Kachezeeni nje!

- Sentensi za rai/ombi

✓ Nisaidi**e/eni**.

Zoezi

a) Eleza maana ya kiimbo kwa kutoa mifano.
b) Tambua sentensi zifuatazo ni za aina gani kutokana na kiimbo.

i) Watu wanakula nyoka?
ii) Watu wanakula nyoka.
iii) Watu wanakula nyoka.
iv) Tafadhali nisaidie.

Silabi

⇒ Tamko moja katika neno/herufi moja au zaidi ambazo hutamkwa pamoja.

Miundo Miwili ya Silabi za Kiswahili

- **Silabi wazi**

⇒ Huishia kwa irabu k.m. o-**a**, (I) i-**ga** (KI), **mbu**-zi (KKI) na u-**ngwa** (KKKI)

- **Silabi funge**

⇒ Huishia kwa konsonanti k.m. **m**-tu (K)

Zoezi

a) Ukitoa mifano, fafanua miundo miwili ya silabi za Kiswahili.
b) Tenganisha silabi katika maneno yafuatayo:
i) inkisari
ii) baiskeli.

Shadda/Mkazo

⇒ Mkazo unaowekwa kwenye silabi fulani ya neno ikiwa imetamkwa kwa msisitizo.
⇒ Alama ya ritifaa hutumiwa kutambulisha shadda.
⇒ Huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka ya mwisho, kwenye vitenzi vishirikishi vya silabi moja au kubadilisha maana ya neno.
✓ ka’lamu, I’mba, thu’mni, ‘leta, n.k.
✓ Kitabu ‘ki mezani.
✓ Bara’bara (njia), ba’rabara (sawasawa), wala’kini (lakini), wa’lakini (kasoro/dosari/ila)

Zoezi

a) Weka shada katika maneno haya:

i) imba

ii) baba

b) Onyesha kwa kupiga mstari iliko shada katika maneno yafuatayo:

i) malaika

ii) nge

Sauti za Kiswahili

⇒ Kuna makundi mawili ya sauti za kiswahili:

a) Irabu

⇒ Sauti ambazo hutamkwa kwa ulaini bila hewa kuzuiliwa katika ala za sauti.

b) Konsonanti

⇒ Sauti ambazo wakati wa kutamkwa hewa huzuiliwa katika ala za sauti.

- **Aina za Ala za Sauti**


a) Ala tuli

⇒ Ambazo hazisogei mtu akitamka k.m. meno, ufizi, kaa kaa gumu, kaa kaa laini na koo/koromeo.

b) Ala sogezi

⇒ Ambazo husogea mtu akitamka k.m. midomo na ulimi.

Matamshi/Uainishaji wa Irabu



a)

b) a ni ya katikati na chini kinywani na midomo ikiwa imeviringa.

c) e ni ya mbele na kati kinywani na midomo ikiwa imetandazwa.

d) i ni ya mbele na juu kinywani na midomo ikiwa imetandazwa.

e) o ni ya nyuma na kati kinywani na midomo ikiwa imeviringa.
f) u ni ya nyuma na juu kinywani na midomo ikiwa imeviringa.

Zoezi

a) Taja makundi mawili ya sauti za Kiswahili.
b) Yatofautishe makundi ya sauti za Kiswahili uliyotaja katika (a)
c) Toa mifano miwili miwili ya irabu ambazo hutamkwa:
   i) midomo ikiwa imeviringa
   ii) midomo ikiwa imetandazwa
d) Eleza jinsi irabu /e/ inavyotamkwa.
e) Taja aina mbili za ala za kutamkia na utoe mfano mfano mmoja mmoja.

Matamshi/Uainishaji wa Konsonanti

MAHALI AINA	MIDOMO	MDOMO MENO	MENO	UFIZI	KAAKAA GUMU	KAAKAA LAINI	KOROMEO
VIPASUO (H) (GH)	p b			t d		k g	
VIPASUO (GH) KWAMIZO (H)					ch j		
NAZALI (GH) (VING’ONG’O)	m			n	ny	ng'	
VIKWAMIZO (H) (VIKWARUZO)(GH)		f v	th dh	s z	sh	gh	h
KITAMBAZA				l			
KIMADENDE				r			

NUSU IRABU VIYEYUSHO	w				y		

⇒ Huainishwa kulingana na inapotamkiwa, kuwepo au kutokuwepo kwa mtetemeko katika nyuzi za sauti na jinsi hewa inavyozuiliwa katika ala k.m. /p/ ni ya midomo, kipasuo na sighuna.

- **Vipasuo**

⇒ Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa, huzuiliwa kabisa na kuachiliwa kwa ghafla na mpasuko mdogo kutokea.

- **Vikwamizo/Vikwaruzo**

⇒ Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa hewa hupitishwa katikati ya ala kwa kukwamizwa.

- **Vipasuo kwamizo/kwaruzo**

⇒ Konsonanti ambayo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa nje kwa nguvu, huzuiliwa kabisa halafu mwanya mdogo huachwa hewa ipite kwa kukwamizwa.

- **Nazali/Ving’ong’o**

⇒ Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa kuna kiasi cha hewa huachiliwa na kupitia puani

- **Kitambaza**

⇒ Konsonanti ambayo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa kwa nguvu, kuzuiliwa na kuachiliwa ipite kando ya ulimi

- **Kimadende**

⇒ Konsonanti ambayo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa, kuzuiliwa na kuachiliwa na kusababisha ncha ya ulimi kupigapiga ufizi mfululizo.

- **Nusu irabu/Viyeyusho**

⇒ Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa hewa hupitishwa katikati ya ala kwa ulaini kama katika utamkaji wa irabu.

Zoezi

a) Tambua kikwamizo cha kaakaa laini na kiyeyusho cha midomo.

b) Tambua konsonanti ambazo si za orodha hii na ueleze kwa nini: /m/, /n/, /ny/,/ng’/, /f/, /b/

c) Tofautisha konsonanti /p/ na /dh/.
d) Taja konsonanti mbilimbili ambazo hujulikana kama:
   i) viyeyusho
   ii) vikwaruzo

Aina za Maneno

Nomino (N)

⇒ Neno linalotaja kiumbe, kitu, hali, mahali, tendo, dhana, n.k.

Aina

- **Nomino za Pekee**

⇒ Ambazo hutaja kitu kwa kutumia jina lake/ambazo hutambulisha upekee wa kitu hicho.
⇒ Mwanzoni huandikwa kwa herufi kubwa.
✓ majina ya watu k.m. **K**amau
✓ mahali k.m. **M**ombasa
✓ siku k.m. **A**lhamisi
✓ miezi k.m. **D**isemba
✓ miaka k.m. 1930
✓ milima k.m. **K**ilimanjaro
✓ Mito k.m. **T**ana
✓ maziwa k.m. **V**ictoria
✓ bahari k.m. **H**indi
✓ Mabara k.m. **A**frica

- **Nomono za Kawaida/Jumla**

⇒ Majina ya jumla ya viumbe/vitu vinavyoonyesha umbile la jinsi moja k.m. mtu, gari, kalamu, n.k.

- **Nomino za Jamii**

⇒ Majina ya makundi ya viumbe au vitu k.m. bunge, jamii, halaiki, bunda n.k.

- **Nomino za Wingi**

⇒ Majina ya vitu vitokeavyo kwa wingi japo kimsingi hazina umoja au wingi k.m. maji, mate, maziwa, mahubiri, marashi, mchanga, ngeu, poda, unga, n.k.

- **Nomino za Dhahania**

⇒ Majina ya viumbe au mambo ya kudhani/yasiyoweza kugusika k.m. k.m ujinga, werevu, malaika, shetani, amani, imani, roho, wazo, dhana, n.k.

- **Nomino za Vitenzi Jina**

⇒ Vitenzi vyenye kiambishi awali **ku** ambavyo huweza pia kutumika kama nomino k.m. **Kucheza** kwake kunaudhi.

Zoezi

1. Sahihisha jedwali lifuatalo

nomino	aina
Juma kisu mazi wa bunda amani kuomba	wingi dhahania pekee kitenzi jina kawaida/ jumla wingi

a) **Kuendesha baiskeli** kwa **kasi** kulimfanya **Hasani** aangushe **bunda** la noti alilokuwa anaenda kununulia **mchanga**.

Sentensi ya Kiswahili

⇒ Sentensi ni fungu la maneno linalojitosheleza kimaana linalotumiwa katika mawasiliano.

Sifa

a) Huwa na ujumbe uliokamilika.
b) Huwa na mpangilio maalum wa maneno.
c) Huwa na muundo wa kiima na kiarifu.

Aina

- **Sentensi Sahili**

⇒ Sentensi rahisi au nyepesi.

Sifa

a) Huwa fupi.
b) Huwa na kitenzi kimoja pekee.
c) Huwasilisha dhana moja.
d) Yaweza kuwa ya neno moja au zaidi.
e) Yaweza kuwa na kiima kilichododoshwa.

✓ Wataenda.
✓ Watoto wawili wanaelekea uwanjani.
✓ Gachiku ni msichana mtiifu.

- **Sentensi Ambatano**

⇒ Inayoundwa kwa kuunganisha sentensi sahili mbili.

Sifa

a) Huwa na vishazi huru viwili.
b) Huwa na kiunganishi.
c) Huwa na vitenzi viwili au zaidi.
d) Hutoa zaidi ya wazo moja.
e) Yaweza kuwa na viima vilivyododoshwa.

✓ Mwanafunzi alipita mtihani ingawa hakuwa anasoma kwa bidii.
✓ Maria aliendelea kupika kwa utaratibu huku akiimba wimbo.

- **Sentensi Changamano**

⇒ Ambayo huwa na kishazi tegemezi kilichochopekwa ndani.

Sifa

a) Huwa na kishazi tegemezi chenye kitenzi kinachovumisha nomino kwa kuirejelea.
b) Huwa na kishazi huru kimoja au zaidi.
c) Huwa na virejeshi (amba na O) au –enye.

✓ Tunda alilonunua jana limeoza.
✓ Mwizi aliiba pesa zilizokuwa kabatini.

Kundi Nomino (KN) na Kundi Tenzi (KT)

- Kundi Nomino ni sehemu katika sentensi inayoarifu kuhusu nomino na hutokea mwanzoni mwa sentensi.
- Kundi tenzi ni sehemu katika sentensi inayoarifu kuhusu kitenzi na hutokea mwishoni mwa sentensi.

Virai

⇒ Vikundi vya maneno vitumiwavyo na binadamu visivyo na maana kamili.
⇒ Tungo zinayoundwa kwa maneno aghalabu mawili au zaidi yanayoashiria kitu kimoja na inayojengwa juu ya neno kuu.

Aina

- **Kirai Nomino (Kn)**
  a) W
  b) N
  c) N+U+N
  d) N+N+U+N
  e) N+$\bar{S}$
- **Kirai Kitenzi**
  a)T
  b) T+E
  c)T+N
  d) T+N+T
  e)TS+T
  f) t+N
  g) t+V+E
- **Kirai Kivumishi(Kv)**
  a)V+E
  b) V+U+V+E
  c)V+V+U+V+E
  d) V+N+V+E
- **Kirai kielezi (Ke)/Chagizo**

a)E
b) E+E
c)E+E+E...

- **Kirai Kihusishi (Kh)**

a)H+N
b) H+N+V
c)H+N+V+E

Zoezi

Bainisha virai katika sentensi ifuatayo

a) Mzazi na watoto wawili werevu sana waliwasili shuleni leo asubuhi kabla ya mwalimu.

Vishazi

⇒ Kundi la maneno lenye kiima na kiarifu likiwa ndani ya sentensi kuu.

Aina

- **Vishazi Huru**

⇒ Vifungu vya maneno katika sentensi ambavyo hutoa maana kamili.

- **Vishazi Tegemezi**

⇒ Vifungu vya maneno katika sentensi ambavyo havitoi maana kamili.

Aina

a) Vishazi tegemezi vya viunganishi k.m. Alimwadhibu **ingawa hakuwa na makosa**.
b) Vishazi tegemezi vya virejeshi k.m. Polisi walimpata mtoto **aliyekuwa amepotea**.

- **Vishazi Viambatani**

⇒ Vinavyoundwa kwa vishazi huru viwili vikiwa vimeunganishwa k.m. **Baba analala** na **mama anapika**.

Zoezi

Bainisha Vishazi Katika Sentensi Zifuatazo

a) Mwalimu amewasili.
b) Amina ambaye ni daktari atakuja.
c) Ametajirika japo hakupata elimu.
d) Mwalimu anafundisha na wanafunzi wanaandika.
e) Tumeanzisha shirika ili tunyanyue hali zetu.
f) Unaweza kuamua kunyamaza au kujitetea.

Shamirisho/Yambwa

Aina

- **Shamirisho Kipozi/Yambwa Tendwa**

⇒ Nomino inayoathiriwa na kitenzi.

- **Shamirisho Kitondo/Yambwa Tendewa**

⇒ Nomino inayotendewa kitendo.

- **Shamirisho Ala/Yambwa Kitumizi**

⇒ Chombo kinatumiwa kufanyia kitendo fulani.

Mifano

✓ Mama alimpikia **baba chakula** kwa **sufuria**.
✓ **Baba** alipikiwa **chakula** na mama kwa **sufuria**.
✓ **Sufuria** ilitumiwa na **mama** kumpikia **baba chakula**.

a) Chakula (Shamirisho Kipozi/Yambwa Tendwa)
b) Baba (Shamirisho Kitondo/Yambwa atendewa)
c) Sufuria (Shamirisho Ala/Yambwa Kitumizi)

Ngeli za Nomino

⇒ Makundi ya nomino katika lugha ya Kiswahili yenye sifa zinazofanana kisarufi.

- **A-WA**

⇒ Huwa na majina ya watu, vilema, viumbe, vyeo na viumbe vya kiroho, n.k.
⇒ Huchukua miundo kama vile M-WA, M-MI, KI-VI, n.k.
✓ mtu-watu,
✓ mkulima-wakulima
✓ mtume-mitume
✓ mkizi-mikizi
✓ kiwete-viwete
✓ kibyongo-vibyongo
✓ nabii-manabii
✓ kuku-kuku
✓ Waziri-Mawaziri

- **U-I**

⇒ Huwa na majina ya mimea, sehemu za mwili, vifaa, matendo, maumbile, n.k.
⇒ Huchukua muundo wa **M-MI**.
✓ Mchungwa-michungwa
✓ Mkoko-mikoko
✓ mkono-mikono
✓ mfupa-mifupa

✓ msumari-misumari
✓ mgomo-migomo
✓ mwendo-myendo
✓ msukosuko-misukosuko
✓ mlima-milima
✓ mwamba-myamba

- **U-YA**

⇒ Huwa na majina ya hali, matendo, n.k.
⇒ Huchukua muundo wa U-MA.
✓ Ugonjwa-magonjwa
✓ upana-mapana
✓ uasi-maasi
✓ uchungu-machungu
✓ ulezi-malezi
✓ uovu-maovu
✓ uhusiano-mahusiano

- **YA-YA**

⇒ Huchukua muundo wa MA-MA.
⇒ Huwa na nomino zipatikanazo kwa wingi.
⇒ Hazibadiliki katika umoja na wingi.
✓ manukato
✓ mauti
✓ maziwa
✓ marashi
✓ mahubiri
✓ majira
✓ maradhi
✓ maafa
✓ mazingira

- **KI-VI**

⇒ Ni majina ya vifaa, sehemu za mwili, vitu, udogo, lugha, n.k.
⇒ Huchukua miundo KI-VI na CH-VY.
✓ kisu-visu
✓ kitabu-vitabu
✓ chakula-vyakula
✓ chanda-vyanda
✓ kijitu-vijitu

✓ kigombe-vigombe
✓ kiguu-viguu
✓ kidovu-vidovu

- **LI-YA**

⇒ Huwa na majina ya sehemu za mwili, dhana, vifaa, ukubwa, n.k.
⇒ Huchukua muundo wa JI-MA, JI-ME, JA-MA, JE-MA n.k.
✓ jicho-macho
✓ jina-majina
✓ jitu-majitu
✓ goma-magoma
✓ jambo-mambo
✓ janga-majanga
✓ jembe-majembe
✓ jeneza-majeneza
✓ wazo-mawazo
✓ tunda-matunda
✓ jua-majua
✓ ziwa-maziwa
✓ ua-maua

- **I-I**

⇒ Huwa na nomino dhahania na vitu visivyoweza kuhesabika.
⇒ Hazibadiliki katika umoja na wingi.
✓ sukari
✓ amani
✓ chai
✓ mvua
✓ Imani
✓ chumvi
✓ subira
✓ imani
✓ amani
✓ furaha

- **I-ZI**

⇒ Huhusisha nomino dhahania na vitu.
⇒ Hazibadiliki katika umoja na wingi.
✓ nyumba

✓ baiskeli
✓ karatasi
✓ redio
✓ meza
✓ dini
✓ dawa
✓ ndizi
✓ jozi

- **U-ZI**

⇒ Huchukua miundo W-NY, U-NY, U-F, n.k.
✓ wayo-nyayo
✓ wakati-nyakati
✓ uso-nyuso
✓ ufa-nyufa
✓ ufunguo-funguo
✓ ufagio-fagio
✓ wembe-nyembe
✓ uwanja-nyanja
✓ ujumbe-jumbe
✓ ukoo-koo
✓ waraka-nyaraka
✓ waya-nyaya

- **U-U**

⇒ Huwa na nomino za dhahania na vitu visivyoweza kuhesabika.
⇒ Hazibadiliki kimaumbo.
✓ Huchukua U au W.
✓ Ujinga
✓ Ulafi
✓ Ulaji
✓ Werevu
✓ Unga
✓ Uji
✓ Ugali
✓ udongo

- **KU**

⇒ Nomino zinazoundwa kutokana na vitenzi k.m. **kuomba** kwake kumemsaidia.

- **PAKUMU**

⇒ Ngeli ya mahali.
⇒ Huwa na nomino moja ‘mahali’.
a) PA (mahali karibu au panapodhihirika) k.m. Kitabu ki**po** **pa**le.
b) KU (mahali mbali au kusikodhihirika) k.m. Mahali **ku**le **ku**nafaa.
c) MU (ndani ya) k.m. Mahali **m**le **m**na siafu.

Zoezi

a) Tunga sentensi ukitumia nomino kutoka katika ngeli ya U-ZI.
b) Andika kwa wingi. Makaribisho aliyopewa yalimfurahisha.
c) Andika katika ukubwa wingi: Paka mweupe amenaswa mguuni.
d) Andika katika wingi wa hali ya udogo: Mtu aliumwa na mbwa.
e) Huku ukitoa mifano, fafanua miundo mitatu ya majina katika ngeli ya LI-YA.
f) Tambua ngeli/viwakilishi ngeli vya nomino zifuatazo:
   i) chakula
   ii) shairi
   iii) mtwana

Uundaji wa maneno

- **Nomino kutokana na mzizi wa kitenzi**

a) danganya-kudanganya, mdanganyifu,udanganyifu
b) soma-kusoma, masomo,msomi,usomaji
c) unda-kuunda, muundaji,uundaji,muundo
d) funika-kufunika, kifuniko, mfunikaji, ufunikaji

- **Kitenzi kutokana na mzizi wa nomino**

a) mlo-kula
b) mlevi-kulewa, kulevuka
c) mwimbaji-kuimba
d) fikra-kufikiri
e) malezi-kulea

f) fumbo-kufumba, kufumbua

- **Nomino kutokana na mzizi wa nomino**

a) mwimbaji-kuimba, wimbo, uimbaji, kiimbo
b) mchezo-kucheza, uchezaji, mchezaji
c) ulaghai-kulaghai, mlaghai
d) hesabu-kuhesabu,uhesabu
e) mdhalimu- kudhulumu, dhuluma, udhalimu

- **Nomino kutokana na mzizi wa kivumishi**

a) -refu-mrefu, urefu, urefushaji
b) -baya-mbaya, ubaya
c) -zuri-mzuri, uzuri
d) -kali-mkali, ukali
e) -eupe-mweupe,weupe

- **Kivumishi kutokana na mzizi wa nomino**

a) ujinga -jinga
b) werevu -erevu
c) mzuri -zuri
d) mpumbavu -pumbavu
e) mpyoro -pyoro

- **Kitenzi kutokana na mzizi wa kivumishi**

a) haramu-kuharamisha, kuharamika
b) halali-kuhalalisha, kuhalalika
c) -fupi-kufupisha, kufupika
d) bora-kuboresha, kuboreka
e) -refu-kurefusha, kurefuka
f) sahihi-kusahihisha, kusahihika
g) -sikivu-kusikia
h) -danganyifu-kudanganya

- **Kivumishi kutokana na mzizi wa kitenzi**

a) dunisha - duni
b) Haramisha - haramu
c) fupisha -fupi
d) sahilisha -sahili
e) tukuka -tukufu
f) fahamu -fahamivu
g) teua -teule
h) nyamaza -nyamavu

i) ongoka -ongofu
j) sahihisha -sahihi
k) danganya -danganyifu

- **Kitenzi kutokana na kielezi**

a) haraka-harakisha
b) zaidi-zidisha
c) bidii-bidiisha
d) hima-himiza

Zoezi

a) Unda neno ulilopewa katika mabano kutokana na maneno yafuatayo:
   i) zingatia (kivumishi)
   ii) sahili (kitenzi)
   iii) taliki (nomino)
b) Unda nomino kutokana na mizizi ya maneno yafuatayo kisha utunge sentensi.
   i) -kali
   ii) lia

Vitenzi

⇒ Kitenzi ni neno linaloeleza kuhusu jambo linalofanywa.

Aina za Vitenzi

- **Kitenzi halisi**

⇒ Kinachofahamisha tendo halisi.
⇒ Hutokea peke yake k.m. Boke **anacheza** mpira.

- **Kitenzi kikuu (T)**

⇒ Kinachoeleza tendo kuu katika sentensi.
⇒ Hutokea pamoja na kitenzi kisaidizi k.m. Baba anataka **kulala**.

- **Kitenzi Kisaidizi (Ts)**

⇒ Kinachosaidia kitenzi kikuu

Maneno yanayoweza kutumiwa kama vitenzi visaidizi

✓ ngali
✓ kuwa
✓ taka
✓ pasa
✓ bidi
✓ huenda

✓ kuja
✓ weza
✓ kwisha
✓ stahili
✓ wahi
✓ maliza

▪ **Vitenzi Sambamba**

⇒ Vinavyofuatana moja kwa moja/vinavyotokea kwa mfululizo.
⇒ Hutumika kutoa maelezo kuhusu tendo moja maalum kwa uwazi zaidi.
✓ Wachezaji **huenda wanaweza kushinda** mchezo wa leo.

▪ **Vitenzi Vishirikishi (t)**

⇒ Vinavyoshirikisha vitu kihali, kitabia au kimazingira.

Aina

a) **Vitenzi Vishirikishi Vikamilifu**

⇒ Ambavyo huchukua viambishi.
✓ Mama **alikuwa** mgonjwa/jikoni/muuguzi.
✓ Aisha **angali** kitandani/mkaidi/ mwanafunzi.

b) **Vitenzi Vishirikishi Vipunguvu**

⇒ Ambavyo havichukui viambishi

kuyakinisha	kukanusha
ni/niko	si/siko
ndiko	siko
yuko	hayuko
li/liko	hali/haliko

Viwakilishi (W) na Vivumishi (V)

☟ Viwakilishi ni viambishi au maneno yanayotumiwa badala ya nomino.
☟ Vivumishi ni maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu nomino.

VIVUMISHI	VIWAKILISHI
Viulizi	**Viulizi**
☟ Maneno ya kuulizia. ☟ Mizizi ni **–pi**, **-ngapi** na **gani**. ✓ Amechukua kitabu	✓ **Kipi** kimepotea? (**W. Kiulizi**) ✓ Amenunuliwa

<table>
<tr><td>kipi?(V. kiulizi)</td><td>mangapi?
✓ Gani imefungwa?</td></tr>
<tr><td>a-unganifu</td><td>a-unganifu</td></tr>
<tr><td>☟ Maneno yanayoundwa kwa viwakilishi ngeli na kiishio a.
☟ Hutoa maana ya umilikaji
✓ Mtoto wa shangazi amelala. (V. a-unganifu)</td><td>✓ Wa Juma analia. (W. a-unganifu)
✓ Cha mlevi huliwa na mgema.</td></tr>
<tr><td>Vimilikishi</td><td>Vimilikishi</td></tr>
<tr><td>☟ Hutoa maana ya umilikaji.
Mizizi<table><tr><td>nafsi</td><td>kuyakinisha</td><td>kukanusha</td></tr><tr><td>1
2
3</td><td>-angu
-ako
-ake</td><td>-etu
-enu
-ao</td></tr></table>✓ Kiatu changu kimepotea. (V. kimilikishi).</td><td>✓ Usichukue chake. (W. kimilikishi)</td></tr>
<tr><td>Sifa</td><td>Sifa</td></tr>
<tr><td>☟ Maneno ya kusifu au kueleza jinsi nomino ilivyo k.m. -fupi, -baya, -kali, -dogo, n.k.
✓ Mti mrefu umeanguka. (V. sifa)</td><td>✓ Alichukua cheupe. (W. Sifa)</td></tr>
<tr><td>Vionyeshi/viashiria</td><td>Vionyeshi/ viashiria</td></tr>
<tr><td>☟ Maneno ya kuonyesha nomino ilipo.
☟ Huwa za karibu, wastani na mbali k.m. hili, hilo, lile.</td><td>Hii ni ya nani? (W. kionyeshi/kiashiria)</td></tr>
</table>

✓ Kiatu **hiki** kimechafuka. (**V. kionyeshi/kiashiria**)	
Viashiria visisitizi	**Viashiria visisitizi**
☟ Maneno ya kutilia mkazo nomino yakizingatia ilipo. ☟ Huwa ya karibu, wastani na mbali. ☟ Huundwa kwa kutumia kiwakilishi ngeli katika kionyeshi cha kwanza k.m. **ki**ki hiki-**vi**vi-hivi, lili hili-**ya**ya haya, n.k. ✓ Chumvi **ii hii** ilimwagika. (**V. kisisitizi**)	✓ **Kuku huku** ndiko kulinyesha. (**W. kisisitizi**)
Virejeshi	**Virejeshi**
☟ Hurejelea nomino au kukumbusha kuihusu. ☟ Huwa amba- na -o-rejeshi. ✓ Mtoto **ambaye** analala ni wake. ✓ Watoto wana**o**lala ni wao. (V. kirejeshi) ✓ Mnyama **ambaye hu**windwa ni nguruwe. ✓ Mnyama awindwa**ye** ni nguruwe.	✓ **Amba**ye aliniibia ninamjua. ✓ Ali**ye**niibia ninamjua. ✓ **Amba**ye hula nyasi ni ng’ombe. ✓ Ala**ye** nyasi ni ng’ombe.
Idadi	**idadi**
☟ Hutaja idadi ya nomino **Aina** a) **Idadi halisi** (iliyo dhahiri) k.m. -moja, sita, n.k. b) **Idadi ya jumla (**isiyo	✓ Nipe **kumi na kimoja**. (**V. idadi halisi**). ✓ Amechukua **machache** tu. (**V. idadi ya**

dhahiri) k.m. -chache, -kadha –ingi, n.k. ✓ Mwalimu **mmoja** na wanafunzi **sita** wameenda. (**V-idadi halisi**) ✓ Vitabu **vichache** vimechukuliwa na watoto **kadha**. (**V. idadi ya jumla**)	**jumla**)
Pekee	**Pekee**
☟ Hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino kwa njia ya pekee. a) –**enye** (u**milikaji)** ✓ Msichana **mwenye** maringo ni yule. (**V. Pekee**) b) –**enyewe** (h**alisi** au **kusisitiza)** ✓ Barua **yenyewe** niliipeleka posta. c) –**ote** (**bila kubakisha)** ✓ Chakula **chote** kimeliwa. d) **-o-ote (bila kubagua)** Mtu **yeyote** anaweza kuugua. e) **-ingine** (s**ehemu ya baadhi ya vitu)** ✓ Mikufu **mingine** imeibwa. f) -ingine-o (m**bali na/zaidi ya)** ✓ Nyuzi **nyinginezo** zilikatika.	✓ **Mwenye** macho haambiwi tazama. (**W.pekee**) ✓ **Yenyewe** yaliiva jana. ✓ Kiliharibika **chote**. ✓ **Popote** paliposafishwa pamechafuka. ✓ Ametorokea **kwingine**. ✓ **Nyingineyo** niliweka katika chakula.
Nomino/majina	
⇒ Nomino/majina ambayo	

hutumika kama vivumishi ✓ Mtu **mzee** hutembea kwa mkongojo. (**V. jina/nomino**)	
	Ngeli
	Viwakilishi ngeli ambavyo huwakilisha nomino k.m. **Li**liiva jana-**Ya**liiva jana.
	Nafsi
	⇒ Maneno au viambishi vinavyotajia nafsi. **Aina** **a)Nafsi huru** ⇒ Maneno ya kutajia nafsi. naf si / umo ja / wingi 1 2 3 / Mimi Wewe yeye / Sisi Nyinyi wao ✓ **Yeye** ni mtiifu. (**W. nafsi huru**) **b) Nafsi tegemezi/viambata** ⇒ Viambishi ambavyo hutaja nafsi.

	naf si / umo ja / win gi 1 / ni / tu 2 / u / m 3 / a / wa ✓ **Wa**lisahau kumwambia. (**W. nafsi tegemezi**)

Vielezi (E)

⇒ Viambishi au maneno yanayoeleza zaidi kuhusu kivumishi, kitenzi au kielezi kingine.

✓ Yeye ni mweupe **sana/ajabu/kwelikweli/kupindukia/pepepe**.

✓ Alikula **pole pole sana**.

Aina

a) **Vielezi vya Namna/Jinsi**

⇒ Ambavyo hueleza **vile** jambo lilifanyika.

Aina

▪ **Vielezi namna mfanano**

⇒ Vinavyoeleza vile jambo lilifanyika kwa kufananisha na nomino au vivumishi.

⇒ Huchukua viambishi **KI** na **VI**.

✓ Anakula **ki**fisi.

✓ Tulifanya kazi **vi**zuri.

▪ **Vielezi namna viigizi**

⇒ Maneno ambayo kiasili ni vielezi k.m. sana, haraka, ghafla, mno, kabisa, pole, barabara n.k.

✓ Mwenda **pole** hajikwai.

▪ **Vielezi namna hali**

⇒ Hueleza hali ya tendo.

✓ Alilelewa **kwa shida**.

✓ Alilewa **chakari**

▪ **Vielezi namna vikariri**

⇒ Huelezea vile jambo lilifanyika kwa kurudiwarudiwa

✓ Alinijibu **kimzahamzaha.**
✓ Tembea **polepole.**
✓ Yeye hufanya kazi yake **hivi hivi/ovyo ovyo**
✓ Mbwa alibweka **bwe! Bwe! Bwe**!
▪ **Vielezi namna ala**
✓ Walimpiga Stephano **mawe/kwa mawe.**
▪ **Vielezi Namna Viigizi**
⇒ Hueleza vile kitendo kilitendeka kwa kutumia tanakali.
✓ Mbuni alianguka majini **chubwi!**
b)**Vielezi vya Idadi/Kiasi**
⇒ Maneno ambayo hutaja kitendo kimetendeka mara ngapi.
Aina
▪ **Vielezi vya idadi halisi**
✓ Tulivamiwa **mara moja.**
▪ **Vielezi vya idadi ya jumla**
✓ Alitoroka **mara kadha/nyingi/chache.**
c)Vielezi vya mahali
⇒ Hutaja mahali kitendo kilitendekea.
Aina
▪ **Vielezi vya mahali vya maneno kamili**
✓ Ndege ilipofika **Nairobi**, ilitua **chini**.
▪ **Vielezi vya mahali vya aina ya viambishi**
⇒ Ni viambishi **po, ko, mo na ni.**
✓ Ali**po**lala palikuwa na siafu.
✓ Wanacheza uwanja**ni.**
d) Vielezi vya wakati
⇒ Hutaja kitendo kililifanyika wakati gani**.**
Aina
▪ **Vielezi vya wakati vya maneno kamili**
✓ Rais atawasili **kesho/mwaka ujao.**
▪ **Kielezi cha wakati cha kiambishi (po** ya wakati)
✓ Nililala nili**po**fika nyumbani
Viunganishi (U)
⇒ Neno au fungu la maneno la kuunganishia.
Aina
▪ **Vya kujumuisha pamoja**
✓ na

✓ aidha (pia)
✓ isitoshe
✓ kadhalika (pia))
✓ tena
✓ mbali na
✓ fauka ya (zaidi ya)

▪ **Vya kukatiza ili kupambanua**

✓ walakini (lakini)
✓ bali (lakini)
✓ ijapokuwa (hata kama)
✓ ingawa (hata kama)

▪ **Vya kuonyesha kinyume cha mambo**

✓ ilhali
✓ licha ya

▪ **Kuonyesha masharti**

✓ budi (lazima)
✓ lazima
✓ sharti
✓ ikiwa (kama)
✓ bidi

▪ **Vya sababu**

✓ kwa
✓ kwa sababu
✓ maadamu (kwa kuwa)
✓ madhali (kwa kuwa)
✓ kwa vile/maana
✓ kwa ajili/minajili ya
✓ mintaarafu (kutokana na)

▪ **Vya kuonyesha Chaguo**

✓ au
✓ ama
✓ wala

▪ **Viunganishi vingine na maana zake**

✓ ila (isipokuwa)
✓ laiti (kama)
✓ lau (kama)
✓ mradi (bora)

✓ angalau (bora zaidi)
✓ bighairi (bila ya kujali) k.m.**Minghairi** vitu vilivyo kwenye kabati vinginevyo unaweza kuvichukua.
✓ seuze/sembuse (kulinganisha ili kuonyesha tofauti)
✓ labda (pengine)

Vihusishi (H)

⇒ Maneno yanayoonyesha uhusiano.

Aina

▪ **Mahali**
✓ juu ya, miongoni mwa, katika, mpaka, hadi
▪ **Wakati**
✓ kabla ya, baada ya, tangu, hadi, mpaka
▪ **Sababu**
✓ kwa, kwani, kwa sababu, mintaarafu ya
▪ **Ala**
✓ Alimkata **kwa** kisu.
▪ **A-unganifu**
✓ Simu **ya** rununu inalia.
✓ Jumba **la** mikutano limeandaliwa.
✓ Kiatu **cha** ngozi hudumu.
✓ Kikome **cha** plastiki ni duni.
▪ **Ulinganisho**
✓ Zaidi ya, kuliko, kuzidi, kushinda.
▪ **Kiwango**
✓ Zaidi ya, kati ya, takriban, karibu
▪ **Vya hali**
✓ Mithili ya, kwa niaba ya

Vihisishi (I)

⇒ Maneno yanayotoa hisia za moyoni.

a) furaha
✓ Hoyee! Haleluya! Alhamdulilahi!
b) hasira
✓ Kefle! Ah! He!
c) majuto
✓ Kumbe! Jamani! Ole wangu! Laiti
d) huzuni/huruma
✓ Pole! Ole! Maskini!

e) kuitikia
✓ Bee! Labela! Naam! Ehee! Ahaa!
f) mshangao/mshtuko
✓ Eti! Salaale! Ajabu! Msalia mtume! Lahaula!
g) kubeza
✓ Mawe! Ngo! Mmm! Mwangalie!
h) kusisitiza
✓ Hata
i) kutakia heri
✓ inshallah

Mwingiliano wa Maneno

⇒ Hali ya maneno kuwa na matumizi tofauti mifano:

- **W kuwa V**

✓ **Huyu** analia.
✓ Mtoto **huyu** analia.

- **V kuwa W**

✓ Vikombe **vizur**i vitavunjika.
✓ **Vizuri** vitaliwa.

- **V kuwa N**

✓ Mti **mrefu** haupandiki.
✓ **Mrefu** alikufa jana jioni.

- **V kuwa E**

✓ Viatu **vibaya** vitachomwa.
✓ Uliifanya kazi **vibaya.**
✓ Mtu **mjinga** ni huyu.
✓ Anaongea **kijinga.**

- **N kuwa V**

✓ **Tajiri** alimdharau Razaro.
✓ Mtu **tajiri** huheshimiwa.

- **N kuwa E**

✓ **Nairobi** ni mji mkuu.
✓ Amewasili **Nairobi.**
✓ **Kitoto** kinalia.
✓ Unaongea **kitoto.**
✓ **Haraka** haina baraka.
✓ Fanya **haraka** tuondoke hapa.
✓ **Sindano** ya babu imepotea

✓ Alidungwa **sindano/kwa sindano** na daktari.
- **E kuwa N**

✓ Niliwasili **jana**.
✓ **Jana** yangu haikuwa nzuri.
- **T kuwa N**

✓ Nataka **kulala** sasa.
✓ **Kulala** kwake kunaudhi.
- **N kuwa U**

✓ **Ila** yake imemwathiri sana.
✓ Watu wote **ila** yeye walikwenda.
✓ Kichwa changu kina **walakini**.
✓ Nimekula **walakini** sijashiba.
- **E kuwa I**

✓ Mwenda **pole** hajikwai.
✓ **Pole!** Usijali utapona.
✓ Amepaka rangi **sawasawa**.
✓ **Sawasaw**a! Siku moja tutakutana.
- **H kuwa E**

✓ Paka amepanda **juu ya mti**.
✓ Ameingia **katika choo**.
- **T kuwa E**

✓ Mtoto **akilia** atatapika.
✓ Aliingia **akilia**.
- **N kuwa I**

✓ Gege anacheza **ala** yake ya muziki.
✓ **Ala!** Waniwekea uchafu katika chakula?

Mofimu

⇒ Kipashio kidogo zaidi katika lugha kisichoweza kuvunjwavunjwa zaidi bila kupoteza maana yake.

Aina

- **Mofimu huru**

⇒ Neno lisiloweza kugawanywa katika vipande mbalimbali na linalojisimamia na kuwa na maana kamili.
✓ Kuku, baba, mama, sana, labda, jana n.k.
- **Mofimu tegemezi**

⇒ Isiyoweza kujisimamia na kujitosheleza kisarufi, mifano:

- **Mzizi** (Sehemu ya neno inayobeba maana kuu na isiyoweza kubadilishwa)

✓ **m-tu, samahe-**k-a, n.k.

- **Nafsi**

✓**Tu**mesahau
- **Ngeli**

✓ **Li**lianguka.
✓ **Ya**lianguka.
- **Kikanushi**

✓ **Si**kumpiga
✓ **Ha**lijaoza.
✓ **Hu**li.
- **Njeo/wakati**

✓ Li**li**iva.
✓ A**na**lia.
✓ Tu**ta**imba.
✓ Ali**po**enda.
- **Hali**

✓ **Me, nge, ngali, hu, ki, ka, n.k.**
- **Mahali**

✓ Ali**po**ingia.
✓Ali**ko**ingia.
✓Ali**mo**ingia.
- **Virejeshi**

✓ Lili**lo**nunuliwa.
✓ Ali**ji**kata.
- **Mtendwa/watendwa/kitendwa/vitendwa/shamirisho**

✓ Alichi**ki**chukua.
✓ Kilicho**wa**ua.
- **Mnyambuliko/kauli**

✓ Alimpig**i**a.
✓ Alimli**li**a
✓ Alinikos**e**a.
✓ Alimto**le**a.
- **Kiishio**

✓ a, e, i, u

Viambishi

⇒ Viungo vyenye maana vinavyofungamanishwa na mziziwa neno ili kulipa maana mbalimbali.

Aina

- **Viambishi Awali**

⇒ **Ambavyo** hutokea kabla ya mzizi.
✓ **A-li-ye-ku-**kata-a
▪ **Viambishi Tamati**
⇒ Ambavyo hutokea baada ya mzizi k.m. ki-pig**-ishw-a-cho**

Mnyambuliko wa Vitenzi

⇒ Kunyambua kitenzi ni kukiongeza viambishi tamati ili kukipa maana tofauti.

Aina za minyambuliko/kauli za vitenzi

▪ **Kutenda**
⇒ Hali ya kawaida ya kitenzi.
▪ **Kutendatenda**
⇒ Hali ya kitenzi kurudiwa.
▪ **Kutendea**
✓ Kwa niaba ya
✓ Badala ya
✓ Sababu
✓ Kuonyesha kitumizi
✓ Mwendo wa kitu kuelekea kingine
▪ **Kutendwa**
⇒ Huonyesha nomino iliyoathiriwa na kitenzi.
▪ **Kutendewa**
⇒ Humaanisha kitendo kimetendwa na mtu badala au kwa niaba ya mtu mwingine.
▪ **Kutendana**
⇒ Unamtenda mtu jambo naye anakutenda jambo lilo hilo.
▪ **Kutendeana**
⇒ Unamtendea mtu jambo naye anakutendea jambo lilo hilo.
▪ **Kutendeka**
⇒ Uwezekano wa kitendo kufanyika
▪ **Kutendesha**
⇒ Mtu au kitu kusababisha kufanyika kwa kitendo.
▪ **Kutendeshea**
⇒ Kusababisha kitendo kitendeke kwa niaba ya mwingine.
▪ **Kutendeshwa**
⇒ Kusababishwa kufanya jambo.
▪ **Kutendeshewa**
⇒ Mtu kusababishwa kitendo kitendeke kwa niaba yake.

- **Kutendeshana**

⇒ Kusababisha kitendo kitendeke kwa mtu naye anasababisha kitendo kicho hicho kitendeke kwako.

- **Kutendesheana**

⇒ Kusababisha kitendo kitendeke kwa niaba ya mtu naye anasababisha kitendo kicho hicho kitendeke kwa niaba yako.

- **Kutendesheka**

⇒ Kitendo fulani kinaweza kusaababishwa.

- **Kutendama**

⇒ Kuwa katika hali fulani bila ya mabadiliko.

✓ lala-lalama
✓ ficha-fichama
✓ shika-shikama
✓ ganda-gandama
✓ chuta-chutama
✓ funga-fungama
✓ kwaa-kwama
✓ unga-ungama
✓ andaa-andama
✓ saki-sakama

- **Kutendata**

⇒ Hali ya mgusano au kushikanisha vitu viwili.

✓ paka-pakata
✓ fumba-fumbata
✓ kokoa-kokota
✓ okoa-okota
✓ kama-kamata

- **Kutendua**

⇒ Hali ya kiyume
✓ choma-chom**o**a
✓ funga-fung**u**a

- **Kutenduka**

⇒ Kuweza kufanyika kwa hali ya kinyume.
✓ chom**ok**a
✓ fung**uk**a

Vinyume vya vitenzi

- ✓ komea-komoa
- ✓ bariki-laani
- ✓ patana-kosana
- ✓ angika-angua
- ✓ mwaga-zoa
- ✓ ziba-zibua
- ✓ tatiza-tatua
- ✓ funika-funua
- ✓ tega-tegua
- ✓ tawanya-kusanya
- ✓ ugua-pona
- ✓ nasa-nasua
- ✓ kwamiza-kwamua
- ✓ kosa-kosoa
- ✓ pakia-pakua
- ✓ twika-tua
- ✓ paa-tua
- ✓ cheka-lia
- ✓ anika-anua
- ✓ simama-keti
- ✓ fukia-fukua
- ✓ inama-inuka
- ✓ funga-fungua
- ✓ furahi-huzunika
- ✓ kumbuka-sahau
- ✓ oa-taliki
- ✓ choka-pumzika
- ✓ uliza- jibu
- ✓ jenga-bomoa
- ✓ ishi-kufa/hama
- ✓ kufa-kufufuka/ishi
- ✓ lewa-levuka
- ✓ anza-maliza/isha
- ✓ saza/bakiza-maliza
- ✓ meza-tapika/tema
- ✓ ingia-toka
- ✓ dharau-heshimu
- ✓ kweya-teremka

- ✓ panda-shuka
- ✓ sifu-kashifu
- ✓ chimba-fukia
- ✓ chafua-safisha
- ✓ cheka-lia
- ✓ panda-shuka
- ✓ babaika-tulia
- ✓ pokea-aga
- ✓ zama-elea
- ✓ vaa-vua

kitenzi	**tendea**	**tendwa**	**tendewa**	**tendana**	**tendeka**	**tendeana**	**tendesha**	**tendeshea**	**tendesheka**
cha ✓ ogopa	chia	chwa	chiwa	chiana	chika	chiana	chisha	chishia	chishika
cha ✓ pamb azuka	chea	0	chewa	0	0	0	chesha	cheshea	chesheka
chwa ✓ jua kuanza kutua	chwea	0	chwewa	chweka	0	0	chwesha	chweshea	chwesheka
fa ✓ tokwa na uhai	fia	0	fiwa	fika	0	fiana	fisha	fishia	fishika
gwa ✓ angukа	gwia	0	gwiwa	0	0	gwiana	gwisha	gwishia	gwishika
ja ✓ sogea karibu	jia	0	jiwa	jika	0	jiana	jisha	jishia	jishika
la ✓ tia chakula kinywani na kumeza	lia	liwa	liwa	lika	lana	liana	lisha	lishia	lishika
nya ✓ enda haja kubwa ✓ angukа matone	nyea	nyewa	nyewa	nyeka	0	nyeana	nyesha	nyeshea	nyesheka
nywa ✓ tia kitu majimaji	nywea	nywewa	nywewa	nyweka	0	nyweana	nywesha	nyweshea	nywesheka

kinywani na kukimeza									
pa ✓ kabidhi	pea	0	pewa	peka	pana	peana	pesha	peshea	pesheka
pwa ✓ maji toka ufuoni hadi mbali ya bahari	pwea	0	pwewa	pweka	0	0	pwesha	pweshea	pwesheka
ta ✓ taga	tia	o	tiwa	tika	0	0	tisha	tishia	tishika
wa ✓ tokea	wia	0	wiwa	wika	wana	wiana	wisha	wishia	wishika

Matumizi ya Maneno na Viambishi Maalum

Maneno Maalum

-
- **ila**

a) isipokuwa

✓ Watu wote **ila** yeye wameenda.

b) kasoro

✓ Hakuna kizuri kisicho na **ila**.

- **labda** (pengine/shaka)

✓ Haonekani siku hizi **labda** amepata uhamisho.

- **ikiwa**

a) (kama/shaka)

✓ Tutamkuta nyumbani **ikiwa** amepewa likizo.

b) masharti

✓ Mgonjwa atapona **ikiwa** atakunywa dawa ipasavyo.

- **walakini**

a) dosari

✓ Ghorofa limebomolewa kwa sababu lilikuwa na **walakini**.

b) lakini/bali

✓ Nimekula **walakini** sijashiba.

- **ingawa/ingawaje** (hata kama)

✓ Nilijilaza kitandani **ingawa** sikuwa na usingizi.

- **ijapokuwa/japo** (hata kama)

✓ Usicheze na nyoka **ijapokuwa** ni mdogo.

- **jinsi**

a) njia/utaratibu wa kufanyia jambo
✓ Sijui **jinsi** ugali unavyopikwa.
b) aina/namna/sampuli
✓ Siwezi kula chakula **jinsi** hii.
c) kulingana na/kama
✓ Alikuja **jinsi** alivyoniahidi.

- **kwa**

a) mahali
✓ Ameenda **kwa** Juma.
b) jinsi
✓ Alisoma **kwa** bidii.
c) sehemu ya kitu kisima/akisami
✓ Amepata alama moja kwa tano katika mtihani.
d) pamoja na
✓ Harusi ilihudhuliwa na wazee **kwa** vijana na tulikula wali **kwa** nyama.
e) kuonyesha kitu kilitumiwa kama kifaa
✓ Alikata mkate **kwa** kisu.
f) sababu
✓ Aliugua **kwa** kunywa maji machafu.
g) kuunganisha vipashio viwili
✓ Leo ndiwe utapika **kwa hivyo** tayarisha viazi.
h) muda/kipindi
✓ Alilia **kwa** nusu sana.
i) kufanya jambo bila kupoteza wakati
✓ Baada ya kula, tulienda moja **kwa** moja kulala.
j) kivumishi cha a-unganifu cha ngeli ya KU
✓ Kucheka **kwa** Maria kunaudhi.
k) umiliki wa mahali
✓ Twende nyumbani **kwangu**.

- **na**

a) kiunganishi
✓ Mama **na** baba wanalima.
b) umilikaji
✓ Kamau **ana** kitabu kizuri.
c) wakati uliopo
✓ A**na**andika barua.

d) kauli/mnyambuliko
✓ Kamau na Juma wanapiga**na**.
e) kuonyesha tofauti
✓ Kiatu hiki ni tofauti **na** kile.
f) mtenzi
✓ Alipigwa **na** mwalimu.
g) kuonyesha ufupisho wa nafsi
✓ Alisaidiwa **nao**.

Zoezi

a) Eleza matumizi ya na katika sentensi zifuatazo:
i) Baba **na** mama wa**na**piga**na** kwani a**na** tabia ya kulewa.
ii) Mtoto aliteswa **na** mama yake kwa kuwa tofauti na wengine **na**mi kikamkanya.

- **wala** (kukanusha)

✓ Sikumtusi **wala** kumpiga.

Viambishi Maalum

- **me/ja** (hali timilifu/kitendo kutendeka na si muda mrefu uliopia)

✓ Mama a**me**wasili.
✓ Mama ha**ja**wasili.

- **hu**

a) mazoea/jambo hutokea kila wakati
✓ Yeye **hu**lala mapema.
b) kikanushi
✓ **Hu**kutibiwa vizuri.

- **li**

a) wakati uliopita
✓ A**li**tupatia zawadi.
b) ngeli
✓ Tunda **li**meiva.
c) kitenzi kishirikishi kipungufu
✓ Jembe **li** ghalani.

- **ni**

a) nafsi ya kwanza umoja
✓ **Ni**liwasili jana.
b) mahali
✓ Twende kanisa**ni**.

c) kitenzi kishirikishi kipungufu
✓ Yeye **ni** daktari.
d) wingi
✓ Toke**ni** nje.
- **ndi-** (kitenzi kishirikishi kipungufu)

✓ Yeye ndiye aliniibia pesa.
- **ji**

a) udogo
✓ Ki**ji**tu kimeanguka.
b) ukubwa
✓ **Ji**bwa limebweka.
c) kirejeshi
✓ Ali**ji**palia makaa.
d) nafsi ya pili
✓ **Ji**chukulie upendacho.
e) kiambishi tamati cha kuunda nomino.
✓ Mwimba**ji** alituzwa.
- **Ki**

a) kitendo ki katika hali ya kuendelea
✓ Tulikuwa tu**ki**la alipoingia.
b) masharti/kitendo kinategemea kingine
✓ Utapita mtihani u**ki**jitahidi.
c) udogo
✓ Kitoto **kinalia**.
d) ngeli
✓ **Ki**tabu **ki**mechukuliwa.
e) kitenzi kishirikishi kipungufu
✓ chakula **ki** mezani.
f) kielezi namna mfanano.
✓ Yeye hula **ki**fisi.
g) kitendo hakifanyiki kamwe
✓ Chai hii hainywe**ki**.
- **ku**

a) kikanushi cha wakati uliopita
✓ Ha**ku**mpiga kwa jiwe.
b) nafsi ya pili umoja.
✓ Ali**ku**pigia simu jana.

c) mahali
✓ Hu**ku ku**mesafishwa.
d) ngeli
✓ **Ku**ugua **ku**memnyenyekesha.
e) mwanzo wa kitenzi
✓ Ameenda **ku**safisha nyumba.

- **ka**

a) mfuatano wa matukio
✓ Tulikula chakula, tu**ka**nywa chai kisha tu**ka**lala.
b) vichwa vya habari
✓ Mwizi **ka**pigwa mawe
c) kutoa amri
✓ **Ka**chezeeni nje!
d) kitendo fulani ni tokeo la kingine
✓ Tulisoma kwa bidii tu**ka**pita mtihani.
e) kutoa nasaha/shauri
✓ **Ka**mwombe babako msamaha.

- **a**

a) Hali isiyodhihirika ya wakati uliopo
✓ Watoto wacheza uwanjani.
b) vichwa vya habari
✓ Waziri **a**aibishwa na wananchi.
c) kitendo kinaendelea
✓ **Twa**enda sokoni.
d) nafsi ya tatu umoja
✓ Yeye **a**liudhika sana.
e) ngeli
✓ Mbuzi yule **a**tachinjwa kesho.
f) kiishio
✓ Mtoto amekul**a** vizuri.

- **nge/ngali** (masharti yanayowezekana au yasiyowezekana)

✓ Ningekuwa na pesa, ningenunua kiatu.
✓ Laiti ningalijua nisingaliingia katika hilo basi.

- **po**

a) wakati
i) maalum
✓ Yeye ana**po**lala hukoroma.

ii) Wowote/mazoea
✓ Mwalimu aingi**apo** wanafunzi husimama.
b) mahali
✓ Pali**po**safishwa pamechafuka.
c) masharti
✓ Mtoto aamka**po**, mpe uji.
d) kikanushi cha ki ya masharti
✓ Akila.-asi**po**kula.
Viakifishi
- **Alama za usemi(“”)**

a) Usemi halisi
✓ “Njoo kesho,” mama akamwambia.
b) Lugha ngeni
✓ “Ninunulie jarida la ‘Parents’”, babake akamwambia.
c) Vipindi, filamu, makala
✓ “Vioja Mahakamani”
d) Semi
✓ “kumwaga zigo”
- **Dukuduku (...)**

a) maneno yameachwa ya kutangulia, kati au ya mwisho. Yaweza kuachwa kwa kuwa makali
✓ Nyani haoni...
b) kukatizwa usemi/kauli
AMINA: Mama ni...
MAMA: Kwanza watoka wapi usiku huu?
c) maneno yanaendelea
✓ Alimwambia ajihadhari anapovuka barabara...
- **Koma/mkato/kipumuo(,)**

a) pumziko fupi katika senyensi
✓ Tulipofika sokoni, tulinunua mboga.
b) kuorodhesha
✓ Alinunua mboga, samaki, nyanya na viazi.
c) kuonyesha mwanzo au mwisho wa usemi halisi
✓ “Njoo kesho,”mama akamwambia.
d) kuandika anwani
✓ Shule ya upili Gatwe, S.L.P 160, Kerugoya.
e) baada ya kutaja jina la mtu anayepewa habari

✓ Daktari, ningependa kukuona.
f) kutenganisha sentensi zenye masharti
✓ Usipofanya kazi, usile.
g) kuandika tarehe
✓ Alizaliwa mwezi wa Julai, tarehe 18, 1999.
h) kuandika tarakimu zinazozidi elfu
✓ 1,000, 13,000, n.k.

- **Ritifaa/kibainishi(’)**

a) herufi imeachwa
✓ wal’otutuma
b) shadda/mkazo
✓ `iba, ka`lamu
c) katika sauti ya king’ong’o
✓ Ng`ombe amekufa.
d) Kufupisha
✓ Tu’shasafisha nguo.
e) katika kuandika miaka yenye namba izilizoachwa
✓ `73-`99.

- **Mshazari/mkwaju(/)**

a) Tarehe
✓ Alizaliwa tarehe 5/6/1998.
b) kuonyesha kumbukumbu
✓ KUMB 1/2009
c) kuonyesha visawe
✓ Nenda katika shule/skuli.
d) Kuonyesha au
✓ Wanawake/wanaume wataajiriwa.

- **Kistari kifupi(-)**

a) kuandika tarehe
✓ 5/6/2006
b) kuonyesha silabi, viambishi au mofimu
✓ sa-la-mu na imb-a.
c) kuonyesha neno linaendelea katika mstari unaofuata.
✓ Usitenganishe sauti za silabi.
d) Kuonyesha mzizi wa neno
✓ -ma,-bwa
e) kuonyesha kudumishwa kwa sauti

✓ Lo-o-o-o!
f) Hadi/ kipindi cha tukio fulani
✓ 1999-2008.
g) Kutenganisha usemi na msemaji
✓ Huo ni upumbavu-Kibaki

- **Kistari kirefu(____)**

a) kutenganisha usemi na msemaji
b) kuonyesha mabadiliko ya ghafla
✓ Wanafaunzi ni wajinga-samahani, simaanishi wote.
c) kutangulia maelezo ya ziada
✓ Walisaidia nchi za Afrika Mashariki- Kenya, Uganda na Tanzania kwa msaada

- **Mstari(_____)**

a) kusisitiza
✓ Jibu maswali mawili pekee.
b) kuonyesha aina za maneno
✓ Mtoto wangu analala (V. kimilikishi).
c) kuonyesha vitabu, majarida na magazeti
✓ Chemchemi za Kiswahili, “True Love”, n.k.
d) kuandika anwani/kichwa
✓ Mwanafunzi Adhibiwa/Kaadhibiwa Vikali

- **Kikomo/kitone/nukta (.)**

a) mwishoni mwa sentensi.
b) kuandika tarehe
✓ 2.3.2013
c) kuonyesha ufupisho wa maneno
✓ Dkt.,Bw.,Bi.,C.C.M
d) kuonyesha takwimu
✓ 4.5, 86.27, n.k.
e) kutenga shilingi na senti
✓ 6.50-shilingi sita na senti hamsini
f) juu ya herufi j na I

- **Nusu/semi koloni/nukta na kituo (:)**

a) kugawa sentensi mbili zinazoweza kujisimamia bila ya viunganishi
✓ Wasichana walifuata maagizo waliyopewa; wafulana waliyagomea.

b) kama kipumziko katika sentensi ndefu
✓ Alipochunguza ile hati aliyokabidhiwa na wale wafanya biashara aliona kuwa si nzuri; akaamua kujitenga nayo.

- **Vifungo/mabano/paradesi( )**

a) kuzingira nambari au herufi katika orodha
✓ (i),(a)
b) kuonyesha maelezo ya vitendo vya msemaji katika mazungumzo, mahojiano au tamthilia
✓ MAMA :(*Akiinama.*) Hebu njoo haraka.
c) kutoa maelezo zaidi
✓ Ema (kifungua mimba changu) chaja leo kutoka marekani.
d) kuonyesha visawe
✓ Mamba (ngwena) huliwa.

- **Herufi kubwa(H)**

a) mwanzoni mwa sentensi.
b) kuandika anwani
✓ S.L.P 1000, Bura.
c) mwanzoni mwa usemi halisi
✓ “Twendeni zetu,” akatwambia.
d) baada ya kiulizi (?) na hisi (!)
✓ Lo! Ulienda? Hebu niambie yaliyojiri.
e) mwanzoni mwa nomino za pekee
✓ Musa
f) ufupisho wa maneno
✓ C.C.M (Chama cha Mapinduzi)
g) mwanzoni mwa majina ya vitabu, majarida, magazeti, vipindi, filamu, n.k.
h) kuandika sifa inayotokana na jina la pekee
✓ Kiganda, Kikristu.

- **Koloni/ Nukta mbili (:)**

a) kuorodhesha
✓ Ukitaka kuandaa samosa, unahitaji vitu hivi: unga, nyama, chumvi, mafuta na kitunguu
b) kutangulia usemi halisi
✓ Alimwangalia kisha akamtupia: “mshenzi.”
c) kuandika mazungumo, mahojiano au tamthilia
✓ MAMA :(*Akiinuka*.) Umechelewa wapi?

d) kutenganisha dakika na sekunde
✓ 9.25:05
e) kutangulia maelezo fulani
✓ Alipofungua mlango alishtuka: mizoga ya punda ilikuwa imetapakaa nje.

- **Hisi/mshangao (!)**

a) kuamrisha
✓ Kachezeeni nje!
✓ Kamau! Unafanya nini?
b) baada ya vihisishi
✓ Masalaale! Pesa zangu zote zimeibwa.
c) baada ya sentensi iliyo mshangao
✓ Gari langu limeibwa!
d) kusisitiza
✓ Kesho msichelewe kuwasili shuleni!
e) kudharau/kubeza
✓ Mwangalie! Kichwa kama jiwe.
f) baada ya tanakali
✓ Mate yalimdondoka ndo! Ndo! Ndo!

- **Kiulizo (?)**

a) mwishoni mwa sentensi iliyo swali
b) mwishoni mwa methali zenye muudo wa swali
✓ Pilipili usiyoila yakuwashiani?
c) kuonyesha shaka
✓ Kenyatta alizaliwa mwaka wa 1945(?)
d) kuonyesha mwaka wa kuchapishwa kwa kitabu haujulikani
✓ Mlacha J (?) Tujijue Ipasavyo

- **Herufi nzito (h)**

a) kusisitiza
✓ Jibu maswali *manne* pekee.
b) kuonyesha wakati/njeo au hali
✓ Nilicheza,Nimelima
c) kuonyesha umoja na wingi
✓ **m**toto-**wa**toto
d) kuonyesha aina ya neno katika sentensi
✓ Mtoto **wake** amelala (kivumishi)

- **Herufi za mlazo/italiki(*h)***

a) kuonyesha aina ya kiambishi au mofimu
✓ Ki-li-*cho*-ib-w-a (kirejeshi).
b) kusisitiza
✓ Jibu maswali *mawili*.
c) kuonyesha jina la kitabu
✓ *Nyota ya Rehema*
d) kuonyesha maneno ya kigeni
✓ Napenda *mukimo.*
e) kuonyesha maelezo ya vitendo vya mhusika katika mazungumzo, mahojiano na tamthilia
✓ AMINA: (*Akiinuka)* Mama ameenda kwa Farashuu.

▪ **Kinyota(*)**

a) kuonyesha neno limeendelezwa vibaya
✓ *kitaabu
b) kuonyesha sentensi haina mpangilio sahihi wa maneno
✓ *Kisu cha hiki ni nani?
c) kuonyesha tanbihi (maelezo ya neno yanapatikana chini mwa ukurasa)
✓ idhibati*
d) kuonyesha sentensi ina makosa kisarufi
✓ *Kuku hii ni ya nani?

Usemi Halisi

⇒ Maneno halisi kama yanavyotamkwa na msemaji.
a) Huandikwa bila kugeuza chochote.
b) Huanzia kwa herufi kubwa.
c) Hunukuliwa kwa alama za usemi ambazo huandikwa zikiwa mbili mbili na moja moja katika dondoo ndogo k.m.
“Mwambie ‘ugua pole’ ukimuona,” baba aliniambia.
d) Koma hutumiwa mwanzoni au mwishoni mwake.
e) Msemaji mpya anapoanza kusema, unapaswa kufungua aya mpya k.m.
Alimuuliza, “Huendi kwa nini?”
“Sikupewa ruhusa,” alijibu Zahara.
f) Baada ya (?) na (!) na (.) maneno huanzia kwa herufi kubwa k.m. Lo! Unatoka wapi saa hii? Aliniuliza.

Usemi wa Taarifa

⇒ Ripoti kuhusu mambo yaliyosemwa na mtu mwingine.

a) Si lazima maneno yatokee yalivyosemwa. Yanaweza kubadilishwa mradi ujumbe ubakie ule ule.

a) Alama za mtajo, kiulizi na hisi hazitumiki.

b) Maneno “kwamba’ na ‘kuwa’ hutumiwa.

c) Baadhi ya maneno na viambishi hubadilika k.m.

usemi halisi	usemi wa taarifa
-angu	-ake
-etu	-ao
-enu	-ao
-ako	-ake
wiki	wiki
ijayo	iliyofuata
kesho	siku
leo	iliyofuata
sasa	siku hiyo
huyu	wakati
hii	huo
ta/ki	huyo
ni	hiyo
na	nge
jana	a
Lo!	li
?	siku
	iliyotangu
	lia
	alishanga
	a
	alitaka
	kujua

VITATE

T/D

Tata

a) hali ya kutoeleweka

✓ sentensi hii ni **tata.**

b) fundo katika uzi

✓ uzi umeingia **tata/umetata.**

Dada
a) ndugu wa kike
Tua
b) shuka kutoka angani
✓ ndege ili**tua** uwanjani.
c) weka chini k.v. mzigo
Dua
a) maombi kwa Mungu
✓ omba **dua**
✓ piga **dua** –apiza/laani

Toa
a) ondoa kitu ndani ya kinginea
b) kinyume cha jumlisha
Doa
a) alama yenye rangi tofauti na mwili wa kitu
b) dosari/ila/walakini
Ndoa
a) arusi/makubaliano rasmi ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mke na mume/chuo
Tundu
b) uwazi mdogo wa mviringo kwenye kitu k.v. sindano
c) kitu maalum cha kuwekea ndege kilichotengenezwa kwa mabati, matete n.k.
Dundu
a) mdudu anayebeba uchafu
b) rundo la vitu /mtumba
Tuma
a) peleka kitu k.v. barua kwa njia ya posta
b) agiza mtu kufanya jambo
Duma
a) mnyama mkubwa mwenye umbo kama la paka
b) kamata, hasa katika vita
K/G
Kuku
a) aina ya ndege anayefugwa nyumbani
Gugu

a) mmea unaoota mahali usipotakiwa
b) mmea wa mwituni mfano wa unyasi

Kuni
a) vipande vya mti vya kukokea moto

Guni
a) shairi la arudhi lililokosa kutosheleza kanuni moja au zaidi ya uandishi

Kuna
b) kwaruza kwa kucha /kitu chenye menomeno

Guna
a) toa sauti ya kuonyesha kukataa, kutoridhika, au kuchukia jambo.

Kenge
a) mnyama kama mjusi mdogo

Genge
a) kundi la watu
b) pango/shimo

Kesi
a) daawa/mashtaka yanayosikilizwa mahakamani

Gesi
a) hewa inayotumiwa kupikia au kutiwa katika vinywaji
b) hewa ambayo haigeuki na kuwa majimaji katika joto la kawaida

CH/J

Changa
a) toa kitu ili kukusanya kwa kusudi fulani
b) siokomaa
c) chanja/pasua vipande vipande vidogo vidogo k.v. kuni

Janga
a) hatari/balaa

Chema
a) kizuri

Jema
a) zuri

Chini
a) kwenye ardhi/sakafu
Jini
a) shetani/ mtu muovu

Choka
a) pungukiwa na nguvu baada ya kufanya kazi
Joka
a) nyoka mkubwa sana

Chungu
a) chombo kinachofinyangwa cha kupikia
b) kinyume cha tamu
c) idadi kubwa (chungu nzima)
d) mdudu mdogo wa jamii ya siafu

Chambo
a) kinachowekwa kwenye mtego kunasia wanyama,samaki n.k.
Jambo
a) habari,tukio shughuli

Kucha
a) elekea asubuhi
b) ogopa
Kuja
a) hali ya kusogea karibu

Chuma
a) pata mali
b) madini magumu yanayotumiwa kujengea na kuundia vitu
c) tungua matunda au maua kutoka mtini
Juma
a) wiki
b) jina la mtu

Chenga
a) hepa kwa hila
b) mchele uliovunjikavunjika(mchele wa chenga)

Jenga
a) aka nyumba
b) fanya madhubuti/imarisha

Mchi
a) mti wa kupondea kwenye kinu
Mji
a) makazi ya watu wengi kulikojengwa nyumba nyingi
b) mahali kaburini anapowekwa mauti
c) sehemu ya kati ya chupa ya mwanamke mja mzito inayounganisha mtoto na mwili wa mama

Kichana
a) kitu cha kuchania nywele
Kijana
b) mtu wa makamo mwenye nguvu/mtoto wa kiume kabla ya kubaleghe

F/V
Faa
c) kusaidia
d) kuwa vizuri
Vaa
a) eneza kitu katika mwili ili kufunika sehemu fulani

Fua
a) safisha nguo
b) tengeneza kitu kutokana na madini
c) toa maji katika chombo
✓ **fua** maji
d) Haku**fua** dafu. (hakufaulu)
Vua
a) pata samaki kwa kutumia wavu, mshipi, ndoana n.k.

b) ondoa nguo mwilini
c) nusuru, okoa, ponya
d) **vua** macho (tazama)

Fika
a) wasili mahali
b) bila shaka/kabisa
Vika
a) valisha

Fuka
a) toa moshi bila kuwaka
b) uji wowote mwepesi (uji **fuka)**
Vuka
a) enda upande wa pili

Fuma
a) piga kwa mkuki
b) ona kwa ghafla bila kutazamia mtu anayetenda jambo ovu
c) tengeneza kitu kwa kusokota nyuzi,ukindu n.k
Vuma
a) julikana kwa watu wengi k.v. habari, mtu n.k.
b) toa sauti nzito k.v. simba,.upepo mkali,.ngoma n.k.

Afya
a) hali nzuri ya mwili/siha
Avya
b) toa mamba
c) tumia ovyoovyo mali, pesa, n.k.
Fito
a) vipande vya miti au chuma vya kujengea nyumba
Vito
b) mawe ya thamani
Fuja
a) tumia vibaya
b) haribu mali, nguo ,chakula n.k.
Vuja

a) pita kwa kitu mahali penye upenyo
✓ Gunia hili lina**vuja.**
Vunja
a) fanya kitu kigumu kuwa vipande vipande
b) badilisha pesa ziwe ndogondogo
c) enda kinyume na kanuni
Futa
a) pangusa
b) chomoa kisu
c) toa maji nje ya chombo/fua maji
Vuta
a) fanya kufuata/burura
b) ingiza hewa au moshi mapafuni
Wafu
a) waliokufa
Wavu
b) utando wa nyuzi wa kufulia samaki,kutegea wanyama,kuweka golini/kimiani n.k
CH/SH
Chaka
a) mahali penye miti iliyosongamana
b) msimu wa kaskasi/joto na ukavu wa ardhi
Shaka
a) wasiwasi
b) tuhumuma

Chali
a) lala mgongo juu kichwa chini
b) mtu anayechekesha watu kwa kuwatolea mkasa
Shali
a) kitambaa cha begani cha shehe
Shari
b) balaa (pata **shari)**
Chati
a) mchoro unaotoa maelezo Fulani
Shati
a) vazi la juu la mwili lenye mikono

Sharti
a) lazima
Choka
a) pungukiwa na nguvu baada ya kufanya jambo kwa muda mrefu
Shoka
a) kifaa cha kukatia na kupasulia miti
Chombo
a) ala ya kufanyia kazi
Shombo
b) harufu mbaya ya samaki
Chokoa
a) tia kitu chenye ncha kwenye tundu au shimo ili kutoa kitu k.m **chokoa** meno
Shokoa
b) kazi ya kulazimishwa (fanyishwa **shokoa)**
c) shamba lililolimwa na kuachwa kumea nyasi
TH /DH
Thamini
a) tia maanani, heshimu
Dhamini
a) toa pesa maakamani ili mshtakiwa asitiwe korokoroni
Thamani
a) kima
Dhamana
a) malipo ya kortini
Thibiti
a) kuwa ya kweli/kuaminika
b) Habari ime**thibiti.**
Dhibiti
a) tia mkononi
b) Nikidhibiti pesa zangu kutoka kwake nitanunua baiskeli.
c) weka chini ya mamlaka
Ridhi
a) kubali
b) pendezwa na jambo
Rithi

a) miliki kitu kutoka kwa mtu aliyekufa ama uliye na uhusiano naye
b) pata jambo au ujuzi kutoka kwa mtu mwingine

A/H

Apa

a) tamka jina aghalabu la Mungu kuthibitisha jambo Fulani

Hapa

a) mahali karibu

Ama

a) au

Hama

a) toka mahali fulani ili kwenda mahali pengine kuishi (gura)

Adimu

a) -a shida kupatikana,nadra

Hadimu

a) -mtumishi (mahadimu)

Ajali

jambo la madhara au hatari

Hajali

a) kinyume cha jali

Auni

a) saidia

Launi

a) rangi

L/R

Lahani

a) tuni

Rahani

a) chumba maalum katika nyumba au chombo cha kuwekea vitu

Lea

a) tunza mtoto

Rea

a) ghadhibika

Lemba

a) nyanganya kwa hila,punja

Remba
a) pamba, rembesha
Fahali
a) ng`ombe dume
Fahari
a) -a kujivuniwa kwa watu
Mahali
a) sehemu ambapo mtu au kitu huweza kukaa
Mahari
a) mali au fedha inayotolewa na mwanamme kupewa wazazi wa mwanamke anayetaka kumuoa
S /SH
Saba
a) namba inayoonyesha idadi
Shaba
a) madini yenye rangi ya manjano
Saka
a) tafuta,winda
Shaka
a) wasiwasi
b) tuhuma
c) kutokuwa na hakika
Suka
a) tikisa kitu
b) pitisha kitu kama nywele baina ya zenyewe kupata mfumo fulani
Shuka
a) enda chini kutoka juu ya kitu
b) kitambaa cha kujifunga kiunoni
Soga
a) mazungumzo ya kupitisha wakati
Shoga
a) jina waitanalo wanawake marafiki
b) msenge
Sababu
a) kinachofanya jambo kutokea,chanzo
Shababu

a) kijana

J/NJ

Jaa

a) tosha
b) tapakaa kila mahali
c) mahali pa kutupia taka

Njaa

a) hali ya tumbo kutaka kupata chakula
b) ukosefu mkubwa wa chakula

Chema

a) kizuri

Jema

a) zuri

Njema

a) nzuri

Jia

a) sogelea karibu

Njia

a) barabara
b) namna au jinsi ya kufanya jambo

Jozi

a) vitu viwili vinavyofanana vilivyo pamoja

Njozi

a) maono yatokeayo usingizini;ruia

Jana

b) siku kabla ya leo,mwaka kabla ya huu
c) buu la nyuki-kama kiluwiwi cha nzi

Njana-samaki mwenye rangi nyekundu

D/ND

Dege

a) eropleni kubwa
b) ndege mkubwa
c) ugonjwa wa watoto unaosababishwa na homa kali

Ndege

a) mnyama aghalabu anayeruka kwa mabawa
b) eropleni inayosafiri angani
c) ndege mbaya/mzuri (bahati nzuri/mbaya)

Duni
a) kitu chenye thamani ya chini
Nduni
b) ajabu/lisilo la kawaida
B/MB
Basi
c) gari la abiria
d) kisha
Mbasi
rafiki
Buni
a) gundua
b) unda
c) tunga
Mbuni
a) ndege asiyeweza kuruka lakini huenda mbio sana
b) mkahawa au mti uzaao kahawa
Bali
a) lakini
b) sijali wala si**bali** (kusisitiza kutojali)
Mbali
a) si karibu
b) tofauti
Mbari
a) ukoo
Bega
a) sehemu ya mwili juu ya mkono na chini ya shingo
Mbega
a) nyani
b) manyoya ya ndege wanayojifunga wachezaji ngoma (jifunga **mbega)**
Iba
a) chukua kitu cha mtu mwingine bila ruhusa
Imba
b) tamka maneno kwa sauti ya mziki
G/NG
Gawa

a) tenga katika sehemu mbalimbali
b) aina ya ndege wa usiku;kirukanjia

Ngawa

a) mnyama afananaye na paka

Guu

a) mguu mkubwa sana

Nguu

a) kilele cha mlima
b) nguru_aina ya samaki

Goma

a) kataa kufanya jambo mpaka masharti fulani yatimizwe
b) ngoma kubwa sana
c) duwi (aina ya samaki)

Ngoma

a) ala ya mziki inayotengenezwa kwa kuwambwa ngozi kwenye mzinga (piga ngoma***)***
b) mchezo wa kufuata mdundo wa ngoma (cheza ngoma)

Koma

a) alama ya kituo
b) acha kufanya jambo

P/B

Pata

a) kuwa na jambo, hali au kitu
b) kuwa kali

✓ Kinolewacho hu**pata**.

Bata

a) ndege mwenye vidole vilivyotandwa aghalabu akaaye majini

Papa

a) samaki mkubwa

Baba

a) mzazi wa kiume

Pana

a) kinyume cha –embamba

Bana

a) finya

Bango
a) uwazi ulio ardhini,mtini au jabalini
Bango
a) kipande cha karatasi ngumu kama kadi
b) bati linalozuia matope juu ya gurudumu la gari au baiskeli
Pacha
a) watoto wanaozaliwa kutokana na mamba moja
Bacha
b) tundu kwenye ukuta; shubaka(*closet)*
Paja
a) sehemu ya mguu kati ya goti na nyonga
Pania
a) kazana ili kufanya jambo lililokusudiwa
Bania
a) zuia kitu bila ya kutaka kukitumia (bania pesa)
Pima
a) tafuta urefu, uzito n.k.
Bima
a) mkataba na shirika wa kulipa pesa ili kupata fidia mtu anapofikwa na hasara
Punda
a) mnyama
Bunda
a) fungu la karatasi,noti,ngozi n.k
Panda
a) enda juu
b) kifaa cha kurushia vijiwe; manati
c) baragumu
d) tia mbegu ardhini ili zimee
Banda
jengo kubwa la kuwekea vitu au wanyama
Pasi
a) fuzu/faulu
b) hati inayomruhusu mtu kusafiri nje ya nchi/pasipoti
c) chombo cha kunyooshea nguo
Basi
a) gari kubwa la abiria

Mbasi
b) rafiki
T/D
Tamu
a) enye ladha ya kuridhisha mdomo
Damu
a) maji mekundu yanayozunguka mwilini
b) ukoo
Taka
a) kuwa na haja ya jambo fulani
b) uchafu
Daka
a) pokea kwa mikono kilichorushwa
b) tunda bichi (nazi daka/danga)
Tokeza
a) fanya kuonekana
Dokeza
a) toa habari za siri kwa uchache
Tai
a) ndege mkubwa mwenye makucha marefu alaye mizoga (*vulture)*
b) kitambaa kinachovaliwa kwenye ukosi wa shati
Dai
a) taka kupewa kilicho chako
b) habari inayosemwa na haijathibitishwa
K/G
Kamba
a) uzi mnene
b) samaki mdogo
c) mnyama wa baharini mwenye miguu mingi ambaye huliwa
d) kata kamba (kimbia)
Gamba
a) ngozi kama pembe ya kasa, samaki ,kasa au kobe(*scales)*
Konga
a) kuwa mzee
b) kusanya vitu au watu mahali pamoja (kongamano)
c) meza maji kidogo ili kupunguza kiu (konga roho)

Gonga
a) kutanisha kitu kimoja na kingine kwa kuvipiganisha
Koti
a) vazi zito livaliwalo juu ya nguo
Korti
a) mahakama
Goti
a) kiungo cha mguu kinachounganisha paja na muundi
Mfugo
a) mnyama anayefugwa nyumbani kwa ajili ya kuliwa au biashara
Mfuko
a) kitu cha kitambaa cha kutilia vitu

Tegua
a) fanya mtego usifanye kazi
b) ondoa chombo kama chungu mekoni
c) fanya kiungo cha mwili kifyatuke
Tekua
a) angusha kwa kusukuma
b) ng`oa kwa nguvu k.v. mmea
Mkuu
a) kiongozi
a) wenye hadhi kubwa
Mguu
a) kiungo cha binadamu au mnyama cha kusimamia au kutembelea
Oka
a) tia ndani ya tanuu kitu ili kiive au kikauke k.v unga uliokandwa au matofali
Oga
a) safisha mwili
b) enye hofu
Pika
a) weka kitu k.v. chakula sufuriani juu ya moto ili kiive
Piga
a) kutanisha vitu kwa nguvu

b) piga chafya, maji, hodi n.k.

Ukali

a) hali ya kutokuwa mpole
b) hali ya uchungu (ladha)

Ugali

a) chakula kinachopikwa kwa unga wa mahindi na kusongwa na maji moto hadi yakauke

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

1. Mke Wangu

⇒ Anwani inaweka msisitizo katika sifa ambazo msimulizi angetaka mke wake awe nazo na tabia za mke aliyemuoa.

⇒ Mkewe ana pingana naye hatimaye anaomba talaka.

Maudhui

Migogoro

⇒ Msimulizi hafanyi kazi na anawategemea wazazi. Aziza haoni mtu asiyefanya kazi kama mume wake.

⇒ Kuhusu kutumia mswaki na burashi, viatu na msimulizi kutotaka muuza madafu aingie ndani.

Ushamba na ujiji

⇒ Aziza kutovaa viatu, kutotumia burashi na dawa ya meno na badala yake mswaki na unga.

Utamaaduni

⇒ Wazazi wa msimulizi japo ni matajiri wanashikilia utamaaduni wa kuwachagulia watoto wachumba au wake.

⇒ Msimulizi hataki kumwoa Salma Fadhil kwa utamaaduni wake wa kuificha sura yake kwa kuiremba marangi ya mAshavu na midomo.

⇒ Utamaaduni wa mume kufanya kazi aweze kukimu familia.

⇒ Utamaaduni wa mavazi/vifaa-viatu, mswaki, unga.

⇒ Msimulizi na hata Fedhele wameacha mila na kugeukia uzungu. Fedhele anavaa kanzu inayomfika mapajani.

⇒ Uigaji wa utamaaduni wa kigeni huweza kuwaathiri wanawake kwa kuwakosesha waume wa kuwaoa kama Fedhele.

⇒ Kuoa watu wenye uhusiano wa damu nao-wazee wa Seluwa mtoto wa shangazi walitarajia msimulizi amuoe.

Ukandamizaji wa wanawake/taasubi ya kiume

⇒ Msimulizi kusema ‘Huyu ni mwanamke na wanawake ni kama watoto wadogo, hawaachi kisebusebu.

⇒ Msimulizi anataka kumwoa mwanamke mshamba amstaarabishe kuonyesha anachukulia mwanamke ndiye anahitaji maongozi ya mwanamme ilhali ni kinyume.
⇒ Kumdharau Fedhele kwa kutembea usiku wakiwa pamoja na mvulana ni kuchukulia wanawake kama vyombo visivyoweza kujidhibiti.

Heshima na utiifu

⇒ Aziza hana heshima kwa mumewe kwani Anamkashifu, anamuumbua na kumzungumzia kwa ujeuri, kejeli na hata akiwa ametoa macho. Anasema ni upuzi kukaa, kuchana nywele na kutembea.
⇒ Msimulizi anamweshimu mkewe kwani licha ya kejeli na ukaidi wake, anamjibu kwa upole na kumruhusu aseme. Anaona kuwa kumwamrisha mkewe lazima kungemshinda-busara.

Kazi na athari za kuikosa

⇒ Msimulizi anadharau kazi za mikono kwa kusema angeonekana wazimu akichoma mihogo.
⇒ Kazi ni muhimu kwa kila binadamu hata awe wa tabaka gani.
⇒ Kukosa kazi kunamwathiri msimulizi kwa kumkosesha mkewe ambaye amchukulii kama mumewe kwa kuwa hafanyi kazi bali anaishi kwa jasho la wengine-wazazi na mtumishi mapanya.

Utabaka

⇒ Kuna matajiri/makabaila (wenye nacho) kama vile msimulizi na wazazi wake na maskini/makabwela (wasionacho) kama vile wazazi wa aziza, mapanya na muuza madafu.
⇒ Matajiri wanaishi kwa jasho la maskini wanaofanya kazi ngumu.
⇒ Watu wa daraja la juu wanaishi mijini na wa daraja la chini shambani.
⇒ Watu wa tabaka la juu wameelimika ilhali wale wa tabaka la chini hawajaelimika kama vile Aziza.

⇒ Watu wa tabaka la juu wanafanya kazi za ofisi na wa la chini kazi za mikono kama vile ukulima, kuchoma mihogo na kuuza, kukwea minazi na kuuza madafu.

Ustaarabu

⇒ Watu wa mjini wanachukuliwa wamestaarabika na wa shambani hawajastaarabika. Kinaya ni kwamba yanayodaiwa ni ustaarabu ni kupuuza utamaaduni asili na kuiga ule wa kigeni.

Ndoa

⇒ Ndoa ya msimulizi inavunjika kwa kukosa kazi.

⇒ Za wengine wa mijini zinavunjika kwa wanaume kutaka kuwadhibiti wake au kuwatoa mambo ya kilimwengu.

⇒ Ndoa huathirika ikiwa watu hawana mtazamo na mwelekeo mmoja.

⇒ Ndoa za matabaka tofauti zaweza kuingia doa na kuvunjika. Unaweza kumtoa mtu shambani ilhali huwezi kutoa ushamba ndani yake.

Elimu

⇒ Humkomboa mwanamke kutokana na udhalilishaji wa mwanamume kwa vile inamwongezea mwanamke hadhi na hata kufanya mwanamume amwogope.

⇒ Huwafanya watu kuwa watumwa kama vile kuwafanya wadharau kazi za mikono au kujiajiri wenyewe na kutaka tu kuajiriwa ofisini-uboi wawe wakitumwa.

⇒ Yaweza kupotosha watu na kuwasahaulisha mila na desturi zao.

Ukengeushi

⇒ Msimulizi ambaye amesoma kumwoa mwanamke ambaye hajasoma.

Ujasiri

⇒ Aziza kumkabili mumewe na kumwambia ukweli bila kuogopa angepigwa au kutalikiwa.

Udhabiti wa msimamo

⇒ Aziza kukataa kutumia burashi, dawa ya meno na viatu.

⇒ Kutaka mume anayefanya kazi na anapotambua sivyo msimulizi alivyo anaamua kumtaliki na kufuata ndoto yake.

Nafasi ya mwanamke katika jamii

⇒ Msomi kama vile wa mjini.
⇒ Ananyimwa elimu kama vile wa shambani.
⇒ Ana uhuru kama vile Fedhele.
⇒ Anathamini kazi na kuichukulia kama kipimo cha utu.
⇒ Ana usemi k.m. Aziza.
⇒ Mtamaaduni kama vile Salma na mamake msimulizi ambaye anamyependekezea mke.
⇒ Mwacha mila kama vile Fedhele anayevaa kanzu hadi mapajani.
⇒ Hana ubaguzi kama vile Aziza hambagui muuza madafu.

Ubaguzi

⇒ Msimulizi anakataa kuoa wanawake walioelimika kwa kuwachukulia hawana maadili na hawafuati utamaaduni. Kinaya ni kwamba amuoa mke aliye mtamaaduni.
⇒ Hataki muuza madafu aingie nyumbani kwake kwa kuwa ni duni.

Ubwana

⇒ Aziza hapendi ubwana.
⇒ Mapanya ni mtumishi na anafanya kazi ya kuosha nguo na vyombo.

Busara/hekima

⇒ Msimulizi anamjibu mkewe kwa upole na hivyo kuzuia mzozo kuwa mbaya zaidi.

Bidii

⇒ Muuza madafu ana bidii kwa kujiajiri mwenyewe badala ya kutegemea kuajiriwa.

Ubahili

⇒ Aziza anaonelea ni ubadhirifu mtu kutoa pesa zake nyingi anunue kiatu kisha akikanyagishe kinyaa na kinyesi majiani.

Ujinga

⇒ Aziza hana elimu na hajui athari ya kwenda msalani bila viatu.

Matumizi ya lugha

Nidaha

⇒ Ngnhngnh!-msimulizi akidharau Fedhele.

⇒ Barabara! Si watu kama vile ninyi?-Aziza kuudhika kwa msimulizi kudharau uchomaji na uuzaji mihogo kama kazi.
⇒ Lo! Mimi nikachome mihogo niuze?-msimulizi kushangaa kwa kupendekezewa na mkewe ajiajiri kazi kama ya uchomaji mihogo.

Taharuki

⇒ Kwa nini Aziza anamtazama msimulizi bila kumzungumzia?
⇒ Msimulizi alimpa aziza talaka?
⇒ Msimulizi alimwoa seluwa?
⇒ Msimulizi alitilia maanani mafundisho ya Aziza na kuanza kufanya kazi?
⇒ Aziza aliolewa na muuza madafu?

Mbinu rejeshi

⇒ Msimulizi kuwaza jinsi alivyomkuta Fedhele Salim Saateni saa mbili usiku kavaa kanzu mpaka mapajani, kafuatana na shoga yake na wanamtia kijana mwanamume katikati yao.
⇒ Anatufahamisha kuna siku wakati wa alasiri Seluwa alienda kuwatembelea yeye msimulizi na mkewe.

Tashbihi

⇒ Uko chini ya wazee wako kama mtoto anayenyonya-Aziza kwa msimulizi.
⇒ Ngozi yake ilivyokacha utadhani msasa-ngozi ya aziza kuwa ngumu kwa kazi za mikono za shambani.

Takriri

⇒ Muuza madafu amevaa kanzu mararu mararu.
⇒ Hebu! Hebu! Aziza akimnyamazisha Seluwa ahakikishe ni sauti ya muuza madafu amesikia.
⇒ Dafu! Dafu! –Sauti ya muuza madafu kama alivyoisikia msimulizi.
⇒ Najua wewe una fikra namna na namna-Msimulizi akimwambia Aziza.

Balagha

⇒ Mangapi umeng’olewa?-Aziza kuonyesha uduni wa mbinu za sasa za kutunzia meno anazotumia msimulizi.

⇒ Sijui mimi nilikuwa narudi kutoka wapi vile?-wakati msimulizi alimuona fedhele usiku. Kinaya ni kuwa yeye pia alikuwa anatembea usiku na kachelewa kurudi nyumbani.
⇒ Kitu kilichokufa kina uzima gani wa kukuhami wewe?-Aziza akidharau kiatu.
⇒ Vipi mtu atafute kazi asipate?-Aziza kuonyesha mtu hawezi kukosa kazi hata kama ni ya kujiajiri.
⇒ Basi wewe ndiye mume wa kunioa mie we?-Aziza hamchukui msimulizi kuwa mumewe kwa kukosa kazi.

Methali

⇒ Kwenye nchi ya vipofu, mwenye jicho moja atakuwa mfalme.
⇒ Kila mtu na kazi yake.-msimulizi kuonyesha hawezi kufanya kazi za mikono.

Nahau

⇒ Nimvumbike mwenyewe mpaka aive-amuoe mwanamke amstaarabishe.
⇒ Kupatia mguu-Aziza hajawahi kufika mjini.
⇒ Tulikwenda sare kwa kupimana-msimuliz na Aziza kuwa sawa.
⇒ Kuwa na kidomo-hakumpenda salma kwa kusema maneno ya watu au kujibizana-kinaya ni kuwa aliyemwoa (aziza) anajibizana naye.
⇒ Nikawaweka kando-msimulizi kukataa kuwaoa wanawake aliochaguliwa eti hawana maadili.

Taswira

⇒ Fedhele salim kuvaa kanzu mpaka mapajani.-kuonyesha uigaji wa utamaaduni wa kigeni.
⇒ Salma Fadhil kujifunika uso na kujiremba marangi ya mAshavu na midomo-kuonyesha utamaaduni. Kinaya ni kuwa msimulizi anakataa utamaaduni ilhali yeye anaufuata kama vile kuchaguliwa mke na anaishia kuoa Aziza aliye mtamaaduni.
⇒ Alinionyesha viganja vyake nikaona namna ngozi yake ilivyokacha utadhani msasa.

Chuku

⇒ Hana kazi ya kumshughulisha labda kujikuna tu anapowashwa-mke wa msimulizi katu hakuwa na kazi yoyote, hakuwa na kazi wala basi.
⇒ Chukua mwiba unishindilie nyayoni mwangu utazame kama hautavunjika kabla ya kunichoma-Aziza kuonyesha jinsi miguu yake ilivyo madhubuti na haihitaji ulinzi wa viatu.
⇒ Alinionyesha viganja vyake nikaona namna ngozi yake ilivyokacha utadhani msasa.

Kinaya

⇒ Anwani mke wangu ni kinaya kwa vile mke aliyemtaka siye aliyempata. Alipata mwenye sifa zile alizozikataa kama vile utamaaduni, uhuru, mwenye usemi, n.k.
⇒ Kudhani mwanamke ndiye anastahili kuelekezwa (Niliona ni wakati wangu kumsoma Aziza ili nipate kumsomesha.) ilhali ndiye anahitaji kuelekezwa.
⇒ Kudhani Aziza kwa kutoka shambani, lazima awe mwepesi, msikivu na mwelekevu.
⇒ Kudhani Aziza angempenda kwa utajiri na angeridhika na maisha ya mjini ya kitajiri na starehe.
⇒ Kukataa salma kwa kuwa mtamaaduni na kuishia kuoa Aziza aliye mtamaaduni pia.
⇒ Kukataa kumwoa seluwa kwa kidomo chake na kuishia kuoa Aziza anayejibizana naye.
⇒ Kumkashifu Fedhele kwa kutembea usiku ilhali hata yeye alikuwa akitembea usiku.
⇒ Mtu ambaye amesoma na anayetoka katika familia tajiri kumwoa mwanamke ambaye hajasoma na anayetoka katika familia maskini.
⇒ Kuoa mwanamke wa shambani ambaye hajasoma na kutarajia asiwe mtamaaduni.

Tabaini

⇒ Aziza alikuwa daima akinitazama kwa kunichuja tena si mara moja wala si mbili.
⇒ Mimi sioni raha kulishwa na mtu ajinabi si baba yangu wala si mume wangu-Aziza hapendi utegemezi.

Tashhisi

⇒ Jawabu lake mtoto yule lilinizungusha kichwa darmadaru-majibu ya Aziza kumshangaza msimulizi.

Utohozi

⇒ Shilingi mbili-msimilizi alizompa Aziza akanunue madafu.
⇒ Burashi-ya kusugulia meno.
⇒ Plastiki iliyotengeneza kifurushi Aziza alikoweka mswaki na unga.

Kejeli

⇒ Nitapata mume wangu au gumegume tu?-Aziza akimdharau msimulizi kwa kuona hastahili kuwa mume wake.
⇒ Pesa mbili nobe zinakushinda kuzivumbua mpaka upewe?
⇒ Lazima tupokee kibivu maadamu mume wangu havumbui kibichi?
⇒ Kitu kilichokufa kina uzima gani wa kukuhami wewe?-kiatu
⇒ Kwa nini nichukue manyoya ya nguruwe nitie kinywani mwangu?-akidharau burashi ya kusugulia meno.

Tanakali

⇒ Aliondoka nyatunyatu akaenda zake ji-ji-Aziza akienda kuchukua vifaa vyake vya kusugulia meno.

Sitiari

⇒ Aziza kuita mswaki manyoya ya nguruwe.
⇒ Kukiita kiatu ngozi ya ngombe aliyekufa.
⇒ Pia kusema Kazi ndiyo maisha bora.
⇒ Kusema muuza madafu ni binadamu kamili.

2.Samaki wa Nchi za Joto

⇒ Anwani ni ya kiistiari
⇒ Kumaanisha unyonyaji au kitu unachokitumia kujifaidi.
⇒ Kuna samaki halisi wa nchi za joto ambao Peter anafanya bishara ya kuwauza nje ya nchi.
⇒ Serikali ya kikoloni kuleta samaki wa aina ya sangara walioangamiza samaki asilia katika maziwa.
⇒ Christine ni samaki kwa kutumiwa na Peter kutosheleza uchu wake. Pia daktari anamtoa mimba ili apate pesa.
⇒ Zac pia ni Samaki kwani Anamfahamu Peter kupitia Zac

⇒ Wavuvi ni samaki kwa vile Peter anawanunulia samaki kwa bei ya chini(kuwapunja) kAsha anawauza na kupata faida kubwa.
⇒ Watu weusi ni samaki kwa vile wanapenda pesa na pesa ni chambo chao.
⇒ Jagtit na Sunja kuibia nchi ya Uganda mapato ya ubadilishaji sarafu.
⇒ Sunja kumlaghai Jagtit kwa kumpa noti ya dola 100 bandia.
⇒ Zac na wengine wanaofanya kazi katika kampuni ya Peter ni Samaki kwani wanatumiwa naye katika biashara yake na faida kubwa ni yake.
⇒ Deogracious pia ni samaki kwani anafanya kazi ya utumishi wa nyumbani kwa Peter.
⇒ Nchi ni samaki kwani Peter anaiibia raslimali ya samaki na wahindi kama vile Sunjal na Jagtit wanaiibia pesa kwa kufanya biashara ya dola ya kimagendo.
⇒ Makahaba wanaotafutwa na wazungu huko ‘half London’ pia ni aina ya samaki kwani chambo chao ni pesa.

Maudhui

Mapenzi nje ya ndoa/vyuoni/shuleni na athari zake

⇒ Christine ni mwanafunzi wa shahada ya Sosholojia katika chuo cha Makerere. Aliye na tamaaa ya mpenzi wa kiume.
⇒ Tamaa yake inasadifiana na kutokea mzungu Peter anayemfahamu kupitia Zac.
⇒ Mwandishi anataka kuonyesha jinsi wasichana vyuoni wanavyojihusisha na mapenzi na watu walio na umri unaozidi wao ili wapate pesa (ushuga dadi).
⇒ Anaonyesha ukosefu wa uwajibikaji kwa vile Christine anapopata mimba anaamua kuitungua.
⇒ Anataka kuonyesha jinsi vijana wasivyochukulia maisha yao kwa umakini na tahadhari na hivyo kuishia kuyaharibu.
⇒ Jinsi watu wanavyojiingiza katika mapenzi ya kupitisha muda kama vile Peter na Christine hawakuwa na lengo la kuoana.

Uzinifu

⇒ Peter na Christine ni wazinifu kwa kufanya mapenzi ilhali hawajaoana.
⇒ Tunafahamishwa huko ‘half London’ kuna wazungu wengine wanatafuta makahaba (ukahaba).

Uwajibikaji

⇒ Peter hana uwajibikaji katika mapenzi kwani hamkingi Christine asipate mimba.
⇒ Hata hivyo Peter anawajibika katika kazi yake kwani halewi akiwa kazini.
⇒ Christine hawajibiki kwani hakubali mimba kama tokeo la vitendo vyake vya utovu wa uadilifu na kuilea bali anaamua kuiavya.
⇒ Zac anawajibika kwa vile anamfahamisha Christine kuwa Peter ana wasichana wengine.
⇒ Deogracius hawajibiki kwa vile hamfahamishi Christine kuhusu Peter ili amwambae.
⇒ Miriam na Margaret hawawajibiki kwani Christine alipowaeleza nia ya kutoa mimba hakuna aliyemzuia au kumshauri dhidi ya kufanya hivyo.

Ukoloni

Mkongwe

⇒ Serikali ya kikoloni kuleta samaki wa aina ya sangara walioangamiza samaki asilia.

Ukoloni mamboleo

⇒ Peter kupunja wavuvi kwa kuwanunulia samaki kwa bei ya chini(unyonyaji).
⇒ Peter kuibia nchi raslimali asili ya samaki.
⇒ Peter kuamrisha wafanyakazi wake kama mnyapara na akipaaza sauti ya juu.
⇒ Huko ‘Sailing Club’ kuna mahali pa wazungu na pa Waafrika.
⇒ Jagtit na Patel kufanya biashara ya magendo ya kuuza dola na hivyo kuibia nchi mapato ambayo ingepatika kutokana na ubadilishaji halali wa dola.
⇒ Huko Sailing Club ni mahali pa wazungu kwani ada ya juu ya kiingilio iliwafanya watu weusi kutopamudu.

Ukosefu wa ajira

⇒ Christine kusema mtu angepata kazi ya kiserikali kwa kubahatika.

Madhila ya wafanyakazi

⇒ Kuamrishwa-Peter Kuamrisha wafanyikazi wake kama mnyapara.

⇒ Kufanyia kazi katika mazingira duni-ofisi kuukuu za kikoloni.

⇒ Wavuvi wanaofanya kazi za mikono wana dhila la kupunjwa na wanaowanunulia wanaowanunulia samaki wao kwa mfano Peter.

Athari ya kumtelekeza mungu/dini

⇒ Christine alikuwa mkristo aliyeokoka lakini aliasi imani yake.

⇒ Hata dadake Dorothy alikuwa ameokoka lakini alikuwa mnafiki kwani alikuwa anajitia uongofu au anajificha chini ya kivuli cha dini.

⇒ Kujitia uongofu huko kukamchochea Christine kuendelea na mapenzi na Peter.

⇒ Christine kwa kuacha wokovu alitumbukia katika uzinifu na matokeo ni kutunga mimba na kuitungua.

⇒ Kuavya mimba kunamwathiri kisaikolojia kwa kuhisi amekosea Mungu na kuishi na woga wa madhara ambayo angepata kutokana na uavyaji mimba huo.

Utabaka

⇒ Peter ni wa tabaka la juu akiwa Uganda ilhali kwao Uingereza ni wa la chini la Cockney.

⇒ Deogracius, Zac na wengine ni wa tabaka la chini.

⇒ Huko Sailing Club ni mahali pa wazungu kwani ada ya juu ya kiingilio iliwafanya watu weusi kutopamudu.

⇒ Watu wa tabaka la juu kama Peter wanaishi katika mitaa ya kifahari kama vile wa ‘Tankhill’.

Tamaa

⇒ Peter kununua dola kimagendo ili aokoe pesa ambazo angalinunulia dola halali katika benki.

⇒ Peter kupunja wavuvi ili ajipatie faida kubwa.

⇒ Peter ana tamaaa ya wanawake. Ana wengine mbali na Christine.

⇒ Peter ana tamaaa ya anasa kama vile zinaa, likizo Nairobi, ulevi, kula nyama choma na kunywa mvinyo na kutafuta makahaba.
⇒ Christine ana tamaaa ya mpenzi wa kiume.
⇒ Zac na wafanyakazi wengine wana tamaaa ya pesa ndio maana wanamfanyi Peter Kazi licha ya kudhalilishwa naye ka kuamrishwa kama mnyapara.
⇒ Jagtit na Sunja wana tamaaa ya pesa na ndiyo sababu ya kuuza dola za kimagendo.
⇒ Madaktari wana tamaa ya pesa na wanamtoa Christine mimba ili wazipate.
⇒ Ami nana tamaa ya uongozi na ndiyo sababu ya kutaka kuangamiza maprofesa wanaopinga uongozi wake dhalimu.
⇒ Christine anasema vijana wengine wana tamaa ya kuwa watu wakubwa anayoiita ndoto za kiwenda wazimu.

Umaskini

⇒ Zac kulazimika kufanya kazi katika kampuni ya Peter akisoma.
⇒ Deogracius anafanya kazi duni ya utumishi kwa Peter.

Uongozi mbaya

⇒ Iddi Amin kufanya jaribio la kuangamiza maprofesa jambo lililosababisha wao kukimbilia uhamishoni.

Heshima

⇒ Zac kuinuka na kumkaribisha Peter kiti alichokuwa anakalia.

Ushauri

⇒ Zac kumshauri Christine kuwa Peter ana wasichana wengine lakini hakutilia maanani ushauri wake (mapuuza).
⇒ Dorothy kumshauri Christine kuwa aliota wazungu wakimpa sumu lakini hakushaurika.
⇒ Margaret na Miriam hawamshauri Christine dhidi ya kuavya mimba na hivyo wanapuuza wajibu wao mkubwa wa kumhifadhi ndugu.

Uavyaji wa mimba na athari zake/ukatili

⇒ Athari za kisaikolojia kuhisi nafsi ikimsuta.
⇒ Kuwa tasa.

⇒ Kuwa muuaji.
⇒ Kumkosea Mungu.
⇒ Kufa.

Matumizi mabaya ya taaluma

⇒ Daktari kumtoa Christine mimba ili apate pesa badala ya kumpa ushauri mwema.

Kasumba

⇒ Zac kutamaani kuwa mmarekani mweusi kwa kupenda kuzungumza sana kama mmarekani mweusi-'Hey man'.
⇒ Kuheshimu wazungu kwa kuchukulia wazungu wote kama wa tabaka la juu ilhali kwao hawaheshimiwi kwa kuwa wa tabaka la chini.
⇒ Watu wa rangi moja kuaminiana kwa mfano Jagtit kumwamini Mhindi mwenzake Sunja Patel ilhali anaishia kumtapeli.

Umuhimu wa kuwa makini

⇒ Peter ni makini kwa kuzikagua dola hadi kupata kuna noti moja bandia.
⇒ Jagtit hakuwa makini akipewa noti za dola na Patel ndipo akatapeliwa.

Bidii

⇒ Zac anafanya kazi katika kampuni ya Peter akiwa angali anasoma.
⇒ Peter ana bidii katika kazi yake na hatumii muda wa kazi kujistarehesha.

Anasa/starehe

⇒ Ulevi k.m. uvutaji sigara, kunywa pombe, uzinzi, Peter kwenda likizo Nairobi kustarehe baada ya biashara kunoga, Christine kujipumbaza kwa mvinyo, Margaret kulewa n.k.

Utovu wa Uaminifu

⇒ Peter ana wasichana wengine mbali na Christine.
⇒ Christine na dadake Dorothy si waaminifu kwa Mungu.

Ulevi na athari zake

⇒ Kusababisha Christine kuwa mzinifu.
⇒ Uzinifu kusababisha mimba isiyotakikana.
⇒ Unusu kaputi kutofanya kazi Christine akitolewa mimba.

Upyaro

⇒ Peter kumita Jagtit mwanaharamu anapotaka kuchukua vipande vya noti bandia.

Unafiki

⇒ Deogracius hamwambii kuwa Peter Peter ana wapenzi wengi.

⇒ Dorothy kuwa na wokovu bandia na anatumia dini kama kivuli (ulokole).

⇒ Peter kuwaonyesha Zac na Christine urafiki kumbe ataka kumtumia Christine.

⇒ Miriam ni rafiki mnafiki kwani hamshauri Christine dhidi ya kuavya mimba.

Uhalifu

⇒ Jagtit kumuuzia Peter dola kimagendo ilhali lilipaswa kufanywa na benki kuu.

⇒ Sunja kumpatia Jagtit pesa bandia.

⇒ Utoaji wanawake mamba.

Taasubi ya kiume/udunishaji wa wanawake

⇒ Peter kutumia wanawake kama vyombo vya kujiburudisha.

⇒ Wazungu kuwatumia makahaba kujistarehesha.

Utamaushi/ujidunishaji

⇒ Christine anajiingiza katika mapenzi kwa ili kujipumbaza au kujidanganya kuwa mtu mwingine au kuwa dubwAsha tu- ujidunishaji.

⇒ Anasema akiwa na na shahada angekuwa kama ng’ombe wa kizungu kwa vile hakuna ajira na ikipatikana mazingira ya kazi ni mabaya na mishahara ni duni.

⇒ Vijana hujiingiza katika myenendo isiyofaa kwa kupoteza matumaini ya maisha ya kesho.

Uingiliaji wa mambo ya wengine

⇒ Watu kumkodolea macho kwa kubusiwa na Peter shavuni.

⇒ Wakasema ‘Hawa Malaya hawana aibu hata chembe’.

⇒ Atakuambukiza ukimwi.

⇒ Ona alivyokondeana.

Ubwana

⇒ Deogracius ni mtumishi wa Peter.
⇒ Wafanyakazi wa Peter anaowaamrisha kama mnyapara.

Ukengeushi

⇒ Miriam na Christine kunywa pombe.
⇒ Miriam kuvuta sigara.
⇒ Mapenzi nje ya ndoa.
⇒ Kutembea kwa wanaume.
⇒ Uavyaji mamba.
⇒ Christine kuacha imani yake na Dorothy kuwa mlokole.

Ukweli

⇒ Zac kuonya Christine Peter ana wanawake wengi.

Matumizi ya lugha

Tashhisi

⇒ Nilivaa tabasamu niliyowahifadhia wanaume, tabasamu ya geresha-Christine kwa Peter.
⇒ Nilijaribu kumjibu lakini sauti ilinikwama kooni. Ukatokea mnong’ono.
⇒ Aibu ilinivaa-Christine akitoka kwa Zac baada ya kukutana na Peter kwa kushindwa kumjibu Peter au kusema haja ya moyo wake.
⇒ Nilikuwa nikiwangwa na kichwa changu kutokana na hedhi.
⇒ Springi za kitanda kulalamikia uzito wake wa ziada-kutoa kelele Peter alipokalia na kuzidisha uzito.
⇒ Mvinyo ulikuwa umenipa ujasiri fulani-Christine kutojishughulisha na Peter.
⇒ Macho yake kila mara yalinihukumu-ya Deogracius.
⇒ Wacha ukimwi uwateketeze-uwaangamize-wakati amemsindikiza Peter akielekea Nairobi.
⇒ Kutokana na mpito wa wakati, nywele za Peter kuwa zinabadilika rangi pengine kutokana na shinikizo la biashara ya nchi za nje ya samaki.
⇒ Nikaachwa nikiadhibiwa na mikondoo ya macho ya watu-baada ya kubusiwa shavuni na Peter.
⇒ Jua liliendelea kuadhibu kila kiumbe –kuwaka vikali Christine akiwa katika matatu.

Taswira

⇒ Deogracius amepinda mgongo kwa umri na mwenye miguu ya matege.
⇒ Kwa Peter, michoro ya kisana ilitundikwa ukutani, makabati ya vioo yaliyosheheni vinywaji vya aina aina na vyombo vya kichina-utajiri.
⇒ Chumba cha Zac kina kuta zilizobambuka rangi, balbu iliyotoa mwangaza hafifu, picha kubwa ya Bob Marley iliyorarukararuka, vitabu vikuukuu viwili vya 'Penguin Classics', kitanda chake kimetandikwa blanketi ya rangi ya kahawia.
⇒ Zac kufungua kikabati kidogo cheusi akatoa sahani mbili nyekundu za plastiki zilizoonyesha kuwa na mafutamafuta, kikombe cha kijani kibichi cha plastiki na glasi iliyokuwa na mavumbi.
⇒ Nikatabasamu nikitaka aone meno yangu yenye weupe wa maziwa.
⇒ Noti za dola za kijani kibichi.
⇒ Wajihi wa Peter ulikuwa wa wekundu usiokoza na wala sio weupe usiotakata. Nywele zake tu ndizo zilikuwa nyeupe
⇒ Tankhill, makasri ya mabalozi yalizungushwa kuta za mawe, juu ya kuta hizo kumechomekwa vigae vya chupa. Kuna mabwawa ya kuogelea na walinzi wa kulipwa-kuonyesha utabaka.
⇒ Peter, akiwa na bombo (kaptula) aliyoipenda sana, alionekana kama mvulana wa miaka 14.
⇒ Alikuwa na maungo mviringo ya ujana, mwili laini kama wa mwanamke na miguu iliyobonyea na iliyopuuka.
⇒ Miriam rafiki yake Christine ni Mtutsi aliyekuwa na wembamba waliopendelea wazungu na macho ya vikombe.

Mdokezo

⇒ Mwiba wa kujidunga… chochote kingetokea akitolewa mimba na asingemlilia au kumlaumu yeyote.
⇒ Fikra zilinipaa kuhusu matokeo ya uovu huu; kuwa tasa… labda kuwa muuaji… ahh… kumkosea Mungu… pengine hata kufa-madhara ya uavyaji mimba.

⇒ Lakini ni…nina jambo nataka kukwambia-Christine -Peter anapomwambia hana nafasi ya kumuona wakati wafanya kazi wanapakia mizigo.
⇒ Angalia hapa… Peter akimwabia jagtit ahakikishe noti ni bandia.

Methali

⇒ Mwiba wa kujidunga…
⇒ Palikuwa na kimya chenye mshindo-baada ya Zac kuwaacha na Peter-walinyamaziana.

Taharuki

⇒ Mwisho wa Christine na Peter ulikuwaje?
⇒ Baada ya kuavya mimba, afya ya Christine ilikuwaje?
⇒ Jagtit alimchukulia hatua gani mhindi mwenzake Sunja kwa kumpa noti ya dola 100 bandia?

Ujinga

⇒ Jagtit kutapeliwa na Sunja kwa kutokagua dola kwa kumwamini eti kwa vile ni wa asili yake hawezi kumlaghai.
⇒ ,Christine kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu asiyemfahamu vyema.
⇒ Kufanya mapenzi bila kinga.
⇒ Kutofahamu tama mbele mauti nyuma.
⇒ Kutoshaurika.
⇒ Kuacha Mungu akijua amwachaye hawezi kuwa na maisha mazuri.
⇒ Kuavya mimba akijua madhara yake na kuua mtoto ilhali hana hata mmoja.

Balagha

⇒ Mbona tusijipatie kinywaji-Zac.
⇒ Ningemwambiaje Peter akinipigia simu?-Baada ya kuavya mimba.
⇒ Mimi? Kwa nini?- Christine Zac anapomwambia Peter alitaka wamtembelee Tankhill-kujifanya hataki ilhali anataka.
⇒ Je, Ni kweli Peter alinitaka?-Christine. kujiuliza kimoyomoyo.
⇒ Kumbe alikuwa mzungu wa tabaka la chini?

Nahau

⇒ Tunapiga gumzo-Peter kuingia na kukuta Christine na Zac wakiongea.
⇒ Kufyata mkia-Christine-Peter alistahili kunyamaza kwa vile alikuwa anaibia nchi samaki.
⇒ Sikutaka kukitia kitumbua cha uhusiano wetu na Peter mchanga-kuharibu mapenzi yao licha yake kuwa na wasichana wengine.
⇒ Kupiga funda kubwa-Christine kujaza kinywaji kwa mara moja baada ya kushindwa kumjibu Peter.
⇒ Nimeavya mimba-nimetoa kijusi tumboni.
⇒ Niligundua ulikuwa Mja mzito-Peter.
⇒ Mwili haukufa ganzi-haukupoteza hisi baada ya sindano ya nusu kaputi-athari ya ulevi.
⇒ Alimpasulia mbarika-Peter kumpa Jagtit habari mbaya kuwa noti ni bandia.

Kinaya

⇒ Christine kujivuta kidogo mbali na Zac ilhali anamtaka.
⇒ Wewe lazima u msichana mwerevu-Peter-ni kinyume.
⇒ Mimi? Kwa nini? Christine Zac anapomwambia Peter alitaka wamtembelee Tankhill-kujifanya hataki ilhali anataka.
⇒ Zac usiwe mpumbavu. Mimi sitakwenda-anataka kwenda.
⇒ Christine kusomea sosholojia ilhali mwenendo wake ni wa kukengeuka.
⇒ Kunyoosha mkono wake alioulegeza kimakusudi kumsalimu Peter-kama htaki ilhali anataka.
⇒ Sauti ya mchuuzi aliyepaaza sauti akimsihi awanunulie watoto wake peremende na kumwambia, “shangazi wakumbuke watoto na waonee huruma”.-ukweli ni kuwa ametenda kitendo cha kikatili cha kuavya mimba.
⇒ Christine kuavya mimba ilhali hana mtoto mwingine.

Utohozi

⇒ Ofisi ya Peter
⇒ Maprofasa-wahadhiri wa chuo kikuu
⇒ Balbu-taa
⇒ Jenereta-kwa Peter-lililojiwAsha umeme ulipopotea
⇒ Wikendi
⇒ Shati-aliyovaa Peter akielekea Nairobi

⇒ Glasi
⇒ Sahani mbili nyekundu za plastiki
⇒ Springi za kitanda
⇒ Kozi-taaluma
⇒ Noti ya dola 100 yenye thamani ya shilingi 1,000,000

Tashbihi

⇒ Peter kumuuliza Christine anasomea kozi gani kama mjomba mkarimu anavyomuuliza mpwa wake.
⇒ Ulaini wa ngozi yake (peter) ulikuwa sawa na wangu.
⇒ Peter aliniongoza katika chumba chake cha kulala kama kwamba hilo lilikuwa jambo la kawaida.
⇒ Peter kuangalia noti bandia kama mwanasayansi aliyekuwa akifanya uchunguzi maabarani-umakini.
⇒ Uhusiano wetu niliuona kama kitendo cha watoto kwenda shuleni-kulazimika/kutokuwa na budi.
⇒ Mhindi alimtumbulia macho kama kwamba alikuwa mzuka-Peter akikagua noti bandia.
⇒ Baada ya kujihisi salama niliingiwa na wazo la kuwa debe bovu-kumfahamisha Peter hali yake ya hedhi.
⇒ Nilitembea barabarani kama mtembea usingizini hadi katika kituo cha matatu-akitoka kwa Peter ofisini baada ya kumwambia aliavya mimba.
⇒ Nikiwa na shahada ningekuwa kama ng’ombe wa kizungu-utamaaushi-hata akisoma, hakuna kazi ,mishahara duni, mazingira mabaya-ofisi kuukuu zilizojengwa wakati wa ukoloni.
⇒ Umati ulipasua kicheko nilichokisikia kama radi.

Mbinu rejeshi

⇒ Christine alikuwa ameokoka wakati mmoja
⇒ Kisa cha Jagtit alichoshuhudia Christine alipompa Peter noto ya dola banda aliyokuwa amepewa na mhindi mwenzake Sunja Patel.
⇒ Christine kueleza jinsi urafiki wao na Peter ulivyoanza kupitia Zac anayefanya kazi katika kampuni yake.
⇒ Zac kueleza Christine jinsi Peter alivyoenda ‘Sailing Club’ na msichana mwingine.

⇒ Kufahamishwa kuwa siku nyingi za Ijumaa jioni, Christine alikuwa anaondoka chuoni na kwenda kumtembelea Peter.

Jazanda/ Sitiari

⇒ Anwani Samaki wan chi za Joto ni Jazanda.
⇒ Samaki waliowala wale asili ni ukoloni mamboleo.
⇒ Ndoto ya Dorothy kuhusu Christine ambapo aliota siku moja Christine alikuwa akipewa sumu na wazungu-akiharibiwa maisha.
⇒ Huu ulikuwa msalaba wangu-mimba ni wajibu Christine pekee kwani hawakupanga na Peter kupata mtoto.

Sadfa

⇒ Kukutana kwa Christine na Peter kupitia Zac wanayesoma naye Makerere na anayefanya kazi katika kampuni ya Peter.
⇒ Christine kuwa kwa Peter kunasadifiana na Jagtit kumtembelea Peter kumuuzia dola. **Uzungumzi nafsia**
⇒ Wewe baradhuli, kwa nini hukusema jambo lolote la maana- Christine akitoka kwa Zac akijisuta kwa kutochukua fursa kuanzisha urafiki na Peter.
⇒ Nikweli Peter alinitaka?-Christine kujiuliza kimoyomoyo.
⇒ Kwani Zac alifikiria sikumjua Peter vyema?-anapoambiwa walienda sailing club na msichana mwingine.

Kuchanganya ndimi

⇒ ‘Penguin Classics’-vitabu vilivyokuwa juu ya dawati ya Zac.
⇒ ‘Hey man’-kasumba ya Zac kuiga Waafrika weusi.
⇒ ‘Half London’-wazungu wanakotafuta makahaba.

Takriri

⇒ Najihisi mlevi, mlevi saana-na-Miriam.
⇒ Hapana, hapana haiwezi kuwa bandia-jagtit kwa peter - kutoamini noti ni bandia.

Kicheko/tashtiti

⇒ Christine kucheka akimwambia Peter kuhusu ndoto ya Dorothy.
⇒ Peter kucheka anapoambiwa ndoto ya Dorothy na Christine.
⇒ Umati ulipasua kicheko nilichokisikia kama radi.

Chuku

⇒ Jagtit alipigwa na butwaa asiweze kuhoji kitendo cha Peter-kurarua noto bandia.

⇒ Umati ulipasua kicheko nilichokisikia kama radi-baada ya kumsikia kijana aliyempaazia Peter Sauti kuwa angeambukizwa ukimwi na Christine.

⇒ Kuwepo Entebbe Sailing Club kungemfanya awe mweusi zaidi-wengi ni wazungu.

Kejeli

⇒ Kicheko ni kejeli kwa mtu kwa kutenda kitendo cha kijinga.

⇒ Christine kusema akiwa na shahada angekuwa kama ng'ombe wa kizungu-elimu isingeboresha maisha yake.

⇒ Christine anasikia sauti ya kejeli katika kicheko cha Peter anapomwambia ndoto kikisema watu weusi ni wajinga na washirikina wakubwa.

⇒ Kijana anayempaazia Peter sauti akimkejeli Christine akisema kuwa angemwambukiza akimwi na alivyokondeana.

3. Damu Nyeusi

Maudhui

Kubaguliwa kwa watu weusi katika nchi ya Marekani

- Kuachwa na mabasi ya abiria yanayoendeshwa na wazungu katika kituo wanapokuwa peke yao kwa kufikiriwa ni majambazi.
- Kukamatwa kwa makosa ambayo watu weupe hawakamatiwi kama vile kuvuka barabara taa nyekundu zikiwaka.
- Adhabu kali kwa makosa wanayofanya-alitozwa faini ya dola 200 au miezi sita gerezani kwa kosa la kutofunga zipu.
- Mkahawani, wanatazamwa kwa dharau na wateja na wahudumu.

- Kufuatwafuatwa na walinzi madukani kwa kushukiwa wataiba.
- Kuonewa vyuoni na wahadhiri wanaotoa alama kwa kupendelea watu weupe na kukandamiza wanafunzi weusi-hawapati shahada wanan'ang'ania kula kalenda au wanakaa muda mrefu bila kuhitimu.
- Huko marekani watu weusi ndio wengi magerezani-jela imeundiwa mtu mweusi.c
- Kutazamwa kwa kudharauliwa na wahadhiri weupe.
- Kuulizwa maswali ya dharau na wahadhiri wazungu na wanafunzi weupe.
- Mikahawani kumtazamwa kwa chuki na wateja na wahudumu.
- Kutendewa vitendo visivyo vya utu kama vile Fikirini aliposahau kufunga zipu, mama mzungu alimwitia polisi ilhali angemwambia tu afunge duka.

Utovu wa utu wema

⇒ Mama mzungu kumwitia Fikirini polisi badala ya tu kumwambia afunge zipu.

Nafasi ya mwanamke

⇒ Ni Kitega uchumi kama vile Fiona ni kahaba na anamuuliza Fikirini kama angependa wafanye mapenzi.

⇒ Ni mbaguzi kwa sababu mama mkahawani anamwitia polisi kwa kutofunga zipu kwa vile ni mweusi.

⇒ Hawana utu kwa vile Fiona anataka apigwe risasi hata anataka kumkata uume (mrija).

Ujinga

⇒ Baada ya kubaguliwa na kudhalilishwa anaamua kujitoa ukiwa wake kwa kuwa karibu na watu weusi ndugu zake waathiriwa wenzake.

⇒ Fikirini kumwamini Fiona na kumfuata ilhali hamjui wala hajamchunguza.

Uzalendo

⇒ Kwa kubaguliwa, Fikirini anaanza kujithamini na kupenda asili yake.

⇒ Anaomba muda umalizike arudi nyumbani.

⇒ Tunahimizwa kuthamini utu wetu/bara letu.

⇒ Nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni.

⇒ Mtu asiyependwa na wengine sharti ajipende, ajienzi na ajionee fahari.

Ulevi

⇒ Fikirini anakumbuka jinsi walilewa waragi na chang’aa katika vitongoji duni vya Mathare.

Elimu

⇒ Fikirini ameenda marekani kusomea shahada ya uzamifu katika somo la kiingereza.

Usaliti

⇒ Mama mzungu kumsaliti Fikirini anapomwitia polisi kwa kusahau kufunga zipu.

⇒ Wamarekani weusi kusaliti Waafrika wenzao kwa hata wao kutenda vitendo vya kuwadunisha kama vile maswali ya kejeli kama Bob kumuuliza Fikirini kwa nini hakai huko kwao kwenye uchawi na washirikina.

⇒ Hata hawawasalamu watu wa asili yao.

⇒ Waafrika wamejisaliti kwa vitendo vyao viofu kama ujambazi na ndiposa wanabaguliwa na wazungu.

⇒ Wazungu wamewasaliti Waafrika kwa kuwabagua.

⇒ Fikirini amesaliti Afrika na Nchi yake kwa kwenda kusomea Marekani akiwa ameacha Vyuo huko.

Huruma

⇒ Bob anamkataza Fiona Kumkata Fikirini uume.

⇒ Hampigi risasi Fiona anapotaka afanye hivyo.

⇒ Anamrushia nguo ili asiende uchi.

⇒ Fiona ana huruma-ni katili.

Ukatili

⇒ Wa Fiona.

⇒ Waafrika kuendelezxa utamaduni wa kukeketa wanawake ili kupunguza tama ya zinaa.

Matatizo yanayokumba bara la Afrika/mambo yasiyo ya uaminifu yanayohalalisha kubaguliwa kwa mtu mweusi

⇒ Ujambazi/uporaji kama wa Bob na Fiona.

⇒ Kushindwa kupambana na umaskini-wanang’ang’ania mkono kufika kinywani.

⇒ Vita

⇒ Tamaaduni mbovu kwa mfano kukeketa wasichana.

⇒ Uchafu
⇒ Kasumba ya kudharau mtu wa ngozi yake na kuwaheshimu wazungu sana kwa kuwachukulia wote ni wa tabaka la juu.
⇒ Utovu wa maadili kama vile ujambazi na ukahaba unaoendelezwa na Fiona na Bob.
⇒ Kutojithamini kwa mfano Fikirini ameacha vyuo nchini mwao na Bob na Fiona wanaishi katika mazingira machafu.
⇒ Kushindwa kupambana na magonjwa.
⇒ Uchawi/ushirikina.

Umaskini

⇒ Watu wa Afrika kupigania mkono kufika kinywani na hivyo hawana wakati wa kufikiria kuhusu rangi.
⇒ Kuna kitongoji duni cha mathare huko Nairobi na Kibuye huko kampala.

Kasumba

⇒ Wamarekani weusi kukataa uAfrika.
⇒ Waafrika wakiwa uzunguni hawasalimu Waafrika wenzao.
⇒ Fikirini kutozwa faini kubwa na jaji mweusi.
⇒ Fikirini kuzungumza kama mmarekani mweusi ‘ Whets up men?’
⇒ Waafrika kuwaabudu watu weupe.-Fikirini kusema anAshangaa vile kwao wanavyowaabudu watu hao wasiowajali.

Ukahaba

⇒ Fiona ni kahaba na anamuuliza Fikirini ‘Do you want a good time, hapa ukumbini patatufaa.

Unyag’anyi/utapeli/ujambazi

⇒ Fiona na Bob walimtapeli Fikirini dola 300.

Uongo

⇒ Fiona kusema Bob ni nduguye.
⇒ Fiona kudai Fikirini anataka kumbaka.
⇒ Fiona kusema ana gari-‘Gari langu ni lile pale’.
⇒ Waingie nyumbani achukue ufunguo.

Unafiki

⇒ Fiona kumhakikishia Fikirini usalama wake.
⇒ Kumwambia ajihisi yuko kwake au kwao.

⇒ Kumwambia ‘You guys are our brothers’ anaposikia atoka Afrika.

Ndoa

⇒ Wamarekani hawajui kutunza ndoa.

Heshima

⇒ Fikirini kupita bila kumgusa Fiona akiingia kwake.

Upyaro

⇒ Bob kusema Waafrika ni wajinga na wenye ushirikina.

⇒ Kumwita Fikirini fala.

kejeli

⇒ Je, kule kwenu watu huvaa nguo au hutembea rabana?

⇒ Je mwaishi mitini kama tumbiri?

⇒ Mbona hambaki kwenu huko kwenye uchawi na ushirikina-Bob.

⇒ Huu weusi wenu unaozidi kiza unatokana na kuangukiwa na lami au kupigwa na mionzi ya jua?

⇒ Ni upi mji mkuu wa Afrika.

⇒ Mtu anaugua ukimwi malaria na polio na utapia mlo huko Afrika?

⇒ Mbona hamwachi kupigana nchini kwenu?

⇒ Nani anataka kuuona uchi wako?

⇒ *You,* wataka kumbaka dadangu kwa nini?

⇒ Nini kinawatoa Afrika kuja kutusumbua hapa marekani?-Bob-kasumba

⇒ Fala kabisa twawezaje sisi kuwa ndugu na tumbiri kama nyie-Bob-kasumba.

⇒ Mbona hambaki kwenu huko kwenye uchawi na ushirikina wenu?-Bob-kasumba

Balagha zaidi

⇒ Mambo ya aibu kama haya unaweza kuwaelezea ndugu zako nyumbani?-kisa cha kutofunga zipu.

⇒ Sasa polisi gani angejua kiingereza kuliko mwanafunzi wa uzamifu katika somo la kiingereza katika chuo kikuu?

Chuku

⇒ Huu weusi wenu unaozidi kiza unatokana na kuangukiwa na lami au kupigwa na mionzi ya jua?

⇒ Mtu sharti avae safu ya maguo pamoja na viatu, viatu vizito kama vya wanajeshi wan chi kavu.-wingi wa baridi.
⇒ Hakuhisi mzizimo wa theluji iliyokuwa inaanguka kama matone ya mvua ya mawe.-anapoambiwa atoke kwa kina Fiona na Bob. Haja ni kunusuru maisha yake.
⇒ Jibaba la miraba mine-Bob.
⇒ Jimama lililofungAsha si haba-Fiona.
⇒ Kila kitu cheupe katika nchi hii,mtu mweusi apate wapi sauti na satua-kutilia mkazo ubaguzi wa Waafrika.
⇒ Alikuwa pandikizi la jimama-Fiona
⇒ Hata akilewa gongo,waragi au chang'aa kiasi cha bahari ya hindi hawezi sema kisa cha zipu kwa aibu.
⇒ Huu weusi wenu unaozidi kiza unatokana na kuangukiwa na lami au kuchomwa na mionzi ya jua?
⇒ Kijasho chembamba kikaanza kumtoka kipajini na kwapani-kusisitiza uoga Fikirini anapogusa mlango kwa Fiona na kukuta umekomelewa.
⇒ Akaumimina mkojo kwenye sakafu ya ukumbi kutokana na hofu-kwa kuonyeshwa mtutu wa bunduki na Bob.

Takriri

⇒ Mtu sharti avae safu ya maguo pamoja na viatu, viatu vizito kama vya wanajeshi wan chi kavu.-kusisitiza jinsi baridi ilivyo nyingi.
⇒ Alijotosa nje tuputupu kama alivyozaliwa-bila nguo akitoka kwa Fiona.
⇒ Tabasamu ilikutana na tabasamu-Fikirini akichekesha Fiona.
⇒ Fikirini kuzoa nguo na kukimbia tuputupu kama mtu aliyepagawa pepo mbaya.

Theluji kufunika kila ncha na kujenga mandhari nyeupe nyeupe.

Tashbihi

⇒ Mtu sharti avae safu ya maguo pamoja na viatu, viatu vizito kama vya wanajeshi wan chi kavu.
⇒ Mambo mengine yanakuwa kama ndoto au jinamizi-kisa cha mkahawani.
⇒ Akitetemeka kama majani ya mgomba kwenye dhoruba.

⇒ Fikirini kuzoa nguo na kukimbia tuputupu kama mtu aliyepagawa pepo mbaya.
⇒ Ananyapia nyapunyapu na kupepesuka pepesupepesu kama mlevi chakari.
⇒ Ananyapia nyapunyapu na kupepesuka pepesupepesu kama mlevi chakari-akielekea chuoni baada ya kuachwa na basi.
⇒ Fikirni alisihi akilia machozi kama mtoto mdogo-Fiona anaposema ‘I say shoot him Bob’.
⇒ Theluji kufuniaka kila kitu kama blanketi la unga.
⇒ Hakuhisi mzizimo wa theluji iliyokuwa inaanguka kama matone ya mvua ya mawe.

Taswira

⇒ Mtu sharti avae safu ya maguo pamoja na viatu, viatu vizito kama vya wanajeshi wa nchi kavu.
⇒ Mikononi kafunika vitanga na vidole kwa glavu nyeusi.
⇒ Theluji kufunika kila ncha na kujenga mandhari nyeupe nyeupe.
⇒ Jimama lililofungAsha si haba-Fiona-mnene.
⇒ Jibaba la miraba mine lililokuwa limevaa miwani ya jua-Fiona.
⇒ Maguo machafu yametapakaa kiholela sakafuni, vumbi limetapakaa kwenye kochi.-uchafu kwa Fiona na Bob.

Utohozi

⇒ Glavu-za kuzuia baridi.
⇒ Dola-alitozwa faini ya dola 200 kwa kutofunga zipu na kuporwa dola 300.
⇒ Faini
⇒ Hana makadi yake mbalimbali-baada ya kuporwa.

Kinaya

⇒ Fikirini kushikwa kwa kutofunga zipu ilhali wanawake huko hawashikwi licha ya kutembea bila nguo.
⇒ Polisi kumuuliza kama anafahamu kiingereza ilhali anakifahamu hata kuliko wao kwani anakisomea.
⇒ Kusema jaji mweusi alikuwa na imani kwa kumtoza faini ya dola 200.

Nyani haoni kudule-kasoro
Kuchanganya ndimi

⇒ Sarafu kadha za quarter-robo kadha za dola.
⇒ How you doing?-Fiona.
⇒ Someone called to say you are exposing yourself-polisi.
⇒ Am cool-Fikirini-kasumba.
⇒ Come fast this dude wants to rape me-uongo wa Fiona.
⇒ Do you speak English-polisi.
⇒ I say shoot him Bob-ukatili wa Fiona.
⇒ Get out of here-Bob akimfukuza Fikirini baada ya kumpora.

Sitiari

⇒ Kisiwa cheusi kwenye bahari ya weupe-Fikirini pekee ndiye mweusi darasani.

Tashhisi

⇒ Rangi mbili zinazokinzana na kufarakana –taswira ya Fikirini kuhusu vita vya watu weusi na weupe.
⇒ Wanawake wenu hawapendi nguo tena zimewachosha na kuwachusha.
⇒ Bado baridi inapenyeza na kuteketeza vyanda.

Mbinu rejeshi

⇒ Anavyotukumbusha jinsi alivyoepuka jela wakati alienda mkahawani baada ya kula akaingia msalani akasahau kufunga zipu.
⇒ Kukumbuka maneno ya Moi.
⇒ Kukumbuka siku walilewa waragi katika vitongoji duni-Kibuye-Kampala na Mathare-Nairobi.
⇒ Fikirini akilia anakumbuka kifo cha mamake akiwa katika shule ya upili.
⇒ Tunaarifiwa Fikirini mara mbili ametozwa faini na polisi.
⇒ Kukumbuka mara ya kwanza alipokwenda darasani jinsi yeye pekee alikuwa mweusi.

Taharuki

⇒ Fikirini alimaliza masomo yake au alikula kalenda?
⇒ Nini kinawafanya wamwangalie vibaya akitoka msalani?
⇒ Ilikuwaje alipofika chuoni bila vifaa hata kadi-vitambulisho?

Nahau

⇒ Kutia na kutoa kidogo-Kusitasita na kukataa anapoambiwa aingie na Fiona.

⇒ Funga duka-zipu.
⇒ Akachutama na kumwomba amwonee imani-amhurumie-Fiona anapopeleka kisu kwenye kinena cha Fikirini akitishia kumkata mrija.
⇒ Ajionee fahari-ajijivunie.
⇒ Alipopiga darubini nyuma alimwona mama mzungu kama hasidi-alipokumbuka.
⇒ Kula kalenda-kukaa miaka mingi bila kufuzu.
⇒ Fikirini amekaziwa macho vibaya-kuangaliwa vibaya kwa kutofunga zipu mkahawani.
⇒ Likija basi lingine na ambalo usukani wake umeshikwa na dereva mweupe mwenye mwoyo mweusi (mwoyo mbaya) yamkini mambo yatakuwa yale yale.
⇒ Maji yamezidi unga-baada ya kuambiwa na Fiona wawe na *good time*-ukahaba.

Tanakuzi

⇒ Likija basi lingine na ambalo usukani wake umeshikwa na dereva mweupe mwenye mwoyo mweusi yamkini mambo yatakuwa yale yale.
⇒ Anatamani arudi kwao na kufaidi utajiri wa umaskini wao ajitenge na umaskini wa utajiri wa marekani.
⇒ Faraja ya wazungu ni kuona ndugu zake weusi wananyanyasika katika mfumo unaomtweza mweusi na kumkweza mweupe

Methali

⇒ Nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni-uzalendo.
⇒ Simba akikosa nyama hula nyasi-Fikirini kutopendelea chakula cha marekani na kulazimika kukila kwa kukosa aina nyingine.
⇒ Usipopendwa jipende-kuhimiza watu kujithamini.
⇒ Leo ni siku ya nyani kufa na ambapo miti yote huteleza-hakuna jambo lake linalofaulu.

Kicheko

⇒ Fikirini kucheka kauli ya Moi akidhani haina mashiko.

Tabaini

⇒ Si kuta, si majani, si matawi-kuonyesha taswira ya theluji kufunika kila mahali.

Majazi

⇒ Fikirini-kujisaili kufikiri zaidi kabla ya kwenda ng’ambo.

Mdokezo

⇒ Siku ya kufa, kifo cha aibu na nguo amevuliwa…

⇒ I say remove your clothes or else…

4.Glasi Ya Mwisho Makaburini

⇒ Hao marafiki kunywa pombe ya mwisho huko.

⇒ Kutopenda kwenda tena katika baa ya makaburini/mavani baada ya kuvamiwa na majambazi.

Maudhui

Mapuuza

⇒ Semkwa, Asha na Josefina kupuuza ushauri wa Msoi wa kutoenda katika baa ya mavani kwa kuhisi jambo baya lingetokea.

Woga

⇒ Baada ya kuvamiwa na majambazi katika baa, Asha kutoa ukwenzi mkali, ukwenzi ukafuatwa na ukwenzi, na kwenzi zikawa mjumuiko wa zogo na ghasia.

⇒ Kuna walioshangaa na kukodoa macho na kung’ang’ania kama masanamu.

⇒ Msoi kukaa akiwa ameangalia mavani.

Itikadi/ushirikina/utabiri/uotaji/ubashiri

⇒ Hisia zinazomfanya kutabiri maovu.

⇒ Msoi anatazamia balaa kubwa litatokea katika baa ya mavani.

⇒ Semkwa Asha na Josefina hawaamini ushirikina.

Ujambazi/uhalifu

⇒ Majambazi walijifanya vizuu na kuibia baa la makaburini na wateja wake kila kitu.

Anasa

⇒ Semkwa, Msoi, Asha na Josefina wanapenda ulevi na burudani.

⇒ Watu wanakwenda katika baa ya mavani kustarehea maisha ya dunia.

Tahadhari

⇒ Msoi ni mwenye tahadhari kwani siku ya mavamizi anakaa akielekea huko makaburini ili kukitokea kama alivyotabiri aweze kujinusuru.

Ukwasi

⇒ Msoi na Semkwa wana pesa hata Semkwa ana gari.

Mapenzi ujanani

⇒ Msoi na Semkwa wana wapenzi Asha na Josefina na wanakwenda kustarehe nao.

Ulevi

⇒ Baa ya mavani

Ushawishi /upotoshwaji na marafiki

⇒ Semkwa anamshawishi Msoi waende katika baa ya mavani wakati alikuwa amekataa.

Udhabiti wa msimamo

⇒ Msoi hana udhabiti wa msimamo na ndio sababu ya kushawishiwa na Semkwa kurudi mavani.

Matumizi ya lugha

Tashhisi

⇒ Kisha hisia humwotesha ndoto.

⇒ Ncha za malaika yake kusimama kama kijiti.

⇒ Leo hisia hiyo kali ilikuwa imeumuka haraka kama hamuri lililojazwa hamira.

⇒ Hutaki kuiacha(imani) ijapokuwa unajua haina haki ya kuketi wala kusimama katika maisha yetu ya kisasa ya sisi vijana yanayoendeshwa kisayansi.

⇒ Vinywaji vyake ni vya kupoza joto la wiki nzima.

⇒ Harufu za mafuta ghali na ya fahari zilikuwa zimekazana kuzikalia juu harufu za vyakula, vinywaji na za maua.

⇒ Harufu kali ya vundo la maiti ilivamia baa na kuzifurusha zile harufu nzuri za maua na manukato ya vyakula.

⇒ Vitu tawanyika, glasi na sahani anguka na vunjika-kuonyesha zogo na ghasia.

⇒ Roho yake mwaguzi inamwambia apaambae apakimbie.

⇒ Kinywaji kilipotua juu ya meza jamaa walinyanyua glasi zao-kilipowekwa.

⇒ Hata mwezi na nyota zimeshuka kidogo kuja kuimarisha furaha yetu.

⇒ Njiani Mbingu ghafla ilikasirika ikafinga uso wake mweusi kisha ikapasua mkonyezo uliotoa ufa mwembamba wa moto mwekundu na fedha, ilifanya hayo

mara moja tu tena bila kutiririsha hata tone moja la **chozi**-mvua-ishara mbaya kwa Msoi.

⇒ Ama kweli itikadi na ushirikina vimekudhibiti kwelikweli.

⇒ Wanapoenda wikendi ni pa wafu na wafu wakiwa mapumzikoni wamechoshwa na kukerwa na siku yoyote ile wangefanya kitu kujihami-itikadi za kishirikina.

⇒ Imani yako imekutawala-Semkwa kwa Msoi.

Taharuki

⇒ Nini kinamfanya Semkwa kutumbua macho?

⇒ Baa iliendeleza huduma baada ya kuvamiwa na majambazi?

⇒ Marafiki hao walirudi tena huko?

⇒ Majambazi hao walijulikana?

Kuchanganya ndimi

⇒ Exotic resort-Msoi anavyopaita baa ya mavani.

⇒ u-exotic

⇒ thriller-wimbo wa Michael Jackson.

Mbinu rejeshi

⇒ Msoi alikuwa amenasa hisia fulani ya kitisho na wasiwasi.

Tashbihi

⇒ Na wewe sharti unigande mimi kama kupe-Msoi kwa Asha anapomshinikiza ale.

⇒ Ukiwa umestarehe kama vile uko peponi.

⇒ Umebaki kulala kochini kama mgonjwa wa malaria?

⇒ Jozi mbilimbili, minenguo, mikatiko, mibenuko, miondoko, mitetemeko kama wagonjwa wa malaria, mtiririko wa jasho kama maji ya mlizamu wa mto.

⇒ Kuna walioshangaa na kukodoa macho na kung’ang’ania kama masanamu.

⇒ Utabakije juu ya kochi kama mgonjwa wa homa na leo ni jumamosi?

⇒ Ukiwa hapo unastarehe kama vile uko peponi mbali na adha za dunia ambako kwa tafsiri ni motoni-sitiari-uzuri.

⇒ Anatutisha kaka, anatutisha sisi kama watoto wadogo, anatutisha kaka-Msoi anapowaambia wataona.

Kejeli

⇒ Si baa mshenzi ya pata sote.

⇒ Bwana huyu naye utadhani haishi karne ya ishirini na moja-Josefina.
⇒ Anataka kutuvunjia raha zetu kwa ndoto zake za ajabu ajabu-takriri.
⇒ Kwani unatutabiria nini hasa bwana ndoto?

Utohozi

⇒ bendi hai ye msegeju-inayotumbuiza wateja.
⇒ Petroli-kinywaji ni petroli ya muziki.
⇒ kauntani-ambako wahudumu wanaenda kuchukua vinywaji.
⇒ glasi-bilauri
⇒ maisha yetu ya kisasa ya sisi vijana yanayoendeshwa kisayansi
⇒ wikendi
⇒ televisheni-waliyofungua Asha na Msoi na kupata habari-vizuu vilikuwa majambazi.
⇒ kochi-coach
⇒ swichi-ya gari la Semkwa
⇒ baa ya mavani

Sadfa

⇒ Imani ya Msoi wafu wangejitokeza kusadifiana na majambazi kujifanya vizuu na kuvamia baa.
⇒ Usiku wa mavamizi walikuwa wametembelea ile baa.
⇒ wimbo taribi kuimbwa.

Balagha

⇒ Una nini Msoi leo?
⇒ Radi ngapi zimepiga tokea dunia kuumbwa?
⇒ Mimweso mingapi imeemeta tokea mbingu kutandazwa na muumba?
⇒ Kipi cha ajabu kitakachomfanya mtu awe na hofu?
⇒ Imani yako imekutawala vile vile au siyo?
⇒ Leo Msoi umebadilisha makao? –tahadhari.
⇒ Umeona ukalie kiti kitakachokupa mandhari ya mava?-Asha.
⇒ Kwani ndiko yatakakozuka mazingaombwe unayoyatabiri?

⇒ Hofu hiyo itoke wapi katika usiku huu mwema uliojaa furaha na utukutu wa ujana-Msoi-kinaya-usiku haukuwa mzuri.
⇒ Wewe utakunywa maji kama mtoto mpaka lini?-Asha.

Ishara

⇒ Mamaya yangetokea
⇒ Mbingu
⇒ Mawingu mazito meusi
⇒ Radi
⇒ Msoi kuzitazama taa na kuziona zilikuwa na mwako wa huzuni.
⇒ Umeme-ishara ya mabaya.
⇒ Baadaye ukope wa mwezi ulistawisha uzuri wake wa fedha katikati ya vipuli vilivyokuwa vikipwitapwita-ishara ya raha kutangulia balaa.

Takriri

⇒ Duru kwa duru
⇒ Utapiga tena na tena
⇒ Anatutisha kaka, anatutisha sisi kama watoto wadogo, anatutisha kaka-Msoi anapowaambia wataona.
⇒ Ukwenzi ukafuatwa na ukwenzi na kwenzi zikawa mjumuiko wa zogo na ghasia.
⇒ Mziki ulikuwa ukitumbuiza chini kwa chini.
⇒ Msoi na Semkwa walifika baa ya makaburini wakati mzuri, wakati mambo ndio kwanza yaingie sura-yatengenee, yawe mazuri.
⇒ Msoi na Semkwa walikaa na kutazamana uso kwa uso-Msoi akelekea mavani-tahadhari.
⇒ Furaha, furaha, furaha imechanua raha, raha, raha.

Taswira

⇒ Majambazi waliojifanya vizuu-kundi la vizuu limejifunga kwa mtindo wa thriller wa mchael Jackson, linakuja kule baa kwa kujikongoja na kujitetemesha na kutoa sauti za kiufu, nyuso nyeupe kama chokaa, mabufuru ya vichwa yanayoning’inia hewani mabango ya nyuso yenye matundu yaliyopoteza macho na pua baadhi vimesongwa sanda vingine mwili mtupu.

⇒ Chakula kilikuwa ndizi za nazi pandikizi la changu wa kukaangwa pembeni na kachumbari ubavuni.

Chuku

⇒ Upeo wa raha hausemeki umekunjuliwa wazi kwa watu hawa wao wenye pesa kuukanyaga mwanzoni bila ya kufika mwisho.

⇒ Kwa muda mfupi mziki ukawa juu ya kila kitu.

⇒ mtiririko wa jasho kama maji ya mlizamu wa mto-kwa kusakata ngoma.

⇒ Hakucheza mpaka muziki ukamwingia damuni kama mwenyewe asemavyo kila siku.

⇒ Hakucheza kwa mizani ya kuchokora ndani mwili wake ili upoteze mifupa wakati wa kucheza.

⇒ Msoi kutumbua macho mpaka yakaonekana yanataka kudondoka chini kutoka vibakuli vyao-anapoona vizuu.

⇒ Msoi na Asha kukimbia bila kutazama nyuma na bila kusita pahala popote.

Mdokezo

⇒ Yaani umegoma…

⇒ Si mimi wala si wewe tunaoamini kwamba watu wafu wapo ndani ya dunia hii…

⇒ Si mimi wala si wewe tunaoamini kwamba watu wafu wapo ndani ya dunia hii… -tabaini

Nidaha

⇒ Lo, wale vizuu-Msoi akitania.

⇒ He! Saa mbili na nusu hujajitayarisha-Semkwa.

Tanakuzi

⇒ Mavani ni pahala pa wafu sisi sote tulichokuwa tukikiona ni kwamba mavani ni pahala pa watu hai.

Nahau

Nahau

⇒ Anaona kuna kitu kinaliza ndege mbaya-kutabiri maovu.

⇒ shingo upande, moyo mzito-Msoi akiamka kwenda kujitayarisha-bila kitaka-kujilazimisha,wasiwasi

⇒ Wakati tayari kung’oa nanga-kuanza safari kuelekea baa.

⇒ Msoi na Semkwa walifika baa ya makaburini wakati mzuri, wakati mambo ndio kwanza yaingie sura-yatengenee, yawe mazuri.

Kinaya

⇒ Hofu hiyo itoke wapi katika usiku huu mwema uliojaa furaha na utukutu wa ujana-Msoi akijijasirisha.

⇒ Mwezi na nyota zimeshuka kidogo kuja kuimarisha furaha yetu leo-usiku haukuisha kwa furaha.

⇒ Na tunywe tujikinge na vizuu na mashetani ya makaburini-pombe haiwezi kuwakinga.

Mbinu rejeshi

⇒ Miaka saba iliyopita walikuwa wamekataa kwenda baa ya mavani josefina akawAshawishi

⇒ Televisheni-matangazo ya yaliyotokea katika baa.

⇒ Semkwa kupiga simu na kueleza jinsi walivyokamatwa na majambazi na kuibiwa kila kitu, pesa, nguo, viatu hata na chupi.

Kicheko

⇒ Sekwa kumshika mkono Msoi anapopepesuka na kutaka kuanguka.

⇒ Wote wakaangua kicheko kabla ya kunywa.

Koja

⇒ Wakala, wakanywa, wakamaliza.

⇒ Jozi mbilimbili, minenguo, mikatiko, mibenuko, miondoko, mitetemeko kama wagonjwa wa malaria, mtiririko wa jasho kama maji ya mlizamu wa mto.

5.Kikaza

⇒ Suruai ya ndani ya aina ya pekee.

Maudhui

Uongozi mbaya na athari zake

⇒ Bwana Mtajika ni kiongozi asiyewajibika- hawezi kulinda kikaza kimepasuka.

⇒ Kwa mtajika mambo yalitendeka kindoto-kauli tupu zisizotekelezwa-ahadi za maneno.

⇒ Ni kiongozi asiyeshughulikia maslahi ya wanatekede, daima yumo ndotoni (chuku)-mwenye mapuuza.

⇒ Madharau/mapuuza-Pima kusema ‘Mimi hufanya kazi yangu kikamilifu (kinaya) lakini sithaminiwi. Kila mara tumedharauliwa, tumepuuzwa na kutothaminiwa na wengine wetu.

⇒ Hawaondoi shida za wananchi baada ya kuchaguliwa-Hali huzidi kuwa mbaya si njaa, si magonjwa wala ufukara, uchochole huzidi-Bi. Chirenga-Cherehani.
⇒ Wanaacha wake wao uongozi na hawawadhibiti.
⇒ Husahau waliowachagua-wepesi wa binadamu kusahau wema na badala yake kukumbuka mabaya.

Ubarakala

⇒ Wadanganyifu-Machupa msemaji wa kijiji anabadilisha uongo kuwa ukweli na ukweli kuwa uongo-kutetea viongozi waovu.-ubarakala.

Ubinafsi

⇒ Machupa kuunga mkono hoja zinazomfaidi na nyingine kuzipinga.
⇒ Hata baada ya serikali kupinduliwa, Machupa alijua namna ya kuishi na hivyo hakuogopa chochote.-angebadili msimamo wake.

Uwajibikaji

⇒ Wananchi hukosa uwajibikaji katika kuchagua kiongozi anayefaa.
⇒ Viongozi kushonewa kikaza kwa ushirikiano wa umma – Wote ni washiriki katika ushonaji wa kikaza.
⇒ Hawachuji wanaotaka kuwapa uongozi, balala yake huwachagua kwa misingi ya ulumbi/umaarufu katika usemaji.
⇒ Wanapaswa kuwachagua kwa uwezo wa vitendo/kutekeleza ahadi.
⇒ Wengi WA wananchi hawaelewi uzito wa ushirika wao katika kushona kikaza (kuchagua kiongozi).
⇒ Uongozi mzuri unawategemea kwa hivyo wamchunje kiongozi vizuri.
⇒ Wana wajibu wa kuwaambia viongozi ukweli k.m. Babu, Cherehani na Pima.

Mapinduzi /ukombozi/Uzinduzi/uchochezi

⇒ Bi. Cherehani kufafanulia wanakijiji chanzo cha tatizo la ukosefu wa mvua.-ujasiri.

⇒ Bi. Cherehani kuwachochea watu waende katika ikulu wakashone kikaza kingine-kung'oa Bwana Mtajika na Bi. Mtajika mamlakani.
⇒ Wanatekede kuelekea katika ikulu ,Bwana Mtajika alitokea mlango wa nyuma naye Bi. mtajika akabebwa taratibu pamoja na kitanda chake akawekwa nje.

Busara

⇒ Wanakijiji kwenda kwa mzee babu kupata majibu ya masuala yanayowatatiza.
⇒ Wakati mwingine angewarushia maneno ya hapa na pale lakini yenye wingi wa hekima.
⇒ Anawapa ushauri-si kila panapo mawingu meusi mvua hunyesha.
⇒ Uchafuzi wa mazingira-mawingu mengine meusi hutokana na **mmchafuko wa mazingira**.

Ukarimu

⇒ Kila aingiaye kwa mzee babu hatoki bila kunywa angalau kikombe cha maji.
⇒ Wanakijiji wanatoa sehemu ya mavuno yao kwa mzee babu-umuhimu wa kuwatunza wazee katika jamii.
⇒ Babu anatumia **vizuri /kutunza/kuhifadhi** chakula anachotunukiwa na wanakijiji na wakienda kwake anawakirimu kwa chakula kicho hicho.

Nafasi ya mwanamke

⇒ Waiga utamaaduni wa kigeni na watovu wa maadili-wasichana wa siku hizi utawakuta wamevuta kikaza juu kwa makusudi ili macho ya wanaume yalimbuke.
⇒ Hapewi uongozi-nadra sana kiongozi kuwa mwanamke katika jamii ya Wanatekede.
⇒ Anayemdhibiti mumewe
⇒ Pumda wa huduma-Bi. Cherehani.
⇒ Waingilia uongozi –Bi. Mtajika kujiweka katika uongozi. Hata katika sherehe rasmi husahau kuwa yeye ni mkewe Bwana Mtajika .
⇒ Wanaowadhibiti waume wao-Bi. Mtajika.
⇒ Wanaojigamba- Bi. Mtajika kusema hakuna kiongozi mwingine kumshinda yeye. –majivuno.

⇒ Jasiri- Bi Cherehani kunena ukweli kuhusu viongozi na kuwachochera wananchi.
⇒ Wabinafsi-Bi. Mtajika kuwanyima wengine nafasi ya kuongea. ,

Utovu wa maadili
⇒ Wakati Bi. Cherehani anatabasamu, wengine mate yanawandondoka-kutamaani mwili wake, wakatamani ya ziada-tafsida.
Umakini/utaratibu
⇒ Mzee babu kutafuna muwa polepole na kwa ufundi mkubwa hadi kumaliza kipande chake.
Matumizi ya lugha
Taharuki
⇒ Baada ya mtajika na bibiye kuondolewa madarakani nani alipewa uongozi?
⇒ Aliyechaguliwa aliongoza vizuri?
Nidaha
⇒ Lo! Haitanyesha.
⇒ Naam,haya ndivyo yalivyo mambo-Pima kuhusu jinsi Bw. Mtajika alivyovunja masharti ya kikaza.
Majazi
⇒ Bwana pima-kupima kikaza.
⇒ Bi. Cherehani –kushona kikaza.
⇒ Machupa-kutokuwa na tabia nzuri-uduma kuwili, ubinafsi.
⇒ Bw. na Bi. Mtajika-kufahamika sana kwa sababu ya uongozi.
Jazanda
⇒ Kikaza-uongozi, madaraka, serikali.
⇒ Kikaza hakipaswi kushikwa kwa namna yoyote ile na mwenziwe kiongozi wa jinsia hiyo nyingine-asiingilie uongozi kwani siye alichaguliwa.
⇒ Washona kikaza –wananchi wanaowachagua vongozi. kumuweka kiongozi madarakani ni jukumu la watu wote.
⇒ Mvua nzito kunyesha baada ya wanajamii kumwondoa mtajika na bibiye madarakani-nchi kupata maendeleo au ufanisi.

⇒ Uzi na shindano za kushonea kikaza-katiba/sheria ambayo kwayo nchi huongozwa.
⇒ Kukiuka maadili ya kikaza-kiongozi kumwacha mkewe kuwa na madaraka makubwa kama kwamba yeye ndiye kiongozi.
⇒ Kushona kikaza kingine-kuchagua kiongozi mwingine kwa kura.
⇒ Mawingu bila mvua-uongozi usioleta maendeleo au usiobadili hali ya wananchi.
⇒ Kutonyesha kwa mvua-matatizo ya wananchi k.v. njaa, magonjwa, umaskini n.k.
⇒ Kijiji Tekede-nchi za Afrika-zinazoendelea.
⇒ Kikaza kupasuka-kiongozi kushindwa kutimiza majukumu yake au kutowajibika kwa kiongozi.
⇒ Hurafa-safari ya kwenda mbinguni ya kobe na ndege
⇒ Kwenda mbinguni-kupata ufanisi au maendeleo/ustawi
⇒ Kobe-kiongozi
⇒ Ndege-wananchi
⇒ Ndege kumpa kobe mabawa-wananchi kumchagua kiongozi ili awaondolee matatizo na alete maendeleo.
⇒ Kope kujipa jina ‘sisi wote’ na kukalia vyakula vilivyoletwa na kuwakumbusha ni vya ‘sisi wote’ - kuonyesha ubinafsi wa viongozi au ku kujilimbikia mali wakipuuza waliowachagua.
⇒ Kobe kuwapa wenzake wanaomfaa chakula - kiongozi kuleta maendeleo katika maeneo waliyochaguliwa-mapendeleo.
⇒ Ndege kuchukua manyoya yao -wananchi kumng’oa kiongozi mamlakani.
⇒ Siku ya tano- kiongozi kuchaguliwa kwa kipindi cha kwanza cha miaka mitano na muda huo huisha bila kuleta maendeleo yoyote.
⇒ Upepo kuchukua na kubeba mawingu kuelekea kila upande mbali na kijiji-mapuuza hata mambo nyeti na kutowajibika kwa kiongozi kukosesha nchi maendeleo
⇒ Jua lililokuwa limeshika kasi kuelekea mapumzikoni kama kwamba linatoroka mvua lilipata nafasi ndogo ya kuwaaga wanakijiji kwa siku hiyo-kutokeza tena baada ya

mawingu kupeperushwa na upepo-shida kurejelea tena kwa viongozi kutowajbika.

Mbinu rejeshi

⇒ Bw pima kukumbusha jinsi miaka miwili iliyokuwa imepita jinsi Bw. Mtajika alivunja masharti ya kikaza na wao kumhurumia.

Msemo

⇒ Walijitahidi lakini hata jitihada hufika kikomo.-kuchoka kumsitiri Mtajika kwa aibu yake.

⇒ Binadamu ni mwepesi wa kusahau wema-hukumbuka tu mabaya-kiongozi kusahau waliomchagua.

⇒ Bi chereani na Bwana Pima kuacha chungu kinatokota bila kuivisha chakula-watu wakiwa na hamu kubwa ya kufumbuliwa fumbo.

⇒ Wenye vyao na vya wengine-viongozi kujilimbikia mali.

⇒ Pole kwa wala jasho lao-wanaopata riziki kutokana na kazi za mikono yao.

⇒ Mapenzi kikoozi-mapenzi mtajika aliyonayo kwa mkewe kumfanya ashindwe kumdhibiti.

Tashbihi

⇒ Yanapozidi (mapenzi) huja kama nguvu za sunami-kutodhibitika.

⇒ Machupa hutafuna na hupuliza kama panya.-hula kuwili.

Nahau

⇒ Kumbe alitonesha kidonda-kukumbusha mambo yaliyokwisha na kusahaulika.

⇒ Tunaendelea kufanya kazi hii kwa nyoyo zote-jinsi wananchi wanavyojitolea kabisa kuchagua viongozi.

⇒ Gonga ndipo usitusimulie hadithi-sema wazi.

⇒ Wamemla mbuzi mzima na mkia utawashinda-kukamilisha kutegua kitendawili cha mawingu bila mvua.

Takriri

⇒ Kikaza kikaza ni cha ushirika

⇒ Mambo yana mambo yake

⇒ Ndio mtindo na sisi tunafuata mtindo

⇒ Machupa msemaji wa kijiji anabadilidha uongo kuwa ukweli na ukweli kuwa uongo

Tabaini

⇒ Si njaa, si magonjwa, si chochote kinachoniambaa-madhila ya wananchi
⇒ Si salamu, si chochote, hakuna kilichotoka kinywani-pima akijizuia kuongea ukweli.

Mdokezo

⇒ Mwafahamu katika safari ya angani namna ndege walivyoshirikiana naye…
⇒ Siri ilikuwa siri…iliwekwa na watu wawili ikahifadhika

Kinaya

⇒ Mawingu mazito mfululizo kwa siku tano hayakuleta mvua
⇒ Siri ilikuwa siri, iliwekwa na watu wawili ikahifadhika-hakuna siri ya watu wawili
⇒ Bi. Cherehani mwenye wingi wa soni kuweza kuongea mbele ya watu na kuwachochea.
⇒ Wanakijiji kuamini waliposhiriki hapakuwa na dosari yoyote
⇒ Kiongozi huyu alitafuta uongozi kwa muda mrefu-Kibaki

Tashhisi

⇒ Upepo kuchukua na kubeba mawingu kuelekea kila upande mbali na kijiji-mapuuza hata mambo nyeti na kutowajibika kwa kiongozi kukosesha nchi maendeleo
⇒ Jua lililokuwa limeshika kasi kuelekea mapumzikoni kama kwamba linatoroka mvua lilipata nafasi ndogo ya kuwaaga wanakijiji kwa siku hiyo-kutokeza tena baada ya mawingu kupeperushwa na upepo-shida kurejelea tena kwa viongozi kutowajbika.
⇒ Jibu lao kuibua maswali zaidi na kuzalisha kitendawili kingine
⇒ Ukweli ulijisukuma kwa nguvu ukafungua kinywa ambacho kwa siku chache alitembea akiwa amekiziba kwa mkono wa kushoto-pima kutovumilia kunyamazia ukweli tena
⇒ Hamjui ukaidi wa mkia wa mbuzi?
⇒ Ya kumsukuma Bi. Cherehani kiasi hiki lazima yawe mazito-ya kumlazimisha kusema lazima yawe ya muhimu sana.

Chuku

⇒ Kila njia ilielekea kwa mzee babu-kuonyesha jinsi walioelekea kwake walikuwa wengi
⇒ Pima akajizoazoa akapata nguvu, ama ni kutokana na uzito ambao ungepasua moyo wake-kutovumilika.
⇒ Lakini tenda lolote baya hata kama ni kuuza nzi basi litakuwa wimbo-kusisitiza usahaulifu wa mema binadamu anayotendwa na badala yake kukumbuka mabaya.

Koja

⇒ Lolote baya, litaimbwa, litachezwa ukumbini, litapandwa, litamea, litapaliliwa, litakua na hata kuvunwa.
⇒ Bwana pima aligundua namna ukweli unavyoweza kuumiza, kuchoma, ukandamiza na hata kunyonga.
⇒ Bi mtajika alijulikana. Hushangaza, akakasirisha, akaudhi.
⇒ Chaguo lilikuwa la kila mmoja ,ama kula, kumeza au kubugia-wanaoenda kwa babu

Balagha

⇒ Hamjui ukaidi wa mkia wa mbuzi?
⇒ Kwani sisi tulimchagua nani?
⇒ Amesema nini? –watu kuchanganyikiwa kwa kutoelewa babu aliyosema.
⇒ Nyote mu washiriki katika ushonaji wa kikaza itakuwaje sisi wawili tuwe na jibu la swali lenu?
⇒ Bwana kiongozi mbona siku hizi husemi? Haongei ili kusuluhisha hata mambo nyeti-hatoi ufafanuzi wowote hata Bi mtajika anaposema hakuna kiongozzi mwingine kushinda yeye.
⇒ Wangapi walio na ujasiri wa kunena ukweli hasa unapohusu uongozi?

Methali

⇒ Waliishi katika msemo wa nyani haoni kudule-wananchi kasoro la chaguo lao la kiongozi
⇒ Mapenzi ni kikohozi-mtajika kushindwa kudhibiti mkewe kwa ajili ya mapenzi.

6.Maeko

⇒ Mambo yanayomuweka mtu mahali
⇒ Mapenzi ya dhati ya Hamduni ndiyo yanamuweka jamila kwa Hamduni k.v. kumpikia, kumfulia nguo, n.k.
⇒ Hayo ndiyo maeko aliyowekwa huyu mwanamke. Alijikuta akistahabu maisha ya ndoa yake na Duni na akichelea kuyakosa.

Unyanyasaji wa wanawake katika ndoa

⇒ Kila aina ya matusi-mtukanifu/matusi mabaya mabaya
⇒ Makovu mwilini-mgongoni na mkononi
⇒ Athari za kisaikolojia-jeraha baya zaidi la moyo wake-moyo ulimuuma na kuatilika
⇒ Mateke na ngumi/kipigo

Mapenzi ya dhati

Ya Jamila kwa Duni

⇒ Jamila kukataa vishawishi
⇒ Kuvumilia ulevi, kupigwa,n.k.
⇒ Kukataa kushawishiwa-udhabiti wa msimamo
⇒ kukataa kupigana na mumewe- Ramla
⇒ Kukataa kumtoroka-Salim
⇒ Kukataa kutafuta mume mwingine
⇒ Kukataa kuvunja ndoa-shangazi
⇒ Kumbembeleza mumewe akiwa mlevi-Hai Du, wajii… onaje? Unalia nini Dii, Duni wangu? Kumpunapuna nywele na kumpigapiga vikofi vya kichwa (utu wema)
⇒ Kumsaidia kuchupisha mguu wake ndani.
⇒ kumsamehe- Hamdai chochote/hajamfanyia makosa yoyote, ni wengi wenye makosa makubwa kuliko

Ya Hamduni ka jamila

⇒ Duni Kumwandalia chai nzito ya maziwa supu na pweza, kumkaangia mayai, mandazi na chapatti, kuandika meza.-bidii, mahiri
⇒ Kumuinjikia maji ya kuoga
⇒ Kumfulia nguo
⇒ Ana **utu** au hisi za kibinadamu anapolevuka-anaomboleza, kulia, kuungama na kuomba msamaha na kutaka aadhibiwe.-anatambua makosa na kutubu.

⇒ Anamhurumia Jamila kwa kutambua kuwa simanzi na usingizi wa machovu na ukiwa wake ni kwa sababu ya kumstahimili
⇒ kuelekea bafuni kuoga wakirushiana mapovu na kucheka na kutaniana

Umakini

⇒ Duni kutenganisha nguo nyeusi na nyeupe, akaziweka katika mabeseni tofauti.

Ulevi na athari zake

⇒ Kurudi usiku wa manane na hivyo kusababisha Jamila kutolala vizuri kwa kukesha akimngoja.
⇒ Kuathirika kiafya-kovu mgongoni, donda mkononi
⇒ Kuathirika kisaikolojia kutokana na maneno ya watu-kidonda moyoni
⇒ Kusumbua watu/majirani kwa kelele na kuwakosesha usingizi wakati wamechoka kwa kazi za mchana
⇒ Harufu mbaya-lile vukuto na vundo la kilevi likawa la mwanzo kuingia ndani na kuzagaa ukumbini
⇒ Kumpiga mkewe k.v. kumrushia teke la mbavu kwa kutopeleka chakula haraka.-ukatili
⇒ Kulala bila kuvua nguo
⇒ Kuwangwa na kichwa baada ya kulevuka siku inayofuata baada ya kulewa usiku.
⇒ Kutumia pesa nyingi
⇒ Kuchukiwa na wanajamii hata wanamtusi- mja wa laana, mlevi, mbwa, mlevi, kafiri, firauni- kudharauliwa na kupuuzwa na kutusiwa na wanajamii kwa tabia yake
⇒ Kushindwa kutimiza majukumu ya ndoa/kulala tu
⇒ Mtu hupoteza utambuzi wa jema na baya-Duni ni mzuri akiwa hajalewa lakini akilewa anageuka na kuwa mbaya - duni anafahamu kwamba usiku uliopita alimtendea karaha mkewe , ukorofi,usimbulizi n.k.
⇒ Kuchelewesha mke kulala akingoja mume mlevi
⇒ Mtu kuwa mpyaro-mwenye matusi

Unafiki/usaliti/uchochezi/ushauri mbaya

⇒ Ramla na Salim si rafiki wa kweli wa Jamila kwa ushauri wanaompa Jamila.

⇒ Salim rafiki wa chanda na pete wa duni anamshauri Jamila amuasi duni kisha yeye angeliweza kutoroka naye.
⇒ Salim kujifanya anamjua Mungu ilhali anampotosha jamila-Billahi shemeji Jamila, amini Mungu usiniamini miye.Mungu haafikiani na maovu.
⇒ Nakuhurumia na nakupenda shemeji kwa nini huikimbii jahanamu hii?

Nafasi ya mwanamke

⇒ Duni mbele yamwanamume
⇒ Mpotoshaji/mshauri mbaya
⇒ Mshauri mzuri kwa upande mwingine-shangazi

Ugumu wa kubadili tabia

⇒ Anaahidi kutorudia makosa lakini ni nadra kutimia miezi miwili mingine kabla ya kusikia Duni akiimba taarab-njia usiku wa manane.

Ukombozi

⇒ Watu wanaomwandama Jamila eti wanamhurumia-madhali na yeye ana mdomo na mikono anayo, akatate kuadhibiwa kama mwana asiye na kwao
⇒ Ramla shoga yake –neno kwa neno –watukanane, ngumi kwa ngumi-wapigane

Ushauri mzuri

⇒ Mpapurane kwa nini mwanangu?-shangazi anamshauri wasipigane (kupapurana) lakini badala yake wavunje ndoa kama haina urafiki-Madhali ndoa ni mkataba ufungao urafiki wa kitambo, basi na uvunjwe ikiwa huo urafiki haukupatikana na badala yake pana vita.

Busara

⇒ Jamila anafahamu hakuna ndoa isiyo na walakini-Ni kweli kwamba usilolijua ni usiku wa giza. Iwapi hiyo pepo nyingine katika dunia hii?
⇒ Analinganisha maisha yake na ya wanawake wengine-ukiona kwako kwachomeka kwa mwenzio kwateketea.

Urembo

⇒ Wengi walimtamani Jamila wamuoe-hata Salim.

Shukrani

⇒ Hata hivyo, baada ya yote alijiona anawajibika kumhimidi mola wake kwamba mume wake ameshafika salama nyumbani kwake.

Matumaini

⇒ Kamwe moyo wake haukupata kujuta wala kuacha kutaraji kuna siku mume wake angetanabahika na yale yote yakafikia mwisho.

Ujipaji moyo

⇒ Ni wanawake wangapi wa aina yake ambao wanafanyiwa anavyofanyiwa na mume wake? Wengi wao hawapati starehe azipatazo.-busara

Nyimbo

Wimbo wa kwanza

⇒ Unaangazia uajabu kwa wakaazi wa Sebleni wa Jamila kuendelea kukaa kwa Hamduni

⇒ Anajua msimamo wa jamila- Ameridhika kwa pendo lake

Wimbo wa pili

⇒ Amempa kibali awaeleze wanasebleni kinachomfanya aendelee kukaa na Duni ili waache kumtafuta au kuingilia mapenzi na ndoa yao.

Wimbo wa tatu

⇒ Kiitikio cha Jamila kwa nyimbo za Duni na anauimba kimoyomoyo-kilichomuweka kwa duni ni mapenzi.

Tashhisi

⇒ Sauti tu ndogo ya paka atafutaye riziki katika madebe ya taka ingeliweza kusafiri mitaa kadhaa kwa mapana na marefu-unyamavu usiku duni anaporudi

⇒ Paka **walimuona hana thamani** mbele ya yale madebe ya taka waliyokuwa wakiyasasambura

⇒ Sauti ilipenya katika kila dirisha na kupanda katika kila roshani ya nyumba hizi

⇒ Siku zote ghasia na zogo la ukorofi wake **zilivuka** paa la nyumba yao na kuteremka chini-kusikika

⇒ Sasa uso wake unabeba simanzi tupu kila wakati hata akiwa usingizini-Duni anavyomuona Jamila

⇒ Moyo ulimwia vigumu kuusaliti-kutokubali ushauri

⇒ Wazo lake lilivuka mipaka na kutowezekana kwa jamila-la salim
⇒ Lile vukuto na vundo la kilevi likawa la mwanzo kuingia ndani na kuzagaa ukumbini
⇒ Teke lilimtupa jamila kwenye kochi

Utohozi

⇒ Ofisini-wanakofanya kazi wakazi wengi wa Sebuleni
⇒ Bendeji-iliyofungwa kwenye mkono wa Jamila
⇒ Kochi-jamila alikotupwa na teke la Duni
⇒ Hoteli-alikowahi kufanya kazi duni na kupata uzoevu wa upishi
⇒ Mabeseni-duni alikoweka nguo nyeusi na nyeupe-umakini
⇒ Kalenda-mwaka
⇒ Kozi

Methali

⇒ Dua la kuku halimpati mwewe-matusi ya wanasebleni hayakumwathiri Duni kiasi cha kumbadilisha
⇒ Tabia haigangiki-ugumu wa kubadilisha tabia ya Duni
⇒ Ni kweli kwamba usilolijua ni usiku wa giza-unaweza kukimbia matatizo ukakabiliwa na mabaya zaidi

Chuku

⇒ Kwa kila baada ya adabu moja aliyopewa, alizidisha vituko viwili
⇒ Alimpiga mkewe kama ngoma ya kimanga popote
⇒ Ambao roho zawazong’ozoka mbichi kwa kukutaka-wana wapenzi makubwa kwake
⇒ Kila aina ya tusi la ndani na nje alilijua yeye ungedhani kasomea kozi maalum yamhayo
⇒ Almuradi kila aina ya ukorofi alikuwa nao bwana huyu akishalewa.
⇒ Alimuona kazamisha kichwa chake kwenye mto uliorowa machozi –duni anavyomuona jamila baada ya kuamka kabla yake
⇒ Daima usingizi wake ni wa machovu na ukiwa

⇒ Mapishi ya duni yalimfurahisha jamila na mara zote alikuwa anajisahau kula kiasi chake, ni lazima avimbiwe tu. –uzuri wa mapishi

Msemo

⇒ Mlevi si mtu-salim-kejeli

Taswira

⇒ Sebleni, nyumba nyingi ni za ghorofa

Nidaha/siyahi

⇒ Maskini! Jamila machozi yalimtoka-Duni kumhurumia/msikitikia kwa madhila anayopitia
⇒ Msalie mtume mwanetu wee!
⇒ Aste, aste baba Duni-kejeli
⇒ Lo! Hata naye mlevi anajua thamani ya kusamehewa.
⇒ Mwisho wa haya utakuwa lini, ya Rabi?

Balagha

⇒ Hadi lini?-ataishi na mumewe mlevi/ataendelea kuvumilia
⇒ Hadi lini Duni ataendelea kurudi nyumbani chakari na wimbo wake huu?
⇒ Mwisho wa haya utakuwa lini, ya Rabi?
⇒ Kwani duni alikuwa mwanamume pekee katika dunia hii ya Mungu?
⇒ Nawe uendelee kubakia matesoni?
⇒ Siku yenyewe ni ipi hasa?-ambayo mumewe angetambua makosa yake na kubadilika?
⇒ Kwa nini akukongeshe mot0to ungali mbichi hapo ulipo? Kwani kakununua? -shoga
⇒ Nipigane?
⇒ Kama hii ni jahanamu, iwapi hiyo pepo nyingine katika dunia hii?-Jamila
⇒ Nini teena? Kwani waadhani naataka kusaidiwa?-haoni lililo jema.
⇒ Unasema nini Duni? Nani amekwambia kwamba mimi unanihusudi?-jamila anapomwona Duni akiathirika sana kwa anayomtendea
⇒ Ni wanawake wangapi wa aina yake ambao wanafanyiwa anavyofanyiwa na mume wake?

Sitiari

⇒ Iweje hasa kinda kama jamila …akubali kuendelea kusinginwa ndani na dume duni kama hili-mchanga-kejeli
⇒ Kama utaweza kumkimbia shetani huyu, basi mimi niko tayari kuenda na wewe popote-chuku
⇒ Kwa nini huikimbii jahanamu hii?

Kejeli

⇒ Iweje hasa kinda kama jamila …akubali kuendelea kusinginwa ndani na dume duni kama hili
⇒ Mlevi si mtu-Salim

Mbinu rejeshi

⇒ Jamila alikuwa ameolewa miaka miwili iliyokuwa imepita
⇒ Duni alikuwa na uzoevu wa upishi kwa kufanya kazi kama mpishi wa hoteli.-aliwahi kufanya kazi hotelini.

Tashbihi

⇒ Alimpiga mkewe kama ngoma ya kimanga popote apatapo-inayopigwa kwa nguvu kwa vigongo
⇒ Akatae kuadhibiwa kama mwana asiye na kwao

Kinaya

⇒ Pengine hii ndiyo sababu ya kuzuka wenye huruma tele nyoyo- si huruma bali ni upotoshaji/uchochezi/ushauri mbaya
⇒ Wimbo wa taarabu wa duni-kuwekewa zogo-yeye ndiye anawawekea wanasebleni zogo kwa mwenendo wake.
⇒ Kusema jamila ameridhika
⇒ Mapenzi kumweka jamila
⇒ Kuahidi angeacha ulevi na ilikuwa vigumu kutimiza miezi miwili
⇒ Salim kijana mtanashati ni rafiki wa chanda na pete wa duni aliye mlevi kupindukia.

Takriri

⇒ Walifika pahala pa kumshauri asikubali. Kabisa asikubali
⇒ liliokuweka oo kuweka- wimbo wa kwanza na wa mwisho
⇒ Meridhika oo meridhika
⇒ Ajibika oo ajibika
⇒ neno kwa neno ngumi kwa ngumi-shoga Ramla-wapigane na watukanane

⇒ Madhali ndoa ni mkataba ufungao urafiki wa kitambo, basi na uvunjwe ikiwa huo urafiki haukupatikana na badala yake pana vita.-shangazi
⇒ uduni wa duni haukuwa katika maeneo haya ya jikoni.

Mdokezo

⇒ Hai Du, wajii…onaje?
⇒ Kwani hata alithubutu kumgusa mkono wake, mara…
⇒ Watu wamelala…Haya basi sikusaidii, najua unaweza kila kitu.
⇒ Mja wa laana,mbwa miye mi…mi…mi…e
⇒ Nisamehe mke wangu…mimi mume wako, mimi … mja wa laana.
⇒ Imekuwa kama ni kosa kuolewa na mimi…
⇒ Unipige…Nipige jamila… uniue…Nilipizie halafu unisamehe
⇒ Imekuwa kama ni kosa kuolewa na mimi…

Uwili

⇒ Duni alizidisha vituko viwili
⇒ Walikuwa wameoana kwa miaka miwili
⇒ Mateso aliyopitia ni ya miaka miwili
⇒ Jamila alipoamka na kumkuta mumewe akilia, walikumbatiana na kukaa chumbani kwa muda usiopungua saa mbili

Uzungumzi nafsia

⇒ Hizi nitazifua jioni-duni baada ya kuroweka nguo za rangi nyeupe na zile nyeusi
⇒ Maskini mwangalie na umwone jamila hivi alivyo… maskini, mtazame sasa namna alivyobadilika wajihi wake.

Taharuki

⇒ Hatima ya Duni ilikuwaje?
⇒ Jamila aliendelea kuvumilia hata baada ya kuona hakubadilika?
⇒ Jamila alimwambia Duni kuhusu fitina ya Salim?
⇒ Kama alimwambia urafiki wa Salim na Duni ulikuwaje baada ya kusikia alimsaliti?

Majazi

⇒ Jamila-wema au hisani anamtendea mumewe licha ya makosa anayomfanyia
⇒ Duni-kitu hafifu au cha thamani ya chini-kujidunisha kwa ulevi na tabia zinazoandamana nao.
⇒ Sebleni-mahali m pa kupumzika nyumbani-kupumzika usiku wakati wanasumbuliwa na Duni

7.Kanda la Sufi
Maudhui
⇒ Mimba ile kwa Masazu ilikuwa kanda la sufi-anachukulia kuwa hawajibiki.
⇒ Uaminifu katika kutimiza ahadi.
Uwajibikaji/jukumu la ulezi
⇒ Babake Sela (mzee Butali) anadhani walimu pekee ndio wanapaswa kuwajibishwa kwa wanafunzi kupoteza mwelekeo lakini hata yeye anawajibika kwani lazima kuwe na ushirikiano wa wazazi na waalimu.-kuwaachia walimu majukumu yote ya kutunza watoto wa kike
⇒ Pia anafikiri mama ndiye aliye na wajibu mkubwa wa kumuelekeza mtoto wa kike lakini wazazi wote wawili wana jukumu sawa.
⇒ Mama anajua tatizo lazima liwajibikiwe na wazazi wawili.
⇒
⇒ Uwajibikaji katika /miongoni mwa vijana-wote wawili wana jukumu la kuzuia kupata mimba-Chris kumlaumu na kumnyooshea Sela kidole kwa kumuuliza kwa nini hukujikinga
⇒ Sela alikuwa na wajibu wa kiutu na moyo wake uliyeyushwa na huruma alipomuona mja akiteseka.-wema uliponza.
⇒ Mwalimu mkuu kuwaandikia wasichana waliopata mimba barua za mapendekezo ili wapeleke katika shule za kutwa walizochagua- kuhakikisha wanaendelea na masomo
⇒ Mwalimu mkuu Margaret anasema kuna umuhimu wa kuwajibikia vitendo vyetu.
Usaliti/uaminifu

⇒ Rozina halati ya Kadogo si mwaminifu kwa kuwapatia Masazu na Sela Kadogo bila idhini ya wazazi wa Sela.-wanaoshirikiana na wengine kutenda maovu.
⇒ Masazu kutaka kukana mimba ya Sela si yake.

Elimu

⇒ Bi Margaret anathamini elimu kwa kuonelea Sela arudishwe katika shule ya kutwa
⇒ Mapenzi shuleni huathiri elimu ya wanafunzi hususan wasichana

Ujinga/ulimbukeni na athari zake

⇒ mapenzi hupofusha`-kuguswa sana na barua za Chris-kudanganyika kwa urahisi na kukubali kufanya mapenzi bila kinga hata bila kupimwa kubainisha kama wana magonjwa ya zinaa, kuamini kwa urahisi mtu kijana asiyemjua
⇒ Sela alisikia wasichana wengine wakizungumzia barua walizotumiwa na wavulana-shinikizo la wanarika

Taasubi ya kiume

⇒ Babake Sela kulaumu mama Sela anapopata mimba.
⇒ Kuwafukuza
⇒ Masazu kutumia sera kama chombo cha kujiburudisha

Umaskini

⇒ Mzee Butali kusema “Sikutumia hela zangu mimi katika elimu hadi nikaitwa pangu pakavu?
⇒ Sela alikaa nyumbani akikitunza kitoto katika ufukara wa pale nyumbani.
⇒ Mama Sela hangeweza kukinunulia kitoto nguo ilibidi matambara yatumiwe kukivisha.
⇒ Masazu kufanya kazi ya kuvuna mkonge na pesa anazopata zinatosha kulipa kodi na kununulia chakula.
⇒ Makao duni-chumba kimoja tu.
⇒ Umaskini wa vijana-Masazu hangemudu utaratibu wa kimila kwenda kwa wazazi wa Sela –kuasi utamaaduni.

Tabia ya kutojali miongoni mwa wanafunzi

⇒ Hawajali umaskini wa wazazi angaa wasome wainue hali yao.
⇒ Hawajali maisha yao ya baadaye.
⇒ Hawajali afya zao.

Vikwazo kwa wanaotaka kufunga ndoa
⇒ Urasimu wa ndoa
⇒ Masazu hangemudu utaratibu wa kwenda kwa wazazi wa Sela.
Ndoa haramu/ukengeushi
⇒ Sela kumfuata Masazu Dafina na kuishi kama mke na mume.
⇒ Wanaume kuishi na wanawake bila kuwa wameoana(Come we Stay).

Uasi wa Vijana

⇒ Masazu na Sela kutoomba kubali wachukue mtoto.
⇒ Radhi za wazazi ni fimbo kubwa ukizikosa.

Athari ya mapenzi katika umri mdogo/shuleni/ Mimba zisizotakikana na athari zake

⇒ Mapenzi ya shuleni si mara nyingi hudumu.
⇒ Kusababisha uzinifu.
⇒ Mapenzi ni matamu lakini mtu akiyapapia huwa machungu kama shubiri.
⇒ Hufanya mtu kuathririka kimasomo.
⇒ Mgogoro baina ya Sela na Masazu.
⇒ Mgogoro kati ya wazazi wa Sela-Sela na mamake kufukuzwa nyumbani.
⇒ Mzee Butali kumlaumu mkewe.
⇒ Sela na Kadogo kufa maji dimbwini.
⇒ Ndoa za mapema na haramu
⇒ Umuhimu wa kujitunza mtu akiwa kijana
⇒ Kufukuzwa shuleni.
⇒ Migogoro baina ya wazazi-mama kulaumiwa.
⇒ Hofu-maisha yangechukua mkondo gani.
⇒ Uavyaji mimba.
⇒ Kusumbua wazazi wanapoitwa shuleni.
⇒ Kupoteza muda wa masomo wakiandikiana au kusoma barua.
⇒ Kukosa utulivu.
⇒ Majuto-mzo wa majuto ulimwandama.
⇒ Kuathirika na kutoweza kutunza makini shuleni-Masazu.

Mila na desturi

⇒ Kuzuia Masazu na Sela kuoana.

⇒ Wanaamua kuiba mtoto kwa Masazu kushindwa kumudu utaratibu wa kawaida wa kwenda kwa wazazi wa Sela.
⇒ Kina mama kulaumiwa binti wakipoteza mwelekeo.

Nafasi ya mwanamke

⇒ Amepewa jukumu la ulezi-mamake Sela kualaumiwa.
⇒ Kumlea mjukuu wake.
⇒ Wanaowajibika-mwalimu mkuu.
⇒ Wenye mapuuza/wasiojali-Sela
⇒ Vyombo vya kujiburudisha vya wanaume-Sela
⇒ Watetezi-mama kumtetea Sela.
⇒ Kadogo ni kielelezo cha watoto wanaoteseka kwa ajili ya makosa ya wazazi wao.
⇒ Ni jasiri

Umuhimu wa mtoto

⇒ Kiungo muhimu kati ya uhusiano kati ya mke na mume.
⇒ Kutoa mzazi upweke
⇒ Kumpa mzazi shughuli

Mapenzi

⇒ Ya Masazu kwa Sela.
⇒ Sela kumfuata baada ya masomo waishi kama mke na mume.
⇒ Ya Masazu na Sela kwa binti yao Kadogo-kumwendea.
⇒ Mama Sela kumlea Kadogo kama mwanawe.
⇒ Mzee Butali kumwelimisha Sela japo ni maskini.
⇒ Wanakijiji kumwombea Sela na mamake msamaha kutoka kwa mzee Butali.
⇒ Butali anawapenda mkewe na Sela kwa kuwaonea huruma na kuwarejesha nyumbani.
⇒ Kumrudisha Sela shuleni.
⇒ Mwalimu mkuu kwa wanafunzi wajawazito.

Ulaghai/udanganyifu

⇒ Masazu kudanganya Sela kuwa ni mgonjwa-kichwa kinamuwanga.
⇒ Kumwarifu Sela kuwa alihisi kichefuchefu-wanapotoka katika ofosi ya sista.
⇒ Barua walizoandikiana ziliwasilisha ahadi za kweli na za uongo.

⇒ Ukiona cha mwenzio chanyolewa chako tia maji- tunaweza kupatwa na yanayopata wengine-mzee Butali hakuwahi kufikiria hali kama ile ingetokea nyumbani mwake.

Ujinga

⇒ Ulimbukeni katika mapenzi kusabaisha wasichana wengi kupata mimba wakiwa shuleni.

⇒ Kufanya mapenzi bila kinga ilhali wangeambukizana magonjwa ya zinaa.

⇒ Kukutana na mtu usiyemjua na kuishia kufanya mapenzi naye bila kujali maisha yake ya awali.

Udhabiti wa msimamo

⇒ Mzee Butali hakulegeza msimamo waondoke nyumbani licha ya Sela na mamake kulia.

Huruma

⇒ Huruma kumwingia na aliwarudisha jamaa zake nyumbani kwa majuto makuu.

Ushauri

⇒ Wazee kumshauri Butali yakimwagika hayazoleki.

⇒ Afanye kama alivyoelekezwa na mwalimu mkuu.

Subira

⇒ Ukosefu wa subira miongoni mwa vijana.

⇒ Subira katika mapenzi-ngono kabla ya ndoa.

⇒ Kusubiri watimize taratibu kabla ya ndoa.

⇒ Kusubiri wamalize masomo.

Matatizo yanayokumba sekta ya elimu

⇒ Mahusiano wa kimapenzi baina ya wavulana na wasichana.

⇒ Wanafunzi wasichana kupata mimba.

⇒ Kufukuzwa shuleni na kupoteza muda wa masomo.

⇒ Kuathiri wenzao na kuiga tabia kama hizo.

⇒ Kutojali miongoni mwa wanafunzi.

⇒ Ukosefu wa karo.

Ujasiri

⇒ Mamake Sela kumtetea anapofukuzwa.

Busara

⇒ Mamake Sela anajua maji yakimwagika hayazoleki.

Unafiki

⇒ Chris kuketi akiwa ameshikilia kichwa kana kwamba kingemdondoka.

Maumizi la lugha

Chuku

⇒ Kanda la sufi-mzigo wa mwenzio ni kanda la sufi.
⇒ Kwake usiku ule ulikuwa mwaka.
⇒ Mpito wa kikonokono wa wakati.
⇒ Masazu kusoma barua mara ya kwanza, akarudia mara ya pili na ya tatu.

Tashhisi

⇒ Mambo haya mawili yaliendelea kuungana kuhujumu mkakati wao (wakati kusonga polepole na hali ya hewa).
⇒ Matone ya mvua yaliyokuwa yakipenya baina ya majani ya mwembe waliojikingia mvua yalitoa sehemu yayo ya hujuma-kuwalowesha.
⇒ Mabasi yalikuwa yameanza kuingia huku yakiendelea kutapika wanafunzi-kuwashukisha. wanapoenda katika shule ya kina Sela ya Askofu Timotheo kulikokuwa na tamaasha za muziki na drama.
⇒ Saa sita usiku kiza kilikuwa kimeuma kila mahali-usiku wanaoendea Kadogo.
⇒ Mara nyingine maji ya kutoka mitini yalianguka kwa matone mazito na kuhujumu Kadogo.
⇒ Akajitahidi kujiopoa lakini utelezi miguuni ukamzidi nguvu.
⇒ Utelezi ule ukamzoa pamoja na mtoto na kumbwaga majini-kuonyesha jinsi Sela na Kadogo walivyoangamia.

Balagha

⇒ Huoni tayari tumesimama hapa kwa muda mrefu?-Masazu akimwambia Sela.
⇒ Kwa hiyo…?-Sela.
⇒ Huyu si mtoto wetu sisi wawili?
⇒ Je, ni kwa nini sisi huwaletea watoto shuleni?-babake Sela anamwambia mwalimu mkuu.
⇒ Mama gani anayemtazama mwana anageuka afriti ?
⇒ Sikutumia hela zangu mimi katika elimu hadi nikaitwa pangu pakavu?-kuonyesha umaskini.

⇒ Baba Sela, nani kasema huu ni msiba wangu?-mamake Sela.

Mdokezo

⇒ Kwa hiyo…?-Sela Masazu anapomwambia wamekaa chini ya mwembe kwa muda mrefiu.

⇒ Sijambo. Sijui wewe?...sista akijibu salamu za Sela.

⇒ Rozina, Rozina, Rozinaa… amka-Sela akimwita Rozina baada ya kuona kuwa Masazu hakufaulu.

Nahau

⇒ Sikutumia hela zangu mimi katika elimu hadi nikaitwa pangu pakavu?-maskini.

⇒ Moyo ulimsisimka-Masazu kumuona Sela na kuingiwa na mapenzi/moyo wake kumpenda.

⇒ Kingewaborongea mkakati-kama kadogo angeamka kilio chake kingewaharibia mpango wao wa kumchukua.

⇒ Ingawa sisi hufanya tuwezayo kuwalinda wanetu, tabia zao hutupiga chenga …-hutukwepa-mwalimu mkuu anawaambia wazazi wa wasichana waliokuwa na mimba.

Kinaya

⇒ Shule anayosomea Sela ni ya dini ambako wanaendeleza shughuli zao kwa utulivu na ustaarabu huku wakizingatia maadili ya hali ya juu ilhali Sela anapata mimba.

⇒ Shule anayosomea Masazu inaitwa lenga juu ilhali analenga mapenzi na kutia wasichana mimba.

⇒ Sela kupata mimba licha ya babake kuwa mkali.

⇒ Sela kupata mimba licha yake kuonekana kuwa msichana anayewajibika.

Utohozi

⇒ Drama-michezo ya kuigiza

⇒ Mabasi ya shule ngeni

⇒ Kliniki- mahali pa wanafunzi kutibiwa shuleni.

⇒ Sista-daktari wa kliniki aliye mtawa wa kikatoliki.

⇒ Ofisini-ya sista daktari

⇒ Glasi ya maji-aliyopeewa Masazu kumezea vidonge viwili.

⇒ Kiberiti cha gesi-hewa iwakayo moto cha Masazu cha kuwashia sigara anachotumia Masazu kumulikia.

Tashbihi

⇒ Kama chui aliyelivizia windo lake na sasa limetokea, akajiandaa-Masazu anapomwona Sela katika pitapita zake katika shule ya kina Sela na kujiandaa kumtongoza.
⇒ Alitunza barua ile kama uhai-Sela iliyokuwa imepuliziwa maashi-chuku pia.
⇒ Kiapo cha Masazu-kuchomeka kidole chake cha shahada ardhini na kumwambia mapenzi yake kwake ni ya dhati) kikalegeza kiwiliwili chake (Sela) mithili ya mbwa anayekabiliana na chatu macho kwa macho-kumfanya akubali penzi.
⇒ Ulimwengu ulivurugika, akawa kama tiara inayopeperushwa na upepo ikaenda arijojo.-Sela kuathirika kwa kupata mimba.

Nidaha

⇒ Pole Chris-akimliwaza kwa maumivu.
⇒ Kijusi kilikuwa kimetungika!-Sela alikuwa na mimba.
⇒ Naam, naam shemeji Masazu-Rozina akimwitika Masazu.
⇒ Ahsante-Masazu akimshukuru Rozina.

Sadfa

⇒ Sela anapotaka kuingia kwa sista kumwarifu kuhusu Masazu naye sista alikuwa akitoka.
⇒ Hapakuwa na wanafunzi wengine katika kliniki ndiposa Masazu akaweza kumtongoza Sela.

Kupitapita kwa Masazu katika shule ya Askofu Timotheo kusadifiana na Sela kutokea ambaye moyo wake unampenda.

Tanakali

⇒ Alikataa katakata-kurudi katika zahanati Sela anapohofu angezidiwa.
⇒ Kroo! Kroo! Kroo! Za vyura usku wa kuendea Kadogo.
⇒ Pata pata pata! Masazu na Sela wakipita kwenye maji na matope wakirudi baada ya kumchukua Kadogo.
⇒ Kadogo alikuwa amelala fofofo alipoendewa.

Sitiari

⇒ Barua ile ilikuwa parafujo fulani moyoni mwa Sela-ilimgusa sana kwa kutowahi kupokea barua nyingine kutoka kwa mvulana.

⇒ Boma la mzee Butali kugeuka na kuwa jahanamu-kuwa na zogo na fujo baada ya kutoka shuleni.

Methali

⇒ Yajapo yapokee-Chris kwa Sela-si tatizo lake-halimhusu.
⇒ Mimba ile kwa Masazu ilikuwa kanda la sufi-mzigo wa mwenzio ni kanda la sufi.
⇒ Mpango uliokuwapo ulikuwa usiku wa giza-Sela na wasichana waliokuwa na mimba kutojua hatima yao baada ya kuelekezwa wasubiri katika chumba cha mapokezi.
⇒ Uchungu wa mwana, aujuaye ni mzazi-mamake Sela.
⇒ Maji yakimwagika hayazoleki-alielewa baada ya ushawishi wa wazee.

Kicheko/tashtiti/kejeli

⇒ Vicheko vya chini kwa chini vilianguliwa na wanafunzi.

Ishara

Giza- tanzia ambayo ingetokea-Sela na Kadogo kufa maji kwa kutumbukia kidimbwini.

Takriri

⇒ Rozina, Rozina, Rozina! Masazu akimwita halatiye Kadogo usiku ule wamemwendea Kadogo.na Sela.

Taswira

⇒ Ilibidi matambara yatumiwe kukivisha kitoto-kuonyesha umaskini wa wazazi wa Sela.
⇒ Walifika mahali mti ulikuwa umeanguka na majani kukingama njiani.
⇒ Mara wakafika sehemu ambapo njia ilikuwa pana lakini kulikuwa na jiti lililoangushwa katikati.
⇒ Palikuwa na dimbwi la maji lililotuama pale.
⇒ Akawa tayari keshaelekea pale na kujikuta katia mguu majini, yamemzagaa na kumfika magotini yanatishia kumsomba.

Mbinu rejeshi

⇒ Tunaelezwa jinsi mapenzi kati ya Sela na Masazu yalipoanza wakati wa tamaasha za muziki na drama katika shule ya kina Sela.

Sadfa

⇒ Sela na sista kukutana mlangoni wakati amempeleka Masazu akatibiwe.

Utatu

⇒ Sela na mamake kukaa kwa jamaa yao kwa majuma matatu.
⇒ Sela kukaa nnyumbani kwao kwa muda wa miezi mitatu akitunza kitoto chake.
⇒ Majina ya wanafunzi watatu kuitwa na mwalimu mkuu wafike ofisini mwake.

Taharuki

⇒ Masazu alifaulu kuwaokoa Sela na Kadogo?
⇒ Alipofaulu kuwaokoa walikuwa wafu au wazima?
⇒ Au wote watatu walikufa maji?
⇒ Rozina aliwaambiaje wazazi wa Sela baada ya kuamka na kukuta Kadogo hakuweko?
⇒ Masazu aliwafahamisha wazazi wa Sela kuhusu maafa yaliyotokea?

8.Shaka ya mambo

taharuki

⇒ Kutokuwa na uhakika wa jambo au jambo la kutuhumiwa.
⇒ Kuna shaka ya mambo kama Esther aliendelea na masomo kwa kusomea usekretari kwani hana pesa.
⇒ Kama Kamata alikuwa anampenda yeye au alikuwa na mapenzi na Grace.
⇒ Ukaribu kati ya Kamata na Grace ulikuwa wa kutia shaka.
⇒ Esther alitoka kwa mzee Mwinyi na kwenda kupanga chumba chake?
⇒ Alihama madaraka na kupanga nyumba yao na Kamata?
⇒ Alibadilishiwa zamu na Grace?
⇒ Miadi muhimu sana aliyonayo Grace ni ya kutiliwa shaka.
⇒ Shaka kama Grace na Kamata walikuwa shule moja na iwapo waliishi Buruburu na wazazi wao.
⇒ Mtu ambaye Grace anaenda kukutana naye ni Kamata au mtu mwingine?
⇒ Yawezekana ndio walipanga abiria aende mkahawani wamshtue kwa tangazo aharakishe asahau pesa?

⇒ Shaka kama Kamata alimpata abiria aliyeacha bunda la pesa au ndege ilikuwa imeondoka.
⇒ Kama Grace na Kamata walimpatia mzungu pesa walizopatiwa na Esther.
⇒ Kama Grace alikuwa anapewa lifti tu na Kamata au walikuwa na mpango wa kwenda kustarehe pamoja kama wapenzi.
⇒ Kama Kamata anampenda Esther jinsi Esther anavyompenda kwa kutompitia Esther mahali pa kazi na kutopokea simu zake hata kuzikata.
⇒ Kuna shaka Grace anapomwita Kamata mpenzi kama ni utani tu au ni kweli. Kamata anamkonyezea jicho.
⇒ Shaka kuwa anakataa kumbadilishia zamu ali apate muda mwingi wa kuwa na Kamata.
⇒ Shaka Grace anapomwomba Esther aendelee na zamu yake hadi usiku ana miadi muhimu sana Nairobi-ni ukweli au ataka wakutane na Kamata?
⇒ Shaka kuwa Grace kutobmbadilishia zamu kama anapenda kufanya kazi hadi usiku ama anataka wawe pamoja na Kamata.
⇒ Kuna shaka kwa nini Kamata anakataa waende disko na Esther badala yake waende katika vilabu kama huko ndiko hata Grace anataka apelekwe na Kamata hataki wakutane.
⇒ Kuna shaka ya Kamata kukata simu ya Esther kama ni kwa kutotaka aijibu wakiwa na Grace asije akajua ana mpenzi mwingine.

Umaskini

⇒ Familia ya Grace kushindwa kumsomesha kozi ya uhazili na kuachiwa jukumu la kujisomesha mwenyewe.

Heshima/utu wema

⇒ Mvulana kumwinukia Esther kiti na kumkaribisha akae katika matatu akielekea kazini.
⇒ Esther kumshukuru kwa kusema , “Ahsante’.

Balagha

⇒ Ugeni au usasa gani?-heshima ya kuinuka huitwa na watu wengine usasa.

⇒ Kwani zamani wavulana hawakuwapa heshima wasichana?
⇒ Hicho ndicho kitu kigeni hapa Afrika?
⇒ Kamata anampenda kwa dhati?
⇒ Kamata kweli anamjali au naye anshughulika kutafuta pesa?
⇒ Kweli Kamata angeinuka na kumpisha yeye Esther kiti?
⇒ Sasa upo ulakini hapo?
⇒ Kazi gani hii ya kuamka alfajiri siku sita kwa wiki na kujisukuma garini macho yamejaa usingizi?
⇒ Sijui amekuja kazini leo? -kukaribia saa sita na Kamata hajafika hajafika.
⇒ Anaumwa?

Ujinga

⇒ Esther kuamini Kamata angempa abiria asiyemjua pasa ilhali hajamweleza wasifu wake.

Unafiki

⇒ Grace kusema Kamata atampa lifti na hataki amcheleweshe.
⇒ Kamata kumwambia Grace atangulie kwenye gari na akishampa abiria pesa angeenda waondoke.

Ulaghai/udanganyifu/utapeli

⇒ Kamata ni tapeli wa mapenzi na pesa.
⇒ Kamata kusema apewe pesa ampelekee abiria na abiria wapo hapo.
⇒ Grace kumwambia Esther ampe Kamata pesa ampelekee.

Subira

⇒ Anataka Kamata astahimili kidogo, lakini ndio hivyo, wanaume hawana subira
⇒ Vijana hawana subira. Esther anataka waishi pamoja na Kamata kama mke na mume kabla ya ndoa.

Anasa/starehe

⇒ Esther ana hamu ya kuenda na Kamata disko kama wafanyavyo vijana wengine.
⇒ Kamata anashughulika na kutafuta pesa na starehe.

Madhira ya abiria wa ndege

⇒ Kucheleweshwa.
⇒ Safari kuahirishwa.

⇒ Kutosikia safari zao zikitangazwa na watangazaji kutisha abiria kimakusudi.
⇒ Kufanya kazi muda mrefu-siku sita kwa wiki

Tamaa

⇒ Esther ana tamaa ya pesa asomee usekretari.
⇒ Kamata ana tamaa ya wasichana.
⇒ Kamata na Grace wana tamaa ya pesa ndiposa wanatumia ulaghai kupata pesa zilizoachwa na abiria.

Uhuru

⇒ Esther anataka asomee usekretari kazi itakayokuwa na uhuru zaidi.
⇒ Amekuja Nairobi kutafuta uhuru lakini mzee Mwinyi anamchunga kama mtoto.-yeye ni amana yao-kitu cha thamani mtu anachopewa na mwingine ili amtunzie-udhibiti wa mwanamke-kuchungwa ili wasiharibike kitabia.

Uaminifu

⇒ Kamata si mwaminifu kwani ana mpenzi mwingine zaidi ya Esther anayeitwa Grace aliye mkuu wa Esther kazini katika mkahawa ulio katika uwanja wa ndege.
⇒ Grace amekosa kumtimizia Esther ahadi ya kumtoa zamu ya kuanzia asubuhi saa kumi na mbili –angembadilishia zamu kila mwezi wa pili na angeingia kazini mchana saa nane na kutoka usiku.
⇒ Esther ni mwaminifu kwa vile mteja anaposahau pesa anazishika upesi na kutoka mkahawani kumpelekea lakini hamuoni.
⇒ Ni mwaminifu katika mapenzi kwa vile anampenda Kamata anamfikiria na kupanga watakavyoishi baadaye naye.

Ukarimu

⇒ Esther kumshikia Grace zamu yake.

Ukengeushi

⇒ Vijana kuishi pamoja kama mke bila kuwa wameoana.

Utamaaduni

⇒ Wanawake hawaheshimiwi na kuwaheshimu ni usasa.

Matatizo ya wafanyakazi

⇒ Kuamka alfajiri siku sita kwa wiki na kujisukuma garini macho yangali yamejaa usingizi.
⇒ Kutobadilishiwa zamu.
⇒ Hangeuliza kwani angefanya hivyo angefikiriwa kuwa mtu matata.
⇒ Mishahara duni.

Matumizi ya lugha

Tashhisi

Mvua ya siku iliyopita ilimbembeleza na kumlaza usingizi mtamu.

Kuchanganya ndimi

⇒ Jommo Kenyatta international airport-anakofanya kazi Esther.
⇒ Mombasa road -barabara gari lililoingia.

Utohozi

⇒ Usekretari-uhazili ambao Esther angesomea baada ya kupata pesa za kutosha.
⇒ Kupiga taipu
⇒ Kompyuta
⇒ Dola elfu-kiasi cha pesa ambacho Esther alikisia abiria aliacha.
⇒ Huduma za kiofisi
⇒ Kaunta –ya mkahawa
⇒ Airport-uwanja wa ndege
⇒ Nambari-ya gari
⇒ Lifti-ambayo Grace anadai anapewa na Kamata
⇒ Tiketi
⇒ Disko-ambako Esther ana hamu ya kwenda na Kamata
⇒ Wiki-anafanya kazi siku sita kwa wiki.
⇒ Dola hamsini-ambazo zilitakikana chuoni kama rubuni ili Esther aweze kusomea kozi ya uhazili

Mbinu rejeshi

⇒ Esthre alitoka kwao miezi mine iliyopita na kwenda Nairobi.
⇒ Babake Esther alikuwa akifanya kazi Nairobi miaka ya sabini.Aliamua kurudi kwao baada ya mzee Jommo Kenyatta kufariki mwaka wa 1978, miaka mitano kabla ya Esther kuzaliwa.

Tashbihi
⇒ Anachungwa kama mtoto kama alivyochungwa nyumbani.
Takriri
⇒ Lakini pesa! Kila kitu pesa.
⇒ Mtu hawezi kupiga hatua duniani bila pesa. Kuzaliwa kunahitaji pesa. Kuolewa pesa. Kuzaliwa kunahitaji pesa.
Msemo
⇒ Wanaume hawana subira
Kicheko
⇒ Esther kumuuliza Grace kama ana mpenzi akicheka.
⇒ Grace kucheka anapoulizwa hivyo.
Mdokezo
⇒ Ndiyo nimebahatika lakini…-Esther akiwaza-kupata usafikiri kumpeleka hadi kazini.
Hapana n’na mengi ya kufanya kabla ya kukutana na … kabla ya miadi yangu-Grace anapoambiwa na Esther itakuwa mapema.
⇒ Esther, sina wakati. Mimi lazima niondo…
Taswira
⇒ Kamata kutokea akiwa amevaa suti ya bluu, shati la manjano hafifu na tai ya kijivujivu, uso wake uking’ara kwa furaha na pia kwa kupakwa mafuta ya kulainisha ngozi.
Nidaha
⇒ Kamata! Hajui anamfikiriaje yeye Esther.
Taharuki
⇒ Kamata alipokuwa hapokei simu ya Esther kwa kuikata au kuacha ikatike?
⇒ Alikuwa wapi?
⇒ Kamata alifanikiwa kumpata mteja aliyesahau fedha?
⇒ Esher aligundua uhusiano uliopo kati ya Kamata na Grace?
⇒ Kama aligundua alifanyaje?
⇒ Hisia zake ziliathirika kiasi gani?
⇒ Esther alifanikiwa kutimiza ndoto yake ya kusomea usekretari?

9.Maskini babu yangu

⇒ Maskini-kihisishi cha kuonyesha huruma

⇒ Kuugua-kushikwa na maradhi Fulani uzeeni.

⇒ Kusingiziwa kuwa mwizi wa mtoto

⇒ Kusingiziwa kuwa mchawi

⇒ Kupigwa, kuuawa na kuteketezwa na umma.

Utamaduni

⇒ Watantele wanawake kujitandia mitandao na kuvalia mavazi marefu yaliyositiri maradufu viwiliwili.

Utabaka na athari zake

⇒ Sakata ina makabila mawili tu, maskini na matajiri

⇒ Watu wa mjini na watu wa shambani

⇒ Huduma bora za kijamii zinapatikana mijini kama vile hospitali bora.

Ubandia wa uhuru

⇒ Haukuleta manufaa kwa watu wote

Uozo

⇒ Ukabila, ufisadi na hongo babu anasema ni vipengee halisi vya maisha ya binadamu.

Bidii

⇒ Babu kutotaka kuacha mifugo wake aende akatembee mjini. Alitembea kwa kuraiwa sana.

⇒ Idili ya babake katika jeshi la polisi kusababisha apandishwe cheo hadi mrakibu wa polisi.

Ndoa

⇒ Kati ya watu wenye asili mbalimbali.

⇒ Ndoa ya babake na mamake msimulizi kupingwa na pande zote mbili.

Heshima kwa wazazi

⇒ Babake msimulizi anajali babake kwa kumchukua kuja kutibiwa mjini.

Ubaguzi

⇒ Ndoa kati ya Watantele na Wamindi na makabila mengine nchini subu ni nadra.

⇒ Ndoa ya babake na mamake msimulizi kupingwa na pande zote mbili.

⇒ Babu Maende na babu Tandeka, mama-Zuhura Kimbaumbau.

⇒ Wazazi hawana ubaguzi-kuna maelewano kati ya mababu na bibi na babu kutembeleana

Umaskini

⇒ Mtaa wa Madongo, eneo la Kochokocho kuwa na watu wa asili mbalimbali.
⇒ Hali zao za maisha ni duni.
⇒ Taswira ya nyumba
⇒ Wanawake kukaanga samaki kandokando ya barabara na kuwauzia wapita njia.
⇒ Kina mama kuuza chapatti zilizokaukiana na mandazi makavu.

Ukatili/uchukuzi wa sheria mikononi

⇒ Msimulizi ana nywele za singasinga.Wakitembea mitaa ya Kochokocho wanavamiwa na Watantele.
⇒ Walipaswa kumpeleka babu Maende kwenye vyombo vya sheria ili ibainike kama alikuwa amefanya makosa.
⇒ Alisingiziwa kuiba mtoto na kumloga-Mtoto mtantele umemtoa wapi? Wee! Waacha! Unawezaje kumpata mjukuu wa kitantele? Mchawi huyu amemroga mtoto mpaka akamwita babu yake. Mwizi wa mtoto!
⇒ Kumpiga, kumuua na kumteketeza- Mama mmoja kumnyaka kibao shavuni, Mchomeni moto. Mwekeni tairi!

Matatizo ya uzeeni

⇒ Babu kushikwa na maradhi fulani ya uzeeni.

Ujasiri

⇒ Babake na mamake msimulizi wanavunja miiko ya kutoolewa na kabila lingine.
⇒ Wanapinga mila potovu na kuanzisha ujenzi wa jamii mpya isiyo na ubaguzi.

Utamaduni

⇒ Mamake kukulia Kisubu na kuimba nao nyimbo za kitamaaduni.
⇒ Huko madongo msimulizi aliwaona wanawake waliojitandia mitandio na kuvalia mavazi marefu.

Matumizi ya lugha

Mbinu rejeshi

⇒ Mamake msimulizi Zuhura kimbaumbau ni Mtantele kutoka Kitolo. Walihamia nchi ya Sakata huko Kabucheka kituo cha biashara miaka ya sitini. babake alikuwa na duka la reja reja-kuonyesha msimulizi ana usuli mseto babu Maende kuumeni na babu Tandeka kuukeni.
⇒ Msimulizi anatukumbusha Jumamosi babu yake aliuawa wakiwa naye.
⇒ Katu sikutaka kukumbuka… Miaka ishirini imepita tangu yalipotokea yaliyotokea.
⇒ Rekodi za santuri-alikosikia babu mtaa wa kochokocho ukiimbwa ndipo akataka wakautembelee.

Takriri
⇒ Sikutaka kutazama nyuma, kupiga darubini nyuma, kukumbuka nyuma.
⇒ Kila siku, kila siku kochokocho-wimbo wa rekodi.
⇒ Nilijiwaza kwamba hayakuwa yalikuwa, yalikuwa hayakuwa-yalitokea au hayakutokea.
⇒ Yale yamesimama yamesimama wima yamesimama wima kwa rehema za Mungu

Nahau
⇒ Kujitonesha donda akitazama nyuma-kujikumbusha msiba uliokwisha na kusahauliwa.
⇒ Shikia shokoa-babake msimulizi alimlazimisha babu aingie katika gari la Toyota Corolla ampeleke mjini hospitalini
⇒ Nilipiga unyende-msimulizi kupiga mayowe kwa kuona babuye akishambuliwa na umati.
⇒ Jamani! Jijini kuna maisha ya kukatisha tamaa sana.-babu alipoona umaskini wa madongo-kupotezesha matumaini.

Tashhisi
⇒ Donda ndugu lililokataa kusikia dawa-kisa cha mauaji ya babu yake kuosahaulika.
⇒ Shinikisho la wenzangu kutaka niandike limenisakama kupindukia-kumlazimisha.
⇒ Nyumba yetu kutawaliwa na vicheko, tabasamu-furaha babu anaposema amepata nafuu kiasi.

⇒ Wauzaji kuwa na kazi kubwa kuliwinga wimbi kubwa la nzi waliotaka kula uhondo-hali ya uchafu katika soko huko madongo.
⇒ Mtaa wenye mabanda yaliyoinamiana na kuoneana imani.
⇒ Yale yamesimama yamesimama wima yamesimama wima kwa rehema za Mungu
⇒ Ukata uliokuwa umewafunika na kuwafanya wa kabika moja la wachochole.
⇒ Kuta za mbavu za mbwamabati yaliyojifunika libasi ya kutu.

Majazi

⇒ Kochokocho-mahali kuliko na vituko vingi hasa eneo la Madongoporomoka.
⇒ Madongoporomoka-kwenye nyumba za udongo ambazo hubomoka hasa wakati wa mvua-makao duni-umaskini.

Mdokezo

⇒ Donda ndugu lililokataa kusikia dawa…

Chuku

⇒ Sakata ina makabila arobaini kama wengine waaemavyo, yapo makabila mawili tu, maskini na matajiri.
⇒ Ukata uliokuwa umewafunika na kuwafanya wa kabika moja la wachochole.-hali mbaya ya umaskini.
⇒ Meno yangu karibu kudondoka kwa hasira nilizokuwa nazo nikijaribu kumtafuna mwanamke aliyemnyaka babu kibao shavuni.
⇒ Mnuko ulioweza kulipua pua-harufu mbaya huko madongo.
⇒ Kitanga changu cha mkono kilizama katika bahari ya kitanga chake (babu) kikubwa.
⇒ Mabanda-labda yanaweza kuanguka kwa upepo wa mtu apigaye mbinja-kuonyesha udhaifu wayo.
⇒ Kidimbwi cha jasho kikawa kinajisawiri kwenye ncha ya mwanzi wa pua yake-babu kuogopa.
⇒ Nilipiga unyende nikalia machozi mpaka yakanikauka.
⇒ Ndoa ya babake na mamake msimulizi ilikuwa ndoa moja katika maelfu.-kuonyesha ubaguzi, ukabila.

Methali

⇒ Yaliyopita hupishwa-anaonelea anastahili kusahau tanzia ya babuye.

⇒ Kinolewacho hupata-mama yake kurithi mila za Wasubu.

Utohozi

⇒ Ekari tano-shamba babu yake alilomiliki

⇒ Mwekeni tairi-gurudumu ili achomwe.

⇒ Hospitalini-mjini ambako babu alipelekwa akatibiwe

Balagha

⇒ Kwao wapi?-babu

⇒ Kwao mashambani au vijijini?

⇒ Yaani mtu kwao hakuwezi kuwa jijini?

⇒ Mtu atasemaje haya ninayosema kuhusu mama yangu ni uongo?

⇒ Mama yangu hakuwa mtoto wa Kitantele aliyelelewa katika mazingira yaliyomzunguka na kunga na kaida za Wasubu?

Mdokezo

⇒ Ingawa mimi nilifurahi hadi… -msimulizi kufurahi babu alipopelekwa mjini akapelekwe hospitali ya jiji.

⇒ Unyende wangu ulipotelea kwenye mzozo uliotokota nje…

Tashbihi

⇒ Wamindi kuoana na makabila mengine hutokea kwa tukizi kama kupatikana kwa mwanasiasa mwadilifu. (uongozi mbaya)

⇒ Vilango vilivyosimama vizingitini kama vibua vya mtamaa vinavyosubiri kuanguka.-makao duni

⇒ Ulimi wake ulikuwa mwepesi kusarifu kisubu kama mwenyeji-wa mamake msimulizi.

Taswira

⇒ Tope jeusi, vichochoro kujaa tope, fodogoo na kila aina ya uozo-uchafu mwingi.

⇒ Mabanda yaliyoinamiana na kuoneana imani

⇒ Kuta za mbavu za mbwa, mabati yaliyojifunika libasi ya kutu.

⇒ Kina mama kuuza chapatti zilizokaukiana na mandazi makavu na maembe dodo.
⇒ Vitoto vingi vya maji ya kunde. Viwili vitatu ndivyo vilikuwa vyeusi kuliko masizi ya chungu cha nyanya wa kabucheka.

Nidaha

⇒ Salaala! Mbona wasirudi kwao wakaishi maisha ya maana kidogo?
⇒ Jamani! Jijini kuna maisha ya kukatisha tamaa sana.-babu alipoona umaskini wa madongo

Utohozi

⇒ Rekodi za santuri-alikosikia babu mtaa wa kochokocho ukiimbwa ndipo akataka wakautembelee.

Tabaini

⇒ Si siahi, si mayowe, si miluzi almuradi fujo moto mmoja.

Taharuki

⇒ Kwa nini kina mama wanaofanana na msimulizi wanamtumbulia macho kama waliona kioja?
⇒ Nini kilifanyika baada ya babu kuuuawa?
⇒ Wauaji walijulikana?
⇒ Walichukuliwa hatua gani?
⇒ Hatima ya ndoa ya wazaziye msimulizi ilikuwaje baada ya kukataliwa?
⇒ Msimulizi alijulikana alikotoka vipi baada ya babu yake kuuawa?

Kinaya

⇒ Baba ya msimulizi ni mrakibu wa polisi ilhali baba yake anauawa kinyama kwa kupigwa na kuchomwa moto.
⇒ Babu Maende japo anaugua ilhali hataki kwenda Pilka kutibiwa bali alilazimishwa.
⇒ Kuuawa baada ya kupona ugonjwa uliomleta siku moja tu kabla ya kurejea kwake.
⇒ Kuambiwa ndoa ilipingwa na pande zote mbili kisha kuna maelewano kati ya mababu na bibi na babu kutembeleana.

10.Ndoa ya samani

⇒ Ndoa kutojengwa kwa misingi ya mapenzi ya dhati bali mali-samani.
⇒ Kuangalia mtu badala ya utu.
⇒ Abu anaghairi kumwoa amali na kurudi Arabuni.
⇒ Wazazi kuingilia ndoa za watoto na kuishia kuzivunja kwa tama zao.
⇒ Umaskini kuwa kikwazo cha mafanikio ya mtu.
⇒ Matatizo ya ndoa za matabaka tofauti.-utabaka kuwa kikwazo katika ndoa.

Utabaka

⇒ Kijijini kulikuwa na watu tajiri na maskini- Kina Abu ni maskini na kina Amali ni wa tabaka la kati-si maskini wala tajiri.

Ujinga

⇒ Amali kufanyiwa maamuzi na mamake yanayoishia kumponza.
⇒ Kumfilisi mwamamume anayekusudia kuolewa naye.
⇒ Kutojua tamaa mbele mauti nyuma

Utunzaji

⇒ Abu kutotapanya mali aliyoipata.

Unyenyekevu

⇒ Ukwasi haukumpa takaburi.

Ukarimu

⇒ Kuwajengea wazazi nyumba nzuri. (anaheshimu wazazi).
⇒ Kutoa mahari kabla ya kuoa.
⇒ Kusaidia baadhi ya jamaa kupata kazi arabuni
⇒ Kuwaajiri marafiki

Ubinafsi

⇒ Mamake amali kutohusisha wazazi wa abu katika mipango ya arusi.
⇒ Kutofikiria maisha ya bintiye bali ataka ajipatie mali.

Bidii

⇒ Abu anatufahamisha hakuwa mzembe.
⇒ Alifanya kila sambuli ya kazi.
⇒ Akajijengea chumba cha msonge kilichokandikwa kwa udongo. (taswira)
⇒ Akaweza kujipatia chakula na kujinunulia nguo.
⇒ Arabuni anafanya kazi ya uhamali ambayo inamtajirisha.

Tamaa

⇒ Ya mama Zena mamake Amali

Upuuzaji wa majukumu

⇒ Babake Amali mzee Kadiri kutomdhibiti mkewe na kutotoa kauli yake.

Utamaushi

⇒ Nilitamauka-kukata tamaa baada ya posa yake kukataliwa.

Utamaaduni

⇒ Mila ya mahari kuwa kikwazo cha vijana kufunga ndoa kwa sababu ya umaskini.

⇒ Mjomba kuhusishwa katika suala la ndoa.

⇒ Nyimbo za ndoa

⇒ Utozaji wa bwana arusi pesa aendapo kumchukua bibi arusi.

Nafasi ya mwanamke katika jamii

⇒ Chanzo cha matatizo ya mwanamke mwenzake au kikwazo cha mafanikio yao.

⇒ Wana usemi/sauti-babake amali kushauriana na mama zena anapoelezwa na mjomba wa Abu lengo la ujumbe wao.

⇒ Mfanya maamuzi badala ya mwanamme au wanaodhibiti waume zao- “Amali hataki kuolewa, tena sijui kama utaweza mahari.” (waongo)

⇒ Yoyote yaliyoamriwa kwake babake Amali yalikuwa mamoja.

⇒ Nyenzo ya kiuchumi

⇒ Wapotoshaji-kumpotosha amali aitishe mali

⇒ Kiumbe duni kisichoweza kujidhibiti-babake kutaka amali aolewe asizalie nyumbani.

⇒ Wananyimwa haki ya kujiamlia mambo yao.

⇒ Wabaguzi

⇒ Wabinafsi

⇒ Wana tamaa, wapenda makuu-mama Zena.

Imani kwa Mungu

⇒ Abu baada ya posa yake kukataliwa na kuamua kusahau mambo ya kuoa alimwomba Mungu ampe mke mwema ambaye angempenda jinsi alivyo.

Uadilifu

⇒ Mwone mtoto amejihifadhi katulia kwao wala si kiguu na njia-Amali.

Ulevi

⇒ Fahami na jamaa wengine walikuwa wakifaidi mairungi-miraa-alipomwambia waende nyumbani.

Umaskini

⇒ Sina sinani, nikiulizwa siungami.

⇒ Abu alisaka kibarua kwa walalaheri na walalahoi.

⇒ Jamaa zake wa karibu walikuwa hohehahe.

⇒ Kijiji kwao walikuwa maskini waliokuwa wakipigiwa mfano.

⇒ Amali nilikuwa fukara wa kutupwa.

Matumizi ya lugha

Utohozi

⇒ Suti-aliyovaa Abu kujiandaa kwa arusi.

⇒ Motokaa-inayombeba Abu siku ya arusi.

⇒ Hospitali-abu alikotakiwa kufanyiwa uchunguzi Abu kabla ya kusafiri Arabuni.

⇒ Kampuni –ya uchukuzi iliyokuwa imemwajiri huko Arabuni.

⇒ Pasipoti-cheti alichohitaji ili kwenda arabuni.

⇒ Mita mia mbili-nyumba bi arusi alikokuwa kutoka mahali walipoegesha gari.

Nahau

⇒ Baada ya kutajirika akaamua kujaribu bahati yake ya kuuasi ukapera-kuoa.

⇒ Sikuwaacha mkono-hakuwapuuza au kuwatenga marafiki zake wa zamani-aliwaajiri.

⇒ Nilikata shauri-pale aliamua kusahau mambo ya kuoa na kuomba Mungu ampe mke mwema ambaye angempenda jinsi alivyo.

⇒ Walikuwa wamefurahi ghaya ya kufurahi-binamu, mdogo wa Abu na jamaa yake kufurahia arusi kupindukia.

⇒ Nimezama katika bahari ya luja-mawazo mengi akiwa garini kuelekea kwa bi harusi.

⇒ Alitimiza mahitaji hayo yote shingo upande-bila hiari/kujilazimisha.
⇒ Mamake kung'ang'ania mtoto wake aandaliwe arusi ya ndovu kumla mwanawe-ya kukata na shoka-kubwa.
⇒ Sikuwa mwenye navyo-tajiri.
⇒ Ilifika mahali fulani nikaamua kupata jiko-kuoa.
⇒ Nilitamauka-kukataa tamaa baada ya posa yake kukataliwa.
⇒ Nilikata shauri kusahau mambo ya ndoa kwa muda-niliamua.
⇒ Usife moyo mwanangu ndoa hupangwa binguni-usikate tama-mjomba baada ya posa kukataliwa.
⇒ Abu alisaka kibarua kwa walalaheri na walalahoi-maskini na matajiri.
⇒ Jamaa zake wa karibu walikuwa hohehahe-maskini.
⇒ Nilikuwa nimeshakata kauli-Abu kuamua kutomwoa amali kwani hampendi ila anapenda mali yake.

Misemo

⇒ Sina sinani, nikiulizwa siungami-umaskini

Chuku

⇒ Bahari ya kitanda-kitanda kikubwa sana.
⇒ Mlangoni nilikaribishwa na harufu ya manukato iliyozidi kiasi cha kukera pua badala ya kunukia.
⇒ Nyimbo za kina mama kuhanikiza janibu zote.
⇒ Miteteo mitamu yenye uwezo wa kukilainisha chochote hata kiwe kigumu kama almasi.
⇒ Nilikuwa fukara wa kutupwa.
⇒ Kijiji kwao walikuwa maskini waliokuwa wakipigiwa mfano.

Mbinu rejeshi

⇒ Jinsi alivyokuwa maskini miaka saba nyuma.
⇒ Alipiga darubini nyuma huko mambo yalikoanzia kiasi cha kujikuta katika hali hiyo-mtanziko-kufikiria kwa kina jinsi alivyopelekwa na mjombake kumposa amali mamake akakataa posa yake.

Taharuki

⇒ Nini kinasababisha wasiwasi wa msimulizi?

⇒ Baada ya abu kuondoka shamra shamra za ndoa ziliendelea au zilikoma?
⇒ Sababu ya abu kuvunja ndoa ilijulikana?
⇒ Amali aliolewa au aliendelea kukaa maisha ya ukapera hadi kifo chake?
⇒ Abu alioa mwanamke mwingine au alighairi kabisa kuoa?

Takriri

⇒ Wimbo-hongera mwanangu eeh hongera a! Mama uchungu mama uchungu
⇒ Kula kwa taabu, kuvaa kwa taabu-umaskini
⇒ Kupata vitu hivyo nilikuwa nimejikalifu ziada ya kujikalifu-amefipata kwa shida-kifurushi cha majani chai, sukari na marashi.
⇒ Mipango ya ndoa kukamilika hadi kufikia siku ya siku-siku ya arusi.

Taswira

⇒ Vitu vingi nyumbani alikuwa amevinunua yeye
⇒ Majilisi ya kiarabu
⇒ Vimeza vidigividogo vya vioo
⇒ Zulia la kiajemi
⇒ Zinga la jokovu
⇒ Runinga kubwa ya rangi
⇒ Bahari ya kitanda
⇒ Godoro kubwa, mito miwili mikubwa
⇒ Shuka za kitanda na foronya zimepigwa darizi kwa nyuzi za rangi ya dhahabu-tamaa ya Zena.
⇒ Akajijengea chumba cha msonge kilichokandikwa kwa udongo
⇒ Amali haachi ushungi na anavaa mavazi ya sitara(decent)
⇒ Amali kumpelekea orodha ya vitu alivyovitaka kwa ajili ya arusi. Alipendekeza anunue samani kutoka Arabuni, akadai mikufu, pete hata herini, mkoba mzima wa nguo, majora na vitambaa na doto za kanga.
⇒ Mtoto kaumbika si haba! Ukiongeza kujipondoa pamoja na michoro ya hina mikononi na miguuni.

Tashbihi

⇒ Uzuri wa amali ulikuwa aula kama hizo pesa-adimu.

⇒ Miteteo mitamu yenye uwezo wa kukilainisha chochote hata kiwe kigumu kama almasi.

Kinaya

⇒ Mzee kadiri anataka amali amwondokee nyumbani asije akazalia huko ilhali hakatai msimamo wa mama ambao ulisbababisha bintiye asiolewe.

⇒ Kinaya abu kutoa mali nyingi amwoe amali kisha kumtelekeza siku ya ndoa.

⇒ Kukataa kumwoa ilhali makosa si yake bali amepotoshwa na mamake.

⇒ Kusifu urembo na tabia yake na anaishia kutomwoa ilhali amepotoshwa na mamake.

Nidaha

⇒ La hasha!-Abu kukataa hakuwa bahili kwa kutimiza mahitaji ya mama zena shingo upande bali aliuona ni ubadhirifu.

⇒ Abu! Changamka nawe. Hii ni siku yako eti!-binamuye.

⇒ Potelea pote! Liwalo na liwe.

Tashhisi

⇒ Amali sidhani kapenda kuolewa nami sikumwoa mimi bali ameolewa na mali yangu.

⇒ Mlangoni nilikaribishwa na harufu ya manukato iliyozidi kiasi cha kukera pua badala ya kunukia.

⇒ Gari letu liliyabinginya masafa polepole

Mdokezo

⇒ Wimbo-tuhangaike naye …

Methali

⇒ Atafutaye hachoki na akichoka keshapata.

⇒ Ya kesho ajua Mungu.

⇒ Ndoa hupangwa binguni.

Kejeli

⇒ Nilipata tetesi alikataa posa yake kwa kuwa hakuwa na uwezo wa kujilisha mwenyewe seuze binti yake.

Majazi

⇒ Mzee kadiri-asiye na msimamo.

⇒ Amali-kitega uchumi kama kazi.

Balagha

⇒ Mimi si yule waliyenikataa kabla sijenda arabuni?

Kweli kinzani

⇒ Abu kutajirishwa na kazi ya uhamali.

Nyimbo

⇒ Wa kwanza-bwana arusi ana majukumu mengi.

⇒ Pili-kujifungua si jambo rahisi na mwanamke anapojifungua hupongezwa.

11.Tazamana na mauti

⇒ Athari na furaha kupita kiasi/kutojidhibiti kwa furaha kuhusu jambo kwaweza kusababisha hasara-kufurahia ndoto yake kutimia.

⇒ Furaha kumfanya Lucy aendeshe gari bila makini kisha kupata ajali na kuaga dunia.

⇒ Falsafa-usikoke moto kabla ndege hujamtia mikononi.

⇒ Alitembea jiji hilo (London) ili kuliambia kwamba msichana mbichi na tajiri anakuja ili jiji lijitayarishe kumpokea hatimaye. (majivuno)

Bidii

⇒ Ya kupata anachokitaka

Upumbavu

⇒ Crusoe lulaghaiwa na Lucy kwa urahisi na kuamini kuwa anampenda bila kuchunguza.

Tamaa

⇒ Ya kwenda London

⇒ Kuwa tayari kutumia ulaghai kuingia London kama vile kujifanya mtalii, mwanafunzi, mkimbizi, n.k.

⇒ Ya utajiri

⇒ Atafanya kazi za siri kwa vile wanaolipwa mshahara hawaruhusiwi kufanya kazi.

Unafiki

⇒ Hampendi crusoe bali anataka kuingia London na kadhalika mali yake.

⇒ Anataka mali anapomtunza.

⇒ Furaha ya Lucy hata kutokwa na machozi ya mamba si shukrani ya dhati.

⇒ Ana hamu ya afe haraka- Hamu ya kutaka mzee yule afe ilizidi maradufu. Angemuua lakini aliogopa sheria.

Elimu

⇒ Mtazamo finyu kuhusu elimu

⇒ Haiwafaidi watu sana-haimtajirishi mtu

Upotoshaji kuhusu maisha ya ulaya

⇒ Habari –pauni 40 hazitoshi kumtunza msafisha choo kazi ni kung'ang'ania balaa.

Uhaba wa kazi

⇒ Anajua kwamba hapa pao nchi ya firauni siku hizi hangepata hata hiyo kazi ya tonge la ugali sikwambii muluki.

Ukengeushi

⇒ kuolewa na mzee.

Ubahili

⇒ mtu bahili na mtunzaji kama yeye atazizalisha pauni arobaini ziwe elfu arobaini. (chuku)

Matumaini/kutokata tamaa

⇒ Miaka mingi kupita bila kwenda uingereza lakini hajakata tamaa

⇒ Alijiaminisha kuwa kila alichokitaka hukipata

⇒ Yeye siku moja ataiona London

⇒ Lini ataiona London, hakukata tamaa japo jibu ni gumu

Matumizi ya lugha

Uhuishi

⇒ Alitembea jiji hilo ili kuliambia kwamba msichana mbichi na tajiri anakuja ili jiji lijitayarishe kumpokea hatimaye.

⇒ Minyororo ya kufungika kwa hamu ya uingereza ilizidi kuufunga moyo wake-tamaa kuzidi

⇒ Ndoto ya lucy ya miaka mingi kupevuka na kujikopoa nje ya akili yake, kuiona imesimama mbele yake kwa dhahiri

⇒ Jiko la chini na juu linamwambia mwenzake asogee huko

⇒ Huku akiacha tabasamu yake imemganda mzungu moyoni mwake

⇒ Kiu ya kuenda London ilikuja kumkaa mioni(kooni) ikamchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri Jangwani kwa miaka mingi bila kugundua maji

Tashbihi

⇒ Kiu ya kuenda London ilikuja kumkaa mioni(kooni) ikamchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri jangwani kwa miaka mingi bila kugundua maji
⇒ Lakini wakishafanya hivyo humpita kama upepo wa kibunga na kumwacha yeye mgonjwa wa tamaa
⇒ Nguo na mavazi aliyonunuliwa juzijuzi ni kama aliyonunuliwa mwaka mzima

Utohozi

⇒ Sinema/filamu-alikokuwa akiona Wingereza
⇒ Pauni arobaini kwa wiki-mshahara wa mkimbizi uingereza wa juma.
⇒ Televisheni, friji-miongoni mwa vifaa ambavyo lucy amesikia wakimbizi hupewa na serikali
⇒ Picha zinazotembea-katika filamu

Kuchanganya ndimi

⇒ Squares-viwanja vya nafasi huko
⇒ Love in London-mchezo uliokuwa ukionyeshwa katika filamu

Balagha

⇒ Kuonyesha ulaghai watu wanaotumia kuingilia mataifa ya magharibi.
⇒ Ajifanye mgonjwa mahututi na maradhi yake hayatibiki hapa pao?
⇒ Ajifanye anakwenda kusoma?
⇒ Tokea lini mtalii mifuko yake iwe mitupu?
⇒ Huyo mwanamume kutoka uingereza atakayekuja kumwoa yeye yuko wapi?
⇒ Nani atakayetoka uingereza kuja kumwoa yeye?
⇒ Vipi Lucy ataingia uingereza?
⇒ Kama si peponi huko ni wapi?
⇒ Waliosoma anawaona nao wamepata nini?
⇒ Kufa kwa mzee huyo si kuko karibu tu?-wakati amechoshwa na siku kusonga polepole.
⇒ Lini angepata nafasi ya kupenya kwenye chungio na kudondokea uingereza?

Taswira

⇒ London barabara zake pana zinazojaa magari na watu pomoni wanaokwenda na kurudi kike kwa kiume vijana

na wazee wote waliovaa kifahari na kitajiri maduka mengi yaliyopachanapachana ambayo hujaa bidhaa za kila aina.

Mdokezo

⇒ Muziki na hasa madisko na sinema…
⇒ Pumzi zinanisonga…Crusoe ana ugonjwa
⇒ Mtaji mkubwa… unaohitajika mtu awe nao kama anaenda kusoma
⇒ Kesho kutwa…waende kwa wakili akaandikishwe utajiri wote wa Crusoe
⇒ Akajiona…la hapana…kutoamini angerithi mali yote ya Crusoe.

Sitiari

⇒ Tama ya kwenda London kuitwa kiu
⇒ Wewe umegeuka sungura aliyezikosa zabibu
⇒ Ni peponi-uingereza
⇒ Eti wanaiita jahanamu-wanaoharibia uingereza jina

Mbinu rejeshi

⇒ Juzi amemaliza shule ya upili ya juu yaani kidato cha sita lakini hakufaulu vizuri
⇒ Hakujali kutofaulu vizuri kwa sababu hakuwa na hamu ya masomo. Hataki riziki kama waliosoma ataka muluki-mali nyingi.

Nahau

⇒ Kazi yake lucy ni kumkanda na kumsinga mafuta mafuta na mafuta ya mgongo wa chupa -unafiki

Takriri

⇒ Siku ingia siku toka miezi pita miezi rejea-muda mrefu kupita bila kufanikiwa kwenda Uingereza

Chuku

⇒ Lucy kumtunza Crusoe mara mbili kama si tatu ya zamani-asikose urithi maana akaribia kufa
⇒ Kumwacha yeye mgonjwa wa tamaa
⇒ Nguo alizonunuliwa juzijuzi tu ni kama alizonunuliwa mwaka mzima
⇒ Viatu havina idadi
⇒ Hawezi hata kutema mate mzee wa watu

⇒ Mtu bahili na mtunzaji kama yeye atazizalisha pauni arobaini ziwe elfu arobaini.

Sadfa

⇒ Lucy kuwa na tamaa ya kwenda Uingereza kusadifiana na Crusoe kutokea na kumsaidia kwenda huko-akipanda ngazi kuelekea sinema.

⇒ Akamwahidi angempa zawadi baada ya sinema kwa kumzuia asianguke anaposhikwa na ugonjwa-(shukrani, ukarimu)

⇒ Lucy kuahidiwa kuandikishwa mali na anapoenda mjini hakurudi tena. Kupata ajali na kupoteza roho yake na maiti kuhifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti.

Misemo

⇒ Watasema mchana na usiku watalala-hawawezi kumwathiri

⇒ Mafuta ya mgongo wa chupa –kujifanya anampenda

⇒ Mapenzi ya kurambishwa asali moja kwa moja kutoka sega la asali.

⇒ Kupaka rangi mbaya uingereza-kuienezea sifa mbaya

Tafsida

⇒ Angemlaza-angemuua Crusoe

⇒ Hawezi kumchangamsha kwa namna yoyote

⇒ Ndiyo ni mwanamume asiye na nguvu ya aina yoyote lakini ana utajiri

Kinaya

⇒ Crusoe kumshukuru Lucy akidai hajapata kumwona mwanamke mwenye imani kama yeye

⇒ Ana bahati kuliko wazee wote wenye umri kama wake kukutana na msichana mwenye huruma kama yeye

⇒ Kutamaani Crusoe afe haraka kumbe ndiye anatangulia na ndoto yake kushindikana

Taharuki

⇒ Baada ya Lucy kufa nani alirithi mali ya Crusoe?

⇒ Alizikwa wapi?

⇒ Siri kwmba hakumpenda Crusoe ilijulikana au alikwenda nayo kaburini ?

12.Mwana wa darubini

⇒ Kananda kuomba asaidiwe na darubini kwa kutoweza kukaribia nyumba ya Mwatela amuone Mwakitawa
⇒ Kujiridhisha nafsi yake kwa kumwangalia mtoto wake
⇒ Kananda kumwita mwanawe mwana wa darubini

Maudhui

Utambuaji wa makosa na toba

⇒ Mwatela kumwandikia Kananda barua ya kumwomba msamaha
⇒ Nimebaini nimekosa mwisho wa kosa
⇒ Katika vita baina ya ubaya na wema, wema daima hushinda
⇒ Angemlipa maovu aliyomfanyia-fidia kwa kumpa nyumba ya kifahari
⇒ Kujitolea kumwelimisha Mwakitawa mpaka afike alikotaka
⇒ Wakili amtafute
⇒ Atie sahihi makubliano-kufuata hatua za kisheria

Ufarikishaji

⇒ Kuzuia Mwakitawa wakutane na mamake kudai ni adui na amepanga kumteka nyara adai pesa 2,000,000 amwachilie
⇒ Asipomlipa atamuua
⇒ Achezee nyumbani
⇒ Akampa silaha-kisu na manati

Adhabu/kisasi kwa maovu

⇒ Mwatela kufutwa kazi kwa ulevi
⇒ Mtoto wake kufa
⇒ Mkewe kuchomeka
⇒ Kulipa fidia
⇒ Kuugua
⇒ kufa

Ulevi na athari zake

⇒ Kupiga mkewe na kusababisha nyumba yake kukosa amani
⇒ Kumbaka yaya wake au kutokuwa mwaminifu katika ndoa/kwa mkewe

⇒ Kufutwa kazi

Dhuluma dhidi ya wanawake

⇒ Kananda kubakwa
⇒ Kulaghaiwa
⇒ Kutoroshwa nchi yake
⇒ Kunyang’anywa mtoto
⇒ Kuoza bila hiari kwa mtu asiyempenda
⇒ Kuuzwa utumwani

Migogoro

⇒ Kupiga mkewe wakati wa ugomvi
⇒ Basi mwite mwakitawa sasa hivi na umwambie ukweli kwamba alikuwa anaua mama yake mzazi

Ubwana na utwana

⇒ Bwana na bibi Mwatela walimwajiri Kananda kama yaya

Umaskini na athari zake

⇒ Wazazi wa Kananda walikuwa miongoni mwa akina pangu pakavu waliokuwwa umma mkubwa nchini
⇒ Wazazi wa Kananda kushindwa kumpeleka shuleni
⇒ Kusababisha kananda aendelee kufanya kazi kwa Mwatela na kumsababishia madhila
⇒ Kushindwa kusaidia Kananda kudai haki kupitia vyombo vya sheria

Imani kwa Mungu

⇒ Kananda kuendelea kumwomba Mungu siku moja amwonee huruma amkutanishe na mwanawe
⇒ Aliamini siku moja Mungu angemkutanisha na mwanawe

Mapenzi ya dhati

⇒ Kananda kwa mwanawe
⇒ Kujitahidi kumtafuta
⇒ Ami yake mbao kusaidia kananda kupata darubini
⇒ Mwatela kuendelea kumpenda mkewe hata baada ya kuchomeka na kuharibika sura
⇒ Upendo wa maria kwa mumewe kwa kuvumilia ulevi na uzinifu wake
⇒ Kukaa naye hata baada ya kufukuzwa kazi na kuishi kwa shida
⇒ Kumsamehe kwa kuzaa nje ya ndoa

Ujasiri

⇒ Kupigania haki ya kumuona mwanawe

Subira na ustahimilivu

⇒ Kuchukua muda mrefu wa kumwangalia mwanawe

Uoga

⇒ Kumwogopa Mwatela na kuamua kumwangalia mtoto kwa darubini

Nafasi ya mwanamke katika jamii

⇒ Maria ni mkombozi
⇒ Ni punda wa huduma
⇒ Ni jasiri
⇒ Hakati tama
⇒ Ni chombo cha mwanamume cha kujiburudisha
⇒ Amenyimwa elimu
⇒ Ana sauti/usemi
⇒ Mvumilivu
⇒ msamehevu

Ukarimu

⇒ Mbao kujitolea kuuza kuku na mbuzi ili kupata pesa za kumnunulia Kananda darubini-kujali maslahi ya wengine

Bidii

⇒ Mwatela kuanza biashara na kutajirika

Ukweli

⇒ Maria kumwambia Mwakitawa ukweli kuhusu mamake

Ujirani mwema

⇒ Jiraniye Mwatela kumshauri kupiga ripoti polisi kuhusu mama mwenye darubini

Mabadiliko

⇒ Mwatela kufutwa kazi
⇒ Kuacha ulevi na kuanza biashara ya uvuvi na kuuza samaki
⇒ Kutajirika
⇒ Mkewe kuwa mwalimu

Udanganyifu na athari zake

⇒ Nusura Mwakitawa amuue mama yake kwa kumdanganya ni adui
⇒ Mwatela kuishi kwa wasiwasi akihofia angejulikana

⇒ Ugonjwa wa shinikizo la damu kwa kuwaza sana namna ya kuficha ukweli
⇒ Kulazimika kulipa fidia Kananda kwa yote aliyomtendea
⇒ Mwatela kumkosa mtoto wake wa pekee kwa kutotaka kuishi tena na babake kwa ulaghai aliomfanyia
⇒ Mtoto kudanganywa mama yake alikufa alipozaliwa
⇒ Mwatela kupeleka ujumbe kwa wazazi wa Kananda kwamba mwanao alitoweka na hakuna aliyejua alikotorokea
⇒ Hakumwoa kananda kama alivyomwahidi
⇒ Amwambie mama Sami mimba ni ya rafiki yake wa huko nyumbani kwao.

Tanzia

⇒ Moto kuua watu watano-watoto wawili na watu wazima watatu
⇒ Maria kuchomeka vibaya

Matumizi ya Lugha

Mbinu rejeshi

⇒ Kananda alizaliwa wakati wa enzi ya ukoloni nchini Kenya
⇒ Uhuru ukitangazwa alikuwa na umri wa miaka kumi na mine
⇒ Wazazi wa kananda walikuwa maskini na hawakuweza kumsomesha alikaa nyumbani
⇒ Jioni ulevi ulimtuma Mwatela kumtia doa Kananda
⇒ Usiku Kananda alipata maumivu ya kujifungua uliotokea mkaza wa moto

Utumwa

⇒ Dereva kuishi na Kananda kwa miezi kadha kabla ya kumuuza kama mtumwa kwa mtu mwingine

Nahau

⇒ Alipanga njama ya kinyama-kumnyang’anya kananda mtoto na kupanga na dereva wa malori makubwa ya Kongo amchukue amfanye mkewe
⇒ Kumtia moyo-kumletea habari za kumpa matumaini ya kumpata mtoto wake kuwa mwatela alihamia Mombasa na mwanao

⇒ Yu hali mahututi-aliporudi kutoka hospitalini
⇒ Nitakutoa roho-angemuua angemwambia mke wake
⇒ Kumtia doa Kananda-kumbaka mkewe alipotembelea wazazi wake
⇒ Kichapo cha mbwa-kikali
⇒ Jaribio la mama Sami kujiokoa liligonga mwamba-lilishindwa
⇒ Walifurahi ghaya
⇒ Hasira za mkizi-zinazomletea mtu hasara
⇒ Wazazi wake walikuwa miongoni mwa akina pangu pakavu waliokuwwa umma mkubwa nchini-maskini hangeweza kusomeshwa kwa sababu ya uchochole wao alikaa nyumbani
⇒ Bwana mwatela alipenda kuchapa mtindi-kunywa pombe
⇒ Wazazi wa kananda walifurahi ghaya -sana hadi upeo wa furaha

Kuchanganya ndimi

⇒ Kampuni ya simba breweries-anakofanya kazi Mwatela
⇒ Oh my god! Mwakitawa! Mwakitawa! Njoo haraka baba yu taabani!
⇒ Benjamin, please don’t die

Utohozi

⇒ Kampuni

Misemo

⇒ Kweli mungu hamtupi mja wake
⇒ Hulka ya mtu haifichiki kwa muda mrefu.
⇒ Kumbe ile asali chungu ilizaa karaha-mimba
⇒ Kananda alilala maskini akaamka tajiri
⇒ Kumbe maisha ni fumbo-barua kwa kananda

Tashhisi

⇒ Jioni ya siku hiyo ulevi wa mwatela ulimtuma kumtia doa kananda
⇒ Ulevi huu ulimpeleka bwana Mwatela katika ngazi nyingine-kumchokoza kananda kwa kumtaka mapenzi
⇒ Kimya chake kikawa kinamchoma ndani kwa ndani

Chuku

⇒ Alilia usiku na mchana

Balagha

⇒ Uniulie nini na ndoa yetu na wewe inamhusu pia yeye?
⇒ Nilikuwa namuua mama yangu?
⇒ Mamangu yupi?
⇒ Nimuue kwa nini?
⇒ Ungemwambia ukweli upi isipokuwa ule niliomwambia?

Uzungumzi nafsia

⇒ Mbona Benjamini Mwatela aliniambia mama yake Mwakitawa alifariki?

Sadfa

⇒ Usiku mmoja wa manane kananda kupatwa na maumivu ya kujifungua na usiku uo huo moto kuzuka katika nyumba ya jirani ukaenezwa na upepo na nyumba ya mwatela na kuangamiza mtoto na kumchoma mama vibaya.
⇒ Mwatela kupelekwa hospitalini alikokuwa amelazwa kananda
⇒ Mwakitawa kutoweka kwa siku nne

Tabaini

⇒ Wazazi wa kananda wakisaidiwa na mbao waliuza vitu vidogovidogo si mbuzi si kuku ili wapate pesa za kununulia darubini

Taharuki

⇒ Mwakitawa alipotoweka kwa siku nne alikuwa wapi?
⇒ Mama angepona baada ya kuchomeka vibaya?
⇒ Mwatela kweli angemuoa?
⇒ Wangefaulu kupata darubini?
⇒ Kananda angefaulu kumtoa mwanawe mikononi mwa Mwatela?

Nidaha

⇒ Mariaa! Kwani hungeweza kusubiri nitoke hospitalini nimwambie mimi mwenyewe?
⇒ Oh my god! Mwakitawa! Mwakitawa! Njoo haraka baba yu taabani!
⇒ Benjamin, please don’t die

Methali

⇒ Mungu si athumani

Taharuki

⇒ Mwisho wa Mwatela ulikuwaje?

⇒ Je alipata mtoto mwingine au alikufa bila mtoto?
⇒ Mwatela na maria walihamia wapi baada ya kumkabidhi kananda nyumba?

13.Mizizi na matawi

⇒ Sitiari-mtoto asiye na wazazi wawili hupata shida kama vile miti hupata ikikosa mizizi na matawi
⇒ Watu huweza kupoteza mizizi na matawi yao lakini bado akabaki mtu
⇒ Mama Sudi alikuwa ni mizizi na baba Sudi alikuwa ni matawi

Maudhui

Nafasi ya mwanamke

⇒ Mlezi mzuri-mama Sudi kumpa malezi mazuri
⇒ Mpatanishi

Athari ya maisha yasiyo ya uadilifu ujanani

⇒ Mimba nje ya ndoa
⇒ Kutupa mtoto
⇒ Kuteseka kwa kumkosa mtoto-umaskini kwa kukosa msaidizi
⇒ Athari za kisaikolojia

Upatanishi

⇒ Sudi mwanangu naomba usahau yote yaliyopita umpokee Bi. Kudura uwe naye kwa hali na mali kuliko hata vile ulivyokaa na mimi-hana ubinafsi (mkweli)

Anasa/starehe na athari zake

⇒ Sudi ana wapenzi kadha-Waridi na Ridhaa
⇒ Mamake halisi Bi. kudura alimtupa ili aendelee na anasa

Udanganyifu

⇒ Sudi kuitwa jina lisilo na uhusiano na la babake wala ukoo wake
⇒ Kumdanganya babake ni Sudi bin Abdalla
⇒ Vile walioana kwa mapenzi makubwa
⇒ Vile alifariki
⇒ Uongo wa mamake ulibainika-njia ya mwongo ni fupi

Ukarimu

⇒ Kumwokota na kumlea
⇒ Kutokana na ukarimu wa sudi wa kumwajiri Bi. Kudura anakuja kumpata mamake halisi.

Heshima

⇒ Sudi hakutaka kumtuma kudura kwa kumwona amemzidi umri

Umuhimu wa mtoto

⇒ Ukitaka kujua hasara za kukosa mtoto tazama faida za mwenye mtoto

Utambuaji wa makosa na kutubu

⇒ Anamuomba Mungu amsamehe

Elimu

⇒ Sudi kusomea shahada ya juu ya udaktari wa sheria nchini moja ulaya

Heshima/mapenzi kwa wazazi

⇒ Kumwajiria mtumishi

Matumizi ya lugha

Balagha

⇒ Nani?-hakuna aliyekosa kujua kuhusu mapenzi yao
⇒ Bila shaka ungemuita asingekataa kuitika na kwa nini akatae?
⇒ Mara ngapi Sudi amekuwa akimuuliza mama yake habari za baba yake?
⇒ Mwanangu tangu lini kipwendacho kikadumu?
⇒ Inakuwaje mtu akiambiwa yeye ni kiumbe wa kuokotwa?
⇒ Husimamaje?
⇒ Huendaje katika dunia ya masuto na nazaa matusi aibu na fedheha?
⇒ Atafayaje Sudi?
⇒ Furaha yangu itoke wapi tena?
⇒ Kwa nini mama yake amfiche?
⇒ Kwa nini asimwambie ukweli?
⇒ Au apige moyo konde afichue siri?-ajikaze kufanya jambo gumu-kusema ukweli
⇒ Hapa alipo mayai yamemuisha mtoto angetoka wapi?
⇒ Angemuambia tu mwenyewe akajua maana kama uharamu utakuwa wa mtoto, kosa la nani?

Nahau/misemo

⇒ Yaliyopita huwa yamepita nasi huwa hatuna uwezo wa kuyarejesha.
⇒ Dunia kuna mambo na katika hayo mambo kuna majambo-maajabu
⇒ Mamake alikwisha mtengenezea kiamsha kinywa-chakula au kinywaji cha asubuhi
⇒ Hunipeleka mbali ya siku zile za asali na maziwa.
⇒ Ndio Kudura huja tukaondoka-tunazaliwa na kufa
⇒ Mahali pa kuweka ubavu-Sudi mamake awe akimpa mtumishi mahali pa kulala
⇒ Atauliza tu ajue moja-mbivu au mbichi-ukweli na uongo wa mambo
⇒ Kukata tamaa-kupoteza matumaini ya kumjua/kumwona babake
⇒ Suti aliyovaa ilimtoa akatoka
⇒ Mapenzi yangu kwake yakazidi mno tangu alipoingia ndani-yaani aliponioa
⇒ Ndipo nami nikampenda kufa na kupona
⇒ Tukapendana kwa moyo mmoja
⇒ Kuna kupata na vile vile kukosa
⇒ Ajue asili na fasili yake-alitaka kumjua babake
⇒ Kupiga deki

Mdokezo

⇒ Ndiyo…maana hata mwenyewe hakuwa na uhakika na uhakika wa jina Lake.
⇒ Basi akawa akiitwa Sudi … Sudi Abdalla

Methali

⇒ Kipendwacho hakidumu
⇒ Damu iliyo daima nzito kuliko maji
⇒ Nguvu za maji ni mawe mlimwengu ni mwanawe
⇒ Kuvyaa kupoma-mamake kukumbuka kauli ya wahenga
⇒ Mungu akuwekavyo ndivyo ukaavyo-majaaliwa
⇒ Mungu akikupa kilema hukupa na mwendo

Tashbihi

⇒ Sudi alikuwa anamuona babake sawa na mhusika wa hadithini-kwa mawazo tu
⇒ Kila siku n’na jambo n’nataka n’kuulize lakini ulimi mzito kama nanga

⇒ Nilimlea mwenyewe naye akakua kama mgomba
⇒ Wote wakalizana kama waliofiwa
⇒ Kwa sudi maneno hayo yalikuwa msumeno butu unaokeketa kwa maumivu makali-yakimchoma sana
⇒ Mama mtu hujaribu kumtuliza na sudi hutulia japo si kama maji ya mtungi-hatulii kabisa

Takriri

⇒ Maneno yake daima yalikuwa hayo hayo
⇒ Abdalla baba yako-Abdalla bin Sudi

Mbinu rejeshi

⇒ Mamake hakufanikiwa kupata mtoto
⇒ Mungu akampa mtoto mzuri wa kiume kwenye pipa la taka
⇒ Akashukuru mungu
⇒ Akamlea vizuri
⇒ Akakua kama mgomba, mnazi unachelewa
⇒ Akamsomesha
⇒ Mtumishi kusimulia kuhusu mtoto aliyemzaa nje ya ndoa
⇒ Alikitumbukiza katika pipa la taka
⇒ Sudi kukumbuka karamu ya siku kuu ya pasaka jinsi walivyokuwa na Waridi kutoka Afrika Kusini- Gaboron

Chuku

⇒ Sudi alikuwa amewaniwa na kila mwanamke
⇒ Dunia yote ikawa yao na kila mtu ametosheka
⇒ Tokea kifaranga hadi kuku kila mtu alijua kuhusu mapenzi ya mamake na babake
⇒ Baba yako alinipenda bila ya kikomo
⇒ Tangu hapo nikawa mkiwa tena wa maisha

Tashhisi

⇒ Msiba mkubwa ukainiangukia-kifo cha mmewe bandia
⇒ Mkonyezo ulikoleza hamu katika noyo za vijana hata wasipate kukumbuka kilichowaleta ughaibuni
⇒ vyote hivyo vikaonekana kushiriki kikamilifu katika dhifa ile
⇒ Sudi alipiga gari lake moto na taratibu likatambaa na kuanza kuyabungunya masafa kuelekea lilikokusudiwa
⇒ Tea breeze-walevi walikuwa wakizungumza na chupa zao za pombe

⇒ Mara Sudi akalipiga mkwaju-alielekea na gari likatimka kuelekea benki
⇒ Ndipo kudura ilipomsaka na kumshika mkono na kisha kumuongoza hadi ilipo damu yake.
⇒ Dunia ina rai zake
⇒ Kwa yule mtumishi wao yalimchoma kwa woga na wasiwasi
⇒ Bado nguvu ya shetani ikimtonesha kwa kumwambia mambo yangekuwa mazuri kama angekuwa na yai lake mwenyewe
⇒ Siku hazikusimama-zilikutwa zikachwa na maisha yakapungua na kuyoyoma
⇒ Alimkuta radhia ambaye alikuwa kachoka kugombana na wakati-kumngojea

Taswira

⇒ Sudi alikuwa kijana mwembamba, mrefu kwa kimo chake, mtanashati
⇒ Suti aliyovaa ilimtoa akatoka

Kuchanganya ndimi

⇒ wasichana kumuita handsome
⇒ Easter get together-karamu ya siku kuu ya pasaka
⇒ Karamu ilifanyika katika hoteli ya royal palm

Anasa/starehe

⇒ Ukumbi ulivuma kwa mtu na muziki, seuze machupa ya soda bia mvinyo na vinywaji vingine kemkem?
⇒ Watu wawili wawili mwanamume na mwanamke

Utohozi

⇒ Bosi-Bi. Kudura anavyomwita mama Sudi.
⇒ Tibirinzi-Tea Breeze-anasa-wacheza ngoma watoto kustarehe kwa bembea treni farasi n.k.
⇒ Walevi madensi madisco

Tanakuzi

⇒ Sudi na Radhia Tea Breeze Wakatazamana na kufurahi palipofurahisha wakahuzunika palipohuzunisha
⇒ Mlikuwa mseto wa furaha na huzuni

Koja

⇒ Yeye atakuwa akikusaidia kazi zako zote za nyumba-kupika, kufagia, kupiga deki (kupangusa na kusafisha sakafu, kufua na kila kitu.

Tanakali

⇒ Kauli yake haikutoka ng’o-mamake Sudi kwa kusikia kuhusu mtoto wa mtumishi anashindwa kusema

⇒ Sadfa

Sudi kumpa Kudura ajira bila kujua na kutokea kuwa ndiye mamake

Tabaini

⇒ Si sudi, si bimkubwa na wala si Kudura

Taharuki

⇒ Sudi alisemaje baada ya kufahamu mamake halisi?

⇒ Alimkubali mamake aliyemtupa?

⇒ Alimkubalia mamake mlezi aondoke?

Takriri

⇒ Basi watu walicheza mpaka wakacheza tena wakafurahi na wapenzi wao hata wakasahau matatizo yao

MSTAHIKI MEYA

MAUDHUI

Migogoro

⇒ Mgogoro wa Meya na wafanyakazi ili kuboresha mazingira ya kazi.

⇒ Baina ya Meya na Siki kwa kutotaka ushauri wake.

⇒ Baina ya Meya na Diwani III kwa kutotaka ushauri wake.

⇒ Baina ya Meya, diwani I na II na diwani III kwa kuwa mwadilifu na wanamtenga na Bili kuingizwa.
⇒ Viongozi na raia kwa kukiuka majukumu kunakosababisha migomo.
⇒ Viongozi na wanataaluma kama vile Siki na Waridi kutokana na mazingira mabaya ya kazi.
⇒ Baina ya Meya na jamii yote kwa umaskini na huduma duni za kijamii.
⇒ Baina ya Meya na askari kwa kuchoka kutumiwa kisha kumkamata na wenzake.

Nafasi ya mwanamke katika jamii

⇒ walezi/mzazi-mama
⇒ wahudumu-Dida
⇒ Anayekata tama/kupoteza matumaini-Waridi
⇒ Jasiri-mama Dadavuo Kaole
⇒ Wavumilivu-Dida
⇒ Watiifu-Waridi
⇒ Hapewi nafasi ya uongozi

Udanganyifu/uongo

⇒ Meya kudanganya baraza halina raslimali za kulipa wafanyakazi ilhali madiwani wanaongezewa mishahara mara kwa mara.
⇒ Kudanganya shehena nyingi zipo katika bahari kuu
⇒ Dawa zingewasili baada ya siku tatu na baada ya siku tatu kupokewa hospitalini.
⇒ Meya kudanganya dawa ziko njiani (shehena nyingi) kuonyesha baraza linajitahidi kuwajibika.
⇒ Baada ya kuiba fimbo wangedanganya raia kuwa ilipotea wakati wa rabsha.
⇒ Kumdanganya mhubiri kwamba ana wito wa kuacha uMeya na kumfuata.
⇒ Meya kumwambia Gedi awaambie wanahabari kuwa yuko mkutanoni.
⇒ Meya-baraza ni miongoni mwa yanayolipa waajiriwa vizuri

Ukweli

⇒ Diwani kutoboa siri kwamba ahadi za Meya ni za uwongo.

⇒ Anatengwa na Meya kwa sababu anafahamika ni mkweli.
⇒ Meya anakiri kuwa aliyoambiwa na diwani III ni ukweli.

Unafiki

⇒ Meya anajifanya anafanya kazi kwa manufaa ya umma ilhali anajinufaisha na washirika wake.
⇒ Meya na baraza lake wanataka kuonekana wawajibikaji kwa mameya wa nje ilhali sivyo.
⇒ Meya anajifanya mcha Mungu, mpole na mnyenyekevu na kwamba ana wito wa kumtumikia Mungu ilhali sivyo.
⇒ Meya kujifanya mpole kabisa anapomkaribisha mhubiri
⇒ Meya anajifanya ameguswa na mhubiri na kuwa husukumwa aache uMeya awe mhubiri.
⇒ Bili anajifanya anamshauri Meya kumbe anakusudia kujinufaisha.
⇒ Diwani I na II wanajifanya wanamshauri Meya kumbe wanajali maslahi yao.
⇒ Mhubiri anamuunga mkono Meya ilhali akijua hali ya raia ni mbaya ili anufaike.
⇒ Gedi anamtii Meya kwa maslahi yake kwa vile anavujisha siri kwa Siki.
⇒ Baraza linataka kuonyesha picha nzuri kwa wageni ili lipewe mikopo.

Ukatili

⇒ Askari wanaua watu katika kutuliza migomo.
⇒ Dida anafurahi wafanyakazi wanapofurumishwa kwa risasi.
⇒ Meya kutoona tatizo kwa mtoto mmoja kufa.
⇒ Meya hajali hali ngumu za wafanyakazi.
⇒ Diwani I anapendekeza nguvu zitumike kuzima mgomo.
⇒ Diwani I anaringia nguvu inayotumika kuwavurumisha wafanyakazi.
⇒ Diwani II anataka hatua kali zichukuliwe dhidi ya wachochezi-wapigwe ili watulie nyumbani
⇒ Meya anacheka wafanyakazi wanapotawanywa na polisi.

Utu

⇒ Siki ana utu kwa kumhudumia mama mwenye mtoto aliyezidiwa licha ya kutokuwa na hela.

⇒ Kwa kuendelea kuhudumia raia licha ya mazingira mabaya ya kazi.
⇒ Meya hana utu kwa kuwapa wafanyakazi chakula kilichopimiwa mbwa.
⇒ Siki ana utu kwa kumhudumia mama.
⇒ Askari hawana utu kwa kuwashambulia watu kwa risasi, magari ya maji na vitoa machozi hata kuwaua.

Usaliti

⇒ Askari kumgeuka Meya na kumkamata na kumuondoa mamlakani licha ya kuwalipa vizuri.
⇒ Askari badala ya kulinda raia wanalinda uongozi wa Meya.
⇒ Meya kusaliti waliomchagua kwa kutoleta maendeleo.
⇒ Meya kusaliti juhudi na ndoto za kupigania uhuru kwa kurudisha unyonyaji.
⇒ Diwani I na II kuwasaliti wananchi kwa kutumia madaraka kujinufaisha badala ya kuwanufaisha waliowachagua.
⇒ Bili anamsaliti Meya baada ya mambo kuharibika.
⇒ Mhazili kuungana na wafanyakazi kugoma licha ya kumuajiri bila sifa za kuajiriwa.
⇒ Gedi kutoa siri kwa Siki kuwa Meya hataki kumuona.
⇒ Diwani III aliyeteuliwa na Meya katika kamati yake kupinga mipango ya kumnufaisha Meya na kuungana na wafanyakazi.
⇒ Siki kuungana na wafanyakazi kuhimiza harakati za ukombozi dhidi ya Meya aliye binamu yake.
⇒ Wafanyakazi waliopaswa kumtii Meya kumgeuka na kumgomea.
⇒ Meya anamsaliti diwani III kwa kumtenga katika maamuzi (utengano)
⇒ Waridi anasaliti taaluma yake kwa kusisitiza wasio na pesa wasipate huduma na kujiuzulu kazi yake na kuwaacha wagonjwa wakiteseka.

Dini

⇒ Viongozi hutumia dini kuficha na kuendeleza maovu yao.
⇒ Meya anamtumia mhubiri kuendeleza uongozi wake mbaya.

⇒ Viongozi wa dini huweza kurubuniwa na waumini wasio waaminifu.
⇒ Meya anamdanganya mhubiri kwamba ana wito wa kuacha uMeya na kumfuata jambo ambalo si kweli.
⇒ Kuna wahubiri wanafiki na wenye tamaa ambao huunga maovu mkono ili wanufaike.
⇒ Meya anaahidi kutoa mafuta ya mhubiri na sadaka kubwa kila mwezi.
⇒ Bili kusema angemweka mikononi mwa bwana hakuna ambalo lingemshinda.

Uongozi mbaya/utumizi mbaya wa mamlaka

⇒ Kutowashirikisha watu katika maamuzi-Siki
⇒ Meya na baraza lake wana uongozi mbaya.
⇒ Meya anatumia mali ya baraza vibaya.
⇒ Meya hajali hali ya wafanyakazi kwa kutoshughulikia madai yao.
⇒ Hajali elimu ya umma kwani anapeleka wanawe wakasomee nje.
⇒ Anapuuza ushauri wa Siki na diwani II na kuenzi ushauri mpotovu wa diwani I na II na Bili.
⇒ Meya anatumia vyombo vya usalama (polisi) kuendeleza uongozi wake mbaya.
⇒ Hafuati kanuni za baraza anapoongezea madiwani na askari mishahara na kandarasi kwa kutojali nakisi katika bajeti.
⇒ Madiwani I na II hawamshauri Meya vizuri bali wanamuunga mkono ili wanufaike.
⇒ Meya kutumia wahudumu wake (Gedi na Dida) kama watumwa.
⇒ Anatumia nguvu na mabavu kuzima migomo badala ya kushughulikia malalamiko ya wafanyakazi.

Ukombozi/uhuru/utetezi wa haki

⇒ Wafanyakazi wa mji wanagoma na kupigania haki zao.
⇒ Diwani III kupinga wazo la Meya kufuta kazi wafanyakazi waliogoma.
⇒ Siki na Diwani III wanaungana na wafanyakazi kupigania haki zao.

⇒ Wafanyakazi wa sehemu nyingine kama vile mhazili, wafanyakazi wa uwanja wa ndege na bohari wanaungana na wafanyakazi kupigania haki zao.
⇒ Askari wanachoshwa na uongozi wa Meya na Diwani I na II na kuwatia mbaroni wawapeleke makao makuu kuelezea hali ya mambo hivyo kuporomosha uongozi wa Meya.
⇒ Waridi kuacha kazi kwa kuzorota kwa mazingira ya kazi.
⇒ Wawakilishi wa wafanyakazi kupeleka malalamiko yao kwa Meya
⇒ Wanaomba wawe na washiriki katika baraza watetee maslahi yao wenyewe.
⇒ Wafanyakazi kugoma.
⇒ Kufanya maandamano.

Ufisadi

⇒ Kutibiwa mafua na kujifungulia ng’ambo kwa kutumia pesa za baraza.
⇒ Meya anatumia cheo kupata mashamba na kuwagawia marafiki pia.
⇒ Meya kumgawia Bili rafiki yake vipande vya ardhi.
⇒ Daktari katika zahanati ya mji wa Cheneo (Siki) ni binamu yake Meya Sosi.
⇒ Bili kupendekeza kesi ya mwanakandarasi iende dhidi ya baraza ili lilazimike kulipa fidia naye awatolee fungu.
⇒ Meya anakubali kushirikiana na mwanakandarasi ili apate gawio.
⇒ Kutumia gharama kubwa katika mapokezi ya MaMeya.
⇒ Wanakubaliana na Bili na Madiwani I na II kuiba fimbo ya Meya na kuiuza ng’ambo.
⇒ Kumlipa Bili kwa huduma za ushauri kinyume na taratibu.
⇒ Meya kumwajiri mhazili wake bila kuwa na sifa stahiki.

Umaskini

⇒ WanaCheneo hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi kama vile:

- Gharama za dawa
- Wagonjwa kukosa hela za kulipia huduma hata karatasi ya kunakilia.

- Nchi ni maskini ombaomba kama anavyosema Waridi.
- Gharama za elimu
- Kutomudu lishe bora kukosa chakula chakula hata wanakula chakula kidogo kilicholala makombo ya mbwa, mizizi na matunda ya mwitu.
- Kukosa kawi/moto kwa vile makaa na mafuta ya taa yamepanda bei tangu sheria ya misitu ishike kasi (utunzaji wa mazingira).
- Mama mfanyakazi wa baraza la Cheneo anashindwa kumudu kununua mafuta ya taa wala makaa.
- Mtoto ana kiriba kwa utapia mlo
- Wafanyakazi kuishi mabandani na kuenda kazini kwa miguu.

⇒ Baraza ni maskini.

- Linategemea misaada/mikopo kutoka ugenini kulipia mishahara ya wafanyakazi.
- Halina fedha za kuwalipa wafanyakazi.
- Wanashindwa kulipa wafanyakazi kwa wakati.
- Limeshindwa kuongeza wafanyakazi mishahara kwa vile bajeti ina nakisi.
- Huduma za elimu na matibabu zimezorota.

Utabaka

⇒ Tabaka la juu kama vile Meya na madiwani

⇒ Tabaka la kati kama vile wafanyakazi wanaolipwa mishahara duni na inayocheleweshwa.

⇒ Tabaka la chini kama akina Kerekecha.

⇒ Tabaka la juu wanatibiwa ng’ambo wakati wengine wanashindwa kumudu gharama za matibabu.

⇒ Wanapata elimu ng’ambo wakati wengine wanashindwa kumudu gharama ya elimu.

⇒ Wanakula chakula kizuri.

⇒ Wana nyumba zenye samani nyingi.

⇒ Wanatibiwa mafua na kujifungulia ng’ambo.

⇒ Wanapata fursa ya kuburudika k.v. kula katika mikahawa ya kifahari.

⇒ Diwani II anamshauri Meya kuendeleza utabaka kwa kusema wafanyakazi walifaa kusukumwa mpaka wajue kuna wenye nchi na wananchi.

Mapendeleo

⇒ Meya anaongeza mishahara ya madiwani na askari ilhali wafanyakazi wengine hawaongezewi.
⇒ Anamwajiri mhazili asiye na sifa za kazi hiyo ilhali wapo vijana wengi waliomaliza chuo kikuu wasio na kazi.
⇒ Kujiongezea mishahara minono.
⇒ Nyongeza kuja baada ya muda mfupi.
⇒ Kupata mshahara wote ilhali wa wafanyakazi unacheleweshwa.
⇒ Wana bima ya matibabu ilhali wafanyakazi hawana.

Uoga

⇒ Meya kuzirai na kuanguka kutoka kitini askari wanapoelekea kumtia pingu kwa kuogopa kwenda jela.
⇒ Diwani I na II wanababaika askari wanapokwenda kuwakamata baada ya mambo kuharibika.
⇒ DI na II kushikwa na butwaa askari wanapoenda kuwashika wachukuliwe wakaeleze hali ya mambo.
⇒ Anapata hofu anapoSikia Siki amemtembelea kwa kuhisi anampelekea habari mbaya.
⇒ Anashtushwa na sauti za wafanyakazi waliogoma.
⇒ Anaogopa kuongea na wanahabari.
⇒ Anawakwepa wafanyakazi, hataki kuongea nao.
⇒ Ana hofu watu wanataka cheo chake.
⇒ Diwani III anasema Meya ana uwezo mkubwa na kushidana aye ni kama kushindana na ndovu (ana uwezo mkubwa) na utapasuka-kupata madhara.
⇒ Meya kushtushwa na sauti za wafanyakazi.
⇒ Meya kunyong’onyea anapoSikia habari za mgomo.
⇒ Meya na mhubiri kuinua mikono juu na kushtuka askari wanapoingia wakiomba kwa kudhani ni watu wabaya wamemwingilia Meya.
⇒ Meya kushtuka na kushika tama tatu anaposema hawawezi kufuata sharti la kumaliza mgomo na kurejea kazini na wanapewa nguvu na uchafu/uvundo.
⇒ Meya anapoSikia wafanyakazi wa uwanja wa ndege wamegoma, ananyong’onyea.

Ujasiri/ukakamavu

⇒ Diwani III kumkaBili Meya na kutoa maoni kuhusu nyongeza ya mishahara ya madiwani ilhali wafanyakazi wamegoma.
⇒ Pia kuongoza wafanyakazi kupigania haki zao.
⇒ Siki kumkaBili Meya na kumkosoa bila hofu.
⇒ Hasiti kuendelea na harakati za mageuzi licha ya vitisho vya Meya, uwezo wake na kuitwa mchochezi.
⇒ Mama ni jasiri. kwa kumpeleka mwanawe hospitalini bila pesa. Anajitoma ndani kwa daktari wakati watu wengine wanamsubiri.
⇒ Siki kumkaBili Meya na kumwambia ukweli. Iwapo umefanya, yapo mendi hayakunyoka. Mnajifikiria tu. Si watu waliowachagua.
⇒ Tatu kumkaBili Meya na kumwambia hawawezi kufuata sharti la kurudi kazini ili malalamoko yao yashughulikiwe.s

Subira/kutokata tamaa

⇒ Siki haachi kazi japo mazingira ya kazi ni mabaya.
⇒ Aliendelea na kazi hata mishahara ilipokuwa midogo.
⇒ Alivumilia mishahara ilipochelewa.
⇒ Aliendelea na kazi hata wafanyakazi walipokuwa wanadharauliwa.
⇒ Anasema hali ikibadilika, mshahara nao utakuja…
⇒ Anashauri wafanyakazi kuvuta subira badala ya kutumia migomo.
⇒ Diwani III anaelewa ugumu wa kufanya mapinduzi lakini hakati tamaa.
⇒ Waridi anakata tamaa na kuamua kuacha kazi baada ya kuona mazingira ya kazi yakiwa mabaya na mtoto wao anapokufa kwa kukosa dawa.
⇒ Diwani III hajafa moyo kuendelea kushauri Meya.

Ushauri/mawaidha

Mzuri/wa busara

⇒ Siki kumshauri tatu kuwa mgomo si njia bora ya kutatua matatizo.
⇒ Kumshauri asikate tamaa kutafuta nafasi ya kumwona Meya kumweleza matatizo yao.

⇒ Siki kumshauri Waridi asiache kazi.
⇒ Siki kumshauri Meya kushughulikia matatizo ya ukosefu wa dawa, mishahara midogo, na kuongezeka kwa gharama ya maisha.
⇒ Alimshauri kutofuata maagizo ya nchi za nje kwani huo ni ukoloni mamboleo. Wazungu kuhimiza mfumo wa kugawana gharama, nchi ni changa. Kupunguza idadi ya wafanya kazi, kufyonza uchumi wa nchi kupitia mikopo.
⇒ Alimshauri asipumbaze watu kwa kutumia nyimbo za uzalendo.
⇒ Alimshauri kuwaSikiliza watu badala ya kuwakwepa.
⇒ Alimshauri asipime mafanikio ya mji kwa kujilinganisha na miji mingine ambayo ni duni kwao.
⇒ Diwani III kumshauri Meya kutoongeza mishahara ya madiwani pekee kwani ingeleta mivutano zaidi.
⇒ Madiwani walipe kodi ili nakisi ipungue.
⇒ Asitumie nguvu kuzima migomo bali aSikilize.
⇒ Kutafuta suluhisho la kudumu
⇒ Kuongeza mishahara kusitishwe mpaka uchumi utakapoimarika.
⇒ Meya alipuuza ushauri huu na kuwaona kama wachochezi wanaomtusi na kutaka kumpindua (usugu). Harekebishi makosa akisahihishwa.
⇒ Siki kumshauri tatu watumie kongamano la maMeya la kila mwaka, wamweleleze Meya shida na asiporidhia shughuli za usafi zizidi kususiwa.

Ushauri mbaya

⇒ Bili rafiki yake Meya na mfanyakazi wa jiji la Cheneo wanapanga na Meya kuiba fimbo.
⇒ Kumshauri Meya kupuuza madai ya wafanyakazi na kutumia nguvu.
⇒ Kushirikiana na mwanakandarasi kulifisidi baraza.
⇒ Kuuza fimbo ya Meya.
⇒ D I –Meya abuni kamati za kumuunga mkono-Meya kusema walipwe vizuri
⇒ Diwani II kumhimiza Meya kuendelea kumtenga diwani III.

⇒ Diwani I na II kumshauri Meya kutumia nguvu kuzima migomo.
⇒ Kuongeza mishahara ya madiwani na walinda usalama.
⇒ Atumie mashindano ya nyimbo za uzalendo kuwapumbaza vijana.
⇒ D I –wafanyikazi wafutwe na kuajiriwa wengine
⇒ D II –walinda usalama waongezewe mishahara na marupurupu kwa 20%
⇒ Wasitozwe kodi
⇒ Kutenga watetezi

Vikwazo vya uogozi/si lelemama/si rahisi

⇒ Wafanyakazi wanapigwa na kuvurumishwa na askari kwa vitoa machozi/mabavu
⇒ Waliogoma wanatishwa kufutwa kazi.
⇒ Gedi awaambie wafanyakazi watafutwa kazi na Meya.
⇒ Hongo.
⇒ Washauri wabaya na wenye tamaa.
⇒ Kamati za huduma za jamii.
⇒ Kutengwa/tenga utawale-Tunatengwa na maamuzi kufanywa-Diwani III
⇒ Sheria za kumlinda Meya
⇒ Kupumbaza watu-Vijana kushindania zawadi kwa kubuni, kutunga na kucheza nyimbo na kupewa zawadi ndogondogo na kuonyeshwa katika vyombo vya habari.
⇒ Kuogofwa-anawasomea *acts* barazani
⇒ Meya kupewa uwezo mkubwa/nguvu nyingi-katiba/Sheria zinazompa uwezo *Mayors act*-inayompa uwezo wa kuchukulia mtu hatua kali-Diwani III
⇒ *Riot act*-Anaweza kuitumia kukunja aliye chini yake kama ua wakati wa alasiri.
⇒ *Collective responsibility*-Kulazimisha kuwajibikia baraza badala ya wananchi
⇒ Diwani III anawaambia kujitolea kwa baraza kutetea demokrasia na hasa uhuru wa kujieleza.
⇒ Vitisho- Meya kusema atakayetaka kufanya kichwa basi na afanye.

Kiburi/majigambo/majivuno

⇒ Wewe tu ndiye hujui mimi ndiye Meya wa baraza la mji wa Cheneo?-Meya kwa Sosi
⇒ Lakini mimi Meya wako-kwa Sosi
⇒ Ni baraza gani lenye udhabiti kama letu ambalo linaongozwa na mstahiki Meya Sosi? Lipi katika ujirani wetu?
⇒ Meya Sosi kujigamba ana pesa nyingi sana na anaweza kuchaguliwa hata mara sita.
⇒ Bili kujigamba kwa starehe anazopata.
⇒ Diwani II kujigamba kuwa ana uwezo wa kutumikia kamati ya Meya.
⇒ Hata mkitaka nne, tano na sita bado watanipa-Meya akijigamba anaweza kuchaguliwa na watu mara zaidi.
⇒ Akili hii walisema ni mali-majivuno ya Meya.
⇒ Udhibiti na ushawishi wa mambo ninao-Meya.
⇒ Diwani II kusema mzee alifahamu kuwa sisi ndio wenye uwezo na unamfaa
⇒ Nisipokuwa nazo, nani atakuwa nazo?-Meya

Dharau/Ujeuri

⇒ Meya kufahamisha wawakilishi wa wafanyakazi hana muda wa kupoteza kwa vile baraza lilikuwa latarajia wageni siku iliyofuata.
⇒ Dida anatufahamisha kuwa wanatusiwa na kudhalilishwa na Meya.
⇒ Meya kutomSikiliza Siki
⇒ Meya kudharau elimu katika shule za umma-elimu ya kawaida isiyomvaa mzazi anayeona mbali.
⇒ Bili-ya kina yakhe-elimu ya maSikini
⇒ Bili-hakuna wakunga wazuri Cheneo
⇒ Madaktari wa kubabaisha

Hasira

⇒ Za watu dhidi ya viongozi
⇒ Meya ana hasira nyingi
⇒ Hasira-Unaona sasa? Mlinidanganya.-Meya anapoarifiwa vijana hawawezi kukubali kuchukua nafasi za wafanyakazi wanaogoma kwani wameshapata picha mbaya ya baraza.
⇒ Anawajibisha wafanyakazi kwa hasira

⇒ Anamkemea Gedi.
⇒ Dida anamtumikia kwa kutetemeka.
⇒ Anapoudhiwa na Siki midomo inamcheza kwa hasira na kuita Gedi amwondoe.
⇒ Waridi anawakemea wagonjwa-mama Dadavuo Kaole.
⇒ Hivi uzionavyo-Meya anapoulizwa na Siki habari za leo ndugu Sosi

Anasa

Bili anajiandaa kisha amwombe Meya aende na mkewe na watoto wakajinafasi.

Haki

⇒ Siki ni mtetezi wa haki.
⇒ Anahimiza watu watibiwe hata kama hawana fedha.
⇒ Diwani III pia.
⇒ Haki za wanaCheneo zimekiukwa
⇒ Haki ya elimu
⇒ Haki ya kuishi-mtoto kufa kwa kukosa dawa
⇒ Haki ya kupata chakula
⇒ Haki ya kuishi katika mazingira safi
⇒ Haki ya usemi
⇒ Haki ya mishahara mizuri
⇒ Haki ya utulivu-wafanyakazi kuvurumishwa na askari
⇒ Haki ya huduma za matibabu

Uchochezi

⇒ Siki anachochea wafanyakazi kudai haki yao.
⇒ Siki amewahi kuchochea mgomo na Meya anataka kujua kama amechochea mwingine.
⇒ Anamchochea diwani III kuendelea kumshawishi Meya.
⇒ Ukosefu wa huduma za kijamii kuchochea wafanyakazi kugoma.
⇒ Siki kuchochea madiwani kuungana kuendelea kumpinga Meya.
⇒ Diwani II kumchochea Meya kuchukua hatua kali dhidi ya wachochezi.
⇒ Wananchi wengine kama vile Siki na viongozi wa wafanyakazi kuchochea kuleta mapinduzi.

Tamaa/uroho/kiu/kutotosheka

⇒ Bili kujifanya mshauri ili afaidike.

⇒ Meya anakula vyakula vingi vilivyoandikwa mezani.
⇒ Kutamani mkewe akajifungue ng’ambo.
⇒ Kutamani watoto wakasomee nje.
⇒ Kutamani kuvinjari au kujiburudisha katika mahoteli ya kifahari. Anamwambia Meya ampeleke akastarehe.
⇒ Diwani I na II wanaomba posho wakati wafanyakazi hawajalipwa mishahara yao midogo.
⇒ Meya ananyakua vipande vinane vya ardhi na kuuza vitatu na kubakiwa na vitano.
⇒ Diwani 1-nguo nzuri
⇒ Diwani 1 kudai marupurupu-overtime

Ubinafsi

⇒ Meya kuagiza chupa moja ya maji ilhali wenzake hawaagizii.
⇒ Meya kujilimbikia mali ilhali wanaCheneo wengi ni maskini.
⇒ Madiwani kutotozwa kodi wakati mama muuza ndizi analipa kodi.
⇒ Meya, Diwani I na II na Bili wanakubaliana kuuza fimbo ya Meya ili kujinufaisha.
⇒ Waridi anajali maslahi yake zaidi-kuuliza Siki kazi hii ina faida gani kwangu?-anapotaka kuacha kazi.
⇒ Maji safi yanapatikana nyumbani kwa Meya tu.
⇒ Meya kuagiza yeye pekee mishahara ya madiwani iongezewe bila kushauriana na mtu.
⇒ Kubinafsisha hazina ya baraza ili kuimarisha umashuhuri wake.
⇒ Madiwani wana bima ya hospitali wakati watu wengine hawana.
⇒ Watoto wa Meya wanapata elimu bora ng’ambo wakati watu wengine wanapata elimu duni.
⇒ Meya anakula vizuri ilhali wafanyakazi wake wanakula makombo na viporo k.v. mamake Dadavuo Kaole.
⇒ Diwani I anaamini jambo lililo muhimu ni yeye kushiba.
⇒ Anapendekeza waongezewe posho licha ya bajeti ya baraza kuwa na nakisi ya 120,000,000.
⇒ Diwani I anataka wanunuliwe suti nzuri sawa na madiwani wa nje.

Dhiki/shida/malalamiko

⇒ Za watu wa Cheneo
⇒ Kushindwa kumudu gharama za matibabu
⇒ Kukosekana kwa dawa-ahadi nyingi dawa zingeletwa
⇒ Gharama za maisha kuzidi kupanda
⇒ Mahitaji yao kuzidi kuongezeka
⇒ Kutopata kwa mishahara/duni
⇒ Kufa kwa njaa
⇒ Watu kufa kwa sababu ya kukosa dawa
⇒ Kutakiwa walipie dawa ilhali hata chakula walacho ni cha kuokota
⇒ Diwani III-watu wengi hawana ajira
⇒ Walio na ajira mishahara yao haitoshi/duni
⇒ Mishahara kucheleweshwa-hata kwa miezi mitatu hailipwi kwa wakati na hulipwa -nusu
⇒ Ukosefu wa ajira-vijana wbgi waliohitimu kutoka chuo kikuu hawana ajira-Meya.
⇒ Wafanyakazi wa baraza kutolipwa kwa wakati-Diwani 111
⇒ Hakuna maji ya kutosha hospitalini-Siki
⇒ Wafanyakazi kuosha vyoo bila glavu-Medi
⇒ Ahadi za uwongo
⇒ Ukosefu wa maji hata hospitalini
⇒ Uchafu hospitalini
⇒ Kukosekana kwa dawa
⇒ Kutakiwa kulipia matibabu/dawa ilhali madiwani wana bima
⇒ Tatizo la usafiri hadi kazini-kwa miguu kutoka mabandani mpaka viatu kuliwa na lami
⇒ Kuosha vyoo bila glavu
⇒ Kutoongezewa mishahara baraza likidai hakuna pesa ilhali lawaongezea madiwani.
⇒ Kukosa watetezi katika vikao vya maamuzi.

Ujinga

⇒ Diwani I haelewi kazi ya wafanyakazi kwa kufikiri ndege zinaweza kutua bila waelekezi.
⇒ Dida haoni haja ya kufanya mageuzi japo hali ni mbaya.
⇒ Anaomba msamaha hata kwa makosa ambayo hajafanya.

⇒ Meya haoni mbali. Hajui kuongezeka kwa shida za watu kuna kiwango kinachoweza kustahimiliwa.
⇒ Anatumia mali ya baraza la Cheneo kwa njia za kijinga ambazo hazileti faida.
⇒ Hajui mambo ananavyokwenda Cheneo. Anakuja kujua hatimaye kwamba maji yanachukuliwa mtoni kwa punda.
⇒ Anadanganywa kwa urahisi na madiwani na rafiki yake Bili.
⇒ Wanamsukuma kwa njaa na tamaa yao lakini hatambui.
⇒ Waridi anaamini haraka anayoambiwa kama vile ahadi za Meya kuhusu dawa.
⇒ Mama haelewi umuhimu wa lishe bora
⇒ Mama kutofahamu usafi-kutotokosa chakula kabla ya kumpa mwanawe (Dadavuo Kaole) kunakosababisha augue
⇒ Ujinga wa watu ndio chanzo cha uongozi mbaya.
⇒ Meya kutegemea mikopo kulipia mishahara-kuachia wajukuu ambao hawakufaidika na mkopo mzigo
⇒ Kuendesha baraza kwa mikopo na wageni wanaowapa mikopo ni washirika katika maendeleo-riba ni mzigo kwa kizazi kijacho-si uzalendo.

Busara

⇒ Diwani III anatambua sheria zinazomlinda Meya na madhara ya kushindana naye.
⇒ Anatambua kuwa watu wameamka na hawadanganyiki.
⇒ Siki anatumia busara kuwapa wagonjwa matumaini ya kuendekea kuishi.
⇒ Anaonelea wafanyakazi wasigome ili kuzuia kuteseka zaidi-mgomo una
⇒ madhara yake ni kufutwa -Siki kwa Tatu
⇒ Anaelewa kuwa watu wenyewe ndio huchangia uongozi mbaya.
⇒ Diwani II anatambua kwa wepesi hali inapoharibika.
⇒ Anaelewa mfuata nyuki hula asali kwa kukubali kila wazo linalotolewa na Meya.

Ubarakala

⇒ Diwani I ni mfuasi kipofu kwa kudharau na kukweza wale Meya anaowakweza.

⇒ Diwani I na II wanatenda mambo kumfurahisha Meya ili wafaidike kutoka kwake.
⇒ Kufurahisha Meya kwa kupiga vita waliotuchagua-Diwani 111.
⇒ Kufaa na kujifaa-wapaswa kujifaa kwa kufaa watu wao-Diwani III
⇒ Kuunga mkono hata yasiyofaa-Diwani 111

Huduma duni za jamii na athari zake

⇒ Afya-vifo vya wagonjwa
⇒ Afya-kukimbilia kutibiwa ng’ambo.
⇒ Elimu-kukimbilia shule na vyuo vya ngambo
⇒ Uchafu-magonjwa
⇒ Migomo
⇒ Wafanyakazi kuuawa
⇒ Viongozi kupoteza madaraka
⇒ Baraza kukosa wafadhili

Mapuuza

⇒ Hali ya kutojali
⇒ Meya anapuuza wafanyakazi na madai yao.
⇒ Meya hajali wagonjwa wanakufa.
⇒ AnapoSikia mtoto alikufa anauliza huyo mmoja tu. Unadhani wangapi wananiunga mkono?
⇒ Hajali baraza lina nakisi ya bajeti bali anaendelea kupanga matumizi zaidi.
⇒ Hajali wafanyikazi wake.
⇒ Hajali ushauri wa Siki na diwani III.
⇒ Meya hajali wafanyakazi wanapogoma-Wenye kugoma acha wagome. Vijana ambao wangeajiriwa kwa mshahara wa chini.
⇒ Kupuuza Siki na wawakilishi wa wafanyakazi.
⇒ Kupuuza ushauri wa diiiiwani 111.

Uwajibikaji

⇒ Diwani III anaungana na kufanya kazi na Meya na madiwani japo wamemtenga.
⇒ Anafanya kazi yake kwa mujibu wa kanuni na taratibu za baraza.

⇒ Gedi anamjulisha Meya wageni wajapo, kupeleka maagizo kwa wengine na kumfahamisha Meya yanayotokea.
⇒ Dida anamhudumia Meya barabara.
⇒ Waridi anatekeleza majukumu yake ya kutibu watu.
⇒ Siki anapatikana kazini mara nyingi.
⇒ Anaulizia hali ya wagonjwa kila wakati.
⇒ Anawatibu na kuwapa wagonjwa matumaini japo hakuna dawa.
⇒ Anafanya jitihada ya kukutana na Meya kujua kuhusu kukosekana kwa dawa.

Utiifu
⇒ Waridi kufuata maagizo ya baraza kutotibu watu wasio na pesa.
⇒ Gedi anatekeleza maagizo yote ya Meya.
⇒ Askari wanatii maagizo ya Meya ya kutumia nguvu kuzima migomo.

Ubadhirifu
⇒ Utumiaji mbaya wa pesa au mali.
⇒ Meya anatumia vibaya pesa za baraza la Cheneo.
⇒ Kusomeshea watoto wake ng’ambo.
⇒ Kumpeleka mke wake kujifungulia ng’ambo.
⇒ Kumpeleka mke wake kutibiwa mafua ng’ambo.
⇒ Kutumia pesa nyingi kuwakaribisha maeya wageni katika mahoteli ya kifahari na vyakula kutoka kila utamaduni duniani na mvinyo ulioagizwa kutoka urusi na divai kutoka ufaransa.
⇒ Kupanga kutumia pesa za baraza kumfurahisha na kumvutia mhubiri.
⇒ Kunyakua viwanja vya baraza pamoja na wandani wake na kuuza ili apate pesa.
⇒ Kumpeleka Bili katika hoteli za kifahari.
⇒ Kumpa Bili marupurupu japo si mfanyakazi wa baraza.
⇒ Kuongezea madiwani mshahara kiholela ili apate umashuhuri.
⇒ Watoto wa madiwani kusafirishwa kwa magari ya baraza hadi shuleni.

Udikteta

⇒ Meya anatumia mabavu kutawala.
⇒ Hatoi nafasi kwa wananchi kutoa maoni yao.
⇒ Anatoa maamuzi kinyume na kanuni za baraza k.v. amri ya nyongeza ya mishahara kwa madiwani, sadaka kwa mhubiri, kumlipa Bili na si diwani.
⇒ Ni mkali kwa wafanyakazi wake na wanamwogopa.
⇒ Kutumia nguvu kuzima mgomo wa wafanyakazi.

Vitisho

⇒ Meya kutishia kuwafuta wafanyakazi wakiendelea na mgomo.
⇒ Anamtisha Siki akirudi kwake atamwadhibu.
⇒ Anamtisha Siki asimchezee hata kama ni binamu yake.
⇒ Anamtisha Siki asipinge mipango ya milenia.

Ulaghai/ujanja

⇒ Meya kushawishi wafanyikazi warudi kazini ndipo madai yao yashughulikiwe.
⇒ Meya, madiwani na Bili kupanga kuiba fimbo ya Meya waiuze ng’ambo-Diwani 1 atoke nayo na kudanganya iliibwa wakati wa rabsha.
⇒ Kudanganya umma kwamba anaujali.
⇒ Kudanganya dawa ziko njiani.
⇒ Kupora vipande vya ardhi vya Cheneo.
⇒ Bili kumpa Meya mbinu ya kuibia pesa kwa kushirikiana na mwanakandarasi kuvunja mkataba, ashtaki, atake alipwe fidia, wagawane, wakubaliane ampe fungu lake baada ya kulipwa.
⇒ Bili ni mjanja au kitatange kwa vile anawaingiza watu katika shida na kutoweka.

Udhabiti wa msimamo

⇒ Madiwani I na II hawana misimamo dhabiti kwani wanaunga lolote mkono lisemwalo na Meya hata kama ni potovu.
⇒ Siki hayuko tayari kuacha kazi hata kama mazingira ya kazi ni mabaya na mishahara inachelewa.
⇒ Hakuyumbishwa na ushawishi wa Meya
⇒ Hakushawishika na diwani III na Tatu kumwona Meya kwa kuwa ni binamu yake.

⇒ Wawakilishi wa wafanyakazi Tatu, Medi na Beka wana msimamo imara.
⇒ Diwani II mwanzoni anamuunga mkono Meya kuwasukuma wafanyakazi lakini hatimaye anaona mbinu hiyo haifai.
⇒ Mwanzoni aliunga mkono kuwafuta kazi wafanyakazi waliogoma lakini mambo yalipobadilika anapinga hatua hiyo.

Uzalendo

⇒ Siki hakubaliani na kuiga mambo yanayoamuliwa na nchi nyingine.
⇒ Anataka uongozi kuendeleza Cheneo badala ya kujiendeleza wenyewe.
⇒ Hakujali mahusiano ya kidugu na Meya bali maslahi ya Cheneo nzima.
⇒ Hafurahi kuliona jiji la Cheneo likiwa chafu.
⇒ Meya si mzalendo kwa kufuja pesa za baraza la Cheneo na kuiba fimbo.
⇒ Tatu, Medi na beak ni wazalendo.
⇒ Diwani III kupinga mipango ya kufuja mali ya umma.
⇒ Siki kutoacha kazi ili awasaidie wagonjwa-Afadhali kuteseka na hawa wagonjwa-kujali maslahi ya wengine-si mbinafsi

Heshima

⇒ Mama kumwambia Waridi tafadhali mwanangu nihurumie
⇒ Siki ana heshima kwa Waridi
⇒ Madiwani kumsimamia Meya
⇒ Diwani 111 anamheshimu Meya

Walio waaminifu na wasio waaminifu

⇒ Diwani III kupinga mipango mipotovu na kutengwa.
⇒ Hana tamaa
⇒ Ni mkweli
⇒ Hana ubinafsi

Maudhui mengine

i) uozo/ukosefu wa maadili/mkengeuko/utovu wa maadili
ii) wizi
iii) mauaji

iv) Uadilifu
v) Uaminifu
vi) Majuto- Meya anajuta akisema heri angemSikiliza Bwana uchumi na kazi mambo yanapoharibika

Sifa/Hulka za wahusika

Kunao:

Waadilifu na wasiowaadilifu
Bidii
Wanaowajibika na wasiowajibika.
Wenye utu na wasionao
Walio na uzalendo na wasionao
Wenye tamaa na wasio nayo.
Wanaokata tamaa na wasiokata tamaa
Wavumilivu na wasio wavumilivu
Wenye msimamo na wasio nao
Wajasiri na waoga
Wenye mapuuza
Wafisadi
Watetezi wa haki/wakombozi
Wadanganyifu
Wanafiki
Wasaliti
Walaghai/wajanja
Wapenda anasa
Wabunifu
Washauri mbaya/mpotoshaji na washauri wema
Maskini
Wapole/Wanyenyekevu

Umuhimu wa Wahusika

⇒ Bili ni kielelezo cha marafiki wanaoweza kupotosha viongozi.
⇒ Mfano wa watu wenye tamaa iliyokithiri.
⇒ Bili, D1 na D11 ni vielelezo vya washauri wanaopotosha viongozi.
⇒ Vielelezo vya viongozi wasiowajibika.
⇒ Vielelezo vya viongozi wanaohujumu uchumi wananchi.
⇒ Vielelezo vya watu walio imara kuleta mageuzi.

⇒ Dida ni kielelezo cha wafanyakazi wanaohatarisha juhudi za ukombozi.
⇒ Askari ni vielelezo vya jinsi vyombo vya dola hutumiwa kuendeleza uongozi dhalimu-askari kulinda baraza.
⇒ Mhubiri ni kielelezo cha jinsi dini inavyoweza kutumiwa kuendeleza uongozi dhalimu.
⇒ Mhubiri ni kielelezo cha viongozi wa dini wanafiki na wanaotumia dini kwa manufaa yao wenyewe.
⇒ Mama ni kielelezo cha wananchi wanaoathirika na uongozi mbaya.
⇒ Diwani III ni kielelezo cha uadilifu katika mazingira ya waliopotoka.
⇒ Madiwani I na II ni vielelezo vya ubarakala.
⇒ Wanatudhihirishia maudhui gani?
⇒ Wanatusaidia kutambua sifa za wengine vipi?

MATUMIZI YA LUGHA

Tashbihi

⇒ Kupinga haya ni sawa na kumkama simba mwenye watoto-Meya akimwonya Siki asithubutu kupinga hoja zake.
⇒ Watu kujifia kama nzi.-tatu kwa Siki-kutokana na magonjwa kwa kukosa dawa
⇒ Juzi mtoto wa kerekecha amekufa kama nzi.
⇒ Inasimama (bahati) kama mtende-Siki anapompata D111 kwake.
⇒ Kushindana na Meya ni kama kushindana na ndovu-Diii-kuonyesha uwezo mkubwa alio nao Meya.
⇒ Inasimama kama ya mtende-Siki kwa D111-kufanikiwa kumpata kwake
⇒ Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji-Siki na Meya hawapatati-mahasimu.
⇒ Kukunja walio chini yake kama ua wakati wa alasiri-riot act

Sitiari

⇒ Kueleza sifa za kitu kwa kusema ni kingine.
⇒ Himizeni hiyo miamba kuangalia maslahi ya watu-Siki akimwambia kheri.

⇒ Vitu hivi viwili (njaa na tamaa) kwa pamoja ni ugonjwa mbaya kuliko tauni.-D111-chanzo cha ushauri mpotovu unaoharibu mji
⇒ Unakanyaga nyoka mkia.
⇒ Siku zote tumeshuhudia wasiotosheka wakipuliza tarumbeta zao za uzushi na sisi tukazizima kwa kukohoa
⇒ Ndiyo huko kuwaua ndege watatu kwa jiwe moja.
⇒ Lazima kwanza mhakikishe kuwa huyo sumu hapati hata fununu ya jambo hili-Meya kurejelea D111
⇒ Hii ni bomu inayoweza kutulipukia usoni-Meya-mpango wa wizi wa fimbo kuweza kuwatia matatani ukijulikana.
⇒ Duniani kuna watu na viatu, paka na panya-Dida
⇒ Bunduki inayotema risasi tatu tatu.
⇒ Magari yanayotapika maji.
⇒ Mshumaa kuwaka-kuendelea kuishi, kuwatia matumaini hadi dawa ziwasili.
⇒ Wana njaa na kiu ambayo haikuzimwa-Siki kwa Meya-malalamiko ambayo hayakushughulikiwa.
⇒ Kumtetea macho, maSikio na sauti Dwani I-ubarakala
⇒ Matunda ya jasho letu-Meya
⇒ Ni kawaida ya debe tupu kupiga kelele-Bili udharau wafanyakazi-wajinga.
⇒ Nina hakika sasa yuko kanisani mwake akiwahudumia kondoo wake-waumini
⇒ Njaa ina nguvu, imeangusha miamba-malalamiko ambayo hayakushughulikiwa huangusha viongozi.
⇒ Siasa ni mchezo mchafu-D111
⇒ Siasa bwana ina vituko vyake. Utapakwa tope si haba.
⇒ Umya hauna pato kubwa. Ofisi ndiyo ina mianya mingi ya kujipatia utajiri-kupewa majukumu ya kuamua na hivyo kutumia fursa kujinufaisha na wenzake.
⇒ Viongozi ni picha ya umma uliowachagua.-D111
⇒ Bili kumuuliza Meya kama mkewe alishapata mgeni-mtoto
⇒ Tumekuwa watumwa siku nyingi-Medi.

Jazanda

⇒ Uozo wa mji unamaanisha uozo wa uongozi wa Cheneo
⇒ Sumu inatumika kumrejelea Siki

⇒ Bomu kumrejelea Siki
⇒ Harufu mbaya-kiwakilishi cha uozo ulio ndani.
⇒ Punda kumaanisha wafanyakazi
⇒ Ndovu kurejelea uwezo wa Meya
⇒ Ndege watatu kumaanisha mambo watatu
⇒ Vyakula vya aina mbalimbali mezani-ulafi
⇒ Watu wenye matumbo yasoyotulia huwa akili zao nazo hazitulii.-watu wenye shida ambazo hazijashughulikiwa hupigana hadi malalamiko yao yashughulikiwe.
⇒ Kukuna matumbo baada ya muda huanza kukuna vichwa
⇒ Kutembea nyuma ya punda aliyeudhika
⇒ Cheo kumlevya mtu kama mtoto na chakula. Atakienzi akiwa na njaa, Akishiba atakipiga teke, hana habari wapo wenzake wanakihitaji wala muda ukipita atakihitaji.
⇒ Beka -ni mgao wa wakubwa kula kwanza na sisi wengine kupigania makombo yanayoanguka chini

Tashhisi

⇒ Kiriba chaongoza
⇒ Kauli zinazoanguliwa katika matamshi hazitekelezwi
⇒ Wakisubiri ugonjwa nao utasubiri ?-Siki
⇒ Sembe na sukumawiki vinawatoa jasho kuvitia mezani-kushindwa kugharamia-Sosi kwa Meya.
⇒ Unadhani nyimbo zinawashibisha na kukata kiu ya uhitaji wao?-kushughulikia matakwa yao.
⇒ Bahati haifungui milango yake zaidi ya mara moja-Bili kwa Meya
⇒ Usafi umetwaliwa na nzi-Waridi kwa hospitali kukosa maji.
⇒ Mlango hatimaye huenda ukasalimu amri-Siki akimhimiza Tatu waendelee kushinikiza kumwona Meya huenda wakafaulu.
⇒ Cheo kinaweza kumlevya mtu asahau alipokuwa jana-D111
⇒ Viatu kuliwa na lami-Tatu kueleza jinsi wafanyakazi wanavyosafiri kwa miguu hadi kazini mpaka viatu vinachakaa chini kwa kukwaruzwa na lami.

Mdokezo

⇒ Kukatiza usemi

⇒ Tatizo … utapia mlo lipo – Siki
⇒ Huenda itasaidia kidogo… mtoto aandaliwe mchanganyiko wa sukari na chumvi. (tashtiti)-si matibabu.
⇒ Meli kupambana na mawimbi-kuwasili
⇒ Lakini daktari ha…-Waridi kwa Siki-mama hajalipa/hana hela
⇒ Ni kama… talk of the devil-Bili
⇒ Lililoandikwa…-D III majaaliwa kukutana kwa D111 na Siki.
⇒ Nashangaa hiki chaleta taabu…
⇒ Nimefika kukuona kama ndugu…-Sosi kwa Meya
⇒ Huenda isichukue muda mrefu… (utabiri wa Sosi unaomtia Meya woga.)
⇒ Hali ikibadilika, mshahara nao utakuja…
⇒ Ni…ni…ni…-Gedi akisita wakati anataka kumfahamisha Meya wafanyakazi wa uwanja wa ndege wamegoma kuwaunga mkono wenzao waliogoma.

Balagha

⇒ Hilo pia wanatuletea sisi hapa?-Waridi
⇒ Dawa gani?-Waridi anapoulizwa na Siki kama dawa zimeigia.
⇒ Lakini si sasa waona matokeo yake-Waridi kwa mama-matokeo ya kumpa mtoto chakula ambacho hakikutokoswa.
⇒ Mpaka sasa wapo watu wasioelewa umuhimu wa lishe bora?-Waridi
⇒ Walipie kitanda kisicho dawa?-Siki
⇒ Tutafanya lipi jingine bora kuliko hili?
⇒ Kasi yote ya nini Waridi? Au dawa zimeingia?
⇒ Kweli kilio chetu kiliSikika pale pale. Nani atakuelezea?
⇒ Siasa gani hiyo?
⇒ Hilo tumefanya lakini wapi?
⇒ Chaguo la wananchi kwa nini basi kulalamika?
⇒ Au unafikiri pakawa na fursa nyingine hii leo ya kuchagua viongozi matokeo yatakuwa tofauti sana?
⇒ Kama wakubwa wenyewe wameisha sema sisi tutafanya nini?-kugawana gharama

⇒ Huoni mstari ulivyo mrefu hapo nje?-Waridi kwa mama.
⇒ Au unadhani hao wengine hawajakuja kutibiwa?-Waridi kwa mama.
⇒ Wewe tu ndiye hujui mimi ndiye Meya wa baraza la mji wa Cheneo?-Meya kwa Sosi-kuonyesha kiburi.
⇒ Ni baraza gani lenye udhabiti kama letu ambalo linaongozwa na mstahiki Meya Sosi? Lipi katika ujirani wetu?-Meya-kuonyesha kiburi
⇒ Utatosheka lini wewe-Meya kwa Sosi
⇒ Huoni Cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano?
⇒ Iwapo mama muuza ndizi analipa kodi ili kulijenga taifa, iweje kwamba madiwani wasilipe kodi?

Tabaini

⇒ Si vyombo vya habari, si wanasiasa, si wasomi-Waridi anapoulizwa na Siki nani alisema nchi ni maskini.

Kinaya

⇒ Meya kuwa na wokovu ilhali anatenda matendo yasiyofaa.
⇒ D1-kuitwa Bwana usalama ilhali anahatarisha usalama wa wafanyakazi kwa kuagiza askaris wawashambulie.
⇒ D11-Bwana uhusiano mwema
⇒ Ulimwenggu wataka watu kama wewe-Meya kwa Bili kwa wazo la mwanakandarasi
⇒ Anwani na jina mstahiki Meya-hastahili kuwa kiongozi
⇒ Bili, mshauri mkuu wa Meya kutopatikana mambo yanapochacha
⇒ Meya kumpa mhubiri sadaka ya laki moja kila mwezi ilhali amekosa kuwapa wafanyakazi wa baraza mshahara na mji unakuwa mchafu mpaka unaanza kuvunda.
⇒ Ndugu Sosi-Siki
⇒ Sasa naona mnautusi ukarimu wetu-Meya kwa wawakilishi
⇒ Meya kuwaambia wawakilishi wa wafanyakazi kuwa baraza lina kanuni zake ambazo lazima ziheshimiwe ilhali haziheshimu.
⇒ Kama hawataki kuonyesha shukrani kwa wanayofanyiwa na baraza letu tukufu, nitawafuta kazi

⇒ Meya kusema anapenda urasimu ilhali anaidhinisha mambo kama vile nyongeza kinyume na kanuni za baraza.
⇒ Nzuri tatu-tatu anapomuuliza daktari habari za siku nyingi.
⇒ Meya kushukuru madiwani kwa kufika kuhudumia baraza lao.
⇒ Ni baraza gani lenye udhabiti kama letu ambalo linaongozwa na mstahiki Meya Sosi? Lipi katika ujirani wetu?-Meyakuonyesha kiburi
⇒ Meya kulinganisha baraza la Cheneo na majirani dhaifu ilhali wanaweza kufanya vyema
⇒ Huoni Cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano?-Meya kwa Sosi-wakati kuna shida nyingi.
⇒ Miaka hamsini baada ya uhuru-miaka mingi kupita na watu wana umaskini-uhuru bandia
⇒ Mstahiki Meya-hastahiki/hastahili kuwa Meya
⇒ Akili hii walisema ni mali-Meya-hana akili
⇒ Kutaka idhaa za baraza zicheze nyimbo za uzalendo kabla na baada ya vipindi maarufu.-Meya si mzalendo. Njia za kupumbaza watu.
⇒ Meya kusema Gedi ni miongoni mwa watu wenye uelewa.
⇒ Mji una amani na utulivu-Meya kwa Gedi
⇒ Lengo la mji ni afya bora na ya bure ilhali watakiwa kulipia matibabu
⇒ Mpango wa maendeleo wa miaka kumi. Meya ana malengo ya kimaendeleo ya milenia.
⇒ Tumeshaingia katika kiwango cha kimataifa.
⇒ Utetezi kuitwa uchochezi-Siki
⇒ Ndugu Meya-mhubiri kwa Meya
⇒ Wageni wanaokuja ni washirika wetu wa kimaendeleo-Meya kwa D111
⇒ Di kuwaita wafanyakazi wajinga-mtu mjinga hahitaji kubembelezwa ilhali ndio wajinga wa…
⇒ Sisi na yeye, nani ana akili zaidi-Bili akirejelea D111
⇒ Meya kusema wafanyakazi hawawezi kuwakilishwa katika baraza kwani lina kanuni zake ambazo mpaka zifanyiwe mabadiliko ilhali hazifuati.

Kuchanganya ndimi

⇒ What do you think this is? Food poisoning?-Siki
⇒ Oh, yes
⇒ I understand
⇒ Dawa ni painkillers tu
⇒ Meya kuitisha glasi ya kunywea maji.
⇒ Yes sir-Gedi kwa Meya
⇒ Nina entertainment vote ya Meya yangoja ualishi tu.
⇒ Kuna mayers act, riot act
⇒ Kile kinachoitwa collective responsiBility
⇒ Hii ni grand idea-wazo la kusitiri wizi/kuzuia watu kuwashuku
⇒ Bloody hens-kudharau kuku waliotaga mayai
⇒ Nonsense-Meya anapokabwa na yai kwa kulibwakia
⇒ Fridge-jokofu/friji anakotumwa Gedi amtolee Meya chupa moja ya maji.
⇒ Faili-file
⇒ Kula sukumawiki na dona (doughnut)
⇒ Entertainment vote ya Meya ambayo yangoja ualishi-idhini ya pesa za burudani za Meya-ubadhirifu
⇒ Wawakilishi wa wafanyakazi wanapotaka kumwona Meya, wanaambiwa diary (shajara) yake imejaa-mapuuza.
⇒ Collective responsiBility-kunyima uhuru wa kwenda kinyume na jambo linaloungwa mkono na wengi.
⇒ Ikiwa hii si insubordination ni nini?-Meya kwa diwani III-kukosa utiifu
⇒ Full- proof-dii baada ya mipango ya kuiba fimbo kumaanisha haiwezi kugundulika.

Utohozi/uswahilishaji

⇒ Daktari
⇒ Nesi
⇒ Meya
⇒ Hospitali
⇒ Sista-mtawa wa kikatoliki
⇒ Wadi ya watoto
⇒ Ofisini-office

Takriri

⇒ Wafanya kazi wa jiji jinsi hospitali yenyewe ilivyo ya jiji.
⇒ Njiani ni njiani na hospitalini ni hospitalini.
⇒ Huna habari kuwa walinichagua hao hao watu-ujinga wa watu ndio chanzo cha uongozi mbaya.
⇒ Safi. Safi kabisa-Meya kuonyeshwa kuridhishwa na heshima za Gedi.
⇒ Sauti ni sauti tu!-Bili-kumhimiza Meya apuuze sauti za wafanyakazi.
⇒ Udumu milele na milele-mhubiri akiombea uongozi wa Meya.
⇒ hujui ngoja ngoja huumiza matumbo/Ngoja ngoja hii haisaidii matumbo-Siki kuhusu dawa
⇒ Mkumbushe tena na tena mpaka apate mwanga wa kile unachokisema-Siki kwa D111
⇒ Endelea, endelea Tatu-Medi akimhimiza aendelee kusema malamiko yao kwa Meya.

Misemo

⇒ Akili hii walisema ni mali-Meya-majivuno
⇒ Fununu sio mbali na ukweli-Meya-kuna wachochezi katika baraza-D111 kuuliza Meya kama ana hakika na anayosema.
⇒ Na kumbuka mtumwa hauawi-Bili kwa Meya hawezi kufungwa kwa sababu alichukua hatua kwa niaba ya baraza.
⇒ Bahati haifungui milango yake zaidi ya mara moja-Bili-kuhimiza asipoteze fursa ya kujipatia pesa kupitia mwanakandarasi.
⇒ Mtu haukati mkono unaomlisha-Meya-hakikisho hawezi kumsahau Bili akipewa pesa na mwanakandarasi.
⇒ Wasemao mchana usiku watalala-Bili
⇒ Kelele za chura hazimzuii ng’ombe kunywa maji-Bili-sauti za wafanyakazi
⇒ Kubahatisha ndiko kupata-Siki anapompata D111 nyumbani kwake.
⇒ Lililoandikwa halifutiki kwa kweli
⇒ Eti siasa ni mchezo mchafu
⇒ Watu hujifunza kutokana na makosa yao
⇒ Mambo haya tunayafahamu tangu utandu hadi ukoko

⇒ Mambo yalikuwa yametiwa chumvi
⇒ Dawa ya adui ni kummegea unachokula-Bili kuhusu mwanakandarasi
⇒ Jina si kitu, tumbo ndilo muhimu
⇒ Misimu-kuwa mteja siku mbili-Bili kutopatikana baada ya mambo kuhariiiibika
⇒ Mtu hali kanuni

Methali

⇒ Huenda hizi ni dalili za mvua
⇒ Hujui ngojangoja huumiza matumbo-ugonjwa hauwezi kungojea dawa.
⇒ Kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji-Bili-Meya hawezi kuathirika na mgomo
⇒ Haraka haraka haina baraka-Waridi kwa Siki
⇒ Ganga ganga za mganga humlaza mgonjwa na matumaini
⇒ Wasemao mchana usiku watalala
⇒ Hizi ni Mbio za sakafuni-Bili-mgomo hautafanikiwa
⇒ Heri nusu shari kuliko shari kamili-Siki kwa Tatu-kucheleweshwa kwa mishahara ni bora kuliko kukosa kabisa.
⇒ Sikio la kufa haliSikii dawa-D111 kwa Siki anapomwambia anaweza kumshawishi Meya-ukaidi/hashauriki
⇒ Msiba wa kujitakia hauna kilio
⇒ Asante ya punda ni teke-kukosa shukrani -Meya anaposema aitiwe mhazili na kuambiwa na Gedi ameshaondoka-alimpa kazi licha ya kutokuwa na hitimu zinazofaa.
⇒ Wengi wape-Meya kwa DIII
⇒ Mazoea yana taabu-kuacha tabia ni vigumu
⇒ Lililoandikwa…(halifutiki)-majaaliwa ya mungu kuonana na D111
⇒ Mtu huvuna alichopanda-viongozi wabaya huchaguliwa na wananchi.-D111
⇒ Mhitaji siku zote ni mtumwa-Meya kuonyesha wafanyakazi waliogoma wangelazimishwa kurudi kazini na mahitaji yao ya kila siku.

⇒ Hakuna bwana, hakuna mtwana-D111 Meya anaposema wafanyakazi ni watumwa kuonyesha kuwa wao na baraza wanahitajiana/huhudumiana.
⇒ Msiba wa kujitakia kilio kamwe hauna-Meya anapoSikia wafanyakazi wakivurumishwa
⇒ Mpiga ngumi ukuta…-Meya wakivurumishwa.
⇒ Yaliyopita yamepita. Tugange yajayo-D1 kwa Meya anapojuta kutomSikiliza D111
⇒ Ya mungu ni mengi-askari wanapoingia ofisini kumtia mbaroni Meya na washirika wake.

Majazi

i) Sosi-kutokana na source kumaanisha chanzo cha matatizo au msimu uaomaanisha kula kwa kutumia cheo kujilimbikia mali.
ii) Kheri-kutokana na uadilifu kwa vile hana tamaa kama wenzake au baraka kwa jamii kwa kupinga maovu.
iii) Siki-kitu kichungu kinachotumiwa kama kiungo. Anasababisha machungu kwa viongozi kwa kupinga uovu wao. Anaongoza maandamano na kushauri Meya kushughulikia malalamiko ya wafanyakazi.
iv) Waridi-aina ya ua linalovutia lakini hunyauka punde tu linapotolewa mtini. Anawapa matumaini wagonjwa. Ghafla anajiuzulu na kuacha wagonjwa wateseke.
v) Cheneo-kitu kilichoenea na kutapakaa kila mahali. Kuenea kwa uozo, mogomo, ukatili, shida n.k.
vi) Shuara –mji ambako ndege zilielekezwa baada ya wafanyakazi wa uwanja wa ndege kugoma-shwari, utulifu.
vii) Kajifahari-mkahawa ambao Meya na Bili waliuzuru-maarufu.

Ulinganuzi

⇒ Kuweka vitu viwili pamoja ili kusisitiza tofauti
⇒ Meya na diwani III
⇒ Diwani 111 na Diwani 1 na 11
⇒ Siki na Waridi
⇒ Shuara na Cheneo
⇒ Tatu, Beka na Medi na Gedi na Dida

Uzungumzi nafsia

⇒ Mhusika mmoja kuongea peke yake.
⇒ Hivi huyu ana nia gani-Meya Dida anapopeleka viyai vidogo
⇒ Meya kuongea peke yake kuhusu dhifa murua ambayo angewapa wageni mameya.
⇒ Meya anapojisemea mwenyewe kuhusu viyai vidogo alivyotengenezewa
⇒ Meya anapojisemea mwenyewe kuhusu mapokezi ya mameya ambao wangezuru Cheneo –vile angewapokea kifahari ili watoe ufadhili.
⇒ Siki anapojisemea kuhusu matatizo ya Cheneo-vile mji umejaa njaa na kuongozwa na wenye njaa ni hatari sana.
⇒ Meya kujisemea diwani III anapomshauri akutane na viongozi wa wafanyakazi tu lakini si kila mtu.
⇒ Meya ofisini akipanga mapokezi ya mameya wageni-Cheneo si mji hivi hivi, wauone ukarimu na maana ya undugu wetu.
⇒ Meya kijisemea D111 anapoondoka-hawa wanaotaka uwaSikilize ni mzizi wa vizazi vya kesho! …Nafikiri ninaweza kuzungumza na viongozi wao si kila mtu-tenga utawale
⇒ Meya kujizungumzia akiwa ofisini kupanga mapokezi ya wageni-atamfurusha mwanakandarasi, hatamu mpya, mipango mipya.
⇒ Dida katika wimbo wake jinsi wafanyakazi walivyofurushwa kwa risasi, vitoa machozi na magari ya maji.

Nidaha/siyahi

⇒ Pole!-Dida akimpa Meya pole
⇒ Alaa!-dii kushangaa anapoSikia wafanyakazi wa uwanja wa ndege wamegoma.
⇒ Kisha unamruhusu kunipunja kwa kuleta viyai kiasi hiki? Eeh?-hasira
⇒ Naam!-Waridi akimwitikia Siki
⇒ Alaa!-Siki akishangaa kwa wagonjwa kufika kwa wingi licha ya dawa kutokuweko.
⇒ La hasha!-Siki akisisitiza si habari za kugoma amepelekea Meya.

⇒ Sadakta! Bora usinisahau-sawa Bili-kuridhika
⇒ Pole!-Siki kwa Waridi kwa jamaa yake kufa-mtoto wa mamake mdogo-binamu
⇒ Asante-Tatu anapokaribishwa na Siki
⇒ Aamen-Meya akiitikia maombi ya mhubiri.

Mbinu rejeshi

⇒ Siki anarejelea amewahi kuanzisha mgomo mwingine
⇒ Uongo wa dawa kuwa bahari kuu unarejelewa mara kwa mara
⇒ Kitoto kufia mokononi mwa Siki kwa njaa na ugonjwa
⇒ Tunafahamishwa na Meya kuwa Siki alikuwa na utundu utotoni.
⇒ Bili kutukumbusha yeye na Meya wamewahi kwenda katika mkahawa wa kajifahari wiki mbili zilizopita kujistarehesha.
⇒ Meya amewahi kumpa Meya ushauri uliomdumisha mamlakani
⇒ Kuna mwanakandarasi aliyekuwa na mkataba na baraza alilomwambia.
⇒ D111-zamani Meya alikuwa anamSikiliza na kutilia maanani
⇒ Bili kutufahamisha jinsi wafanyakazi walivyovurumishwa na askari kila mtu na mguu wake kumponya wanapoongea na Meya na madiwani.
⇒ Dida katika shairi lake anatufahamisha jinsiwatu walivyovurumishwa wakatimua mbio sana kwa kuogopa kuuawa.
⇒ Beka kueleza jinsi juzi mtoto wa kerekecha alikufa kama nzi mikononi mwa kerekecha akitazama.
⇒ Mama akieleza Siki mtoto alianza kuendesha lini siku iliyotangulia baada ya chakula alichotoa kwa bwana kwa kutokitokosa wali na maharagwe yaliyolala.
⇒ Meya kutufahamisha kuhusu mwanakandarasi aliyepewa kandarasi na Meya wa zamani ya kupelekea baraza bidhaa na ana mkataba ambao haujakwisha na ungeisha miaka mitatu iliyofuata.

⇒ Siki kueleza jinsi mara ya mwisho alipokuwa kwa Meya jinsi aliamuru asiruhusiwe kuingia kwake nyumbani au ofisini
⇒ Jinsi alivyofahamishwa hilo na mfanyakazi mmoja wa Meya aliyesoma naye shule moja.
⇒ Kufahamishwa na DI jinsi Bili alikuwa akipigiwa simu tangu siku kabla iliyopita na hakuwa akipatikana.

Taharuki

⇒ Mtoto kulazwa, kupewa mchanganyiko wa sukari na chumvi hatima yake gani?
⇒ Sauti za wafanyakazi
⇒ Askari wanapoingia Meya akiombewa na mhubiri-Nini kimejiri?
⇒ Wafanyakazi wa uwanja wa ndege kugoma wageni wakitarajiwa siku hiyo, nini kitajiri?
⇒ Mama anapoingia ghafla bila kufuata utaratibu Waridi anamkemea watakubali kumhudumia kwa dharura aliyo nayo?
⇒ Pale Gedi anapoingia ofisini ya Meya wakiwa na D1 na D11 akihema na akiongea kwa kusitasita, kimetokea nini?
⇒ Wageni kukaribia kuwasili na mji ni mchafu na hakuna uwezekano wa kuajiri vijana nini kitajiri?
⇒ Wafanyakazi kugoma na wageni wanatarajiwa kuwasili siku hiyo saa tano unusu usiku. Nini kitatokea?

Nahau/semi

⇒ Meya kumwambia Gedi amwambie Dida aende mbio
⇒ Yamenifika shingoni
⇒ Unamkanyaga nyoka mkia-Siki kwa Meya
⇒ Watu sasa wanafahamu mbivu na mbichi-D111 ukweli.
⇒ Ndiyo huko ndiko kuwaua ndege watatu kwa jiwe moja
⇒ Mlango huenda hatimaye ukasalimu amri
⇒ Wanakipeleka chombo mrama
⇒ Ni kazi ya kijungu meko/jiko-Beka-ya kumpatia mtu riziki tu.
⇒ Tangu utandu mpaka ukoko-wawakilishi kusema wanaelewa vyema yanayoendelea katika baraza, kutenga DIII na kufanya maamuzi na wanaomuunga mkono.

⇒ Kupiga hatua-kupata ufanisi/maendeleo mapya kila uchao-Meya
⇒ Unadhani nyimbo zinawashibisha na kukata kiu ya uhitaji wao?-kushughulikia matakwa yao.
⇒ Nyumba yangu aione paa-Meya-Gedi asimruhusu Siki asiwahi kuingia kwake.
⇒ Mbivu na mbichi-Diwani III
⇒ Kupunguza joto
⇒ Bili-ya kina yakhe-elimu ya maSikini
⇒ Bili kutaka kujua kama mkewe Meya ashajifungua-kupata mtoto.
⇒ Msikate tamaa-Siki kwa Tatu-msipoteze matumaini.
⇒ Inavunja moyo-kuona watu wakivurumishwa na askari-kuSikitisha
⇒ Si wengi wanaoweza kuwakosoa jamaa zao wanapokipeleka chombo mrama
⇒ Mimi niko radhi kutekeleza uyatakayo ingawa shingo upane-DIII kwa Meya anapomshinikiza-bila hiari.
⇒ Kazi ya kijungu meko-beka-isiyo na akiba/cha kuweka.
⇒ Tangu utandu hadi ukoko-Medi-wanajua yote kuanzia mwanzo mpaka mwisho yanayoendelea katika baraza.
⇒ Anaungana na mahasidi kunitoa roho-Meya anarejelea mhazili-kuporomosha uogozi wake.
⇒ Yote haya yametiwa chumvi na wanahabari-Meya akielekea kushikwa-kufanywa yaonekane makubwa.
⇒ Halafu nitiwe ndani-Meya kwa Bili –afungwe gerezani
⇒ Uma na kuvuvia-dhuru mtu kwa kutumia ujanja asielewe.

Taswira

⇒ Mwandishi anapotueleza kuhusu meza ya maakuli ya Meya kwamba imejaa mayai na vyakula kutuchorea picha ya ulafi.
⇒ Maelezo ya Waridi huleta hali halisi ya zahanati.
⇒ Uvundo na maji ya taka unachora picha ya mji ilivyo.
⇒ Wafanyakazi wanavyokabiliwa na polisi kutembeza virungu na risasi.
⇒ Siki anapomwambia Meya kwamba anaingiza kidole kwenye mzinga wa nyuki-hatari.

⇒ Picha ya mtoto mgonjwa ya Waridi akimwambia Siki-kitoto chenyewe kiriba chaongoza-kuvimba tumbo kwa utapia mlo.
⇒ Dida-picha ya hali ya mambo wafanyakazi walivyofurushwa-wazee kutimua mbio, bunduki, magari ya maji.
⇒ Picha ya usafiri wa wafanyakazi na madiwani wakielekea kazini-kwa kutembea kutoka mabandani jua likiwaka au kukinyesha na viatu kuharibiwa na lami na madiwani wanasafiri katika magari yenye vifaa vya kusafisha hewa.

Tashtiti/kicheko/vichekesho/dhihaka

⇒ Meya kujifanya mwokovu na kutoa matamko ya kidini-Aamen, Aamen.
⇒ Meya kutumia pesa vibaya na wagonjwa wanapewa mchaganyiko wa chumvi na sukari.
⇒ Pale diwani na wandani wake wananaswa na askari baada ya mambo kufikia kiwango kibaya na Bili hajulikani aliko
⇒ Diwani I na II wanacheka baada ya kuambiana kwamba siku zote wanazizima tarumbeta za wasiotosheka kama kwa kukohoa tu.
⇒ Meya anacheka baada ya kujisemea kuhusu maandalizi ya wageni wanaokuja.
⇒ Diwani I na II wanacheka baada ya kuambiana kwamba siku zote wanazizima tarumbeta za wasiotosheka kama kwa kukohoa tu.
⇒ Meya anacheka baada ya kujisemea kuhusu maandalizi ya wageni wanaokuja.
⇒ Dida anacheka baada ya kuigiza matendo ya askari walivyovurumisha wagomaji.
⇒ Meya na mhubiri kupokezana mikono wakicheka.

Utatu

⇒ Mtoto mgonjwa ana miaka mitatu
⇒ Alikufa akiwa na miaka mitatu
⇒ Kuua ndege watatu kwa jiwe moja
⇒ Madiwani watatu
⇒ Wawakilishi watatu wa wafanyakazi

⇒ Dawa zingefika bandarini baada ya siku tatu na baada ya siku tatu zingefika hospitalini
⇒ Meya na madiwani wawili wanakamatwa-jumla ya waliokamatwa ni watatu
⇒ Bunduki inayotema risasi tatu tatu-Dida akieleza kuhusu kuvurumishwa kwa wafanyakazi na askari.

Nyimbo

⇒ Sauti ya Siki anapojisemea
⇒ Njaa ina nguvu, imeangusha miamba-viongozi
⇒ Mwenye tumbo tupu anahitaji ashughulikiwe bila kucheleweshwa.
⇒ Sauti za wafanyakazi zinachukua muundo wa ushairi
⇒ Kilio-wanataka kuSikilizwa
⇒ Kudai haki, jasho, damu
⇒ Maslahi yao kuangaliwa
⇒ Malipo bora
⇒ Huduma za afya
⇒ Kudhalilishwa
⇒ Kupuuzwa daima
⇒ Mshahara zaidi
⇒ Dawa hospitalini
⇒ Sauti ya Dida

Kweli kinzani

⇒ Tumetembea lakini hatuendi mbele-Siki
⇒ Kwenda tunaenda lakini kinyumenyume

Chuku

⇒ Kufanya Cheneo kote kuwaka moto wa mafanikio-maendeleo makubwa
⇒ Kupuuzwa daima-sauti ya wafanyakazi-kukataa kabisa kusikilizwa
⇒ Wanadai takriban kila kitu-Gedi anapoulizwa na Meya wafanyakazi wanataka nini
⇒ Vijana waliohitimu kushindwa kupata hata utopasi-kusisitiza ukosefu wa ajira.-Meya
⇒ Udumu milele na milele-mhubiri akiombea uongozi wa Meya.
⇒ Kumbe wazee huwashinda mbio vijana-Dida-kutimua mbio sana kujinusuru.

Sadfa

⇒ Siku wageni wanatarajiwa kuwasili kusadifiana na mgomo wa wafanyakazi wa uwanja wa ndege na wale wa bohari kuwaunga wenzao mkono.

⇒ Siku Siki anaenda kwa Meya na kwa DIII anawakuta wakiwemo.

⇒ Siku ambapo Meya na DI na II wanapokutana ndipo wanatiwa mbaroni.

⇒ Gedi kumpelekea Meya maji kunasadifiana na upepo kubadili mkondo wa harufu ya taka na kufanya Meya kulalamika kuhusu maji.

⇒ Siki ni binamu ya Meya. Binamu yake Waridi kufa kwa kukosa dawa.

⇒ Bili-kusitiri wizi/kukomesha malalamiko-kutangaza fimbo imeibwa na uchunguzi unafanywa mara moja kisha kuanzisha mazungumzo na wafanyakazi na kufanya waonekane wao ndio wasiotaka suluhu.

⇒ Wizi kupagwa kusadifiana na mgomo ili kusingizia rabsha.

⇒ Ziara ya mameya wageni inasadifiana na migogoro baina ya baraza na wafanyakazi.

⇒ Ule wakati Meya anasema hali yataka kutumia nguvu na angewapa askari amri kunyoosha mambo ndipo askari wanatokea si kufanya analotaka bali kumtia mbaroni.

⇒ Kutiwa mbaroni kwa Meya na diwani I na II kunasadifiana na wao kuwa katika mkutano wa kujaribu kutatua mambo.

MSTAHIKI MEYA (Ziada)

MANDHARI

- Mandhari ya tamthilia ya “Mstahiki Meya” ni mji unaoitwa Cheneo. Mji huu unatawaliwa na Baraza linaloongozwa na Mstahiki Meya pamoja na madiwani.
- Mji wa Cheneo una zahanati ambayo inafurika wagonjwa wakitafuta matibabu ingawa hakuna dawa.
- Mandhari ya nyumbani kwa Meya inaashiria kwamba ni nyumba ya kifahari iliyo na makochi na zulia lenye kuwaza ya kupendeza.

- Mitaa ya Cheneo imejaa uvundo kwa sababu ya kutozolewa taka, hasa baada ya mgomo wa wafanyakazi.
- Mandhari ya Mji huu ni kielelezo cha jinsi ilivyo miji mingi humu nchini kutokana na usimamizi mbaya.

MUHTASARI WA MAONYESHO
SEHEMU YA KWANZA
ONYESHO LA KWANZA
(Onyesho hili linafanyika kwenye zahanati wakati wa jioni)

- Daktari Siki anazungumza na waridi ambaye ni nesi (muuguzi). Daktari anaonekana mwenye wasiwasi. Anauliza wagonjwa wamefika wangapi zahanatini. Naye Waridi ana-dokeza kuwa wagonjwa waliofika ni wengi kuliko siku iliyo-tangulia.
- Hata hivyo, lililo wazi ni kuwa hakukuwepo na dawa hata kidogo. Waridi anasema kuwa Meya aliwataka wawashauri wagonjwa wasubiri dawa; kwamba walikuwa wameagiza da-wa zingefika hospitalini baada ya siku sita. Hata hivyo, Daktari Siki hakubaliani na madai hayo. Anasema, “Wakisubiri ugo-njwa wao utasubiri? Hujui ngoja ngoja huumiza matumbo?” (ukurasa 3)
- Waridi anamwambia Siki kuwa hata wagonjwa zaidi wakipokelewa hawataweza kusaidika. Aidha wagonjwa we-nyewe hawana uwezo wa kulipia huduma. Hii ni kutokana na umaskini. Anaongeza kusema kuwa mfumo huu wa wago-njwa kugawana gharama ya huduma unahimizwa na wazu-ngu. Maoni ya Daktari Siki ni kuwa si kweli kwamba watu ni maskini kwa sababu nchi ni maskini.
- Mama mmoja mfanyakazi wa Baraza la Jiji anaingia ali-kokuwa daktari na nesi. Analalamika kuwa mtoto wake wa pekee aliyembeba alikuwa mgonjwa na kwamba alikuwa anataka usaidizi kabla mtoto kufa.
- Anapoambiwa aeleze hali ya mtoto anasema kuwa amekuwa akiendesha tangu siku iliyotangulia. Hii ni baada ya kula kiporo ambacho mama mtu alitoa kwa mwajiri wake anakofanya kazi. Huku ni kwa Mstahiki Meya wa jiji la Che-neo.

- Hapo mtoto anapokelewa kwenye wodi na nesi. Baadaye Waridi anasema kuwa baada ya kumchunguza mtoto huyo alibaini kuwa aliugua pia utapiamlo. Hii ni kutokana na uko-sefu wa lishe bora.
- Anashauriwa na daktari ampe huduma ya kwanza ili kumpa matumaini. Onyesho linapofika mwisho ni bayana kuwa nesi ana imani kuwa dawa walizoahidiwa zingefika hospitalini. Hata hivyo Daktari Siki anatofautiana naye akia-mini kuwa ahadi ya dawa ni siasa tu za Meya.

ONYESHO LA PILI
(Onyesho hili linafanyika nyumbani kwa Meya)

- Hii ni siku iliyofuata ile ya onyesho la kwanza kule zaha-natini. Mazingira ya mahali hapa ni ya kupendeza. Yanao-nyesha uwezo mkubwa wa kiuchumi alio nao Meya. Meya yuko peke yake akijapatia staftahi. Anapiga funda zito la chai ambalo linamchoma. Anamtuma Gedi, mpambe wake, aka-mwite Dida. Dida ni mhudumu wa hapo nyumbani kwake. Anakuja na kunyenyekea mbele ya Meya, japo Meya anaka-shifu unyenyekevu wake. Meya analalamika pia kuwa mayai aliyoletewa ni madogo. Anamwamrisha kwamba aliyekuwa akiyaleta amshauri asiyalete tena.
- Dida anapotoka anaingia daktari Siki. Siki ni binamuye Mstahiki Meya. Kwa sababu hii Siki anamwita jina lake ambalo ni Sosi. Meya hafurahishwi na hatua hiyo ya Siki ya kutomtambua kama Meya. Anamwambia, “Pamoja na salamu zako, lazima uniite Sosi? Wewe tu ndiye hujui kuwa mimi ndiye Meya wa Baraza la mji wa Cheneo?” (Ukurasa 10)
- Siki anasema hayo si muhimu. Kilicho muhimu ni yale ambayo yalimleta hapo kwa Meya. Inabainika kuwa sababu ya daktari huyu kuja hapa ni kuwasilisha matatizo ya wafanyakazi wa jiji la cheneo.
- Katika mazungumzo yao, Meya anatetea maendeleo katika jiji hili. Hata hivyo Siki anapuuza maendeleo haya na

kusema kuwa watu wana shida (Ukurasa 11). Anaongeza kuwa wananchi wana matatizo kama vile njaa (Ukurasa 12). Meya anatetea uongozi wake na kusema kama asingekuwa mzuri asingechaguliwa mara tatu. Anajisifu kuwa amedumisha utulivu na imani katika eneo lake.

- Daktari Siki anamshtumu Meya na Madiwani wenzake kwa kutofikiria watu waliowachagua. Analinganisha tabia hiyo na kuwatusi wananchi. Kulingana naye uongozi wa Meya ni ukoloni mamboleo. Aidha anatahadharisha kuwa hatua hiyo ni hatari kama kukanyaga nyoka mkia (Ukurasa 15). Kilele cha yote hayo, Mstahiki Meya anamtaka Gedi amtoe Siki nje kwa nguvu. Lakini Siki anasema angeombwa aondoke angeondoka tu na wala hakuna nguvu ambazo zahitajika.
- Punde Meya anamtuma Gedi akamwambie mhazili amw-andalie mkutano wa kamati ya Meya ambao ungefanyika ala-siri hiyo.

ONYESHO LA TATU

(Mandhari ni ofisini mwa Meya)

Ni katika mkutano ambao Meya aliitisha. Washauri wake (Diwani I,II, na III) wanamsubiri Meya.

Mazungumzo ya Diwani I, II, na III yaonyesha kuwa raia wam-eanza kupinga uongozi dhalimu wa Meya. Diwani II anasema kuwa Meya kuwaita yaonyesha hali si nzuri. Diwani I aona hili kama dogo. Anasema wameona wengi wakilalamika nao (Diwani I na II) wakawanyamazisha. Diwani III awaambia kuwa sasa watu wamezinduka na wanataka vitendo si maneno.

Mazungumzo kati ya Diwani I,II na III yaonyesha uzalendo wa kijinga wa washauri wa Meya. Diwani I anajibu kauli ya Diwani III kuwa jukumu lao ni kulitetea baraza la Mstahiki Meya. Diwani I na II wanaona kama heshima kubwa waliotunukiwa kuhudumu katika kamati ya Meya. Diwani III anaonya Diwani I na II dhidi ya ubinafsi, uzalendo wa kijinga na ukatili. Hawaku-chaguliwa kupiga vita raia, walichaguliwa kuleta maendeleo katika Cheneo yote. Meya anaingia na kuwajuza madiwani hali si nzuri. Anasema kuwa baadhi ya madiwani wamezindua raia na

kuangazia udhaifu wa Baraza wa kutowajibikia majukumu yake. Ni dhahiri kuwa uongozi wa Meya haujatekeleza majukumu yake. Hivyo kuzorota kwa hali ya usafi mjini. Meya anashi-ndwa kunywa maji aliyoletewa na Gedi kutokana na harufu mbaya nje.

Ili kurekebisha hali, Diwani I anasema atawaambia vijana kutumia nguvu(kutembeza virungu) ili watu wasiandamane.

Vilevile Diwani I na II wanatarajia kuinua viwango vya uzale-ndo kwa kutumia hila zifuatazo:

i. Mashindano ya vijana ya kubuni.
ii. Kutunga na kucheza nyimbo. Yaonyeshwe katika vyombo vya habari.
iii. Vijana kujionea fahari. Diwani III anaonya wenzake dhidi ya mipango hii isiyofaidi wanyonge.

Analalamikia:

a) Mishahara duni ya wafanyakazi.
b) Ukosefu wa ajira.
c) Kucheleweshwa kwa mishahara.
d) Mataifa yenye uwezo mkubwa kiuchumi yanadhibiti mataifa machanga. Mfano: Kubuni sera za uajiri na kupunguza wafanyakazi. Pia Baraza haliwezi kuo-ngeza mishahara kwani mataifa hayo hayajatoa mikopo.

- Diwani III apendekeza watafute mbinu za kukabiliana na hali duni ya maisha badala ya kuwadanganya watu kuwa dawa zimeagizwa na hali sivyo.
- Asema kuwa ahadi hizi za uongo zinawashinikiza wafa-nyakazi kutaka kujieleza. Mazungumzo kati ya Meya, Diwani I, II na III yamedhihirisha tamaa na ubinafsi wa uongozi wa umma.
- Meya aidhinisha uundaji wa kamati ambazo hazina umu-himu, nyongeza ya mishahara au marupurupu ya walinda usa-lama na kutotozwa kodi kwa madiwani. Kinaya ni kuwa Bara-za lina nakisi(deficit) ya shilingi milioni mia moja na ishirini, ingawaje hata mama muuza mboga analipa ushuru.

- Diwani I na II wanadai kuwa wanahitaji kuvaa vyema katika mapokezi wasije wakajidunisha mbele ya mameya. Meya anamwamuru Diwani III kukubaliana na njama zao za matumizi ya kiholela ya mali ya umma.

Masuala yanayoibuka katika onyesho:

a) Uongozi mbaya.

i. Meya anawateua washauri wanaoendeleza maslahi yake, mfano, Diwani I na II.
ii. Meya aidhinisha matumizi ya kiholela ya fedha huku akijua baraza halina pesa.
iii. Meya,Diwani I na II wanapinga ushauri wa Diwani III kuhusu matumizi bora ya pesa.
iv. Mbinu hasi za uongozi na propaganda.
v. Jiji limekuwa chafu.
vi. Kamati zisizofaidi raia ili kumuunga mkono Meya.
vii. Vitisho (matumizi ya virungu).
viii. Meya aidhinisha kutotozwa kodi kwa madiwani.

b. Hali duni ya maisha/umaskini.

i. Ukosefu wa ajira.
ii. Mishahara duni.
iii. Kupunguzwa kwa wafanyakazi.

c. Utetezi wa haki.

i. Diwani III atetea haki za wafanyakazi.
ii. Pia apinga nyongeza ya mishahara kwa madiwani.
iii. Ukoloni mamboleo.
Mataifa ya wafadhili yalazimisha Cheneo kupunguza wafanyakazi.
iv. Ubinafsi/tamaa.
Madiwani I na II na Meya waidhinisha madiwani kuongezwa mishahara na kutolipa kodi.

SEHEMU YA PILI

ONYESHO LA KWANZA

(Mandhari ni ofisini mwa Meya)

- Meya yumo katika uandalizi wa kuwapokea mameya. Katika uzungumzi nafsia, apanga kuagiza divai na mvinyo kutoka ng’ambo. (Ubadhirifu).
- Onyesho lina mazungumzo kati ya Meya na Bili aliye ra-fiki yake na mshauri wake. Ushauri wa Bili waongozwa

na ubi-nafsi. Anamshauri Meya kuliibia baraza kupitia mwanakanda-rasi. Meya atamhimiza mwanakandarasi kulishtaki baraza kuhusu kukatizwa kwa kandarasi kabla ya wakati kuisha, bara-za limfidie naye ampe Meya asilimia fulani ya fidia. Bili amku-mbusha Meya asimsahau kwa hili.

- Meya ameshamgawia Bili vipande vinne vya ardhi ya umma. Walitumia pesa za umma. Meya alimpeleka bibi yake ng'ambo kuzalia huko, kuwapeleka wanawe kusomea huko,kujistarehesha kwenye hoteli za kifahari; yeye, Bili na familia yake.
- Katika onyesho tunaona juhudi za wafanyakazi za kupi-gania haki zao. Meya na Bili wakiwa ofisini sauti za wafanya-kazi wanaolia malipo bora, huduma za afya, na kuthaminiwa zinasikika. Meya anashtuka akimlaumu Siki kuwa ndiye ana-yechochea.
- Bili anamhimiza Meya kupuuza sauti hizi, anaziona kuwa kelele za chura ambazo hazipaswi kumzuia Meya kufanya analolielewa. Meya anadai kuwa hajakataa kuwahudumia wafanyakazi. Ukweli ni kwamba ingawa Meya anadai kushu-ghulikia mahitaji ya wafanyakazi, anapoambiwa na Gedi kwamba wafanyakazi wamegoma, anatuma Gedi awaambie kuwa kama hawataki kuonyesha shukrani kwa baraza, baraza litawafuta kazi. Anawatisha kuwa kuna vijana waliohitimu katika vyuo vikuu na hawajapata hata kazi ya utopasi.
- Tabia ya viongozi ya kukabiliana kikatili na wapigania haki inajitokeza katika onyesho hilo. Meya anamtuma Gedi amwagize afisa mkuu wa usalama awaite polisi wawatawanye wafanyakazi waliogoma.

Maswala muhimu:

a) Uongozi mbaya.
b) Ubadhirifu wa mali ya umma.
c) Ufisadi – kupitia kandarasi.
d) Tamaa na ubinafsi.
e) Unafiki – ushauri mbaya wa Bili, alitaka anufaike.
-Meya amsifu ili azidi kumpa ushauri
-Meya na mwanakandarasi.

ONYESHO LA PILI
(Mandhari ya onyesho ni ofisini mwa Siki)

- Siki anapokea simu kutoka kwa Tatu. Tatu na Siki wana-agana kukutana ofisini mwa Siki.
- Uzungumzi nafsia unatokea baada ya mazungumzo haya ya simu unaodhihirisha kwamba wafanyakazi hawajaridhi-shwa na hali ya mambo. Siki asema kwamba aliwaambia vio-ngozi kuwa watu wenye ugonjwa wa njaa ni hatari huangusha wenye nguvu.
- Maneno ya Siki yathibitika Waridi anapoingia ofisini mwa Siki na kumwambia kwamba ajiuzulu; analalamika ukosefu wa dawa ambao umesababisha kifo cha binamu yake, malimbikizo ya mishahara na kudorora kwa usafi hospitalini. Anamwambia Siki kuwa wafanyakazi watagoma. Jambo hili litathibitika Tatu anapokuja ofisini mwa Siki.
- Mazungumzo kati ya Siki na Tatu yatathibitisha kuwa wawakilishi wa wafanyakazi wamekuwa wakitaka kukutana na Meya kuwasilisha malalamishi yao. Meya hajadiriki kukutana nao akidai kuwa shajara yake imejaa. Hii ndiyo sababu Tatu anakuja amwombe Siki azungumze na Meya kwani ni mabinamu, huenda akasikizwa. Siki amwambia amejaribu bila mafanikio. Tatu amwambia Siki kwamba ameona suluhisho ni mgomo.
- Siki anaonyesha ukomavu na uwajibikaji kwa kumwo-nyesha Tatu madhara ya mgomo. Anamwambia wachukue hatua polepole wasije wakateseka zaidi. Amjuza Tatu kuwa mameya wanakuja kutembelea Cheneo, wafanyakazi wakim-sisitizia Meya umuhimu wa usafi na kutishia kususia shughuli za kusafisha, huenda akawasikiliza.
- Aidha Siki anaahidi kuwajibikia kilio cha wafanyakazi kwa kuzungumza na Diwani III.

Masuala ibuka:

a) Dhuluma

i. Kiongozi hasikii vilio vya wafanyakazi.
ii. Asema shajara yake imejaa hawezi kuonana na akina Tatu.
iii. Malipo duni.

iv. Malimbikizo ya mishahara.
v. Viongozi wanatoa ahadi za uongo kwa wafanyakazi.
vi. Vifo kutokana na ukosefu wa dawa.
vii. Ukosefu wa maji katika zahanati.

b) Upiganiaji haki

i. Waridi anajiuzulu kufuatia hali duni katika mazingira ya utendakazi.
ii. Wafanyakazi wamesusia kazi.
iii. Tatu amekuja kumwona Siki kwa ushauri kuhusu namna ya kuwasilisha malalamishi yao.
iv. Siki amezungumza na Meya na Diwani III kuhusu hali ya wafanyakazi.
v. Siki anamshauri Tatu waende hatua kwa hatua wasije wakajihasiri zaidi.

ONYESHO LA TATU
(Mandhari ni ofisini mwa Meya. Unafiki wa kidini unadhihi-rika)

- Mhubiri amekuja kumwombea Meya. Awali Bili alimwambia Meya kuwa anahitaji maombi. Meya anamshu-kuru mhubiri, naye mhubiri kwa unafiki anasema kwamba Meya ni ndugu mpendwa na mhubiri akiitwa na ndugu sharti aitike. Anadai kuwa kutotii ni kutomtii Mungu.
- Uhusiano wa Meya na mhubiri unaongozwa na ubinafsi. Meya anajidai kupendezwa na dini, hata anamwambia mhu-biri kwamba kila wakikutana kuna kinachomsukuma kutaka kuacha kazi ya udiwani na kumfuata mhubiri.
- Nia ya Meya nikujipendekeza kwa mhubiri ili amwombee naye Meya ajidumishe mamlakani. Mhubiri anausifu ucha Mungu wa Meya na kumwombea Meya kwa nia ya kumvuta Meya kumtolea sadaka (unafiki). Meya na mhubiri waingiwa na jazba na hatima yake ni Gedi kuingia kujua kinachoende-lea.
- Tendo hili la Gedi na maafisa wa usalama linaleta uche-shi unaodhamiriwa kuwasuta Meya na mhubiri kwa kutumia ofisi ya umma kwa maslahi ya kibinafsi. Mhubiri anapuuza ‘uvamizi’ huu na kuchukulia kama mateso

yanayowapata kati-ka harakati za kuendeleza kazi ya Bwana. Kauli yake yaonye-sha unafiki.

- Ubadhirifu na ukosefu wa uwajibikaji wa Meya unajito-keza. Analibebesha baraza mzigo wa kifedha kwa kumwahidi mhubiri sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi. Vilevile Meya anampa kazi ya kumwombea kila juma na kumwahidi kugha-ramia petroli atakayoitumia katika safari yake.

Masuala muhimu:

a) **Unafiki**

i. Meya ajifanya mpole anapozungumza na mhubiri
ii. Meya kudai ana hamu ya kuacha umeya na kuingilia uhubiri.
iii. Sadaka ya kumvutia mhubiri kwake na si sababu ya ucha Mungu.
iv. Mhubiri kumsifu Meya kwa kutafuta upendo wa Mungu na kumhimiza kufuata dini. Hila ya kumvuta Meya kwake.
v. Mhubiri anamwombea Meya ili apate sadaka na pesa za petroli.
vi. Meya aitikia ‘Amen’ kujifanya mcha Mungu.
vii. Meya anamwambia mhubiri kwamba baraza limeta-mbua mchango wa wahubiri. Hii ni hila ya kujionyesha mwema.

b) Tamaa ya ubinafsi

i. Mhubiri kumwombea Meya ili afaidike na sadaka inayo-tolewa na baraza.
ii. Meya ataka kuombewa ili adumu uongozini.

ONYESHO LA NNE

(Mandhari ni nyumbani mwa Diwani III)

Siki amekuja kumwona Diwani III kama alivyomwahidi Tatu.

- Mazungumzo ya Siki na Diwani III ni ya kuzungumza na Meya. Anamwambia Siki kuwa Meya; sikio la kufa,halimsikilizi tena; anawasikiliza washauri wake wanaompotosha. Cheo ki-memlevya kiasi cha kusahau alipotoka.

- Diwani III anachukizwa na vitendo vya kikatili vya askari wa baraza kuwatawanya wafanyakazi wanapotaka kulalami-kia hali zao. Vilevile tamaa ya madiwani inaonekana na wana ushawishi kwa Meya. Meya huwaalika tu wale ambao wanari-dhia matakwa yake. Diwani III hashirikishwi katika vikao vina-vyohusu matumizi ya fedha lakini baadaye huaminishwa kute-kelezwa yaliyoazimiwa katika vikao hivyo.
- Onyesho ladhihirisha uwezo mkubwa alio nao Meya. Kuna sheria ambayo inampa Meya mamlaka ya kukabiliana na migomo (anaweza kunyamazisha yeyote)
- Kuna sheria ambayo inampa mamlaka ya kumchukulia yeyote hatua .
- Uwajibikaji wa pamoja wa madiwani unawanyima uhuru madiwani waadilifu, kama vile Diwani III kupinga maamuzi ya wengine(wengi wape).
- Meya ndiye anayeamua kuhusu matumizi ya viwanja vya umma. Jambo hili linapalilia ufisadi.
- Siki analiona tendo la madiwani kutoshughulikia raia kama usaliti. Naye Diwani III anamkumbusha wajibu wa raia, hasa wanataaluma katika uteuzi wa viongozi, anawashutumu wanataluuma kwa kutojiingiza katika siasa wakisema kuwa siasa ni mchezo mchafu. Anamwambia Siki kwamba hata watu wakapewa fursa nyingine,watachagua viongozi hao hao tu. Kwa hivyo hata raia wamechangia katika tatizo la uongozi mbaya.
- Siki amsihi Diwani III kumhimiza Meya kushughulikia ma-slahi ya wanyonge. Diwani III anaonyesha kuwajibika kwa ku-mwahidi Siki kwamba atamzungumzia Meya kuhusu hali ya wafanyakazi, asema Meya apaswa kusikiliza malalamishi ya wafanyakazi na sio kujinyakulia ardhi, yeye na wenzake. Ana-msisitizia Siki kuwa wote wapaswa kushirikiana kubadili hali kwani raia na uongozi wote wamekosa - raia wanawachagua viongozi hawa, nao viongozi wanawadhulumu.

Masuala muhimu:

- Meya na madiwani wenzake wanaunda sera na mbinu za uongozi mbaya, wao ni zao la umma uliowachagua.

- Raia walalamika uongozi eti ni mbaya na hawataki kujii-ngiza katika siasa eti ni mchezo mchafu. Wanataaluma waadi-lifu kama Siki wameshindwa kujiunga na siasa.
- Mgogoro unazuka kati ya wanasiasa na wanataaluma. Mfano: Siki na Meya ni kama maji na mafuta.
- Onyesho pia laonyesha pingamizi ambazo zinafunga juhudi za kujikomboa kwa unyonge:
  i) Mamlaka makuu ya Meya.
  ii) Uwajibikaji wa pamoja wa madiwani.
  iii) Kutengwa kwa washauri bora.
  iv) Matumizi ya vyombo vya dola, mfano, Askari kuwanyamazisha wapigania haki.
  v) Tamaa na ubinafsi wa viongozi.
  vi) Viongozi waadilifu na raia kutojiingiza katika siasa.
  vii) Dhuluma – askari wanawatawanya watu wanaolala-mika ukiukaji wa haki.
  viii) Kusingiziwa kwa washauri wapotovu kama Diwani I na II.

SEHEMU YA TATU
ONYESHO LA KWANZA
(Mandhari ni ofisini mwa Meya)
Meya amemwita Diwani III ambaye amefika. Pia mwenyewe alikuwa na nia ya kumwona Meya. Mazungumzo baina ya Meya na Diwani III yadhihirisha kuwa uongozi wa Meya umekosa busara.

- Amtaka aongeze madiwani mshahara mara moja huku ajua mwezi umebakia siku mbili na mishahara tayari imeanda-liwa. Diwani III anapomwambia haya, Meya asema kuwa hilo si neno, la muhimu ni kulipwa kwa hiyo nyongeza.
- Mazungumzo pia yaonyesha ukiukaji wa kanuni za bara-za. Diwani III anamwambia Meya kuwa hashiriki katika kikao kilichoamua nyongeza hii ingawa ndiye anayehusika na fedha.
- Vile vile wafanyakazi wamegoma kudai nyongeza ya mi-shahara, aeleza kuwa nyongeza kwa madiwani italeta

mivuta-no zaidi kwani uwezo wa kifedha wa baraza ni mdogo.

- Meya aonyesha ubaguzi na mapuuza anaposema hadha-rani kutokuwa na mivutano kwani madiwani ni madiwani na hawawezi kunyimwa haki zao. Hata hivyo Diwani III anamku-mbusha kuwa wafanyakazi ndio wanaotaabika kuzalisha mali ambayo wadiwani wanaila. Asema hakubaliani na Meya kuwaona madiwani kuwa wenye thamani kuliko wafanyakazi. Asema kuwa hao wafanyakazi ndio waliowachagua madiwani kuwawakilisha.
- Diwani III amwonyesha hasara ya mgomo wa wafanya-kazi kwa pato la baraza. Pato limepungua kwa kukosa kuku-sanya kodi mwezi jana. Meya anadai kuwa anawafahamu wafanyakazi, wangerudi baada ya siku chache kutokana na haja ya mahitaji ya kila siku. Asema wafanyakazi ni wahitaji hivyo ni watumwa.
- Diwani III amwambia Meya kuwa baraza linahitaji wafa-nyakazi jinsi wafanyakazi wanalihitaji baraza. Anapendekeza nyongeza ilipwe kwa madiwani na wafanyakazi baada ya wali-ogoma kurudi kazini.
- Kiburi na mtazamo finyu wa Meya waonekana pale ana-pomwambia Diwani III kuwa wafanyakazi wakigoma, kuna vijana wengi wanaoweza kufanya kazi hii kwa malipo ya chini na kuwa kazi wanazofanya ni za mikono zisizohitaji mtu kufu-nza. Diwani III anaposema kuwa hata kazi za mikono zinahitaji mikono na akili zilizozoea, Meya aliona kama hujuma na ana-mwambia Diwani III angoje wakati wake wa kutekeleza ayata-kayo. Kauli hii yaonyesha kiburi na kujiamini kwa Meya.

Mazungumzo kati ya Meya na Diwani III pia yaonyesha hali ya utegemezi wa mataifa machanga kwa yale yenye uwezo mku-bwa wa kiuchumi. Meya asema kuwa wageni wanaokuja wa-tawapa mikopo ya kulipia mishahara yao. Diwani III amwonya dhidi ya utegemezi huu kwani utaachia vizazi vijavyo madeni. Meya asema kuwa wao hawatakuwepo hivyo hivyo haina haja kujishughulisha. Diwani III amkumbu-sha kuwa japo kiongozi huweza kuondoka mamlakani,athari za uongozi wake, hudumu vile

vile wafanyakazi wanaotaka awasikilize ni mzizi wa vizazi vya kesho. Kauli hii inamchoma Meya. Aamua kuwasikiliza viongozi wa wafanyakazi.

Masuala muhimu:

Onyesho laonyesha jinsi viongozi hufilisisha jamii kwa kuandama sera mbovu za uongozi.

Tamaa na ubinafsi wa Meya wamfanya kushinikiza Diwani III kutia nyongeza ya mishahara kwa madiwani na huku baraza halina fedha.

Badala ya kutafuta jinsi ya kuongeza pato la baraza, anatege-mea mkopo kutoka kwa wageni kulipia nyongeza ya misha-hara. Maazimio ya Meya yanadhibitiwa na mahitaji ya sasa, hawazii hali ya kesho ya raia waliomchagua. Haoni ugumu wowote kulipia nyongeza ya mishahara kwa wachache huku akiviachia vizazi vya kesho mzigo wa kulipa madeni hayo.

a) Uongozi mbaya
   - Kuamrisha nyongeza ya mishahara ya madiwani na baraza halina uwezo.
   - Kikao kinaidhinisha matumizi ya fedha pasipo Diwani III na ndiye anayehusika na fedha.
   - Meya hawazii athari za uongozi wake.
   - Meya anakosa kuafikia wazo la Diwani III kuwa wabuni mikakati ya kuimarisha pato la baraza.
   - Meya atumia hali ya uhitaji wa wafanyakazi kuwanya-nyasa zaidi,asema watundu tu.

b) Ubaguzi
   - Madiwani wanaongezewa mishahara huku wafanya-kazi wakabaki na mishahara yao duni.

c) Utetezi wa haki.
   - Diwani III anapinga hatua ya Meya ya kuongezea mi-shahara ya madiwani na hiyo, wafanyakazi wanahitaji kuongezewa mishahara.

ONYESHO LA PILI.

(Mandhari ni ofisini mwa Meya)

Onyesho linapoanza, Meya yu ofisini. Sauti za wafanyakazi wanaolalamikia haki zao zinasikika. Kisha mlio wa risasi na wafanyakazi wanaotawanywa. Kuwatawanya wafanyakazi

kunamtia Meya fahari. Anacheka na kuuona huu kuwa msiba wa kujitakia. Bili, Diwani I na II wanaungana na Meya jinsi walivyokuwa wamepanga miradi ya uzalendo ambayo kwa kweli ni mbinu ya kujidumisha mamlakani. Mazungumzo kati ya Meya, Diwani I na II na Bili yanaonyesha unafiki wa viongozi. Bili asema kuwa matumizi ya nguvu ya-weza kutoa picha mbaya kwa wageni. Anataka wageni wape-we picha nzuri ili wafaidike. Baada ya kikao kifupi, Diwani I na II wanadai ovataimu kufidia kutopewa soda na Meya. Diwani II apendekezaBili alipwe kwa kumshauri Meya. Meya anapohofia kuwa Diwani III hata-idhinisha malipo haya, Bili anapendekeza wauze fimbo ya Meya, aona hapana haja kubeba dhahabu tupu mkononi, watafute soko ng'ambo.

Badala ya Meya na madiwani kulinda fimbo, wanaafikiana na kauli ya Bili.

Bili apendekeza Diwani I atoke na fimbo na kwa kuwa ndiye anahusika na usalama, hapana atakayekagua kisha atangaze kuwa fimbo imepotea baada ya wiki.

Meya aanzishe mikutano na wafanyakazi kuwafanya waone-kane kuwa ndio wasiotaka makubaliano.

Baada ya Meya kukubali kauli hii, anataka wote kuahidi kuhi-fadhi siri hii ya wizi na wasithubutu kumwambia Diwani III.

Masuala muhimu:

Pingamizi inayokabili juhudi za wanyonge kujikomboa ni vio-ngozi kukabiliana na migomo/maandamano kikatili.

i) Viongozi wanazidi kulipora baraza kupitia njama za kifisadi, mfano, kudai ovataimu.
ii) Ubinafsi wao wajitokeza wanapokubaliana kuiuza fi-mbo ya Meya ili kujilipa. (Fimbo ni kiwakilishi cha umeya)
iii) Ukosefu wa uwajibikaji wajitokeza katika kuuza fimbo.

Muhtasari

i) Utetezi wa haki – wafanyakazi kupitia kwa viongozi wao wanadai maslahi bora.
ii) Ukatili – askari kuwatawanya waandamanaji.

iii) Ufisadi – Meya aidhinisha kuibiwa kwa fimbo.
iv) Diwani I na II wanlipwa ovataimu kushiriki katika kupanga njama za kujiendeleza kama vile kuuza fimbo.
v) Bili analipwa kwa huduma ya lishe ambao ni mpango wa kuliibia baraza.
vi) Tamaa ya ubinafsi – Meya anaruhusu wizi wa fimbo ya Meya ili afaidike.
vii) Unafiki – bili apendekeza wasiwapige waandamanaji ili kuwapa wageni picha nzuri.
viii) Uongozi mbaya – Meya anamwachia Bili kumwamulia masuala muhimu kuhusu uongozi wa Baraza. Bili ndiye anayependekeza fimbo iuzwe.

ONYESHO LA TATU

(Mandhari ni nyumbani mwa Meya. Onyesho zima ni uzu-ngumzi nafsia wa Dida, mfanyakazi wa Meya)

Kupitia mbinu rejeshi, Dida anakumbuka kisa cha askari kuwa-tawanya wafanyakazi kwa bunduki na vitoa machozi na jinsi walivyoambiwa kujiponya.

Anaonyesha unafiki na uongo wa viongozi ambao hata wa-nyonge wanapokufa wanasema hawakufa.

Uigizaji na uzungumzi nafsia wa Dida pia unaonyesha ubaguzi unaoendelezwa na viongozi.

Asema kuwa kuna roho ya mtu na uhai wa mwenye nguvu (mtu)unathaminiwa kuliko wa wanyonge (kiatu). Amkashifu Meya kwa ubaguzi huu kwa kusema kwamba yeye na watu wake wana roho za watu ndiposa akawapeleka ng’ambo penye utulivu na pasipo na usumbufu kama Cheneo.

Vile vile Dida asema kuwa nyumba ya Meya inanadhifishwa huku mji mzima ukienea uvundo wa kutisha.

Masuala muhimu.

Ucheshi katika uzungumzi nafsia wa Dida unaonyesha viongo-zi wanavyotumia vyombo vya dola (askari) kujidumisha mamlakani.

Usaliti wa viongozi kwa raia unajitokeza kupitia kwa ubaguzi umeendelezwa na Meya, mfano:

a) Udhalimu .

I) Waanyakazi wa nyumbani (Dida) hutukanwa na waajiri wao.
II) Askari wanawatawanya wafanyakazi kupitia nguvu.

b) Ubaguzi
i) Dida asema kuna roho ya mtu na ya kiatu.

c) Ubinafsi .
I) Dida anajisuta kuwa hajali na mambo yasiyomhusu. Anasema hana haja ya kushughulika.

SEHEMU YA NNE
ONYESHO LA KWANZA
(Mandhari ni ofisini mwa Meya)

Meya anazungumza na wawakilishi wa wafanyakazi, Tatu, Beka na Medi. Kupitia malalamishi, dhiki zinazowakumba wa-fanyakazi zinabainika. Medi anamwambia Meya japo wame-pewa ajira na ujira kama anavyodai Meya, ajira hii haijali ma-slahi wala heshima ya watu.

Pia maneno ya Beka yaonyesha kwamba wafanyakazi hawali-pwi nusu ya mishahara tu,bali pia nyakati zingine mishahara ni duni na inachelewa.

Ajira waliyo nayo haiwafaidi hata baada ya kustaafu (hawa-wezi kuweka akiba).

Wanasisitiza kuwa ajira hiyo inawaumbua. Hata baada ya ku-fanya kazi kwa miaka, hawaoni matunda. Hawana akiba.

Kuna ubaguzi katika nyongeza kwa kuwa madiwani tu ndio hupata nyongeza. Beka anasema kuwa kipindi kirefu kimepita tangu kupewa nyongeza. Pia asema kuna ubaguzi katika uwa-nja wa matibabu, wanyonge wanapaswa kulipia huku madiwa-ni wakiwa na bima ya matibabu.

Jibu la Meya kuhusu malalamishi laonyesha kiburi na ukatili.

Tatu apinga hili akisema kuwa hawawezi kuwa sawa kwani:

a) Madiwani na watoto wao wana usaidizi wa baraza lakini wafanyakazi watembea kutoka mabandani mwao katika hali zote (jua au mvua).

b) Beka asema madiwani wala vizuri huku wanyonge waki-pigania makombo yaliyosazwa na wakubwa.

Meya aona maneno ya wawakilishi hawa kama kuliumbua baraza. Ajaribu kuwalaghai kuwa wangesubiri hadi wamalize kuwapokea wageni. Anawabainishia kuwa uongozi wake hautishiki kwa kelele na vitisho vyao, asema sharti pawe na mwelekezi na mwelekezwa.

Meya hatoi utatuzi wowote kwa matatizo ya wafanyakazi. Anawaambia wawakilishi kwamba hakuna pesa. Anawadanganya kuwa atawasilisha kauli zao kwa madiwani kisha ata-waita kuwapa kauli za madiwani.

Jaribio la Tatu la kuomba kushirikishwa katika kikao cha madi-wani linakataliwa na Meya akidai kuwa kanuni za barazahazi-ruhusu, na hata kama zingeruhusu, hawawezi kuwa na kikao na watu waliogoma. Meya ajaribu kutumia hila kuwafanya wawakilishi kufutilia mbali mgomo.

Kupitia Tatu, kuzinduka na kukamaa kwa wanyonge kunajitokeza anapomwambia Meya kuwa hawatafuata kauli yake. Mgomo utaendelea japo vyoo na majitaka yanawasubiri wafanyakazi kuyashughulikia. Tatu asema hili litasababisha kipindupindu. Meya astushwa na haya.

Tatu awashiria wenzake kuondoka. Meya anamwita lakini Tatu na wenzake wanageuka na kumtazama kisha kuondoka. Meya anaathirika na kubaki ameshika tama.

Masuala muhimu:

Mgogoro kati ya Meya na wafanyakazi haujatatuliwa.

Hali ngumu ya maisha ya wafanyakazi inajitokeza.

Onyesho ladhihirisha yafuatayo:

a) Ututetezi wa haki
   i) Tatu, Medi na Beka wamekuja kuonana na Meya wakilia haki za wafanyakazi.

b) Dhuluma
   i) Mishahara duni.
   ii) Kulipwa nusu mishahara.
   iii) Kutotolewa kwa nyongeza za wafanyikazi.
   iv) Ubaguzi kimatibabu - wafanyakazi walipie lakini ma-diwani wakose.

v) Mazingira duni ya kazi - hamna glavu.Wafanyakazi wanatakiwa kurudi kazini kabla ya malalamishi yao kutatuliwa.
vi) Watetezi wa wafanyakazi kutoruhusiwa karibu na kikao cha madiwani.

ONYESHO LA PILI
(Mandhari ni ofisini pa Meya.)

Mgogoro kati ya wafanyakazi na Meya umefika upeo wa juu.
Mgomo wa wafanyakazi umeahirisha shughuli za usafi na wageni wanatazamiwa kuja Cheneo. Hali hii imemtia Meya wasiwasi na anaitisha kikao na Diwani I naII.
Katika kikao, Meya analalamikia Diwani I na II kwamba mambo hayakwenda kama walivyotarajia. Mgomo wa wafanyakazi unaendelea licha ya Meya kujaribu kuwashawishi wawakilishi wao kuwataka wafanyakazi kurudi kazini.
Diwani I anadai kwamba wafanyakazi hawahitaji kubembelezwa, wao ni wajinga. Meya na Diwani II wasema kuwa matumizi ya nguvu yangesawiri picha mbaya katika jamii ya kimataifa. Jambo hili ni hatari kwa misaada wanayotarajia.
Matokeo ya kiburi cha Meya ni:

a) Uchafu na uvundo kuenea mjini.
   i) Diwani I apendekeza watumie vyombo vya habari na vipazasauti kutangazia ajira kwa vijana wasio na ajira. Meya kwa ukosefu wa busara anakubali na kusema jambo hili lifanywe mara moja. Diwani II apinga hili kwani tayari watu wana picha mbaya kuwahusu, hawataitikia wito katika mazingira haya, watadhani wanadanganywa.
   ii) Meya anazinduka na kuona kuwa madiwani walimdanganya, hawakumwambia ukweli. Diwani I anasema hawakumdanganya. Diwani II anasema kwamba walimshauri kadri ya uwezo wao. Inabainika kupitia maneno ya Diwani I kwamba walimwamini Bili sana. Bili sasa amewasaliti. Hajaonekana kwa siku mbili na hata wakimpigia

simu hapatikani. Meya ajuta kwa kutomsikiza Diwani III. Hapa athari za kusikiliza washauri potoshi na kupuuza washauri wenye hekima inajitokeza.

iii) Mgomo wa wafanyakazi wa uwanja wa ndege na wale wa bohari la mafuta ili kuwaunga wenzao mkono unasababisha wageni kutoweza kutua Cheneo. Wameelekezwa kutua mji jirani. Vile vile wage-ni wanahofia kipindupindu kwani hoteli hazina maji yanayoweza kufikia viwango vya kimataifa. Zinanunua maji kutoka mtoni.

iv) Meya na Diwani II wanahisi pana haja ya kutumia nguvu, anaamua kuwaamrisha askari kuyanyoosha mambo. Amtuma Gedi kuwaita askari. Hata hivyo mambo yanakuwa kinyume. Badala ya Meya kuwatolea amri, wao ndio wanaompa maagizo. Wanamwambia kuwa wametumwa kumwarifu kuhusu kuahirishwa kwa safari ya wageni. Vile vile wametu-mwa kumchukua Meya, Diwani I na II kwenda makao makuu kuzungumzia hali ya mambo.

Masuala muhimu:

Mapinduzi

i) Askari wanawakamata Diwani I na II na Meya kwenda kueleza kuhusu hali ya mambo.

ii) Badala ya Meya kutoa amri, askari ndio wanaomwamrisha.

Upiganiaji haki

i) Wafanyakazi wamegoma kupinga uongozi dhalimu.

Usaliti

i) Bili atoroka baada ya sakata ya wizi wa fimbo ya Meya.

DHAMIRA

Dhamira ni **kiini** au **lengo**.

Dhamira hujumuisha:

i. Funzo au maadili.
ii. Falsafa au mtazamo wa mwandishi kuhusu suala linalozungumziwa. Aweze kusifu (kutukuza) au kukashifu.

Dhamira ya tamthilia ni kufanyia tashtiti au kukashifu uongozi mbaya wa Meya wa Cheneo. Ni fisadi.

i) Analifisadi baraza kwa kuidhinisha kutotozwa kodi kwa madiwani.
ii) Kutumia fedha kwa burudani – entertainment vote.
iii) Kujinyakulia viwanja na vingine kumpa Bili.
iv) Kumzuia mwanakandarasi ili waliibie baraza.

Uongozi mbaya unahusisha, hila, propaganda na kuwategemea washauri – Diwani I na II na Bili wanaompotosha.

Neno ‘ Mstahiki Meya’ ni kinaya kwani mwandishi analiweka uozo wake wazi. Vile vile mwandishi anakejeli kutowajibika kwa viongozi hasa kuhusu masuala muhimu ya kibanadamu, kwa mfano:

i) Dawa hospitalini.
ii) Nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi.
iii) Ukosefu wa vyakula.
iv) Usafi wa kimazingira, na kadhalika.

Kwa hivyo wale wenye sifa hasi wapaswa kurekebisha.

MAUDHUI

UONGOZI MBAYA

Uongozi mbaya ni ule usiowajibikia mahitaji ya umma. Uongozi mbaya unaendelezwa na Meya, Diwani I na II na Bili. Uongozi wao unasababisha kuzorota kwa hali ya maisha mjini Cheneo.

Uongozi unadanganya umma eti shehena ya dawa imo njiani yaja. Jambo hili linaleta maafa kutokana na ukosefu wa dawa katika zahanati. Waridi asema wameambiwa wasubiri dawa.

Uongozi unawataka wagonjwa walipie kitanda zahanatini na ilhali hakuna dawa. Hii ni dhuluma kwa wagonjwa. Viongozi washinikiza kugawana gharama na raia wanyonge wasioweza kununua hata chakula.

Baada ya kuchaguliwa na raia, viongozi wanakataa kusikia vilio vyao. Siki anamkumbusha Meya kuwa watu walimchagua kwa imani kuwa ataboresha hali zao.
Viongozi wabaya hupuuza ushauri kutoka kwa washauri bora. Meya akataa ushauri wa daktari Siki kuhusu kupanda kwa gharama ya maisha na mishahara duni wafanyakazi.
Viongozi hawa huwatelekeza raia katika njaa na umaskini. Watu wanakufa kwa magonjwa. Kitoto kinafia hospitalini kwa kula chakula chenye vijisumu, utapiamlo na wengine kula mizizi na matunda mwitu.
Viongozi hawa hutumia ulaghai/udanganyifu kupata kura. Meya amwambia daktari Siki kuwa amechaguliwa mara tatu na hata akitaka ya nne, tano au sita atachaguliwa kwani ana akili, na akili ni mali. Meya awaambia wawakilishi wake kwamba atawaelezea madiwani malalamishi yao ilhali anajua hatafanya hivyo.
Viongozi wabaya hutumia mbinu hasi kutawala. Propaganda, vitisho na vishawishi kuwadhibiti raia, mfano, nyimbo za kiza-lendo, idhaa za utangazaji, vijana wavitembeze virungu na kuwaandalia hafla na mashindano ili kuwafanya kutulia.
Viongozi wabaya huendeleza wizi wa mali ya umma. Mfano, kujigawia viwanja na kuiba fimbo ya Meya, na kadhalika.
Viongozi hawa hufanya uteuzi mbaya wa washauri. Meya anateua washauri wa kumpotosha, mfano, Diwani I na II na Bili.
Viongozi wabaya huwanyanyasa wafanyakazi. Hawawalipi kwa wakati, kulipwa nusu mishahara, mazingira mabaya ya kazi, hamna glavu na dawa.
Viongozi wabaya huendeleza ubadhirifu wa mali ya umma. Mapokezi ya kifahari ya Mameya (mvinyo na divai), mke wa Meya kuzalia ng’ambo, Meya anamwalika Bili na familia yake katika hoteli ya kifahari. Asema ana entertainment vote.
Uongozi huu huchangia uharibifu wa mazingira. Viwango vya usafi vinazorota hivi kwamba wahofia kipindupindu na kua-hirisha safari.
Uongozi mbaya hutumia vyombo vya dola vibaya. Askari

wanatumia virungu kuwatawanya wafanyakazi wanaolala-mikia maslahi yao. Pia Meya anatumia mamlaka aliyopewa kisheria kukabiliana na migomo na wanaompinga (aweza kumchukulia mpinzani yeyote sheria).
Viongozi wa kidini wanaendeleza tamaa na unafiki. Mhubiri anaenda kumwombea Meya ili kusaidika kwa sadaka atakayo-pewa.

HARAKATI ZA UKOMBOZI

Wanyonge na watetezi wa haki wanatumia mbinu mbalimbali kuushinikiza uongozi wa Cheneo kushughulikia maslahi yao.

Mfano :

i) Siki amtaka Waridi kumlaza mtoto hospitalini japo hamna dawa ili kumpa mama mtoto matumaini.
ii) Siki anakashifu hali ya wagonjwa kuhitajika kulipia kitanda bila dawa.
iii) Siki anakwenda kwa Meya kupigania haki za raia.
iv) Diwani III anapigania haki za wanyonge. Anasisitiza kubuniwa kwa mpango wa kuwanufaisha watu kwa mahitaji, kama vile ajira na mishahara bora.
v) Diwani III anapinga uundaji wa kamati za madiwani, anaziona kuwa zisizo na umuhimu kwa baraza.
vi) Diwani III anapinga wazo la kutowatoza kodi madiwa-ni.

UONGOZI BORA

Uongozi bora unadhihirika kupitia kwa mhusika Siki kwa kuwa anampa Waridi maelekezo ya kumsaidia mtoto mgonjwa hos-pitalini. Vile vile, anawakubalia wagonjwa hospitalini bila malipo ili kuwapa matumaini.
Vile vile, Siki anamkashifu Meya kwa kudanganya kwamba dawa zimeagizwa ilhali ni uongo.
Anamkumbusha Meya kuhusu wajibu wake wa kuyaboresha maisha ya waliomchagua. Amshauri Meya kuhusu umuhimu wa kujitahidi kujiendeleza zaidi badala ya kujilinganisha na majirani dhaifu. Asema kuwa Cheneo inarudi nyuma badala ya kuendelea.
Viongozi bora hutoa ushauri bora bali sio kupotosha. Siki am-shauri Tatu kuhusu masuala ya mgomo.

Viongozi bora hawakati tamaa, mfano, hata hali inapokuwa mbaya zahanatini, Siki hajiuzulu bali anasema kuwa ni afadha-li kuteseka na wagonjwa ili kuwapa matumaini.
Pia uongozi bora unadhihirika kupitia Diwani III ambaye ana-pinga njama za Meya, Diwani I na II za kuinua kiwango cha uzalendo kupitia kwa propaganda. Anasema kwamba haoni lolote la kuwanufaisha wanyonge.
Anapinga pendekezo la uundaji wa kamati za madiwani kwa kusema kwamba huenda zisiwe na umuhimu kwa baraza.
Vile vile, anapinga sera dhalimu kwa nyongeza ya mishahara kwa walinda usalama ya madiwani na kutotozwa kodi. Asema kuwa baraza halina uwezo wa kumudu nyongeza hizi na kuwa kutolipa kodi kutapunguza pato la baraza.
Viongozi bora hupigania haki za wanyonge. Diwani III ana-mwambia Meya, Diwani I na wa II kwamba wangojee kuima-rika kwa uchumi ili nyongeza ya mishahara ifikishwe hata kwa wanyonge.
Tatu, Beka na Medi ni viongozi bora kwa kuwa wanapigania haki za wafanyakazi kwa hali na mali. Hawa wana ari ya kuona kuwa wafanyakazi wamepata nyongeza ya mishahara na ma-zingira bora ya kazi.

USALITI

Usaliti ni kufanya kinyume na imani na matarajio ya mtu, jamii, falsafa, na kadhalika.
Uongozi wa baraza unaisaliti imani ya wanyonge na wafanya-kazi wa hospitalini kwa kuwadanganya kuwa dawa zimeagi-zwa ilhali hazijaagizwa.
Meya anausaliti undugu na Siki kwa kumfukuza nyumbani kwake na kutosikiliza malalamishi yake kuhusu hali duni ya wafanyakazi.
Diwani I na II wanasaliti wadhifa wao wa kumshauri Meya kwa kukubaliana na maamuzi yake mabaya badala ya kumkanya.
Meya anayasaliti mamlaka yake kwa kupuuza malengo ya mji katika mpango wa maendeleo ya miaka kumi- afya bora na ya bure akisema mipango ya miaka kumi ni upuuzi,

jambo amba-lo linasababisha kutekelezwa kwa shughuli za kudumisha afya ya umma.
Meya na washauri wanaisaliti imani ya raia waliowachagua kwa kutobuni mikakati ya kuboresha hali za raia hao. Hata watu wanapomlilia Meya hasikilizi.
Uongozi wa baraza unasaliti umma kwa kushindwa kuhakikishia raia usalama wa chakula. Siki anasema kwamba watu wanakufa kwa kula mizizi na matunda mwitu.
Washauri wa Meya wanachukulia jukumu hilo ni kulitetea baraza badala ya kuwatetea wanyonge. Diwani III anamwonya Diwani I na II kwamba hawakuchaguliwa kumfurahisha Meya kwa kuwapiga vita waliowachagua kuwa madiwani.
Meya analisaliti baraza kwa kulifisadi hazina yake. Anataka mwanakandarasi kulishtaki baraza afidiwe naye Meya amege-we sehemu yake.
Nchi inawasaliti wasomi kwa kutobuni nafasi za kazi. Wanao-hitimu masomo ya chuo kikuu hawapati kazi. Meya anasema kuwa kuna vijana wengi waliohitimu chuo kikuu na hawana kazi hata ya utopasi.
Meya, Diwani I na II wanamsaliti Diwani III kwa kutomhusisha katika maamuzi ya nyongeza ya mishahara ya madiwani, uu-zaji wa fimbo ya Meya na kuidhinisha malipo ya ovataimu ya Diwani II, marupurupu ya Bili na kwamba Diwani III ndiye anayehusika na masuala ya fedha.

- Meya anausaliti wadhifa wake wa umeya kwa kuidhinisha kuuzwa kwa fimbo ya Meya ambayo ndiyo sasa kitambulisho cha umeya. Vile vile kumruhusu Bili kumwendeshea shughuli za baraza na hali Bili sio mfanyakazi wa baraza.
- Ni kutokana na usaliti wake wafanyakazi wanagoma kwa sababu ya hali yao duni katika kufanya kazi. Pato la baraza linapungua kwa kutokusanya kodi. Ziara ya wageni inaahiri-shwa kwa sababu ya viwango vya chini vya usafi.
- Bili anamsaliti Meya, Diwani I na II kwa kutoroka baada ya kuuza fimbo ya Meya ng’ambo.
- Mhubiri anausaliti wajibu wake wa kidini kwa kumsifu Meya badala ya kumkosoa. Anamwombea kwa kuwa atapata sadaka.

Katiba inatumiwa kuwakandamiza raia badala ya kuwatetea. Meya ana nguvu nyingi kikatiba zinazompa mamlaka maku-bwa kuwanyamazisha wapinzani. Vile vile Diwani II asema kwamba kuna kifungu kinachosisitiza uwajibikaji wapamoja, kitumiwe kumshinikiza kila mtu kukabiliana na maamuzi ya meya, Diwani I na II hata kama jambo linalopitishwa halina umuhimu wowote.

DHULUMA

Dhuluma ni hali ya kunyima haki, kuonea, kunyanyasa au hata kutesa.

- Wanyonge wananyimwa huduma bora za kimatibabu. Zahanati haina dawa ila tu za kudhibiti uchungu. Vile vile hakuna karatasi hata za udodosi. Wagonjwa wanatarajiwa kununua.
- Wanyonge wanahitajika kulipia gharama za matibabu licha ya kuwa hawana mapato mazuri. Wanatakiwa kulipia vitanda ilhali hakuna dawa.
- Serikali imewatelekeza wanyonge katika njaa na umas-kini. Wanakula chakula duni, mtoto anaugua utapiamlo na Siki anasema kwamba watu wanakufa kwa kula mizizi na matunda mwitu.
- Viongozi wanawasaliti raia waliowachagua kwa kutozi-boresha hali zao na huku gharama ya maisha inazidi kupanda.
- Wapiganiaji haki wanazuiwa kulalamikia haki zao kwa Meya. Meya anamfukuza Siki kwake. Anamwambia Gedi kuwa ahakikishe kwamba Siki haingii kwake tena. Tena anasema shajara yake imejaa, hakutani na wafanyakazi.
- Viongozi wanakosa kushughulikia usafi wa mji. Harufu ya taka kutoka barabarani inayafanya maji yaliyo kwenye chupa kutonyweka.
- Wafanyakazi wanapewa mishahara duni, wakati mwingi-ne nusu na inayocheleweshwa. Waridi asema kwamba msha-hara wa mwezi uliopita wamelipwa nusu. Pia Tatu analalami-ka malimbikizo ya mishahara. Anasema kuwa malipo yao ya mishahara sasa yako nyumamiezi mitatu.

- Wafanyakazi wanadhulumiwa kwa kufanya kazi katika mazingira duni. Medi anasema kuwa wanaosha vyoo bila glavu.
- Wafanyakazi hawapati nyongeza ya mishahara. Madiwani wanaongezwa. Jambo hili laonyesha ubaguzi unaowapendelea madiwani. Wafanyakazi wanadhulumiwa vile vile, wanakabiliwa kikatili na askari wanapogoma kudai haki zao (vitoa machozi vinatumiwa).
- Wafanyakazi wa nyumbani wanatukanwa na kudhalilishwa. Dida asema kazi ya askari ni bora kuliko ya wafanyakazi wa nyumbani wanaotusiwa na kudhalilishwa na Bwana.
- Diwani III anadhulumiwa kwa kunyimwa nafasi ya kushi-riki katika maamuzi yanayohusu matumizi ya fedha licha ya kwamba ndiye anayehusika na masuala ya fedha, mfano, nyo-ngeza ya madiwani.
- Wanyonge wanaonewa kwa kubaguliwa kimatibabu. Madiwani wana bima ya matibabu lakini wanyonge walipie ilhali hakuna dawa.
- Vitisho vinavyotolewa kwa wafanyakazi ni kuwadhulumu. Watafutwa wakigoma.
- Nia ya Meya ya kuchukua mikopo ni dhuluma kwa vizazi vijavyo kwani vitaachiwa mzigo wa kulipa mikopo wasiyoele-wa.
- Meya anataka wafanyakazi kurudi kazini kabla ya malala-mishi kushughulikiwa. Atumia ujanja eti madiwani hawawezi kuzungumza na watu waliogoma. Kwa hivyo ataka kuwashi-nikiza Medi, Tatu na Beka kufutilia mgomo.

UFISADI

- Meya anatumia pesa za umma kumpeleka mkewe kuzalia ng’ambo pamoja na kumstarehesha Bili na familia yake.
- Meya anajigawia ardhi ya umma kwa njia isiyo halali. Vile vile anamgawia Bili vipande vinne vya ardhi ya umma.
- Meya amshauri mwanakandarasi kulishtaki baraza ili apewe fidia kisha ammegee Meya kiasi fulani cha fidia ile.
- Meya anatumia hazina ya baraza kumlipa mhubiri ghara-ma ya usafiri na kumlipa sadaka ya laki moja kila mwezi.

- Uongozi wa zahanati unaendeleza ufisadi kwa kuwaibia wagonjwa. Wanalipa ilhali hakuna dawa.
- Meya, Diwani I naII wanapanga njama za kunufaika ku-tokana na hazina ya baraza. Wanabuni kamati za madiwani ili kupata upenyu wa kuendelea kulifisadi baraza huku wakiu-ngana mkono na madiwani.
- Vile vile Meya asema kuwa ‘Entertainment vote’ bado inawasubiri. Atumia pesa za umma kujistarehesha ilhali umma unateseka.

ULAGHAI/UNAFIKI/UDANGANYIFU

Ulaghai ni njia ya kutumia ujanja au uongo kupata una-chotaka. Unafiki ni kujifanya umwema ilhali u mwovu.

- Meya adanganya kuwa shehena ya dawa imeagizwa na hali si kweli. Unafiki huu unakusudiwa kuwapumbaza watu waone kuwa baraza linawajibika.
- Meya alitumia udanganyifu ili kuchaguliwa. Anamwa-mbia siki hata yeye akitaka kuchaguliwa mara nne, tano na sita, watu watamchagua tu kwani yeye ana akili.
- Meya anatumia nyimbo za kizalendo kama ujanja wa kurudisha nyoyo za raia na kuwasahaulisha dhuluma anazo-wafanyia.
- Diwani II (Bwana Uhusiano Mwema) awaambia watu uwongo kuwa vijana hawatatumia nguvu(kupiga raia) ilhali hilo ndilo lililokuwa kusudi la meya, Diwani I na II; si kwamba wanajali watu.
- Diwani I ananuia kutangazia watu kuhusu kujitolea kwa baraza la Cheneo kuleta demokrasia na hasa uhuru wa kujie-leza. Huu ni unafiki ili kuwapoza raia.
- Vilevile anampendekeza Diwani II kuandaa tamasha ya vijana kushindania zawadi kwa kubuni na kucheza nyimbo. Hili ni hila inayonuiwa kuwafanya vijana kuhisi kuwa wanathami-niwa kwa kutunukiwa zawadi na kuonyeshwa kwenye vyombo vya habari, lengo ni kuwapumbaza wasitambue dhuluma wanazotendewa. Lengo ni kuibua hisia za kizalendo miongoni mwao.
- Uundaji wa kamati za madiwani ni hatua ya kinafiki ya kuwateka akili madiwani wengi wamuunge mkono Meya na washauri wake.

- Kuteuliwa kwa madiwani wenye ushawishi mkubwakuo-ngoza kamati ni hila ya kuhakikisha kuwa kamati zimedhibi-tiwa kulingana na maslahi ya Meya na kufanya upinzani kupu-ngua.
- Bili amshauri Meya kutumia ulaghai kupata pesa kutoka kwa mwanakandarasi, alishtaki baraza limlipe fidia na kisha mwanakandarasi ammegee fidia ile. Amwambia meya asimsa-hau baada ya wizi huu.
- Kinafiki Meya anajifanya mpole na mcha Mungu mbele ya mhubiri ili washirikiane naye. Kinafiki mhubiri ashirikiana na Meya ili kupata sadaka na pesa za petroli. Meya kwa unafi-ki asema karibu aache kazi aende kushirikiana na mhubiri.
- Bili anawambia Meya, Diwani I na II kuwa kuwapiga watu kunaweza kusawiri picha mbaya kwa wageni. Ni vyema wa-wape sifa nzuri, ndio umuhimu wa kuuma na kuvizia. Huu ni unafiki, kutoa picha nzuri nje na huku ndani ni uozo.
- Bili anapendekeza njia ya ulaghai ya kuiba fimbo ya Meya kisha itangazwe iliibiwa wakati wa ghasia na uchunguzi umea-nzishwa. Hatimaye Bili anatoweka na fimbo.
- Meya awadanganya wawakilishi wa wafanyakazi kuwa atawasilisha malalamishi yao katika Baraza la Mawaziri. Huu ni uongo. Kwa hila anawaambia kuwa hawawezi kukutana na watu waliogoma ili warudi kazini.

UKOLONI MAMBOLEO

- Ukoloni mamboleo ni hali ambayo ingawa ukoloni ume-shaondoka, bado mzungu anazidhibiti nchi huru kwa njia nyi-ngine. Mfano, kupitia kwa elimu, mifumo ya kisiasa kiuchumi, na kadhalika.
- Katika tamthilia, maamuzi muhimu yanatolewa na mzu-ngu. Waridi anamwambia Siki kuwa wazungu wanahimiza mfumo wa kugawana gharama.

- Mahusiano ya waajiri na wafanyakazi ni ya ukoloni. Meya anawaamrisha Gedi na Dida, Meya aitikwa ‘Yes sir’. Dida ana-lalamika kwamba bwana anawadhalilisha.
- Viongozi wanaendeleza unyonyaji ule ule wa wakoloni. Mfano, wafanyakazi wanalipwa mishahara duni huku madiwani wakiendelea kuongezwa mishahara. Wafanyikazi ndio wanaozalisha mali ilhali hawanufaiki.
- Mwongozo wa mipango ya kimaendeleo unatolewa na mataifa yenye uwezo mkubwa. Meya anapuuza maendeleo ya miaka kumi na kuthamini malengo ya kimaendeleo ya milenia. Asema wameingia kiwango cha kimataifa.
- Mataifa yenye nguvu yatawala mataifa machanga kupitia mikopo. Vilevile mataifa haya yanapendekezwa kupunguzwa kwa wafanyakazi. Meya asema mataifa hayajatoa mikopo kwa hivyo hawawezi kuongezwa mishahara.
- Bidhaa kutoka nchi za kikoloni zinachukuliwa kuwa bora. Meya asema ataagiza mvinyo kutoka Urusi na divai kutoka Ufaransa kupapia ya kigeni na kupuuza ya Kiafrika ni ukoloni mamboleo.
- Elimu ya Mwafrika inachukuliwa kuwa duni na ndiyo sababu meya anawapeleka watoto wake kusoma ng’ambo. Asema elimu ya hapa ni kawaida mno.
- Vilevile utabibu wa kigeni unachukuliwa bora kuliko wa Cheneo. Mkewe Meya ameenda kujifungulia ng’ambo. Meya adai ng’ambo ndiko kwenye wakunga hasa, kwamba madak-tari wa hapa ni wa kubabisha tu.
- Meya anathamini uraia wa ng’ambo. Mfano, asema kuwa mtoto wake akizaliwa huko atapata uraia huko huko.
- Kuwepo kwa vikaragosi wanaoendeleza maslahi ya viongozi. Gedi, Diwani I na II ni vikaragosi wa Meya. Wakoloni walitumia vikaragosi ili kufanikisha utawala wao.

TAMAA NA UBINAFSI

Tamaa ni husuda au hamu kubwa na ubinafsi ni hali ya kujipendelea.

- Meya ana tamaa ya uongozi. Anawaambia Diwani I na II kwamba hataki kusikia mtu amekufa asije akapata tatizo wa-kati wa uchaguzi. Hii ndio sababu anaunda kamati za

madi-wani ili aungwe mkono katika utawala wake. Vilevile hawatozi kodi na kuwapa nyongeza ili naye afaidike.

- Meya ananyakua mali ya umma kujipa yeye na rafikiye Bili. Meya anajinyakulia viwanja vinane na kumpa Bili vinne.
- Tamaa ya pesa inamfanya kukatiza kandarasi kabla yaku-isha kwa mkataba na kutoa kandarasi kwa mtu mwingine kwa masharti yake, akilishtaki baraza alipwe fidia ili naye apate sehemu yake.
- Bili ana tamaa kwa kuwa anamwambia meya kuwa baa-da ya fidia asimsahau. Vilevile anapendekeza kuuzwa kwa fimbo ya Meya ili naye anufaike.
- Mhubiri anakwenda kumwombea Meya na kujifanya kufurahishwa na hulka ya Meya ya kutafuta upendo wa Mungu ili kufaidika. Hatimaye anapata sadaka na pesa za petroli.
- Meya na washauri wake wanajihudumu badala ya kuwa-hudumia raia. Badala ya kusikiliza malalamishi ya wafanyakazi na kuyakubali, wao wanapanga mbinu za kuinua uzalendo ili waendelee kutawala na kunufaika.
- Meya anapanga mapokezi ya kifahari kwa mameya kwa lengo la kuwafurahisha ili watoe mikopo.
- Ni kutokana na tamaa ya kulipwa ovataimu na marupu-rupu ambapo Bili na Diwani II wanapanga kuiba fimbo ya meya ili waiuze ng’ambo.
- Madiwani wana tamaa na ubinafsi mkubwa kwani wana-jipatia nyongeza ya mishahara, kutotozwa kodi na wamejipa bima ya matibabu, na huku raia wanalipa katika zahanati isiyo dawa. Mkewe Meya anaenda kujifungulia ng’ambo.
- Tamaa na ubinafsi wa Meya unamfanya kutosikiliza mao-nyo ya Diwani III kuhusu nyongeza ya mishahara kwa madi-wani na ushauri wa Daktari Siki kuhusu dhiki wanazozipitia raia. Anamwona Diwani III kama anayehujumu uongozi wake.

UWAJIBIKAJI

Hii ni hali ya kutenda linalompasa mtu.

- Siki anaonyesha kuwajibika kwa kumwambia waridi awashughulikie wagonjwa ingawa dawa zilikuwa hazipo. Waambiwa wasubiri. Siki asema kuwa ni heri wafe kwa ugonjwa si ukosefu wa matumaini.
- Siki amwambia Waridi amwandalie mtoto mchanganyiko wa sukari na chumvi katika maji ili mtoto asaidike. Ni wajibu wake kushughulikia wagonjwa.
- Vilevile Siki anaona ni wajibu wake kuenda kumwona Meya kuhusu ukosefu wa dawa katika hospitali pamoja na ku-panda kwa gharama ya maisha. Hivyo wanyonge hawawezi kumudu kulipia matibabu.
- Kama jamaa yake Meya, Siki anaona ni wajibu wake ku-mkosoa meya kuhusu uongozi wake hasa kutosikiliza waliom-chagua. Hii ndio sababu alimshauri Meya kuwa haifai kupima ubora wa baraza kwa kigezo cha ubora wa majirani. Muhimu ni kupiga hatua mbele.
- Vilevile amwonya Meya dhidi ya kukubali waliyoamua watu wengine (adiwani) pasipo kushirikisha raia. Haya yana-husu sera ya kugawana gharama katika kupata huduma za kimatibabu.
- Diwani III anawajibika kwani anasisitiza kuwa lazima ku-we na mpango wa kuwanufaisha raia na kuwa uzalendo hauji kwa watu kuimbiwa nyimbo lakini kwa kutafuta suluhisho la ukosefu wa ajira, kushughulikia mishahara duni na kulipwa kwa wakati.
- Vilevile aona ni wajibu wakekupinga ubinafsi wa madi-wanikutotozwa kodi, nyongeza ya mishahara kwa madiwani, marupurupu ya walinda usalama, na kadhalika. Asema baraza lina deni la millioni mia moja na ishirini.
- Vilevile Siki anawajibikakumweleza Tatu kuhusu athari za mgomo. Anamshauri kumshinikiza Meya kukutana na Tatu na wawakilishi wengine wa wafanyakazi.
- Tatu, Beka na Medi wanawajibika kama viongozi wa wa-fanyakazi kwa kuwa wanaendea Meya kutoa malalamishi ya wafanyakazi. Pia wanatambua ulaghai wa Meya wa kutaka wafutilie mbali mgomo.
- Gedi anawajibika kama mpambe wa Meya kwa kuwa anatumikia kwa uaminifu na heshima. Anaposikia kelele za

maombi ofisini mwa Meya anadhani anashambuliwa, kuingia huku akiamrisha kila mmoja kulala chini.

- Makao makuu yanawajibika kwa kuwa yanamshika Meya, Diwani I na II kwa kueleza kiini cha mambo kuwa jinsi yalivyo katika mji wa Cheneo.

K.C.S.E 2013.

Jadili mchango wa Wanacheneo katika kuivunja jamii yao.(alama 20)

i) Baadhi ya viongozi wamekosa kuwajibika, kwa mfano, Meya, mhubiri na kadhalika.
ii) Wananchi hawaungani katika kupinga viongozi dhalimu, mfano, Diwani I na II.
iii) Meya anawapuuza raia – kuporomoka kwa uongozi wake.

UKOSEFU WA UWAJIBIKAJI/MAPUUZA

Baraza lina mapuuza na kutowajibika kwa usimamizi (usiofaa) wa zahanati. Wanadanganya kuwa dawa zimeagizwa na hali hazijaagizwa. Jambo hili linasababisha vifo hasa vya watoto.

- Badala ya Meya kubuni mikakati ya kukabiliana na hali duni ya kiuchumi, adai kwamba hakuna baraza lenye udhabiti kama la Cheneo. Asema Cheneo kisiwa cha kupigiwa mfano (kinaya).
- Meya kutowajibika kwake anapuuza onyo la Siki kuwa ni hatari kuongoza watu wenye njaa na kiu. Anasema kuwa watu hao ndio waliomchagua tena kwani ana akili. Mapuuza haya hatimaye yasababisha kuporomoka kwa uongozi wake.
- Meya anapuuza malengo ya mji katika mpango wa mae-ndeleo wa miaka kumi kwa kudai kuwa wana malengo ya ki-maendeleo ya milenia. Upuuzaji huu unamfanya kutozingatia afya ya raia ambayo ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi ya raia na vifo vinatokea.
- Diwani I na II wamekosa kuwajibika kama washauri wa Meya. Badala ya kumkosoa wanampotosha. Wanakubaliana kuwepo na nyongeza ya marupurupu na mishahara ya walinda usalama, kutotozwa kodi kwa madiwani. Hawazii kuwa baraza haliwezi kutoa malipo haya kwani tayari lina nakisi.

- Meya anakosa uwajibikaji anapounda kamati za madiwa-ni bila kuwazia gharama yake. Alijua kuwa Baraza halihitaji kamati hizi, ila akaziunda ili kujifaidi.
- Meya hawajibiki kwa kumwachia Bili amwendeshee shu-ghuli za uongozi, mfano, kulifisidi baraza kwa kufidia kanda-rasi, kuuza fimbo ya Meya na ndiyo kitambulisho cha umeya.
- Pia kupitia unafiki na ulaghai, Meya anazorotesha utoaji wa huduma za afya na kisha atumia pesa za umma kumpeleka mkewe akazalie ng'ambo na watoto wake wakasomee mle.
- Kutokana na ubadhirifu wake, Meya aamua kutumia pesa za baraza kumnunulia mhubiri petroli ili kuja kuliombea bara-za na kumpatia sadaka ya laki moja kila mwezi ili azidi kumwo-mbea Meya. Anaagiza divai na mvinyo kutoka ng'ambo.
- Raia wanakosa kuwajibika kwa kuwachagua viongozi wabaya. Meya asema akitaka kuchaguliwa mara nne, tano ama sita bado atachaguliwa. Vile vile wanataaluma hawataki kujiingiza katika siasa kwa kuwa wanaogopa kuchafuliwa. Hivyo hawawezi kuiupinga uongozi.
- Viongozi wameshindwa kuwajibikia usafi wa mji. Baraba-ra zimejaa taka na uvundo kuhanikiza kote. Ingawaje nyumba ya Meya inanadhifishwa na Dida, mtumishi wa nyumbani.
- Vile vile Meya anakataa kuwajibikia kosa lake. Anapoa-mbiwa na askari II kwamba yeye na washauri wake wanahi-tajika makao makuu kuelezea hali ya mambo anadai kuwa yote hayo yametiwa chumvi na wanahabari, kwamba si kweli inavyodaiwa.

MAUDHUI MENGINE

1. **Juhudi za kupigania haki**
   a) Siki
   b) Diwani III
   c) Tatu,Beka,Medi
   d) Mwanakandarasi
   e) Wafanyakazi- migomo
2. **Umaskini/hali duni ya kiuchumi**

a) Zahanati haina dawa
b) Dhiki ya njaa – utapiamlo/vijisumu/mizizi na matunda mwitu
c) Zahanati haina karatasi za udodosi
d) Mazingira duni ya kazi – hawana glavu
e) Hoteli hazina maji
f) Baraza lina nakisi
g) Mgomo wa wafanyakazi
h) Malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi

WAHUSIKA

MEYA (Meya wa baraza la Mji wa Cheneo)

-Mwenye majivuno - Anamwambia Siki kuwa hakuna baraza lenyeufanisi kama la Cheneo. Vile vile anaona kuwa watu wa-tamchagua hata mara sita na wagombana na Siki kwa kuto-mwita ‘Mstahiki Meya.’

-Mwenye tamaa -Aidhinisha nyongeza ya mishahara ya ma-diwani naye anufaike. Anakubaliana na njama ya kuiba fimbo ya Meya, amejinyakulia viwanja vinane vya umma, na kadha-lika.

-Mwongo -Asema wameagiza dawa ilhali ni uongo kwa hivyo watu wanazidi kuumia kwa ugonjwa.

-Mwenye mapuuza -Anapoambiwa na Siki kuwa kitoto kime-mfia mkononi kwa ugonjwa , anasema kuwa huyo ni mmoja tu, kwamba Cheneo ina watu wengi na kwamba anaungwa mkono na wengi.

-Mbishi - Anabishana na daktari Siki anapomwambia kuwa watu wengi wanakufa kwa njaa kwa kutoweza kumudu kwa mahitaji ya kimsingi.

-Mpenda kunung’unika -Ananung’unika mambo madogo madogo kama vile udogo wa mayai aliyoletewa huku akisema anapunjwa. Pia anapokabwa na yai na chai analalamika kuwa ni hujuma ya mfanyakazi wake Dida.

-Mwenye mtazamo finyu - anapuuza mpango wa miaka kumi akitumainia malengo ya kimelenia yaliyopangwa na wageni. Pia ataka mikopo ya kulipia mishahara ya madiwani badala ya kuanzisha miradi ya kukuza uchumi.

Hataki kufahamu kuwa anadhulumu vizazi vijavyo.
-Ni fisadi - Ajinyakulia viwanja vinane, alimpa Bili vinne na anatumia pesa (Entertainment vote) kujistarehesha na rafi-kiye Bili. Pia anataka mwanakandarasi alishtaki baraza limlipe fidia naye apate sehemu yake kutoka kwa mwanakandarasi. Anahusika katika njama ya kuuzwa kwa fimbo ya Meya ng'a-mbo.
-Mjinga - Amepofuka kiasi cha kutotambua kuwa washauri wake wanampotosha, haoni unafiki wa Bili wala hawazii ku-husu hasara za mgomo.
-Mbadhirifu - Anatumia pesa za umma ovyo, mfano, kujista-rehesha katika hoteli za kifahari, kuidhinisha malipo yasiyo na halali (ovataimu na marupurupu ya ushauri), mkewe kwenda kuzalia ng'ambo, utoaji wa sadaka na pesa za petroli kwa mhubiri.
-Mwenye ulafi - Ameandikwa vyakula vingi mezani na ana-bwakia yai kwa ulafi linamchoma. Vile vile analafia chai kisha anamlaumu mtumishi kuwa na njama.
-Msaliti - Haoni tatizo kuwa mtoto mmoja amekufa. Anawa-cheka wafanyakazi wanapotawanywa na askari na hajali kuwa wafanyakazi wanapitia hali ngumu ya maisha.
-Kiongozi wa kiimla(dikteta) - Anatawala kwa mabavu na hatoi nafasi kwa yeyote kutoa maoni yake (daktari Siki na Diwani III). Anatoa amri ya nyongeza ya mishahara kwa madi-wani na kuwagombeza wafanyakazi, Dida,Gedi na Askari.
-Mwenye vitisho - Atishia kuwafuta kazi wafanyakazi wana-ogoma na Diwani III atishiwa kuwa hawezi kufanya atakayo angojawe Meya.
-Mnafiki - Mbele ya mhubiri anajifanya mcha Mungu na ajifa-nya mpole na mnyenyekevu na anayehitaji maombi, asema aona kama ataacha umeya akafanye kazi ya Bwana. Kwa una-fiki anawataka viongozi wa wafanyakazi kufutilia mgomo.
-Mbaguzi - Awaongezea madiwani mishahara na kuwahini wafanyakazi. Madiwani wana bima za matibabu na huku wa-fanyakazi wanalipa zahanati isiyo na dawa.

UMUHIMU WA MEYA

- Ni mfano wa viongozi wanotumia madaraka yao vibaya ili kujinufaisha, kuwanufaisha marafiki (Bili) na wanaowaunga mkono (Diwani I na II).
- Ni mfano wa viongozi wanaoendeleza ubaguzi katika jamii wanazoongoza. Vile vile anaonyesha ujinga.
- Meya ni mfano wa viongozi katili, fisadi na wa kidikteta ambao hutumia vitisho kuwakomesha wapinzani. Hutumia ufisadi kuungwa mkono.
- Aonyesha unafiki wa kidini miongoni mwa watu ili kuufi-cha uovu wao.
- Ametumiwa kudhihirsha ukweli wa methali “Kikulacho ki nguoni mwako” kwa kuwa alimwamini Bili hata kumkubalia kuiuza fimbo ya Meya, hatimaye akamtoroka na kumzimia simu.
- Ametumiwa kuonyesha viongozi wa Afrika walio na ma-baki ya ukoloni. Hawa wanaendeleza ukuloni mamboleo. Mfano anavyomwamrisha Gedi na Dida ni jinsi ambavyo mzungu alimwamrisha Mwafrika.

DAKTARI SIKI

-Ana uwajibikaji - Anauliza hali ya wagonjwa na kuwapa ma-tumaini hata ingawa hamna dawa zahanatini. Anakutana na Meya kumwambia kuwa wagonjwa hawamudu kulipia mati-babu na anamwelekeza Waridi kumfanyia mtoto mwenye utapiamlo huduma za kwanza. Haachi kazi ya udaktari licha ya mazingira magumu.

-Mtetezi wa haki - Ameenda kwa Meya kutetea hali duni ya wagonjwa. Ameenda kuwatetea wafanyakazi na anataka wa-gonjwa walazwe hata kama hawana pesa, kwa hivyo ni mwe-nye utu.

-Mshauri mwema - Anamshauri Meya kushughulikia matatizo ya wanacheneo. Mishahara kuchelewa, duni na mazingira duni ya kazi. Anamshauri na kumtahadharisha Tatu kuhusu madhara ya mgomo. Amshauri Waridi asiache kazi licha ya mazingira duni na kadhalika.

-Mvumilivu/Mstahimilivu/Mwenye subira -Anavumilia kazi-ni licha ya mazingira duni na kuchelewa kwa

mishahara na ka-dhalika.
-Mzalendo thabiti -Hakubaliani na yanayoamuliwa na nchi zingine, mfano, kugawana gharama na mipango ya kimae-ndeleo ya kimelania badala ya mipango ya maendeleo ya miaka kumi. Hakuyumbishwa na uhusiano wake na kindugu na Meya bali na maslahi ya Cheneo mzima.
-Mwadilifu - Ingawa wana uhusiano wa Kinasaba na Meya, hatumii undugu huo kuuficha uovu wa Meya. Badala yake anamkosoa na kumkumbusha wajibu wake kwa raia waliom-chagua. Vile vile hataki kujiingiza katika siasa kwani anaziona kama mchezo mchafu.
-Mwenye mawazo mapevu - Anamwambia Meya kuwa haifai wao kujilinganisha na majirani dhaifu lakini ipo haja ya wao kupiga hatua mpya.
UMUHIMU WA DAKTARI SIKI

- Ni kielelezo cha maafisa wa umma ambao ni waadilifu, hashirikiani na Meya katika uozo bali anamwonya dhidi ya kuwasaliti raia waliomchagua.
- Ni mfano wa raia ambao wako tayari kuwakosoa viongo-zi wabaya. Amwambia Meya kuwa mambo hayajanyooka, ya-namngojea yeye Meya na wenzake kuyanyoosha.
- Siki anatuonyesha ukosefu wa uwajibikaji wa viongozi wa umma. Haya yanatokea na ubinafsi wa viongozi.
- Kupitia kwake tunaona uadilifu wa baraza la viongozi, kwa mfano, Diwani III. Anamwambia Waridi kuwa ingekuwa Bw. Uchumi na Kazi aliyekuwa amesema dawa zimeagizwa angeamini.
- Kupitia kwake hali duni ya hospitali za umma imesawi-riwa. Hamna dawa na karatasi za udodosi. Kitoto kidogo ki-nafia mikononi mwake.
- Kielelezo cha wanamageuzi wanaotambua kuwa ili kule-ta mageuzi na maendeleo, urafiki na undugu unafaa kuekwa kando katika uongozi.

DIWANI III (BW. UCHUMI NA KAZI)
(Anahusiana na masuala ya fedha)

-Mkweli -Anamwambia Meya, Diwani I na II kuwa haoni mi-pango ya kuwanufaisha watu, kwani watu wengi hawana aji-ra.
-Mtetezi wa haki -Asema kuwa madiwani hawakuchaguliwa kumfurahisha Meya, wanahitaji kuwafaa na kuwaletea watu mafanikio. Vile vile wanapaswa kusikiliza vilio vya watu. Ana-pinga nyongeza ya mishahara kwa madiwani.
-Ni jasiri -Anapinga maamuzi ya Meya, Diwani I na II ya kue-neza propaganda kwamba baraza linaloendeleza demokrasia na uhuru wa kujieleza ilhali watu wanapigwa.
-Mwenye kuwajibika -Anakashifu kitendo cha viongozi kuwa-danganya watu kuwa dawa zimeagizwa. Anapinga nyongeza ya mishahara ya madiwani na kutotozwa kodi.
-Mng'amuzi wa mambo -Anatambua kuwa kuwapa watu a-hadi wasioweza kutimiza ni kuchochea ari yao ya kutaka ku-jieleza
-Mwadilifu -Anakataa kushiriki katika njama ya Meya na ma-diwani wenzake kulifisidi baraza. Anapinga uundaji wa kamati za madiwani kwani ni za kuendeleza ubadhirifu.
-Amepevuka kimawazo -Amfananisha Meya na mtoto amba-ye japo alikuwa na njaa awali akishashiba chakula hukipiga teke bila kujali wanaokihitaji. Meya amelewa na uongozi na cheo na kusahau alipokuwa hapo awali.
-Mnyenyekevu - Atoa kauli kuwa japo walichaguliwa na raia, si kwamba wao ndio bora kuliko wengine wasiochaguliwa, kwamba wapo wengine bora.
-Mwenye matumaini -Ingawa amekuwa akimkanya Meya bila mafanikio, anamwambia Siki kwamba bado hajakata tamaa, kwamba atasema na Meya tena na tena hadi Meya atakapo-ona umuhimu wa maneno ya Diwani III.
-Mwaminifu - Ingawa hakubaliani na vitendo viovu vya Meya, bado anaenda kumwona Meya anapomwita.
-Mwenye utu - Anajali maslahi ya wafanyakazi. Anawaambia Meya kuwa wafanyakazi ndio wanaochomwa na jua kuwale-tea viongozi mazao na wao wanayala kivulini.

-Mpenda usawa -Anapinga ubaguzi wa Meya kuwamadiwani hawawezi kulinganishwa na watu wengine. Ataka wafanyaka-zi na madiwani wapate nyongeza uchumi ukiimarika.
-Mzalendo - Asingetaka vizazi vya kesho kuachiwa jukumu la kulipia mikopo visivyoifahamu. Angetaka kuitumikia nchi na watu wake. Pia anapinga maamuzi yanayochangia katika ku-lifilisi baraza.

UMUHIMU WA DIWANI III

- Diwani II ni kielelezo cha viongozi kisasa ambao huwa-thamini raia waliodhulumiwa.
- Ametumiwa kuufichua uozo wa Meya kuwa afisi ya Meya ina penyu nyingi za kujipatia utajiri, mfano, Meya pekee ndiye anayeamua jinsi viwanja vya umma vitakavyotumiwa.
- Anaonyesha sera mbovu za uendeshaji wa mali za umma na usimamizi mbaya wa fedha. Mfano, mamlaka kuhusu ma-tumizi mabaya ya viwanja vya umma. Vile vile kulingana na yeye Meya ana mamlaka ya kuumchukulia mtu yeyote hatua.
- Ametumiwa kuonyesha umuhimu wa kuwajibika suala la uchaguzi wa viongozi. Siki kuwa raia ndio wanaowachagua vi-ongozi wabaya. Wataaluma wahitajika kuingia katika siasa.
- Aonyesha umuhimu wa viongozi katika kushirikiana ka-tika kuboresha uongozi na hali ya maisha. Amwambia Siki kwamba ni jukumu la wote kushirikiana ili kung’oa uozo ulio-ko.
- Ni kielelezo cha viongozi ambao hupinga sera hasi za uo-ngozi hata ingawa ni viongozi pia. Mfano, anapinga uamuzi wa Meya na Diwani I na II kuwa madiwani waongezewe mi-shahara, uundaji wa kamati na uchukuzi wa mikopo.
- Ametumiwa kuonyesha usaliti wa Meya. Meya anamwa-mbia Diwani III kuwa hata kama walichaguliwa na raia kuwa-wakilisha katika udiwani ni kazi na kwamba uwakilishi watoao si wa bure.

DIWANI 1(BW USALAMA)
(Ndiye diwani anayehusika na usalama)
-Mweye mapuuza - Diwani II anapomwambia kuhusu wito, anasema wameshuhudia wasiotosheka wakitangaza malala-mishi yao nao wakawazima kwa kukohoa tu. Anamwambia Meya kuwa awaache wanaotaka kugoma wagome, wataji-poza wenyewe.
-Mwenye kiburi - Anasema waliwanyamazisha walalamishi kwa kukohoa tu. Anajivuna kuteuliwa kwao kuwa macho na maskio ya Meya.
-Mzalendo wa kijinga - Anasema kwamba jukumu lao ni kuli-tetea Baraza la Mstahiki Meya ili kuonyesha uaminifu wake kwa Meya bila kuona kuwa baraza ni la umma, si la Meya. Pia badala ya kumwonya Meya, anakubaliana na mipango yake ya kifisadi.
-Mwenye mtazamo finyu -atoa tatizo la uso kamakutumia vijanakuwapiga raia ili watulie nyumbani.Haoni kwamba ma-tumizi ya nguvu yataufanya uongozi kuchukiwa na raia.
-Mnafiki -Anatumia propaganda kuamshauzalendo wa vijana, tamasha za kushindania tuzo mbalimbali zipeperushwe katika vyombo vya habari eti vijana watafurahia. Anamsifu Meya kwa kuwatawanya wafanyakazi.
-Fisadi - Amwomba Meya kutumia mamlaka aliyonayo kuu-nda kamati za madiwani ili madiwani wawaunge mkono.Ana-kubaliana na wazo la Bili na kuiba na kuuza fimbo ya Meya.
-Mwenye ubinafsi/tamaa -Anadai ovataimu pamoja na mali-po ya Bili kwa ushauri. Hatimaye anakubaliana na hoja ya kuuza fimbo ya Meya na anaridhia madiwani kutotoza kodi.
-Mwenye mtazamo finyu - Anawaza tu kuhusu nguo na udha-ifu wakati wa matembezi ya mameya badala ya shida za wa-nanchi na nakisi inayolikumba Baraza.
-Mpenda ubishi - Diwani III anapopinga kutotozwa kwa madi-wani hadi uchumi uimarike, abishana akidai kuwa uchumi ta-yari umeimarika na siye anayehusika na

maswala ya uchumi.
-Mpyaro -Anawatusi wafanyakaziwaliogoma vinyangarika wasiokuwa na shukrani. Anamtusi Diwani III akidai ni mwenye usodai anayejidai kukamilika.
-Kikaragosi - Anakubaliana na maamuzi yote ya Meya hata yasiyo ya busara kusudi asimuudhi ili naye anufaike.
UMUHIMU WA DIWANI I

- Ametumiwa kuonyesha usaliti wa baadhi ya viongozi wa umma. Anashindwa kuwahakikishia wafanyakazi usalama, wanapigwa na polisi na kufanya kazi katika mazingira yasiyo salama kwa afya zao, ukosefu wa glavu vilevile kufanikisha kutoweka kwa fimbo ya Meya badala ya kuilinda.
- Ni kielelezo cha viongozi wasioajibika, anaridhia sera mbovu kama marupurupu ya walinda usalama, nyongeza kwa madiwani na kutotozwa kodi na kuuza fimbo ya Meya.
- Ni kielelezo cha viongozi fisadi katika jamii. Anashiriki katika njama za uundaji wa kamati za madiwani ili kulifisadi baraza. Ataka kulipwa ovataimu, na kadhalika.
- Ni kikaragosi anayeridhia matumizi yote ya Meya hata yasiyo ya busara, mfano, kuuza kwa fimbo ya Meya.
- Ni kielelezo cha viongozi wasiowajibika wenye tamaa na wanafiki.

DIWANI II(BW. UHUSIANO MWEMA)
-Ni kikaragosi - Anaafikiana na maamuzi yote ya Meya,hata yasiyo na busara. Meya anapomwambia lazima ulimwengu upate msimamo wa baraza, Diwani II anasema hajawai kum-vunja Meya kwa lolote
-Mnafiki - Anasema atahakikisha kwamba mashindano yame-peperushwa moja moja kupitia vyombo vya habari ilikuibia uzalendo wa raia. Anapendekeza kuundwa kwa kamati za madiwani ili kuhakikisha wameungwa mkono katika njama zao kifisadi.
-Mwenye mawazo finyu - Anajishughulisha na vile tu madi-wani wanavyoonekana machoni pa wageni badala ya kuzua mikakati ya kuinua hazina ya baraza. Anasema si

vizuri kuone-kana hivi hivi mbele ya wenzao**.**
-Ni fisadi - Anakubaliana na mawazo ya Diwani I kupewa ova-taimu na kuiba fimbo ya Meya, iuzwe wadai ilitoweka wakati wa mgomo wa wafanyakazi.
Mwenye ubinafsi/tamaa - Ataka kulipwa ovataimu,nyongeza ya mishahara, kutotozwa kodi na kuunda kamati ili kuungwa mkono. Vile vile ashiriki katika njama ya kuuzwa kwa fimbo ya Meya ng`ambo.
Mwenye ubaguzi - Yeye ajiona bora kuliko wafanyakazi. Ase-ma kuwa wanapaswa kusukumwa kabisa ili wajue kuna wana-nchi na wenye nchi.
Mbadhirifu - Apendekeza Bili alipwe kwa huduma za ushauri na si Diwani wa Baraza. Haya ni matumizi mabaya ya mali ya umma.
Mwepesi wa kuhadaiwa - Yeye, Meya na Diwani I wanaha-daiwa na Bili, wanashirikiana katika kuuzwa kwa fimbo ya Meya
Mshauri mpotovu - Yeye na Diwani I wanamshauri Meya visi-vyo kwa lengo la kujinufaisha.
-Katili - Yeye na wenzake wafurahia wakati wafanyakazi wa-natawanyishwa kikatili na askari ili kuzima mgomo.
UMUHIMU WA DIWANI II
-Ni kielelezo cha washauri wapotoshi wanaopotosha viongozi. Mfano, uundaji wa kamati za madiwani, nyongeza ya mishara kwa madiwani na marupurupuya walinda usalama.
-Kupitia kwake tunaona mbinu hasi za uongozi, mfano,Propa-ganda ili kijihifadhi mamlakani, tamasha kwa vijana, na ka-dhalika.
-Ametumiwa kuonyesha kutowajibika kwa viongozi. Wanashi-rikisha Bili katika maamuzi muhimu na hivyo Bili anawalaghai fimbo ya Meya na kutoweka.
-Ametumiwa kuonyesha ubinafsi na baguzi wa viongozi. Wao wanufaike pasipo kujali Wanacheneo wengine.

BILI
(Rafiki,msiri na mshauri wa Meya)

-Mnafiki - Ajifanya rafikiye Meya ilhali anataka anufaike. Ana-mwita Meya ndugu. Anamshauri wasitumie nguvu ili watoe picha mzuri kwa wageni na anawakumbusha Meya, Diwani I na II umuhimu wa kuuma na kuvivia.
-**Mpenda kuiga** - Anasema hata naye atampeleka mke wake ng`ambo kama wa Meya.
-Fisadi - Anashiriki njama za kuiba mali ya umma.Mfano, ana viwanja vinne, kuiba fimbo ya Meya na anamshauri Meya kuibia baraza kupitia kandarasi.
-Mdanganyifu-Anawadanganya Meya, Diwani I na II kuwa ataitafutia fimbo soko ng`ambo lakini anatoweka.
-Mwenye tamaa/ubinafsi - Amwambia Meya kuwa akisha pata sehemu yake kutoka kwa mwanakandarasi asimsahau. Vilevile atoweka na fimbo ya Meya ili ajinufaishe yeye mwe-nyewe.
-Amepotoka kimaadili - Anamibia rafikiye na msiri wake Meya baada ya Meya kumpa viwanja vinne na anapanga na Meya kuliibia baraza kipitia mwanakandarasi.
-**Ni jasiri-** Anamwabia Meya kama hawezi kushawishi mwa-nakandarasi aende mahakamani, atampangia yote yaende kwa mpango. Vile vile ashiriki wizi hatari wa fimbo ya Meya.
-**Mwenye mapuuza -** Amwambia Meya kuwa kelele za wafa-nyakazi ni sauti za chura, awaache waseme. Auona mgomo wa wafanyakazi kama mbio za sakafuni tu.
-**Ni mwenye dharau -** Anawaita wafanyakazi debe tupu na sauti zao kelele za chura.
-**Ni katili -** Yeye, Diwani I na II wanafurahia kutawanywa kwa wafanyakazi kikatili na askari.
-**Mshawishi -**Anamshawishi Meya aliibie baraza kupitia mwa-nakandarasi, kuiba na kuuza fimbo ya Meya, na kadhalika.
-Mpenda ya kigeni -Asema elimu ya humu nchini ni ya kina yakhe.
UMUHIMU WA BILI

- **A**metumiwa kuonyesha ujinga wa viongozi wa umma wanaochukua ushauri wowote kipofu. Hatimaye viongozi hawa huhasirika kama anavyofanya Meya.
- Aonyesha usaliti, kwa vile anamtoroka Meya wakati anapomhitaji zaidi licha ya fadhili zote alizotendewa.
- Ni mfano wa Waafrika wanaopuuza dini za kiafrika za kupapia ya kigeni, mfano, elimu, huduma za afya, utamaduni, na kadhalika.
- Aonyesha wizi wa mali ya umma unavyotekelezwa na viongozi wakiwafaa marafiki zao.

WARIDI
(Muuguzi katika zahanati)
-Mwepesi wa kushawishika - Anaamini vile anavyosema Me-ya kuwa dawa zimeagizwa.
-Mwenye kukata tamaa - Anasema hawana cha kufanya kwa-ni nchi ni maskini. Anajiuzulu kazini kwa sababu ya mazingira magumu kazini.
-Mwenye ubinafsi - Anaamua kujiuzulu pale tu binamu yake anapokufa kwa kukosa dawa. Vile vile alitaka waliolazwa hos-pitalini walipe ilhali hamkuwa na dawa.
UMUHIMU WA WARIDI.
-Kupitia kwake sera mbovu za usimamizi wa zahanati unaone-kana. Wagonjwa walipe na huku hakuna dawa.
-Ni mfano wa viongozi wa umma ambao hufuata maagizo bila kuuliza swali, watu kununua karatasi za udodosi, asema ni amri ya wakubwa.
-Kupitia kwake tunaona uvumilivu wa Siki. Siki anamhudumia mtoto pamoja na kuwa Waridi alimtaka asubiri nje. Asema wagonjwa wakiwaona, wanapata tumaini.

GEDI
(Mpambe wa Meya)
-Ni mzalendo wa kijinga - Anafuata yote anayoambiwa na Meya kwa ‘Yes sir.’ Hamshauri Meya lolote ila kufuata yote anayoambiwa.

-Mwenye pupa - Anaposikia sauti za Meya na mhubiri wakio-mba, aamua moja kwa moja kuwa Meya amevamiwa. Anawa-ita askari na kuingia humo kwa pupa wakiwaambia wainue mikono juu.
-Ni mwaminifu katika kazi yake - Hata anapoona mambo ni mabaya haondoki kama Bili au mhazili wa Meya.
UMUHIMU WA GEDI

- Anaendeleza maudhui ya ukoloni mambo leo. Mfano, anampigia Meya saluti amjibu ‘Yes sir’ na kutoa shukrani pasi-po sababu, ‘Thank you sir.’
- Aonyesha ujinga wa watumishi wa umma. Kumshukuru Meya kwa kumtolea amri.
- Ni kielelezo cha vyombo vya dola vinavyotumiwa kuka-ndamiza haki za umma, mfano, wafanyakazi wanaogoma.

DIDA
(Mhudumu wa nyumbani kwa Meya)
-Mcheshi - Anaigiza jinsi askari wanavyopiga kwata kwa kuigi-za maneno kisauti, mfano, ‘let rat let rat.’
-Aonyesha kuwa na ubinafsi - Anapokashifu ukatili wa Meya anajiuliza anayataka nini haya mambo. Mameya wawepo naye azidi kunadhifisha nyumba zao hata kama mji mzima unanuka kwa uvundo.
UMUHIMU WA DIDA

- Ni kielelezo cha dhuluma wanazozipitia wafanyakazi wa nyumbani. Asema kazi ya nyumbani haina heshima kwani bwana anawatusi.
- Ndiye anayeonyesha viongozi wanavyotumia bunduki na vitoa machozi kuwanyamazisha raia.
- Anaonyesha mbinu hasi za utawala, watu wanapouawa, viongozi wanasema hawakufa.
- Dida ametumiwa kuonyesha tatizo la ubaguzi katika suala la usalama. Anasema kuna roho ya mtu na ya kiatu.
- Ametumiwa kufanyia tashtiti askari kwa kuigiza vitendo vyao.

MHUBIRI

-Mnafiki -Anamwita Meya ndugu mpendwa . Anaitika kwa ‘Amen’ za uongo lengo likiwa kumfanya awe muumini apate sadaka.
-Mwenye tamaa/ubinafsi -Anamwombea Meya na baraza kwa nia ya kupata pesa.
-Amekosa uwajibikaji -Baada ya kuukosoa uongo mbaya, anaendelea kuuombea udumu.
UMUHIMU WA MHUBIRI

- Ametumiwa kuonyesha jinsi watawala wanavyotumia unafiki wa kidini kwa kumwita ndugu.
- Anamwombea Meya uongozi wake udumu milele na maombi yaliyojaa jazba.
- Anatoa mfano wa viongozi wa kidini wanaovyeo/nafasi kuwapora raia - aombea Meya ili afaidike na sadaka.

TATU, BEKA NA MEDI
(Wawakilishi wa wafanyakazi)
-Ni waajibikaji -Wanataka kwenda kwa Meya kuwasilisha malalamishi yao.
-Ni jasiri -Wanamwambia Meya (Tatu) kwamba wao hawawezi kuwa sawa na tabaka la Meya.
-Ni wenye busara -Tatu awaambia Medi na Beki kwamba haina maana ya kuvutana kwani mvutano hausaidii. Anamwa-mbia Meya kuwa nia ya wafanyakazi si kuwaitisha bali ni kupi-gania ubora wa maisha.
-Wenye msimamo thabiti -Meya anapowaambia kwamba hawawezi kushiriki kikao na waliogoma, wanamwambia kuwa mgomo utaendelea.
UMUHIMU

- Waonyesha dhiki wanazozipitia wafanyakazi, hali duni ya kikazi, ukosefu wa vifaa, mishahara duni, kucheleweshwa kwa mishahara, na kadhalika.
- Kupitia kwao maudhui ya ubinafsi, utabaka na ubaguzi yanajitokeza, mfano, ukosefu wa dawa lakini madiwani wana bima za matibabu, kulipwa kwa na magari ya usafiri, na kadhalika.

- Wanaendeleza maudhui ya uzalendo wanakaidi rai ya Meya kwamba hawawezi kazi. Hawangesaliti wenzao.

ASKARI I NA II

-Ni wazalendo wa kijinga -Wanaposkia vilio vya Meya na mhubiri, wanaingia kwa fujo na kuwaamuru wainue mikono juu.

-Wenye uwajibikaji - Askari I anamwambia kwamba ni kazi yao kufika mara Meya anapowahitaji.

-Ni jasiri-Askari II anamwambia Meya kuwa wametumiwa kutoka makao makuu kuwachukua Meya, Diwani I na II kwa kuelezea hali ya mambo Cheneo.

UMUHIMU WA ASKARI

- Waonyesha jinsi vyombo vya dola hutumika kwa masla-hi yao, mfano, wafanyakazi.
- Waonyesha ujinga wa askari ambao hufuata amri za vi-ongozi pasipo kutumia akili.
- Wanaendeleza ukuloni mamboleo “Yes sir!” na kadha-lika.

MTINDO

KINAYA

Kuna aina tatu za kinaya:

i) **Kinaya cha kiusemi -** Usemi unaotolewa huwa na maana iliyokinyume.
ii) **Kinaya cha kihali** - Matendo ya wahusika yanakuwa kinyume cha matarajio ya msomaji.
iii) **Kinaya cha kidrama** - Wahusika hawafahamu ma-mbo fulani lakini msomaji anafahamu (kinaya dra-ma).

Mfano:

- Meya analalamika viyai kuwa amepunjwa ilhali yeye ana-wapunja wafanyakazi kwa maisha duni. Pia ni kinaya kwake kama kiongozi kulalamikia mambo madogo madogo.
- Ni kinaya kuwa watu walimchagua Meya kuboresha hali za maisha lakini anawateleka katika magonjwa, njaa, ukosefu wa lishe bora, hali duni za kikazi, na kadhalika.

- Ni kinaya kuwa wananchi wanawachagua viongozi wale wale licha ya kutoridhishwa na viongozi wale. Meya amwa-mbia Siki kuwa watu watamchagua hata mara sita akipenda.
- Ni kinaya Meya kusema kuwa Cheneo ni kisima cha ku-pigiwa mfano ilhali watu wanakufa kwa kula mizizi na matu-nda mwitu. Vile vile, watoto wanakufa kwa njaa na utapia-mlo.
- Ni kinaya kwa Meya kujidai kwa Siki kuwa ana akili nyingi na hali anapumbazwa na Bili. Mfano, kuuzwa kwa fimbo ya Meya, kuibia baraza kupitia mwanakandarasi, na kadhalika.
- Ni kinaya Diwani I kusema baraza linatetea demokrasia na uhuru wa kujieleza na huku wafanyakazi wanapogoma ku-dai haki zao wanatawanywa na viongozi.
- Ni kinaya Diwani II kupendekeza kuundwa kwa kamati za madiwani na huku baraza haliwezi kumudu gharama za kama-ti hizo. Kile anachotaka ni madiwani wawaunge mkono.
- Ni kinaya Meya kuidhinisha nyongeza ya mishahara kwa madiwani, marupurupu, ya walinda usalama na kutotozwa kodi kwa madiwani na huku baraza tayari lina nakisi ya milioni 120.
- Ni kinaya kuwa watu wa tabaka la chini wanalipa kodi licha ya mishahara duni hali madiwani wenye mishahara mi-nono hawalipi.
- Ni kinaya kuwa Meya ambaye anastahili kulinda mali ya umma anajigawia viwanja vinane, vinne anampa Bili, na ka-dhalika.
- Ni kinaya wafanyakazi wanaoshiriki katika kuzalisha mali ilhali ndio wanaolipwa mishahara duni na viongozi ndio wa-nostarehe.
- Ni kinaya Bili kuwaita wafanyakazi wahalifu ilhali yeye ndiye mhalifu mkuu. Anampotosha Meya, anashiriki ufisadi kulihujumu baraza na wizi wa fimbo ya Meya.

MAJAZI

A. Siki: Siki ni kinywaji kichungu sana (shubiri). Yaani ni mtu mwenye kupenda ukweli hata kama

utakuwa mchungu kiasi gani. Siki alitoa maneno machungu kwa viongozi. Anamshauri Meya kwa ajili ya wafanyakazi kinyume na matarajio ya Meya.

B. Kheri: Ni neno linalomaanisha neema,baraka, afadhali au bora. Huyu ni Diwani III. Ni mtu ambaye ni baraka kwa wananchi kwani yeye alikuwa mtetezi wao. Alimpa Meya mashauri mazuri lakini Meya aliyapuuza. Yeye ni bora ukilinganisha na madiwani wengine.

C. Sosi: Ni jina analoitwa Meya ambaye ni binamu yake Siki. Ni jina linalotokana na neno la kiingereza 'source' yaani chanzo cha matatizo. Pia ni msimu unaomaanisha kula. Meya anatumia cheo chake kwa kujitajirisha.

D. Waridi: Ni aina ya ua linalovutia lakini hukauka mara li-napotolewa mtini. Waridi anaonyesha huruma na imani kwa wagonjwa.

E. Cheneo: Ni kitu kilichoenea. Cheneo ni mji ulio na uenezi wa uozo, migomo, ukatili, unyanyasaji, na kadhalika.

TASHBIHA

- *"Watu kujifia kama nzi"* **(Ukurasa 38).** Tatu asisitiza jinsi watu wanavyokufa kwa ukosefu wa dawa.
- Siki anasema, "*Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji."* (Ukurasa 45)- Hawaelewani.
- Diwani II asema,"*Bahati ikisimama imesimama."* Siki anamkatiza, "*inasimama kama mtende.'* (Ukurasa 45) Hapa Siki amempata Diwani III licha ya shughuli zake nyingi.
- *"Kupinga haya ni sawa na kumkama Simba mwenye watoto"* (Ukurasa 14) - Meya akisisitiza kuwa wameingia kiwango cha kimataifa. Hivyo mipango ya kimaendeleo ya kimelania.
- Meya akitumia *Riots acts* inatosha kumkunja kila aliye chini yake *"kama ua wakati wa alasiri."*

UHAISHAJI/TASHIHISI

- *"Njaa ina nguvu imeangusha mlamba"* (Ukurasa 34).

Njaa imepewa uhai - kuwa na nguvu kuonyesha kuwa wanao-dhulumiwa wana uwezo wa kung’oa viongozi dhalimu.

- *“Mlango hatimaye huenda ukasalimu amri”* (Ukurasa 39). Mlango umepewa uwezo wa kutii, inaonyesha kwamba wakiendelea kushirikiza kukutana na Meya, huenda nafasi ikapatikana.
- *“Kuna roho za mtu na kiatu”* (Ukurasa 65). Kiatu kimepe-wa uwezo wa kuwa na roho. Kiatu ni wafanyakazi na mtu ni viongozi.
- *“Magari yanayotapika maji”* (Ukurasa 65). Magari yame-pewa sifa ya kutapika maji yakiwatawanya wafanyakazi.
- *“Wanatawala nzi na harufu”* (Ukurasa 73).
  Nzi na harufu zimepewa uwezo wa kutawala. Haya mambo ya uchafu mjini.

METHALI

- **Ngoja ngoja huumiza matumbo.** (Ukurasa 2)

Siki akamwambia Waridi kuwa wagonjwa watahasia wakingo-ja dawa ambazo kwa haki hazijaagizwa.

- **Haraka haraka haina baraka.**(Ukurasa 2)

Waridi anajua kauli ya Siki kuwa kwa vile Meya amesema ni heri wasubiri.

- **Ngoja ngoja za mganga huleta matumaini.** (Ukurasa 6)

Sikiamwambia Waridi kuwa heri kumpa mtoto mchanganyiko wa chumvi na sukari ndani ya maji ili ampe mama matumaini.

- **Sikio la kufa halisikii dawa.** (Ukurasa 46)

Maana ni kuwa uovu wa Meya hauwezi kutibika. Umefikia kiwango cha juu.

- **Uhitaji siku zote ni mtumwa.** (Ukurasa 54)

Wafanyakazi hata wakigoma, watarudi kazini kwa sababu sana mahitaji ya kimsingi.

- **Heri nusu shari kuliko shari kamili.** (Ukurasa 39)

Siki anamwambia Tatu ili kumwonya dhidi ya mgomo kwani huenda kukawasababisha wafanyakazi matatizo zaidi.

- **Lililoandikwa halifutiki kamwe**.(Ukurasa 45)

Inaonyesha kuwa ni majaaliwa ya Siki na Diwani III wakutane.

- **Msiba wa kujitakia hauna kilio.** (Ukurasa 57)

Meya asema methali kurejelea wafanyakazi walipokuwa wa-kitawanywa na askari. (Sauti msiba kuwa kujitakia)

- **Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.**

Anarejelea wafanyakazi kushindana na baraza.

- **Wasemao mchana usiku watalala.** (Ukurasa 31)

Bili akimwambia Meya asiogope kusemwa, anaziita kelele za chura.

MASWALA BALAGHA

i. *“Mbona nisiwe na hakika?”* (Ukurasa 2). Waridi amw-uuliza daktari swali hili kuonyesha ana uhakika kuwa dawa zingefika.

ii. *“Hujui ngoja ngoja huumiza matumbo?Unadhani wa-ngapi wananiunga mkono?”*(Ukurasa 12). Meya amwonyesha Siki wapo watu wengi wanaounga mko-no viongozi wake.

iii. *“Wewe waona Meya mwenyewe mchezi?”* (Ukurasa 28). Meya amuuliza Bili kuonyesha ukweli wake.

iv. *“Nisipokuwa nazo nani atakuwa nazo”* (Ukurasa 28). Meya aonyesha Bili kuwa yeye ana pesa na muhimu Bili ajue hili jambo kwani li wazi.

v. *“Nilikusahau lini ndiyo sasa nije kukusahau?”* (Ukurasa 30). Meya anamwambia Bili kuonyesha uaminifu wake kwa Bili.

vi. *“Sasa kazi hii ina faida gani kwangu?”*(Ukurasa 36). Waridi amwuliza Siki wakati alipokuwa akitaka kujiuzulu.

vii. *“Nani atatuchezea?”*(Ukurasa 43). Mhubiri amwuliza Meya ili kumhadaa eti ana mambo na ndio sababu askari wakaja mara moja.

viii. *“Unafikiri hakuna watu wanaoweza kuhudumu vyema zaidi kuliko sisi?”* -kusisitiza kuwa kuna watu wanao-weza kuongoza vyema kuwaliko wao.

ix. *“Kuna raha gani watoto wetu wanafukuzwa shule kwa sababu hatuwezi kuwalipia karo*? *Kuna raha*

gani kutazama watoto wetu kufa taratibu mikononi mwetu kwa sababu hatumudu tena gharama ya matibabu? Tena katika hospitali ya mwajiri wetu? Hospitali hiyo imejengwa na nani kama si sisi waajiriwa wake?” (Ukurasa 70) - Tatu amuhimiza Meya kutokana na matatizo yanayowakumba wafanyakazi.

x. *“Tugangeje ya kesho bila kuganga ya sasa?”* (Ukurasa 70) - Hapa Meya aonyesha majuto kwa kutorekebisha mambo na sasa muda wa kuyarekebisha haupo tena.

xi. *“Mimi nisipotumia choo, wataajiriwa kufanya nini?”* (Ukurasa 52) - Balagha hii yaonyesha kiburi cha Meya.

UZUNGUMZI NAFSIA
(Mhusika ajizungumzia)

- Meya anapofuzwa na Gedi kuwa Siki amekuja kumwona anajizungumzia. Asema Siki alipokwenda kumwona awali ali-mletea bahati mbaya. (Ukurasa 10)
- Ofisini pake kabla ya Bili kuingia Meya anajizungumzia (Ukurasa 24). Namna anapanga kumtumia mwanakandarasi wa awali na asema hata mwanakandarasi akishtaki ni bure.
- Baada ya Siki kuongea na simu, anajizungumzia (Ukurasa 34). - Aonyesha msimamo wake kuhusu hali katika baraza la Cheneo. Pia dhiki inayowakumba wafanyakazi, mfano, njaa na magonjwa.
- Baada ya mazungumzo baina ya Meya na Diwani III, Meya anajizungumzia, anarudia yale maneno ambayo Diwani III alimwambia kuhusu haja ya kuwasikiliza wafanyakazi. Hatimaye anaamua kukutana na uongozi wa wafanyakazi.

UCHESHI

Unafanyia tashtiti udhalimu wa Meya na Dida anapoigiza askari. Let rat! Let rat! Let rat! Badala ya Left right! Left right. Haya yanamkejeli Meya.

KUCHANGANYA NDIMI

- Gedi ana mazoea ya kumjibu Meya ‘Yes sir’. Hizi ni athari za kikoloni.
- Bili anamhimiza Meya kuwa na ‘Gentleman’s Agreement’ na yule mwanakandarasi ili amegewe kiasi fulani cha fidia (Ukurasa 29).
- Diwani III asema kuwa kuna ‘Mayor’s Act’ ambayo ana-weza kutumia kumkandamiza kila mtu. Vile vile kuna ‘Riot Act’.
- Meya amtuma Gedi amletee soda katika ‘fridge’ (Ukurasa 17).
- Meya asema kuna vijana wamehitimu vyuo vikuu ‘fresh’ kabisa na hawana kazi hata ya utopasi (Ukurasa 21).
- Meya amwambia Bili kuwa ana ‘Entertainment Vote’ yangoja ualishi tu (Ukurasa 27).
- Ikiwa hii si ‘insurbodination’ ni nini? (Ukurasa 55). Meya akimtisha Diwani III kwa kutokubaliana naye.
- Diwani II adai walipwe ‘overtime’ (Ukurasa 61) na pesa zinapokosekana, wanapendekeza kuuzwa kwa fimbo ya Meya.
- Katika mpango wa kuiba na kuuza fimbo ya Meya, Diwa-ni II asema kuwa mpango waliozua ni ‘foolproof’ (Ukurasa 62).
- Meya asema hana pingamizi kwa kuwa ni ‘grand idea’ (Ukurasa 62).
- Siki anasema ‘Oh yes’ kisha kwa mama mwenye mtoto utamfuata ‘sista hapa’ hadi kwenye wadi ya watoto (Ukurasa 5).
- Meya amwambia Gedi kuwa Siki alione nyumba yake paa ‘Alright’(Ukurasa 15).
- Meya asema ameuza viwanja vitatu na amebakisha vita-no‘Incase’(Ukurasa 27). Hasa ile ‘prime plot.’
- ‘Amen’ wanavyoitika Meya na mhubiri wanapoomba.

KUHAMISHA NDIMI

Waridi anamuuliza daktari, “What do you think this is? Food poisoning?” (Ukurasa 5).

UTOHOZI

- **M**eya – mayor.

- Daktari amwambia mama mwenye mtoto “utamfuata sista (sister) hadi kwenye wadi (ward) ya watoto” (Ukurasa 5).
- Milenia- millenium.
- Meya alihitajiwa aundiwe kamati (committee) za madi-wani.
- Meya asema uamuzi wa baraza ni demokrasia (democra-cy) (Ukurasa 22).
- Meya asema mwanakandarasi ameenda kortini (court) (Ukurasa 28).
- Meya asema baraza litagharamia petroli (petrol) ya mhu-biri (Ukurasa 44).
- Medi asema wafanyakazi wanaosha vyoo bila glavu (glo-ves) (Ukurasa 70).
- Swichi (switch) - Diwani I asema anabofya simu tu kutoka mbali na kazi inafanyika.

SADFA

Matukio mawili kutokea wakati mmoja bila kupangwa au kutarajwa.

Mfano:

- Daktari Siki na Waridi wanaendelea na mazungumzo yao wakati uo huo mama mwenye mtoto mgonjwa anaingia hospitalini.

-Diwani I na II na III wanaendelea na mazungumzo yao kisha kwa ghafla Meya aingia.

-Meya na Bili wanaendelea na mazungumzo yao na wakati uo huo sauti za wafanyakazi zinaskika.

-Meya na mhubiri wanapoomba kwa kelele na jazba, askari I,II na Gedi wanaingia na kuwaamrisha walale chini.

-Diwani I na II wanaendelea na mazungumzo yao na wakati uo huo, Gedi anaingia ghafla na habari kuwa wanahitajika katika makao yao.

LAHAJA

Ya mwananti kuuvunda nti (Ukurasa 50). - Mwananchi kuivunja nchi.

Diwani III asema, “ndiyo yale ya ngome itauumiza naswi tu mumo ngomeni” inatuumiza naswi - na sisi.

Meya anasema, “ndo unamaanisha ni” (Ukurasa 11). Ndo-

ndiyo.

MBINU YA UTATU

I. Mtoto mgonjwa ana miaka mitatu.
II. Mtoto alikufa akiwa na miaka mitatu.
III. Mtoto alikuja baada ya siku tatu.
IV. Kuua ndege watatu kwa jiwe moja.
V. Madiwani ni watatu.
VI. Kuna wawakilishi watatu wa wafanyakazi.
VII. Dawa zitafika bandarini baada ya siku tatu.
VIII. Baada ya siku tatu kutoka bandarini dawa zitafika hospitalini.
IX. Meya na madiwani wawili wanakamatwa. Jumla ya waliokamatwa ni watu.

MASWALI YA KUDURUSU

a) **Maswali ya insha**

1. Fafanua mikakati anayotumia Mstahiki Meya ili kuwe-za kusalia mamlakani. (alama 20)
2. Eleza matumizi ya mitindo ifuatayo:- (alama 20)
   a) Kinaya
   b) Jazanda
   c) Majazi
   d) Sadfa
3. Fafanua jinsi dhana ya ukoloni mamboleo inavyojito-keza katika tamthilia ya “***Mstahiki Meya.***” (alama 20)
4. Eleza changamoto zinazowakabili Wanacheneo. (alama 20)
5. “*Siku ya kufa kwa nyani miti yote huteleza.*”Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea tamthilia ya “***Mstahiki Meya***” (alama 20)
6. Dhihirisha ufaafu wa anwani “***Mstahiki Meya***.” (alama 20)
7. Eleza umuhimu wa wahusika wafuatao katika tamthi-lia ya “***Mstahiki Meya.”***
   a) Waridi (alama 10)
   b) Siki (alama 10)

8. “Tamthilia ya ***Mstahiki Meya*** imesheheni utetezi wa haki kwa mapana na marefu.” Thibitisha. (alama 20)

b) **Maswali ya Muktadha**

1. “Wewe ndiye wa kuniambia. Mimi nimekuuliza wewe.”
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Ni mambo yepi yaliyosababisha mnenaji na mnenewa kuwa katika hali waliyoko sasa.(alama4)

c) Eleza sifa za mnenaji na mnenewa. (alama 8)

   d) Fafanua tofauti za sifa kati ya mnenaji na mnenewa. (alama 4)

2. “Kuna mji gani wenye amani na utulivu kama wetu?”
   a. Yaweke maneno haya katika muktadha wake.(alama 4)

   b**.** Taja mbinu mbili zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)

   c. Fafanua maudhui manne yanayoendelezwa kupitia kwa mnenaji. (alama 8)

   d. Taja wahusika wengine wawili walio na sifa sawa na mnenewa na utoe sababu. (alama 4)